Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

# HISTORIA KUU YA AFRIKA·

Juzuu Lililofupishwa

# VI Afrika kwenye Karne ya Kumi na Tisa hadi miaka ya 1880.

MHARIRI J.F. ADE AJAYI



TUKI · CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM · UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

Historia Kuu ya Afrika · VI

# Afrika Kwenye Karne ya Kumi na Tisa Hadi Miaka ya 1880

MHARIRI J.F. ADE AJAYI

Toleo Lililofupishwa

TUKI · CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM · UNESCO

**Jina la Asili: GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL VI**

© UNESCO 1999
ISBN 9976 911 27 0

*Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.*
*Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.*
*Toleo la Tafsiri ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.*

Historia Kuu ya Afrika · VI

# Afrika Kwenye Karne ya Kumi na Tisa Hadi Miaka ya 1880

## Toleo Lililofupishwa

**UNESCO Historia Kuu ya Afrika**

| | |
|---|---|
| **Juzuu I** | *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*<br>Mhariri **J. Ki-Zerbo** |
| **Juzuu II** | *Staarabu za Kale za Afrika*<br>Mhariri **G. Mokhtar** |
| **Juzuu III** | *Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kami na Moja*<br>Mhariri **I. Hrbek** |
| **Juzuu IV** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita*<br>Mhariri **J. Ki-Zerbo na D.T. Niane** |
| **Juzuu V** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane*<br>Mhariri **B.A. Ogot** |
| **Juzuu VI** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi Miaka ya 1880*<br>Mhariri **J.F. Ade Ajayi** |
| **Juzuu VII** | *Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935*<br>Mhariri **A. Adu Boahen** |

## Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

| | |
|---|---|
| **Juzuu VIII** | *Afrika Kuanzia 1935*<br>Mhariri **A.A. Mazrui**<br>Mhariri Msaidizi **C. Wondji** |

Toleo lililofupishwa la
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO

**Limechapishwa na:**

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110
Dar es Salaam, Tanzania

Pamoja na:
UNESCO Publishng
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris

Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.

# *YALIYOMO*

Dibaji na Amadou-Mahtar M'Bow aliyekuwa Mkurugenzi wa UNESCO (1974-87) vii
Wasifu wa Mradi na B.A. Ogot, aliyekuwa Mwenyekiti, Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-83) xii
Maelezo ya Wendo xv
Shukrani za kupatiwa picha xvi
Wanakamati wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika xvi
Orodha na Wasifu wa Waandishi waliochangia kwenye juzuu kuu xviii

1 *Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa: masuala na matumaini* 1
2 *Afrika na uchumi wa dunia* 10
3 *Mielekeo na nyendo mpya katika Afrika kwenye karne ya kumi na tatu hadi kumi na tisa* 15
4 *Ukomeshaji wa biashara ya watumwa* 28
5 *Mfekane na kuibuka kwa madola mapya ya Kiafrika* 41
6 *Athari za Mfekane katika Koloni la Rasi* 53
7 *Waingereza, Makaburu na Waafrika nchini Afrika Kusini, 1850-80* 63
8 *Nchi za Bonde la Zambezi* 72
9 *Pwani na bara ya Afrika Mashariki 1880- 1845* 84
10 *Pwani na bara ya Afrika Mashariki 1845-1880* 93
11 *Watu na dola za ukanda wa Maziwa Makuu* 106
12 *Bonde la Kongo na Angola* 119

*13 Kipindi cha mvuvumko wa Misri, 1805-81* *137*

*14 Sudani katika karne ya kumi na tisa* *148*

*15 Ethiopia na Somalia* *158*

*16 Bukini (Madagaska) 1800-1880* *172*

*17 Sura mpya ya maendeleo ya Maghrib: Algeria, Tunisia na Libya* *185*

*18 Moroko kutoka mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa hadi 1880* *198*

*19 Ruwaza mpya za maingilio ya Ulaya katika Maghrib* *208*

*20 Sahara katika karne ya kumi na tisa* *218*

*21 Mapinduzi ya Kiislamu katika karne ya kumi na tisa huko Afrika Magharibi* *227*

*22 Ukhalifa wa Sokoto na Borno* *234*

*23 Messina na himaya ya Kitorodbe (Kitukuloor) hadi mwaka 1878* *248*

*24 Nchi na watu wa Senegambia na ya Juu Guinea* *261*

*25 Nchi na watu wa mzingo wa Niger na Volta* *271*

*26 Dahomey, nchi ya Yoruba, Borgu na Benin katika karne ya kumi na tisa* *288*

*27 Delta ya Mto Niger na eneo la Kameruni* *301*

*28 Kutawanyika kwa Waafrika duniani* *314*

*29 Hitimisho: Afrika kwenye mkesha wa ushindi wa Wazungu* *324*

Bibliografia *332*

Faharasa *356*

Sherehe *375*

# *Dibaji*

**AMADOU - MAHTAR M'BOW**
*Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)*

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayounganisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezewa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya

bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokeazaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuniwa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika,* ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya

Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi 1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa)* kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha sehemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia;* kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihausa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa

kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kiteknolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika,* na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepukana na inadi katika utafiti wa masuala muhimu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini aambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii.Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayowezesha kueleweka kwa vipengele

fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*[1] yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika.

*Historia Kuu* inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika*. Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambarao upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

*Historia* hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika

[1] Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu:
*Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuvuka Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukoloni Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika weusi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyama vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.*

Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa elimu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginepo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na vipengele vinavyoelezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango walioutoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.

# Shukrani za kupatiwa picha

Allen na Thompson, *Narrative of an Expedition,* London, 1848, 27.4*

Al-Refei, Abdel-Rahman., *Açr Mohammad 'Ali,* Dar al-Nahdal al-Micriyyah, Kairo, 1930, 13.3 (Tol. 4) 1982, Dar el-Maaref, Kairo, © Judge Helmy Shahin, 13.4

Archives du Ministére des Affaires éstrangères, Paris, kwa ruksa ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Ufaransa, p. 4.1

Arhin, K., kwa ruksa ya Asantehene wa Ghana, 25.2

© *Arts of Asia,* Hong Kong, Machi-Aprili 1978, uk. 89, 28.1

Barbour, N., *Morocco,* Thames na Hudson, 1965, Paris, 19.3

Basel Mission Archives, 25.9

Bennett, N.R na Brooks G. E. (wah.) *New England Merchants in Africa: A history through documents,* 1802-1865, Boston University Press, Boston, 1965, © Peabody Museum of Salem, picha na Mark Sexton, 9.3

Bennett, N. R., *Mirambo of Tanzania,* Oxford University Press, New York, 1971, © Jumba la Makumbusho ya Taifa, Dar es Salaam, 10.4

Binger, L., *Du Niger au Golf de Guinée,* Hachette, Paris, 1892, 24.2*, kwa ruksa ya Bodleian Library (shubaka na.: 710.11.s.8/1), Juz. I, uk. 19, 25.5*, 25.6**, Juz. II, 25.7*

Bowdich, T. E. *A Mission From Cape Coast Castle to Ashantee,* John Murray, London, 1819, 25.3*

Burton, R., *The Lake Region of Central Africa,* Longman, Green Longman na Roberts, London, 1860, Juz.II, uk. 80 and 278, © Royal Geographical Society, London, 10.2, 10.3

Burton, R., *First Footsteps in East Africa,* Routledge na Kegan Paul Ltd, London, 1894, picha zilitolewa tena na Sasor Publisher, London, 15.4

Cameron, V.L., *Across Africa,* Daldy, Isbister na Co, London, 1877, Juzl. 1, uk. 352, 12.2* *Church Missionary Gleaner,* 1855, 26.3*

Collection Bibliothéque Générale et Archives, Rabat 18.3

de Chassiron, Ch., *Aperçu pittoresque de la Régence de Tunis, Imprimerie de Bénard, Paris,* 1849, 17.4**

Denham, Clapperton and Oudney, *Narrative of Travels and Discoveries in Northern and Central Africa,* London, 1826, 22.3*

Deschamps, H. *Histoire de Madagascar*, Berger-Levrault, Paris, 1960, 16.4** (haki zote zimehifadhiwa)

Ellis, W., *Three Visits of Madagascar*, J. Murray, London, 1858, picha ya mbele ya jalada, kwa ruksa ya Maktaba ya Uingereza, 16.6, 16.7

Evans Pritchard, E., *The Sanusiya of Cyrenaica*, Oxford University Press, Oxford, 1949, © Oxford University Press, 17.5*

Fagg, W. B. na Pemberton, III, J. (mh. Holcombe, Bryce), *Yoruba Sculpture of West Africa*, New York, 1962, © National Museum, Lagos, 26.1

French National Museums, 17.3

Frey, Colonel, Côte *Occidentale d'Afrique*, Flammarion, Paris, 1890, 20.1*

Gamitto, A. C. P.(taf. I. Cunnison), *King Kazembe*, Atica, Lisbon, 1960, © Atica, Lisbon, 12.6*

Holt, P.M. na Daly, M., *History of the Sudan*, Weidenfeld na Nicolson, London, 1979, kwa ruksa ya The National Trust, Kingston Lacy, Bankes Mss, 14.2, kwa ruksa ya George Weidefeld na Nicolson Ltd, London, 14.3, © BBC Hulton Picture Library, 14.5

Ikime, O., *Merchant Prince of the Niger Delta: the rise and fall of Nana Olomu, Last Governor of the Benin River*, Heinemann, London, 1968, 27.2

Institut fondamental d'Afrique Noire (I.F.A.N.), Dakar, 23.2

Johnston, H.H., *British Central Africa*, Greenwood Press, London, 1897, 3.1*

Johnston, H.H., *British Central Africa*, Methuen and Co., London, 1897, uk.421, 8.2*

Julien, Ch. A., *Histoire de l'Algérie contemporaine: conquete et colonisation*, Presses Universitaires de France, Paris, 1964, 17.1**, 17.2**, 19.2**

Laroui, A., *Origines sociales et culturelles du nationalisme marocain, Maspéro*, Paris, 1977, 18.4

Lefebvre, T., *Voyage en Abyssinie* (1845-54), Paris, picha zimetolewa na Sasor Publisher, 15.2, 15.3

Ling Roth, H., *Great Benin, Its Custom, Art and Horrors*, Kings na Sons, Halifax, 1903 (nakala halisi kutoka kwa Globus, 1897. Juz. I, uk. xxii), 26.4, 26.5*

Mage, E., *Voyage dans le Soudan occidental*, Hachette, Paris, 1868, © Hachette, Paris, 23.5, 23.6

Magyar, L. *Reisen in Sud Afrika in den Jahren 1849 bis 1857*, Pest na Leipzig, 1859, 12.7*, 12.8

M'Bokolo, E., *Noirs et Blancs en Afrique équatoriale*, Editions de l;Ecole des Hautes Etudes en sciences sociales, Paris, 1981 ( picha zilitolewa kutoka du Belley, Griffon, 'le Gabon', *Le Tour du Monde*, 1865), 27.5, 27.6

Miers, S., *Britain and the Ending of the Slave trade*, Longman, London, 1975, © The Illustrated London News Picture Library, 4.2

Museum of the Institute of Ethiopian Studies, Addis Ababa, 15.7

Museum of Toulouse, © Jean Dieuzaide, Toulouse, 18.1

Museum of Versailles, photothéque, Groupe Press de la Cité, Paris, 19.1

Mutibwa, Ph., *The Malagasy and the Europeans*, Longman, London, 1974, Direction e la Presse et de la Publication, Ministére de l'Information, Madagascar, 16.2, 16.3

Nachtigal, G. (taf. na mh. Fisher, A. G. B. and H.J.), *Sahara and Sudan*, Hust, London, 1974, © Hust, London, Juz. II, 1980, 22.2*, 22.4*

National Army Museum, London, 7.2

Nigerian Information Service Centre, Ubalozi wa Nigeria, Paris, 27.3

Omer-Cooper, J., *The Zulu Aftermath*, Longman, London, 1966 (nakala halisi kutoka Gardiner, A. F., *Narrative of a Journey to the Zoolu country*, London, 1836), © Slide Centre Ltd, 1.1 (nakala halisi kutoka Livingstone, D. and C., *Narrative of an Expedition to the Zambezi*, John Murray Publishers, London, 1865), 8.3*

Photothéque, Musée de l'Homme, Paris, © 26.6

Pogge, P., *Im Reiche des Muata Jamvo, Berlin* 1880, 12.11*

Porter, A. T., *Creoledom*, Oxford University Press, Oxford, 1963, kwa ruksa ya Foreign and Commonwealth Office Library, 3.3.

Raison-Jourde, F., *Les Souverains de Madagascar*, Karthala, Paris, 1983, Fonds Grandidier du Muéee des Collections scientifiques. Tsimbazaza,Antananarivo, 16.5

Rassan, H., *Narrative of a British Mission to Theodore, King of Abyssinia*, Murray, London, 1869, picha zilitolewa na Sasor Publisher, London, 15.5, 15.6

Roger Viollet, H., © Harlingue-Viollet, Paris, 28.3

Rohlfs, G., *Meine Mission nach Abessinien*, Leipzig, 1882, picha zilitolewa na Sasor Publisher, London, 15.8

Saunders, C., *Black Leaders in African history*, Heinemann, London, 1978 (nakala halisi kutoka kwa John Aitken Chalmers, *Tiyo Soga, A Page of South African Mission* Work (Tol. 1) 1877), 3.2

Schweinfurth, G., *The Heart of Africa*, Sampson, Low, Marston, Low na Searle, London, 1873, Juz. I, Frontispiece, 12.5*, 14.4

Snouk Hurgronje, C., *Mekka in the latter part of the nineteenth century: daily life, customs and learning: the Muslims of the East-Indian Archipelago*, E.J. Brill, Leiden, 1870, © E. J. Brill, 28.2*

Stanley, H.M., *Through the Dark Continent*, Sampson, Low, Marston, Low na Searle, London, 1878, Juz. I, uk. 89, 11.2*, 11.3*, uk. 474, 11.4*, uk. 322, 11.5*

Sullivan, G. L., *Dhow chasing in Zanzibar Waters*, Frank Cass Publishers, London, 1873, © Frank Cass Publishers, 4.1*

© The Tate Gallery, London, 13.2

Vansina, J., *Art history in Africa*, Longman, London, 1984, © Staatl. Museum für Völkerkunde, Munich, 6.1, © Photo Institut des Musées Nationaux du Zaire (IMNZ), no. 73.381.1.1, 73.381.2, 70.8.2 (kushoto kwenda kulia), 12.3, © The Walters Art Gallery, Baltimore, 12.9, © Museum für Völkerkunde, Berlin, 12.10, © Werner Forman Archive, London, 20.2, © Frobenius Institut, 25.4

* kwa ruksa ya Syndics of Cambridge University Library

** kwa ruksa ya Bibliothéque Nationale, Paris.

Tunasikitika kuwa hatukuweza kupata hati miliki ya wenye pleti 27.5, 27.6 na tutafurahi kupata taarifa zozote zitakazotuwezesha kupata hati miliki hizo.

# *Wasifu wa Mradi*

*B.A. OGOT*[1]
*Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)*

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

(a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.

(b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya sehemu zote za bara ambazo mara nyingi hutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande

[1] Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wapya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.

(c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.

(d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahsusi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vote vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huthibitisha muswada wa mwisho. Inapoona kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaoonekana mrefu na mgumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika.* Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imeikataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.

Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusisitiza umuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano miongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maelewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.

# *Maelezo kuhusu Wendo*

Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na `kabla ya enzi ya Ukristo' na `-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

(i) 230 KS = - 350

(ii) 2900 KK = - 2900

1800 WK = + 1800

(iii) Karne ya tano KK = Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo

Karne ya tatu WK = Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.

# *Wanakamati wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika*

*Tarehe zilizotajwa chini zinaonyesha tarehe za kuwa wajumbe*

Profesa J.F.A. Ajayi
(Nigeria), 1971
Mhariri Juzuu VI

Profesa F.A. Albuquerque Mourao
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. Adu Boahen
(Ghana), tangu 1971
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama
(Niger), 1971- 8 (alijiuzulu 1978);
alifariki 1982

Dkt. (Blbi) Mutumba M. Bull
(Zambia), tangu 1971

Hayati Profesa P. Chanaiwa
(Zimbabwe) tangu 1975 ; alifariki 1993

Profesa P.D. Curtin
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa M. Difuila
(Angola) kuanzia 1978

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop
(Senegal),1971- 86; alifariki 1986

Profesa H. Djait
(Tunisia), tangu 1975

H.E.M. El Fasi
(Moroko), tangu 1971; alifariki 1991
Mhariri Juzuu III

Profesa J.D. Fage
(Uingereza), 1971 - 81 (alijiuzulu)

Hayati Profesa J.L. Franco
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dkt. V.L. Grottanelli
(Italia), tangu 1971

Hayati Profesa E. Haberland
(Ujerumani), tangu 1971; alifariki 1992

Dkt. Aklilu Habte
(Ethiopia), tangu 1971

Hayati H.E.A. Hampaté Bâ
(Mali), 1971 - 8; alijiuzulu
alifariki, 1991

Dkt. I.S. El-Hareir
(Libya), tanqu 1978

Dkt. I. Hrbek
(Chekoslovakia), tangu 1971
alifariki 1993
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Dkt. (Bibi) A. Jones
(Liberia); tangu 1971

Hayati Abbé Alexis Kagame
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa I.N. Kimambo
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo
(Burkina Faso), tangu 1971
Mhariri Juzuu I na IV

Bw. D. Laya
(Niger), tangu 1979

Dkt. A. Letnev
(Urusi), tangu 1971

Dkt. G. Mokhtar
(Misri), tangu 1971
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa
(Uganda), tangu 1975

Profesa L.D. Ngcongco
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane
(Senegal), tangu 1971
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),
tangu 1975

Profesa B.A. Ogot
(Kenya), tangu 1971
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary
(Madagaska), tangu 1971

Hayati Profesa W. Rodney
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dkt. E. Williams
(Trinidad na Tobago), 1976-8;
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui
(Kenya)
Mhariri Juzuu VIII,
Siyo mwanakamati

Profesa C. Wondji
(Ivory Coast)
Mhariri Msaidizi wa Juzuu VIII
Siyo mwanakamati

*Ukatibu wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi*
Kitengo cha Ushirikiano wa Kimataifa wa Utamaduni, Uhifadhi na Ukuzaji wa Tamaduni
UNESCO
1, rue Miollis, 75015 Paris

# *Wasifu wa waandishi waliochangia kwenye Toleo Kuu*

*Toleo lililofupishwa lilitayarishwa kutoka kwenye matini za toleo kuu liloandikwa na waandishi wafutao*:

SURA 1 J. J. Ajayi (Nigeria); mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi karne ya kumi na tisa, mwandishi wa machapisho mengi na makala kwenye majarida kuhusu historia ya Afrika; alikuwa Makamu wa Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Lagos, Profesa Mstaafu, Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Ibadan.

SURA 2 I. Wallerstein (Marekani); mtaalamu wa soshiolojia ya Kiafrika na mfumo wa uchumi wa dunia; mwandishi wa machapisho mengi na makala; alikuwa Profesa wa soshiolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Columbia, New York na Chuo Kikuu cha McGill, Montreal; Mkurugenzi wa Kituo cha Taaluma za Uchumi, Mifumo ya Kihistoria na Staarabu cha Fernand Braudel, SUNY, Binghamton.

SURA 3 A. Adu Boahen (Ghana); mtaalamu wa historia ya kikoloni ya Afrika Magharibi; mwandishi wa machapisho na makala mengi kuhusu historia ya Afrika; alikuwa Profesa na Mkuu wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Ghana.

SURA 4 S. Daget (Ufaransa); mtaalamu wa biashara ya utumwa Afrika kwenye karne ya kumi na tisa; mwandishi wa machapisho na makala mengi kuhusu biashara ya utumwa Afrika; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Nantes; amefariki.

SURA 5 L. D. Ngcongco (Botswana); mtaalamu wa historia ya Kusini mwa Afrika; amechapisha sana kuhusu Botswana kabla ya ukoloni; alikuwa Mkurugenzi, Taasisi ya Taifa ya Maendeleo, Utafiti na Nyaraka;, Profesa na Mkuu, Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Botswana.

SURA 6 E. K. Mashingaidze (Zimbabwe); mtaalamu wa historia ya Kusini mwa Afrika; alikuwa mhadhiri, Chuo Kikuu cha Taifa cha Lesotho na alikuwa Balozi wa Zimbabwe huko Umoja wa Mataifa; Katibu Mkuu, Harare.

SURA 7 N. M. Bhebe (Zimbabwe); mtaalamu wa historia ya Kusini mwa Afrika; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu Kindebele; alikuwa mhadhiri, Chuo Kikuu cha Swaziland; mhadhiri mwandamizi, Chuo Kikuu cha Zimbabwe.

SURA 8 A. F. Isaacman (Marekani); mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu historia ya kijamii ya Msumbiji kwenye karne ya kumi na tisa na ishirini; Profesa wa historia, Chuo Kikuu cha Minnesota.

SURA 9 A. I. Salim (Kenya); mtaalamu wa historia ya Afrika Mashariki; mwandishi wa makala mengi kuhusu watu wanaozungumza Kiswahili; Profesa na Mwenyekiti, Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Nairobi.

SURA 10 I. N. Kimambo (Tanzania); mtaalamu wa historia ya Afrika Mashariki; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia ya watu wa Tanzania kabla ya ukoloni; alikuwa Afisa Mkuu Taaluma, hivi sasa ni Profesa, Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

SURA 11 D. W. Cohen (Marekani); mtaalamu wa historia ya kianthropolojia ya Afrika kwa kutumia mbinu za anthropolojia na historia jamii kuangalia matatizo ya kihistoria ya maeneo ya ziwa kwenye karne ya kumi na tisa; anashughulikia zaidi anthropolojia na historia zilizotolewa na

Waafrika wenyewe nje ya maeneo ya kitaaluma; Profesa wa Historia na Anthropolojia, Chuo Kikuu cha Johns Hopkins, Baltimore.

SURA 12 J. L. Vellut (Ubelgiji); mtaalamu wa historia ya Afrika ya kati; mwandishi wa machapisho na makala mengi kuhusu Kongo, Jamhuri ya watu wa Kongo na Angola; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Louvain.

SURA 13 A. Badel-Malek (Misri); mtaalamu wa sosiolojia na falsafa ya jumii ya Uarabuni; mwandishi wa machapisho na makala mengi kuhusu Uarabuni na Afrika na Asia, siasa na nadharia ya jamii; Mkurugenzi wa utafiti, kituo cha Taifa cha Utafiti wa Kisayansi; Paris; Mratibu wa Mradi, Mhariri Mkuu (SCA-NNST), Chuo Kikuu cha Umoja wa Mataifa, Tokyo; mwandishi gazetini, Kairo.

SURA 14 H. A. Ibrahim (Sudan); mtaalamu wa historia ya Misri na Sudan karne ya kumi na tisa na ya ishirini; mwandishi wa machapisho na makala mengi; Profesa wa Historia na Mkuu wa Kitivo, cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Khartoum.

B.A. Ogot (Kenya); mtaalamu wa historia ya Afrika, mwasisi wa mbinu za historia simulizi; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia ya Afrika Mashariki; alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Louis Leakey; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

SURA 15 R. Pankhurst (Kingereza); mtaalamu wa historia ya Ethiopia; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia na utamaduni wa Ethiopia; alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Ethiopia, Addis Ababa, Profesa wa Taaluma za Ethiopia; Taasisi ya Taaluma za Ethiopia, Addis Ababa.

SURA 16 P. W. Mutibwa (Uganda); mtaalamu na mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia ya Madagaska kwenye karne ya kumi na tisa; Profesa wa Uchunguzi wa Historia, Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala.

SURA 17 M. H. Cherif (Tunisia); mtaalamu wa historia ya jamii na siasa ya Afrika Kaskazini; mwandishi wa makala mengi kuhusu historia ya Afrika ya Kaskazini; Profesa na Mkuu wa Kitivo cha Sayansi za Jamii, Tunis.

SURA 18 A. Laroui (Moroko); Mtaalamu wa historia ya Maghrib; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu historia ya Moroko na historia ya karne ya kumi na tisa ya Afrika ya Kaskazini; Profesa wa Historia ya Sasa, Chuo Kikuu cha Rabat.

SURA 19 N.A. Ivanov (Urusi); mtaalamu wa historia ya zamani na ya sasa ya Afrika Magharibi; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia ya sasa ya Afrika Magharibi, Mkuu wa utafiti, Tasisi ya Taaluma za Mashariki, Akademia ya Sayansi ya Urusi, Mosko.

SURA 20 S. Baier (Marekani); mtaalamu wa historia ya uchumi ya Afrika Magharibi na hususan Sahel ya Afrika Magharibi; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu uchumi wa Sahel; alikuwa Mkurugenzi Msaidizi wa Kituo cha Taaluma za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Boston; hivi sasa ni Mhandisi Mwandamizi wa Vifaa tendani huko Acces Technology, Natick, Massachusetts.

SURA 21 A.A. Batran (Sudan); mtaalamu wa historia ya Uislamu Afrika; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu Udugu wa Kidini, Usufi na Mabadiliko ya Usomi Afrika Magharibi na Kaskazini, Profesa wa Historia ya Afrika, Chuo Kikuu cha Howard, Washington, D.C.

SURA 22 M. Last (Uingereza); mtaalamu wa historia na Sodhiolojia ya Afrika; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu historia na utamaduni wa Wahausa, maisha ya kitaaluma ya Sudan Magharibi; Profesa Mshiriki kwenye Anthropolojia ya Jamii, Chuo Kikuu Kishiriki, London.

SURA 23 M. Ly-Tall (Mali); mtaalamu wa historia ya Mali; amechapisha kuhusu Himaya ya Mali na maisha ya al-Hadjdj Umar Tall. Alikuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Mali, UNESCO, alifanya kazi IFAN, Chuo Kikuu cha Dakar.

SURA 24 Y. Person (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Afrika, hasa Mandingo; amechapisha kazi nyingi kuhusu historia ya Afrika; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Paris 1, Panthéon-Sorbonne; amefariki.

SURA 25 K. Arkin (Ghana); mtaalamu wa anthropolojia jamii; hasa historia na utamaduni wa Waakan; amechapisha kazi nyingi kuhusu Asante; Profesa wa Taaluma za Kiafrika Taasisi ya Taaluma za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Ghana.

J. Ki-Zerbo (Burkina Faso); mtaalamu wa historia ya Afrika na mbinu zake mwandishi wa kazi nyingi zinazohusu Afrika ya watu weusi na historia yake; alikuwa Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Dakar, Profesa wa Historia na Mbunge, Burkina Faso.

SURA 26 A.I. Asiwaju (Nigeria); mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu Wayoruba na Waaja na athari ya mipaka ya kikoloni kwa Waafrika; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Lagos.

SURA 27 E.J. Elango (Cameroon); mtaalamu wa historia ya Cameroon; Mhadhiri Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Yaounde.

M. Metegue N'Nah (Gabon); mtaalamu wa historia ya Afrika ya Kati; Mkuu Idara ya Historia; Chuo Kikuu cha Libreville.

SURA 28 F.W. Knight (Jamaica); mtaalamu wa historia ya kutawanyika kwa Waafrika duniani; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu Cuba, jamii ya Watumwa na kutawanyika kwa Waafrika duniani, Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Johns Hokins, Baltimore.

Y.A. Talib (Singapore); mtaalamu wa Uislamu, Malay na Mashariki ya Kati, hasa Kusini-Magharibi ya Uarabuni, mwandishi wa kazi nyingi kwenye somo hili; Mkuu, Idara ya Taaluma za Kimalay; Chuo Kikuu cha Taifa cha Singapore.

P.D. Curtin (Marekani) mtaalamu na mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia ya Afrika na ya biashara ya utumwa; Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha John Hopkins, Baltimoe.

SURA 29 J.F. Ade Ajayi (Nigeria)

# 1 Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa: masuala na matumaini

## Taswira

Juzuu hili inaitazama historia ya Afrika katika karne ya kumi na tisa kabla ya kugombaniwa na nchi za Ulaya na uanzishwaji wa utawala wa kikoloni. Karne hii inastahili kutazamwa kwa undani, siyo tu kwa vile ni kipindi kilichokuja mara tu kabla ya uhuru, bali pia kutokana na matukio muhimu na mageuzi ya kimapinduzi yaliyotokea katika kipindi hicho. Ni muhimu kuanza kwa kuzitazama sifa za ujumla za karne ya kumi na tisa na umuhimu wake kwa ujumla katika historia ya Afrika ambayo imejadiliwa sana.

Ukiilinganisha karne hii na zile zilizotangulia, utaona kuwa vyanzo vya historia ya Afrika vilikuwa vingi zaidi katika karne ya kumi na tisa. Kulipatikana vyanzo vipya vilivyotokana na masimulizi ya wasafiri, wamisionari, wafanyabiashara, wajumbe wa kibalozi na mawakala wengine wa serikali waliojipenyeza bara, aghalabu kwa mara ya kwanza. Maandishi mengi kuhusu Afrika ambayo hayakuwa yamefahamika awali yaligunduliwa. Lugha nyingi za Kiafrika zilianza kuandikwa katika maandishi ya Kizungu. Baadhi ya Wazungu na mawakala wao wa Kiafrika walipendezewa na mapokezi ya historia ya jumuiya mbalimbali na wakaanza kuyarekodi. Pamoja na kazi hii bado dhana potofu zilibuniwa kwamba jamii za Kiafrika zilikuwa zimedumaa na kwamba hapakuwepo na mageuzi yoyote ya maana yaliyotokea kabla ya kuanzishwa kwa ukoloni. Mara tu baada ya dhana hiyo potofu kuvunjwa, ikaja dhana nyingine kwamba mageuzi yote muhimu katika historia ya Afrika yalitokea mnamo karne ya kumi na tisa. Dhana hii potofu nayo ilipobatilishwa kama inavyodhihirishwa na matendo na matukio muhimu yalivyorekodiwa katika majuzuu ya UNESCO yaliyotangulia ya *Historia Kuu ya Afrika,* ilianza kudaiwa kuwa mageuzi yaliyotokea katika karne ya kumi na tisa yalikuwa ya aina tofauti na mageuzi yaliyotokea kwenye karne zilizotangulia kwa vile yalisababishwa na msukumo wa kutoka nje.

Kwa sababu ya mazoea ya kuelezea mageuzi ya Afrika ya karne ya kumi na tisa kwa kutazama zaidi shughuli za Wazungu zilizokuwa zikiongezeka katika bara hili, karne ya kumi na tisa mara nyingi imeshughulikiwa kama kitangulizi tu cha kipindi cha ukoloni. Maendeleo yote muhimu yaliyofanyika kwenye bara zima katika kipindi hiki, yameelezewa kama matokeo ya Wazungu kuingiliana na Waafrika na pia kama dalili ya

kipindi cha ukoloni. Katika kujaribu kutoa maelezo ya ujumla, wanazuoni mbalimbali waliangalia zaidi maendeleo yaliyotokea Ulaya badala ya michakato ya ndani na mwelekeo wa kihistoria wa ndani ya jamii za Kiafrika. Hii ndio maana, kwa mfano, mabadiliko nchini Misri yanaelezewa kama matokeo ya matendo ya Napoleon Bonaparte na wala sio matokeo ya matarajio ya wananchi. Vilevile, Mfekane nchini Afrika ya Kusini inaelezewa, sio kama matokeo ya mageuzi ya ndani ya jamii ya Wanguni, bali kama mageuzi yanayotokana na kuwepo kwa Wazungu.

Kwa hiyo, madhumuni ya sura hii ni kuangalia hali ya Afrika katika karne ya kumi na tisa, sifa za ujumla za kipindi hicho, mwendelezo wa mambo ya kipindi cha nyuma, mageuzi na mambo mapya yaliyotokea katika kipindi hicho, pamoja na mwelekeo mpya kwa siku zijazo. Ni muhimu kuangalia ni kwa kiasi gani mageuzi katika karne ya kumi na tisa ni mwendelezo wa maendeleo ya karne ya kumi na nane. Vilevile yafaa kuangalia ni kwa kiasi gani mageuzi hayo yalitokana na mambo ya ndani ya nchi na kwa kiasi gani yanatokana na upanuzi wa shughuli za watu wa Ulaya na ushirikishwaji wa uchumi wa Afrika katika mfumo wa dunia. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuelewa vema mkondo wa maendeleo ya Afrika katika karne ya kumi na tisa na umuhimu wa Ulaya kwa maendeleo au udunishaji wa maendeleo ya Afrika.

## *Demografia na misafara ya watu*

Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, Waafrika walikuwa wamegawanyika katika makundi tofauti ya kitamaduni na kilugha, na kila kundi lilikalia eneo lenye mipaka maalumu. Mchakacho wa kujitambulisha kiutamaduni ulikamilika katika maeneo mengi ilipofikia karne ya kumi na sita. Hata hivyo, maeneo mengine katika Afrika Mashariki (nje ya uwanda wa juu wa ukanda wa Maziwa Makuu) na Bukini bado kulikuwa na uhamaji mkubwa wa watu kuelekea kwenye maeneo ambayo hayakuwa na watu wengi katika karne ya kumi na saba na kumi na nane. Lakini, kufikia mwaka 1800, utulivu ulipatikana katika ukanda huu.

Wakati miguro, kwa maana ya misafara mikubwa ya watu katika eneo kubwa la nchi, katika Afrika inaweza kusemwa kuwa ilikoma mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, bado watu waliendelea kuhamahama ili kukidhi haja ya shughuli zao. Mfano wa watu kama hao ni wafugaji waliotafuta malisho, wafanyabiashara na mafundi stadi waliosafiri kwenda mbali na kuunda makazi mapya wakati wakifanya biashara zao. Wengine ni wawindaji waliokuwa wanazunguka huko na huko kutafuta wanyama. Misafara hiyo haikutelekeza kabisa makazi ya awali au kusambaratisha watu. Misafara hiyo ilikuwa ya kawaida na kwa kawaida ilifanyika kwa kuzungukia eneo fulani maalumu. Hata hivyo matokeo fulani fulani kama vile ukame, maradhi ya kufisha, vita na kuvunjika kwa dola zilizokuwepo na wingi wa watu katika eneo, kulisababisha misafara ya watu kuondoka moja kwa moja kutoka kwenye eneo lao la asili. Mfano wa misafara ya aina hii katika karne ya kumi na tisa ni kama ile ya Wa-Fang katika ukanda wa misitu ya Ikweta barani Afrika, Wachokwe wa Angola, Wayoruba wa Oyo ya Kale na msafara wa Mfekane miongoni mwa Wanguni wa kaskazini wa Natal katika eneo la Kusini mwa Afrika.

Inasemekana kuwa idadi ya watu katika Afrika kabla ya mwaka 1800 isingeweza kuongezeka sana, na imedaiwa kwamba kila mwaka kati ya kila watu kumi elfu kulizaliwa watu hamsini zaidi ya wale waliokufa. Kwa kiwango hicho, idadi ya watu ingaliweza kuongezeka maradufu katika kipindi cha miaka elfu moja. Makadirio haya yanathibitishwa na hali ya Afrika Kaskazini ambako kilimo shadidi cha umwagiliaji maji kingeongeza sana idadi ya watu, lakini haikuwa hivyo kwa sababu ya kutokea vipindi vya tauni na ukame. Lakini katika maeneo ya nyanda za majani na misitu ya Afrika Magharibi, Kati, na Kusini, ukuzaji wa njia za kilimo (mara nyingi ufugaji ukiwa kwenye nyanda za majani) ulisababisha ongezeko la watu na msongamano wa watu katika baadhi ya maeneo kama vile kwenye nchi ya Waigbo, Kusini Mashariki mwa Nigeria, nyanda za majani za Kameruni na Ukanda wa Maziwa Makuu wa Afrika Mashariki.

Hata hivyo, katika maeneo haya, hususani Afrika ya Magharibi, na Magharibi-Kati, katika karne ya kumi na saba na kumi na nane, ukuaji wa idadi ya watu uliathiriwa zaidi na biashara ya watumwa. Ni dhahiri kuwa athari za biashara hiyo hazikulingana. Baadhi ya dola ziliitumia hali ya kuwepo kwa biashara ya watumwa kujiimarisha na kuwadhoofisha majirani zao. Dola dhaifu zilizoshindwa kujilinda ndizo zilizoathirika sana na kupoteza idadi kubwa ya watu; athari ambayo inaonekana hadi leo. Watu wengi walitelekeza makazi yao yaliyokuwa kwenye ardhi yenye rutuba, na jamii zilizobakia zilijaribu kujitafutia maisha kwenye maeneo magumu ya milimani.

Athari za ujumla za upunguaji wa idadi ya watu kutokana na biashara ya watumwa zilikuwa mbaya sana kwa Afrika yote. Kuanzia mwaka 1650 hadi 1850, idadi ya watu wa Afrika ilikuwa inapungua na kwamba kiwango kidogo cha uchumi wa Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa kwa kiasi kikubwa kilikuwa ni matokeo ya kupungua kwa idadi ya watu. Hata dola zenye nguvu ambazo zilifikia umaarufu na kupata maendeleo zaidi ya ndani zilidumaa kwa sababu ya kufukarika kwa majirani zao. Kwa hiyo, biashara ya watumwa ndiyo ilikuwa sababu ya udhaifu wa mfumo wa dola, na kutetereka na kudhoofika kwa mifumo ya siasa na uchumi katika Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Kukua kwa idadi ya watu katika karne ya kumi na tisa hakukuwa kwa haraka kwa sababu kampeni za kukomesha biashara ya watumwa zilichukua muda mrefu kufanikiwa. Ilikuwa baada ya mwaka 1850 ambapo palikuwa na punguzo kubwa la idadi ya watumwa waliosafirishwa nje kuvuka bahari ya Atlantiki. Wakati huo huo, upelekaji wa watumwa Zanzibar na Bahari ya Hindi uliongezeka. Aidha, kuongezeka kwa bidhaa mbadala za kupeleka nje kama vile mafuta ya mawese, mpira na pembe za ndovu kuliongeza mahitaji ya watumwa wa ndani waliotumika katika kutafuta bidhaa hizo mpya na kuzisafirisha hadi pwani. Kwa hiyo utumwa wa ndani uliongezeka sana katika karne ya kumi na tisa, na uliambatana na kupoteza maisha ya watu wengi katika vita na katika uvamizi wa kukamata watumwa. Kutokana na kukomeshwa kwa biashara ya watumwa ya nje, idadi ya watu wa Afrika ikaanza kukua kwa mara ya kwanza tangu karne ya kumi na saba. Idadi ilipungua tena kutokana na athari za mwanzo za utawala wa kikoloni na vita vya upinzani kabla ya kuanza kupanda tena polepole mwanzoni, na kisha kwa kasi, kuanzia miaka ya 1930.

## *Shauku ya mataifa ya ulaya yaongezeka*

Hali hii ilijidhihirisha kwanza kutokana na safari za ugunduzi zilizofanywa ili kupata taarifa sahihi kuhusiana na sura ya nchi ya Afrika pamoja na bidhaa zake kuu za kilimo na viwanda. Sababu ya kuingilia mambo ya Afrika ilitokana kwanza na jitihada za Uingereza za kuzuia upanuzi wa Ufaransa wakati wa Mapinduzi ya Ufaransa na vita vya Napoleon ambavyo vilienea hadi barani Afrika, na pili, kukomesha biashara ya watumwa. Wafaransa walikuwa wamekwishaingia Aleksandria, na Kairo nchini Misri. Mwaka 1789, Waingereza waliyabadilisha makazi ya watumwa huru huko Freetown kuwa koloni la Uingereza. Kisha walikamata koloni la Waholanzi pale Cape of Good Hope Rasi ya Tumaini Jema, mwaka 1795. Wafaransa walifukuzwa kutoka Misri na wakalazimishwa kuunga mkono jitihada za kukomesha utumwa. Jambo hili liliwachochea kuanzisha ngome sehemu za pwani na vituo vya biashara huko Afrika Magharibi.

Ushindani wa muda mrefu wa Waingereza na Wafaransa pamoja na kampeni za kusimamia upigaji marufuku wa kusafirisha nje watumwa kutoka Afrika ukawa ndio msingi wa kukua kwa shauku na Ulaya na Marekani juu ya Afrika. Hata hivyo, ni lazima tuepuke kutilia chumvi ukubwa wa mafanikio yao katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Ukomeshaji wa utumwa ulihitaji kupita mara kwa mara kwa meli za kivita za Kiingereza, Kifaransa, na Kimarekani, kukagua bahari na kujaribu kuweka vizuizi. Wanamaji walihitaji kuwa na vituo pwani. Hali hii ilichochea wafayabiashara waliotaka kupata faida katika kipindi hiki cha mpito kutoka biashara ya watumwa hadi kwenye biashara ya karanga, mafuta ya mawese, mpira, karafuu, pembe za ndovu au bidhaa nyingine. Hali hii pia ilitoa fursa kwa wamisionari waliotaka sio kuwaingiza katika Ukristo watu wa pwani tu, bali pia watu wengi zaidi wa bara.

Wareno walidai maeneo makubwa ya nchi za Angola na Msumbiji, jambo ambalo walihimizwa na Uingereza mara kwa mara kwa madhumuni ya kuwazuia Wafaransa. Lakini, walipata shida kubwa katika kudumisha ngome zao pwani au kuweka usalama kwenye njia zilizoelekea kwenye mashamba yao makubwa (*prazos*) waliyoyaanzisha huko bara. Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, walitegemea zaidi wafanyabiashara machotara wa Kiafrika (*pombeiro*), na urafiki wa watawala wenyeji, katika kufanya biashara na watu wa bara.

Baada ya mwaka 1815, Wafaransa walihuisha vituo vyao vya kibiashara huko Senegambia, hususani Saint-Louis na Gorée nje kidogo ya pwani ya mji wa baadaye wa Dakar. Jitihada za kuanzisha makazi ya kilimo huko bara zilishindikana. Waliukamata mji wa Algiers mwaka 1830 na ilibidi washindane na upinzani wa Waalgeria wakiongozwa na Amiri Abd al-Kadir kwa zaidi ya miaka 20. Mpango wa kuwapa makazi watumwa walioachiwa huru kwenye vijiji vya kilimo kuzungukia Freetown ulifanikiwa sana. Mafanikio haya yalitokana kwa kiasi kikubwa na kazi zilizofanywa na wamisionari wa Kidachi na Kiingereza ambao walitoa huduma kama waalimu, wanaisimu, mameneja wa mashamba na wasimamizi. Kulikuwa na jitihada za kutekeleza mpango wa Freetown mahali pengine kwa kiwango kidogo, kwa mfano huko Liberia chini ya Wamarekani, Libreville chini ya Wafaransa, na Freretown karibu ya Rabai,

Afrika Mashariki, chini ya Waingereza. Kuenea kwa Wakrioli kutoka Freetown hadi miji mingine ya pwani kama vile Banjul (awali ukiitwa Bathurst), Cape Coast, Badegry, Lagos na mbali zaidi kulisaidia kueneza shughuli za kimisionari na kibiashara za Waingereza.

Athari za kimisionari zilienea pia Afrika Kusini, lakini jitihada za kukuza uchumi hazikufanikiwa sana. Wakulima wa Kikaburu waliendelea kuchukia utawala wa Kiingereza, hususani ukomeshaji wa watumwa na jitihada za kurekebisha uhusiano wao na Waafrika. Makaburu wakaidi walisafiri safari ndefu na ngumu hadi bara ili kujinufaisha kutokana na vuguvugu la Mfekane. Lakini walichofanikiwa kukifanya ni kuukokota utawala wa Kiingereza nyuma yao. Kwa hiyo hadi mwaka 1850 Afrika Kusini íkabakia kuwa ni koloni la wakulima mafukara wa Kiingereza na Kikaburu, waliosambaa katika vikundi vidogo vidogo baina ya dola za Kiafrika, huku maafisa wa kikoloni wa Kiingereza wakiwa kama wapatanishi wenye kupendelea upande mmoja. Ugunduzi wa dhahabu na almasi na matumaini ya uchumi wa viwanda yalikuwa ni matukio ya baadaye. Vilevile, shughuli za kimisionari hazikuwa kichocheo kikuu cha mageuzi katika Afrika hadi ilipofikia nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa. Shirika la Roho Mtakatifu (*Holy Ghost*) lilianzishwa mwaka 1847 na lile la Mapadre Weupe (*White Fathers*) lilianza mwaka 1863. Mnamo mwaka 1850, David Livingstone alikuwa bado yuko kwenye safari ya kwanza ya kimisionari.

Athari za kibiashara za Ulaya zilienea pengi na kwa haraka kuliko athari za kimisionari katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Hii ilitokana na ukweli kwamba biashara ya Ulaya katika karne ya kumi na tisa ya bidhaa za kilimo na nyinginezo iliyojulikana kama biashara halali ilitokana na biashara ya watumwa iliyofanyika kabla ya karne ya kumi na tisa. Wadeni na Waholanzi waliendelea na biashara hata baada ya zama za biashara ya watumwa kuisha na hawakuondoka mpaka Waholanzi walipouza ngome yao ya Akkra mwaka 1850 na kusalimisha Kasri ya Elmina mwaka 1871.

Mfumo wa biashara mpya ulikuwa sawasawa na ule wa zamani. Watu walewale walioendesha biashara ya watumwa, haohao ndio walioanzisha biashara mpya. Vilevile mfumo wa kuaminiana na kutoa bidhaa kwa mkopo kwa wafanyabiashara wa Kiafrika uliotumika kwenye biashara ya watumwa ulikuwa pia ndio msingi wa biashara mpya. Wazungu walibaki pwani na kufanya kazi na walanguzi wa Kiafrika waliochukua bidhaa kupeleka bara na kurudisha mazao pwani. Uendeshaji na mahitaji ya biashara mpya yaliathiri mfumo wa kijamii wa baadhi ya dola za pwani. Biashara mpya, athari za kimisionari na elimu ya Ulaya hususani miongoni mwa watumwa huru waliorudishwa, ilikuwa inajenga tabaka jipya la watu bora. Baadhi yao ambao walijirundikia utajiri walitaka kushiriki kwenye kutawala. Hata hivyo, hali hii haikuleta mageuzi ya haraka katika muundo wa jamii, au katika kuachana na ukale, kwa sababu watu hao kwa ujumla ilibidi watumie utajiri wao kupata vyeo vya uchifu wa kijadi, na kwa kupitia vyeo hivyo kujipatia madaraka ya kisiasa.

Kwa maneno mengine, upanuzi wa biashara ya Ulaya ulitegemea zaidi mifumo ya biashara ya ndani ya Afrika iliyokuwepo. Mifumo ya biashara ya ndani haikutegemea

sana vichokoo vya nje bali vichokoo vilivyokuwepo miongoni mwa jamii za Kiafrika kama vile mfumo wa uzalishaji wa kilimo, ufundistadi na uzalishaji viwandani. Biashara ya nje ilikuwa muhimu kwa baadhi ya watawala ambao waliiona kama chanzo kikuu cha kupatia bunduki. Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, biashara ya nje haikuwa muhimu sana katika maisha ya Waafrika wengi. Kwa hali hiyo, pamoja na kukua kwa biashara ya nje, Waafrika walitumia nguvu zao zaidi kwenye kilimo kuliko biashara.

## *Mifumo ya Kilimo*

Msingi wa uchumi wa jumuiya zote za Kiafrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa ulikua ni kilimo. Shughuli zote nyingine ikiwa ni pamoja na biashara, siasa, dini, ufundisadifu, ujenzi, uchimbaji madini na uzalishaji viwandani zisingewezekana kufanyika bila kilimo. Kwa hakika, mfumo wa kilimo uliathiri mfumo wa mahusiano wa kijamii, ruwaza za mamlaka, uhusiano na majirani na hata namna jumuiya za Kiafrika zilivyokabiliana na vichokoo vya nje kama vile biashara. Ni muhimu kuzitazama sifa kuu za mifumo ya kilimo ya baadhi ya jamii za Kiafrika zilizokuwepo mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa ili kusisitizia kiasi cha mwendelezo wa mambo ya nyuma. Zipo sehemu chache ambazo zingaliweza kuwa mbali kupita ilivyo kwa Bunafu iliyoko Busoga kaskazini, Afrika Mashariki. Watu walihamia kwenye eneo hilo mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Waliishi kwenye nyumba zilizotawanyika na wala sio kama jumuiya kwenye vijiji. Kulikuwa hakuna soko rasmi la kuuziana bidhaa lakini kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kijamii, polepole watu wakajenga moyo wa kijumuiya. Kaya ilikuwa ndio kitengo cha uzalishaji na umilikaji wa ardhi. Hata hivyo, pamoja na umbali kati ya nyumba hizo, mfumo wa kubadilishana bidhaa ukajitokeza polepole, ukionyesha kuwa kaya hata kule Bunafu zilikuwa hazijitoshelezi. Mageuzi ya kijamii yalitokea Bunafu katika karne ya kumi na tisa kuhusiana na upanuzi wa biashara na mabadiliko ya kijamii na kisiasa yaliyoambatana nayo. Lakini yote haya yaonekane sio tu kama matokeo ya vichokoo vya nje lakini kama mwendelezo na matunda ya mielekeo na ruwaza mifumo ziliyorithiwa kutoka karne ya kumi na nane. Hii ni pamoja na dhana ya utaratibu (wa kijamii), na mfumo wa serikali wa utawalamsonge ambao wahamiaji walikuja nao kutoka kwenye madola waliyoyahama.

Kilimo katika vijiji na maeneo ya shamba ya Tunisia kilikuwa tofauti na kile cha Bunafu, sio tu kutokana na aina ya udongo na aina ya mazao yaliyopandwa, bali zaidi ni kutokana na mfumo wa umilikaji ardhi. Katika nyanda zenye rutuba za Tunisia, jangwa haliwi mbali sana, kwa hiyo kilimo shadidi cha kwenye Oasisi ndicho kilichowezekana. Umilikaji wa ardhi ulitawaliwa na sheria ya Kiislamu ambayo watawala katika maeneo ya mijini na machifu wenyeji kwenye maeneo ya vijijini waliitafsiri tofauti. Msingi mkuu ulikuwa kwamba ardhi ilimilikiwa kwa pamoja na jumuiya nzima na kwamba watawala waliigawanya ili itumiwe, na makadhi ilisuluhisha ugomvi juu ya ardhi hiyo. Mijini, shinikizo la wingi wa watu lilichochea biashara ya ardhi. Shinikizo hili lilionekana kuongezeka vijijini na kwenye maeneo ya

shamba. Lakini katika nusu ya kwanza yote ya karne ya kumi na tisa, mfumo wa kijadi, kwamba ardhi haiwezi kununuliwa na kuuzwa, ulidumu. Kadhalika, kama ilivyokuwa Bunafu, kaya zilikuwa ndio vitengo vya uzalishaji na umilikaji wa ardhi. Masoko yalikuwepo ila kaya ziliendelea kuuziana mazao kwa biashara ya kubadilishana.

Katika maeneo ya kilimo ya kuzunguka Kano, madaraka ya mtawala mkuu au Amiri yalidhihirika zaidi kuliko katika vijiji vya Watunisia. Kano ilikuwa kitovu cha biashara ya wenyeji na ya kimataifa iliyohusu utengenezaji wa nguo na utiaji rangi katika nguo na katika ngozi. Wafanyabiashara na watawala wa Kano walifanya kazi kubwa katika kusimamia uchumi hadi sehemu za mashambani. Lakini uzalishaji mkubwa wa kilimo ulikuwa mikononi mwa wanakijiji. Kaya ilikuwa ndio kitengo cha uzalishaji na wanakaya wote walishiriki katika kilimo na kazi za jumuiya. Ardhi ilikuwa chini ya uangalizi wa mtawala ambaye alidhibiti upatikanaji wake, matumizi na uuzaji wake. Watawala wachapakazi walitumia nafasi hii kuigawa ardhi na kuwahimiza mafundistadi na mafundi mchundo kukaa ndani au karibu na Kano. Zaidi ya hayo, watawala pamoja na baadhi ya wafanyabiashara waliendeleza mashamba makubwa kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo na viwanda. Jihadi ya mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, iliyopelekea kuanzishwa kwa serikali ya Kiislamu, ilileta matumizi ya sharia za Kiislamu kwenye umilikaji wa ardhi. Lakini utaratibu wa kilimo na umilikaji wa ardhi wa karne ya kumi na nne haukuachwa ghafla. Badala yake, maamiri wapya wa Kifulani waliingiza polepole desturi na kaida za Kihausa, jinsi karne ilivyokuwa inaingia.

## *Mifumo ya utawala*

Kimsingi, kulikuwa na mifumo miwili ya utawala katika Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Mfumo mmoja ulikuwa wenye serikali kuu, utawala msonge, utaratibu unaoeleweka na utozaji ushuru, ambao ulionekana kwenye falme na dola zenye serikali kuu. Mfumo wa pili ulikuwa usio wa mabavu na wenye serikali zisizo rasmi za mabaraza ya wazee na watu maarufu ulioonekana kwenye jamii zisizo na mamlaka kuu. Mifumo hii miwili isionekane kama yenye kupingana bali kama kitu kimoja chenye pembe mbili tofauti ambapo dola nyingi huangukia sehemu ya katikati na kuchukua baadhi ya sifa za kila upande. Hakukuwa na jamii isiyo na dola kwa sababu hata kwenye jamii za ndani kabisa ambazo hazina mamlaka kuu kama tulivyoona kwa Bunafu, kulikuwa na hali ya ujumuiya na serikali yenye utaratibu. Jumuiya nyingi ambazo hazikuunganishwa na mamlaka kuu ziliunda vikundi vya ushirika, vyama vya marika, klabu za siri, makundi ya jando, nyago, na asasi nyingine ambazo huvuka mipaka ya koo ambazo zilitumika kuunda umoja na kudumisha amani. Mfano mzuri unaojulikana sana ni ule wa Waaro ambao walidumisha amani katika eneo kubwa miongoni mwa Wa-igbo na watu wengine wa kusini mashariki mwa Nigeria kwa kupitia mtandao wa kikanda wa wafumu na makazi ya kibiashara.

Hata hivyo, maendeleo mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa yameonyesha upendeleo wa miundo-unganifu ya madaraka yenye watendaji badala ya viongozi wa kimila. Himaya kubwa ambazo hazikuwa na uongozi wa kati ziligawanyika kwenye himaya ndogondogo za kimabavu zaidi. Miliki mpya ya Khalifa wa Sokoto ilikuwa



1.1 *Dansi la Sherehe huko Mbelebele, kambi ya jeshi la Wazulu 1836*

kubwa na iliyosambaa sana. Khalifa mwenyewe alidumisha utawala wa kidini na madaraka kamili ya kiserikali yalikuwa chini ya maamiri. Nchini Afrika Kusini, Wasotho-Tswana waliishi kwenye vijiji na tawala za kichifu ambapo watawala waliziweka pamoja shughuli za jando. Wanguni wa kaskazini waliishi kwenye kaya zilizotawanyika na machifu wao wakiwa na madaraka madogo tu. Hata hivyo, maendeleo yaliyoongezeka katika kipindi cha kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na nane, pamoja na kuanzishwa kwa zao la mahindi, yalitoa shinikizo kubwa kwenye ardhi. Mfumo wa kilimo ambao ulifanya ng'ombe wapate malisho machungu wakati wa mvua na malisho matamu mwishoni mwa kiangazi haukuhimili shinikizo hilo. Hali hii ilileta mashindano makubwa katika kumiliki ardhi na ng'ombe. Kadhalika, ilisababisha kuigwa kwa sherehe za Wasotho-Tswana za kufanya shughuli za jando kwa pamoja, kwa ajili ya kuandikisha askari jeshi. Haya yalikuwa ni mapinduzi ya Mfalme Shaka yaliyochochea hali ya Mfakane.

## *Uwezo wa ndani*

Mwanzoni mwa nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, shughuli za mataifa ya Ulaya

zilikuwa zaidi sehemu za pwani. Hata hivyo, vuguvugu kuu za kimapinduzi zilianzia bara: vuguvugu la jihadi huko Afrika Magharibi, Mfekane huko Afrika Kusini, Muungano wa Ethiopia, upanuzi wa Imerina huko Bukini, na kuanguka kwa himaya ya zamani ya Oyo huko kusini-magharibi mwa Nigeria. Inaoneka wazi kwamba vichokoo vya ndani kama vile mageuzi katika jamii, mifumo ya kilimo cha uzalishaji, na biashara ya ndani vilikuwa muhimu zaidi kuliko vichokoo vya nje kama vile ukomeshaji wa utumwa, kuongezeka kwa Wazungu na biashara katika kuzusha vuguvugu hizo. Hata mageuzi ya Muhammad Ali katika Misri, japo yalianzia kwenye pwani ya Kairo, yalitokana na mapambano ya kupigania uhuru ambayo chanzo chake ni katika karne ya kumi na nane kabla ya Napoleon kuja Misri. Mashehe maarufu wa Misri walikusudia kupambana na utawala wa Kituruki na wangeona afadhali kumuunga mkono Pasha wa Albania anayeyathamini mapambano hayo ya kitaifa kuliko kukubali kurejeshwa kwa utawala mbaya wa Kituruki.

Inaonekana dhahiri kwamba katika sehemu nyingi za Afrika, na katika miktadha tofauti kihistoria, kitamaduni, kidini na kiuchumi, kulikuwa na tamaa kubwa sana ya mageuzi. Ilikuwa ni kutokana na hali hii, japo kulikuwa na shaka nyingi, watawala kadha wa Kiafrika waliwakaribisha kwa tahadhari Wazungu, wakitarajia kunufaika na kuwepo kwao kwa kuimarisha madaraka yao na ubora wa majeshi yao. Kwa sababu hizo hizo, wengi waliwakaribisha wamisionari na mawakala wao huku wakijaribu kupunguza athari zao za kijamii na kiutamaduni. Karne ya kumi na tisa inaweza kuitwa Zama za Afrika za Maendeleo Zaidi. Wazungu walitumia nafasi hii ya tamaa ya mageuzi kujiimarisha na mwishowe kutumia hali hiyo kuleta utawala wa kikoloni na kuzima juhudi za ndani za kuleta mageuzi na maendeleo.

## *Hitimisho*

Vichocheo vipya vya mageuzi vilianzishwa katika historia ya Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Baadhi ya vichocheo muhimu vilikuwa ni kampeni dhidi ya biashara ya watumwa, utafutaji wa bidhaa mpya za biashara na juhudi mpya za wamisionari. Yote haya yaliongeza kuwepo kwa Wazungu. Hawa Wazungu walikuja kufanya biashara lakini mwishowe waliingilia kati maisha ya kijamii, kiuchumi na kidini ya watu. Biashara mpya ilipanua shughuli za kibiashara kwa kuongezea kichocheo kwenye mfumo wa biashara uliokuwepo. Kwa hiyo, biashara mpya ilitokana na biashara za Kiafrika na mifumo ya kilimo ya kipindi cha kabla ya karne ya kumi na tisa. Mwendelezo wa mambo ya karne ya kumi na nane pamoja na vichocheo vya ndani vya mageuzi katika karne ya kumi na tisa, ndivyo vilivyokuwa muhimu zaidi kuliko vichocheo vya nje vilivyowakilishwa na kuwepo kwa Wazungu na biashara mpya.

# 2

# Afrika na uchumi wa dunia

## *Kuanzia mifumo ya biashara za `kifahari' hadi biashara `muhimu'*

Mgawanyo wa Afrika mwishoni mwa karne ya kumi na tisa lazima uonekane kama matokeo na wala sio chanzo cha kuishirikisha Afrika ndani ya uchumi wa dunia. Ushirikishwaji huu unaweza kusemwa kuwa umeanza katikati ya karne ya kumi na nane na kuanzisha mageuzi makubwa katika uchumi wa Afrika.

Kabla ya mwaka, 1750, Afrika ilikuwa na viungo bayana vya kibiashara na dunia ya nje. Kulikuwa na mtandao wa kibiashara uliotoka nje ya mipaka ya Bara hili na kuvuka Bahari za Mediterania, Hindi na Atlantiki. Hata hivyo, biashara hii ya mbali ilikuwa hasa ni kwa ajili ya kubadilishana bidhaa za kifahari kama vile dhahabu, shanga, ngozi na chumvi, ambazo zilikuwa chache lakini zenye faida kubwa. Biashara hizi zilikuwa ni sehemu ndogo sana ya bidhaa zinazozalishwa katika eneo hilo na ni watu wachache sana waliozalisha bidhaa hizi. Biashara ya aina hii inaweza kuelezewa kuwa haikuwa muhimu kwa maana kwamba kwa pande zote mbili, kuingiliwa au kuachwa kwa biashara hii kungeweza kutokea bila kuathiri msingi wa shughuli za uzalishaji.

Ruwaza ya biashara ya kuvuka Bahari ya Hindi haikubadilika sana kati ya mwaka 1500-1800. Mawanda na aina ya biashara haikubadiliwa hata walipokuwepo Wareno na Wazungu wengine katika eneo hilo. Baadhi ya Wazungu hao walijaribu kilimo cha mashamba makubwa katika bonde la mto Zambezi. Tofauti iliyokuwepo baina ya biashara ya mbali ya kifahari na kilimo cha mazao yasiyo ya biashara ilibaki palepale.

Katika Afrika Magharibi na Kati, kulianzishwa biashara ya mbali ya watumwa. Biashara hii ya watumwa ilikuwa ni matokeo ya mfumo wa uchumi wa kibepari wa dunia, ambao chanzo chake kilikuwa Ulaya. Ukanda wa Karibiani wa Amerika ya Kusini ambako mashamba makubwa mengi yalianzishwa ulikuwa ni sehemu ya maeneo ya pembezoni ya mfumo huu wa uchumi wa kibepari. Watumwa kutoka Afrika ya Magharibi na kati walitumiwa kutunza mashamba hayo. Idadi ya Waafrika waliosafirishwa kwenda Karibiani kwa kupitia biashara ya watumwa ilipanda polepole kati ya mwaka 1450 na 1650, na ilipanda kwa haraka zaidi kati ya mwaka 1650 na 1750, wakati idadi ya watumwa ilipoongezeka mara tatu. Mtindo wa uzalishaji na mfumo wa kisiasa ulirekebishwa ili kukidhi mahitaji ya biashara ya watumwa. Kwa mfano, ununuzi wa Waafrika kama watumwa ulirasimishwa, na hali hii ikaathiri mahusiano ya kijamii na mfumo wa siasa. Ni vigumu kusema kwa uhakika ni wakati gani hasa urekebishaji

huu ulifikia hatua ambapo biashara hii ilikoma kuwa ya bidhaa za kifahahari, ikawa ya bidhaa muhimu. Lakini inawezekana kuwa haikuwa kabla ya mwaka 1750, wakati kiwango cha biashara kilipoongezeka kwa kasi kubwa. Kipindi kati ya 1600 na 1750, kwa dunia ya kibepari, kilikuwa ni cha kuhesabu faida na mafanikio yao na kujaribu kujiendeleza juu ya mafanikio waliyoyapata katika maeneo ambayo yalikwisha shirikishwa (katika mfumo huo) katika karne ya kumi na sita. Upanuzi na ushirikishaji wa maeneo mengine ulikuja baada ya mwaka 1750.

## *Kuenea kwa Ubepari*

Afrika iliingizwa ndani ya mfumo wa dunia wa kibebari sambamba na Urusi, himaya ya Ottoman, India na nchi zilizobaki za Amerika ya Kusini kati ya mwaka 1750-1850. Wakati Afrika ilipokuwa inaingizwa kwenye mfumo wa uchumi wa dunia, haikuwa na uchumi mmoja ijapokuwa ilikuwa na ruwaza za uchuni wa kikanda ziliyovuka mipaka ya jumuiya moja moja. Ushirikishwaji wake katika ubepari wa dunia haukuleta tu mageuzi katika sekta muhimu za uzalishaji bali pia katika mfumo wa siasa wa maeneo hayo. Hali hii ilijumuisha udhoofishaji wa mifumo ya siasa iliyokuwepo na kuanzisha mifumo mipya ya kikoloni juu yake; ijapokuwa hatua hii ya pili ilichukua muda mrefu kukamilika. Ushirikishwaji huu haukufanyika mara moja. Ilikuwa ni kazi ya polepole ambayo haikufuta mara moja taratibu za awali zilizoshika za kilimo, na fikra za zamani na amali zilizoambatana nazo. Kilichofanyika kilikuwa ni kwamba uzalishaji wa bidhaa muhimu ulielekezwa kwenye soko la dunia. Hii ilimaanisha uundaji upya wa nguvu kazi ambayo ilizalisha bidhaa zenye faida. Yote haya yalikuwa ndio msingi wa kiuchumi wa ushirikishwaji katika uchumi wa kibepari na athari zake za kisiasa.

Ni muhimu kutaja kuwa Afrika haikujichagulia kuingizwa kwenye uchumi wa dunia. Afrika ilikumbwa tu na matukio, licha ya upinzani, na kufikia mwaka 1850 ilikuwa tayari imekwisha ingizwa kwenye mfumo wa dunia. Ushirikishwaji huu haukuanzia na kuacha biashara ya watumwa na kuhamia kwenye biashara halali. Ushirikishwaji haukutegemea mabadiliko hayo, na ulifanyika hata kwenye maeneo ambayo hayakuwa na biashara ya watumwa kama vile Afrika ya Kusini. Mageuzi ya biashara yalikuja kwa sababu uingwazaji wa Afrika kwenye mfumo wa dunia ulifanya ionekane dhahiri kuwa biashara ya watumwa haikuwa na faida kwenye mfumo mzima kwa ujumla. Sasa kuhesabu faida kulijumuisha sio tu gharama za uzalishaji, au ununuzi wa watumwa, bali pia gharama nyingine zilizotokana na kuwaondoa kutoka Afrika ambako wangeweza kuzalisha mali ghafi kwa ajili ya uchumi wa dunia.

## *Ushirikishwaji wa Misri na Maghrib*

Uchumi wa Misri kabla ya mwaka 1730 uliunganishwa na ule wa himaya ya Ottoman. Misri iliipatia himaya ya Ottoman nafaka, na ilikuwa kituo cha kupitishia bidhaa nyingi za biashara ya mbali kati ya himaya hiyo na Mashariki ya Kati na ya Mbali. Lakini katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, udhaifu wa kiuchumi wa himaya ya Ottoman ulisababisha utozaji kodi uliokithiri na manung'uniko mengi miongoni mwa

wakulima wa Misri. Tatizo hili lilikuja sambamba na upanuzi wa uchumi wa kibepari wa Ulaya na utafutaji wa maeneo mapya ya kushirikisha. Hali hii ilidhihirishwa na ushindani wa Ufaransa na Uingereza katika kulitawala eneo hilo.

Huu ndio ulikuwa usuli wa mapambano ya uhuru ambayo Muhammad Ali alijaribu kuyaanzisha dhidi ya utawala wa Ottoman. Mageuzi yake yalizingatia uzalishaji wa pamba kwa ajili ya soko la Ulaya chini ya udhibiti wa serikali. Hali hii ilisababisha mageuzi katika mfumo wa umwagiliaji maji, umilikaji ardhi na mahusiano ya kijamii. Mfumo mpya wa kilimo na tamaa ya utawala mpya wa kinasaba ya kudhibiti eneo la mfereji wa Suezi, na kujaribu kuitawala Sudani, yalileta adha nyingi kwa wakulima. Hali hii ilileta maasi ya Urabi ya mwaka 1881-82.

Jitihada za kuishirikisha Maghrib kwenye uchumi wa dunia zinaweza kuhesabiwa tangu mwishoni mwa karne ya kumi na tano. Lakini juhudi hizi hazikufanikiwa hadi katikati ya karne ya kumi na tisa wakati Moroko na Tunisia zilipoanza kusafirisha bidhaa za kutosha za viwanda, chakula, wanyama na hata madini kwenda Ulaya. Algeria ilipinga sana ushirikishwaji huu wa kiuchumi, na labda ndio maana ilitiishwa mapema kuliko nchi nyingi za Maghrib na kuingizwa kwenye uchumi huo kwa nguvu.

## *Ruwaza ya Afrika Magharibi*

Huko Afrika Magharibi, biashara mpya ilileta mabadiliko sio tu kwenye bidhaa walizobadilishana, bali pia katika namna watu walivyoendesha uzalishaji, jambo ambalo baadaye liliathiri mifumo yao ya kisiasa. Mabadiliko katika mfumo wa uzalishaji yalichochewa zaidi na kuondolewa kwa biashara ya watumwa, ijapokuwa mabadiliko haya yalianza muda mrefu kabla ya kuondolewa kwa biashara hiyo. Katika bidhaa mpya za biashara, mafuta ya mawese yalitia fora zaidi na kushamiri zaidi katika eneo la delta la Mto Niger. Mwanzoni, biashara ya mafuta ya mawese ilifanyika sambamba na biashara ya watumwa; lakini mwishoni mwa karne ya kumi na tisa biashara hiyo ya mafuta ilianza kushuka ghafla. Gold Coast na Dahomey yalikuwa pia maeneo ambapo biashara ya mafuta ya mawese ilifanyika. Hata hivyo kushiriki kwa Dahomey kikamilifu katika biashara ya watumwa kulisababisha ishirikishwe kwenye mfumo wa uchumi wa dunia hata kabla biashara halali haijaanzishwa.

Bidhaa nyingine mpya katika biashara ya Afrika Magharibi na dunia ya nje zilikuwa ni mpira na karanga zilizolimwa katika pwani ya juu ya Guinea na Senegambia. Hata hivyo, sio jitihada zote za kuzalisha mazao mapya ya biashara zilifanikiwa, hasa pale ambapo Wazungu walishiriki moja kwa moja. Muhimu zaidi ni kwamba Wazungu walikuwa wanachukua nafasi za wafanyabiashara wa Kiafrika kama walanguzi wa kuchukua bidhaa kutoka bara na kuzileta pwani. Bidhaa mpya za kigeni ziliingizwa katika uchumi wa Afrika katika kipindi hiki. Bidhaa za kutoka nje zilizoongoza zilikuwa ni bidhaa za pamba, ambazo ziliingizwa kwa wingi na kuchukua nafasi ya bidhaa zilizokuwa zinazalishwa na wenyeji. Baadhi ya wazalishaji hao wenyeji wa bidhaa za pamba waliamua kuanzisha mitindo mipya ya nguo na kuuza bidhaa zao kwenye masoko madogo.

## *Afrika ya Kusini*

Mfumo wa ushirikishwaji wa Afrika Kusini kwenye uchumi wa dunia wa Kipepari ulikuwa tofauti na ule wa sehemu nyingine za Afrika. Hii ilitokana na kukosekana kwa biashara ya watumwa na kuwepo kwa jumuiya ya walowezi weupe kwenye eneo hilo. Ushirikishwaji wa eneo hilo kwenye uchumi wa dunia ulianza na urekebishaji wa njia zake za uzalishaji. Ufugaji wa kibiashara wa kondoo ulianzishwa katika koloni la Cape na vilevile mashamba mengi ya miwa yalianzishwa huko Natal.

Shinikizo la uchumi unaobadilika lilisababisha Makaburu kuhamia bara, katika msafara ulioitwa *The Great Trek*. Matokeo ya uhamaji huu yalikuwa ni mapambano makali ya kugombea raslimali, yaani ardhi, na wafanyakazi, kwa ajili ya uzalishaji uliolenga soko la dunia. Katika koloni la Cape, kilimo cha wakulima wadogo Waafrika kiliendelea kuwepo sambamba na kilimo cha mashamba makubwa ya Walowezi Weupe.

Hali ya Angola ilikuwa tofauti. Huko, biashara ya watumwa na pembe za ndovu iliendelea. Biashara hii ilidhoofisha mifumo ya kisiasa ya bara. Biashara ya watumwa ilipokomeshwa jitihada zilifanywa na walowezi weupe kuanzisha mashamba makubwa, lakini mradi huu mwishowe ulishindwa. Baada ya hapo, hapakuwepo na zao la maana la biashara lililopandwa kwenye eneo hilo. Kutokana na kusambaratika kwa mifumo ya kisiasa ya wenyeji, hapakuwepo na kitu kingine zaidi ya kutawaliwa na kushirikishwa kwenye uchumi wa dunia.

## *Ushirikishwaji uliochelewa wa Afrika ya Mashariki*

Afrika ya Mashariki ilichelewa kushirikishwa kwenye uchumi wa dunia wa kibepari. Mahusiano yake ya mwanzo na dunia ya nje yalikuwa ni kwa kupitia biashara ya watumwa iliyovuka Bahari ya Hindi. Ukuaji wa Zanzibar kama muuzaji maarufu wa karafuu nchi za nje uliifanya iingie kwenye uchumi wa dunia katikati ya karne ya kumi na tisa. Bukini ilizalisha mchele na nyama ya ng'ombe ambavyo vilisafirishwa hadi Mauritius. Zaidi ya hayo, Bukini ilijulikana kwa kuwa na mashamba makubwa ya miwa. Lakini athari za ushirikishwaji wa eneo hili kwenye uchumi wa dunia zilicheleweshwa hadi kipindi cha kinyang'anyiro cha Afrika. Mageuzi yaliyotokea katika mahusiano ya uzalishaji yalisababisha pia mabadiliko kwenye mifumo ya kisiasa ya vikundi vya Kiafrika vilivyohusika.

## *Athari za ushirikishwaji*

Athari za kutoka nje, yaani za kuwepo kwa Wazungu na biashara katika ujenzi wa madola barani Afrika, hazipaswi kusisitizwa mno. Madola mengine, kama lile la Rozvi yaliendelea bila kuwa na mahusiano yoyote na Wazungu, ambapo baadhi ya jumuiya katika delta ya Mto Niger, ambazo zilifanya biashara kwa bidii na Wazungu, hazikuweza kujenga madola yenye mamlaka kuu imara.

Tokeo moja kubwa la ushirikishwaji ni kwamba ulisababisha ujenzi wa miundo ya kisiasa ambayo ilisaidia na kuhakikisha utendaji mzuri wa uchumi kwa kuzingatia mahitaji ya biashara ya nje. Hii inamaanisha kwamba kulikuwa na marekebisho ya ndani

kwa ndani katika baadhi ya madola ya Kiafrika katika karne ya kumi na tisa. Serikali nyingine za kigeni ziliitikia hali hii kwa kuanzisha serikali za kikoloni katika Afrika. Kwa upande mwingine, athari za uchumi wa dunia wa kibepari zilizotokea mara moja ni kuzuka kwa biashara ya watumwa, kuanzishwa kwa mashamba makubwa yanayolimwa na watumwa, na kukomeshwa kwa utumwa.

Kushirikishwa kwa Afrika kwenye uchumi wa dunia kuliimarisha umaarufu wa Uingereza kama dola lenye nguvu zaidi katika dunia ya kibepari. Sera ya biashara huria iliipa Uingereza manufaa mengi ya kiuchumi barani Afrika. Wafanyabiashara wa Kiingereza walikuwa mbele sana kuliko wengine mintarafu manufaa na mafanikio ya kiuchumi. Lakini umaarufu huu wa kiuchumi baadaye ulitishiwa na madola mengine ya Ulaya na Marekani. Mwishowe, kufikia mwaka 1900, sehemu kubwa ya Afrika ilitawaliwa na Uingereza, Ufaransa, Ureno, na Ujerumani.

## *Hitimisho*

Afrika iliingizwa kwenye uchumi wa dunia wa kibepari kuanzia mwaka 1750, ukiondoa Afrika Mashariki iliyoshirikishwa baadaye. Baadhi ya madola ya Kiafrika yalivunjwa na kushirikishwa kwenye uchumi huo kwa nguvu. Hata hivyo ushirikishwaji wa madola mengi ulikuwa wa polepole, na uliambatana na marekebisho kwenye mifumo iliyokuwepo ili ikidhi mahitaji ya biashara mpya na uchumi wa dunia. Matokeo ya mchakato huu hatimaye yalikuwa ni utawala wa kikoloni barani Afrika.

# 3

# *Mielekeo na nyendo mpya katika Afrika kwenye karne kumi na tatu hadi kumi na tisa*

Katika sura hii, tutabainisha na kuchambua mielekeo nyendo mpya ambazo zilitawala miongo minane ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa. Athari ya mielekeo hiyo itatathminiwa na jitihada zitafanywa mwishoni mwa sura hii kufikiria kungetokea nini kama Afrika isingetawaliwa na wakoloni mwishoni mwa karne ya kumi na tisa.

## *Mielekeo mipya ya kidemografia*

Mwelekeo wa kwanza miongoni mwa mielekeo hiyo mipya unahusiana na mabadiliko ya idadi ya watu. Ukomeshaji wa biashara ya watumwa ulisababisha ongezeko la polepole la idadi ya watu wa Afrika. Hali hii ilitokea hasa kwenye miongo mitatu ya mwisho ya karne ya kumi na tisa, tofauti na karne iliyotangulia ambapo idadi ya watu wa Afrika ilikuwa inapungua.

Mbali na kukua kwa idadi ya watu kulikuwa pia na mtawanyo mpya wa watu katika karne ya kumi na tisa. Mtawanyo huu mpya ulichukua sura ya uhamaji na misafara ya ndani. Uhamaji huo ulijumuisha pia ule wa Wanguni kutoka jimbo la Natal la Afrika kwenda sehemu mbalimbali za Kusini, Kati, na Afrika Mashariki. Kadhalika ulijumuisha ule wa Wayoruba baada ya kuanguka kwa Oyo ya Kale kutoka maeneo ya nusu savana ya Kaskazini mwa nchi ya Wayoruba na kwenda kwenye maeneo ya misitu sehemu za Kusimi.

Katika misafara yote miwili, shughuli za wahamiaji zimesababisha kuundwa kwa jamii mpya za kisiasa. Kwa upande wa Wanguni, kulikuwa na falme mpya kama zile za Wagaza, Waswazi, Wandebele, Wasotho, na Wapedi. Kwa upande wa nchi ya Wayoruba miji mipya kama vile Ibadan, Abeokuta, Midakeke na Sugamu ikawa vituo vya mamlaka ya kiserikali.

## *Mapinduzi ya kiislamu*

Kuenea kwa Uislamu kutoka Uarabuni hadi Afrika, shughuli ambayo ilianza kwenye karne ya saba hivi tukiondoa matukio machache, kuliendelea kwa utulivu na kusaidiwa sana na biashara hadi mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Lakini zoezi hili likachukua sura ya kijeshi huko Kaskazini Magharibi na Afrika Magharibi katika karne ya kumi na tisa. Katika Sudani Magharibi yaani ukanda wa Savana wa Afrika Magharibi

pekee, kulikuwa na jihadi kuu nne na ndogondogo nyingi kwa karne yote. Jihadi kuu zilikuwa ni ile ya Uthman dah Fodio huko Uhausa mwaka 1804; jihadi ya Shehe Ahmad kule Massina mwaka 1818; ya Al-Haji Umar katika maeneo ya Bambara kutoka 1852; na ile ya Samori Ture katika miaka ya 1870.

Ukiondoa jihadi ya Samori Ture, jihadi nyingine zote zilipangwa na kuongozwa na Wafulbe au Wafulani ambao walizagaa Sudani Magharibi yote. Hawa waliona jihadi kama nafasi ya kurekebisha Uislamu uwe kama ulivyokuwa unaendeshwa zamani. Hatua hii ilikuwa ni njia ya kusafisha madhambi ya kisiasa na kijamii, na kupunguza hali mbaya ya kiuchumi ya jamii. Malengo yao yalikuwa ni kuunda tawala za kidini, yaani falme zinazotawaliwa kulingana na sharia na amri za Kiislamu. Ijapokuwa Samori Ture hakuwa Mfulani, lakini alikuwa wa kundi la watu waliosilimu na kuelimika walioitwa Wajuula ambalo ni sehemu ya Wasonike. Jihadi yake ilifanikiwa, na shabaha yake ilikuwa ni kuwasilimisha watu na kuutumia Uislamu kuunda umoja miongoni mwao, hususani kwa ajili ya mapambano dhidi ya wavamizi wa Kizungu.

Mafanikio ya jihadi yalileta mageuzi ya kisiasa na kijamii. Kisiasa, yalisababisha kuundwa kwa himaya kubwa kama vile Uhalifa wa Sokota, himaya kubwa ya Samori Ture, na himaya ya Masina ambayo baadaye ilimezwa na himaya ya Al-Haji Umar.

Jihadi zilisababisha pia mageuzi makubwa katika mamlaka za kisiasa huko Sudani Magharibi. Jihadi za Wafulani zilibadilisha wafalme wa zamani wa Kihausa na kumweka Amiri mpya wa Kifulani, Vilevile watawala wa Kisoninke walibadilishwa na wasomi wa Kijuula. Jihadi ya Sokoto pia iliacha alama zake kwenye himaya ya Borno. Kwa kupitia harakati za Shehe Muhammad al-Kanemi, nasaba ya kifalme ya zamani ya Borno, yaani Wasaifawa, ilibadilishwa na nasaba mpya ya kimageuzi ambayo ilifufua ustawi wa himaya.

Kijamii, jihadi, kwa kutumia mafundisho na mahubiri ya viongozi, zilisababisha utakaso wa Uislamu. Jihadi ziliboresha maarifa kuhusu mafundisho ya Kurani na kazi za wanasharia maarufu wa Kiislamu, na kukatisha tamaa uhai wa dini za asili ambazo ziliendelea kuchanganyika na shughuli za Uislamu. Kadhalika, jihadi ziliutoa Uislamu huko Sudani Magharibi katika kuwa dini ya Ikulu na miji mikuu ya watawala na kuufanya dini ya jumuiya nzima. Hata hivyo, kuanzishwa kwa madhehebu mbalimbali kulileta utengano wa kiimani. Kulikuwa na madhehebu makuu mawili yaliyopingana: Udugu wa Tijaniyya na Kadiriyya. Madhehebu ya Tijaniyya ambayo alikuwemo al-Haji Umar yaliwavuta watu wengi wa kawaida. Hali hii inaelezea kwa nini madhehebu haya yalikuwa na watu wengi kuliko yale ya Kadiriyya ambayo yalikuwa ya watu wa tabaka la juu. Jihadi pia zilileta maendeleo katika kiwango cha uanazuoni wa Kiislamu na kisomo cha umma katika karne ya kumi na tisa. Mwisho, jihadi zilileta hisia za mshikamano na muungano wa kitamaduni wa kiislamu ambao ulidumu hadi leo miongoni mwa jamii mbalimbali za ukanda za Sudani.

Hata hivyo, viongozi wa jihadi hawakuweza siku zote kutimiza nia yao ya kutaka kutawala himaya zao kwa sharia za Kiislamu tu. Katika matukio kadha walilazimika kuruhusu baadhi ya asasi za kisiasa - kijamii zilizokuwepo kuendelea kufanya kazi. Hali hii ilisababisha kutokea kwa mseto wa tamaduni: utamaduni wa Wahausa/Wafulani

katika nchi ya Wahausa, na utamaduni wa Wajuula/Wasoninke katika ukanda wa Niger. Uislamu pia ulipata mashiko kwenye maeneo mengine ya Afrika. Ulienezwa Senegambia kutokana na juhudi za wanamageuzi mbalimbali na mashehe. Uliimarishwa Sirenaika, Sahara Mashariki na Libya kwa kupitia udugu wa Wasanusi, na huko Sudani Mashariki kwa kupitia harakati za Mahdi. Huko Uganda, Uislamu ulienea kwa jitihada za Waarabu na wafanyabiashara Waswahili, na mamluki wa Kiislamu walioajiriwa na majasusi waliosafiri bara.

## *Shughuli za kimisionari za kikristo*

Mwelekeo mwingine muhimu katika karne ya kumi na tisa ulikuwa wa kufufua na kupanua Ukristo katika Afrika. Kanisa la mwanzoni lililoshamiri Afrika Kaskazini na kuenea kuelekea juu ya mto Nili hadi Fezzan lilifunikwa katika karne ya saba na wimbi la Uislamu. Kanisa hilo ambalo lilikuwa karibu litokomezwe kabisa limeacha vikundi vichache vya Ukristo asilia wa Mashariki, na Kanisa la Kikhufu (Coptic) la Kimonofisita *(Monophysite)*, huko Misri na Ethiopia. Jitihada za Wareno za kueneza imani ya Kikristo katika karne ya kumi na tano na kumi na sita mwanzoni zilishika hatamu sehemu kama vile Kongo, Benin na Warri. Lakini kujihusisha kwake na biashara ya watumwa kulijihakikishia kushindwa. Kunako mwongo wa mwisho wa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, ari ya kimisionari iliamka tena Ulaya. Hali hii ilitokana na mwamko wa kiinjili ulioongozwa na John Wesley, na pia kuenezwa kwa mawazo ya kupinga biashara ya watumwa na moyo wa ubinadamu. Wimbi la shughuli za kimisionari za Kikristo katika Afrika kwenye karne ya kumi na tisa lilikuwa na nguvu kubwa kiasi kwamba athari zake zilikuwa za kimapinduzi kama zile za jihadi za Kiislamu. Hata hivyo, zilikuwepo tofauti kubwa. Katika kipindi hiki, wanamageuzi wa Kiislamu walitoka ndani ya jamii na kupigana kwa upanga. Lakini kuenea kwa Ukristo kuliongozwa na wageni wa kimisionari waliofundisha maadili ya Biblia, lakini huku wakikokota nguvu za kijeshi na ubeberu wa Ulaya nyuma yao. Hadi mwaka 1840, kulikuwa na mashirika ya kimisionari zaidi ya kumi na tano yakifanya kazi Afrika. Mashirika hayo ni pamoja na *Church Missionary Society* (CMS), (Chama cha Kimisionari cha Kanisa); *the Basel Evangelical Missionary Society,* (Chama cha Kiinjili cha Kimisionari cha Basel), * Switzerland; *the North German and Bremen Missionary Society* (Chama cha Kimisionari cha Udachi Kaskazini na Bremen); *the United Presbyterian Church* (Kanisa la Muungano la Kipresbiteri) ya kutoka Scotland, na *The Society of African Missions* (Chama cha Misioni za Afrika) kutoka Ufaransa. Jinsi karne ilivyokuwa inasonga mbele, idadi ya mashirika ya Kimisionari yaliyokuwa yanafanya kazi Afrika yaliongezeka pia.

Hadi kufikia katikati ya karne ya kumi na tisa, katika Afrika Mashariki na Kati, kulikuwa na shirika moja tu la kimisionari kwa jina la *Church Missionary Society*. Hadi mwaka 1873, alipokufa David Livingstone, kulikuwa na mengine mawili: *The Universities Mission to Central Africa* (UMCA) (Misioni ya Vyuo Vikuu katika Afrika ya Kati) lililoanzishwa mwaka 1857; na *The Catholic Society of the Holy Ghost* (Chama

cha Kikatoliki cha Roho mtakatifu) kililoanzishwa 1863. Lakini katika kipindi cha miaka minne baada ya kifo cha Livingstone, misioni nyingine nne zilikuja kwenye ukanda huu kutokana na kutangazwa kwa safari za Livingstone na mazingira ya kifo chake. Misioni hizo mpya zilikuwa: *The Livingstone Mission* (Misioni ya Livingstone) iliyoundwa mwaka 1875; *The Blantyre Mission* (Misioni ya Blantyre) iliyoundwa mwaka 1876 *the London Missionary Society,* (Chama cha Kimisionari cha London); na *the Catholic White Fathers.* (Shirika Katoliki la Mapadre Weupe). Misioni hizo zilifanya kazi Malawi, Buganda, Tanzania, na katika maeneo mengine ya Afrika Mashariki na Kati.

Katika Afrika ya Kusini yote kulikuwa na mashirika ya kimisionari mawili tu mwishoni mwa muongo wa kwanza wa karne ya kumi na tisa. Mashirika hayo yalikuwa *The Moravian Mission* (Misioni ya Kimoravi), na *The London Missionary Society.* Lakini kuanzia mwaka 1816, mashirika mengi ya mamisionari ya Kiprotestanti na Kikatoliki kutoka Ulaya na Marekani yalijaa kwenye ukanda huu. Miongoni mwao yalikuwepo ni *The Church Missionary Society* (CMS), *the Norwegian Missionary Society,* (Chama cha Kimisionari cha Norwa) *The Wesleyan Missionary Society* (Chama cha Kimisionari cha Kiwesley); *The Glasgow Missionary Society* (Chama cha Kimisionari Glasgow); *The United Presbyterian Missionary* (Misoni ya Muungano wa Kipresibiteri); *The Berlin Society* (Chama cha Berlin); *The Rhenish Society, the Paris Evangelicals* (Waeneza Injili wa Paris) na *The USA Mission to Zululand and Mosega* (Misioni ya Marekani katika nchi ya Wazulu na Mosega).

Tofauti na misioni nyingi katika maeneo mengine ya Afrika, misioni zilizokuwa kusini mwa Afrika zilijihusisha kikamilifu na masuala ya kisiasa ya ukanda huo. Baadhi yao ziliweza hata kujenga urafiki wa karibu na baadhi ya wafalme wa Kiafrika. Kwa mfano, Mch. Robert Moffat na Mfalme Lobengula walikuwa marafiki wakubwa. Lakini tawala za kikoloni kusini mwa Afrika hazikupendelea urafiki huu ambao waliuona kuwa hatari kwa maslahi ya wakoloni. Viongozi wa Kiafrika waliwatilia shaka wamisionari kwa sababu walitumiwa mara nyingi kama mawakala wa wakoloni wa kufanya mapatano na watawala wa Kiafrika.

Shughuli za wamisionari katika Afrika zilitofautiana. Kwanza kabisa, walijenga makanisa, kuhubiri injili na kuwapata waumini. Kama sehemu ya kujitoa kwao kidini, walifasiri Bibilia kwa lugha za Kiafrika. Pili, walitaka kuendeleza kilimo miongoni mwa wenyeji. Ili kufikia lengo hili, walianzisha mshamba ya majaribio na mashamba makubwa. Zaidi ya hayo waliinua hali za maisha za watu kwa kuwafunza stadi muhimu kama vile uashi, useremala, uchapaji na ushonaji. Vilevile walistawisha biashara. Lakini muhimu zaidi ya yote, walifundisha kusoma na kuandika na elimu ya Ulaya. Walianzisha shule za msingi, vyuo vya mafunzo na shule za Sekondari. Ni muhimu kufafanua kwa ufupi shughuli hizi za kielimu katika maeneo mbalimbali ya Afrika.

## Afrika Magharibi

Misioni iliyojukana kama *The Church Missionary Society* ilianzisha Koleji ya Fourah Bay huko Sierra-Leone mwaka 1827. Kufikia mwaka 1841 walikwisha kuwa na shule za msingi ishirini na moja. Mnamo mwaka 1842, walianzisha shule mbili za sekondari

hukohuko Sierra-Leone - moja ya wavulana na ya pili ya wasichana. Mwaka 1859 walianzisha shule moja ya wavulana huko Lagos. Wamethodisti (*Wesleyans*) nao walikuwa na shule za msingi ishirini na nne nchini Gold Coast ilipofika mwaka 1846. Walianzisha Sekondari yao ya kwanza maarufu kwa jina la *Mfantsipim School* mwaka 1876. Miaka mitatu baadaye walianzisha *The Methodist Boys High School* mjini Lagos. Kuanzishwa kwa shule na wamisionari hakukuishia pwani tu; kuliendelea hadi bara jinsi wamisionari walivyokuwa wanapenya kuingia huko.

Afrika ya Mashariki na Kati

Katika Afrika Mashariki na Afrika ya Kati, jitihada za wamisionari za kuleta elimu zilianza baadaye lakini zilitoa matunda bora. Kufikia mwaka 1830, kulikuwa na shule mjini Livingstone iliyokuwa na wanafunzi mia nne. Shule hii ilikuwa pia na karakana na kiwanda cha uchapaji kilichochapisha vitabu vya kiada vya mwaka wa kwanza kwa shule za msingi na tafsiri za Biblia. Shirika la *The London Missionary Society* lilitoa ripoti yake mwaka 1835 na kusema kuwa lina wanafunzi elfu nne katika shule zake nchini Bukini. Kufikia mwaka 1894 kiwango cha kuandikisha wanafunzi katika shule za nchini Bukini kilikuwa sawa na kile cha Ulaya Magharibi.

Afrika ya Kusini

Msaada kutoka kwa serikali za Cape na Natal katika karne ya kumi na tisa ulisaidia misioni kuweka msingi mkubwa katika sekta ya elimu. Walianzisha shule za msingi nyingi, na wakaanza kujenga vyuo vya ualimu na shule za sekondari kuanzia mwaka 1840. Kwa mfano, *The Glasgow Missionary Society* walianzisha seminari kule Natal mwaka 1841 ikiwa na idara ya viwanda ambayo ilifundisha stadi nyingi kama vile uashi, useremala, ujenzi wa matorori, uhunzi na baadaye uchapaji na ujalidi. Wakatoliki pia walijihusisha na shughuli hii na walianzisha nchini Natal shule ya bweni chini ya usimamizi wa nyumba ya masista wa Familia Takatifu (*The Holy Family*), shule ya msingi na makazi ya wakimbizi. Mwaka 1868 misioni za Kifaransa zilianzisha taasisi ya ualimu pale Amanzimtote na seminari ya wasichana kule Natal kwenye miaka ya katikati ya 1860. Waangalikana walianzisha Koleji ya Mtakatifu St. Albano miongoni mwa Wazulu mwaka 1880.

Matokeo ya kuenea kwa Ukristo na elimu ya Ulaya Magharibi katika karne ya Kumi na tisa yalikuwa ni mapinduzi kwenye jamii za Kiafrika. Waafrika walipata ufundi mwingi na mitazamo mbalimbali ya mawazo ya Ulaya. Katika maeneo mengi, waliendeleza mifumo ya kijadi ya ujenzi wa nyumba kwa kutumia stadi mpya walizopata. Wengine, hususani walioingia kwenye dini mpya, waliiga mavazi ya Ulaya Magharibi. Shughuli za wamisonari zilitoa kipigo kibaya sio tu kwenye dini za jamii za Kiafrika, lakini pia kwenye uhusiano wa kifamilia kwa kushutumu kuabudu mizimu, miungu ya jadi, uchawi na ndoa za wake wengi. Kuanzishwa kwa Ukristo kuliongeza idadi ya dini zinazofuatwa Afrika. Hali hii ilisababisha kugawanyika kwa jamii za Kiafrika kwenye makundi yanayopingana. Kwa upande mmoja kulikuwa na mgawanyo kati ya waumini na wasiowaumini, na kwa upande mwingine kulikuwa na mgawanyiko

miongoni mwa waumini, kama vile kati ya Waprotestanti na Wakatoliki. Mgawanyiko huu wa pili ulisababisha migogoro mikubwa ya kijamii; hususani nchini Uganda na Bukini.

## *Kukua kwa tabaka la wasomi wa elimu ya kizungu*

Kukua kwa tabaka la Waafrika walioelimishwa, hususani kwa Kiingereza na Kifaransa, kuliwakilisha athari ya kijamii iliyo kubwa kupita zote za shughuli za kimisionari. Tabaka hili la wasomi wa elimu ya Kimagharibi mwanzoni lilijitokeza sehemu za pwani na baadaye sehemu za bara.

Katika Afrika Kusini, asasi za elimu baada ya shule za msingi kama vile *The Lovedale Missionary Institution* katika Natal zikawa vituo vya kutoa wataalamu ambao baadaye waliunda tabaka la wasomi. Asasi kama hizo zilitoa walimu, wamisionari, makarani, waandishi wa habari, wakalimani, mafundimchundo na wakulima. Baadhi ya wasomi hawa kama vile Tiyo Soga, Nehemiah Tile, Mch. Kenyane na James M. Divane, wote wakiwa mapadre walifanya, kazi kubwa katika kueneza Ukristo miongoni mwa Wabantu kwenye miaka ya 1880 na 1890. Wengine kwa mfano John Tengo Javabu, baadaye katika karne hii walikuwa maarufu sana kwenye siasa za Cape. Hata hivyo, hadi mwaka 1880 idadi ya wasomi katika Afrika Kusini ilikuwa ndogo ikilinganishwa na idadi ya watu weusi katika eneo hilo.

Katika Afrika Mashariki na Kati, vilevile wasomi walikuwa wachache. Kwa mfano, Ilikuwa hadi miaka ya 1890 ndipo Waafrika walipopewa daraja la upadre wa Kanisa la UMCA nchini Tanganyika. Tabaka la wasomi lenye mwamko wa kisiasa halikujitokeza nchini Kenya hadi miongo ya mwanzoni mwa karne ya ishirini. Hali hii inatokana na ukweli kwamba shughuli za kielimu za wamisionari hazikuvuka elimu ya msingi hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tisa.

Katika Afrika Magharibi, kiasi kikubwa cha wasomi kiliandaliwa hadi kufikia mwaka 1880, na nchi iliyoongoza katika suala hili ni Sierra-Leone. Wasomi wa Sierra-Leone walioitwa Wakrioli, walikuwa waanzilishi wa shughuli mbalimbali za kimisionari katika sehemu nyingine za Afrika Magharibi. Hawa walikuwa ni pamoja na James Africanus Horton, aliyekuwa daktari, Samwel Ajayi Crowther, mtumwa huru wa Kiyoruba aliyeelimika na kupewa daraja kama askofu wa kwanza Mwaafrika wa Kanisa la Kianglikana. Mwingine ni James Johnson, padre mwingine ambaye pia alikuja kuwa askofu. Wengine ni pamoja na Edward Wilmot Blyden wa Liberia ambaye asili yake ni visiwa vya West Indies huko Amerika; Onmba Payne, H.E. Macaulay, na Essien Ukpabio wa Nigeria. Huko Gold Coast walikuweko wanu kama John Mensah Sarbah, J.P. Brown, A.W. Parker na J.H. Brew.

Hata hivyo, sio wasomi wote wa Afrika Magharibi na hata wa Msumbiji na Angola walijishughulisha na taaluma maalum, au kufanya kazi kama watumishi wa serikali na mawakala wa kanisa. Kundi kubwa la wasomi lilijiingiza kwenye sekta ya biashara kama wafanyabiashara au wachuuzi.

Tabaka hili la wafanyabiashara, ijapokuwa lilijazana pwani, lilijipenyeza pia sehemu



*3.1 Kanisa la Church of Scotland Mission huko blantyre (Malawi)*



**3.2** Tiyo Soga



3.3*Shule ya kijiji cha Charlotte Sierra Leone, c. 1885*

zote za bara. Walipandikiza vionjo vya kigeni, walitumia bidhaa za nje kutoka Ulaya, na walitoa mchango mkubwa katika kuingiza sehemu za bara mawazo na bidhaa za Ulaya. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba hadi mwishoni mwa miaka ya 1880, kulizuka tabaka jipya la kijamii katika Afrika likijumuisha wasomi waliokuwa kwenye utumishi wa serikali, huduma za kanisa na katika biashara za binafsi.

## *Itikadi ya Kihabeshi (Uhabeshi)*

Itikadi ya uhabeshi ni moja kati matokeo mawili makuu yalitokana na kutokea kwa tabaka la wasomi katika Afrika. Tokeo la pili, mapinduzi ya fikra, lilitokana na hili la wanza. Matokeo yote haya mawili yalikuwa muhimu sana katika historia ya Afrika katika karne ya kumi na tisa. Uhabeshi ni istilahi inayoaminiwa kuwa imeundwa kutokana na nukuzi kutoka kwenye Biblia (Zaburi 68, mstari 31) kwamba Uhabeshi itamnyooshea Mungu mikono yake. Chama kilichotumia istilahi hii kilikuwa na madhumuni ya kidini na kisiasa. Vuguvugu hili lilichipuka kutokana na mateso na hasira walizopata Waafrika kutokana na kubaguliwa na Wazungu kwenye vyeo vya kanisa na vya kiserikali, hususani katika robo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa. Hali hii

ilisababisha baadhi ya wazee wa kanisa kujitenga na makanisa yaliyokuwepo, mwanzoni wakihifadhi mambo mengi ya liturujia. Hata hivyo, baadaye wazee wengine walianzisha makanisa kwa kutumia liturujia zao mpya au kwa kurekebisha walizorithi ili zikidhi taratibu za ibada za jadi za Kiafrika. Kutokana na chuki dhidi ya ubaguzi ndani ya kanisa, watu wengine wakaanza pia kuwaongoza wafuasi wao katika kupinga maonevu ya kisiasa na kiutawala. Kwa hiyo Uhabeshi ulikuwa ni vuguvugu la kudai uhuru wa kidini na kisiasa.

Madhumuni ya vuguvugu hili yalikuwa ni kuanzisha makanisa huru ya Kikristo chini ya uongozi wa Waafrika, yasiyotawaliwa na misioni za kigeni na yanayoendeshwa kulingana na tamaduni na mila za Kiafrika. Lilianzia Afrika Kusini miaka ya 1860, na katika miaka ya 1880 kanisa huru la kwanza la Kiafrika likaundwa kwenye kanda hii na padre Mwafrika wa kanisa la Ki-Wesley aliyeitwa Nehemiah Tile. Kutoka Afrika Kusini, itikadi ya Uhabeshi ikaenea kote Afrika ya Magharibi, Mashariki na Kati. Katika Afrika Magharibi, kikundi cha viongozi wa kanisa wa Kinigeria, maarufu miongoni mwao akiwa T.B Vincent, ambaye baadaye alijulikana kama Mojola Agbebi, ndicho kilichoanzisha vuguvugu hilo. Sehemu ya madai yao ilikuwa ni kuhifadhi majina na mavazi ya kienyeji, na kutumia lugha za asili katika kuabudu.

Wasomi katika Afrika Magharibi walisonga mbele zaidi kuliko wenzao kwenye sehemu nyingine za Bara la Afrika. Walidhamiria kukanusha dhana potofu kuhusu uduni wa watu weusi. Walifanya hivyo kwa kutumia makala, vitabu majarida na hotuba. Hali hii iliibua mapinduzi ya kisomi ambayo baadaye yalieneza dhana kuhusu hadhi ya watu weusi, umoja na ushirikiano wa watu weusi (*Pan Africanism*), na utambulisho wa kipekee wa Kiafrika unaoitwa "Haiba ya Mwafrika". Viongozi wa mapinduzi haya ya kisomi katika Afrika Magharibi walikuwa James Africanus Horton, Edward Wilmot Blyden na James Johnson.

### James Africanus Horton (1835-1883)

Horton, mhitimu wa uganga wa Chuo Kikuu cha Edinburgh, alizaliwa na wazazi wa Kiigbo nchini Sierra-Leone. Alilaani ubaguzi wa rangi na kudai kuwa mtu mweusi hakuwa duni mbele ya mtu mweupe. Kwake yeye, Waafrika walikuwa na uwezo wa kuendelea na kilichotakiwa ni watu wenye uwezo kuthibitisha thamani ya Bara hili kwa ulimwengu wa nje. Zaidi ya hayo, aliamini juu ya umoja na ushirikiano wa watu weusi na kudumisha uhuru wa kisiasa wa watu weusi. Kazi zake ni pamoja na *An African View of the Negro's Place in Nature* (Maoni ya Mwafrika kuhusu Nafasi ya Mtu mweusi katika Maumbile Asilia) (1865), *West African Countries and Peoples: A Vindication of the African Race* (Nchi na Watu wa Afrika Magharibi: Ithibati ya (Utu wa) Jamia ya Kiafrika *(1868)* na *Letters on the Political Condition of the Gold Coast (Barua kuhusu hali ya Kisiasa ya Gold Coast (1870)*.

### Edward Wilmot Blyden (1832-1912)

Alizaliwa West Indies na baadaye akahamia Liberia ambako alisomea na kuishi. Alihubiri majivuno ya kijamia kwamba Waafrika wajivunie mbari yao na wasioane na

watu wasio Waafrika ili kudumisha ubora na hadhi ya jamia nyeusi. Kwake yeye, Uislamu na ndoa za wake wengi hulingana na haiba ya Mwafrika. Kwa hiyo, alihubiri imani yake kuhusu "Haiba ya Mwafrika", kuelezea utambulisho wa pamoja wa mwafrika. Kazi zake ni pamoja na *African Colonization* (Kutekwa kwa Afrika na Wakoloni) *(1862), Vindication of the Negro Race* (Ithibati ya (utu wa) Mtu Mweusi) *(1857)* na *From West Africa to Palestine* (Kutoka Afrika Magharibi hadi Palestina) (1873).

James Johnson (1836-1917)
Alizaliwa na wazazi wa Kiyoruba na kuelimishwa nchini Sierra-Leone kwenye shule iliyoitwa *The Freetown Grammar School* na kisha *Fourah Bay College*. Alijiunga na kanisa la CMS na kuhamishiwa Nigeria mwaka 1874. Alihubiri utaifa na Uhabeshi nchini Nigeria. Uhabeshi ulichukua sura ya kusifu na kutukuza mafanikio ya zamani ya jamia nyeusi na kuelezea mapambano ya kudai mamlaka na nafasi katika serikali ya kanisa na utawala wa kiraia. Alieneza itikadi ya Uhabeshi kwa kupitia mahubiri na maandishi yake. Alilaani dhana ya uduni wa jamia nyeusi na aliamini kuwa Afrika lazima ifundishwe Ukristo na Waafrika. Yeye aliona kuwa ni lazima kuwe na kanisa huru la Kiafrika, linalotawaliwa na kuongozwa na Waafrika pekee. Aliona kuwepo kwa Wazungu kama pingamizi ya kudhihirisha uwezo wa Waafrika. Mnamo mwaka 1880, alipumnzishwa na uongozi wa kanisa kazi yake kama Mkaguzi wa vituo vyote vya CMS vilivyoko ndani kabisa kwenye nchi ya Wayoruba. Hata hivyo baadaye aliteuliwa kuwa Askofu msaidizi.

Kutokana na wingi wa maandishi yaliyotolewa na wasomi hawa, kiwango cha usomi cha hoja zao, na aina ya mawazo yaliyotolewa, inadhihirika wazi kuwa kulikuwa na mapinduzi ya fikra katika Afrika, hususani Afrika Magharibi, katika karne ya kumi na tisa. Mada kuu za mapinduzi haya ni pamoja na dhana ya utambulisho wa pamoja wa Waafrika (Haiba ya Mwafrika), umoja na ushirikiano wa Waafrika (wa Afrika yote), mapambano ya uhuru wa kisiasa na kidini, na kukua kwa hadhi mpya na kujiamini kwa watu weusi.

## *Mielekeo mipya ya kisiasa*

Maendeleo muhimu ya kisiasa na mielekeo inaweza kuonekana katika Afrika kwenye karne ya kumi na tisa. Hii ni pamoja na hali kama vile kuongezeka kwa kuundwa kwa tawala unganifu, kuleta usasa, na mapambano kati ya Waafrika na wazungu.

Katika karne ya kumi na tisa, kulikuwa na mwelekeo wa kuanzisha miundo unganifu ya kisiasa katika Afrika. Mfano wa mwelekeo huu unaweza kuonekana kwenye dola za jihadi zilizotajwa hapo juu: Ukhalifa wa Sokoto, himaya ya Massina, himaya ya Al-Haji Umar, na himaya ya Samori Ture. Kadhalika dola za Kingumi zilizofuatia kutokea kwa Shaka, mfalme wa Wazulu, na Mfekane. Mifano mingine ya mwelekeo huu inaweza kuonekana Ethiopia (Uhabeshi), Bukini, na Buganda. Dola zilizokuwa zinapingana nchini Ethiopia mwishowe ziliungana kupitia ushindi wa kijeshi chini ya uongozi wa Menelik II. Nchini Bukini, Mfalme Andriana impoinimerina na waliomfuatia baadaye

waliunganisha dola za kimwinyi zenye chokochoko za Bukini ya Kati na kuunda Ufalme mmoja. Katika nchi za Afrika Magharibi, Sierra-Leone na Liberia, ambazo zilianzishwa kama makazi ya watumwa huru, nazo pia zilianzisha mwelekeo wa uunganifishaji.

Waliziunganisha dola nyingine huru zilizokuwa bara na kuunda serikali za kitaifa. Mielekeo hiyo ya uunganifishaji ilijitokeza pia nchini Misri na ukanda wa Maziwa Makuu ambako Buganda, Bunyoro, na Burundi zilipanua tawala na uwezo wao kwenye maeneo makubwa zaidi.

Mwelekeo mwingine wa kisiasa katika karne ya kumi na tisa, zaidi ya ule wa kuunda tawala unganifu, ni ule wa kuleta usasa au mwamko mpya. Usasa huu ulijitokeza katika masuala ya kijamii, kivita na kikatiba. Katika eneo la kijamii, mahusiano na Wazungu yalileta maendeleo mapya kama vile reli, simu za kuandika, mashine za kilimo, mashine za uchimbaji wa madini, mitambo ya uchapaji, elimu ya ufundi na mitaji ya fedha. Mtazamo wa Waafrika kuhusu fursa na mazingira haya ulikuwa wakati mwingi wenye hadhari na shaka. Matokeo yake ni kutoiga kama vipofu bali kuiga kwa kufanya marekebisho kulingana na mazingira yao na kutafuta mwafaka. Kwa mfano, kiwanda cha uchapaji kilifika Misri mwaka 1822 na Luanda ya Wareno mwaka 1841. Machimbo ya kwanza ya kisasa yalifunguliwa huko Algeria mwaka 1845 na nchini Gold Coast katika miaka ya 1870.

Usasa pia ulijidhihirisha kwenye eneo la katiba. Kuwepo kwa wasomi wengi wenye elimu ya Kizungu na maulama wa Kiislamu, kulidai marekebisho mapya ya mfumo wa utawala uliokuwepo karibu katika dola zote za Kiafrika. Kwa upande wa maulama, jibu la madai yao ya kutaka washirikishwe kwenye siasa lilipatikana kwenye jihádi za nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa.

Lakini sio kila mara madai yao yalifanywa kwa vita kama walivyofanya viongozi wa Kiislamu wa Kifulbe na Kijuula huko Sudani Magharibi. Katika maeneo mengine ya Afrika Magharibi, hususani katika pwani ya Magharibi, madai ya madaraka ya wasomi wapya yalifanywa kwa taratibu za kikatiba. Mfano mmojawapo ni katiba ya shirikisho la Wafante ya 1874. Katiba ya Shirikisho la Wafante ilinuiwa kukuza ushirikiano miongoni mwa makundi ya Wafante yaliyounda shirikisho hilo. Haya yalikuwa maendeleo ya kusifika na yangeweza kuwa na athari kubwa kwenye historia ya eneo hilo kama Waingereza wangeruhusu katiba hiyo itekelezwe kikamilifu. Mfano mwingine wa mageuzi ya kikatiba ni ule wa Bodi ya Muungano wa Uongozi wa Egba mjini Abeokuta iliyoundwa ili kuanzisha taratibu za kikatiba za Ulaya kwenye taratibu za kijadi za kisiasa, kuendeleza "ustaarabu", na kueneza Ukristo. Vilevile bodi hiyo ili ingeendeleza biashara kwa kulinda bidhaa za wafanyabiashara wa Kizungu na wahamiaji walioingia Sierra-Leone kama raia wa Uingereza.

Mielekeo ya kisiasa ya karne ya kumi na tisa iliyojadiliwa hapo juu ilikuwa muhimu kiasi cha kuwa na athari kwenye dola za kikoloni zilizoanzishwa baadaye. Mingi ya mielckeo hii iliselelea hadi kipindi cha ukoloni, na kuathiri matatizo na ruwaza za utawala wa kikoloni.

## *Mielekeo mipya ya uchumi*

Kulikuwa pia na mielekeo mipya ya kiuchumi katika Afrika kwenye karne ya kumi na

tisa. Mageuzi ya kusisimua zaidi ni yale yalioambatana na kuondolewa na kuzimwa kwa biashara ya watumwa na kuingizwa kwa biashara ya bidhaa za kilimo. Umuhimu wamageuzi haya ni kwamba yalileta mgawanyo mpya wa mapato. Kutokana na kuzimwa kwa biashara ya watumwa, wafalme na watawala hawakuwa tena na ukiritimba wa biashara na mapato yaliyotokana na biashara hizo. Watu wa kawaida ambao sasa walishiriki kwenye biashara ya mazao walipata mgao wao wa pato la biashara. Mgawanyo huu mpya wa mapato ulizaa kundi jipya la matajiri kwenye maeneo ya mashambani na mijini. Maendeleo ya kilimo hiki cha kusafirisha nje mazao yalisababisha kushirikishwa kwa uchumi wa Kiafrika kwenye uchumi wa dunia wa kibepari wa kutafuta faida kubwa na kulimbikiza mitaji. Lakini kwa vile mageuzi hayakuambatana na mageuzi ya teknolojia katika njia za uzalishaji na usindikaji wa bidhaa viwandani kabla ya kuzisafirisha, Afrika ikabaki kuwa mlishaji tu wa uchumi wa viwanda na wa kibepari wa Ulaya.

Mageuzi mengine ya kiuchumi katika karne ya kumi na tisa yalikuwa ni kukamilishwa kwa muungano wa kibiashara wa Afrika. Hii ilimaanisha kwamba sehemu mbalimbali za Afrika ambazo hazikuwa na uhusiano kabla ziliunganishwa kwa kupitia biashara katika karne hii. Kulianzishwa njia za biashara zilizoungamisha Afrika ya Mashariki, Kati na Kaskazini pamoja kwa kutumia wafanyabiahara Waarabu, Waswahili, Wayao, Wakamba, na Wanyamwezi katika Afrika Mashariki; wafanyabiashara Watio, Waovimbundu, na Wachokwe katika Afrika ya Kati; wafanyabiashara Waarabu wa Misri na wafanyabiashara Waarabu wa Sudani kuvuka jangwa la Sahara. Matokeo yake yalikuwa ni muungano wa kibiashara wa Afrika, kuongezeka kwa mahusiano ya ndani katika Afrika, na kuongezeka kwa wawekezaji Waafrika, walanguzi na wachuuzi. Jambo muhimu zaidi ni kwamba mageuzi yalisaidia kuyafungua polepole maeneo ya bara kwa mataifa ya Kizungu na Kiarabu/Kiswahili, hali ambayo matokeo yake ya kusikitika ndio mada kuu ya Juzuu la VII la *Historia Kuu* ya UNESCO.

## *Hitimisho*

Kutokana na mjadala wa hapo juu, ni dhahiri kwamba kama pasingekuwepo na utawala wa kikoloni katika Afrika, mielekeo mipya mingi iliyotajwa ingeendelea kwa nguvu ileile. Kisiasa, mwelekeo wa uunganifishaji ungeendelea na matokeo yake yangekuwa ni kuundwa kwa mataifa yenye nguvu. Majaribio ya kikatiba kama yale ya Shirikisho la Fante yangeanzisha msingi wa ushirikiano kati ya wasomi na watawala wa kijadi. Ukristo na Uislamu ungeendelea kama ulivyokuwa wakati wa ukoloni na kasi ya kuenea kwa elimu ya kizungu ingeongezeka. Zaidi ya hayo, kutokana na muungano wa kibiashara wa bara hili, Afrika ingekuwa na mwelekeo wa kukuza uchumi wa ndani na kujitegemea. Umoja wa Afrika na hisia za utambulisho wa kijamia ungeleta muungano wa kiitikadi wa bara lote. Bahati mbaya utawala wa kikoloni ulikomesha maendeleo yote haya.

Hata hivyo, jambo moja muhimu bado limebaki – kwamba karne ya kumi na tisa kabla ya kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni ilikuwa kwa hakika ni karne ya

kimapinduzi ambayo ilishuhudia kujitokeza kwa mielekeo mipya na shughuli ambazo athari zake ni kielelezo cha mwisho wa Afrika ya zamani na mwanzo wa Afrika ya kisasa.

# 4

# *Ukomeshaji wa biashara ya watumwa*

Katika sura hii tutachunguza ukomeshaji wa biashara ya watumwa iliyovuka bahari ya Atlantiki; matatizo yaliyokuwepo wakati wa shughuli hiyo, mwenendo wa ukomeshaji wa watumwa na matokeo yake. Ni lazima idokezwe hapa kwamba siyo jumuiya zote za Kiafrika zilishiriki katika biashara ya watumwa iliyovuka Atlantiki. Jumuiya nyingine zilizokuwa ndani zaidi barani hazikuwa hata na fununu kuhusu jambo hilo, wakati wakazi wa pwani kwa upande mwingine walishiriki kikamilifu katika biashara hiyo kiasi kwamba biashara hiyo iliathiri mifumo yao ya kisiasa na ya kijamii. Wakati idadi fulani ya Waafrika walichuma utajiri wa kibinafsi kutokana na biashara hii ya kuuza binadamu, athari ya jumla kwa bara la Afrika ilikuwa ya maafa. Takwimu za biashara zinaonyesha kwamba katika kipindi cha karne ya kumi na nane pekee takriban Waafrika milioni saba walibadilishwa kwa bidhaa za Kizungu na silaha. Idadi hii ni kubwa zaidi kuliko ile biashara ya watumwa iliyovuka Sahara, na ile ya Bahari ya Hindi zikijumuishwa pamoja. Kampeni ya ukomeshaji wa biashara ya watumwa haikutoka Afrika. Ilianzia huko Ulaya kwa kiasi fulani kutokana na sababu za ubinadamu; na kwa kiasi fulani kutokana na kupungua kwa umaarufu wa biashara ya Atlantiki pamoja na upatikanaji wa uhuru huko Marekani; na pia kubadilika kwa kubadilika kwa mwelekeo wa Ulaya kutoka Amerika kwenda Mashariki ya mbali na Afrika.

## *Msukumo wa Magharibi katika ukomeshaji wa utumwa*

Mawazo ya Wazungu kuhusu Waafrika yalianza kubadilika katika karne ya kumi na nane walipoanza kumwona Mwafrika kwa mwelekeo wa kibinadamu zaidi. Jambo hili lilileteleza kudai ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Biashara ya watumwa ilianza kuonekana kama biashara ovu ambayo ilisababisha vifo kwa idadi kubwa ya watu, ilizuia upanuzi wa biashara za aina nyingine katika pwani ya Afrika, na kuruhusu unyama kustawi barani. Watetezi wa ukomeshaji utumwa walijitahidi kutumia Ukristo, teknolojia ya ustaarabu wa Magharibi, na biashara ya kawaida hasa katika bidhaa za kilimo, katika kuizima biashara ya watumwa. Hata hivyo, kwanza walipaswa kuushawishi umma huko Ulaya na Marekani kukubali ukomeshaji wa utumwa, halikadhalika fikra za serikali kuhusu biashara ya watumwa zilitakiwa nazo kubadilishwa.

Huko Ufaransa, katika karne ya kumi na nane, fikra na mawazo ya kiyakinifu

yaliyoenezwa kutokana na kazi za wanafalsafa kama vile Diderot yalihimiza ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Huko Uingereza, watu walifundishwa kuhusu fadhila na huruma kupitia njia za kidini ambazo zilichochewa na mzinduko mkubwa wa shughuli za uenezaji injili. Huko Marekani, tayari kikundi cha Quakers kilikuwa kinafanya kampeni dhidi ya biashara ya watumwa na kilikuwa kinawashawishi watu wengine kufanya hivyo. Pamoja na mabadiliko haya katika mawazo ya umma, serikali zilikuwa zinarekebisha mtazamo wao kuhusu biashara ya watumwa. Ukomeshaji wa kwanza rasmi wa biashara ya watumwa ulikuwa ule wa Denmark mnamo mwaka 1802. Uingereza ilifuatia katika mwaka 1807, baada ya kufanyika kwa midahalo kadhaa iliyoongozwa na William Wilberforce katika bunge kuhusu suala hilo. Wanazuoni kadhaa wametoa hoja kwamba Uingereza ilitetea sana ukomeshaji wa utumwa sio kwa sababu za kibinadamu bali kwa sababu za kiuchumi. Hii ni kwa sababu biashara ya watumwa katika Atlantiki ilikuwa na manufaa zaidi kwa wafanyabiashara wa Kiingereza wa kipindi cha karne ya kumi na saba na kumi na nane kuliko ilivyokuwa kwa uchumi na viwanda wa karne ya kumi na tisa. Katika kipindi cha baadaye, Uingereza ilihitaji zaidi mali ghafi na masoko ya Mashariki ya Mbali na ya Afrika kuliko ilivyohitaji mashamba ya sukari ya visiwa vya West Indies. Kipengele cha ubinadamu kilikuwa muhimu katika kuwahamasisha watu wachukue hatua za kukomesha biashara ya watumwa na utumwa. Lakini sababu za kiuchumi ndizo zilizowezesha na kufanikisha ukomeshaji wa biashara hiyo.

Kampeni ya ukomeshaji wa biashara ya watumwa huko Magharibi iliongozwa na Uingereza. Baada ya kushindwa kwa pendekezo la ukomeshaji wa biashara ya watumwa kwa pamoja katika mwaka wa 1787 na 1807, Uingereza ilibuni mpango wa utekelezaji wenye vipengele vitatu ili kutia kani shughuli hiyo.

Hatua ya kwanza ilikuwa kuyafanya mataifa mengine kutunga sheria ambazo zingeharamisha raia wao kujihusisha na biashara ya watumwa. Hatua ya pili ni ile ya kutayarisha mikataba ya pande mbili ambayo wanamaji wa pande zote mbili wangeruhusiwa kupekua meli na kukamata meli za biashara za taifa jingine endapo zingepatikana zikiendesha biashara ya watumwa. Ya tatu ni ushirikiano kupitia tume za pamoja zenye uwezo wa kuhukumu meli za watumwa zinazokamatwa, na kuwaachilia huru watumwa wanaopatikana ndani ya meli hizo. Ni jambo la ajabu kuona kwamba mpango huu haukuanzishwa Afrika, kulikotoka watumwa, ulielekezwa zaidi huko Ulaya na Marekani kulikokuwa na wanunuzi wa watumwa hao.

Mpango huu wa awali ulileta matokeo yenye ncha mbili. Kwa upande mmoja mpango huu uliwavutia watu wenye moyo mwema na waliuunga mkono. Pia uliungwa mkono na baadhi ya serikali kama njia mojawapo ya kubembeleza fadhila za kiuchumi kutoka kwa Waingereza. Kwa upande mwingine, ulipingwa na serikali zilizoona mpango huu wa kukomesha biashara ya watumwa kama njia mojawapo ya Waingereza ya kuzitawala bahari na biashara ya ulimwengu. Serikali zenye msimamo huu ziliona uwezekano wa mpango huu wa kuathiri vibaya majeshi yao ya majini, makoloni na shughuli zao za biashara. Kwa mfano Ureno, Hispania, Marekani na Ufaransa zilitumia na kusambaza kahawa, pamba, sukari na tumbaku vilivyozalishwa katika mashamba yao yaliyohudumiwa na watumwa wa Kiafrika. Kulikuwepo pia mawakala wa meli na

mashirika yaliyoneemeshwa na biashara ya watumwa, na vikundi kama hivi havikutaka kuchukua hatua yoyote ya kukomesha biashara kwa upole.

Serikali zilizokuwa dhaifu zilisalimu amri kwa shinikizo la Waingereza la kukomesha biashara ya watumwa, lakini katika hali nyingine, mpango huu ulikubalika tu baada ya vitisho kutoka Uingereza. Denmark, Uholanzi na Sweden zilitia sahihi ya makubaliano ya kukomesha utumwa kwa pamoja na Uingereza. Hispania na Ureno zilikubali kuizima biashara kwa fidia kutoka Uingereza mnamo mwaka 1817, ijapokuwa Ureno haikukomesha biashara hiyo moja kwa moja hadi ilipofikia mwaka 1842, baada ya tishio kutoka Uingereza. Brazil iliendelea na biashara hadi 1850, wakati Kuba haikukomesha biashara hiyo hadi ilipofikia mwaka 1866. Nchi nyingine zilizokuwa na nguvu zaidi kisiasa kwa upande mwingine, zilitumia njia nyingine kujibu mapigo ya shinikizo la Waingereza ambalo waliliona kama uvamizi wa mamlaka yao. Ufaransa na Marekani ziliendelea na biashara hiyo kwa miaka kadhaa kabla ya kuikomesha kabisa. Ufaransa ilikubali kuikomesha biashara hiyo katika miaka ya 1830, wakati Marekani haikuikomesha hadi ilipofikia nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa.

Wenye mashamba huko Marekani na katika visiwa vya West Indies walipinga ukomeshaji wa biashara ya watumwa kwa sababu mbalimbali. Hawakuona maana yoyote katika kukomesha biashara ya watumwa kwa kutumia hoja ya ubinadamu. Watu hawa walikuwa wabaguzi wa rangi kiasi kwamba hawakuweza kuona ni kwa vipi ukomeshaji wa biashara ya watumwa ungewasaidia watu weusi. Waling'ang'ania kwa muda mrefu iwezekanavyo hadhi kubwa za kijamii pamoja na faida nyingi za kiuchumi walizojikusanyia kutokana na umilikaji wa watumwa na nguvu-kazi za watumwa hao katika mashamba yao. Zaidi ya hayo, upinzani wao uliimarishwa na kuhitajika sana kwa bidhaa zilizozalishwa na watumwa huko Magharibi. Wakati huo huo, Magharibi, iliyokuwa inaongozwa na Uingereza, ilikuwa inashinikiza upigwaji marufuku wa uingizaji wa watumwa ambao wenye mashamba waliwaona ni muhimu katika kuongeza utoaji wa bidhaa hizo.

## *Mchakato wa Ukomeshaji wa Utumwa*

Ukomeshaji wa biashara ya watumwa ulikabidhiwa makamanda wa meli za kivita zilizoendesha shughuli zake sio tu katika pwani ya Afrika ya Magharibi, bali pia katika bahari ya Mediterania. Ufaransa iliongoza operesheni hizo katika bahari ya Mediterania kama moja ya mbinu zake za kuliwezesha jeshi lake la majini kuitawala bahari hiyo iliyozungukwa na nchi kavu. Kwa muda, katika miaka ya 1830, Uingereza ilionekana kupoteza uongozi wake katika kukomesha biashara ya watumwa. Shughuli za meli za kivita zilikuwa na ushindi katika sehemu fulani tu. Meli za Waingereza zilikamata meli za watumwa za Wafaransa kati ya Mauritius na Bukini katika bahari ya Hindi. Lakini hakukuwepo na kanuni makataa za namna ya kuwashughulikia waliokamatwa. Mara nyingine watumwa waliokuwa chomboni waliachiliwa huru, na mara nyingine walisambazwa katika mashamba ya wenyeji. Meli za Wafaransa zilizokamatwa na Wafaransa wenyewe katika bahari ya Marekani zilishtakiwa na watumwa waliookolewa

walipelekwa Kayenne. Hata hivyo zoezi zima la ukomeshaji wa biashara hii lilikuwa na ukosefu wa uwiano wa aina mbalimbali. Katika hali ambayo meli za watumwa zilikamatwa na kushtakiwa na Tume za pamoja, hukumu ilitolewa juu ya meli na sio juu ya wafanyabiashara. Huko Marekani pia kulikuwepo na tofauti kadhaa zilizopingana katika zoezi la ukomeshaji biashara ya watumwa. Kwa kweli, nguvu za Tume iliyojaribu kukamata meli za watumwa zilitegemea mwelekeo wa wenye mashamba kwa kipindi hicho cha ukamataji wa meli. Kwa sababu hiyo, ni meli chache sana zilizokamatwa, licha ya takribani meli sabini za kijeshi kutoka mataifa mbalimbali kulishiriki katika eneo hilo.

Kulikuwepo na meli chache zaidi za kivita katika pwani ya Afrika ya Magharibi; na vikundi vya merikebu za kivita za Waholanzi, Wareno na Wamarekani vilishughulika kwa vipindi tu, na hivyo kutokuwa na athari kubwa katika eneo hilo. Ni merikebu za Uingereza na Ufaransa pekee zilizokuwepo katika operesheni ya kudumu. Kikundi cha merikebu za Ufaransa kilianzishwa mnamo mwaka 1818 na kilifanya kazi pekee hadi mwaka 1831 wakati kilipoanza kushirikiana na kundi la merikebu za kivita za Uingereza. Hata hivyo majivuno ya utaifa na ushindani havikuruhusu makubaliano ya 1831-3 kati ya Ufaransa na Uingereza kufaulu kukomesha biashara ya watumwa. Mnamo mwaka 1845 idadi ya meli za kivita kwa kila upande ilifikia ishirini na sita, na ilikuwa ni tangu mwaka huo kikosi halisi cha majini cha kupambana na biashara ya watumwa kilipoibuka. Zilikuwepo pia merikebu tano za Marekani na sita za Wareno zilizovinjari katibu na upwa Kongo. Hata hivyo, mwaka 1849 Ufaransa iliteleleza wajibu wake, na baadaye, Himaya ya Pili ilikuza biashara ya watumwa kwa siri. Kwa jumla, merikebu za Wafaransa hazikufaulu katika kukomesha biashara ya watumwa, na msimamo wake katika shughuli za ukomeshaji biashara ya watumwa ulikuwa tata.

Jukumu la kuhakikisha ushindi wa utaratibu huu liliiangukia Uingereza. Hata hivyo Uingereza ilikuwa na upungufu mwingi kwa upande huu. Moja ya matatizo yake makuu lilikuwa ni kwamba meli zake ishirini na sita za kivita hazikufaa kwa kazi ya kuikagua bahari ya Alantiki; hazikuwa na wepesi wa kuzishinda merikebu za wafanya biashara. Kwa hivyo ukomeshaji wa dhati ulitegemea matendo ya maofisa wa merikebu za Waingereza, ambao wengi kati yao walikwishatekwa na wazo la kukomesha biashara ya watumwa huko London, na walikuwa waumini wa kweli katika suala hilo. Hatimaye walikaidi makao yao makuu huko nyumbani katika mambo kadhaa na hata kudharau sheria za kimataifa kutokana na kujali sana ustawi wa binadamu.

Wakiwa wamejawa na ari ya ubinadamu, maofisa wa manowari za Uingereza walipekua na kukamata bila uhalali vyombo vya baharini vya Wafaransa na Wamarekani hata kabla mataifa hayo hajatoa ahadi ya kushiriki katika zoezi la ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Jambo hili lilisababisha malalamiko na fujo za kidiplomasia katika uwanja wa kimataifa. Juu ya hilo kulikuwepo na kiwango cha juu cha vifo vya watumwa wakati wa kukombolewa na wanamaji hawa. Kulikuwepo pia na vifo vya mabaharia, ama kutokana na magonjwa, au wakati wa kurushiana risasi za mizinga na merikebu za watumwa.

Wafanyabiashara ya watumwa pia waliyafanya majukumu ya kikundi cha merikebu

na vita yawe magumu zaidi. Walifanikiwa kuzikwepa merikebu hizo kwa vile walikuwa na taarifa zote muhimu za nyendo zao. Walitumia bendera bandia pamoja na njia nyingine za udanganyifu ili kuepuka kugundulika na kukamatwa. Hii ilichangia katika kuongezeka kwa vurugu. Makapteni wa vikundi vya merikebu na magavana wenyeji wa makazi ya Magharibi kama vile Liberia walianza safari za bara kuwaadhibu wafanya biashara ya watumwa. Vituo vya biashara hatimaye navyo vilishambuliwa na kuangamizwa. Mifano ya vituo hivyo ni kama vile vilivyokuwa Cape Mount ambavyo vilishambuliwa kwa mabomu na gavana wa Liberia, Mchungaji Jehudi Ashamum. Watumwa waliopatikana kutokana na safari hizo waliachiwa huru na kupelewa Sierra Leone, Gambia na Mauritius.

Opereshení hizi zilichukuliwa huko Ufaransa na Uingereza kuwa zimefanikiwa. Kutokana na jambo hili, iligunduliwa kuwa ilikuwa muhimu kuwahusisha viongozi wa Kiafrika katika wendo wa ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Kufuatia uamuzi huo, mbinu mbili mpya zilianzishwa. Ya kwanza ilikuwa kwamba mikataba ilianza kutiwa sahihi kati yao na viongozi wenyeji walioahidi kutumia ñjia za amani au za nguvu kuzima biashara ya watumwa katika maeneo yao. Mbinu ya pili ni kwamba Ufaransa na Uingereza zilizingira vituo muhimu vya kusafirisha watumwa nje, ili kusitisha upelekaji wa watumwa. Maingiliano haya yaliashiria mwanzo wa diplomasia ya mabavu. Hali hii ilijitokeza hasa pwani ya Afrika Magharibi kati ya 1841 na 1850, mahali ambapo palikuwa ndio kitovu cha biashara ya watumwa waliovuka Atlantiki.

Kipindi cha 1841-1850 kilikuwa pia maarufu kwa biashara ya watumwa ya kuvuka Sahara. Nchi za Magharibi hazikuwa na namna yoyote ya kukomesha biashara hiyo kwa sababu ilikuwa moja kwa moja mikononi mwa Waafrika na haikuenea nje ya mipaka ya Afrika. Lakini katika muongo uiliotajwa, serikali kadhaa za Afrika ya Kaskazini zilishawishiwa kukomesha biashara ya watumwa. Kati ya 1841-42, Utawala wa Muda wa Tunisia ulikomesha biashara ya watumwa, na Sultani wa Ottoman aliipiga marufuku biashara hiyo mnamo mwaka 1857. Majaribio yote haya ya kufuta biashara ya watumwa, hata hivyo, hayakupunguza kwa kiwango kikubwa idadi ya watumwa waliokuwa bado wanasafirishwa nje, na jitihada za baadaye hazikuonyesha matunda yoyote.

Katika kutafuta mtu wa kumlaumu kutokana na kushindikana kukomeshwa kwa biashara ya watumwa, watetezi wa ukomeshaji wa biashara hiyo huko Ulaya walitoa hoja kwamba endapo kutakosekana mnunuzi wa watumwa, basi biashara hiyo haitakuwepo. Kwa upande mwingine wenye watumwa walisisitiza kwamba upatikanaji wa uhakika wa watumwa kutoka Afrika ndiko kulikofanya waendelee kuhitajika huko nje. Kwa maoni yake, watumwa wasipopatikana hata soko lao litafifia. Hivyo lawama juu ya kuendelea kwa biashara hiyo, ilielekezwa kwa Waafrika wenyewe.

## *Jibu la Afrika*

Katika miongo miwili ya mwisho ya karne ya kumi na nane, kabla ya biashara ya watumwa kukomeshwa rasmi huko Magharibi, zaidi ya Waafrika milioni moja waliuzwa

huko Amerika. Kwa hakika kitendo cha kutunga sheria ya ukomeshaji wa biashara ya watumwa huko Ulaya hakikutosha kusitisha biashara hiyo mara moja. Mataifa mengine kama vile Ureno na Brazil bado yaliendelea na biashara hiyo ambayo, hata katika karne ya kumi na tisa, mara nyingine ilishamiri kama ilivyokuwa katika karne iliyotangulia. Kutekelezeka kwa Agizo la kukomesha biashara ya watumwa katika pwani ya Afrika Magharibi nako kulikuwa kwa wasiwasi. Vituo vya jadi vya biashara ya watumwa katika maeneo yaliyodhibitiwa na Wazungu kama vile Sierra Leone, Liberia na Gold Cost vilifungwa. Lakini kwa vile viongozi wa kisiasa wa jamii hizi walikuwa dhaifu, zoezi la kukomesha biashara ya watumwa halikuvuka nje ya mipaka yao. Sehemu nyingine kama vile Dahomey, ambako biashara ya watumwa ilikuwa nguzo muhimu ya ukoo wa mtawala, na iliathiri msuko wa muundo wa kisiasa, biashara ya kawaida ya watumwa iliendelea. Kulikuwa na uhakika wa upatikanaji wa watumwa kutoka Sudan ya Kati, na vita miongoni mwa Wayoruba vilifurisha soko la Whydah kwa watumwa. Viongozi wa jadi na wafanya biashara ya watumwa wa pwani waliwapatia watumwa wafanya biashara wa Ureno na Brazil ambao walitajirika kwa biashara hii kabla ya kugeukia biashara ya bidhaa nyinginezo.

Katika delta ya Niger na Kalabari Kongwe (Old Calabar), biashara ya watumwa iliendelezwa na vikundi vilivyoendesha biashara za bidhaa nyingine kwa wakati mmoja. Kulikuwepo na taasisi za kienyeji pamoja na vikundi rasmi ambavyo vilihusika na sehemu kubwa ya biashara ya watumwa ya eneo hilo. Miongoni mwao walikuwemo makuhani na waheshimiwa, waaguzi wa Arochukwu, "Nyumba za Mtumbwi" na jumuiya ya Ekpe. Biashara iliratibiwa kwa kanuni zilizojulikana kwa muda mrefu, na watumwa walipatikana kutoka sehemu za mbali kama vile Sokoto, Benue, Nupe na Kaskazini-Magharibi ya Kameruni. Kulikuwepo pia na sheria za jadi na desturi za jamii ambazo ziliruhusu watumwa kuchukuliwa kutoka karibu zaidi na nyumbani, kutoka maeneo ya ndani zaidi ya delta.

Hakuna namba kamili inayoweza kutolewa juu ya idadi halisi ya Waafrika waliouzwa kuvuka Atlantiki wakati wa miaka sitini ya mwanzo ya kipindi cha ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Ni makisio ghafi tu yanayoweza kupatikana kwa kuangalia mabadiliko katika ukubwa wa biashara hiyo. Kati ya 1807 na 1867, ilikisiwa kuwa kiasi cha vyombo vya baharini 4,000 vya Wazungu na Wamarekani vyenye uzito wa takriban tani milioni moja vilikuwa bado vinajishughulisha na biashara ya watumwa; kwamba walifanya kiasi cha safari 5,000 na kusafirisha nje kiasi cha Waafrika 1.9 milioni kwa kuvuka Atlantiki kutoka maeneo kati ya Senegal na Msumbiji, asilimia themanini wakiwa wanapakiwa kusini ya Ikweta. Hii ni pungufu kidogo ya jumla ya watumwa waliosafirishwa katika biashara ya kuvuka Sahara, na ile ya Waarabu katika bahari ya Hindi, kati ya 1800 hadi miaka ya 1880.

Ijapokuwa ni kweli kwamba biashara ya watumwa ilisababisha uharibifu mkubwa kwa Afrika, si vigumu kuelewa upinzani uliotoka kwa viongozi wa Afrika. Baadhi ya majasuri kama vile Tippu Tip na Rabel, waliwatumia watumwa kuimarisha nguvu zao za kisiasa. Hata hivyo upinzani wa viongozi wa pwani na wa walanguzi wa watumwa unaelezeka tu kwa misingi ya kiuchumi. Wakati watu na viongozi wa maeneo

yaliyoporwa walikuwa wakilalamika kuhusu uovu wa biashara hiyo, viongozi wa pwani na wafanya biashara waliojihusisha na biashara ya watumwa waliiona biashara hiyo kama shughuli yenye faida, iliyokuwa na mtandao na muundo ambao walikataa kuachana nao bila kuwepo kwanza kwa biashara nyingine badala yake. Upinzani wao kwa ukomeshaji wa biashara ya watumwa ulizingatia tu fikra za uchumi za muda mfupi bila kufikiria athari za muda mrefu kwao na kwa majirani zao.

Ukomeshaji wa biashara ya watumwa uliwaokoa watu wengi kutoka utumwani huko Marekani. Kiasi cha robo ya idadi nzima ya meli za watumwa zilizojihusisha na biashara hiyo labda zilikamatwa na vikundi vya merikebu zilizopinga utumwa na hatimaye kushitakiwa katika mahakama zilizoanzishwa kwa madhumuni hayo. Kwa jumla, kiasi cha Waafrika 160,000 waliachiwa huru. Lakini wendo wa kuuanzishia makazi na maisha ya kawaida ulikuwa mchungu na mrefu. Baadhi waliishi maisha ya kubahatisha katika mashamba ya watumwa huko Brazil na Kuba; wengine waliishi katika makazi ya Wafaransa kwa ajili ya watumwa waliochiwa huru, huko Guyana, Senegal na Gabon, bila kuwa na hadhi inayoeleweka. Ni huko Sierra Leone na Liberia pekee ambapo wengine kati yao walipata uhuru halisi uliolindwa na hadhi ya kisiasa iliyotambulika kisheria.

## Sierra Leone

Jaribio la Sierra Leone liliwakilisha suluhisho la kwanza lililowezekana juu ya tatizo lililowakabili watumwa walioachiwa huru ili kuwawezesha kuishi tena maisha ya kawaida. Sierra Leone ilianzishwa mwaka 1788 kama makazi ya huruma na kama sehemu ya vuguvugu la kupinga utumwa. Uhurishaji wa watumwa ulikuwa usaidiwe kwa kuwaingiza katika Ukristo na ustaarabu wa Magharibi. Walikuwa pia wapatiwe mwelekeo wa kibiashara. Lakini pamoja na malengo hayo bora, makazi haya hayakufaulu mwanzoni kutokana na hali mbalimbali zilizokuwa zinapingana. Kuwaandikisha walowezi haikuwa kazi rahisi, na uingizaji wa lazima wa malaya wa Uingereza haukusaidia chochote. Walowezi walipambana na hali ya hewa ngumu na isiyo na afya, na kiwango cha vifo kilikuwa cha juu sana. Tena kulikuwepo na chuki kutoka kwa majirani Waafrika na uvamizi wa Wafaransa wakati wa vita vya Napoleon. Kulikuwepo pia kutotengamaa kisiasa kulikosababishwa na njama za ndani, na kushindwa kwa kampuni iliyokuwa na madaraka ya uongozi wa koloni kutimiza wajibu wake. Ilipofikia mwaka 1802, idadi ya walowezi ilishapungua kutoka 2,089 na kufikia 1,406. Ni katika kipindi hiki serikali ya Uingereza ilipoingia kuliokoa koloni hili kwa kulichukua kama koloni la Kifalme na kulitumia kama kambi ya watumwa waliochiwa huru kutokana na vita dhidi ya utumwa. Watumwa wengi zaidi walioachiwa huru waliletwa hapa, na ilipofikia mwaka 1811, jumla ya watu ilishafikia 4,000. Ilipofikia mwaka 1838, tayari Waafrika 21,000 walikuwa wakiishi Freetown na vijiji kadha vilivyouzunguka mji huo. Ilipofikia mwaka 1830 idadi ya watu ilishaongezeka karibuni mara tatu.

Vizazi mbalimbali vya walowezi vilipambana na seti tofauti za matatizo. Kizazi cha kwanza kilipambana na tatizo la kuanzisha jamii mpya. Ukuaji usiosita wa idadi ya watu

ulihitaji kuendelezwa zaidi kwa huduma zilizokuwepo. Gavana Charles MacCarthy, ambaye kipindi chache cha utawala kilikuwa kati ya 1816-1823, aliikabili hali hii kwa kuboresha hali ya maisha katika vijiji vya mwanzo vilivyokuwepo na kujenga vingine vipya. Ruzuku kutoka serikali ya Uingereza ilionyesha kuwa na manufaa makubwa. Freetown ilikuwa sio tu makao makuu ya utawala wa koloni na ya Makamu Mkuu wa Jeshi la Wanamaji, bali pia kituo rasmi cha ukombozi cha Tume ya Pamoja iliyokuwa ikihukumu meli za watumwa zilizokamatwa. Koloni lilifunguliwa kwa biashara ya nje mnamo mwaka 1831; kutokana na hili, ruzuku kutoka serikali ya Uingereza iliondolewa, na wakazi walitakiwa kuchukua madaraka juu ya masuala yao na kujitegemea.

Katika kipindi hiki kigumu cha majaribu, dhima ya wamisionari katika kuhakikisha maisha na maendeleo ya koloni ilikuwa muhimu sana. Wamisionari, wakiwa wanafadhiliwa na watu kutoka kwenye matabaka ya juu na ya watawala nchini Uingereza, walifika kueneza Ukristo na ustaarabu wa Magharibi, na kupigania ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Licha ya migogoro baina yao na wenyeji wafanya biashara ya watumwa, wamisionari walishirikiana na uongozi wa kiraia katika koloni, hasa katika kuwapatia maisha mapya watumwa waliochiwa huru katika vijiji vya kilimo vilivyozunguka Freetown, ambamo wamisionari walikuwa ndio mameneja. Shule kadhaa zilianzishwa na Kiingereza kikawa lugha ya mawasiliano. Wamisionari walitumia Sierra Leone kama maabara ya mafunzo na mchanganuo linganifu wa lugha za Kiafrika. Waliwaajiri wakalimani, makarani na mawakala wa kimisionari kutoka Freetown kwa ajili ya kujipenyeza sehemu nyingine za Afrika ya Magharibi.

Matatizo yaliyokikabili kizazi cha pili cha walowezi yalihusiana na ukuaji wa makazi hayo. Katika miaka ya 1840, wakati kampeni za ukomeshaji wa biashara ya watumwa ilipokuwa katika upeo wake wa juu, kiasi cha watu 2,000 walikuwa wanaingia nchini kila mwaka, na hivyo kusababisha tatizo la mahali pa kuishi. Ili kupunguza shinikizo la nafasi liliyokuwepo, baadhi kati ya watumwa waliochiwa huru waliandikishwa katika jeshi la Uingereza, wengine walilazimisha kuhamia Gambia, na wengine walipatiwa fursa ya kuchagua kuhamia visiwa vya West Indies. Wazo la kwenda visiwa vya West Indies halikuwavutia wengi kwa vile walikuwa na hofu kwamba safari ya kwenda Marekani ingeweza kuwasababishia hali moja au nyingine ya utumwa. Walipendelea kuhamia vijijini. Hata hivyo wamisionari waliwasaidia wengine kati yao kurejea katika vijiji vyao vya asili ambavyo vingi vilikuwa katika nchi ya Yoruba. Wakati huo huo, wengine kati yao waliokuwa Freetown walipata madaraka ya juu katika jamii, lakini walipaswa kupambana na mienendo ya majikwezo ya walowezi wa mwanzo kutoka Uingereza na Nova Skotia ambao waliendeleza tofauti za kitabaka.

Maendeleo ya uchumi yalikuwa ya taratibu. Kwanza kulikuwepo na uzalishaji wa chakula, hasa mchele. Pili, kulikuwepo na kilimo cha mazao ya kuuza nje kama vile sukari, tangawizi, na buluu; na uvunaji wa rasilmali asilia kama vile kahawa na mbao. Biashara ya rasilmali asilia ilishamiri zaidi kuliko ile ya mazao ya kuuza nje, na biashara ya mbao ilikuwa na faida sana. Hata hivyo ustawi huu wa uchumi haupaswi kutiliwa mkazo kupita kiasi. Waingereza waliupa uchumi huu msaada mdogo sana wa kiutawala. Ushindi wake ulithibitisha kuwa hili lilikuwa zoezi lenye manufaa. Faida iliyopatikana

haikutosha kulipatia koloni mtaji halisi wa msingi, ijapokuwa iliwapatia utajiri watu wachache. Hadi kipindi cha pili cha karne ya kumi na tisa, tamaduni mbalimbali za Sierra Leone zilishaunganishwa pamoja kuunda jamii ya Krioli, "iliyostaarabika" kwa maendeleo yake peke yake ya ndani. Mwaka 1853, wananchi wa Sierra Leone walifanywa raia wa mfalme wa Uingereza.

Liberia

Historia ya Liberia ilitofautiana kidogo na ile ya Sierra Leone. Liberia ilikiwa ni zao la shauku ya "kusaidia na kustaarabisha Waafrika." Ilianzishwa na Chama cha Ukoloni cha Marekani, na Serikali ya shirikisho ya USA ilisaidia kwa kuiongezea idadi ya watu kwa kuwapeleka watumwa walioachiwa huru na merikebu za doria ili kuishi huko. Liberia ilikuwa pia ni matokeo ya nia ya kujaribu kupunguza athari za watu weusi waliopatiwa uhuru wao huko Marekani.

Tatizo la kwanza lililowakumba walowezi wa Liberia lilitokana na chuki ya viongozi wa nchi jirani za Kiafrika, ambao walichukia kuingiliwa na wageni katika nchi yao na kuwa tishio kwenye biashara ya watumwa ambayo ilikuwa shughuli yao kuu ya kibiashara ya kuvuka bahari. Pingamizi lao lilidhibitiwa na walowezi chini ya uongozi wa Mch. Jehudi Ashmum, na hivyo kutoa mwanya kwa koloni kuendelea kuwepo. Koloni lilipewa jina la Liberia mnamo mwaka 1824, na Monrovia ukawa ndio mji mkuu. Liberia ilitawaliwa na Chama cha Ukoloni cha Marekani kwa kumtumia kiongozi rasmi ambaye, kutokana na umbali, aliachiwa huru kwa kiasi fulani kutawala kulingana na ufafanuzi binafsi wa hati iliyoidhinisha makazi hayo. Biashara ilihamasishwa na idadi ya watu katika makazi hayo iliendelea kukua jinsi miaka ilivyopita. Kimuundo, Liberia iliundwa sio tu na Waafrika walioachiwa huru; idadi kubwa ya walowezi wa mwanzo walikuwa watumwa waliotolewa utumwani huko kusini mwa Marekani kwa masharti kwamba wangehama.

Mambo matatu yalichangia kuwepo na kukua kwa makazi hayo. La kwanza linahusiana na ujasiri wa wakazi dhidi ya chuki kutoka kwa majirani na mazingira magumu. Makazi mengine matatu yalianzishwa Bassa Cover, Sinoe na Cape Palmas (Maryland); makazi ya mwisho yaliunganishwa na Liberia mnamo mwaka 1856. Pamoja na matatizo yote yaliyojitokeza, wakazi walionyesha uwezo mkubwa wa kushinda matatizo. Ardhi haikuwa na rutuba, hakukuwepo na biashara, hakukuwepo na mtaji, na nguvukazi ilikuwa ghali sana. Lakini kuwepo kwa walowezi pale pwani sio tu kwamba kuliwafukuza wafanya biashara ya watumwa, bali pia kulikomesha biashara ya watumwa katika eneo hilo.

Jambo la pili ni tabia binafsi za watu waliokabidhiwa madaraka ya uongozi katika makazi hayo. Wengi wao walitokea kuwa watu wenye uwezo mkubwa wa kiutawala, waliomakinika na watendaji wazuri. Mifano ya watu kama hao ni Thomas Buchanan, aliyeirekebisha katiba ili iendane na mazingira ya pale; J.B. Russwurm, gavana wa Maryland kuanzia 1836 hadi 1851; na J.J. Roberts, gavana wa Liberia kutoka 1841 hadi 47, na Rais kuanzia 1847 hadi 1856.

Jambo la tatu lilikuwa hadhi ya Liberia. Baada ya Waingereza kusaili "utaifa" wa

taifa "huru" linaloendeshwa na walowezi, Liberia ilitangazwa rasmi kuwa huru tarehe 26 Julai 1847. Kutokana na uhuru huo, uraia wa Liberia ulikuwa wazi tu kwa watu weusi. Kwa hali hiyo, ikawa Jamhuri ya kwanza ya Kiafrika iliyoundwa na watumwa walioachiwa huru pamoja na Waafrika huru waliozaliwa Marekani.

Katika karne ya kumi na tisa, Liberia haikuwa imeendelea kiuchumi kama ilivyokuwa Sierra Leone. Umuhimu wa jaribio hili katika nchi hizo mbili sio tu kwamba ziliashiria vuguvugu la uhuru katika karne ya ishirini, bali kwamba ziliwakilisha wazo zuri la kwamba nchi mpya za Kiafrika zinaweza zikaundwa katika ardhi ileile iliyokuwa imeathiriwa vibaya na biashara ya watumwa. Hata pamoja na umuhimu huu uliojitokeza, ushindi wa Liberia na Sierra Leone haukuweza kuwatosheleza wakomeshaji wa biashara ya watumwa ambao walishindwa kukubaliana juu ya njia maalum za kuchukua ili kuleta ufanisi katika kuzima biashara ya watumwa. Ushinde wa makazi mengine yaliyojaribiwa kuanzishwa huko Lokoja katika ndagano ya Niger-Benue ulileteleza kuenea kwa ukosoaji wa mkakati mzima wa ukomeshaji wa biashara ya watumwa.

## *Kulinda biashara mpya*

Katika enzi za ukomeshaji wa utumwa, nchi za Magharibi kwa jumla zilijali zaidi kulinda biashara mpya za mazao ya kilimo kuliko kufanikisha ukomeshaji wa biashara ya watumwa. Biashara ya bidhaa nyingine haikushindana kikwelikweli na biashara ya watumwa; iliendelea sambamba na biashara hiyo. Kama kulikuwepo na ushindani wa aina yoyote, basi ulikuwa miongoni mwa mataifa ya Magharibi ambayo yaliigawa Afrika katika himaya zao za kiuchumi. Zaidi ya hayo, mapinduzi ya viwanda na teknolojia huko Uingereza na Ufaransa yalizua soko kubwa la bidhaa za Kiafrika kama vile mafuta ya mawese, ambayo yalihitajika kulainisha mashine, na kama mali ghafi ya kutengeneza sabuni na mafuta ya taa.

Kiasi cha mafuta ya mawese kilichosafirishwa nje kwenda Uingereza na Ufaransa kiliongezeka kwa kiasi kikubwa kati ya 1814 na 1870. Ufaransa pia iliingiza karanga na aina fulani ya njugu kutoka Senegal na Gambia kwa ajili ya kutengeneza sabuni za nyumbani. Ukuaji wa biashara hii uliwakilisha uanzishaji wa biashara ya kuchukua nafasi ya biashara ya watumwa. Maeneo makuu ya uzalishaji wa mafuta ya mawese yalikuwa Dahomey, delta ya Niger na Kameruni. Hata hivyo, upanuzi wa biashara hii mpya ulimaanisha kustawi kwa utumwa wa ndani kwani watumwa walihitajika kusaidia katika uzalishaji na uuzaji wa mafuta ya mawese. Mabadiliko haya ya kiuchumi nayo yaliongezewa kasi na ueneaji wa Ukristo, elimu ya Magharibi na athari nyingine za kitamaduni kutoka Ulaya na Marekani.

Wamisionari wa Kiprotestanti na wa Kikatoliki walikuwa mawakala wazuri wa athari za Magharibi. Sehemu nyingine kama vile Senegal ambako utamaduni wa Kiislamu ulikuwa tayari umeshamiri, jitihada za kueneza elimu na Ukristo zilizofanywa na wamisionari hazikuwa na mafanikio makubwa. Misioni ya Moyo Mtakatifu wa Maria (*Saint Coeur de Marie*) huko Gabon nayo ilipata mafanikio kidogo chini ya Mhashamu Bessieux. Baada ya misioni kugundua uwezo wao mdogo mbele ya Uislamu, ziliamua



**4.1** *Kikundi cha wanawake wa Kioromo kikiwa ndani ya chombo HMS Daphne, mwaka 1867, baada ya kuokolewa kutoka jahazi la biashara ya watumwa Afrika ya Mashariki.*

**4.2** *Watumwa walioachiwa huru katika shamba la misioni ya Vyuo Vikuu huko Mbweni karibu na Zanzibar - Ulipaji wa ujira.*



kufunza kikundi cha wasomi na kuanzisha shule nyingi ili kutimiza azma hii. Kwanza walianzisha makao huko pwani. Waliingia Badagry mnamo mwaka 1842, Wyhdah 1843, Kalabari 1846, na kiungo chao cha bara kilikuwa Abeokuta.

Misioni za Kiprotestanti, tofauti na wenzi wao Wakatoliki, walijihusisha na shughuli za wenyeji na kutafuta athari za kidunia. Ukristo kwao haukukumbatia kuwaingiza tu watu kwenye dini, bali pia kwenye elimu, utamaduni, mahusiano ya kitabaka na uchaguzi wa kisiasa. Walifundisha stadi kama vile usanifu majengo, useremala, uchapaji na tiba za Kizungu. Hii ilikuwa na athari kubwa kwa watu. Baadhi yao waliiga utamaduni wa Kimagharibi upande wa mavazi, chakula na maisha ya nyumbani. Hili lilikuwa tabaka jipya la kati ambalo wamisionari walilitegemea katika kupanua mkondo wa biashara ya kuingia na kutoka pwani. Kwa hali hiyo wamisionari wa Kiprotestanti walichukua jukumu la wanamageuzi. Huko Abeokuta, waliingilia katika masuala ya wenyeji ya kisiasa na ya kijeshi. Walipata msaada wa vikosi vya Waingereza dhidi ya Dahomey, iliyokuwa inaingilia ardhi ya Abeokuta. Kupofikia mwaka 1890, misioni zilikuwa zimejiingiza kabisa katika maendeleo ya maeneo hayo, jambo ambalo lilileteleza kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni.

## *Hitimisho*

Kwa kuhitimisha, hatuna budi kusisitiza kwamba katika miongo minane ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa, kupungua kwa biashara ya watumwa hakukutufikisha popote karibu na kufuta kabisa biashara hiyo. Biashara ya watumwa ilikoma huko Senegal na Gorée mwaka 1824, ijapokuwa maeneo ya karibu karibu yaliendelea kuwa na operesheni za hapa na pale hadi 1866-67. Katika miaka ya 1848-50, Liberia ilipata msaada wa merikebu za Wafaransa dhidi ya merikebu za watumwa za kimataifa. Biashara ya watumwa huko Côte d'Ivoire haikuwa ya kutimiza mahitaji ya nje, ila mahitaji ya ndani ya ukanda huo. Kwa kiasi kikubwa pia Gold Coast haikuthiriwa na biashara ya watumwa katika kipindi cha ukomeshaji.

Hata hivyo, katika eneo lilio kati ya Lagos na Wyhdah, shughuli za watumwa ziliendelea hadi zilipodhibitiwa kwa njia za kidiplomasia na za mabavu na Uingereza na Ufaransa kwenye miaka ya 1860. Sera ya kutiliana mikataba na kuhimiza umilikaji wa ardhi ilitumika kudhibiti biashara hiyo katika eneo kati ya Benin na Gabon. Kati ya Kongo na Angola, shughuli za watumwa zilikatishwa tamaa na udhibiti mkali kutoka meli za doria za Uingereza na Ureno. Inaweza kuonekana dhahiri kwamba biashara ya watumwa haikukomeshwa wakati mmoja katika maeneo mbalimbali ya bara la Afrika.

Pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa ya kipekee. Kati ya miaka 1860 -1870, wakati biashara ya watumwa ilikuwa inakufa huko Magharibi na Kusini, Afrika ya Mashariki ilikuwa inashuhudia kuhuishwa kwa biashara hiyo katika pwani ya Mashariki. Jitihada za Uingereza za kuzima biashara hiyo kwa kutiliana mkataba na Sultani wa Zanzibar zilikuwa na athari kidogo tu. Ni pale tu kulipoanzishwa utawala wa kikoloni katika eneo hilo, ndipo biashara ya watumwa ilipofikia mwisho wake. Ucheleweshwaji huu ulitokana na ukweli kwamba wakomeshaji wa biashara ya watumwa huko Magharibi hawakujua

ukubwa wa biashara ya watumwa iliyoendeshwa na Waarabu hadi ilipogunduliwa na Livingstone.

Itikadi ya ukomeshaji wa biashara ya watumwa iliwafanya watu wawatendee watumwa wa Kiafrika kibinadamu zaidi. Aidha, ilizua wazo la "kuifungua" Afrika kwa dunia nzima. Hata hivyo, shauku ya watu wa Magharibi kwa Afrika ilitokana zaidi na tamaa yao ya kuinyonya Afrika kuliko heshima yao kwa amali za Kiafrika. Kufikia mwaka 1870, biashara ya watumwa kwa kiwango kikubwa ilishakomeshwa, sio tu kutokana na shughuli za nchi za Magharibi, bali pia kutokana na ushirikino na Waafrika. Mkabala wa Waafrika katika ukomeshaji wa utumwa ulionyesha uwezo mkubwa wa kukubali mabadiliko licha ya tishio la kuvurugika kwa uchumi. Baada ya karne ya mapambano ya kukomesha utumwa, nchi za magharibi ziliridhika na zikayatumia mafanikio hayo kuhalalisha kutekwa kwa bara la Afrika (na wakoloni).

Hivyo, kwa namna fulani biashara ya watumwa ilibadilishwa kwa ukoloni. Chini ya utawala wa kikoloni, mabaki ya biashara ya watumwa na utumwa kama asasi ya jamii vilikomeshwa. Hata hivyo, baadhi ya aina mbaya zaidi za ukoloni, kama vile mfumo wa ubaguzi wa rangi huko Afrika ya Kusini, zilikaribiana sana na utumwa. Mapambano dhidi ya kudhalilishwa kwa utu wa binadamu yanapaswa kuendelezwa, na utambuzi wa unyama wa biashara ya watumwa unaongezeka. Ni vyema kutilia maanani kwamba wakati wa matembezi ya Papa Yohane Paul II huko Gorée, Februari 1992, kwa niaba ya Ukristo wa Ulaya, aliwaomba msamaha watu wa Afrika kwa karne za biashara ya watumwa. Kadhalika, lipo vuguvugu linalozidi kupamba moto la kutaka Afrika na Waafrika walioko uhamishoni kudai fidia kutokana na madhara yaliyosababishwa na biashara ya watumwa.

# 5

# *Mfekane na kuibuka kwa madola mapya ya Kiafrika*

Sura hii inahusu asili ya Mfekane, mapinduzi yaliyoanzia miongoni mwa Wanguni wa Kaskazini na kuenezwa na shughuli za kijeshi na za kisiasa-kijamii za Shaka, Mfalme wa Wazulu, na maluteni wake wengine. Ijapokuwa mapinduzi hayo yalianzia Afrika ya Kusini, lakini yalienea hadi katika Msumbiji na Zimbabwe ya sasa, na kaskazini hadi kusini mwa Tanzania katika Afrika Mashariki. Jinsi Mfekane ilivyoendelea, kwanza ilivuruga na kisha ilijenga upya mifumo ya madola iliyokuwepo katika maeneo ya Wabantu ya Afrika ya Kusini na ya Kati.

Kwa Kibantu, neno Mfekane lina maana ya "kuponda" na "kupiga nyundo". Kama ambavyo jina lenyewe linaashiria, ni kweli kulikuwepo na athari za kupondwapondwa kwa miundo ya kisiasa katika maeneo yaliyozungumza Kibantu huko Afrika ya Kusini. Mfekane ilianza katika muongo wa kwanza wa karne ya kumi na tisa na kulipna mfululizo wa matukio ambayo yalisababisha nasaba tawala zilizokuwepo kuzidiwa nguvu na kubadilishwa; dola za zamani zilitekwa na kuingizwa katika miliki mpya; makundi ya watu yalilazimika kuacha maskani yao ya jadi na kuhamia kwingine; uchumi ulidunishwa, na katika matukio kadha wakazi wote wa vijiji fulani walifurushwa ama kutekwa na kutiwa utumwani. Mfekane ilileteleza kupungua kwa idadi ya watu katika eneo kubwa la Afrika ya Kusini na hivyo kutoa mwanya kwa wahamiaji walowezi wa Kizungu walioitwa Makaburu kuichukua ardhi ya Waafrika. Makaburu hawa sio tu kwamba walipora sehemu nzuri kuliko zote za ardhi ya Waafrika kwa ajili yao binafsi, bali pia waliwafanya Waafrika kuwa watumwa na kupora ardhi yao iliyokuwa imebakia.

Hata hivyo Mfekane haikuleta athari hasi tu. Ilikuwa pia na matokeo chanya. Katika maeneo kadhaa ya Afrika ya Kusini, Mfekane ilitoa fursa ya kuibuka kwa falme na himaya unganifu; baadhi ya himaya hizo zimedumu hadi leo. Ndani ya madola yenyewe ya Kiafrika, Mfekane ilichochea ubunifu wa viongozi wa kisiasa wa Kiafrika na kuwalazimisha kuboresha mbinu zao za kijeshi na ustadi wao wa kisiasa.

Ili kuelewa misukumo iliyoleteleza mapinduzi haya, sifa zake za msingi na ubora wa mabadiliko yaliyotokana nayo, hatuna budi kwanza kutafiti hali ya mazingira ya kijiografia ya Unguni ya kaskazini, kuelewa namna mazingira hayo yalivyowaumba wakazi wake, na jinsi wakazi wenyewe walivyoyafinyanga mazingira yao. Muhimu zaidi ya yote ni ile sera ya baadhi ya viongozi wa Kinguni ya kudhibiti uzalishaji mali na uzazi

miongoni mwa watu wao ili kuhakikisha kuwepo kwa nguvukazi ya ziada iliyokuwa tegemeo la nguvu za mfalme na utawala wa dola.

## *Nchi na desturi za kilimo za Wanguni wa kaskazini*

Jamii za maeneo ya Wanguni wa Kaskazini zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujirekebisha kulingana na mahitaji ya maumbile ya mazingira kutokana na karne nyingi za kuishi na kulima katika eneo hilo. Ardhi ya Wanguni wa kaskazini ipo kati ya mto Pongolo na Tugela, na magharibi imepakana na bonde la Mzinyathi. Ni mkoa wenye miinuko mikali ambamo mito kadhaa imetengeneza mabonde yenye kina kirefu. Miinuko hii mikali inasababisha tofauti za hali ya hewa ambazo nazo husababisha woto wa aina mbalimbali. Wakulima waliofuga na kulima katika eneo hilo walilazimika kujirekebisha kufuatana na mazingira hayo, lakini pia waliingilia utaratibu asilia wa woto wake.

Kwa jumla woto wa eneo hili la Wanguni wa Kaskazini ulikuwa hasa wa aina mbili: upande mmoja ulikuwa ni wa misitu - misitu halisi ya miti ya mbao, na misitu ya vichaka (yaani misitu iliyodumaa yenye miti na vichaka duni); upande wa pili, katika sehemu za mabonde, kulikuwa ni eneo la nyasi la savana. Wahamiaji asilia wa Kinguni walikuwa wamebadilisha woto wa eneo hili jinsi karne zilivyopita. Walilisukuma nyuma eneo la misitu na kuongeza eneo la savana kwa manufaa yao wenyewe. Hatua hii ya makusudi ya kuingilia taratibu za uotaji wa mimea kwa karne kadhaa hatimaye ilileteleza ruwaza tata ya woto ambapo kulikuwa na mchanganyiko wa aina mbalimbali za malisho yaliyoukiliwa zaidi na kiasi cha mvua pamoja na aina ya udongo. Kwa mfano, kulikuwepo na mbuga-chachu katika maeneo ya mvua nyingi zaidi ambayo wakulima waliyapendelea kwa mifugo wakati wa kiangazi; na mbuga-tamu katika maeneo makavu ya miinuko ambayo waliyapendelea wakati wa majira ya baridi. Uwezo huu wa kufikia mbuga za aina mbalimbali ndio wakulima walioufikiria kuwa unawapa malisho ya kutosha kwa mifugo yao kwa mwaka mzima.

Maeneo mengine ya Afrika ya Kusini hayakufanana na hayo yaliyoelezwa hapo juu. Hata yale maeneo yaliyokaliwa na jamii za Wasotho-Watswana katika savana ya Transvaal, ambayo yalikuwa na mbuga-tamu kwa mifugo yao, hayakuwa na mifumo ya mito ya kuyapatia unyevu wa kutosha kama ilivyokuwa katika maeneo ya Wanguni wa Kaskazini. Aidha, jumuiya nyingine kati ya hizi zilikuwa na malisho yaliyokuwa na mbung'o ambao walisababisha ugonjwa wa malale kwa watu na wanyama. Zaidi ya hayo, wakulima walioishi katika mbuga za Transvaal kabla ya ukoloni walikosa faida iliyotokana na mchanganyiko wa aina mbalimbali za maeneo ya kufugia kama waliyokuwa nayo Wanguni wa Kaskazini. Hata hivyo, ruwaza ya makazi ya jamii za Wasotho-Watswana ilionyesha kuwa jamii hii ilikuwa na eneo kubwa zaidi la wazi kuliko lile la Wanguni wa Kaskazini. Hivyo tatizo la msongamano makazini ambalo baadaye liliwakabili Wanguni wa Kaskazini halikuvipata vikundi vya Wasotho-Watswana. Kuishi karibukaribu kwa vikundi vya Wasotho-Watswana hakukutokana na shinikizo la idadi kubwa ya watu, bali kulitokana na kujikusanya kwao kwenye maeneo machache yaliyotawanyika ambayo yalikuwa na maji.

Mwanzoni utengemano wa jimbo hilo haukutishiwa kwa vile kulikuwepo urari mzuri kati ya ongezeko la watu na la wanyama, na uhuru wa kutumia aina mbalimbali za malisho yaliyokuwepo. Lakini, kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na nane, ongezeko la idadi ya watu liliathiri upatikanaji wa ardhi na rasilimali nyingine zilizohusiana. Ongezeko hilo la idadi ya watu wakati huo lilitokana kwa kiasi fulani na kukubaliwa kwa mahindi kuwa zao kuu la chakula katika jimbo lile, na hivyo kusababisha shinikizo juu ya ardhi. Pamoja na hili kulikuwepo na hali ya wasiwasi na vurugu iliyotokana na mashindano makali ya kuwania rasilimali zilizokuwa zinapungua miongoni mwa madola tofauti katika ukanda huo. Kama vile hali hii haikuwa mbaya ya kutosha, kulikuwepo pia na njaa kali katika eneo la Wanguni wa Kaskazini mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Njaa hii ilitambulika, pamoja na mambo mengine, kutokana na vikundi vya watu wenye njaa, vilivyotangatanga vikipora vyakula katika maghala na kufanya mambo kuwa magumu zaidi.

## *Muundo wa jamii za Wanguni wa kaskazini*

Ni wazi kutokana na yaliyopita kuwa ongezeko la watu miongoni mwa Wanguni wa Kaskazini, halikutokana na uhamiaji mkubwa katika maeneo haya, bali lilisababishwa na ukuaji wa kawaida wa ndani kwa ndani. Ardhi na rasilimali nyingine zinazohusiana zilipozidi kupungua, jumuiya nyingine zilianza kuteka kwa nguvu ardhi na malisho yaliyomilikiwa na wengine. Zahama hii iliwafanya viongozi wengine kuchukua hatua za kudhibiti uzalishaji na uzazi. Ili kuelewa vyema mwenendo huu, hapana budi kuutafiti muundo wa jamii ya Wanguni katika kipindi cha kabla ya ukoloni.

Jamii iligawanywa katika kaya au maboma, kila boma likiongozwa na mtu aliyechaguliwa kutokana na nasaba ya kuumeni. Idadi ya wake aliokuwa nao kiongozi huyu ilitegemea hadhi yake ya kijamii. Kila mke na watoto wake waliishi pamoja katika nyumba yao na kuzalisha chakula kwa mahitaji yao wenyewe. Kulikuwepo na mgawanyo wa kazi kufuatana na jinsia; wanaume walijishughulisha na ufugaji na uwindaji, wakati wanawake walisimamia uzalishaji wa mazao. Familia za kifalme zilikuwa na mpangilio tofauti. Zaidi ya shughuli za uzalishaji wa kawaida za wanafamilia na jamaa zao, maboma ya kifalme pia yaligeuzwa makambi ya kijeshi kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na nane na kuendelea. Makuruta wa jeshi wa kiume kutoka pande zote za nchi waliishi katika makambi hayo, na miongoni mwa kazi walizomfanyia mfalme ni uzalishaji wa mazao.

Kulikuweko pia makuruta wa kike, ila wao hawakuishi makambini kama wenzi wao wa kiume. Hawa waliishi katika maboma ya baba zao. Hata hivyo, si wanaume wala wanawake walioruhusiwa kuoa au kuolewa bila ruhusa ya mfalme. Mara nyingine walikaa kwa takriban miaka kumi kabla ya kuachiliwa kuoa au kuolewa. Kutokana na utaratibu huu, wafalme wa miliki za Wanguni wa kaskazini waliweza, pamoja na mambo mengine, kudhibiti sio tu kiwango cha uzalishaji mazao bali pia kiwango cha kuzaliana kwa binadamu. Hakuna taarifa kamili zinazoonyesha ni lini utaratibu huu ulianza

miongoni mwa Wanguni wa kaskazini, lakini inawezekana kwamba katika upanuzi wao, walivijumuisha vikundi kadhaa vya Wasotho katika himaya yao ya kisiasa, na mwishowe kuiga njia ya Wasotho-Watswana ya kuunganifisha shughuli za jando kwa lengo la udhibiti wa kisiasa.

Maelezo kadhaa yamekwisha kutolewa kuhusu Mfekane. Sababu zinazotolewa zinaanzia kwenye shinikizo la idadi ya watu hadi kufikia kipengele cha athari ya Wazungu. Miongoni mwa athari za Wazungu zinazotajwa ni pamoja na zahama zilizotokana na uhamaji wa wakulima wahamiaji wa Kikaburu kuelekea mashariki katika karne ya kumi na nane, na kipengele cha biashara ya Wazungu katika ghuba ya Delagoa. Katika nadharia zote hizi ni ile ya shinikizo la idadi ya watu pekee inayoelekea kulingana na ukweli, na inayoweza kuhimili jaribio la kuhakikiwa. Kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, mchanganyiko wa mambo yaliyozungukia suala la upungufu wa ardhi uliosababishwa na ongezeko la idadi ya watu yalileteleza machafuko na vurugu katika dola nyingi za Wanguni wa kaskazini. Pia kipindi hiki kilishuhudia mabadiliko muhimu na ya msingi katika muundo wa jamii hizo ili kikabiliana na hali inayobadilika. Kulikuwepo na ubunifu katika mbinu na mpangilio wa kijeshi. Mifano ya wabunifu wakubwa wa wakati huo ni Zwide wa Wandwandwe, Dingiswayo wa Wamthethwa na Shaka wa Wazulu.

Falme kuu tatu zenye nguvu zilizuka kutokana na mfululizo wa vita vilivyozingira dola za Wanguni. Ufalme wa kwanza ni ule wa Shirikisho la Wandwandwe chini ya Zwide, wa pili ulikuwa wa dola ya Waswazi iliyotawaliwa na Sobhuza, na ufalme wa tatu ulikuwa ni Shirikisho la Wamthethwa lililotawaliwa na Dingiswayo. Dola kubwa hizi tatu zilitawaliwa na wafalme wakuu waliozitoza ushuru miliki nyingine ndogondogo, jumuiya na koo. Miliki zilizokuwa chini ya himaya za dola hizi zilitambua udhibiti wa kiongozi mkuu katika masuala yaliyohusiana na miviga ya kifalme, taratibu za jando, ulipaji wa ushuru na upiganaji wa vita. Hata hivyo, miliki hizo zilikuwa na uhuru mkubwa wa kuendesha mambo yao ya kawaida ya siku kwa siku.

## *Wandwandwe*

Miliki ya Wandwandwe ilifikia umaarufu wake katikati ya karne ya kumi na nane. Watu waliounda taifa hili hapo mwanzoni walihama kutoka ufalme wa Waihembe katika bara ya Ghuba ya Delagoa karibu na mwisho wa karne ya kumi na saba. Mwishowe walilowea katika bonde la Mto Pongolo pamoja na vikundi vingine vya Wanguni. Hapo viongozi wa Wandwandwe walianza sera ya upanuzi kwa kuzitiisha na kuziingiza katika kabila lao jumuiya ndogondogo za jirani. Wakati huu ndipo walipochukua jina la Wandwandwe ili kujitofautisha na majirani zao. Nguvu za kisiasa za Wandwandwe ziliongezeka sana jinsi walivyozidi kuziteka jumuiya kadhaa na kuzifanya zao, na hata mipaka yao ikawa mipana sana. Jambo hili liliwafanya viongozi wa Wandwandwe kuwa viongozi wa kwanza wa Kinguni kuanzisha taifa kubwa kutokana na jumuiya kadhaa ndogondogo za ukanda huo. Ili kufikia lengo hili, hawakutumia nguvu za kijeshi tu, bali pia walitumia asasi za zamani na kuzirekebisha ili kukidhi madhumuni mapya.

Jukumu kubwa zaidi la kujenga Shirikisho la Wandwandwe lilimwangukia Zwide aliyeingia madarakani mwaka 1790. Alianza kwa kujenga juu ya misingi iliyoanzishwa na babu wa baba yake kwa kutumia desturi na mazoea ya zamani. Alifikia kilele cha utawala wake karibuni wakati mmoja na jirani na mpinzani wake wa Shirikisho la Wathethwa, Dingiswayo.

Ufalme wa Wandwandwe kama ilivyokuwa kwa miliki nyingine za Wanguni katika ukanda huo, ulitumia rejimenti zilizoundwa kutokana na jando za jadi za wanaume na wanawake wa hirimu moja. Upo uwezekano kwamba Zwide na watangulizi wake walikuwa kati ya viongozi wa kwanza wa Kinguni kuona umuhimu wa kisiasa wa kuratibu tohara na jando katika kiwango cha taifa zima. Kuanzia wakati huo sherehe hizi zilipangwa kutoka makao makuu, na vijana, wavulana kwa wasichana, kutoka nchi zote zilizokuwa chini ya Wandwandwe, walijumuishwa katika marika ya kitaifa. Nyakati za vita, marika haya yaligeuzwa kuwa regimenti za kijeshi. Zaidi ya manufaa ya kijeshi ya vikundi hivi vya kitaifa vya hirimu, marika haya yalisaidia pia kulehemu pamoja sehemu mbalimbali za Shirikisho la Wandwandwe.

Ili kuimarisha mamlaka yao na kujenga imani ya kutoshindika, viongozi wa Wandwandwe walitegemea kwa kiasi kikubwa sihiri pamoja na athari za kidini. Kwa mfano, Zwide alitumia idadi kubwa ya majusi na waganga kujenga na kueneza uvumi kuhusu nguvu zake kwa jumuiya zote za jirani. Pia alitumia harusi za kidiplomasia kuimaarisha uhusiano wake na dola nyingine katika ukanda huo. Dada yake aliolewa na Dingiswayo, mtawala wa Wamthethwa, na binti yake aliolewa na Sobhuza, mfalme wa Waswazi.

Hata hivyo Zwide alikuwa mwerevu wa kutosha wa kutoruhusu miungano hiyo ya kinasaba kuwa kipingamizi katika sera zake za upanuzi. Hivyo, ingawa Sobhuza alikuwa mkwe wake, Zwide alivamia makao yake makuu kwa vile Sobhuza alidai kumiliki ardhi ya kilimo yenye rutuba ya Wandwandwe katika bonde la Pongolo. Jeshi la Wandwandwe lilishinda na kumtimua Sobhuza kutoka Pongolo, likamswaga yeye na wafuasi wake kuelekea kaskazini ambako baadaye alianzisha msingi wa taifa la Waswazi.

## *Waswazi*

Vikundi ambavyo baadaye vilijulikana kama Waswazi vilitokana na koo mbalimbali za Wangwane na Watsonga zilizokuwa chini ya uongozi wa nasaba za kifalme za Dlamini. Vikundi hivi viliunganishwa pamoja na kuwa kiini cha taifa la Waswazi. Kiongozi wa Waswazi, Sobhuza, alizileta koo mbalimbali na jumuiya nyingine katika eneo hili chini ya udhibiti wake wa kisiasa, muhimu miongoni mwao vikiwemo vikundi vya Wasotho.

Jumuiya za Wasotho zilizotungamanishwa na Sobhuza katika ufalme wake zilikuwa na mfumo wa rejimenti za marika ambao aliuiga, na jambo hili liliimarisha muungano wa jumuiya nyingine zilizotekwa. Vikundi vya hirimu vya Waswazi vilitumika tu wakati wa vita. Watemi wa jumuiya zilizoshindwa hawakuangamizwa, bali walipewa kiasi fulani cha uhuru katika mambo yaliyowahusu wao wenyewe, na vijana wao

walijumuishwa katika rejimenti za hirimu za Waswazi. Kisha baada ya kudhihirisha uaminifu wao, koo za Kisotho zilitendewa sawa na raia wa Kinguni ndani ya taifa la Waswazi.

Sobhuza pia alikazana kuimarisha nafasi yake na kuhakikisha usalama wa ufalme wake mpya kwa kudumisha uhusiano wa amani na majirani zake. Ni kwa sababu hii Sobhuza alioa mmoja wa mabinti wa Zwide, kiongozi wa Wandwandwe, na pia kuwapeleka vijana wa Kiswazi kama ushuru kwa Shaka, kiongozi wa Wazulu. Sobhuza aliendelea na juhudi zake za kutafuta amani hata pale zilipopuuzwa, na hili liliiwezesha himaya yake kuwa na amani kwa kiasi na kuepuka mashambulizi ya vikosi vya maangamizi vya Shaka.

Sobhuza alirithiwa na mwanawe, Mswazi, mnamo mwaka 1840. Mswazi alipotawazwa tu alipambana na matatizo ya ndani na ya nje. Ndani, ilimbidi kupambana na maasi kadhaa katika Ikulu yaliyokuwa na nia ya kumwondosha madarakani na, licha ya mageuzi mengi aliyoyafanya, maasi haya yalibakia kuwa jambo la kawaida katika utawala wake. Yeye pia alijiingiza katika sera ya ndoa za kidiplomasia ili kuunganisha taifa lake. Alioa katika familia nyingi za watawala wa vikundi vilivyoshindwa, na alioza wanawali wa kifalme wa Kiswazi kwa watawala wa vikundi hivyo. Msimamo huu wa kuoleana ulitekelezwa na umma mzima. Matokeo yake ni kwamba mgawanyiko wa kimbari takribani ulifutwa kabisa katika jamii ya Waswazi. Nje ya nchi, Mswazi alipambana na maadui kadhaa kama vile majeshi ya Wazulu yaliyoongozwa na Mpande mnamo mwaka 1846, lakini ufalme wake ulinusurika.

### *Wamthethwa*

Ufalme wa Mthethwa ulianzishwa na Kayi, na ulikuwa maarufu wakati wa Dingiswayo, mjukuu wake. Kama ilivyokuwa kwa tawala nyingine za Wanguni, nguvu za Wamthethwa zilijengwa juu ya ushuru uliokusanywa kutoka kwa jumuiya zilizokuwa chini yake, uporaji wa ng'ombe, jeshi lililoundwa kwa rejimenti za hirimu, na biashara na Ghuba ya Delagoa. Dingiswayo alifikia kilele cha nguvu zake wakati mmoja na Zwide, mkinzani wake ambaye pia alikuwa mtawala wa ufalme jirani wa Undwandwe. Dingiswayo alileta mabadiliko kadhaa katika rejimenti za hirimu katika himaya yake. Alifuta desturi za tohara ambazo kwa kawaida zilifuatana na uundaji wa marika ili kuondoa kipindi cha kutiwa kumbini kwa wari kilichodaiwa na kaida hizo. Pia alichukua muundo wa kifua-na-pembe kwa ajili ya jeshi lake.

### *Wazulu*

Dingiswayo, mtawala wa Wamthethwa, aliuawa katika vita dhidi ya Zwide na vikosi vyake vya Wandwandwe mnamo mwaka 1818. Shaka, ambaye alikuwa kiongozi wa utawala mdogo wa Wazulu na jenerali katika jeshi la Dingiswayo alichukua utawala wa Shirikisho la Wamthethwa. Matokeo yake ni kwamba aliwafanya Wamthethwa sehemu ya taifa la Wazulu. Aliruhusu mfumo wa jadi wa utawala wa Mthethwa kuendelea chini ya uongozi wa kijana mdogo, mtoto wa Dingiswayo, ambaye alipewa mwangalizi

aliyepokea amri kutoka kwa Shaka. Katika kushughulikia vikundi vingine, Shaka alisisitiza juu ya kuvishirikisha kikamilifu (katika taifa la Wazulu). Mara nyingi watawala wa watu walioshindwa waliondolewa na kuwekwa watawala wapya kutoka katika familia za Wazulu, ijapokuwa mara nyingine, watemi wa vikundi vikubwa walibakizwa na kuruhusiwa kiwango fulani cha uhuru katika kuongoza mambo yao wenyewe.

Mafanikio makubwa zaidi ya Shaka yalikuwa katika namna alivyopangilia upya jeshi lake. Aliimarisha marekebisho ya asasi za jamii, kama vile marika, kwa ajili ya jeshi. Alibadilisha na kuboresha baadhi ya mbinu zake za kijeshi wakati wa vita alivyopigana kwa ajili ya kupanua ufalme wa Wazulu. Alibadilisha mkuki mrefu wa kutupa kwa mkuki mfupi zaidi kwa ajili ya mapambano ya karibu. Alianzisha ngao ndefu na kukataza askari wake kuvaa makubadhi ili waweze kuwa na mwendo wa kasi zaidi. Aliweka jeshi la kudumu la watu wakakamavu na wenye nidhamu ya hali ya juu waliokuwa wanaishi makambini na ambao walipaswa kubaki makapera mara nyingine kwa kiasi cha miaka kumi kabla hawajaruhusiwa kutoka jeshini. Katika mbinu zake za kijeshi, muundo wa "pembe-za-ngombe" ndio uliovutia zaidi kuliko miundo mingine.

Jeshi la Shaka lilikuwa shupavu na lisilokuwa na huruma kwa maadui. Nia yake ya kutaka kushinda na kuteka vikundi vyote vya Wanguni wa kaskazini ilimsababishia mapambano ya ana kwa ana na Zwide, mtawala wa Wandwandwe, ambaye hatimaye alimshinda mwaka 1820. Kushindwa kwa Zwide kulimaanisha kuanguka kwa dola la Wandwandwe. Wakati vikundi kadhaa vilivyounda Undwandwe viliikimbia nchi, idadi kubwa ya vikundi vya Wandwandwe vilibakia na kuwa vibaraka wa Shaka.

## *Wagaza*

Dola la Wagaza liliundwa kutokana na kikundi kidogo cha watu walioongozwa na Soshangane ambacho kilijitenga na Wandwandwe mara baada ya Zwide kushindwa. Soshangane aliweka makao yake katika nchi ya Watsonga, ambamo alishinda na kuteka madola mengine madogomadogo.

Nguvu za uchumi za ufalme wa Gaza zilijengwa juu ya udhibiti wa biashara kati ya bara na makazi ya biashara ya Wareno katika Ghuba ya Delagoa. Hata hivyo, badala ya kupanua na kujinufaisha na fursa hii ya kibiashara, dola la Wagaza lilitegemea vita kwa moyo wote. Vikosi vya Soshangane vilipigana na majirani zao wote. Mamlaka yake yaliimarishwa na jeshi lililokuwa na mfumo wa rejimenti za hirimu, na ambalo liliiga mbinu nyingine za kijeshi kutoka kwa jeshi la Wazulu.

Hata hivyo jamii ya Wagaza ilibakia imegawanyika kikabila. Kikundi cha Wanguni asili kutoka kusini kiliunda tabaka la juu la kijamii, wakati ambapo vile vikundi vipya vilivyojumuishwa kutoka jumuiya za Watsonga vilibakia katika tabaka la chini. Soshangane hakutumia rejimenti zake za hirimu kuingiza jumuiya zilizotekwa katika kikundi kikubwa. Badala yake, rejimenti za hirimu za Watsonga zilibakia katika wilaya zao chini ya maofisa wa Kinguni. Watsonga walibaguliwa na mara nyingi ndio waliopoteza watu zaidi katika vita.

### *Wandebele*

Taifa la Wandebele lilianzishwa na Mzilikazi, mtoto wa mtawala wa ufalme mdogo wa Khumalo uliokuwa chini ya Zwide, mfalme wa Wandwandwe. Mwaka 1818, Mzilikazi alikuwa mtawala wa Khumalo baada ya kifo cha baba yake. Baada ya Zwide kushindwa na Shaka, mtawala wa Wazulu, Mzilikazi alihamishia utii wake kwa Shaka. Hata hivyo, baadaye aligombana na Shaka na kukimbia kutoka eneo hilo pamoja na watu wake. Alihamia katika eneo walimokuwa wanaishi Wasotho na pale alianzisha dola lake la Wandebele ambalo lilikuwa tajiri na lenye nguvu sana. Alitumia vita kuziunganisha jumuiya nyingi za Wasotho katika dola la Wandebele. Mzilikazi alitishiwa vikali na maadui wenye nguvu na wanyang'anyi. Jambo hili lilimfanya ahamishe makao yake makuu mara kadhaa hadi alipotamakani Bulawayo. Hapo napo alivijumuisha vikundi vingine kadhaa katika ufalme wake na ilimlazimu kupigana vita kadhaa vya kujilinda na vingine vya uchokozi hadi mwaka 1850. Alikuwa na mawasiliano mazuri na Wazungu. Aliwaruhusu wamisionari, wafanyabiashara na wawindaji kuingia nchini mwake. Ushirikiano wake na Wazungu ulitayarisha njia kwa ukanda huo kufanywa koloni. Mzilikazi alifariki mwaka 1868.

Ufalme wa Wandebele ulikuwa wa kivita, na ili kuujenga, ilimbidi Mzilikazi kunakili mambo kadhaa kutoka himaya ya Wazulu. Alitumia mfumo wa rejimenti za hirimu kuwajumuisha katika taifa lake watu aliowateka, na kusawazisha migawanyiko ya kijamii katika ufalme wake. Nafasi ya mfalme ilikuwa muhimu sana katika kujenga umoja wa ufalme. Tukio la kila mwaka lililojulikana kama sherehe za "tunda la kwanza" lilianzishwa ili kuwaleta pamoja kwenye makao makuu watu wote waliounda ufalme huo. Akiwa mtawala, Mzilikazi alikuwa na mamlaka juu ya mifugo ya taifa. Pia aliwatunza wanawali wote waliotekwa, na kwa kupitia regimenti za hirimu, alidhibiti wakati murua wa kuoa kwa watu wake. Kwa hali hiyo alitawala sio tu uwezo wa watu wake wa kuzalisha mali, bali pia uwezo wao wa kuzaliana.

Kwa vile ufalme wa Wandebele ulikuwa ni dola la kijeshi, mpangilio wa kijeshi ulichagamana na, na mara nyingine ulikuwa chini ya kivuli cha, uongozi wa kisiasa wa taifa. Jeshi lilipangwa katika vikosi, kila kikosi kikiwa na kamanda wake. Makamanda nao walisimamiwa na majemadari wanne wa divisheni ambao walipokea amri kutoka kwa Mzilikazi. Mfumo wa rejimenti za hirimu katika dola la Wandebele ulikuwa umekomaa sana. Karibuni watu wazima wanaume wote walikuwa wanajeshi, na waliunda rejimenti zilizoishi mijini kwenye maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili yao.

Katika ufalme wa Wandebele, mamlaka yote yalihodhiwa na Mzilikazi. Wajumbe au makamanda wa vijiji waliteuliwa na kusimamiwa na yeye mwenyewe. Taifa lake liliundwa vyema na liliongozwa vizuri. Watu waliotekwa, wengi wao wakiwa Washona, walisimilishwa katika dola ya Wandebele, lakini nao pia walichangia mambo yao mengine ya kimaisha na ya kidini kwenye utamaduni wa Wandebele.

### *Wasotho*

Ufalme wa Wasotho ulioanzishwa na Mushweshwe (Moshoeshoe) ni mojawapo ya

madola yaliyojitokeza wakati wa vurugu za Mfekane. Ufalme huo uliundwa kutokana na jumuiya ndogondogo za wazungumzaji wa Kisotho walioishi kaskazini na magharibi ya milima ya Drakensberg. Mushweshwe alipata umaarufu wake kwa kuwalinda watu wake dhidi ya mashambulizi ya baadhi ya majirani zao. Aliwahamisha watu wake kutoka maskani yao ya awali na kuwapeleka katika boma lililojengwa mlimani la Thaba Bosiu. Ni katika mlima huu ambapo Mushweshwe alianza kujenga makao makuu ya taifa la Wasotho. Aliwashinda majirani zake na kuwaweka ndugu zake kama magavana wa watu hao. Katika hali kadhaa aliruhusu utawala wa jadi wa nchi zilizoshindwa kubaki ilimradi watambue na kukiri ukuu wa uongozi wake. Alizikaribisha jumuiya ndogondogo za watu waliotenguliwa kutoka kaya zao za asili katika machafuko ya Mfekane, na kuwajumuisha katika muundo wa dola la Wasotho.

Mushweshwe alikabiliana na tatizo la uhasama wa majirani zake wenye nguvu. Mkabala wake ulikuwa ni ule wa kuwa tayari kupigana wakati akifikiria jinsi ya kuwatuliza maadui wenye nguvu, na kufanya kila lililowezekana kuepusha shari iliyoelekezwa kwa taifa jipya la Wasotho. Pia aliwagombanisha majirani wenye nguvu. Hakutegemea tu uwezo wa kijeshi wa jeshi lake. Alikuwa na sifa za mwanadiplomasia bingwa na mwanasiasa mwerevu wakati aliposhughulika na majirani zake. Endapo pamoja na hatua zote hizi bado alivamiwa, basi alitumia vizuri fursa ya ngome yake ya mlimani na mara nyingi alifanikiwa kuwashinda maadui zake. Ushindi wa mara nyingi wa jeshi lake ulilitia moyo dola lake na hivyo kueneza sifa za Mushweshwe.

Dola la Wasotho lilikuwa tajiri sana kwa kuzingatia wingi wa makundi yake ya ng'ombe. Hata hivyo, dola hilo lilibughudhiwa mara kwa mara na wanyang'anyi wenye silaha ambao walipora mifugo hiyo. Hatimaye Wasotho waliweza kuwashinda wanyang'anyi kadhaa waliokuwa hodari sana kama vile Wagrikwa na Wakorana. Wasotho waliteka farasi wao na kufaulu kuwatumia katika kuanzisha na kuzalisha farasi wao wa taifa waliojulikana kama "Farasi Wadogo wa Basotho." Polepole matumizi ya farasi hawa yaliwageuza Wasotho kuwa taifa pekee, miongoni mwa Wabantu wa Afrika ya Kusini, lililopigana kwa kutumia farasi.

Mwaka 1833 Mushweshwe aliwakaribisha wamisionari wa Kikristo katika ufalme wake. Alitarajia kwamba kuwepo kwa wamisionari Wazungu kungezuia uvamizi wa Makaburu, na kwamba wamisionari wangemsaidia kuwa na uhusiano na watu wa nchi za nje na kupata silaha. Chama cha Wamisionari cha Kueneza Injili cha Ufaransa ndicho kilichoitikia mwaliko wake. Makao yao makuu yalikuwa Morija, ambapo walianzisha shule na kituo cha mafunzo, mashine ya uchapaji na kituo cha kilimo. Walikuwa na vituo kadhaa vya nje ya misioni ambako waliendeleza kilimo, biashara mbalimbali na asasi za elimu. Walikuwa ni washauri waaminifu kwa mfalme na walijaribu kuwa wasuluhishi kati yake na Makaburu na maofisa wa Kiingereza waliokuwa Natal na Cape. Walianzisha msingi wa utamaduni mpya wa Kikristo kwa Wasotho, na hivyo kuwa kiungo cha kuleta umoja na chombo muhimu katika jitihada za mfalme za kujenga taifa.

Miaka ya 1830 ilikuwa muongo wa mapambano makali kati ya Wasotho na Makaburu (walowezi wakulima weupe). Kuingilia kati kwa Waingereza katika suala hili kuliwaathiri vibaya Wasotho kwa sababu, wakati wakidai kutopendelea upande wowote,

Waingereza waliitambua jamhuri ya Makaburu kwenye nchi ya Wasotho. Jambo hili liliwapa Makaburu fursa ya kuendelea kutishia kuwepo kwa taifa la Wasotho. Mwishowe, katika jitihada za kuokoa ufalme wake usimezwe na dola la Makaburu, Mushweshwe aliiomba Uingereza kuuweka chini ya himaya yake. Kwa kufanya hivyo, aliokoa ufalme wake usivunjwe, na pia aliweka msingi wa taifa jipya lililokuja kujulikana kama Lesotho.

## *Wakololo*

Wakololo walikuwa kundi la watu waliozungumza Kisotho ambao waling'olewa kutoka maskani yao ya asili wakati wa msukosuko wa Mfekane. Wavamizi walikamata mifugo yao yote, na wakiwa wamefilisiwa, walilazimika kukimbilia mahali pa usalama wakiwa na Sebetwane kama kiongozi wao. Katika kutangatanga wakitafuta makazi mapya na mifugo, waliungana na vikundi vingine vilivyokuwa vikitangatanga kama wao. Baada ya kushindwa vibaya katika vita vya Dithakong katika mwaka 1823, walielekea kaskazini kupitia nchi za vikundi kadhaa vya Wasotho na Watswana hadi Ziwa Ngami. Hali ya jangwa na upinzani kutoka kwa jumuiya zilizoishi jangwani iliwashawishi kutokuendelea na safari ya kuelekea pwani ya Atlantiki. Kwa hivyo Wakololo walivuka Zambezi na kufanya makazi kwenye uwanda wa juu wa ndagano ya Zambezi na Kafue. Ijapokuwa waliweza kuzuia mashambulizi kutoka kwa Watswana, vikundi vya Wanguni na Wandebele, walitumia fursa ya mgogoro wa urithi uliokuwepo katika ufalme wa Lozi kuuvamia ufalme huo na kulikalia eneo lake la magharibi mwa uwanda wa juu.

Taifa la Wakololo lilisitawi vizuri sana chini ya uongozi wa Sebetwane. Aliwaingiza Walozi katika taifa la Wakololo na kujaribu kuchanganyika nao sana kwa kuchukua wake kutoka kwao. Pia aliwaingiza Walozi katika chombo kilichokuwa kinafanya maamuzi ya kitaifa. Alibakiza mfumo wao wa kisiasa, na sehemu nyingine mfumo huu uliishi sambamba na mfumo mpya wa Wakololo mpaka mifumo yote miwili ilipounganika. Sebetwane alivikusanya vijiji vyote vilivyotekwa katika majimbo yaliyoendeshwa na maofisa Wakololo ambao pia walikusanya ushuru kutoka kwa watu waliotekwa.

Kijamii, lugha ya Kikololo ilizungumzwa katika ufalme mzima. Hata hivyo Sebetwane hakuzilazimisha jamii alizoziteka kufuata mfumo wa jando za marika. Pia mwenyewe hakujitenga kama walivyofanya wafalme wa jadi wa Walozi, bali aliwaruhusu raia zake wote kuwasiliana naye. Hatua hii ilimfanya apendwe sana na watu wake na hadi alipofariki, wote walikwisha kupata hisia kali za utaifa wa Kikololo.

Baada ya kifo cha Sebetwane, warithi wake waliweka utawala wa mabavu juu ya ufalme wa Kololo. Jambo hili lilisababisha raia wao wa Kilozi kuasi na hatimaye Wakololo walipinduliwa na ufalme wa Kilozi kurejeshwa. Hata hivyo jambo hili halikuashiria mwisho wa athari ya Wakololo. Baadhi yao waliwapangilia wenyeji wa bonde la Shire walioitwa Wamanganja katika jumuiya kadhaa ndogondogo ambazo baadaye ziliunganishwa katika falme mbili chini ya watemi wa Kikololo. Kwa hali hiyo Wakololo waliwatawala Wamanganja. Na, licha ya kubughudhiwa mara kwa mara na Wanguni, athari ya Wakololo katika bonde la Shire ilibakia hadi mwaka 1890.

## *Madola ya Wanguni ya Ng'ambo ya Zambezi*

Baada ya Wandwandwe kushindwa na Shaka mnamo mwaka 1820, ufalme wao uliporomoka na baadhi ya wenyeji wakakimbilia pande tofauti. Kikundi kilichoongozwa na Zwangendaba kilipokuwa kinahama kilisababisha machafuko makali kutokana na vita vyake vya mfululizo dhidi ya jumuiya zilizokuwa zinaishi kwenye maeneo kilimopita, au jumuiya kilizokutana nazo njiani. Kikundi hicho kiliiangamiza himaya ya Chamgamire, kiliwashinda Warozwi na kupigana vita vingi dhidi ya jumuiya za Wachewa na Watumbuka. Baada ya kifo cha Zwangendaba kama mwaka wa 1848, kundi lake liligawanyika katika vikundi kadhaa vilivyoendelea kutishia mataifa mengine katika ukanda huo.

Kikundi kimoja kati ya vikundi hivyo, kile cha Wanguni wa Msene, kiliongozwa na Nqaba. Kikundi hiki kiliendesha kampeni nyingi za kijeshi dhidi ya majirani zake. Baadaye kilishindwa katika vita dhidi ya Wakololo walioongozwa na Sebetwane.

Wanguni wa Maseko ni kikundi kingine kilichotokana na ufalme wa Wandwandwe ulioporomoka. Kikundi hicho mwishowe kilianzisha dola yake kusini-mashariki mwa Tanzania chini ya Mputa.

## *Hitimisho*

Mfekane yaweza kuonekana kwamba ilitokana na mchanganyiko wa mabadiliko kadhaa ya kisiasa-kijamii. Ilianzishwa na shinikizo la idadi ya watu, na upungufu wa ardhi uliochochewa na njaa kali. Yalifuata mapambano ya kugombea rasilimali za eneo la Wanguni wa kaskazini zilizokuwa zinapungua. Mapambano ya kupanua himaya na kujinusuru bila shaka yalihusisha pia ushindani wa biashara mpya ya bidhaa zilizotoka nje katika Ghuba ya Delagoa. Hata hiyo, kama ilivyodhirishwa na muundo na tabia ya madola mapya, inapaswa kusisitizwa kwamba mapinduzi yaliyowakilishwa na Mfekane yalikuwa matokeo ya msingi ya jitihada za ndani na sio athari kutoka nje. Baadhi ya madola hayo yaliunda mifumo imara ya kijeshi iliyojikita katika vikundi vya marika. Wengine walitumia mambo kadhaa ya miundo ya jamii za jadi ili kuhifadhi madola yao ya kitaifa.

Mfekane ilileteleza kuzuka kwa madola mapya kama vile Lesotho na Swaziland ambayo yamedumu hadi leo, na ni sehemu ya jumuiya ya mataifa ya dunia. Madola mengine yaliyoibuka wakati wa Mfekane hayakudumu baada ya vifo vya waasisi wake, na mengine yalipondwa na ubeberu wa Kizungu. Mfekane pia ilisababisha kupotea kwa umaarufu wa mataifa yaliyokuwepo kama vile Wamthethwa, Wandwandwe, Wangwane na Wahlubi.

Madola ya Mfekane yalikuwa katika viwango viwili. Kulikuwepo na madola ya kibeberu yenye sera kali za uchokozi wa kijeshi kama vile falme za Wazulu, Wandebele na Wagaza. Katika kundi la pili kulikuwepo na falme za kujihami kama vile Wasotho, Waswazi na Wakololo. Katika madola yote ya Mfekane asasi za ufalme na ukoo zilikuwa muhimu sana. Mfekane ilishuhudia kuibuka kwa viongozi wapya kama vile

Shaka, Mzilikazi, Sobhuza, Zwangendaba na Sebetwane, waliokuja kubeba majukumu muhimu kuhusiana na majaaliwa ya watu wao katika karne ya kumi na tisa.

Vita vya kipindi cha Mfekane vilipunguza idadi ya watu katika maeneo yaliyoathiriwa. Hivyo madola mengi ya Afrika ya Kusini yalidhoofishwa na kuwekwa katika hali ya kuweza kuvamiwa kwa urahisi na makaburu. Pia Mfekane iliwasambaza upya wakazi Waafrika wa eneo la kusini mwa Afrika kwa kufanya sehemu nyingine ziwe na idadi kubwa ya watu na nyingine zibakie na idadi ndogo sana. Makaburu walifaidika na hali hii, na katika kile kilichorejelewa kama Safari Kuu Ndefu na Ngumu (*The Great Trek*) katika miaka ya 1830, waliingia katika sehemu zilizokuwa zimehamwa kwa muda na kubakiwa na wakazi wachache tu. Kutoka kwenye vituo vya uhakika kama hivyo, Makaburu walipigana vita kadhaa ili kuteka makazi zaidi, mifugo na nguvukazi rahisi. Hivyo walijijenga katika eneo la Transvaal pamoja na bonde la mto Orange kwa kudhulumu taifa la Wasotho. Waingereza waliwapendelea, wakawaruhusu kupata silaha na risasi bila masharti, huku wakijaribu kuwazuilia majirani zao Waafrika fursa kama hiyo ya kupata silaha. Hivyo Mfekane iliwezesha upanuzi wa makazi ya Wazungu ndani ya Afrika ya Kusini.

# 6

# *Athari za Mfekane katika Koloni la Rasi*

Kwa mujibu wa ukali na athari yake, Mfekane inaweza kufananishwa na jihadi za Wafulani huko Afrika Magharibi. Hata hivyo ni lazima ifahamike kuwa ijapokuwa mlipuko wa Mfekane ulionekana kuwa wa ghafla sana, mambo yaliyousababisha yalikuwa yakijilimbikiza kwa kipindi cha miaka kadhaa. Kipindi cha robo ya mwisho ya karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa kilishuhudia kuibuka taratibu kwa tawala kubwa kama vile za Wandwandwe na Wamthethwa, zikiwa na viongozi wa kijeshi wenye nguvu. Ni kutokana na mashindano ya falme hizi kubwa kutaka kuteka maeneo ya nchi za jumuiya ndogondogo pamoja na rasilmali zao kulikosababisha mlipuko ulioitwa Mfekane.

Koloni la Rasi lilijumuisha eneo lililokaliwa na Wazungu na lile lililokaliwa na Waafrika upande wa magharibi wa mto wa Great Fish. Upande wa magharibi kuzunguka Cape Town ndilo eneo ambalo wakulima wa Kidachi wa mwanzoni walilowea kuanzia katikati ya karne ya kumi na saba. Hadi ilipofikia miaka ya 1820, tayari walikuwa ni Makaburu (wakulima) waliokuwa wanazungumza Kiafrikaana. Walipendelea kuishi katika mashamba yao makubwa katika kaya za upweke, wakiwa wamezungukwa na idadi kubwa ya watumishi wa Kiafrika, hasa wale wa kabila la Wakhoisan. Waingereza walikuwa wameliteka koloni mnamo mwaka 1795, hasa kutokana na nafasi yake muhimu katika safari ya kwenda Mashariki ya Mbali. Makaburu waliuchukia utawala wa Waingereza, na waliziona shughuli za maofisa wa Kiingereza, wamisionari au wafanya biashara, kama uvamizi usiovumilika katika mtindo wao wa maisha. Waingereza nao walitaka kusimika mamlaka yao. Walitaka hasa kutawala mpaka wa mashariki wa koloni hilo ambako walowezi walikuwa wameanza kupambana na Wanguni wa Kusini, zaidi wakiwemo Waxhosa ambao walikuwa na nguvu kuliko Wakhoisan wa Rasi ya Magharibi. Ili kuimarisha kuweko kwao humo nchini na kusaidia kutuliza hali iliyokuwepo, Waingereza, katika mwaka wa 1820, waligawa ardhi kwa walowezi wa Kiingereza katika sehemu ya Albany, karibu na Port Elizabeth.

Mahusiano miongoni mwa makundi mbalimbali ya Waafrika katika eneo hili yalikuwa ni ya amani kwa wastani. Mara chache palikuwa na migongano kati ya Wanguni wa kusini walioshi katika eneo la Cape ya Mashariki, na jirani zao Wakhoisan wa upande wa magharibi, na pia miongoni mwa Wanguni wenyewe kwa wenyewe. Bali mizozo hiyo kwa kawaida haikuvuka mipaka ya maeneo yanayohusika, na ilidhibitiwa

vilivyo. Kwa upande wa mahusiano kati ya Waafrika wa eneo hilo na majirani zao wa Kizungu, hali ilikuwa tofauti kabisa.

Mipaka ya Mashariki ya Rasi kuzunguka mto Great Fish, ilikuwa kwa uhakika mkoa wenye chuki kali na migogoro ya waziwazi kati ya Wazungu na Waafrika. Mambo yaliyosababisha migogoro hiyo yalikuwa ni mengi, kuanzia migogoro ya mipaka, wizi wa mifugo na mashindano ya kupata maeneo mazuri kwa ajili ya kilimo. Kwa kuangalia matukio yaliyokuwepo ni wazi kwamba katika mkesha wa Mfekane uhusiano kati ya Wazungu na Waafrika katika mkoa wa rasi haukuwa wa amani.

## *Hali ya uchumi na matarajio*

Kabla ya mlipuko wa Mfekane, hali ya kiuchumi na matarajio katika Koloni la Rasi (Cape) ilikuwa imepooza. Kundi jipya la Wazungu lilioingia katika Rasi mwaka 1820 ndilo lililohimili pigo hili kubwa la matatizo ya kiuchumi. Kilimo ambacho kilitakiwa kiwe uti wa mgongo wa uchumi na chanzo cha uhai wa watu wa Albany hakikushamiri. Matatizo yaliyosababisha hali hii ni mengi: walowezi wengi hawakuwa na ujuzi wala uzoefu katika kilimo; eneo lililogawiwa kwa kila mmoja wao lilikuwa dogo lilipolinganishwa na shamba la wastani la Kaburu kwa sababu maofisa hawa wa Kiingereza walitaka kuishi karibukaribu ili kuhakikisha ulinzi na udhibiti. Isitoshe, katika mwaka wa 1823 kulitokea mafuriko ambayo yaliharibu mazao yao mengi.

Matatizo haya yalisababisha wakulima wengi kutelekeza ardhi yao na kuvamia sehemu za katikati ya mji ambako walitafuta aina nyingine za ajira. Zaidi ya hayo, kulikuwepo na tatizo sugu ambalo liliwakumba sio tu walowezi wapya bali hata wakoloni wa zamani wa Kiholanzi katika makazi yao ya zamani katika Rasi. Hili lilikuwa ni tatizo la upungufu wa vibarua rahisi wa kuwasaidia katika mashamba yao. Wakati masetla wa zamani waliruhusiwa kuwatumia watumwa na kuajiri Waafrika mashambani na majumbani mwao, kutokana na shinikizo la ukomeshaji wa watumwa, masetla wapya hawakuruhusiwa kutumia watumwa wala kuajiri Waafrika. Matokeo yake ni kwamba masetla wapya waliathiriwa vibaya zaidi na tatizo hili, pamoja na jitihada zilizofanywa mnamo mwaka 1824 na Chama cha Kuwasaidia Masetla Wenye Dhiki, za kuchangisha fedha za kuwasaidia.

Matatizo haya ya kiuchumi yalikuzwa zaidi na hali mbaya ya usalama katika mipaka ya mashariki ya Rasi. Hili ni kwa sababu, pamoja na matatizo yao ya kiuchumi, wakulima hawa walitakiwa kulinda mipaka ya mashariki dhidi ya uchokozi wa Waafrika. Kwa hali hiyo, katika mkesha wa Mfekane, suala la upungufu wa nguvukazi lilibakia kuwa kidonda kibaya kwa Wazungu wa Koloni la Rasi, na hapakuonekana dalili ya amani ya kudumu katika mipaka ya mashariki.

## *Jibu la awali la Rasi 1823-8*

Uharibifu mkubwa uliosababishwa na vitendo vya Wazulu uliwafanya watu wengi - makundi yaliyokimbia makwao na watu binafsi - kukimbia kutoka majumbani mwao



**6.1** *Wanasesere wakiwakilisha mwanamume na mwanamke wa Kisan wanaouzwa huko Cape Town, mapema karne ya kumi na tisa*

kuelekea magharibi kwa kuvuka milima ya Drakensberg. Watu hawa walipokuwa wakikimbia walivamia vikundi vingine vilivyoishi katika maeneo waliyoyapitia, wakawaibia mifugo yao na kuteketeza nyumba zao na mazao yao. Jambo hili lilizua mfululizo mwingine wa wahamaji ambao walitimuliwa na makundi haya ya wazururaji. Baadhi ya wakimbizi waliofanikiwa kulifikia Koloni la Rasi, walijikuta wamekwisha kupoteza utambulisho wa vikundi vyao na viongozi wao. Walikuwa hawana mahali pa kuishi, huku wakiwa na njaa na bila usalama. Watu hawa hawakuwa tishio la kijeshi kwa vile hawakuwa na viongozi wala silaha. Walikuwa wanatafuta msaada, na fursa ya kulowea na kuanza maisha upya.

Jibu la Wazungu kwa idadi hii kubwa ya Waafrika waliokuwa wanaingia katika eneo lao lilitawaliwa na mahitaji mawili muhimu waliyokuwa nayo kabla ya kuzuka kwa Mfekane. Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, matatizo yao yalikuwa ni upungufu wa nguvukazi rahisi na kukosekana kwa usalama katika mipaka ya mashariki. Kwa bahati nzuri, wakimbizi wa Kisotho na Kitswana walianza kumiminikia katika Rasi wakati uleule masetla wapya wa Albany walipokuwa wanayakimbia mashamba yao kutokana na upungufu wa nguvukazi rahisi. Hivyo kwa msaada wa serikali ya Rasi, wakulima Wazungu waliweza kuwatumia wakimbizi hawa kikamilifu kuwafanyia kazi kwa gharama nafuu katika mashamba yao.

Jinsi muda ulivyopita maoni ya masetla Wazungu kuhusu wakimbizi wa Kisotho na Kitswana yalianza kubadilika. Wakati wengine waliwaona wakimbizi hawa kama watu wavivu na wasioaminika, wengine waliwaona kuwa watu wenye manufaa na faida kubwa. Hapa hatuna budi kutilia maanani kwamba, licha ya maoni ya walowezi wa Kizungu kuhusu manufaa ya wakimbizi hawa, Wasotho na Watswana walikuwa na manufaa makubwa katika kufanya kazi za sulubu za masetla hawa ambazo majirani zao Wakhoisan hawakupenda tena kuzifanya.

Ingawa haiwezekani kutoa idadi kamili ya Wasotho na Watswana waliotafuta hifadhi katika Rasi, makadirio ya harakaharaka yanaweza kutupa idadi ya kuanzia mamia kadhaa hadi watu elfu moja. Idadi ya wakimbizi walioingia katika Koloni la Rasi iliongezeka kila mwaka katika miaka mitano ya mwanzo ya Mfekane. Lakini hadi kufikia miaka ya mwisho ya 1820, tayari walishaanza kurejea katika nchi zao; idadi ya wakimbizi waliokuwa wanarejea makwao iliongezeka kwa kiasi kikubwa baada ya Mushweshwe kuanzisha dola la Wasotho.

Hata hivyo, umuhimu wa kuwepo kwa wakimbizi hawa katika Koloni la Rasi haupaswi kupuuzwa. Kufika kwao kwa wakati mwafaka kuliwasaidia masetla kutatua tatizo la upungufu wa wafanyakazi ambalo liliwakera kwa muda mrefu. Kuwepo kwao vilevile kuliimarisha utegemezi wa nguvukazi rahisi katika maendeleo ya uchumi wa Koloni, na hivyo kuathiri kanuni ya kujitegemea ambayo ilitarajiwa kutumika katika maeneo mapya ya masetla wa Kizungu. Zaidi ya hayo, kupatikana kwa nguvukazi rahisi katika Rasi kulileteleza mwelekeo wa kujipatia ardhi kubwa zaidi, kuacha kilimo shadidi na kujikita katika utaratibu wa zamani wa Makaburu wa kilimo cha mawanda mapana katika maeneo makubwa ya ardhi.

Wakimbizi wa Kitswana na Wakisotho nao pia walifaidika na kipindi walichoishi katika Koloni la Rasi. Sio tu kwamba walifadhiliwa kwa kupewa mahali pa kuishi wakati walipokuwa taabani, bali pia walilipwa kwa huduma walizotoa. Kutokana na hali hii, wengi kati yao waliweza kujipatia mali ambayo waliruhusiwa kuondoka nayo waliporejea katika nchi zao.

Ingawa kuwepo kwa wakimbizi wa Kitswana na wa Kisotho katika Rasi kuliondosha tatizo la ukosekanaji wa nguvu kazi uliokuwa umewakabili masetla, lakini hakukutatua tatizo lao la pili, lile la kuwapo kwa hali ya wasiwasi katika mipaka ya mashariki. Hii haimaanishi kwamba uhusiano kati ya masetla wa Kizungu wa koloni la Rasi na majirani zao Wanguni wa Kusini kama vile Waxhosa katika mipaka ya Mashariki wakati wote ulikuwa wa chuki na mapambano. Kulikuwepo pia ruwaza ya uhusiano wa kibiashara kati yao.

Makundi hayo mawili yalipotambua kwamba yanategemeana katika kupata bidhaa mbalimbali yalilazimika kuingia katika mapatano ya kibiashara. Waxhosa walikuwa na pembe za ndovu, pembe, ngozi, nyama na mpira, vitu ambavyo walivibadilisha kwa vifaa kutoka nje kama vile shaba, shanga, vifungo, bunduki, baruti na pombe kali kutoka kwa Wazungu. Hivyo, mfumo wa kubadilishana mali kwa mali ulianzishwa kati ya maselta Wazungu na majirani zao Waxhosa. Kutegemeana huku kibiashara kulishamiri kiasi cha kukwamisha juhudi zote za serikali ya kikoloni katika Rasi za kukukomesha. Udhibiti imara wa serikali katika mipaka uliongeza tu kasi ya biashara ya magendo.

Katika mwaka wa 1821 kulianzishwa maonyesho ya kawaida ya biashara katika mpaka wa Mashariki. Maonyesho haya yalianzishwa kama tukio la mara moja kwa mwaka, lakini ilipofikia mwaka 1824 tayari lilikwisha kuwa gulio la kila wiki. Zaidi ya hayo, maonyesho hayo hayakuwa kituo cha biashara tu, bali pia baraza la maingiliano na mawasiliano muhimu kati ya weusi na weupe. Hata hivyo, chini ya maelewano yaliyoletwa na soko hili, kulikuwepo na chuki kali kati ya weupe na weusi. Katika nchi ya Waxhosa watu walijihusisha na biashara ya siri ya silaha kati yao na wafanya magendo wa Kizungu. Waxhosa walikuwa wanajikusanyia silaha kwa matayarisho ya shambulio kali dhidi ya weupe ambapo wangelipiza kisasi cha kuporwa kwa ardhi ya mababu zao na maselta hao. Shambulio hilo lilikuja 1834-5, likifuatiwa na vita vingine kadhaa ambavyo Waxhosa walipigana na Wazungu, bila kutaja ukamataji na utekaji wa mara kwa mara wa watoto wa Kizungu; baadhi ya watoto hao baadaye waliwaua.

## *Tishio kutoka nje na jibu la pamoja la weusi na weupe*

Uimara wa uhusiano kati ya weusi na weupe katika Rasi haukutishiwa sana na matukio ya Mfekane kabla ya mwaka 1828. Wakimbizi wa Kitswana na Kisotho waliomiminikia katika Rasi baada ya mwaka 1823 hawakuwa tishio kwa jumuiya ya maselta; waliingizwa kwa amani katika maisha yao ya kiuchumi, na hatimaye walirejea makwao. Mara chache kulikuwepo na ushirikiano kati ya weusi na weupe kama vile wakati Wampondo, ambao ni kikundi kimojawapo cha Wanguni wa Kusini, walipolizuia jeshi la Shaka kuingia nchini, na hivyo kuwa kama kinga kwa masetla wa Kizungu.

Hata hivyo, mnamo mwaka 1828, kikundi tofauti cha wakimbizi, Wangwane, wakiongozwa na Matiwane, walifika kutishia wenyeji wa Rasi. Walikuwa tofauti na wakimbizi wa Kitswana na wa Kisotho kwa vile walikuwa na utambulisho wa kikundi pamoja na kiongozi. Hali ilizidi kuwa ngumu zaidi kwa sababu kuingia kwa Wangwane katika mkoa wa Rasi kulitokea sambamba na nia ya jeshi la Wazulu, likiongozwa na Shaka, kujipenyeza katika Rasi. Tukio hili lilisababisha wasiwasi mkubwa miongoni mwa jumuiya ya maselta weupe. Kwa hivyo, mara Wangwane walipoingia katika eneo la Waafrika katika mkoa wa Rasi, walishambuliwa na majeshi ya kikoloni ya Rasi, ambayo yaliwadhania kuwa Wazulu. Pambano hili, hata hivyo halikuleta matokeo yoyote ya mkataa. Kwa hivyo matayarisho yalifanywa kwa ajili ya vita vikubwa dhidi ya Wangwane. Ili kufanikisha lengo hili, weupe waliomba msaada wa majirani zao Waxhosa na Wathembu. Hivyo jumuisho la vikosi vya weupe na weusi ndilo lililowashambulia na kuwashinda Wangwane.

Mapigano haya yalikuwa muhimu sana kwa sababu mbili. Ya kwanza ni kwamba kushindwa kwa Wangwane kuliondosha kwa uhakika mmoja wa mawakala wenye nguvu na waharibifu wa Mfekane. Kuanzia wakati huo, koloni la Rasi na majirani zake wa Kiafrika waliondokana na tishio kali kutoka nje. Pili, wakati madhumuni ya watu weupe ya kujiingiza katika mapigano hayo hayakuwa wazi sana, hasa kwa vile eneo lao halikuwa kwenye hatari kubwa ya kuvamiwa wa Wangwane kwa wakati ule, kampeni ya 1828 ilikuwa ni fursa kwa weusi na weupe (Waingereza na Waxhosa) kuahirisha chuki zao na kushirikiana katika jukumu la pamoja. Hii inamaanisha kwamba pamoja na migogoro ya mara kwa mara ya siku za nyuma, uhusiano kati ya maselta wa Kiingereza na Waxhosa ulikuwa na uwiano ambao ulionekana kutishiwa na wavamizi kutoka nje, na ambao ulilazimisha kuwepo kwa ushirikiano kati ya makundi haya mawili.

## *Kuibuka kwa Mfengu*

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, Mfekane ilisababisha watu wengi kuwa wasikwao, bila utambulisho wa kikundi wala kiongozi, na kuwafanya watangetange kutoka sehemu moja hadi nyingine. Watu wengine kati ya hawa waliokimbizwa kutoka makwao, hasa kutoka Unguni ya kaskazini, walianza kuingia katika eneo la Wanguni wa Rasi (yaani Unguni ya kusini). Walifika wakiwa ni mtu mmoja mmoja au vikundi vidogovidogo, na kwa vile walikuwa maskini na bila makazi, walikuwa ombaomba. Kutokana na kitendo hiki cha kuombaomba walipewa jina la "Mfengu." Jina *Wamfengu* mwishowe lilitumika kwa ujumla kuwaita wakimbizi kutoka Unguni ya kaskazini ambao walipokelewa katika eneo la Unguni ya kusini baada ya kutimuliwa na kutawanywa na Mfekane.

Idadi ya wakimbizi hawa ilianza kuongezeka kwa kiasi kikubwa kati ya 1822 na 1828; idadi hii ilikuzwa zaidi na Wangwane waliosalia baada ya kushindwa katika vita vya pamoja vya weusi na weupe katika eneo la Rasi. Wamfengu walipokelewa kwa moyo mkunjufu na vikundi vya Wanguni wa kusini - Waxhosa, Wathembu, na Wampondo - ambao waliwapatia chakula, ardhi na mifugo. Wamfengu wengi waliweza kujipatia mali kiasi kutokana na kufanya kazi kwa bidii. Kwa hiyo, wale waliolowea katika nchi ya Wampondo na Wathembu waliunganishwa katika jumuiya za wenyeji

wao. Lakini wale waliokuwa katika nchi ya Waxhosa walijihisi kubaguliwa na hawakuingizwa katika jumuiya ya Waxhosa.

Haieleweki ni jambo gani lililosababisha uhusiano mzuri uliokuwepo hapo awali kati ya Wamfengu na wenyeji wao Waxhosa kuwa mbaya. Lakini mara hali hii ilipojitokeza, uhusiano wa Waxhosa na Waingereza, ambao tayari ulikuwa wa kuvutana, ulizidi kuwa mbaya. Zaidi ya hayo uhusiano wa chuki kati ya Wakhosa na Wamfengu ulitumiwa vibaya na nguvu fulani za nje ili kudumisha mgawanyiko kati ya Waafrika na hivyo kukuza maslahi yao. Nguvu hizi za nje zilikuwa ni kutoka Chama cha Wamisionari cha Wamethodi wa Ki-Wesley, walowezi Wazungu na serikali ya koloni la Rasi.

Kuwepo kwa wamisionari wa ki-Wesley katika ardhi ya Waxhosa katika mwaka 1827 kuliingilia wendo wa kuwaingiza Wamfengu katika jamii ya Waxhosa, jambo ambalo lilikuwa tayari limeshajionyesha kama tatizo. Wamisionari walitafsiri uhusiano kati ya mtawala na mtawaliwa kati ya Waxhosa na Wamfengu kuwa sawa na uhusiano kati ya bwana na mtumwa. Hatimaye, wamisionari waliona huruma juu ya hali mbaya za Wamfengu na, pamoja na serikali ya Rasi, waliona walihitaji kufanya jambo fulani ili kutatua tatizo la Wamfengu. Wamfengu nao kwa upande wao walianza kuwatazama wamisionari, serikali ya Rasi na masetla Wazungu kama wakombozi wao.

Vikundi hivi vya nje, hata hivyo, vilikuwa na nia iliyofichika kwa kujihusisha na utetezi wa Wafengu. Wamisionari walitaka Wamfengu waridhie kupokea mafundisho ya Kikristo. Serikali ya Rasi na masetla weupe walitumaini kwamba kwa kuwachochea Wamfengu kupoteza imani yao kwa watawala wa Kixhosa, wangepatikana upesi zaidi kuajiriwa kama nguvukazi rahisi katika mashamba yao. Zaidi ya hayo, Wamfengu walikuwa wamewakinai Wakhosa, na walikuwa wakitafuta fursa mpya ya kujitenga nao kabisa na kutafuta maskani mapya ya kuishi na kujitafutia maisha mapya.

Huu ndio uliokuwa usuli wa Vita vya Sita vya Mpakani vya 1834-5 kati ya Waingereza na Waxhosa. Katika mgogoro huu, Wamfengu walikataa kujiunga na Waxhosa kulivamia koloni la Rasi; badala yake, walijitia katika kuwalinda wamisionari na wafanyabiashara, kuwapeleleza Waxhosa, na kutoa siri za mipango na nyendo zao kwa Waingereza. Mwishowe, mnamo tarehe 9 Mei, 1835, kiasi cha Wamfengu 16,000 waliondoka katika ardhi ya Waxhosa wakiwa na mifugo na mbuzi waliokuwa mali ya watemi wa Waxhosa, chini ya ulinzi wa kijeshi uliotolewa na vikosi vya Waingereza, kuelekea makazi mapya waliyopewa katika Rasi na serikali ya Rasi.

Mara walipofika eneo lao jipya, Wamfengu waliwasaidia Waingereza kuwashambulia na kuwatimua Waxhosa. Kadhalika, walitoa nguvukazi rahisi kwa masetla wa Kizungu. Wamfengu vilevile warishirikiana na wamisionari kwa kuruhusu watoto wao wafundishwe na wamisionari; aidha, watu wengi wazima pia walihudhuria ibada za kanisani. Wamfengu vilevile walitumiwa kuwadhoofisha Waxhosa katika migogoro iliyofuatia kati yao na weupe kwa kuwa eneo walilopewa walowezi lilikuwa baina ya Waxhosa na koloni la Rasi.

## *Makaburu wa Safari Ndefu (TREK)*

Kushindwa kwa Waxhosa katika mwaka 1835 hakukumaliza migogoro ya mpakani. Vita

vingi zaidi vilitokea kwenye miaka ya 1846, 1850-53, na 1877-8, wakati Waingereza walipojaribu kuhamisha mpaka kutoka mto mmoja hadi mwingine ndani zaidi kuelekea mashariki. Kusema kweli Makaburu wengi walipendelea kuhamahama, wakiwa wanajihusisha na kilimo cha mchanganyiko, huku wakitafuta, bila kutulia, ardhi kubwa na nzuri zaidi. Kama tulivyoona, jambo hili lilikuwa kweli pia kwa Wanguni wa kusini ambao walitokea kuwa pingamizi kwa Makaburu waliokuwa wakisambaa kuelekea mashariki. Katika kipindi cha Mfekane, makaburu wengi tayari walishalowea mbali kupita mto Great Fish ambao ulikuwa mpaka wao rasmi na Waxhosa. Serikali ya Rasi ilitumia fursa ya kushindwa kwa Waxhosa kujitwalia sehemu kubwa ya ardhi ya Waxhosa ili kupanua koloni la Rasi. Wakati ofisi ya koloni, kwa kiasi fulani ikishinikizwa na wamisionari, ilipokataa utwaaji huu wa ardhi, makaburu kadhaa katika jimbo lililopendekezwa waliamua kuhamia nje ya maeneo yaliyokuwa chini ya mamlaka ya Waingereza. Walichukia wamisionari wa Kiingereza, sheria za kazi za Kiingereza, mfumo wa sheria wa Waingereza na sera zao za ardhi. Kuhama huku kwa idadi kubwa ya watu mara nyingi kunajulikana kama Safari Ndefu Kuu, na makaburu walioshiriki katika safari hii walijulikana kama Makaburu wa Safari Ndefu.

Kati ya 1835 na 1841 zaidi ya Makaburu 6,000 - wanaume, wanawake na watoto - wakiwa na mali zao zinazohamishika zikiwa zimepakiwa katika mikokoteni ya maksai, na watumishi wao wa Kiafrika, ng'ombe na kondoo, waliondoka katika jimbo jipya na sehemu nyinginezo za Rasi ya Mashariki. Walikwenda kwa vikundi vya misafara iliyoandaliwa kwa utaratibu maalumu na kuingia maeneo ambayo maskauti walikuwa wameshabainisha kuwa yalikuwa na wakazi wachache. Maeneo haya, hata hivyo, yalikuwa ni ardhi teule yenye rutuba, iliyokaliwa na watu wengi, lakini ambayo sasa ilikuwa imehamwa kwa muda kutokana na Mfekane, iliyosababisha vikundi vingi vilivyoitamani ardhi hiyo viipiganie. Vikundi viwili vilivyokuwa na nguvu zaidi katika eneo hili vilikwa ni Wazulu, ambao sasa wakitawaliwa na Dingane, na Wandebele chini ya Mzilikazi, mmojawapo wa majenerali wa zamani wa Shaka.

Kikundi kimoja cha Makaburu kilielekea Natal, kikafanya shauri na Dingane kupata ardhi ambayo ingewaruhusu Makaburu kuifikia bahari. Dingane alielekea kukubalina nao, lakini kwa vile hakuwaamini Makaburu, aliwavizia njiani na kuua Makaburu 350 na karibuni watumishi wao 250. Makaburu waliunda upya vikosi vyao, wakarudi na kupambana vikali na Wazulu na kuwashinda vibaya. Tukio hili liliashiria mwanzo wa kuporomoka kwa Wazulu kutokana na mgawanyiko uliotokea katika familia ya kifalme, wengine wakiwatumia marafiki wa Kikaburu dhidi ya wenzao.

Vikundi vingi zaidi vya Makaburu hata hivyo vilielekea kaskazini kwenye ardhi ya rutuba sana katika nyanda za juu, pande zote mbili za mto Vaal. Punde walikabiliana na Mzilikazi, ambaye pia alikuwa amechagua eneo hilo hilo kwa ajili ya vikosi vyake na wafuasi wake wa Kindebele. Makaburu waliweza kujikusanyia marafiki Waafrika wa kutosha waliojihisi kutishiwa na Mzilikazi. Wakiwa na bunduki, pamoja na kuungwa mkono, walifanikiwa kumng'oa Mzilikazi ambaye aliamua kwenda kaskazini zaidi, kuvuka Limpopo kuelekea eneo ambalo sasa ni Zimbabwe. Makaburu waliolowea kusini mwa Vaal baadaye walijiunga pamoja na kuunda Orange Free State, wakati eneo

lililokaliwa na masetla wa upande wa pili wa Vaal lilipewa jina la Transvaal.

## *Hitimisho*

Vuguvugu la Mfekane lilisababisha mabadiliko ambayo yaliathiri vipengele vya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kijeshi vya maisha ya jamii za Afrika ya Kusini. Kushadidia kwa mabadiliko hayo hata hiyo kulitofautiana kati ya eneo na eneo, na pia kulitegemea hali ya watu waliohusishwa. Kutokana na maelezo hayo hapo juu, ni dhahiri kwamba aina tatu za maathura wa janga la Mfekane waliingia Koloni la Rasi. Kwanza walikuwepo wakimbizi wasikwao na wenye njaa, yaani, Watswana, Wasotho, Wamfengu na Wanguni wengine wa kaskazini, ambao walifika kutafuta hifadhi, chakula na ulinzi. Wa pili ni jeshi la Shaka, Mfalme wa Wazulu, ambalo lilifika kwenye ardhi ya Mpondo, lakini halikuweza kupenya kutokana na pingamizi kutoka kwa Wampondo. Wa tatu walikuwa ni vikundi vingine vya uchokozi kama vile Wangwane ambao walilitia wasiwasi jimbo la Rasi kwa kuwepo kwao katika ardhi ya Wathembu. Wangwane hawa walidhaniwa kwa makosa kuwa ni Wazulu wa Shaka, na vikosi vya pamoja vya Waingereza, Waxhosa na Wathembu viliwashambulia na kuwashinda. Muungano huu wa kijeshi kati ya weusi na weupe haukudumu kwa sababu uliyeyuka mara baada ya kutoweka kwa tishio la Wangwane.

Hata hivyo, athari za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni za Mfekane zilikuwa za kudumu zaidi katika koloni za Rasi kuliko zile za kijeshi na kisiasa. Kufika kwa wakati muafaka kwa wakimbizi wa Kisotho na Kitswana kulizinusuru wilaya za masetla kama vile Albany katika Rasi zisiporomoke kabisa kutokana na ukosefu wa vibarua. Kupatikana kwa wafanyakazi wengi kulidhoofisha kanuni pacha za masetla za kujitegemea na kuendesha kilimo shahidi ambazo zilikuwa msingi wa kuanzishwa kwa makazi mapya ya kilimo.

Zaidi ya hayo, kuhamia kwa Wamfengu katika Rasi katika mwaka 1835 pia kulihakikisha upatikanaji wa mfululizo wa nguvukazi rahisi kwa masetla weupe.

Athari za kisiasa za Wamfengu kwa wenyeji wao Waxhosa zilifutika baada ya wao kuondoka na kuhamia katika ardhi ya Waingereza katika Rasi, ambako, wakiwa raia wa Waingereza, walipigana dhidi ya Waxhosa. Athari za kiutamaduni za Wamfengu kwa masetla weupe na kwa majirani zao weusi si rahisi kutathminiwa hasa kwa vile Wamfengu walikuwa na utamaduni unaofanana na ule wa Wanguni wa Rasi. Athari ya Wamfengu ilikuwa na umuhimu zaidi hasa kwa kuwa wao walikuwa kundi la kwanza la Wanguni kupokea Ukristo na elimu ya Magharibi, na hivyo kuchukua dhima muhimu kama wakala wa kuleta mambo ya kisasa miongoni mwa vikundi vingine vya Kiafrika katika Rasi, wakiwa wao ndio walimu, makarani, makasisi, na mabwana shamba.

Mwishowe, Mfekane ilikuwa muhimu kwa historia ya Afrika ya Kusini sio tu kutokana na vikundi vya watu ilivyoviingiza katika Koloni la Rasi. Labda, muhimu zaidi ni dhima yake ya kuwavutia Makaburu wa Safari Ndefu kuingia katika maeneo yaliyozungukwa na mataifa ya Kiafrika yenye nguvu. Kabla ya Mfekane, walowezi wa Kizungu walikuwa katika kona moja ya Afrika ya Kusini, wakikabiliana na pingamizi la

Wanguni wa kusini. Mfekane na Safari Kuu Ndefu vilifika kama mlipuko mkubwa uliowatawanya masetla wa Kikaburu miongoni mwa madola ya Wanguni ya kaskazini na kusini, yaliyoundwa upya na kuimarishwa na Mfekane. Mgogoro wa kijamii uliokuwa katika mpaka wa Mashariki wa Koloni la Rasi, baada ya miaka michache tu uliweza kuenea katika nchi nzima ya Afrika Kusini.

# 7

# *Waingereza, Makaburu na Afrika nchini Afrika Kusini, 1850-80*

Kabla ya mwaka 1880 Afrika Kusini haikuwa na umuhimu mahsusi wa kisiasa; ilikuwa ni eneo tu la kijiografia lililojumuisha makoloni ya Waingereza, jamhuri za Makaburu na madola ya Waafrika. Hadi 1870, Waingereza, ambao walijiona kuwa na kiasi fulani cha mamlaka juu ya eneo hili, walisita kuchukua udhibiti wa kisiasa wa eneo zima kutokana na matatizo ya kifedha. Lakini kuanzia 1870 na kuendelea, walipigana vita na kutwaa madola mengi ya Kiafrika katika eneo hili. Mwelekeo huu wa kibeberu ulisababisha kuwepo vita kadha wa kadha baina ya Waingereza na Makaburu. Kutokana na vita hivyo, Waingereza walijichukulia sehemu kubwa ya Afrika Kusini. Hivyo katika kipindi cha kati ya 1850 na 1880, Waafrika polepole walipoteza ardhi na uhuru wao, Makaburu waliungana zaidi, na makoloni ya Kiingereza yalipata namna fulani ya serikali za madaraka.

## *Kujitoa kwa Waingereza kutoka Bara*

Waingereza walianza kujitoa kutoka bara ya Afrika Kusini kwenye miaka ya 1850. Awali walikuwa wameyashikilia maeneo hayo kutokana na shinikizo la Sir Harry Smith, Gavana na Balozi wa Cape. Aliteka nchi ya Waxhosa na eneo kubwa kati ya mito ya Orange na Vaal lililokuwa na jumuiya za Waafrika na Makaburu. Kama ilivyotarajiwa, sera hii ya upanuzi ilileta vita vikali kwa sababu watu waliokandamizwa walihitaji kulinda uhuru wao, na hususan Waafrika hawakutaka kupoteza ardhi yao.

Upinzani wa kwanza wa kutumia silaha ulifanywa na Makaburu ambao mwaka 1848 waliwafukuza Waingereza kutoka kwenye eneo lao. Lakini hawakuuimarisha ushindi wao kwa sababu Waingereza walilipiza kisasi, wakawashinda vibaya na kuliteka tena eneo hilo. Hata hivyo, suala la uwekaji mipaka lilikuwa tatizo kwa Waingereza. Kila jitihada waliyofanya kuweka mipaka kati ya Waafrika na Makaburu daima iliridhisha upande mmoja na kuuacha mwingine ukinung'unika. Hii ilipelekea upande usioridhika kuvuka mipaka na kupora mifugo ya upande mwingine. Husasani ufalme wa Wasotho chini ya Mushweshwe, ulipunjwa sana na marekebisho haya ya mipaka. Aidha, Waingereza walitaka kuimarisha nafasi yao kwenye eneo hilo kwa kugonganisha kundi moja dhidi ya jingine huku wakijifanya wapatanishi wa kujitolea. Mfano wa tukio la namna hii, ambalo liliwageukia Waingereza wenyewe, ni kuzuka kwa vita kati ya




**7.1** *Ramani ya Afrika Kusini ikionyesha dola na watu, 1850-80 (N. Bhebe)*

vikundi viwili vya Waafrika, Wataung na Watlokwa. Waingereza waliwasaidia Watlokwa na wakalishinda jeshi la Wataung na kupora zaidi ya ng'ombe 3,000. Hii iliwafanya Wasotho chini ya Mushweshwe waungane na jeshi shinde la Wataung, na kwa pamoja wakawashinda Waingereza na marafiki zao wa Kiafrika, na kupelekea kwenye kuanguka kwa utawala wa Waingereza katika eneo hilo mnamo 1851.

Hiki kilikuwa kipindi ambapo Waingereza pia walikuwa na matatizo makubwa na Waxhosa wa Cape Colony. Vita vya Waingereza -Waxhosa vya 1850-3 vilisababishwa na Waingereza kuingilia mambo ya Waxhosa. Kwa kutangaza koloni katika eneo la Waxhosa, Waingereza waliwapokonya Waxhosa ardhi yao na hata kuwapatia sehemu ya ardhi hiyo Wamfengu na vikundi vingine vya Waafrika vilivyowatii Waingereza. Zaidi ya hayo, Waingereza waliwaweka kwa mabavu mahakimu wa Kizungu katika nchi ya Waxhosa, ambao hawakujua chochote kuhusu sheria za Kiafrika. Aidha walibatilisha baadhi ya mila za Kixhosa, kama vile ulipaji wa mahari. Mambo yote hayo yaliwaudhi sana Waxhosa na walitafuta kila njia ili wajikomboe kutoka kwenye ukoloni wa Waingereza. Nafasi hiyo ilipatikana pale Waingereza walipomwondoa madarakani chifu wa Kixhosa na kujaribu kumsimika Mzungu pahala pake. Wananchi walipinga jambo hili na mnamo Desemba 1850 wakaanza kuyashambulia majeshi ya Kiingereza na vituo vya kijeshi vilivyokuwepo kwenye ardhi yao. Waafrika wengine wengi waliungana na Waxhosa na kupigana vita dhidi ya Waingereza. Vita viliendelea hadi Oktoba 1852 wakati Waingereza hatimaye walipowashinda Waxhosa na kupora idadi kubwa ya ng'ombe wao.

Vita hivi vya gharama kubwa dhidi ya Waxhosa na kuvurugika kwa utawala wa Waingereza katika bara ya Afrika Kusini kuliwafanya Waingereza waanze kujitoa katika eneo hilo. Ili waweze hapo baadaye kupita bara pasi na matatizo, Waingereza waliwapatia Makaburu wa bara uhuru. Aidha, walifanya nao mkataba wa kutowauzia Waafrika silaha na risasi, na hivyo kuhakikisha kuwa Wazungu daima watakuwa na zana bora za kivita kuliko Waafrika.

Kabla ya kujitoa kabisa kutoka bara, Balozi mpya wa Uingereza alitaka kuonyesha nguvu mpya ya jeshi la Waingereza kwa kuushambulia ufalme wa Mushweshwe. Hata hivyo, upinzani mkubwa alioupata kwa Wasotho ulimfanya ajitoe bara haraka. Uzoefu huu uliimarisha zaidi imani kwamba itakuwa ni gharama kubwa mno kwa Waingereza kudumisha utawala wao kwenye bara ya Afrika Kusini. Kwa vile Waingereza walitengwa na ufalme wa Mushweshwe, walitafuta urafiki na vikundi vingine vya Makaburu katika eneo hilo.

Mashariki mwa Cape Colony, Waingereza walipora ardhi ya Waxhosa waliotiishwa na kuwauzia wakulima wa Kizungu na nyingine kuwapatia Wamfengu. Waingereza pia walitaka kuliendeleza eneo hili kama ukanda wa kujikinga dhidi ya mashambulizi ya Waafrika kutoka mashariki. Hadi kufikia 1854, Waingereza walikuwa wamejitoa katika masuala ya Waafrika na Makaburu huko bara. Lakini walidumisha mamlaka yao huko Cape Colony na Natal ili kuwanyima Makaburu njia ya moja kwa moja ya kufika baharini na kwenye kituo cha jeshi la wanamaji la Waingereza. Natal na Cape Colony zilipatiwa serikali za madaraka ili ziweze kuwajibika kwa gharama za ulinzi na utawala

wake. Mnamo 1853, Cape Colony ilipatiwa katiba ya kibunge ambapo Natal ilipata Baraza la Kutunga Sheria mwaka 1856.

## *Cape Colony na Natal Kabla ya 1870*

Waingereza waliipatia Cape Colony namna fulani ya serikali ya madaraka kunako 1853 kutokana na sababu mbalimbali kuanzia zile za shinikizo la koloni lenyewe hadi sababu za kiuchumi. Serikali ya madaraka ilizingatiwa katika katiba ya kibunge. Katiba hii, huku ikilinda maslahi ya wafanyabiashara matajiri wa Kiingereza, ilitoa ushiriki wa kisiasa mdogo sana kwa Makaburu, Machotara na Waafrika. Haki ya kupiga kura ilitegemea utajiri wa mtu, ilihali mtu alilazimika kuwa raia wa Kiingereza mwenye haki ya kupiga kura na mwenye mali nyingi katika Cape ndipo astahili kugombea kiti katika bunge. Bunge, ambalo liligawika katika mabaraza mawili, liliruhusu matajiri wakubwa tu kuingia kwenye baraza la juu. Baraza la chini lilijumuisha Waingereza wenye mali ya thamani ya pauni 25 au mshahara wa pauni 50 kwa mwaka. Manmizi ya Kiingereza katika kuendeshea shughuli za bunge pia yalilazimisha idadi kubwa ya Makaburu kushindwa kugombea hata viti vya baraza la chini.

Bunge la Cape lilitawaliwa na masuala mawili muhimu. Moja lilihusu matakwa ya wazungumzaji wa Kiingereza wa wilaya za mashariki mwa Cape ya kuligawa koloni kwa vile waliogopa kutawaliwa na wazungumzaji wa Kiholanzi wa wilaya za magharibi. Suala jingine lilihusu mgogoro wa mara kwa mara kati ya mamlaka ya utendaji na mamlaka ya kutunga sheria. Kwa vile muundo wa kisiasa haukuwa na mawaziri, katiba ilitoa madaraka makubwa mno kwa Gavana. Hivyo utendaji kazi mzuri wa katiba ulitegemea haiba ya Gavana na hali ya uchumi ya koloni. Hali ya uchumi ilipokuwa mbaya na Gavana akawa mzembe, palitokea misuguano mingi kati ya bunge na mamlaka ya kiutendaji. Hata kupatiwa serikali ya madaraka kwa Cape mnamo 1872 hakukukomesha migongano ya mara kwa mara kati ya Gavana na bunge. Madaraka ya kikatiba ya Gavana yaliendelea kuchochea migongano kati yake na Baraza la Mawaziri la Cape ambalo wajumbe wake walikuwa warasimu.

Wakati wa utawala wa Magavana George Grey na Philip Wadehouse huko Cape, Waxhosa wa mashariki walipoteza kabisa uhuru wao. Masetla wa Kizungu walipandikizwa katika nchi ya Waxhosa ili "kuwastaarabisha" wenyeji, na mamlaka ya kisiasa ya machifu yalipunguzwa kwa kiwango kikubwa. Kuthibitisha utiifu wao, machifu wa Kixhosa walilipwa mishahara na Waingereza. Waxhosa pia walitozwa kodi na kutumikishwa kwenye miradi ya umma kwa ujira mdogo sana. Matatizo yote haya yaliwafanya Waxhosa na majirani zao Wathembu watafute masuluhisho ya kidini mnamo 1856-7. Katika kutekeleza ubashiri wa kidini, waliwaua ng'ombe wao wote na kuteketeza hifadhi yao ya nafaka wakiamini kuwa, kutokana na nguvu fulani za kimiujiza, Waingereza watahama, nao watarejeshewa ng'ombe na nafaka zao, na pia wataendelea kupata bidhaa zilizotengenezwa huko Ulaya. Unafuu huu uliotarajiwa haukupatikana, na watu wengi walikufa kwa njaa, ilihali wengine walikwenda Cape kutafuta ajira kwa Wazungu ili waweze kujikimu.

Gavana wa Cape alitumia udhaifu huu wa Waxhosa na Wathembu kuchukua sehemu kubwa ya ardhi yao, na baadaye aliwahimiza walowezi wa Kizungu kufanya makazi katika ardhi hiyo. Hatimaye, mwaka 1865, alililiteka eneo hili na kulifanyia sehemu ya Cape Colony kwa sababu matatizo ya kifedha yalifanya iwe vigumu kwake kulibakiza eneo hilo kama koloni tofauti.

Natal hali kadhalika ilishuhudia maendeleo ya kikatiba kwenye kipindi cha kabla ya 1870. Makaburu wengi wa Natal walianza kuhama kutokana na manung'uniko kadhaa dhidi ya sera ya Waingereza. Baadhi ya matatizo ya awali yaliyokabiliwa na serikali ya Kikoloni ya Natal yalihusu utawala wa Waafrika. Ili kutatua tatizo hili Waafrika waliwekwa katika hifadhi maalum (rizavu) chini ya machifu wao na majumbe ambako sheria za kimila ziliruhusiwa kutumika. Ili kuliendesha koloni, Waingereza walianzisha kodi ya kibanda kwa Waafrika ambao maliasili yao pia ilinyonywa bila simile. Kufuatia kuondoka kwa Makaburu ambao walihamia bara wakati wa Mfekane, Waingereza wengi walikuja kufanya makazi Natal. Mnamo 1856, Natal ilifanywa koloni na kupatiwa baraza la kutunga sheria. Lakini ni Wazungu tu ndio waliokuwa na haki ya kupiga kura. Waafrika walinyimwa haki ya kupiga kura kwa kukosa sifa za kuwa na mali nyingi, za kimakazi na nyinginezo.

Uchumi wa Natal ulitegemea tasnia ya sukari. Hata hivyo, Waafrika waligoma kufanya kazi kwenye mashamba ya miwa kwa sababu ya ujira mdogo mno. Hatimaye, wakulima wa Natal walilazimika kutumia vibarua wa mkataba kutoka India kwenye mashamba yao ya miwa.

Hivyo katika Natal na Cape Colony Wazungu waliimarisha utawala wao wa kisiasa huku Waafrika wakinyonywa na kunyimwa haki ya kumiliki ardhi. Hali kadhalika hatua mbalimbali zilichukuliwa kuhakikisha kuwa mshikamano wa kijamii wa Waafrika unaharibiwa kabisa.

## *Jamhuri za Makaburu kabla ya 1870*

Wakati Waingereza wanajitoa kutoka bara ya Afrika Kusini, Makaburu walikuwa wamegawanyika katika vikundi vingi. Baadhi yao walikuwa kaskazini mwa Mto Vaal, na wengine walikuwa kusini. Jamhuri mbili za Makaburu hatimaye ziliibuka katika maeneo haya: ya Orange Free State iliyopo kusini na ya Transvaal (Jamhuri ya Afrika Kusini) iliyopo kaskazini.

Jamhuri ya Orange Free State ilikuwa na matatizo kadhaa wakati ilipoanzishwa. Licha ya umaskini na ukosefu wa muundo wa kiutawala, ilikuwa pia dhaifu sana kijeshi. Hali hii iliifanya ionewe na jirani yake mwenye nguvu, yaani ufalme wa Wasotho wa Mushweshwe, ambao ilikuwa na mgogoro wa mpaka nao. Mapigano makali ya kugombea mipaka yalizuka mara kwa mara baina ya pande hizo mbili, na yalisababisha jamhuri hii ya Makaburu kuingiliwa bila kupenda na Waingereza kutoka Cape Colony na Jamhuri nyingine ya Makaburu ya Transvaal iliyokuwa kaskazini.

Tatizo jingine lililoikumba Orange Free State ni mfarakano wa wananchi wake. Hii ilisababishwa na kuanzishwa kwa vikundi vitatu vinavyopingana ndani ya jamhuri.

Kikundi cha kwanza kilichoitwa cha "watiifu" kilijumuisha Makaburu waliotaka jamhuri itekwe tena na kurejeshwa kwenye Cape Colony. Kikundi cha pili kilikuwa cha "wapenda muungano" ambao walitaka muungano kati ya Orange Free State na Jamhuri ya Transvaal iliyokuwa kaskazini. Kikundi cha tatu kilijumuisha wale waliotaka uhuru kamili wa Jamhuri ya Orange. Kwa vile kila kimoja cha vikundi hivi kilipigania msimamo wake ukubalike na vikundi vingine, migogoro mingi ilizuka katika jamhuri. Ilipofika 1863, juhudi zote za kuiunganisha Orange Free State na ama Cape Colony au Transvaal zilikuwa zimeshashindikana na watu wa Orange walianza kutazama ndani katika kutafakari juu ya majaaliwa ya taifa lao.

Uhusiano kati ya Orange Free State na Transvaal kabla ya 1850 haukuwa imara. Kulikuwepo na jitihada nyingi za kuziunganisha jamhuri hizi mbili lakini zote hazikufanikiwa. Mnamo Juni 1857, jamhuri hizo mbili zilitia sahihi makubaliano ambayo kwayo kila moja ilitambua uhuru wa mwenzake. Hata hivyo makubaliano hayo hayakukomesha jitihada za kuziunganisha jamhuri hizi mbili. Mwaka 1860 Jamhuri ya Orange ilimpigia kura Rais wa Transvaal, M.W Pretorius, ili awe Rais wao pia (1960-63). Hii ilikuwa ni nafasi nzuri kabisa kwa jamhuri hizi mbili kuungana, lakini bunge la Transvaal lilikataa na kumlazimisha Pretorius kujiuzulu uraisi wake wa Transvaal. Waingereza walifanya kila lililowezekana kuzuia muungano wa madola ya Kikaburu. Walihofu kuwa kwa kuungana Makaburu wangeweza kuanzisha mashirikiano na mataifa ya nje ambayo bila shaka yangekuwa tishio kwa makoloni na vituo vya majeshi ya wanamaji vya Waingereza. Hivyo walichukua hatua za kuwashawishi Makaburu na kuvunja moyo wa muungano wa jamhuri hizi mbili.

Licha ya utengano baina ya jamhuri hizi mbili, Transvaal pia haikuwa na umoja na mshikamano wa ndani, na ilichukua muda mrefu zaidi kabla haijaibuka kama dola imara. Makaburu wa Transvaal walitawanyika sana na walikuwa na tofauti kubwa za kidini, mambo ambayo yalikuwa ni pingamizi kwa muungano wake hadi 1860 wakati walipoweza kusawidi katiba mwafaka ambayo iliweka bayana nafasi ya serikali (utendaji) na bunge. Pretorius alichaguliwa tena kuwa Rais wa Transvaal mnamo 1864 na aliitawala jamhuri hiyo hadi 1870.

## *Uhusiano wa Makaburu na Waafrika kabla ya 1870*

Uharibifu mkubwa ulioletwa na Mfekane ulipelekea kwenye maangamizo ya jumuiya nyingi za Kiafrika huko Transvaal na Orange Free State. Baadhi yao walimezwa na ufalme wa Wandebele ilihali wengine waliweza kujikusanya tena chini ya viongozi wenye nguvu kama vile Mushweshwe.

Hata hivyo Wandebele walifukuzwa na Makaburu, na baadhi ya jumuiya walizozishida zilitiishwa na kujumuishwa kwenye madola ya Makaburu. Waafrika hawa sio tu walitaabishwa kwa kunyonywa moja kwa moja bali pia kwa kubaguliwa na Makaburu kutokana na rangi yao. Katika katiba ya Transvaal, mathalani, watu weusi hawakuwa sawa na weupe, na weusi walilazimishwa kubeba vitambulisho walivyopatiwa na serikali ama na waajiri wao wakati wote. Waafrika walitumikishwa bila malipo

kwenye mashamba ya weupe; watoto wao pia walifanywa "wanagenzi" na kulazimishwa kuwafanyia kazi wakulima weupe hadi wavulana walipofikia umri wa miaka ishirini na mitano na wasichana miaka ishirini na moja. Zaidi ya hayo, Waafrika walipaswa kuwasaidia Makaburu wakati wa vita.

Makaburu wa Transvaal walijitahidi kuimarisha nafasi yao kwa kupanua himaya yao huku wakiwabana majirani zao wa Kiafrika. Hata hivyo, walipambana na upinzani mkubwa kutoka kwa Waafrika hao. Upande wa magharibi Watswana waliwapinga ambapo Wapedi walipigana nao vikali upande wa mashariki, hadi mpaka unaokubalika na pande zote mbili ulipowekwa mwaka 1857. Upande wa kaskazini, Wavenda na Wasotho walifanikiwa kuwazuia Makaburu. Baada ya kuvishinda baadhi ya vikundi vya Wasotho kwenye mapigano yaliyochukua siku ishirini na tano, Makaburu walidhani kwamba walikuwa wamekomesha upinzani wa Waafrika kwenye maeneo ya kaskazini. Lakini maasi ya Wavenda ya 1859 na 1867 yaliwafukuza Makaburu nje ya eneo hilo la Wavenda.

Upinzani mkubwa zaidi dhidi ya Makaburu ulifanywa na taifa la Wasotho la Mushweshwe ambao kwa ujasiri mkubwa walipinga uingiliwaji wa ardhi yao na Makaburu. Hata hivyo, kutokana na kuzeeka kwa Mushweshwe, magomvi ya wana wa mfalme yaliwafanya watu wafarakane. Mamlaka ya Mushweshwe kwa baadhi ya vikundi vilivyokuwa chini yake yalianza kumomonyoka. Hali hii iliwapa mwanya Makaburu kuwashambulia kwa urahisi. Hatimaye, kutokana na ongezeko la uchokozi wa Makaburu, Mushweshwe aliwashawishi Waingereza kuiteka Lesotho. Nao hatimaye walifanya hivyo kunako 12 Machi, 1868.

## *Uenezi wa Waingereza katika Afrika Kusini 1870-80*

Raghba na uenezi wa Waingereza katika Afrika Kusini ulikuja sawia na uvumbuzi wa madini - almasi na dhahabu - kwenye eneo hili. Wakati huohuo, jamhuri za Makaburu na madola ya Waafrika yalipigania machimbo ya almasi. Waingereza walijitolea kuzipatanisha pande hizi mbili na hawakuruhusu upatanishi huu ufanywe na taifa jingine lolote la nje. Waliwapatia Waafrika migodi iliyogombaniwa na kisha wakaliteka eneo hilo na kulifanya Griqualand ya Magharibi ambayo baadaye ilijumuishwa kwenye Cape Colony. Hatua ya Waingereza ya kupokonya migodi ya almasi na jinsi walivyodhibiti upanukaji wa Jamhuri za Makaburu kwenye eneo hilo iliwakera sana Makaburu na hivyo kuharibu uhusiano wao wa baadaye na Waingereza.

Sababu za uenezi wa Waingereza katika Afrika Kusini kwenye miaka ya 1870 baada ya kujitoa awali kwenye miaka ya 1850 zinafungamana na masuala ya kiuchumi, hasa kufuatia ugunduzi wa almasi kwenye eneo hilo. Ili kuimarisha mashiko yao Afrika Kusini, Waingereza walijaribu kuunda shirikisho dhaifu la madola ya weupe yaliyokuwepo katika eneo hilo. Shirikisho hilo lilitarajiwa lijumuishe jamhuri mbili za Makaburu - Orange Free State na Transvaal-Cape Colony, Natal na Griqualand. Kwa bahati mbaya juhudi zote za Waingereza za kuyaunganisha pamoja madola haya kazikuwa na mafanikio kwa vile hayakutaka kuunda shirikisho hilo. Zaidi ya hayo,

mizozo juu ya migodi ya almasi ilizuia kuwepo kwa shirikisho la Afrika Kusini.

Kutokana na hali hii Waingereza waliamua kutumia nguvu ili kuleta shirikisho. Wakitumia nafasi ya ugombezi wa mpaka baina ya Makaburu wa Transvaal na Wapedi - dola la Waafrika - Waingereza waliiteka Transvaal mwaka 1877 kwa matumaini ya kuitumia kama chambo katika mpango wao wa shirikisho. Ili mpango ufanikiwe, Waingereza walidhani ni muhimu pia kuteka madola mengine ya Waafrika katika eneo hilo. Na lengo lao la kwanza likawa kuiteka himaya ya Wazulu (Zululand). Licha ya upinzani wa kishujaa wa mfalme wao, Setshwayo, na uongozi wake mzuri wa kivita uliojitokeza kwenye vita vya Isandhlwana vya Januari 1879, Wazulu hatimaye walishindwa kutokana na ubora wa bunduki za Waingereza. Setshwayo alikamatwa Agosti 1879 na kupelekwa Cape Town ambako alifungiwa. Waingereza hawakuiteka nchi ya Wazulu bali waliidhoofisha kabisa kwa kuigawanya katika maeneo huru kumi na matatu yaliyokuwa chini ya machifu.

Vita dhidi ya Wazulu havikufanikisha lengo la kupiganwa kwake, yaani kuwa mwanzo wa kujumuishwa kwa madola ya Waafrika katika shirikisho la Afrika Kusini. Hali hii ilisababishwa na viongozi wa Kiingereza huko London na pia nchini Afrika Kusini kuwa na mikabala tofauti kuhusu suala la shirikisho; na, muhimu zaidi, vita dhidi ya Wazulu vilifuatiwa na vita vya Waingereza-Makaburu na vile vya Cape-Lesotho, ambavyo vyote vilivunjavunja kabisa wazo la shirikisho.

## *Kushindwa kwa shirikisho*

Makaburu huko Transvaal hawakupendezwa kabisa na utekwaji wa jamhuri yao na Waingereza mwaka 1877, na kwa miaka mitatu walijaribu kuwashawishi Waingereza wawape uhuru wao na kuondoka katika ardhi yao. Madai ya Makaburu yaliongezeka kadri Waingereza walivyozidi kukataa maombi yote ya Makaburu na kusisitiza kwamba Transvaal ingepatiwa tu serikali ya madaraka ndani ya shirikisho. Ilipofikia Desemba 1880, uvumilivu wa Makaburu uliwaishia na wakajitangazia uhuru wao kwa kuirejesha tena serikali yao ya jamhuri. Hii ilipelekea kwenye vita dhidi ya Waingereza, na mnamo Februari 1881, Makaburu, wakiongozwa na Paul Kruger, Piet Joubert na M.W. Pretorius, walipata ushindi mkubwa kwenye vita mashuhuri vya milima ya Amajuba. Vita viliisha rasmi kwa kutiliana sahihi mkataba wa amani uitwao Mapatano ya Pretoria mnamo Agosti 1881. Mkataba huo ulikuwa mwanzo wa kuongezeka kwa uhuru wa Makaburu. Baadaye yalifuata Mapatano ya London ya 1884 ambapo Waingereza waliwapatia Makaburu uhuru kamili katika masuala yote, isipokuwa mambo ya nje, na hasa uhuru kamili katika kuyashughulikia madola ya Waafrika ambayo yaliendelea kunyimwa zana za kivita.

Vita vya Lesotho vilihusishwa na juhudi za serikali ya kikoloni ya Cape kuyanyang'anya silaha madola ya Waafrika kama hatua ya kwanza ya kutekeleza mpango wa kuanzisha kwa nguvu shirikisho la watu wa Afrika Kusini. Kukataa kwa Wasotho kusalimisha bunduki zao ndiko kulikosababisha vita vya Cape na Wasotho vilivyoanza Septemba 1880. Baada ya miezi saba ya mapigano, vita vilimalizika bila



7.2 *Makomando wa Kikaburu, 1880*

kupatikana mshindi kamili. Hata hivyo, huu ulikuwa ni ushindi wa kisiasa kwa Wasotho kwa sababu walibaki na bunduki zao baada ya vita.

## *Hitimisho*

Shughuli za Waingereza nchini Afrika Kusini kwenye kipindi tunachokijadili (1950-80) zilileta matokeo kadhaa. Ingawa jitihada zao za kuunda shirikisho la eneo kwa nguvu zilishindwa, lakini walifanikiwa kuvidhoofisha vikundi kadhaa vya Waafrika kama vile Waxhosa, Wasotho, Wamfengu na Wakhoikhoi, ambao wote waliwekwa chini ya Cape Colony. Mfumo wa kisiasa wa mataifa mengine kama vile Wazulu na Wapedi ambao walikuwa bado hawajajumuishwa ulivurugwa na kukawa na fujo miongoni mwa watu. Baadhi ya Makaburu kama wale wa Griqualand ya magharibi walipoteza utawala wao, lakini jamhuri kuu za Makaburu huko Orange Free State na Transvaal zilijipatia uhuru wa kufanya mambo yao isipokuwa katika masuala ya mashirikiano na mataifa mengine ya Ulaya mbali na Uingereza. Wakati huohuo, Waingereza waliendeleza udhibiti usio thabiti wa maeneo mbalimbali ya Afrika ya Kusini kwa kuangalia hali ya mambo kupitia maofisa wao wakazi.

# 8

# *Nchi za Bonde la Zambezi*

Katika sura hii, tutazingatia Afrika ya Kati na kuangalia mabadiliko makuu yaliyotokea huko kati ya 1800 na 1875. Eneo linalozingatiwa linajumuisha lile la mataifa ya sasa kama vile Malawi, Msumbiji na Zambia. Sababu za ndani za mabadiliko katika jumuiya za wenyeji zitachunguzwa kwa kifupi kwani ziliathiri sio tu maendeleo ya jumuiya zinazohusika, bali pia mkabala wa wananchi dhidi ya sababu za nje za mabadiliko hayo. Mambo ya nje yaliyoleta athari kubwa ni biashara ya watumwa ya kuvuka bahari iliyoiingiza Afrika ya Kati kwenye uchumi wa dunia, na maingilio ya Wanguni/Wasotho. Umuhimu wa sababu hizi mbili pia utajadiliwa. Kama usuli wa mjadala huu, hatuna budi kwanza kuangalia mielekeo ya kipindi cha kabla ya karne ya kumi na tisa katika eneo hili, na baadaye kuhitimisha kwa uchunguzi mfupi wa eneo hili kabla tu ya "kingang'anyiro cha nchi za Ulaya" kuikumba Afrika.

## *Mkesha wa Karne ya Kumi na Tisa*

Mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi ya karne ya kumi na tisa yalikuwa sehemu ya mfululizo wa mabadiliko ya karne iliyotangulia. Mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa yalikuwa yakifanyika katika ukanda huu kwenye karne zilizotangulia na kuacha athari thabiti. Umuhimu wa mabadiliko ya karne ya kumi na tisa ni kwamba yalikuwa ni ya kasi zaidi na athari yake ilikuwa kubwa zaidi.

Mabadiliko makubwa ya kisiasa yalikuwa yametokea katika bonde la Zambezi kabla ya karne ya kumi na tisa. Vikuhdi kadhaa vya Washona na Walunda vilikuwa vimewashinda wenyeji wa eneo hili na kutamakani hapo. Matokeo yake ni kwamba vikundi vingi vya wenyeji vilijumuishwa kwenye mfumo wa kidola ama wa Washona ama wa Walunda. Mchakato huu wa uundaji wa dola pengine ulianzia kusini mwa Mto Zambezi kwa kulazimisha mamlaka ya Washona juu ya wenyeji. Hii ilipekelekea kwenye uanzishwaji wa madola kadhaa huru ya Washona yaliyodhibiti vizuri eneo la Zambezi hadi kwenye karne ya kumi na tisa. Walunda pia walijipenyeza kwa kiasi kikubwa katika eneo hili kabla ya 1800. Uhamiaji wa kwanza wa Walunda ulifanyika karne ya kumi na saba, na kipindi chote cha karne ya kumi na nane walijiimarisha na kupanua mamlaka yao kwenye eneo hili. Ilipofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, madola mengi ya Walunda yalikuwa yamefikia kilele cha usitawi, na mengine yalikuwa yakipanuka kwa haraka.




**8.1** *Watu wa siasa za Afrika ya Kati, 1800-80 (A.F. Issacman)*

Himaya za Walunda na Washona zilikuwa na sifa bainifu zilizofanana hasa katika mpangilio wa jamii zao. Kila dola ilikuwa na mfalme aliyechukuliwa kuwa na nguvu za kiungu, na aliyekuwa na uwezo juu ya rutuba ya ardhi na usitawi wa wananchi wake. Alikuwa ndiye msimamizi pekee wa ardhi, na alikuwa na haki kamili ya kuigawa. Kama malipo ya ukarimu wake, alipata kutoka kwa wananchi wake kodi, huduma na rasilimali nyinginezo. Hata hivyo, falme hizi zilizokuwa katika makundi mawili hazikuweza kuanzisha miundo unganifu na imara ya serikali kuu. Hii ilisababishwa na mambo kadha, ikiwemo migogoro ya urithi katika Ikulu, utovu wa utii miongoni mwa maofisa wa ngazi za chini, maasi dhidi ya viongozi wakandamizaji, mifarakano ya kikabila, na ukosefu wa jeshi la kudumu la kuchunga amani nchini. Mambo haya yalipelekea kwenye migogoro ya mara kwa mara na kumomonyoka kwa falme za Washona na Walunda.

Licha ya maendeleo haya ya kisiasa, yalikuwepo pia mabadiliko ya kiuchumi Afrika ya Kati kwenye kipindi cha kabla ya karne ya kumi na tisa. Kulikuwepo na mtandao imara wa biashara katika eneo ambamo bidhaa kama vile chuma, chumvi, nguo na nafaka zilibadilishwa mara kwa mara miongoni mwa wenyeji kama Wasena, Wachewa, Wabisa na Walozi. Vikundi hivi vya wenyeji sio tu vilifanya biashara baina yao, bali pia vilitoa bidhaa kwa ajili ya bandari za Bahari ya Hindi za pwani ya Afrika Mashariki. Bidhaa hizo zilijumuisha meno ya tembo na dhahabu. Biashara hii ya kuvuka bahari hata hivyo ilikuwa ya kiwango kidogo na ilianza kuongezeka tu mwishoni mwa karne ya kumi na nane.

Mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi yaliyojadiliwa hapo juu pia yalipelekea kwenye mabadiliko ya kijamii hasa katika mfumo wa kikabila wa jamii za Afrika ya Kati. Maingiliano ya watu mbalimbali tofauti hayakusababisha kuoana tu, bali pia kuanzishwa kwa makabila mapya kama vile Wasena, Watonga wa Zambezi, na Wagoba. Aidha kulikuwepo na ukopeshanaji wa kiutamaduni - vikundi vya wahamiaji viliiga baadhi ya vipengele vya utamaduni wa wenyeji ilihali wenyeji nao walichota tabia kadhaa kutoka kwa wahamiaji. Wakati mwingine ukopeshanaji huu uliibusha tamaduni changamani.

Hivyo, ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane hali katika Afrika ya Kati haikuwa na utulivu mkubwa kisiasa wala kiuchumi. Kutekwa na kuingiliwa na wahamiaji kulikotokea awali kulileta mambo mapya katika eneo hili wakati ambapo biashara nayo ilikuwa ikiongezeka. Mabadiliko yote haya aghalabu yalileta wasiwasi kwenye jamii ya kienyeji na hivyo kulifanya eneo liweze kuzidiwa nguvu kiurahisi na wafanyabiashara wa nje pamoja na wavamizi wachokozi.

## *Biashara ya watumwa na kujumuishwa kwa Afrika ya Kati katika uchumi wa ulimwengu wa kibepari*

Kushiriki kwa nguvu kwa watu wa Afrika ya Kati katika biashara ya watumwa kulianza hasa kwenye nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa na hatimaye kukaliingiza eneo hili kwenye uchumi wa ulimwengu wa kibepari. Waliuza watumwa huko Bukini (Madagascar) na visiwa vya jirani kupitia Afrika Mashariki, na kuvuka Bahari ya Hindi hadi Mashariki ya Kati. Biashara ya kuchuuza watu ya Afrika ya Kati iliambatana na kiwango kikubwa zaidi cha utumiaji nguvu, vurugu na uharibifu wa mifumo ya kisiasa

kupita hali ilivyokuwa huko Afrika ya Magharibi. Hata kama jamii za wafanyabiashara wa Afrika ya Kati zilipata faida fulani ya mali, polepole watu wa Afrika ya Kati waliingizwa kwenye mfumo wa biashara wa kimataifa ambao hawakuweza kuudhibiti, na wakawa katika hali dhaifu ya utegemezi.

Mambo kadhaa yalipelekea kwenye upanuzi wa biashara ya watumwa Afrika ya Kati wakati mapambano ya kukomesha biashara hiyo huko Afrika Magharibi yalikuwa ndiyo kwanza yanapamba moto. Kwanza, kulikuwepo na mahitaji ya wafanyakazi katika mashamba ya miwa yaliyokuwa yakizidi kupanuka ya Kuba na Brazil ambayo hayakuweza kutoshelezwa na watumwa kutoka Afrika Magharibi na eneo la Kongo. Wafanyabiashara ya watumwa walianza kutafiti masoko ya Msumbiji. Halafu kulikuwa na mahitaji ya wafanyakazi kwenye mashamba ya Wafaransa katika visiwa vya Reunion, Ushelisheli na Maskarene vya Bahari ya Hindi, na kadhalika kwa ajili ya watawala ambao walikuwa wakiendelea kuimarisha utawala wao nchini Bukini. Mahitaji makubwa zaidi, hata hivyo, yalitoka kwa watawala wa Kiomani wa Zanzibar na maeneo ya jirani. Mfumo wa njia za kibiashara uliokuwepo tayari uliiunganisha bara na masoko ya pwani ya Kilwa, kisiwa cha Msumbiji na Kilimani (Quelimane), ambako, licha ya watumwa, meno ya ndovu pia yaliuzwa. Jambo jingine lililochangia katika kupanuka kwa biashara ya watumwa katika kipindi hiki ni kutokujishughulisha sana kwa kikosi cha meli za kivita za Waingereza katika eneo hili ili kuizuia biashara hiyo.

Wafanyabiashara ya watumwa wenyeji - Wayao, Wabia na Wachikunda - walilikabili ongezeko la mahitaji ya watumwa kwa kupanua shughuli zao. Walipanua shughuli zao za kibiashara hadi kufikia maeneo mapya kaskazini na kusini mwa Zambezi katika harakati za kutafuta watumwa, na bandari za Bahari ya Hindi zikawa vituo vikuu vya kusafirishia watumwa nchi za nje. Wakati huohuo meno ya ndovu pia yakawa bidhaa muhimu ya biashara. Bidhaa hizi mbili zilikuwa na uhusiano wa karibu, kwani watumwa ndio waliobeba meno ya ndovu vichwani mwao wakati wa safari zao kuelekea pwani. Ilipofikia katikati ya karne ya kumi na tisa, Afrika ya Kati ilikwisha kuwa kituo kikuu cha kutoa watumwa na meno ya ndovu. Pwani ya Afrika Mashariki ambako ndiko watumwa walisafirishwa kwenda nchi za nje ilianza kupata ufufuo wa kiuchumi. Idadi ya kutosha ya watumwa walisafirishwa kwenda Brazil, lakini Kisiwa cha Zanzibar ndicho kilichokuwa mpokeaji mkuu wa watumwa.

Ukuaji wa biashara ya watumwa na meno ya ndovu uliviingiza vikundi kadhaa katika mashindano ya udhibiti wa biashara hiyo dhidi ya Wayao, Wabisa na Wachikunda. Vikundi vya nje ya Afrika ya Kati kama vile wafanyabishara wa Kimakua, Kiswahili na Kiarabu pia wakawa mashuhuri katika biashara ya eneo hili. Ilipofikia katikati ya karne ya kumi na tisa, jamii nyingine kama vile Wamambari, Walozi na Wakololo, pia zilitaka kushiriki kwenye uchumi wa eneo hili uliokuwa ukiendelea kupanuka. Hivyo kuongezeka kwa mahitaji ya nje ya watumwa kulileta hali ambamo eneo kubwa la kaskazini mwa Zambezi lilijishughulisha sana na utoaji wa watumwa na meno ya ndovu.

Tabia ya biashara hii ilipata mageuzi makubwa baada ya takribani mwaka 1840. Namna ya kupata watumwa ilibadilika sana ambapo mashambulizi na utekaji vilichukua nafasi ya njia za kibiashara za amani za kupatia watumwa. Vikundi vyote vya

wafanyabiashara sasa vilitumia nguvu kama njia ya kudumisha ubabe wao wa kiuchumi na ya kukidhi mahitaji ya watumwa ya pwani yaliyozidi kuongezeka. Hali hii nayo iliathiri mpangilio wa kisiasa wa ukanda huu. Madola mapya yaliundwa na vikundi kadhaa vya wafanyabiashara ili kuhakikisha upatikanaji wa ukakika wa mateka na meno ya ndovu. Wakitumia silaha za Ulaya, walivishinda vikundi vingi vya wenyeji na wakawabadilisha mateka wao kwa silaha zaidi na hivyo kuwezesha upanuzi zaidi. Ingawa madola haya yalikuwa huru kisiasa, lakini yalikuwa ni mwendelezo usio wa moja kwa moja wa nguvu za kiuchumi na kivita za Ulaya katika eneo kubwa la Afrika ya Kati. Kwa hiyo biashara ya masafa marefu iliyapa madaraka matabaka mapya ambayo mamlaka yake yaliwanyonya na kuwakandamiza wenyeji ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa kibepari wa dunia.

Mahali ambapo wafanyabiashara ya watumwa hawakunyakua moja kwa moja nafasi ya kuwa watawala wa kisiasa, basi walichangia sana katika mmomonyoko wa mamlaka ya kisiasa ya watawala wa kienyeji kwa kuleta migawanyiko ya ndani na kuchochea maasi ndani ya vikundi. Pia waliingilia moja kwa moja siasa za wenyeji na hivyo kusababisha kuporomoka kwa madola ambayo tayari yalikuwa dhaifu. Hata hivyo, si mara zote kwamba athari za wafanyabiashara ya watumwa kwa ustawi wa kisiasa wa wenyeji zilikuwa hasi. Kwa upande wa ufalme wa Wabemba, mathalani, mwungano kati ya watawala wenyeji na wafanyabiashara wa Kiarabu/Kiswahili uliimarisha dola na kuwapatia utajiri mkubwa watawala wake. Hali hii pia iliwahusu machifu wengine kadhaa katika eneo hili. Wafanyabiashara ya watumwa wa nje daima walikuwa tayari kufanya urafiki na kikundi chochote cha wenyeji ili kuzuia uanzishwaji au upanuzi wa uwezo wa kibiashara wa wapinzani.

Hata hivyo, uimarishaji huu wa dola uliotokana na ushirikiano na wafanyabiashara ya masafa marefu wa nje hatimaye uliweza kuwa chanzo cha udhaifu. Mahitaji ya watumwa na meno ya ndovu yaliweza kuwa makubwa mno kiasi cha kushinikiza kutoa watumwa zaidi na zaidi kama njia pekee ya kudumisha utajiri wa dola na ya kupatia silaha ili kuendeleza ubabe katika eneo. Baadhi ya madola, baada ya kuutumia kupita kiasi udhaifu wa majirani zao, wakiwapora ng'ombe wao au wakiyaharibu mashamba yao, na kuwatia utumwani watu au kuwalazimisha wakimbilie kwenye maeneo yenye ulinzi zaidi, yalijigeukia yenyewe na kuanza kuwatia utumwani raia wake. Huu ulikuwa mkakati wa kujimaliza wenyewe, kwani ungeweza kusababisha maasi ya watu wengi, na uharibifu wa ushikamano na uthabiti wa dola. Mfano mzuri ni ule wa Wamakua ambao kwenye miaka ya 1850 walitambuliwa kama dola kubwa na wauzaji wakuu wa watumwa katika Kisiwa cha Msumbiji. Ilipofikia miaka ya 1870 walikuwa wamegawanyika gawanyika na hawakuweza kuuzuia uvamizi wa Wareno. Sera hiihii ya kutoona mbali ilichangia, kwa kiasi fulani, kuangusha mfumo wa *prazo* wa Zambezi, ambapo *Waprazeros* wa Kiafrika-Kireno walijighilibu wenyewe, wakaanza kuwatia utumwani Waafrika kwenye ardhi yao, na kusababisha kuenea kwa uasi na kufukuzwa kwa *Waprazeros* wengi.

Hata hivyo, eneo la Washona lililokuwa kusini mwa Zambezi halikuathirika kwa urahisi na mashambulizi toka kwa wafanyabiashara ya watumwa wa nje. Madola ya

Washona yalikuwa na nguvu za kutosha, na hivyo yaliweza kuzuia mengi ya mashambulio. Zaidi ya hayo, kutokana na ujio wa Wanguni wa Gaza katika eneo hili kwenye kipindi cha baada ya 1830 na zuio la Waingereza la bandari zilizokuwa zikisafirisha watumwa nje, biashara ya watumwa katika eneo hili ilianza kuwa na matatizo na baadaye ikakosa faida kabisa. Matokeo yake ni kuwa watumwa hawakuuzwa tena nje bali walitumiwa humo humo ndani ya eneo. Katika Afrika ya Kati watumwa walifanyishwa kazi za lazima za kuzalisha mali nchini. Wakati mwingine, kwa kutegemea watumwa, watu huru waliweza kukusanya bidhaa nyingine kama vile meno ya ndovu, nta, na mpira kwa ajili ya mauzo ya nje, na hivyo kuweza kudumisha usitawi wao wa kibiashara.

Biashara ya watumwa ilikuwa na faida zake chache, mathalani, ilileta katika eneo hili mazao mapya kama vile tumbaku, mahindi, mpunga na muhogo; ilisababisha uvumbuzi wa teknolojia ya msingi kama vile mitego ya Chikunda, maghala ya nafaka na silaha; na ilichochea upanuzi wa baadhi ya viwanda vya kienyeji. Lakini faida hizi zilikuwa ni ndogo mno zikilinganishwa na udumavu wa ujumla wa kiuchumi katika eneo hili uliosababishwa na biashara ya watumwa. Hapana shaka kwamba biashara ya watu ilipelekea katika kupungua kwa idadi ya watu na kuharibika kwa uchumi wa vijiji kutokana na kuwauza nje ya jumuiya zao wenyeji, wanaume na wanawake, wenye nguvu. Hali hii pia ilileta njaa. Zaidi ya hayo, magonjwa ya kuambukiza kama vile kipindupindu na ndui, ambayo ni ya kawaida miongoni mwa jumuiya za Bahari ya Hindi, kwa bahati mbaya yalienezwa katika bara ya Afrika ya Kati. Magonjwa haya ya mlipuko yaliua watu wengi sana. Hali hii ilipunguza zaidi uzalishaji mali vijijini, jambo ambalo kwa upande wake lilisababisha utapiamlo na magonjwa. Athari ya kijamii ya hali hii ilikuwa ni ongezeko kubwa la tuhuma za uchawi miongoni mwa wenyeji. Baadhi ya watawala walitafuta suluhisho la matatizo haya kwa kujitahidi kupata watumwa zaidi ili kuziba pengo la upungufu wa watu katika jumuiya zao, jambo ambalo lilizidi kukuza biashara ya watumwa.

Kwa ujumla, kushiriki kwa Afrika ya Kati katika biashara ya watumwa kuliufanya uchumi wa ukanda huu uwe tegemezi zaidi kwa mfumo wa biashara wa dunia na hali hii ilikwamisha zaidi maendeleo ya eneo hili. Madola makuu ya kibiashara yalipoteza uhuru wao wa kiuchumi. Ushindaniaji wa watumwa vilevile uliongeza uhasama miongoni mwa vikundi vilivyokuwa vikifanya biashara hiyo. Wakati huohuo, kutegemea silaha za Ulaya na marafiki wa nje kulizifanya jumuiya za wafanyabiashara wenyeji ziwe rahisi kuingiliwa na watu wa nje. Baadhi yake, kama vile Wasena, walifikia hatua ya kupoteza kabisa uhuru wao.

Kufuatia kukomeshwa kwa biashara ya watumwa, baadhi ya wafanyabiashara na watawala wa Kiafrika walijaribu kudumisha uwezo wao mkubwa wa kiuchumi kwa kutafuta bidhaa nyingine kama vile nta, kahawa, karanga na mafuta ya uto, ambazo walizibadilisha kwa silaha na bidhaa za matumizi toka Ulaya. Mafanikio ya hatua hii yalishadidia tu ukuaji wa utegemezi wa jumuiya za wenyeji kwa uchumi wa dunia ambao hazikuweza kuudhibiti. Nafasi ya chini ya Afrika ya Kati katika mfumo wa kibiashara wa dunia iliweza kujidhihirisha pia kwenye ubadilishanaji usio na usawa uliotawala biashara ya watumwa ambapo binadamu wenye nguvu walibadilishwa kwa



8.2 `Ruga-Ruga' (mchukua watumwa)



8.3 *Shangama wa Soshanane walipowasili Shapanga kukusanya kodi ya mwaka kutoka kwa Wareno*

bidhaa mbalimbali zenye kung'ara lakini zisizo na thamani na zisizodumu.

Aidha kulizuka tofauti kubwa za kitabaka katika jamii. Ingawa eneo hili kwa ujumla liliendelea kuwa masikini, lakini watawala pamoja na tabaka la wafanyabiashara walizidi kuneemeka na kutajirika. Hata hivyo, wakati mwingine, tabaka la wafanyabiashara wenyeji liliungana na wafanyabiashara wa nje kudhoofisha uwezo wa kiuchumi wa watawala wa kienyeji na kuanzisha hegemonia yao ya kiuchumi, na hivyo, kupelekea kwenye uporomokaji wa haraka zaidi wa madola ya namna hiyo.

Mojawapo ya matokeo muhimu ya ongezeko la maingiliano ya kibiashara lilikuwa ni kiwango kikubwa cha ukopeshanaji wa amali za kiutamaduni kilichojitokeza miongoni mwa vikundi mbalimbali. Mwenendo huu ulikuwa na ruwaza tatu. Kwanza, wageni waliingizwa kwenye utamaduni wa wenyeji wao (wawindaji Wachikunda walijumuishwa kwenye jumuiya za Wansenga, Waambo na Watonga wa Bondeni). Kwa upande mwingine, wenyeji waliiga utamaduni wa wageni (k.m. wafanyabiashara wa Kiyao walisilimu kutokana na maingiliano yao na Waarabu). Tatu, lilikuwa suala la maafikiano

ambapo maingiliano ya tamaduni tofauti mbalimbali yalipelekea kwenye uanzishwaji wa vikundi vipya vya kikabila na kiutamaduni.

## *Athari za uvamizi wa Wanguni na Wakololo*

Uvamizi wa Afrika ya Kati wa Wanguni na Wakololo ambao ulianza kwenye miaka ya 1820 ulikuwa ni mwendelezo wa matukio ya awali kwa namna mpya na kwa kiwango kikubwa zaidi. Kuingia kwa wingi kwa watu hawa wa Kusini mwa Afrika katika Afrika ya Kati kulikuwa ni sehemu ya uhamiaji mpana na uundaji wa madola ulioanza karne kadhaa kabla ya karne ya kumi na tisa. Vikundi vikuu vitatu vya Waafrika wa kusini mwa Afrika viliingia Afrika ya Kati kwenye karne ya kumi na tisa. Kikundi cha kwanza ni cha Wanguni wafuasi wa Soshangane, cha pili pia ni cha Wanguni kilichoongozwa na Zwangendaba, ambapo cha tatu ni cha wahamiaji wa Kikololo wenye asili ya Kisotho chini ya uongozi wa Sebetwane.

Vikundi hivi vitatu vilikuwa na sifa bainifu zilizofanana. Mikakati yao ya kivita na silaha zao zilitokana na Wazulu na wote walikimbia maeneo yao ya asili huko kusini mwa Afrika ili kutafuta usalama. Wote walitambua umuhimu wa kushirikisha idadi kubwa ya wageni ili kuibuka kama kikundi chenye nguvu za kivita na kisiasa. Kila kimojawapo cha vikundi hivi kilianzisha madola ya kivita katika Afrika ya Kati kwa kuwateka wenyeji, na kuweka umuhimu mkubwa katika kupata silaha mpya kwa ajili ya kupanua maeneo waliyoyatawala na kutafuta utajiri.

### Wanguni wa Gaza chini ya Soshangane

Kikundi hiki kiliyaacha makazi yake ya asili kwa kuhofia mashambulizi ya Wazulu. Kadiri walivyosafiri kuelekea kaskazini walivijumuisha vikundi vingine vya Wanguni ili kupanua jumuiya yao. Mwaka 1831, walipambana kivita na Wanguni wa Zwangendaba na kuwashinda. Ushindi huu uliwawezesha kupanua mipaka yao. Walisonga mbele kuelekea Afrika ya Kati ambako walizishinda falme kadhaa za Washona. Maeneo yaliyotekwa na Wanguni wa Gaza katika Zimbabwe ya sasa hayakujumuishwa kwenye himaya yao, ila yaliporwa mara kwa mara na kulazimishwa kulipa kodi ya mwaka.

Kitovu cha himaya ya Soshangane kilikuwa Msumbiji ya kusini na maeneo ya magharibi yake. Wakazi wa maeneo haya walifanyiwa ukatili mkubwa. Walilipishwa kodi kubwa na vijana wao wa kiume waliingizwa kwenye rejimenti za marika za Soshangane ambako walibaguliwa na Wanguni wa Gaza. Hii ilisababisha uhasama mkubwa kati ya wakandamizwaji waliokuwa wengi na watawala wa Kinguni. Baadhi ya wenyeji walijaribu kurejesha uhuru wao kwa kuhama maeneo yaliyokuwa chini ya utawala wa Soshangane; wengine hata walishirikiana na Wareno kama njia ya kuwafukuza Wanguni. Kifo cha Soshangane kilichomfika hatimaye kiliaminiwa na Wanguni kuwa kilisababishwa na raia wake ambao hawakuridhika na utawala wake.

### Wanguni wa Zwangendaba

Zwangendaba na wafuasi wake wa Kinguni waliacha makazi yao ya kihistoria huko

kusini mwa Afrika na kuanza safari ya miaka ishirini wakitafuta makazi mwafaka zaidi. Wakati wa kipindi hiki walikutana na vikundi vingi na kupata wafuasi wapya. Walipambana na Wanguni wa Gaza ili kudhibiti eneo la Ghuba ya Delagoa, wakavuka Mto Zambezi, wakaisambaratisha himaya ya Warozwi ya Changamire iliyokuwa imegawanyikagawanyika, na wakapita bila matatizo kwenye sehemu za magharibi mwa Ziwa Malawi kabla ya hatimaye kufanya makazi huko Mapupo. Hapo Zwangendaba alianzisha sera ya usimilishaji ili kuwajumuisha kikamilifu wageni, ambao waliunda asilimia kubwa zaidi ya wafuasi wake, katika utamaduni wa Kinguni. Mifumo ya rejimenti za marika na nasaba za Kinguni ilitumika kama asasi muhimu za mjumuiko wa kijamii.

Zwangendaba pia alibuni mfumo unganifu wa utawala. Akiwa ndiye mfalme, alikuwa ndiye dola na mamlaka ya mwisho. Rejimenti za marika ziligeuzwa na kuwa jeshi la dola, na viongozi wake wakateuliwa na mfalme na kuwajibika kwake. Hivyo, wakati Zwangendaba akifa, dola la Wanguni lilishakuwa miliki yenye nguvu na mashuhuri katika Afrika ya Kati. Hata hivyo, kifo chake kilileta mizozo mingi ya urithi ambayo hatimaye ilipelekea kwenye dola kuvunjika na kugawanyika katika vikundi kadhaa. Uhasama wa madola ya wenyeji yenye nguvu katika eneo hilo ulizidi kuharibu mambo. Ilipofikia 1870, vikundi viwili - Wanguni wa Mpezeni na Wambwela - viliweza kujitwalia miliki za kutosha. Vingine, kama kikundi kilichoongozwa na Kiwere Ndhlou na kile cha Wagwangara, pia vilijitenga kiutawala. Wagwangara hatimaye waliingia Tanzania katika Afrika ya Mashariki.

Wakololo

Wakololo walikuwa ni Wasotho ambao, kama watu wengine, walikuwa wakiikwepa Mfekane. Walikimbia kutoka Dithakong chini ya Sebetwane, mtemi wao, wakitafuta makazi mapya. Wakati wakikimbia kuelekea kaskazini, walishindwa katika mapigano dhidi ya vikundi vingine kama Watswana na Wandebele. Hatimaye, kunako takriban 1835, waliwasili kwenye mipaka ya ufalme mkubwa na wenye nguvu wa Walozi kwenye nyanda tambarare za Mto Zambezi. Ulikuwa ni wakati mzuri ambapo mfalme wa Walozi alikuwa ndiyo tu amefariki dunia baada ya kutawala kwa miaka 50, na kulikuwepo na migogoro mingi ya ndani miongoni mwa wanaukoo tawala na pia changamoto kutoka kwa vikundi vya chini. Pamoja na hayo ilichukua miaka kadhaa kabla Wakololo hawajawashinda kabisa Walozi.

Baadaye Sebetwane alishughulikia uunganishaji wa kisiasa na kijamii wa taifa kubwa la Walozi katika utamaduni wa Kisotho. Ili kufanikisha azma hii aliingia ndoa nyingi za kidiplomasia na kutekeleza sera ya upatanishi na Walozi. Katika muda mfupi Kikololo kikawa lugha kuu ya mawasiliano mapana ya himaya ambapo Walozi walionyesha utii wao kwa Wakololo kwa kuilinda himaya mpya dhidi ya uchokozi kutoka nje. Hata hivyo, mambo kadhaa yalizuia utekelezaji mzuri wa sera hii ya usimilisho. Kifo cha Sebetwane mwaka 1883 kilileta migogoro mikubwa ya urithi iliyoliteteresha taifa jipya hadi kwenye msingi wake. Mfalme mpya alitengua sera ya baba yake ya upatanisho na Walozi na badala yake akaanzisha utawala wa mabavu uliowakandamiza Walozi kwa

kila hali. Kunako 1864, Walozi walimgomea, wakajikomboa wenyewe na kuwaua karibu Wakololo wote.

Hii hata hivyo haikumaliza athari za Wakololo kwenye eneo la Zambezi. Wakimbizi wa Kikololo walijikusanya na wakamfuata mmisionari, David Livingstone, hadi Bonde la Shire ambako Wamanganja waliogawanyika katika vikundi vidogovidogo walikuwa wakinyanyaswa na wafanyabiashara ya watumwa wa Kiyao na Kiarabu. Ilipofikia mwaka 1870, Wakololo walikuwa wameshafaulu kuongoza siasa za Bonde la Shire na waliwaunganisha Wamanganja katika dola na kisha kuitawala.

Uvamizi wa Wanguni-Wasotho Afrika ya Kati ulikuwa na athari za kudumu katika mfumo wa kisiasa wa eneo hili. Wageni hawa walianzisha falme mpya zilizojumuisha baadhi ya vikundi vya wenyeji. Katika harakati hizo walisababisha pia kuvunjika kwa baadhi ya falme za kale kama vile za Kirwozi, Kiundi na Kilundu. Dola mpya zilikuwa unganifu na zenye watu wengi. Zaidi ya hayo, rejimenti za marika zilikuwa ndizo sifa bainifu kuu ya madola hayo.

Licha ya mafanikio ya awali ya wavamizi wa Kinguni na Kikololo na utekaji wao wa maeneo makubwa, walipingwa mara kwa mara na wenyeji waliotaka kurejesha uhuru wao. Pia juhudi zao za kupanua mipaka ya madola yao mapya zilizuiwa kwa nguvu na majirani zao wenye uwezo. Yote haya yalikuwa ni pingamizi la kivita kwa madola mapya, na mfano wa Walozi unaonyesha ni kwa kiwango gani upinzani wa wenyeji unaweza kuwa na mafanikio.

Wakati Wanguni na Wakololo wakianzisha madola yao katika Afrika ya Kati, kulikuwepo pia mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni katika kipindi hicho. Kwa vile madola mapya yalijumuisha mielekeo ya kiutamaduni iliyotofautiana, kiwango cha usimilishaji kilikuwa na kasi zaidi mwanzoni mwa uundaji wa dola kuliko wakati madola yalipokuwa yamekua kikamilifu. Ruwaza halisi ya utamadunishaji vilevile ilitofautiana toka mahali hadi mahali. Mahali pengine watu waliotawaliwa walichukua utamaduni wa wavamizi. Pengine kinyume chake kilitokea. Baina ya pande hizi mbili kulikuwepo na maingiliano ya imani na maadili yaliyopelekea kwenye uanzishaji wa tamaduni changamani.

Athari moja kuu ya mtawanyiko wa Wanguni ambayo haijachunguzwa kwa kina ni ukuaji wa matabaka mapya ndani ya himaya za Wanguni. Kukosekana kwa amani kulikosababishwa na Mfekane kuliibusha uongozi wa kijeshi ambao nguvu yake ilitegemea ushuru na nyara ulizopata. Kiuchumi, viongozi hawa walikuwa na hadhi inayofanana na ile ya watawala wa Kilunda na Kishona wa Afrika ya Kati. Kadiri vikundi vya Kinguni vilivyoelekea kaskazini ya Mto Zambezi, ndivyo polepole vilivyopoteza nafasi ya utekaji nyara huo. Hivyo baadaye walitegemea zaidi ushuru na wakaanza kuwanyonya watumwa wao ili kuhakikisha wanakuwa na chanzo cha kudumu cha utajiri. Udhalilishaji huu wa wenyeji wengi hadi kufikia kiwango hicho cha kitumwa unaeleza sababu za upinzani wa wenyeji dhidi ya Wanguni.

Wahamiaji wa Kinguni na Kisotho hawakujihusisha moja kwa moja katika biashara ya watumwa. Badala ya kuwauza watumwa nje, wao waliamua kuwatumia ndani ya nchi. Hata hivyo, shughuli zao za kivita zilichangia sana kudhoofisha jamii nyingi na

kuzifanya zishambuliwe kwa urahisi na wapiganaji/wafanyabiashara ya watumwa. Hivyo uvamizi wa Wanguni waweza kusemwa kuwa ulirudisha nyuma maendeleo ya kijamii na kisiasa ya jumuiya nyingi na kukwamisha maendeleo kwa ujumla.

## *Kwenye mkesha wa `Kinyang'anyiro'*

Kwenye mkesha wa `Kinyang'anyiro', hali ya mambo katika Afrika ya Kati haikuwa tulivu kabisa. Miaka sabini na tano ya kwanza ya karne ya kumi na tisa ilishuhudia mamkio kama vile uanzishwaji wa vikundi vipya vya kikabila, ongezeko la mabadilishano ya kiutamaduni na kukua kwa migawanyiko ya kitabaka. Ujumuishwaji wa ukanda huu katika uchumi wa dunia kupitia kwenye ushiriki wake katika biashara ya watumwa na meno ya ndovu pia ulikawiza ustawi wa vijiji na kuongeza utegemezi wake wa kiuchumi. Shughuli za kivita za wafanyabiashara ya watumwa na wahamiaji wa Kinguni-Kikololo hazikuchangia kuleta hali ya amani na utulivu katika eneo hili. Juu ya haya kulikuwepo pia migawanyiko na migongano ya ndani ambayo iliziweka jamii za Kiafrika katika hali isiyoweza kuzuia ubeberu wa Ulaya.

Hata hivyo, kulikuwepo na himaya chache ambazo hazikufuata mkumbo huu. Madola kama vile ya Wabemba, dola la Walozi lililojikomboa chini ya Lewanika na dola la Mwenemutapa - yote haya yalipata nguvu na kurejesha umaarufu wake. Lakini, kwa ujumla, mwelekeo wa matukio ya karne ya kumi na tisa ulikuwa ni wa kudhoofisha falme za Afrika ya Kati na hivyo kuzifanya ziwe rahisi kuvamiwa na mataifa ya Ulaya.

# 9

# Pwani na bara ya Afrika Mashariki 1880- 1845

## *Jumuiya za Pwani, k. 1800*

Ili kuelewa mabadiliko yaliyotokea katika maisha ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki na bara yake kwenye kipindi kinachojadiliwa na sura hii, ni muhimu kuchunguza hali ya kisiasa na kiuchumi ya pwani ya takriban mwaka wa 1800. Kisiasa, jumuiya za pwani zilikuwa zimetengana, kila moja ikiwa huru kutoka kwa nyingine na kila moja ikiwa na watawala wake. Athari ya jumla ya Waarabu wa Oman ilikuwepo Mombasa, Zanzibar na Kilwa tu, na hata katika maeneo haya Waarabu hao waligawana madaraka na wenyeji wa Kiswahili na Kishirazi.

Huko Mombasa, viongozi wa wenyeji - Waswahili - walishiriki katika uendeshaji wa kisiasa wa mji huo. Familia ya Mazrui toka Oman iliendelea kuwa huru kutoka kwa watawala wa Kiomani wa Zanzibar kwa sababu ya ushirikiano wao wa karibu na masheikh wenyeji wa Kiswahili ambao walichangia nao utawala. Hata kwa kipindi fulani baada ya utawala wa Wamazrui kupinduliwa, viongozi wa Kiswahili waliendelea kuwa mashuhuri katika uendeshaji wa mji. Huko Zanzibar, mtawala wa kienyeji kwanza alikuwa na sauti katika serikali ya watu wake, akiwa msimamizi mkuu wa nkusanyaji wa kodi waliyotozwa wenyeji. Hata hivyo, kadiri mashiko ya Waomani yalivyozidi kuimarika katika eneo hili, polepole alipoteza mamlaka yake ya kisiasa. Wakati huohuo, wenyeji wa Zanzibar walipokonywa ardhi zaidi na walowezi wa Kiomani ambao waliyanyemelea hasa maeneo yenye rutuba kaskazini na mashariki mwa kisiwa.

Pamoja na kuwepo kikosi cha kulinda ngome cha Waomani kwenye kisiwa cha Kilwa, Sultani mwenyeji alibakishiwa cheo chake na sehemu ya moja ya tano ya ushuru, na alikuwa na mamlaka ya kiutawala kwenye pwani ng'ambo ya Kilwa Kisiwani. Upotevu wa mamlaka yake hankusababishwa tu na kuwepo kwa Waomani, bali pia kudhoofika kiuchumi kwa Kilwa Kisiwani yenyewe, kulikosababishwa na kuinukia kwa mji pinzani wa Kilwa Kivinje huko bara, ambao ulifanikiwa kuelekeza biashara ya watumwa na meno ya ndovu kutoka kisiwani kwenda depo ya bara.

Sehemu nyingine ya pwani iliyobaki ilikuwa chini ya mamlaka ya watawala wa kienyeji, na ilikuwa huru toka kwa utawala wowote wa Kiomani. Watu wa Vumba Kuu ambao walikuwa ni mchanganyiko wa Washirazi, Waafrika na Masharifu wa Kiarabu walikuwa na mamlaka huru ya kisiasa. Ilipofikia 1800, Malindi, mji mwingine miongoni mwa miji ya pwani, ulikuwa umefifia sana kutokana na familia yake ya kitawala




**9.1** *9.1 Pwani na Bara: watu na njia kuu za biashara, 1800-50 (A.J. Salim)*

kuhamia Mombasa kwenye karne ya kumi na sita. Kaskazini mwa Malindi vilikuweko visiwa vya Lamu na Pate. Ilipofikia 1800, Pate ilikuwa imeshaporomoka kutoka kwenye nafasi ya umashuhuri wa kibiashara iliyokuwa nayo katika karne za kumi na saba na kumi na nane kutokana na migogoro ya urithi na mapambano na kisiwa jirani cha Lamu. Ushindani kati ya visiwa hivi viwili baadaye ulirahisisha kuingilia na kutawaliwa kwao na Zanzibar. Bara, mkabala na visiwa vya Lamu na Pate, waliishi Wabajuni ambao walienea pia kwenye mlolongo wa visiwa vidogovidogo vya pwani ya Somalia. Uchumi wao ulikuwa wa bahari na katika kipindi chote kinachojadiliwa waliweza kudumisha uhuru wao wa kisiasa.

Wakati huohuo, pwani ya Benadir kaskazini zaidi, ikiwa na Mogadishu, Merka na Brava kama miji yake mikubwa, iliendelea kujitawala yenyewe. Kuanzia mwanzoni mwa karne, baadhi ya Waarabu na Wahindi walishiriki katika biashara ya miji hii mitatu, lakini eneo hili lilibakia huru hadi 1842, wakati athari ya utawala wa Kiomani ilipofika Mogadishu. Hata wakati huo uhusiano ulibakia kuwa wa kiuchumi zaidi kuliko wa kisiasa.

## *Usultani wa Oman*

Kuibuka na kukua kwa athari ya Oman katika Afrika Mashariki kulikuwa ni matokeo ya mambo mbalimbali, baadhi yake yakiwa ndani ya Usultani wa Oman, na baadhi kutoka nje. Hata hivyo, jambo muhimu zaidi bila shaka lilikuwa tamaa za kiuchumi na werevu wa Sultani Seyyid Said (1806-56), ambaye alijichukulia awali ya yote kuwa ni mwanamfalme mfanyabiashara. Kwa kufuata sera ya kutofungamana na upande wowote kati ya Ufaransa na Uingereza wakati wa Vita vya Napoleon, Said aliweza kupanua mahusiano ya safari za baharini na ya nje ya Oman hadi kufikia kiwango ambapo alikuwa ni tishio hasa kwa meli za Uingereza, na mataifa yote haya mawili yalijitahidi kufanya urafiki naye. Hususani Waingereza, ili kuilinda njia yao ya biashara ya kuelekea India, walimsaidia Said kujiimarisha Oman, na hatimaye wakaitwaa Aden mwaka 1839.

Utengemano wa ndani ya nchi yake ulimwezesha Seyyid Said kupanua uchumi wake pasi na vikwazo. Aliona kuwepo kwa mifarakano na udhaifu kwenye pwani ya Afrika Mashariki kuwa fursa nzuri kwa upanuzi wa kiuchumi na kisiasa. Aidha aliona haja ya kupambana na tamaa ya nchi za Ulaya kwa kukita mikakati yake mwenyewe. Alianza kufanya mawasiliano na wenyeji na watawala kwa kushauriana na kufanya mikataba nao, na kujihusisha kwenye ushindani wa wao kwa wao.

Ilipofikia 1823, alikuwa amekwisha kufaulu kuwa na mashiko katika visiwa vya Pate na Lamu, na jumuiya chache za jirani. Wapinzani wake wakuu walikuwa ni Wamazrui - nasaba ya kifalme iliyotawala Mombasa, pia wakiwa na chimbuko la Oman - ambao waliishawishi Uingereza kuiweka Mombasa chini ya ulinzi wao mwaka 1824. Hatua hii iliharibu kwa kiasi fulani mahusiano kati ya Sultan Said na Uingereza. Hata hivyo ulinzi huu wa Waingereza haukudumu muda mrefu kwa sababu Waingereza walionyesha kumpendelea Said, na Wamazrui hawakuwa na raghba tena juu ya ulindwaji huo kwa vile uliwalazimisha kugawana ushuru wao na Waingereza ambao walikuwa wameshindwa kuwasaidia (Wamazrui) kurejesha maeneo yao yaliyotekwa.




9.2 *Pwani ya kaskazini na bara: njia za biashara, 1880 (A.I. Salim)*



**9.3** *Sa'id bin Sultan, Sultan wa Zanzibar (1804–56)*

## *Uhusiano wa Kibiashara wa Pwani/Bara*.

Muda mfupi baada ya Said kupata udhibiti wa Mombasa aliamua kuhamishia makao makuu ya usultani wake Zanzibar, mji ambao ulikuwa ukikua kwa haraka kama kituo cha kibiashara chenye shughuli nyingi. Saidi alivutiwa sio tu na suhula (vifaa) za kimeli za Zanzibar, bali pia na rutuba ya kisiwa na uwezekano wake wa kuzalisha mazao ya kilimo. Aliamua kuhodhi biashara yote ya kisiwa na akaendelea kukifanya kuwa kituo kikuu cha uchumi katika pwani ya Afrika Mashariki.

Baadhi ya bidhaa za biashara zilizopatikana hapo ni meno ya ndovu, watumwa, karafuu, sandarusi, simbi na bidhaa za kutoka nje kama vile nguo za pamba, shanga, nyaya, mikufu, magobori, baruti, vyombo vya kauri, kioo (vyombo vya kioo), visu na mashoka. Nafasi za Zanzibar iliimarika pia kutokana na kutambulika kwake kupitia mikataba ya kibiashara na mataifa ya nje kama vile Marekani, Uingereza na Ufaransa.

Meno ya ndovu na watumwa ndizo bidhaa zilizokuwa na faida kubwa zaidi kwa Usultani wa Oman kwa sababu ya mahitaji yake makubwa ndani na nje ya nchi. Wayao, kikundi cha bara, walikuwa na mtandao wa biashara ya masafa marefu walioutumia kuleta pwani meno ya ndovu na watumwa. Shughuli zao zilienea kuzunguka Ziwa Nyasa, na bidhaa zao zilifika pwani ya Zanzibar kupitia Kilwa Kivinje. Kwa hakika, kukua kwa umaarufu na usitawi wa Kilwa Kivinje kulitokana na kuongezeka kwa mashirikiano ya kibiashara kati ya watu wa pwani na bara katika karne ya kumi na tisa.

Wabisa, watu wengine wa bara, pia walishiriki katika biashara na pwani. Pamoja na Wayao, walileta meno ya ndovu na watumwa Kilwa Kivinje. Lakini ushindani kati yao uliwafanya Wayao wajishughulishe zaidi na biashara ya watumwa ilihali Wabisa walijikita katika biashara ya meno ya ndovu. Ilipofikia 1850, Kilwa Kivinje kilikwisha kuwa kituo kikuu cha biashara kwenye pwani ya kati ya Msumbiji na Zanzibar, ambako watumwa, meno ya ndovu na bidhaa nyinginezo kama vile mpunga, sandarusi na tumbaku zilipitishwa kupelekwa nje.

Watumwa walipatikana kupitia mashambulizi na vita, ingawa sio mapigano na mashambulizi yote yaliyotokea yalisababishwa na haja ya kuteka watumwa. Zaidi ya hayo, watu waliotiwa utumwani mara nyingi walitoka katika vikundi vya bara ambavyo vilikuwa vikifanya biashara ya watumwa kama vile Wayao, Wabisa, Wamakua na Wangindu. Watumwa wachukuliwa bara na kukusanywa kwenye vituo vya misafara. Kutoka hapo walipelekwa pwani.

Walikuwepo wafanyabiashara ya masafa marefu wengine kwenye eneo la kaskazini mwa Ziwa Nyasa; waliokuwa mashuhuri zaidi ni Wanyamwezi, Wakamba na Wamijikenda. Hawa walianzisha mahusiano na pwani kwa mara ya kwanza kunako takriban mwaka 1800, na baada ya muda mfupi wakaimarisha mitandao ya kibiashara kati ya eneo hilo la bara na pwani.

Baadaye, kadiri bei za watumwa na meno ya ndovu zilivyozidi kupanda, baadhi ya wafanyabiashara wasio Waafrika walianza kuingia bara. Msafara wa kwanza ulioongozwa na wasio Waafrika kuelekea bara ulifika Unyamwezini mwaka 1824 na ilipofikia 1845, wafanyabiashara wengi wa pwani, hasa Waarabu, walikuwa wamekwisha penya ndani ya bara hadi kufika Buganda, ambako walikaribishwa na mfalme aliyetarajia, sio tu kuongeza biashara, bali pia kupata bidhaa muhimu na misaada ya kijeshi.

Kaskazini zaidi, wafanyabiashara wengine wa bara walikuwa wakianzisha mahusiano na watu wa pwani, na mitandao mipana ya kibiashara kama ile ya Miji Kenda iliziunganisha bara na pwani katika mfumo mmoja wa kiuchumi ambamo meno ya ndovu, tumbaku, nguo, samaki, shanga, nazi, ufuta, mtama na nyaya zilibadilishwa.

## *Athari za kijamii na kiuchumi za biashara iliyokuwa ikipanuka*

Upanuzi wa biashara katika pwani na bara ya Afrika Mashariki ulikuwa na athari zake muhimu. Kwa mfano, upanuzi wa Wakamba nje ya makazi yao ya asili hadi kufikia kwenye maeneo ambayo hayakuwa na rutuba ya kutosha uliwafanya waanze uwindaji, ufugaji na biashara ya kubadilishana mali kama njia ya kujikimu. Walifanya biashara na majirani zao kama vile Wakikuyu, Waembu na Wamasai, na baadaye wakapanua mtandao wao wa biashara hadi pwani. Waliandaa misafara yao kwenda pwani na waliongoza katika biashara ya masafa marefu kwenye maeneo ya kaskazini ya bara ya Afrika Mashariki hadi miaka ya 1850, nafasi yao ilipochukuliwa na Waarabu na Waswahili.

Kutokana na mahusiano haya ya kibiashara kati ya pwani na bara, mfumo wa kuishi katika makazi yenye ngome ya Wamiji kenda yaliyoitwa *kaya* ulianza kudhoofika. Watu walianza kuziacha kaya ili kwenda kufanya biashara. Mtawanyiko huu ulififisha umoja na mshikamano wa kaya, ukamomonyoa mamlaka ya wazee na kuua mfumo wa uongozi wa marika. Jamii sasa ilipangiliwa kwa ufinyu zaidi, kwa mujibu wa nasaba au ukoo mdogo. Kadhalika, waliibuka matajiri waliokuwa na wafuasi na waliojijengea umaarufu. Miongoni mwa matajiri hao ni Ngonyo wa Kigiriama, Mwakikonge wa Kidigo na Kivui wa Kikamba.

Upande wa kaskazini, kulikuwepo pia na mahusiano imara ya kibiashara kati ya wakazi wa visiwa vya Lamu na Pate kwa upande mmoja, na Wapokomo na Waoromo kwa upande mwingine. Kaskazini zaidi, miji ya Kibenadir ya Brava, Meku na Mogadishu kwenye pwani ya Somalia pia iliunganishwa kibiashara na bara. Mashirikiano yote haya ya kibiashara kati ya pwani na bara polepole yalionyesha athari za wazi za kijami na kiutamaduni.

Mojawapo ya athari hizo ilikuwa ni desturi ya kuoa wake wa kigeni. Kuoana huku miongoni mwa vikundi tofautitofauti kulipelekea kuanzishwa kwa undugu miongoni mwa jamii zilizohusika. Vilevile watu wa mashariki mwa Kenya waliingiza katika jamii zao matambiko mapya. Zaidi ya hayo, wakazi wapya yaliingizwa kwenye miji ya pwani, na kuifanya iwe mikubwa zaidi na yenye tofauti wa kikabila. Wafanyabiashara wa Kiarabu na Kiafrika na watumwa kutoka sehemu mbalimbali za bara walipatikana kwenye miji yote hiyo. Maingiliano ya kiutamaduni kati ya Wabantu na Waarabu, na kati ya Wabantu na Waswahili yalitokana na kukua kwa matumizi ya watumwa wa nyumbani (wa kazi za ndani) kwenye mashamba na kuenea kwa usuria. Katika Usultan wa Oman desturi ya kuoa wake wa kigeni ilikuwa imeenea sana hasa miongoni mwa tabaka la watawala. Maingiliano ya kiutamaduni kati ya Waarabu na wenyeji wao huko pwani yalikuwa makubwa kiasi cha kwamba kulikuwepo na tofauti bayana za kiutamaduni kati ya Waarabu wa Oman walioishi nyumbani (Uarabuni) na wenzao "walio-Afrikishwa" na kuishi katika miji ya Kiswahili. Wakati huohuo, uhusiano kati ya vikundi vya Waafrika vya pwani uliimarika zaidi kutokana na ushirikiano wa kiuchumi na kijamii.

Hali kadhalika kulikuwepo na mabadiliko kadhaa huko bara yaliyotokana na kushiriki kwa watu katika biashara ya pwani. Kulikuwepo na upanuzi wa baadhi ya himaya kufuatana na kiwango cha ushiriki wao katika biashara ya masafa marefu. Pia, mtindo wa uvaaji nguo wa wanaume wa Kiswahili uliigwa bara. Baadhi ya watawala wa bara walijenga upya miji yao mikuu kwa mtindo wa pwani, wakipamba vitala vyao na bidhaa za pwani na hata kukuza hamu ya vyakula vya pwani. Lugha ya Waswahili - Kiswahili - kama lugha ya mawasiliano mapana ya tabaka la wafanyabiashara pia ilienea sana huko bara.

Hata hivyo, sio vikundi vyote vya bara viliathiriwa na utamaduni wa pwani. Wakikuyu, kwa mfano, hawakuonyesha raghba yoyote katika biashara ya pwani, hata wakati misafara ya Waarabu na Waswahili ilipoingia katika ardhi yao. Wamasai waliwazuia wafanyabiashara wa Kiarabu na Kiswahili kuingia kwenye ardhi yao.

Licha ya matukio ya kibiashara yaliyojadiliwa hapo juu, matukio muhimu ya kijamii na kisiasa pia yalitokea miongoni mwa watu wa eneo la Maziwa Makubwa. Kuliibuka jumuiya kamili za kisiasa zenye utambulisho maalum kama ile ya Baganda. Buganda ilistawi kama dola unganifu yenye asasi sanifu za kisiasa. Lakini vikundi vya mashariki mwa Ziwa Viktoria, isipokuwa ufalme wa Wawanga, havikuanzisha dola zozote unganifu.

## *Biashara ya kimataifa ya Oman*

Seyyid Said alitekeleza sera ya uchumi ya kuhimiza biashara na makazi ya Wahindi katika Zanzibar. Waasia hawa walikuwa na busara nyingi katika kufanya biashara na walishika nafasi zilizo muhimu kabisa kama mawakala wa ushuru, walanguzi, mabepari na wakopeshaji fedha na wafanyabiashara ya jumla nchini Zanzibar. Ingawa kuwepo kwao na shughuli zao huko Zanzibar hazikuwapatia sauti yoyote katika siasa na uendeshaji wa shughuli za kiserikali, nafasi yao ya kiuchumi iliimarika sana. Baadhi yao walitajirika sana kiasi kwamba hata baadhi ya Masultani wa Zanzibar waliwakopa fedha. Pia bidhaa zilizoagizwa kutoka Asia zilikuwa za lazima kwenye misafara ya Waarabu na Waswahili. Hiki kilikuwa chanzo muhimu cha utajiri kwa walanguzi na mabepari wa Kiasia waliovuna sehemu kubwa zaidi ya faida ya sekta ya Kiasia ya biashara ya Zanzibar.

Said pia alianzisha kilimo cha karafuu kisiwani Zanzibar. Alitumia nguvukazi ya watumwa kuendeleza tasnia ya karafuu na akawa mwuzaji mkuu nchi za nje wa zao hilo lililofika hadi Bombay nchini India. kwa hakika, ilipofikia 1843, India ilikwisha kuwa mnunuzi mkuu wa karafuu za Zanzibar.

Kutokana na kuongezeka kwa umaarufu wa karafuu, Waarabu wa Kiomani kadha katika visiwa vya Zanzibar na Pemba walianza kulima karafuu katika mashamba makubwa. Jambo hili lilikuwa na matokeo mengi: lilivunja ukiritimba wa Said katika biashara ya karafuu; lilipelekea kwenye kuifanya karafuu iwe tasnia ya kitaifa miongoni mwa Waarabu wa Oman; liliongeza mahitaji ya nguvukazi ya watumwa, na pia liliongeza biashara ya watumwa ya Afrika Mashariki; lilifanya mazao mengine

yapuuzwe kama vile nazi na mpunga; na ilileta matatizo ya ardhi kisiwani Zanzibar. Matatizo haya ya ardhi hasa yaliharibu kwa kiasi fulani mahusiano kati ya Waarabu wa Oman na wakazi wa asili wa Zanzibar walioporwa ardhi yao na Waarabu.

Zaidi ya hayo, Said alitiliana sahihi mikataba ya kibiashara na mataifa ya Marekani, Uingereza, Ufaransa na Ujerumani. Hii ilichangia sana katika maendeleo ya kiuchumi ya Zanzibar katika Afrika Mashariki. Bidhaa za Marekani kama vile sukari, shanga, vyombo vya shaba, sandarusi, baruti na nguo/vitambaa vya pamba viliagizwa na Zanzibar ilihali Wamarekani walisafirisha kwa meli meno ya ndovu, sandarusi, na karafuu hadi kwao. Waingereza punde waligundua kuwa Sultani wa Zanzibar alikuwa na umuhimu wa kipekee katika ukomeshaji wa biashara ya watumwa katika Afrika Mashariki na kwa hiyo wakahitaji kuwa na nafasi fulani ya kisiasa nchini Zanzibar licha ya nafasi ndogo waliyokuwa nayo katika biashara ya Afrika Mashariki.

Hata hivyo, sera za kibishara na kiuchumi za Said sio tu ziliifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha kibiashara kwenye pwani ya Afrika Mashariki, bali pia polepole ziliuingiza uchumi wa Afrika Mashariki kwenye mfumo wa kibepari wa (nchi za) Magharibi. Taathira hasi ya hali hii ni kwamba wafanyabiashara kutoka Ulaya, Marekani na Asia walitajirika kwa kuwafukarisha wenyeji wa Afrika Mashariki, na hivyo kusababisha kudumaa kwa maendeleo yao. Rasilimali (watu na nyenzo) za Afrika Mashariki zilinyonywa kupitia ubadilishanaji usio na usawa uliokuwa ukifanywa kati ya wafanyabiashara wa kigeni na wenyeji. Uagizaji toka nje wa baadhi ya bidhaa zilizotengenezwa viwandani kama vitambaa vya pamba ulidhoofisha na hata kuviua baadhi ya viwanda vya nguo vya nchini. Jambo jingine muhimu kama hili lilikuwa uuzaji nje wa watumwa na upunguzaji wa rasilimali (watu na nyenzo) ulioambatana na uuzaji huo, ambao ulichangia sana katika kukwamisha maendeleo ya eneo hili.

## *Hitimisho*

Katika kipindi kinachojadiliwa, yaani 1800-1845, pwani na bara ya Afrika Mashariki zilikuwa na madola huru ambayo yalijishughulisha na biashara kwenye viwango vya ndani, kandani au nchi za nje. Polepole, watawala wa Oman walianza kupanua athari zao za kiuchumi na kisiasa na kuzitaka tawala za wenyeji ziukiri utawala wa Zanzibar. Kulikuwepo pia na ukuaji wa biashara ya masafa marefu ulioanzishwa na vikundi vya Waafrika huko bara. Baadaye, wafanyabiashara wa Kiarabu na Kiswahili walikwenda hadi bara kutafuta bidhaa zaidi. Biashara ya masafa marefu iliyokuwa ikipanuka ilikuwa na athari zake za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kwa vikundi vingi vya bara. Athari hizo zilijumisha ueneaji wa Uislamu na lugha ya Kiswahili. Lakini baadhi ya matukio muhimu kama vile uvamizi wa Wanguni yalitokea bara pasi na kuhusiana na biashara ya masafa marefu.

Mwisho, maendeleo na ukuaji wa athari za kibiashara za Zanzibar yalipelekea kwenye ubadilishanaji (wa bidhaa) usio na usawa kati ya Afrika Mashariki na (nchi za) Magharibi. Aidha yaliuingiza uchumi wa Afrika Mashariki kwenye mfumo wa kibepari na hivyo kusababisha kudumaa kwa maendeleo ya eneo hili.

# 10

# *Pwani na bara ya Afrika Mashariki 1845-1880*

Katika sura iliyotangulia tumeona jinsi jamii za bara ya Afrika Mashariki zilivyokuwa zikistawi zenyewe (bila misukumo ya kutoka nje) hadi robo ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Mabadiliko mbalimbali, kama vile miguro ya watu na marekebisho ya kisiasa, yalikuwa yakitokea katika jamii nyingi, lakini ni maeneo ya pwani na ya visiwa vya Unguja na Pemba tu ndiyo yaliyokuwa yameingizwa katika mfumo wa kiuchumi wa kimataifa. Kwa hiyo sura hii itachunguza kuingizwa kwa maeneo ya bara katika mfumo wa kiuchumi wa kimataifa, uvamizi wa Wanguni kutoka Afrika ya Kusini, mapambano baina ya makundi ya Wamasai, na kuongezeka kwa maslahi na maingilio ya Wazungu katika Afrika Mashariki baina ya 1845- 1884.

## *Kujipenyeza kwa Waomani na kukua kwa biashara*

Misingi ya biashara ambayo iliyaleta pamoja maeneo ya pwani na ya bara katika himaya moja ya kibiashara ilikuwa imekwisha wekwa katika miaka ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa. Kufikia mwaka wa 1840, biashara ya pembe za ndovu na watumwa ilikuwa inakua kwa haraka sana na ilikuwa inaliingiza eneo la bara katika mtandao wa kibiashara wa pwani. Bidhaa hizi mbili ziliiwezesha Afrika Mashariki kuingizwa katika mfumo wa kiuchumi wa kimataifa ambao nao uliathiri kukua kwa biashara katika eneo hili kabla ya kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni.

Kuanzishwa kwa uchumi wa mashamba makubwa huko Unguja na Pemba kuliwezesha kuongezeka kwa biashara ya watumwa sehemu za bara. Kufikia mwaka 1880, wakati ambapo Unguja ilikuwa makao makuu ya himaya ya sultani wa Oman, kilimo cha karafuu kilikwisha kuwa shughuli muhimu ya kiuchumi katika himaya ya sultani, na kilikuwa kinaendeshwa kwa nguvukazi ya watumwa. Kilimo hiki kilisababisha kuzuka kwa tabaka la wenye kumiliki ardhi ambao awali walikuwa Waarabu na baadaye walikuwa Washirazi wenyeji wa Unguja, na Wahindi. Kuongezeka kwa mahitaji ya nguvukazi ya watumwa katika mashamba ya karafuu na nchi za ng'ambo kulifanya biashara ya watumwa iongezeke mno katikati ya karne ya kumi na tisa.

Biashara ya pembe za ndovu nayo ilikua sana katika kipindi hiki. Kulikuwa na ongezeko la mahitaji ya pembe huko Ulaya na Amerika. Lakini biashara ya pembe

ilikuwa imedhibitiwa barabara na wafanyabiashara Wahindi ambao walianzisha vituo vyao vya biashara katika pwani ya Afrika Mashariki. Kutokea hapo, pembe zilisafirishwa kwenda India, na kutoka India zikasafirishwa tena kwenda Ulaya. Waamerika wachache walikuwepo pwani ya Afrika Mashariki wakifanya biashara hii, ijapokuwa kwa kiwango kidogo, na waliwategemea sana wafanya biashara Wahindi.

Maendeleo haya ya kibiashara yalisababisha kukua kwa biashara ya masafa marefu ambayo iliunganisha taratibu bara na pwani. Njia za biashara ya masafa marefu zilitandaa kutoka kwenye miji tofauti ya pwani hadi vituo mbalimbali huko bara. Mitandao hii ya kibiashara iliiunganisha polepole bara na pwani katika mfumo wa biashara ya kimataifa.

Hata hivyo, isidhaniwe kuwa dhima ya Waafrika katika biashara ya masafa marefu ilikuwa ndogo na kwamba walikuwa waathirika tu wa masilahi ya kibiashara ya Wazungu. Ni kweli na dhahiri kuwa biashara ya watumwa ilikuwa na athari mbaya sana kimaadili na kijamii kwa jumuiya za Afrika Mashariki. Lakini Waafrika walishiriki kikamilifu katika biashara hii. Wakati mwingine kushiriki kwao kuliathiri sana maendeleo ya jamii zilizohusika, kwani muundo wa jamii ulibadilika taratibu ili kukidhi mahitaji ya biashara hii. Aidha biashara hii ilikuwa na mchango mzuri kwa uchumi wa jamii za Kiafrika, kwani iliwezesha kuingizwa kwa mchele na mahindi. Mchango wake kitamaduni ni kwamba iliwezesha kuenea kwa Uislamu na lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, athari ya jumla ya biashara ya masafa marefu, na matokeo ya kuunganishwa kwa Afrika Mashariki katika mfumo wa biashara ya dunia, ilikuwa na maafa makubwa kwa eneo hili. Wafanyabiashara wa pwani kama vile Wahindi na washirika wao Waafrika walikuwa watu wa kati tu wa wafanyabiashara Wazungu ambao ndio waliopata faida kubwa. Kwa hivyo Waafrika wa Afrika Mashariki waliingizwa katika uchumi wa dunia kwa masharti yasiyokuwa na masilahi kwao. Nguvu ambazo zingeweza kutumika kukuza uchumi wao na mtandao wa biashara ya ndani kwa manufaa ya eneo hili zilitumika kutafuta mali ghafi na watumwa kwa kubadilishana na bidhaa za anasa zisizokuwa za kudumu ambazo ziliwanufaisha watu wachache tu katika jamii. Wakati mwingine tasnia za asili za Waafrika kama vile viwanda vya nguo za kufumwa kwa mikono vya Tanzania kusini magharibi, na viwanda vya milumba (nguo za magome) katika eneo la Ziwa Viktoria, vilikufa kutokana na kuingizwa kutoka nje nguo za pamba zilizotengenezwa Ulaya.

Kuunganishwa kwa eneo la bara ya Afrika Mashariki na pwani kulifanyika kwa kupanua na kunasibishwa njia za biashara zilizokuwapo. Mtandao wa biashara ya masafa marefu katika eneo hili ulikuwa na njia kuu nne: Njia ya Kilwa kuelekea bara, njia za kuelekea Tanzania ya Kati, njia ya bonde la mto Pangani na njia za kutokea Mombasa kuelekea Bara.

## *Njia kuu nne za biashara*

Njia za biashara ya masafa marefu zinazoanzia Kilwa kuelekea bara ya Afrika Mashariki ndizo kongwe kuliko zote. Njia hizi zilichochewa na mahitaji ya watumwa katika visiwa




*10.1 Biashara katika Afrika Mashariki ya karne ya kumi na tisa (ilichukuliwa kutoka kwa P. Curtin, S. Feierman, L. Thompson na J. Vansina, Historia ya Afrika, 1978, uk. 399)*

vilivyokuwa vikitawaliwa na Wafaransa vya Reunion na Mauritius mnamo karne ya kumi na nane. Njia hizi zilipitia eneo la Ziwa Nyasa na kuliunganisha na Kilwa. Eneo hili lilidhibitiwa na Wayao ambao walileta Kilwa pembe za ndovu, nta na watumwa. Uendeshaji wa biashara hii katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa uliwapa Wayao umaarufu katika nusu ya pili ya karne hii. Kwa hivyo biashara iliyokuwa ikifanyika, katika eneo hili ilikuwa na athari ya kudumu kwa jamii ya Wayao. Kabila hilo, ambalo hapo awali lilikuwa limegawanyika katika tawala ndogo ndogo, liliungana pamoja na kufanya jumuiya kubwa zaidi katikati ya karne ya kumi na tisa, hata kabla ya uvamizi wa Wanguni. Machifu wa Wayao hatimaye walipata nguvu zaidi na hawakuweza kushindwa kwa urahisi au kunyanyaswa na Waarabu ambao baadaye walianza kuingia bara. Wayao waliendelea kudhibiti biashara katika eneo hili, lakini wakakubali kushirikiana na Waarabu ambao waliwapatia bunduki na bidhaa nyingine. Maeneo ambayo yalikuwa nje ya mamlaka yao yalikuwa Khota-Khota na Karonga katika nchi ya Malawi ya sasa.

Katika miongo ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa, sehemu kubwa ya biashara iliyokuwa ikifanyika katika njia za biashara zilizopitia katikati ya Tanzania ilifanywa na Wanyamwezi. Lakini baadaye wafanyabiashara Waarabu waliopewa mitaji na Seyyid Said na Wahindi waliokuwa pwani walianza kuingia bara. Hivyo, ingawa katika bara ya Kilwa Waarabu walikuwa wateja wa machifu wa Wayao, lakini katika eneo la kati la Tanzania Waarabu walishiriki kikamilifu zaidi katika biashara. Njia za biashara za kati ziliunganisha miji ya pwani kama vile Bagamoyo na nchi ya Wanyamwezi pamoja na Ujiji ambayo ipo magharibi zaidi kando kando ya Ziwa Tanganyika. Baadhi ya njia zilifika hadi Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo huko Afrika ya Kati, na sehemu za Karagwe na Buganda zilizoko kaskazini magharibi mwa bara la Afrika Mashariki. Njia iliyoelekea kusini iliungana na njia za Kilwa katika eneo la Ziwa Nyasa. Katika njia za kati, Waarabu walianzisha vituo vyao vya biashara walivyovitumia kukusanyia pembe na watumwa.

Makazi mawili muhimu ya Waarabu yalizuka katika vituo hivi vya biashara. Makazi ya kwanza yalikuwa koloni la Waarabu la Unyanyembe katika nchi ya Wanyamwezi, na ya pili yalikuwa Ujiji katika pwani ya Ziwa Tanganyika. Waarabu wa Ujiji hawakuwa ni koloni huru bali waliunganishwa katika mfumo wa utawala wa wenyeji. Lakini kwa kuwa wale wa Unyanyembe waliendelea kuwa kikundi tofauti, waliingia katika ushindani wa kibiashara na watemi wa Kinyamwezi, jambo ambalo liliwafanya wapigane mara kwa mara.

Njia ya bonde la Pangani haikudhibitiwa na kundi lolote. Wasambaa ndio walioanza kufanya biashara katika bonde la Pangani baina ya 1836 na 1862. Walikuwa wamepata maarifa ya biashara ya masafa marefu walipokaa kwa muda kule Zanzibar hadi njaa ilipowasambaratisha wengi wao. Baadaye Semboja, mfalme wa Wazigua, alishiriki katika biashara hii na kujaribu kuidhibiti. Hata hivyo si Semboja wala wafanyabiashara wa Kizigua waliweza kufanya biashara kikamilifu katika njia ya bonde la Pangani hadi bara. Waarabu na Waswahili kutoka pwani ndio waliokwenda na kupita vituo vya biashara vya Wazigua katika tambarare za Upare na Usambaa na kuendelea hadi nchi



**10.2** *Mitindo ya nywele na unyozi ya Kinyamwezi*

**10.3** *Wafanyabiashara wa Kinyamwezi barabarani*



ijulikanayo sasa kama Kenya. Kukosekana kwa mamlaka yenye nguvu kulisababisha kuanzishwa kwa vituo vya biashara mahali ambapo wafanyabiashara wa pwani waliweza kuwa na mawasiliano na watawala wenyeji tofauti tofauti. Jambo hili lilisababisba ushindani na kuchochea mapigano ya mara kwa mara baina ya watawala mbalimbali wenyeji na wasaidizi wao.

Biashara katika sehemu za bara ya Mombasa ilidhibitiwa na Wakamba kabla ya 1880. Njia ya kaskazini iliyopitia Ukambani ilikuwa moja kwa moja chini ya uangalizi wa Wakamba, ilhali njia nyingine iliyoelekea Mlima Kilimanjaro ilidhibitiwa na wafanyabiashara Waarabu na Waswahili kutoka pwani.

Biashara ya masafa marefu miongoni mwa Wakamba ni ya zamani sana kwa sababu walitawala biashara katika eneo hili kwa zaidi ya karibu karne moja kabla ya 1836. Mnamo karne ya kumi na tisa walikuwa wakiingizwa polepole katika mtandao wa biashara ya kimataifa ambapo walibadilisha bidhaa zao kwa vitu vilivyoingizwa kutoka nje. Katikati ya karne ya kumi na tisa, misafara ya Wakamba haikuwa tu inafika pwani na kwa majirani zao Wakikuyu, bali pia maeneo ya mbali zaidi kupita Mlima Kenya.

Katika miaka ya 1880, wafanya biashara Waarabu na Waswahili walikwisha kudhibiti njia ya biashara ya Wakamba. Walifanikiwa kufanya hivi baada ya kudhibiti maeneo ambayo yalikuwa vyanzo vya pembe. Biashara ya watumwa ilikuwa muhimu pia wakati huu. Njaa na vita baina ya makundi ya Wakamba vilisambaratisha jamii ya Wakamba na kuwafanya wawauze watu wao kwa Waarabu na Waswahili ambao walikuwa wafanyabiashara maarufu wa watumwa.

Athari ya biashara ya masafa marefu katika jamii za Afrika Mashariki

Katika kuchunguza athari za biashara ya masafa marefu katika jamii za Afrika Mashariki, ni muhimu ieleweke kwamba sio jamii zote za Afrika Mashariki zilihusika moja kwa moja na mfumo huu wa biashara. Wakati ambapo makao makuu ya falme na madola yenye nguvu yalikuwa vituo vya biashara, nchi zisizokuwa na tawala unganifu hazikunufaika na biashara hii na badala yake zilishambuliwa mara kwa mara na madola yenye nguvu kwa ajili ya kusaka watumwa. Hata hivyo, jamii za wafugaji zisizokuwa na tawala unganifu kama Wamasai ndizo pekee ambazo hazikuathirika katika kipindi hiki.

Biashara ya masafa marefu kimsingi iliathiri msingi wa uchumi wa jamii. Baadhi ya athari zake zilionekana kuwa na manufaa, japokuwa zikichunguzwa kwa undani zilikuwa na maafa makubwa. Madola makubwa yalianzishwa katika maeneo ambayo awali yalikaliwa na mataifa madogo. Kwa mfano taifa la Wanga la huko Kenya ambalo hapo awali lilikuwa taifa dogo lilikua na kuwa na utawala unganifu. Utawala wake ulienea katika nchi jirani za Kisa na Buholo. Nguvu za kijeshi za Wanga zilitokana na kuwatumia mamluki wa Kimasai, na matumizi ya bunduki walizozipata kutoka kwa wafanyabiashara wa pwani waliojipenyeza bara. Kwa hiyo kukua kwa utawala wenye nguvu wa Wanga kulitokana na kuangamizwa kwa tawala dhaifu zaidi zilizokuwa majirani zake ambazo zilishambuliwa mara kwa mara na hatimaye kuunganishwa nao.

Biashara ya masafa marefu ilikuwa pia na athari ya kuharibu mshikamano wa mataifa uliokuwapo. Biashara hii iliwatia moyo watawala wasaidizi kufanya uasi na

kujitwalia mamlaka makubwa zaidi kwa kushirikiana na wafanyabiashara wavamizi kutoka pwani. Hali hii ilipotokea ilisababisha kudhoofika kwa baadhi ya falme. Katika bonde la Pangani kulikuwapo na tawala mbili zilizokuwa kubwa kiasi: ufalme wa Wasambaa na ufalme wa Wagweno. Madola haya hayakuweza kushiriki kikamilifu katika biashara ya eneo hili kwa sababu yalikuwa katika maeneo ya milima. Kwa hiyo hayakuweza kudhibiti njia za misafara ambazo zilipitia katika nchi tambarare za himaya zao. Watawala wasaidizi waliokuwa karibu na njia hizi za biashara waliwakaribisha wafanyabiashara Waarabu na Waswahili katika miji yao bila kuarifu makao makuu. Kutokana na kuidhibiti biashara, waliunda vikundi vyenye silaha ambavyo viliwawezesha kuasi makao makuu. Jambo hili liliyayumbisha madola hayo na kuyafanya yagawanyike katika tawala ndogo ndogo. Mbali ya falme za Wagweno na Wasambaa, balaa hili lilizikumba pia falme za Wapare katika bonde la Pangani.

Yalikuwapo pia madhara ya kijumla yaliyotokana na biashara ya masafa marefu. Biashara ya watumwa haikuwa tu inadhalilisha utu, bali ilikuwa na madhara makubwa kijamii na kiuchumi. Viwanda vya wenyeji havikuweza kuhimili ushindani na bidhaa za viwandani zilizoingizwa kutoka Ulaya. Viwanda vilivyoathirika zaidi yumkini vilikuwa ni vile vya nguo za kufuma kwa mikono vya Tanzania ya kusini magharibi ambavyo vilifishwa na nguo zilizoingizwa nchini kutoka Ulaya. Aidha kilimo cha kujikimu kilipuuzwa kwa sababu ya kutoa aula kwa biashara ya vitu vya anasa, na pia kutokana na vurugu na hali ya kutotengamaa iliyosababishwa na mashambulio ya kusaka watumwa. Biashara hii ilionekana kuwapa nguvu Wazigua katika bonde la Pangani. Kwa kuidhibiti biashara hii waliweza kuunda tawala kubwa zaidi. Hata hivyo, ukiachilia mbali ufalme ulioanzishwa na Kisabengo karibu na Morogoro, ambao ulidumu hadi ulipovamiwa na Wajerumani, tawala za aina hii zilidhoofishwa na migogoro ya ndani na kusambaratika.

Magharibi mwa Tanzania, biashara ya masafa marefu ilizusha ushindani wa kibiashara. Ulikuwapo uhasama miongoni mwa machifu wa Waafrika, miongoni mwa walowezi wa Kiarabu, na baina ya machifu wa Waafrika na walowezi wa Kiarabu. Ushindani huu wa kutaka kudhibiti biashara ulisababisha vurugu ambazo nazo zilichochewa na kuhamahama kwa watu kulikosababishwa na uvamizi wa Wanguni. Katika hali hii ya wasiwasi, viongozi jasiri kama vile Msiri wa Wasumbwa, Simba na Nyungu ya Mawe wa Wanyamwezi, walipata wafuasi wao binafsi ambao waliwawezesha kuanzisha dola. Watawala wengine wa Tanzania ya magharibi kama vile Mirambo waliitumia hali ya vurumai iliyokuwapo kujiongezea nguvu na kupanua mipaka ya madola yao. Lakini kudumu kwa tawala hizi hakukutegemea mafanikio ya kijeshi ya awali ya viongozi wao, bali kuwapo kwa msingi imara wa utawala wenye ufanisi na ushirikishwaji wa mataifa yaliyoshindwa vitani. Hii ndio sababu iliyofanya utawala wa Nyungu ya Mawe, kwa mfano, kuendelea kudumu hata baada ya kifo chake, ilhali himaya ya Mirambo ilisambaratika mara tu alipofariki.

Baadhi ya falme kubwa katika eneo la Maziwa Makuu zilipata nguvu kwa kushirikiana na wafanyabiashara wa pwani. Zilijilimbikizia bunduki na kuwavamia majirani zao na nchi zisizokuwa na tawala unganifu katika eneo hilo. Makundi mengine ya bara ya kaskazini-kati ya Afrika Mashariki hayakuathiriwa sana na biashara ya

masafa marefu. Walishughulika kidogo sana na wafanyabiashara wa pwani na kwa hakika hawakupenda wageni kutembelea vijiji vyao. Rwanda na Burundi, kwa mfano, zilizuia biashara hii kutoingia katika nchi zao na zilifanikiwa kuzuia mashambulio kutoka kwa majirani zao ambao walikuwa na bunduki walizopata kutokana na biashara ya masafa marefu. Halikadhalika Wamasai kama tulivyokwishaona kwa kiasi kikubwa hawakuathiriwa na biashara ya masafa marefu.

## *Uvamizi wa Wanguni*

Wanguni walitokea Afrika ya Kusini walipoyakimbia maskani yao kama mwaka 1820 kutokana na mashambulio ya mara kwa mara ya Shaka. Walielekea kaskazini chini ya kiongozi wao Zwangendaba na walizunguka huko na huko hadi walipofika uwanda wa juu wa Ufipa, Tanzania ya magharibi, mapema miaka ya 1840. Wakati huu walikwisha jizatiti na kuwa taifa la kijeshi.

Wakimbizi wa Kinguni walibadilika na kuwa taifa la kijeshi kwa kuiga utaratibu wa Wazulu ambapo wageni walikubalika kuwa sehemu ya jamii kwa njia ya ukoo au makundi ya marika. Hivyo Wanguni waliweza kuwachukua na kuwajumuisha watu waliokutana nao na kuwashinda katika safari yao ya kuelekea kaskazini. Waliweza pia kutumia uwezo wao wa kijeshi kujihami kwa kuwashambulia majirani zao na kuwateka wanaume na wanawake wenye nguvu pamoja na ng'ombe. Kwa njia hii waliweza kuongeza idadi yao kwa mateka wa kivita ambao walijumuishwa katika mfumo wa jamii wa Wanguni. Hadi walipowasili uwanda wa juu wa Ufipa, watu waliotekwa na kujumuishwa katika taifa la Wanguni walikuwa ndio wengi zaidi.

Zwangendaba alipofariki mwaka 1848, kulizuka mfululizo wa mizozo ya kugombea madaraka ambayo hatimayeililigawa taifa katika makundi matano. Makundi matatu kati ya haya yalielekea kusini na kuanzisha falme katika nchi za Zambia na Malawi ya sasa. Kundi la nne liliselelea upande wa kaskazini na kuendelea kuwashambulia majirani zao. Kundi la mwisho ambalo lilijulikana kama Wagwangara nalo liligawanyika katika falme mbili: Ufalme wa Mshope na ufalme wa Njelu.

Umuhimu wa uvamizi wa Wanguni ni kuanzishwa kwa tawala za Wanguni katika ardhi ya Tanzania. Falme mbili zilizotajwa juu ziliendelea kuwa na nguvu hata wakati wa ukoloni. Utumiaji na unasibishaji wa mbinu za kivita za Wanguni uliofanywa na baadhi ya makabila ya Tanzania ni mojawapo ya matokeo muhimu ya uvamizi wa Wanguni. Mbinu za kivita za Wanguni ziliyaimarisha makabila yaliyozitumia na kuyawezesha kukabili vurugu na wahaka uliosababishwa na biashara ya masafa marefu, uvamizi wa wafanyabiashara wa pwani na kuongezeka kwa mahitaji ya watumwa. Baadhi ya makabila, kama vile Wasangu na Wahehe katika Tanzania ya sasa, walitumia mbinu za kivita za Wanguni sio tu kwa ajili ya kujihami, bali kwa ajili ya kuunda taifa kubwa ambalo liliendelea kuwa na nguvu na kuweza kupambana vikali na Wajerumani wakati wa kipindi cha ukoloni.

Kwa hiyo Tanzania ya kusini ilishuhudia mabadiliko mengi ya kijamii na kisiasa katika kipindi cha pili cha karne ya kumi na tisa. Baadhi ya mabadiliko haya



**10.4** *Mirambo, 1882 au 1883*

yalianzishwa na biashara ya masafa marefu na kuzidishwa na uvamizi wa Wanguni. Wakati ukoloni ulipoingia kwenye miaka ya 1880, Tanzania ya kusini ilikwishakuwa na madola yenye nguvu sana katika ukanda huu, kama vile falme za Wanguni, Wahehe na Wasangu.

## *Vita vya Wamasai*

Vita vya Wamasai vilivyopiganwa katikati ya karne ya kumi na tisa viliathiri historia ya eneo kubwa la kaskazini mashariki ya bara ya Afrika Mashariki katika kipindi cha pili chote cha karne hiyo. Hii ni kwa sababu mfululizo wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyochukua muda mrefu hatimaye viliwadhoofisha Wamasai ambao walikuwa wameudhibiti uwanda wa juu wa Uasin Gishu, jambo ambalo lilikuwa muhimu katika mgawano wa mamlaka katika eneo hili.

Vita hivi vilisababishwa hasa na ugomvi uliotokana na mashindano ya kudhibiti ng'ombe na ardhi ya malisho, vitu ambavyo vilifikiriwa kuwa muhimu kwa utamaduni wa ng'ombe wa Wamasai au mtindo wao wa maisha wa ufugaji.

Vita vya mwanzo huenda vilisababishwa na kugombania ardhi ya malisho katika uwanda wa juu wa Uasin Gishu. Vita vya pili vilianza baada ya njaa kuu ya 1836 ambayo iliathiri sehemu nyingi za Afrika Mashariki. Inaelekea kuwa mashambulio mengi yalifanywa wakati huu ili kufidia mifugo iliyoangamia wakati wa ukame. Hali hii ilisababisha mapambano katika eneo lote la Wamasai. Vita vya pili vilipokaribia kuisha, udhibiti wa Wamasai katika uwanda wa juu wa Uasin Gishu ulianza kupungua na kuashiria kuongezeka kwa nguvu ya makundi mengine kama vile Wanandi na Wakipsigi. Kupungua kwa udhibiti wa Wamasai katika uwanda huu kuliwawezesha wafanyabiashara wa pwani kutumia njia za misafara zilizopitia Kenya ambazo hapo awali walikuwa wakizikwepa.

Vita vya mwisho vya Wamasai vilipiganwa katika uwanda wa juu wa kaskazini. Kutokana na vita hivi, makundi ya Wamasai yenye nguvu katika uwanda wa juu yaliangamizwa na yaliyonusurika yalisambaratika. Wamasai waliopoteza ng'ombe wao waliacha maisha ya kuchunga na kuamua kuwa wakulima. Wamasai wafugaji walioshinda katika vita hivi walipoteza sehemu ya ardhi yao na kuathiriwa na maradhi kama vile kipindupindu na ndui ambayo yalienea sehemu hii baada ya vita hivi vilivyodumu mwa muda mrefu. Maradhi haya ya binadamu na wanyama hatimaye yaliwadhoofisha Wamasai kwa ujumla na kuwafanya washindwe kupinga kutawaliwa na wakoloni.

## *Kuongezeka kwa mashinikizo ya Wazungu*

Mashinikizo ya Wazungu katika Afrika Mashariki baina ya 1845 na 1884 yalihusiana na shughuli nne zilizoingiliana, yaani, kupiga marufuku biashara ya watumwa, kueneza Ukristo, upelelezi wa kijiografia wa Afrika Mashariki na kuanzishwa kwa biashara halali katika eneo hili.

"Biashara halali" maana yake ni biashara ya bidhaa nyingine isipokuwa watumwa.




*10.5 Njia za uhamaji kuelekea kaskazini za Wangoni wa Zwangendaba, Maseko na Msene (J.D. Omer-Cooper, 1966 uk. 66)*

Hadi mwaka 1845, pembe za ndovu zilikwisha kuwa bidhaa muhimu kwenye biashara ya kimataifa katika Afrika Mashariki. Ijapokuwa biashara ya pembe ilidhibitiwa na wafanyabiashara Wahindi, ambao walisafirisha pembe hizo hadi Bombay, bidhaa hii ilisafirishwa tena kwenda Ulaya. Hivyo, kwa mujibu wa mwelekeo wake, ni dhahiri kuwa biashara ya Afrika Mashariki ilikuwa ikielekea Ulaya. Kampuni za Wamarekani na Wadachi zilifanya biashara moja kwa moja na Afrika Mashariki, zikibadilisha vitambaa vya pamba na vifaa vya bati kama vile sufuria kwa pembe za ndovu.

Juhudi za serikali ya Uingereza kuzuia biashara ya watumwa Afrika Mashariki haikufanikiwa, na biashara hii iliendelea hadi wakati wa ukoloni. Iliwawia vigumu sana masultani wa Unguja kuzuia biashara ya watumwa kwa sababu uchumi wa kilimo cha viunga huko Zanzibar ulitegemea nguvukazi ya watumwa ili kuzalisha karafuu. Juhudi yoyote ya kupiga marufuku biashara ya watumwa ingeleta athari mbaya kwa uchumi wa Zanzibar iwapo hapangekuwa na namna nyingine ya kupata nguvukazi rahisi. Hata huko bara kulikuwa na viunga vya nafaka katika ukanda wa pwani ambavyo vilihitaji nguvukazi ya watumwa. Ilikuwa vigumu kutofautisha watumwa waliokuwa wakisafirishwa nje na wale ambao walikusudiwa kupelekwa kwenye mashamba ya hapa hapa. Aidha wafanyabiashara ya watumwa daima walibuni mbinu mpya za kukwepa wasikamatwe.

Hadi 1856, shughuli za Wazungu zilikuwa zikifanywa pwani na Unguja. Kwa hivyo Ulaya ilifahamu mambo machache sana kuhusu yaliyokuwa yakifanyika huko bara. Taarifa za safari za wapelelezi kadha ndizo baadaye ziliwatanabahisha kuhusu yale yaliyokuwa yakitendeka ndani ya bara ya Afrika Mashariki. Safari za David Livingstone katika Afrika Mashariki na Kati ndizo hasa zilizoivutia shauku ya Wazungu kwa bara ya Afrika Mashariki. Kabla ya safari hizi, wamisionari watatu Wadachi waliotumwa na shirika la CMS lililokuwa na makao yake karibu na Mombasa walikwisha safiri hadi bara. Wamisionari hawa walikusanya taarifa muhimu kuhusu bara ya Afrika Mashariki ambazo zilikuwa za manufaa kwa wapelelezi na wamisionari wa baadaye. Kutokana na kuifahamu vyema bara ya Afrika Mashariki kufuatia ziara zake nyingi alizofanya, Livingstone alishauri kufanyike biashara kubwa na Afrika Mashariki ambayo ingeunganisha bara hii na Ulaya ya Kikristo na kufutilia mbali maovu ya biashara ya watumwa.

Hivyo shughuli za wamisionari katika Afrika Mashariki zilianza na suala la watumwa walioachiwa huru. Mashirika ya CMS, UMCA na Mapadre wa Roho Mtakatifu yalishiriki katika tatizo hili baina ya 1858-1873. Wakati wamisionari wakiishughulikia pwani, wapelelezi wa Ulaya nao walikuwa wakiishughulikia bara baada ya kuhamasishwa na juhudi za wamisionari. Wapelelezi hawa walifichua unyama wa biashara ya watumwa iliyokuwa ikiendeshwa na Waarabu, jambo ambalo lilichochea raghba ya wamisionari.

Mashinikizo ya Wazungu katika bara ya Afrika Mashariki kabla ya 1884 yalifanywa hasa na mashirika ya wamisionari. Misheni za Waprotestanti kama vile *CMS*, *UMCA*, *London Missionary Society*, *the Scottish Free Church* na shirika la Wakatoliki la *White Fathers*, ziliingia bara baada ya kifo cha Livingstone mwaka 1873, kuanzisha vituo vingi

na kueneza imani ya Kikristo. Shughuli za kibiashara zilizokuwapo zilikuwa chache sana na zilifanywa hasa kwa ufadhili wa misheni, kama vile zile za makampuni ya Livingstonia Central African Trading Company na *British India Steam Navigation Company*, ambayo yalihusishwa na *Scottish Free Church*.

Kutokana na maelezo yaliyotangulia, ni dhahiri kuwa kazi ya umisionari katika Afrika Mashariki baina ya 1845-1884 ilikuwa katika hatua zake za mwanzo. Hata hivyo ilikuwa na athari kubwa kwa wenyeji. Kwa kuwa wamisionari walikuwa huru kufanya wapendavyo wakati huu kuliko wakati wa kipindi cha ukoloni kilichofuata, walianzisha makoloni ambayo yaliwavutia watumwa walioachiwa huru, wakimbizi wa kisiasa, watumwa waliotoroka, na watu wengine ambao hawakuridhika na hali yao. Hali hii iliviíanya vituo vya misheni kujaa watu na kusitawi kwa kuyadhoofisha madola ya Waafrika yaliyokuwapo. Hivyo jamii za asili ambazo zilikwisha nyonywa kiuchumi na biashara ya kimataifa zilidhoofika zaidi kiasi cha kutoweza kujihami dhidi ya uvamizi wa wakoloni. Kwa maana hii twaweza kusema kuwa wamisionari waliuandalia njia utawala wa kikoloni ambao ulianzishwa kwenye miongo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa.

# 11

# *Watu Na Dola za Ukanda wa Maziwa Makuu*

## *Utangulizi*

Ukanda wa Maziwa Makuu ni eneo lenye watu wengi na lipatalo maji ya kutosha, lililopo Afrika ya Mashariki na Kati likienea katika baadhi ya sehemu ambazo leo zinajulikana kama Uganda, Kenya, Zaire na Tanzania. Jiografia yake inatawaliwa na bonde Kuu la Ufa ambamo hupatikana maziwa makuu hayo ambayo hupokea maji ya mito kadhaa. Kabla ya utawala wa kikoloni kuingia, eneo hili lilikuwa na mambo ya kufanana katika historia, uhamiaji wa watu na miundo ya kijamii na kisiasa.

Karne ya kumi na tisa ilishuhudia ukanda wa Maziwa Makuu ukiendeleza matukio yaliyokwishaanza katika eneo hilo. Katika mwanzo wa karne, nchi za ukanda huu zilikuwa bado katika kukuza na kujaribu kujizatiti kikamilifu kwa kuanzisha taasisi mpya na kuingiza maeneo mapya chini ya himaya zao. Ukanda huu uliendelea na hali ya chokochoko iliyokuwepo karne ya kumi na nane kutokana na upinzani wa kila wakati wa vitendo vya mara kwa mara vya uasi dhidi ya watawala kwa mfano, waasi wa nasaba ya kifalme au watu walioshindwa katika kugombea kazi zenye wadhifa mkubwa kuingia mafichoni na kukusanya jeshi la uvamizi au kushirikiana na watawala wa dola nyingine.

Kutotengemaa huku hata hivyo hakukuzuia dola kutoingiliana. Dola hizi hazikuwa zimejitenga bali zilifanya mtandao wa mawasiliano na uhusiano wa kidiplomasia miungano, arusi baina ya koo za kifalme, mabadilishano ya kibiashara na harakati za kijeshi ambazo zote kwa pamoja zilionekana na watawala kuwa muhimu katika kukabiliana na udhaifu wa ukanda huo.

Katika mambo ya ndani kila dola ilikuwa na mvuto mkubwa kwa watu walioiunda, hasa katika kushughulikia matakwa yao kuhusu kuendelea kwa maisha yao ya nyumbani, uzalishaji, biashara, mawazo na utekelezaji wa dini.

## *Utaratibu wa Kisiasa*

Katika karne ya kumi na tisa ukanda wa Maziwa Makuu ulikuwa na dola nyingi zenye ukubwa na nguvu zinazotofautiana. Kila dola ilikuwa na mfalme aliyetokana na




**11.1** *Ukanda wa Maziwa Makuu (baada ya D. Cohen)*

nasaba ya kifalme. Katika huduma ya utawala wa dola walikuwepo pia washauri, madiwani, maofisa wengine waliowekwa kwa mfumo wa ngazi na mafundi mchundo. Kama ilivyoelezwa hapo awali, mapambano kutoka ndani na nje yalibakia kuwa matukio muhimu katika siasa za ndani.

Matukio mawili yliyohusiana yaliathiri hali ya siasa ya ukanda huu katika karne ya kumi na tisa. La kwanza lilihusu kuibuka na kukua kwa nguvu za baadhi ya nchi. Hili liliwezekana kutokana na kuwepo kwa kazi na bidhaa za biashara, kukua kwa taasisi za utawala msonge na uongozi mwerevu wa athari na nguvu mpya zilizoingia ukandani. Tukio la pili lilikuwa kupanuka kwa haraka kwa nchi nne kongwe za ukanda, zikiwa ni Buganda, Rwanda, Burundi na Bunyoro. Kila moja ya dola hizi nne ziliweza kupanuka kwa kuimarisha udhibiti wa utawala wake, kuondoa upinzani wa uongozi wa kisiasa, kupeleka mapambano nje kwa njia ya vita vya upanuzi wa kuteka maeneo mapya ambayo matokeo yake yalipanua nchi na kuwaletea utulivu mkubwa ndani ya mipaka yao. Ili kupata msingi imara zaidi wa uchumi, dola hizi zilitaifisha maeneo yote ya kimkakati ukandani ya uzalishaji wa biashara. Pia walichukua na kuunganisha mambo na nguvu mpya zilizoingia kwenye ukanda wao mpana. Umaarufu wao uliongezeka na wakajulikana.

Kiashirio cha mabadiliko katika falme hizi kuu katika karne ya kumi na tisa kilikuwa urefu wa kipindi cha utawala cha watawala wao. Kamanya, mtawala wa kwanza wa Kibaganda katika karne ya kumi na tisa, alitawala kwa miaka ipatayo 35. Alirithiwa na Suna aliyetawala kwa miaka 20 na Mutesa aliyekalia kiti kwa miaka 28. Hii ilikuwa tofauti na hali iliyokuwepo katika karne ya kumi na nane, ambapo si chini ya wafalme kumi na moja walitawala Buganda. Hali kama hii ilitokea Rwanda ambako wafalme watatu walitawala katika karne ya kumi na tisa kila mmoja akitumia sio chini ya miaka 30 kwenye madaraka. Katika Burundi kipindi cha utawala kilikuwa kirefu kiasi kwamba ni wafalme wawili tu walitawala katika karne ya kumi na tisa na hali wanne walitawala katika karne iliyotangulia. Mfalme aliyetawala kwa kipindi kirefu katika Bunyoro katika karne ya kumi na tisa alikaa kitini kwa miaka 29.

Tawala hizi ndefu zilikuwa na uwezo wa kuimarisha siasa za kila moja ya dola hizi nne. Watawala walikuwa na nafasi ya kurekebisha utawala wo na kuongeza nguvu zao.

Tawala hizi ndefu pia ziliwapa nafasi ya kujizatiti madarakani. Kuliwezesha kuwepo mfungamano kati ya tawala na tawala kwani mipango na sera ziliendelezwa kutoka tawala moja hadi nyinginge. Hii ilikuwa na matokeo ya jumla ya kuyapa maana na uelekeo mlolongo wa kisiasa. Pia iliruhusu kuchipua na kukua kwa taasisi za jamii za familia, huduma za jamii, uzalishaji, ubadilishanaji na ugawaji unaotosheleza wa miji mikuu na vitala.

Kwa muda mwingi wa karne ya kumi na tisa, Buganda, Rwanda, Burundi, na Bunyoro zilibakia kuwa dola kubwa za ukanda wa maziwa makuu. Matukio katika kila moja ya nchi hizi yaliendelea kuathiri nchi nyingine ndogo ambazo idadi yake ilikuwa zaidi ya mia - mbili - nyingi kati yao zilipoteza uhuru wao na kuwa nchi tegemezi. Kwa maneno mengine. falme kubwa zilikuja kuwa vituo vya mvuto kwa



**11.2** *Buganda mwaka 1875: Mji Mkuu wa Kabaka.*

**11.3** *Kabaka Mutesa pamoja na watemi na maofisa*



watu kutoka nchi ndogo ndogo na hivyo kuchangia katika udhaifu wao.

Kwa kuweza kupata rasilmali mpya kutoka nje kama bidhaa za biashara, wafanyabiashara wa nje na wamisionari wa Kikristo na Kiislamu, falme kuu zilizidi kuwa na nguvu kuanzia katikati ya karne ya kumi na tisa. Kwa bahati mbaya, ushindani wa kumiliki raslimali hizi za nje kulisababisha tatizo lingine katika ukanda huu. Ushindani wa wahusika wakuu wa kambi tofauti ukawa ni sababu nyingine ya mgawanyiko. Ingawa, kwa ujumla, nguvu hizi mpya ziliongeza nguvu za nchi hizi nne kubwa, ziliwafanya kuzidisha hali ya kukosekana usalama katika eneo lao.

## *Uzalishaji na Utoaji*

Kadri nchi za Ukanda wa Maziwa zilivyokuwa kisiasa, zilitafuta kuanzisha msingi imara wa kiuchumi ili kuhudumia vitala na miji yao mikuu kwa kudhibiti uzalishaji wa chakula na biashara katika ukanda. Hii ndiyo hasa iliyokuwa kazi yao kubwa tangu karne ya kumi na nane, kama upanuzi wa Buganda ndani ya Kyaggwe katika karne ile unavyodhihirisha. Lengo la Buganda wakati huo lilikuwa mikoa inayozalisha ya Kyaggwe. Hivyo, dola kubwa za ukanda wa Maziwa zilitamani vituo vya uzalishaji vilivyowazunguka ambavyo walivitumia kwa manufaa yao.

Kulikuwa na njia nyingi za kukusanya mapato kutoka kwenye maeneo haya tajiri. Kwanza, kabisa, sehemu shiriki za nchi kubwa na zile zinazowategemea zilileta mara kwa mara kodi kwenye miji mikuu na vitala vya mfalme aliye madarakani. Malipo haya ya kodi hayakuwa ya kujitolea. Yalikuwa yakitolewa kwa nguvu na maajenti wa watawala wa dola kubwa. Hii ilisababisha kutokuelewana kwingi na kuharibu mahusiano kati ya nchi kubwa na zile tegemezi. Kutokuelewana huku kuliathiri vibaya biashara katika ukanda huu na kulijitokeza zaidi katika vituo vya uzalishaji. Hivyo chakula kutoka sehemu tegemezi za ukanda zililisha vitala na miji mikuu ya falme kuu. Ingawa michango ya chakula kutoka sehemu hizi kwenda makao makuu ilikuwa ya mara kwa mara kulikuwa na wakati wa dharura kama vile wakati wa vita ambapo ililazimu kupeleka majeshi ili kulazimisha matoleo ya ziada kutoka kwa wazalishaji.

Mtindo mwingine wa utoaji ni ule uliowakilishwa na uanzishaji wa mashamba ya serikali chini ya uangalizi wa maofisa walioteuliwa ambao kazi yao ilikuwa kuhudumia mahitaji ya miji mikuu na vitala vya watawala. Kwa mfano, katika Buganda, Rwanda, Nkore, Karagwe na Burundi, kulikuwa na mashamba hayo ya kifalme ambayo yalitoa chakula sio tu kwa kaya za watawala bali pia kwa machifu wao wakuu. Mashamba haya ya serikali yaliendeshwa hata kuweza kuongeza uzalishaji kwa taarifa ya muda mfupi sana.

Licha ya utaratibu huu wa uzalishaji wa kutoka kitovuni falme zenye nguvu zilikuwa na utaratibu wa utoaji na uchukuaji ushuru kutoka kwenye maeneo yaliyo nje ya utawala wao wa kisiasa. Huu ulikuwa wa aina mbili. Ya kwanza ilihusu uchukuaji usiokuwa na kanuni lakini uliotegemewa. Matoleo haya yalikuwa hayana kanuni kwa sababu yalifanyika katika vipindi tofauti tofauti. Hata hivyo, walengwa

hata mara moja hawakukosa rasilimali ya kushindwa kulipa. Ukweli kuwa wakati wote walikubali baada ya kwanza kukataa na hata bila kulazimishwa, inaonyesha dhahiri kuwa waliyategemea madai hayo. Mfano mmoja ni unyonyaji wa Busoga ya kati na Buganda wa ndizi zilizokaushwa na vitu vingine. Ukusanyaji huu wa kawaida uliwalazimisha Wabasoga waongeze uzalishaji wao zaidi ya matumizi yao halisi, walihifadhi ziada iliyopatikana kwa ajili ya kulipa ushuru.

Mfano mwingine ni uchukuaji wa chumvi kutoka eneo la ziwa George kulikofanywa na Bunyoro.

Aina ya pili ilihusu ukusanyaji wa ushuru ambao haukuwa na kanuni ambao haukutegemewa kutoka kwenye maeneo ya mbali. Ukusanyaji katika sehemu hizi za mbali ulichukuwa zaidi sura ya kijeshi. Makundi yenye silaha yalishambulia eneo na kuchukua kila walichokipata kama ni mateka, ng'ombe, vifaa vya chuma, na mali nyingine inayobebeka. Vikosi vya Buganda vilivyoingia Busonga ni kielelezo dhahiri cha jambo hili. Kuweko kwa jeshi la Waganda katika Busonga ya kati kuliharibu utaratibu wa uzalishaji wa eneo hilo. Katika karne ya kumi na tisa Rwanda pia ilipeleka vikosi vya kijeshi katika sehemu za kaskazini na magharibi yake na kujipatia vifaa vya thamani na ng'ombe. Mashambulizi haya, kwa ujumla, yaliharibu uzalishaji na biashara katika sehemu husika. Baadhi ya maeneo ambayo yalishambuliwa kwa ajili ya chakula yalipata mahitaji yao kutoka maeneo ya jirani ambayo yaliongeza uzalishaji wao ili kumudu mahitaji ya nje. Zaidi, mashambulizi haya yalikuwa na matokeo ya kuanzisha njia za kuaminika za kwendea maeneo yaliyopangwa kushambuliwa.

Programu za kuchukua za baadhi ya falme kuu katika ukanda huu, zilipata upinzani kwa vitendo katika maeneo ya uzalishaji kwenye karne ya kumi na tisa. Kwa mfano, mashambulizi ya jeshi la Buganda yalipingwa katika mashariki na magharibi ya Busonga. Ili kujiongezea makusanyo, Buganda ilitafuta njia za kupata bunduki, ikaingilia kati siasa za ndani za vikundi vingine na kuongeza kiwango cha mashambulizi yake ya kijeshi ili kupata maeneo mapya kutokana na maeneo ya zamani ya uzalishaji kuporomoka. Haya yote yalipingwa kwa nguvu na sehemu ya kitovu ya uzalishaji. Hali hii, hata hivyo, haikuwa ya pekee kwa Buganda. Makusanyo ya Rwanda pia yalipingwa na watu waliokuwa magharibi na kaskazini-magharibi yake katika kipindi karibu chote cha karne ya kumi na tisa.

## *Ulazimishaji, Vurugu na Soko*

Upingamizi wa makusanyo yaliyokuwa yakifanywa na dola kuu, yalisababisha matokeo mengi mojawapo likiwa kufa kwa taratibu kwa maeneo ya uzalishaji na utoaji ushuru. Hii iliathiri pia vitala na miji mikuu kwani ilibidi njia bora na ghali kuchukuliwa ili kuendeleza upatikanaji wa kiasi kikubwa cha ushuru kutoka maeneo nje ya yale yenye kuzalisha mara kwa mara. Upingamizi uliongeza kiwango cha vurugu katika ukanda huu. Zaidi, biashara iliathirika mno kutokana na vurugu hizo.

Ugomvi mkubwa ulizuka katika karne ya kumi na tisa wakati baadhi ya maeneo



**11.4** *Nyumba ya hazina na mapambo ya mfalme Rumanyika wa Karagwe*

**11.5** *Vita vya majini katika Ziwa Viktoria kati ya Wabaganda na watu wa visiwa vya Buvuma, 1875*



ya uzalishaji katika ukanda wa maziwa kuwa malengo, kwa wakati mmoja, ya nchi mbili au tatu zinazokusanya ushuru. Kwa mfano, eneo la Budiope la kaskazini ya Busoga na Bugerere lililopo magharibi ya Naili yalikuwa kwa wakati huohuo malengo ya Bunyoro na Buganda, wote wakitaka kuchukua mazao ya sehemu hizo. Hii ikasababisha ugomvi mkubwa kati ya nchi hizi mbili kwa muda mrefu wa karne. Ugombeaji huu wa ushuru kati ya dola zenye nguvu za kanda hii kutakuwa kumesababisha matukio mengi. Pengine katika sehemu nyingine kulisababisha kuanzishwa kwa umoja wa kujilinda kati ya makundi yalipayo ushuru. Kwa wengine, pengine imeweza kupunguza idadi ya watu na kiwango cha uzalishaji wa sehemu zilizolengwa. Na bado katika sehemu nyingine, pengine uzalishaji ulizidishwa zaidi ya matakwa ya sehemu husika.

Ingawa katika sehemu nyingine za Ukanda wa Maziwa walikuwa wakizalisha zaidi ya mahitaji yao, nyingine zilikuwa na uhaba mkubwa wa chakula. Uhaba huu, uliotokea mwanzoni mwa masika na wakati wa majira marefu na miaka ya mavuno haba ulithibitiwa kwa ufunguzi wa masoko ya muda ukandani. Masoko haya yaliwekwa wakati wa matatizo kwa kubadilishana mifugo, nafaka, samaki, mboga za majani na vitu vya kutengenezwa; navyo vilithibitiwa na watu kutoka nasaba kuu katika eneo.

Katika baadhi ya maeneo, kwa mfano magharibi ya Kenya, mazao ya chakula yalikuwa haba kutokana na mvua isiyoaminika na vipindi virefu vya kiangazi. Hii ikasababisha watu wahame sehemu hizo na kwenda kwenye sehemu bora na za mwinuko kandani humo. Utaratibu wa kuhama kwenye miinuko, ambao unaendelea mpaka leo, umesababisha watu wengi sana kuishi vijijini na hivyo kuchangia katika kuuchosha udongo na uharibifu wa hifadhi za misitu.

Watu wengine walibaki kwenye nyanda za chini na kuendelea kupata uhaba wa chakula, huku masoko ya muda yakiwapa afueni. Walifuga ng'ombe ambao walitumiwa kama mali ya kuweza kubadilishana.

## *Misafara ya biashara*

Kulikuwa na mtandao mkubwa wa biashara katika ukanda wa maziwa katika karne ya kumi na tisa. Kwa upande mmoja kulikuwa na mitandao ya kimkoa au misafara ambayo ilimilikiwa na vikundi fulani vya eneo hilo, na kwa upande mwingine kulikuwa na njia za kimataifa za kibiashara ambazo ziliunganisha ukanda wa maziwa na pwani ya Afrika Mashariki. Biashara ya kimkoa ilionyesha kuwa, ilisababishwa na ukosefu wa kujitegemea kwa vikundi vilivyohusika na uzalishaji. Hivyo, mabadilishano ya biashara yalisababisha uanzishaji wa mtandao mpana wa mawasiliano. Moja ya mtandao wa kimkoa wa biashara ulikuwa na kituo chake Ziwa Kivu. Rwanda ilishiriki kikamilifu katika mfumo huu wa biashara. Vifaa vikubwa vilivyobadilishwa vilikuwa shanga zilizofumwa, ng'ombe na chakula.

Shanga zilizofumwa, zilizojulikana kama *butega* zilitumiwa sana katika




**11.6** *Njia za biashara za ukanda wa Maziwa Makuu (bauda ya D. Cohen)*

mabadilishano katika eneo la Kivu na hii, kwa namna moja, iliongeza uzalishaji katika eneo hilo.

Mtandao mwingine wa kanda uliunganisha sehemu za mashariki ya Ziwa Victoria. Nchi ya Bukerebe ilitawala biashara ya sehemu ya mashariki ya mtandao huu wa mashariki ya Ziwa. Nchi hii, mapema katika karne, ilipitia mapinduzi ya kilimo hivyo iliweza kupanga uzalishaji wa mazao tofauti kama mahindi na mihogo, na pia kuanzisha aina mpya ya matunda na ulezi ukandani. Uwezo wa kuzalisha chakula cha ziada uliwawezesha wachuuzi wa Bukerebe wahame kutokana na njaa huko Buzinza na Usukuma, kwa kubadilisha chakula katika viwango vya kinyonyaji kwa vifaa vya bati na ng'ombe na hivyo kuchukua nafasi muhimu katika mzunguko wa biashara. Wafanyabiashara wa Basuba walitawala mtandao wa biashara wa ncha ya kaskazini ya Maziwa ya mashariki. Walisafirisha chumvi, watumwa, ndizi zilizokaushwa, nafaka, maharagwe, mifugo, samaki na chuma kupitia Ziwa Victoria, hivyo kuyaunganisha masoko ya kusini ya Bukerebe na Busoga ya kusini na yale masoko ya kaskazini ya Buvuma.

Wafanyabiashara wa Basuba walianzisha mtandao mwingine wa kikanda katika eneo la maziwa ya chumvi katika Uganda magharibi. Vikundi hivi vilimiliki kabisa uzalishaji na uuzaji wa chumvi. Katika sehemu zote za maziwa ya chumvi na mtandao wa Maziwa ya mashariki kama ilivyoelezwa hapo juu, wafanyabiashara waliendesha himaya zao za biashara na masoko bila kuhusisha nchi za ukanda wa Maziwa Makuu na waliweza kutoa kwa ajili ya mahitaji ya nchi hizo pale tu waliposhurutishwa kijeshi kufanya hivyo.

Mtandao mwingine mkubwa wa kibiashara katika karne ya kumi na tisa ulijikita kwa ujumla, katika eneo la Bunyoro na kuenea hadi maeneo ya jirani. Vifaa vya chuma na chumvi vilikuwa vifaa muhimu katika mabadilishano ingawa bidhaa nyingine kama chakula na mifugo navyo vilifanyiwa biashara. Ubadilishaji huu ulikuwa na matokeo ya kuchochea uzalishaji zaidi katika baadhi ya maeneo husika. Mfano mmojawapo ni uzalishaji ulioongezeka wa sesame uliofanywa na Wakingo. Bunyoro ilichukua nafasi kubwa katika mtandao huu wa biashara. Mazao kutoka bonde la Ziwa Kyoga yalipelekwa kwenye soko la Nyoro. Mawakala wa himaya ya Bunyoro na wa nchi zake tegemezi walitoza kodi uzalishaji, uchukuzi na uuzaji wa bidhaa, chakula na mifugo iliyokuja kutoka ziwa Kyoga na Uganda Magharibi.

Umuhimu wa Bunyoro katika soko la ukanda huu hauhitaji maelezo zaidi. Watawala wake na wale wa Toro walitoa mchango mkubwa katika mfumo wa mabadilishano ya uwanda wa magharibi wa ukanda wa ziwa bila kuathiri utaratibu wa usafirishaji na ubadilishanaji wa bidhaa.

Ubadilishanaji wa kimataifa ulihusu kuingia katika kanda hii kwa Waarabu na wafanyabiashara wa Kiswahili wakijihusisha katika eneo la Unyamwezi. Walikuja kwa mara ya kwanza kwa kupitia kwenye mtandao wa Bukerege ambao hatimaye waliuchukua. Waliingia ndani zaidi ya ukanda huu kwa kupitia njia zilizokuwa

zikitumiwa na wafanyabiashara wa maziwa ya chumvi. Walileta katika ukanda huu bunduki kwa kubadilishana na watumwa na pembe. Wavumbuzi wa Kizungu, wamisheni wa Kiislam na Kikristo baadaye walifuata nyayo za hawa wafanyabiashara wa nje hivyo kufungua njia kwa nguvu mpya za mabadiliko katika ukanda wa maziwa makuu.

Wakati Waarabu na Waswahili wakiingia eneo lizungukalo Ziwa Victoria, Buganda ilikuwa ikitafuta, kuanzisha uhusiano wa moja kwa moja wa kibiashara nao katika upande wa kusini wa ziwa. Hii ilipunguza zaidi mvuto wa Bukerebe katika mashariki na kaskazini. Hata hivyo, mvuto wa Buganda katika ukanda huu haukuanzisha mtandao mpya wa masoko kama walivyofanya Bukerebe.

Kama ilivyozungumzwa awali mamlaka za Bunyoro zilichochea upanuzi wa mabadilishano ya biashara katika ukanda wa Magharibi wa ukanda wa Maziwa. Shughuli za Buganda ziliharibu na kusonga shughuli za ununuzi katika sehemu hiyo hiyo. Katika karne ya kumi na tisa Buganda ilikuwa nchi ya vita au yenye kuchukua ushuru huku ikiwa haina mpango wa kupanua mabadilishano katika ukanda mdogo. Lakini wakati huo huo Buganda ilikuwa ikishiriki kikamilifu katika mabadilishano ya nje kutoka kwenye fuko za Ziwa Victoria hadi pwani ya Afrika Mashariki. Tofauti kati ya michango ya Bunyoro na Buganda katika maisha ya uchumi ya ukanda wa Maziwa ulikuwa katika viwango walivyojihusisha katika biashara. Wakati Bunyoro ikishiriki kikamilifu katika biashara ya kanda na hata kuchangia katika upanuzi wake, Buganda ilishambulia nchi nyingine za ukandani kama suluhisho la kutatua matatizo ya kukosa bidhaa za kienyeji za aina yo yote, hivyo kufaidika bila kuchangia katika biashara ya kanda, wakati huo huo Buganda iliingia katika mfumo mpana wa biashara ya kimataifa ambao ulikuwa ukiingia kwa uhakika katika ukanda wa maziwa kutoka pwani ya Afrika Mashariki na kuweza kwa kiasi fulani kuiondoa Bunyoro kujihusisha katika biashara hii ya nje. Hii ilisababisha kupungua kwa mvuto wa Bunyoro ukandani.

Biashara ya nje kutoka pwani ya Afrika ya Mashariki hadi kanda ya Maziwa ilihusu mabadilishano ya bunduki kwa ajili ya pembe na watumwa waliopatikana ukandani. Bidhaa nyingine za anasa ziliingizwa katika ikulu ya Buganda. Hatimaye Ikulu ya Buganda ilipendelea bidhaa za nje na hii baadaye ilichangia sana katika kutawaliwa kwake.

## *Kukua kwa tofauti na wasiwasi*

Kufikia robo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa tofauti nyingi na wasiwasi zilijitokeza katika ukanda wa maziwa ambao ulifanya watu, wanyonge na wenye nguvu, kuomba msaada wa Wazungu pale walipoanza kuingia kwenye ukanda. Kupatikana kwa bunduki kwa nyingi ya nchi zenye nguvu sana kulizidi kuwaongezea nguvu za kijeshi na kuwa na kauri kubwa katika mahusiano yao na jirani zao wanyonge. Hii iliongeza zaidi hali ya kutokuwepo usawa kama ilivyojionyesha katika

kunyonywa kwa wanyonge, na misafara ya kukamata watumwa iliyofanywa na watu wenye nguvu zaidi. Kulikuwa na wimbi jipya la upinzani na machafuko mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, wakati makundi fulani yalipojaribu kuwang'oa watawala wa dola kuu za ukanda wa Maziwa. Nguvu iliyokuwa ikizidi kukua iliyojijenga kwenye miji mikuu ya kanda ilianza kuleta wasiwasi katika miongo mitatu ya mwisho ya karne. Watu wa kawaida katika Bunyoro, Rwanda na Busoga walipinga mahitaji yaliyopita kiasi ya wafalme wenye nguvu kwa kuondoka majumbani kwao au kwa kujenga makao yao kama ngome.

Katika robo ya pili ya karne ya kumi na tisa katika Busoga, watu walikuwa na mtazamo mpya kuhusu nchi. Tabia ya watu kuwa tayari kuhama na kuacha ardhi yao kulidhoofisha mamlaka ya nchi. Hivyo, wakati mji mkuu ulikuwa ukijikusanyia silaha zaidi, watu walikuwa wakijikwamua kutoka kwenye aina yo yote ya sheria ambayo nchi ilikuwanayo juu yao kwa kuhama ili kutafuta nafasi za kuvutia zaidi mahali pengine.

Upinzani uliolekezwa, kwenye mamlaka za kisiasa imara katika karne ya kumi na tisa, ulihusu pia kuzidisha mamlaka ya taasisi za kidini hata kama ni kwa muda mfupi. Hivyo taasisi za kidini zilianza kukua na kuvutia walezi na hii iliathiri taasisi za kisiasa. Kwa mfano, katika eneo la Bunafu la Busoga, kulizuka tapo la kidini lililotokana na mtoto aliyepagawa aliyeitwa Womunofu. Pia katika Rwanda, Bunyoro na kusini-magharibi ya Uganda kulikuwa na matapo ya kidini yaliyoitwa *kubandwa* yakitokana na mungu wa kike aliyeitwa Nyabingi. Mara nyingi matapo haya yalikuja kutoa upinzani kwa mamlaka za kisiasa kama ilivyotokea Rwanda. Baadaye, yalitumiwa katika ukanda huo, kama chanzo cha upinzani dhidi ya ukoloni wa Ulaya.

## *Hitimisho*

Katika karne ya kumi na tisa ukanda wa Maziwa Makuu ulikuwa ni uwanja mkubwa wa ugomvi na mapambano baina ya makundi na nguvu tofauti. Ugomvi huu ulikuwa na viwango viwili. Katika kiwango kimoja, nchi zilishindana ili kumiliki zana za kilimo na rasilmali maalum, kama chumvi, ng'ombe na chuma. Pia walishindana kuweza kumiliki mifumo ya biashara.

Kwa kiwango kingine, watu binafsi walijitahidi kulinda maeneo yao ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Lakini katika karne ya kumi na tisa, utawala katika ukanda huu ulikuwa umejihusisha zaidi katika kuwanyonya watu bila huruma kuliko katika kulinda manufaa yao. Hii ilisababisha matokeo tofauti kutoka kwa watu kutokana na mipaka na nafasi yao. Wengine walihamisha uzalishaji na uuzaji mbali na mahitaji ya utawala, wengine waliacha sehemu zao kama aina ya upinzani dhidi ya shinikizo la utawala lililokuwa likiongezeka, wengine walitafuta usalama kwa kuingia jumuia za kidini ambazo kwa kuzitumia waliweza baadaye kujitahidi kuuangusha utawala wa kisiasa uliokuwepo. Kwa hiyo, watu katika ukanda wa maziwa makuu walijitahidi mara nyingi katika karne ya kumi na tisa kubadili

msimamo wao kwa utawala wa nchi, huduma za jamii, uzalishaji na uuzaji. Hatimaye, nchi hizi zilipitia mabadiliko muhimu katika uzalishaji, mabadilishano, uhusiano baina ya nchi na vile vile katika uhusiano kati ya dola na watawaliwa.

# 12 *Bondẹ la Kongo na Angola*

Sura hii inazungumzia eneo ambalo kwa upande wa magharibi linapakana na bahari ya Atlantiki, upande wa mashariki na safu ya milima ya Nili-Zaire, kaskazini na savana ya Ubangui, na kusini na uwanda unaotengamisha mabonde ya Zaire na Zambezi. Mada nyingi zitashughulikiwa katika historia ya sehemu hii kati ya 1800-1880. Zitajumuisha uzalishaji, biashara na siasa. Pia, tutaangalia hali ya maisha ya jumuia zilizokuwa katika eneo hili ili kuona ni mwendelezo upi na mahusiano ambayo jamii hizo ziliweza kuwanayo. Mabadiliko yaliyoletwa na karne ya kumi na tisa hasa katika nyanja za uchumi na pia ongezeko la athari zilizotokana na mabadiliko hayo kwenye historia ya kijamii na ya kisiasa itachunguzwa. Katika muktadha huu, sura hii itachunguza athari ya kushuka na kupanda kwa uchumi wa dunia katika sehemu hii ya Afrika ya Kati na hatua zilizochukuliwa na watu dhidi ya ushindani wa nje na wa ndani.

## *Uzalishaji: Miundo ya uchache na wingi wa idadi ya watu*

Jamii za Afrika ya Kati katika kipindi kinachozungumziwa zilionyesha kuendelea kwa baadhi ya taratibu zilizochukuliwa kutoka kwenye karne iliyotangulia katika kugawanyika kwa idadi ya watu, mifumo ya uzalishaji na matarajio ya kupata msingi wa uchumi wa jamii. Iliyokuwa muhimu zaidi ilikuwa mgawanyo wa idadi ya watu usio sawa uliosababishwa na hali tofauti za kijiografia, kiuchumi, kijamii na kihistoria.

Idadi ndogo ya watu ilikuwa kusini mwa msitu wa mvua na ambako, kutokana na udongo mbaya, ukulima ulikuwa wa kiwango cha chini. Mazao makuu yalikuwa nafaka za muda mrefu za Kiafrika, ulezi mwembamba na mtama. Kutokana na aina hii ndogo ya ukulima kushindwa kukidhi mahitaji ya watu ilibidi ukusanyaji wa chakula, uwindaji na uvuvi visaidie. Kwa kweli, vyanzo hivi vingine ndivyo vilivyotoa karibu chakula chote kilichotumika.

Sehemu zilizokuwa zimekaliwa na watu wachache zilikuwa na uhusiano na zile zenye watu wengi ambazo zilielekea kupunguzia watu waliozidi kwenye sehemu zilizokuwa na watu wachache. Maeneo yenye watu wachache na yale yenye watu wengi yaliungana; maendeleo katika upatikanaji wa maji na hivyo kuwepo sehemu zenye rutuba, au katika




**12.1** *Magharibi ya Afrika ya Kati kwenye karne ya kumi na tisa (Baada ya J.L. Vellut)*



**12.2** *Kijiji cha Umanyema; jimbo la kaskazini- Mashariki la Himaya ya Luba miaka ya 1870*

mbinu za kilimo au ulimaji wa mazao mapya kulisababisha ulimaji uliobobea na ongezeko la idadi ya watu. Kwa maneno mengine kuwepo kwa sehemu zenye idadi ya watu wengi katika Afrika ya Kati kulisababishwa na maendeleo au upanuzi wa kilimo. Kulikuwa na sehemu katika bonde la Lualaba na katika eneo la Kongo zilizokuwa na kilimo cha kizamani kilichobobea na katika karne ya kumi na tisa maeneo ya watu wengi yaliibuka huko Angola baina ya Wambudu na Wavimbundu. Katika Zaire, upenyu uliokuwa na watu wengi katika njia panda ya Misitu ya mvua na savana karibu latitudi 5% ya kusini haikuwa na mipaka hadi katikati ya karne ya ishirini.

Kuhusu maendeleo ya kilimo katika Afrika ya Kati, karne ya kumi na tisa iliwakilisha kilele cha mwelekeo uliokuwa umeanza karne chache zilizopita. Mwelekeo huo ulianza kwa kusambaa kwa ufuaji chuma katika karne ya kumi na tano miongoni mwa Wabantu. Hii ilisababisha mabadiliko kadhaa katika karne za kumi na saba na kumi na nane kama vile kutawaliwa kwa nchi mpya, kuanzishwa kwa nasaba mpya na upanuzi wa nguvu za kisiasa. Ilipofika karne ya kumi na tisa, maeneo yote yenye watu wengi yaliboresha ukulima wao kwa kuchukua mazao ya Kimarekani kama mahindi, mihogo, viazi vitamu na maharagwe. Kulikuwa na ongozeko katika uzalishaji kwa kuwa ardhi nyingi yenye rutuba ililimwa kishadidi zaidi.

Matukio yaliyoelezwa hapo juu pengine yalichukua zaidi ya karne mbili kutokea. (1600-1850). Ilipofika 1850, mazao ya Kimarekani yalienea sana na katika eneo la Kongo yalikwishazoeleka sana na hayakuonekana tena kama mazao ya kutoka nje.

## *Demografia, jamii na siasa katika sehemu zenye watu wengi*

Maendeleo ya jumuia zenye kilimo anuwai yalisababisha matukio muhimu katika demografia ya Afrika ya Kati. Hii ni kwa sababu tofauti na jumuia ambazo hatimaye zilikumbatia kilimo na kufuga wanyama na zile ambazo ziliwinda na kukusanya chakula, jamii zilizokuwa na kilimo anuwai zaidi zilikuwa na kiwango kikubwa cha ongezeko la watu. Hata hivyo, kiwango cha ongezeko la watu hata katika jamii hizi zenye kilimo changamano kilikuwa kidogo ukilinganisha na tarakimu za karne ya ishirini kwa sababu ya kiwango kikubwa cha vifo katika jumuia za aina hiyo katika karne ya kumi na tisa.

Mambo mengi yalisababisba kuwepo kwa kiwango kikubwa cha vifo. Kulikuwa na biashara ya utumwa na vurugu zake. Kulikuwepo pia na magonjwa ya mara kwa mara na milipuko ya magonjwa ya kuambukiza ambayo dawa za waganga wa kienyeji au wafanyabiashara kutoka Angola na pwani ya Waswahili ambao walikuwa na ufahamu wa dawa za Kizungu hakukufua dafu. Ingawa kukua kwa idadi ya watu katika karne ya kumi na tisa kulikuwa ni kwa kiwango cha chini kwa vipimo vya kisasa, idadi hiyo ilikuwa bila shaka yoyote imepiga hatua ukilinganisha na karne zilizopita. Idadi ya watu iliyozidi ilihamia kwenye maeneo yenye kuendesha kilimo anuwai zaidi. Hii ilisababisha kuwepo kwa jumuia zilizotulia ambazo hatimaye ziliyabadilisha mazingira mabaya na kuwa ya kufaa.

Maendeleo ya vitu na historia ya kijamii na kisiasa ya sehemu hii yaliathiriana. Katika baadhi ya sehemu, maeneo yenye idadi kubwa ya watu yalikua kwa misingi ya miundo ya siasa yenye mfumo wa katikati. Mifano ya aina hii ilikuwa Mangbetu na Zande katika Kusini-Mashariki mwa Zaire. Katika sehemu nyingine sababu za kisiasa zilichochea kukua kwa idadi ya watu ambako pia kuliongeza uzalishaji kama vile Burundi, Rwanda na kwa uzoefu wa Washi, katika karne ya kumi na tisa. Uhusiano huu kati ya vitu na watu haukuwa wa upande mmoja; uzalishaji wa ziada uliokuwa ukiongezeka ulileta ongezeko la idadi ya watu, na hii ilisababisha uzalishaji zaidi. Lakini hii pia inaweza wakati mwingine kusababisha kufifia kwa uwezo wa kisiasa kama ilivyotokea katika Zaire ya magharibi ambako ongezeko la idadi ya watu lilileta mabadiliko ya siasa kali katika muundo wa jamii.

Ongezeko katika uhamiaji lilisababisha kuwepo kwa jumuia yenye nguvu magharibi ya kitovu cha nchi ya Waluba katika karne ya kumi na tisa. Kila mhamiaji alisahau utambulisho wake na wote kujiona wamoja, hivyo kuleta uamsho wa kikabila kati yao. Uzoefu wao wa pamoja wa kihistoria uliwawezesha sana wao kujitambua, wakati shughuli za kibinafsi, ongezeko la idadi ya watu na uzalishaji wa kilimo vilibakia kuwa mambo muhimu ya uhai wa jamii. Pia Wachokwe wengi waliacha maskani yao huko Tshikapa ya juu na Kasaiya ya juu ili kuwinda na kukusanya chakula katika msitu wa wazi; pamoja na wanawake kadhaa wa Kilunda ambao walikamatwa kama watumwa. Wanawake wa Kilunda ambao walisimilimishwa katika jamii ya Kichokwe walifahamu jinsi ya kulima mhogo hata kwenye udongo mbaya na hivyo Wachokwe wakaingizwa kwenye kilimo.

## *Ushindi Dhidi ya Udongo Duni*

Kitu kingine muhimu katika karne ya kumi na tisa katika historia ya eneo linalozungumziwa ni ushindi dhidi ya udongo duni. Pamoja na ufugaji wa wanyama, hii ilirahisisha uanzishaji wa jumuia za watu katika sehemu kame sana, na kuongeza idadi ya watu katika baadhi ya maeneo yenye watu wachache. Mfano mmojawapo ni Angola ya kusini.

Angola ya kusini lilikuwa eneo lenye mchanga, kavu na lenye mvua isiyo na uhakika. Watu wa ukanda huu walichangia historia ya pamoja na hii ilileta mshikamano wa kikabila kati yao. Walitambulika kutokana na udongo wao na kuenzi kwao ukulima na uzalishaji wa wanyama. Wanajulikana kwa ujumla kama Waovambo, ambao katika yao kuna makundi mengi madogo madogo ya Wakwanyama, Wandongo, na Wakwambi. Kujaa kwa mto Cuvelai na kufurika kwa mbuga za nyasi katika baadhi ya maeneo ya Angola ya kusini kuliwezesha Waovambo kushinda ukame na kulilima eneo hili. Walitumia umwagiliaji maji na pia samadi ya wanyama mashambani mwao kama mbolea.

Usilimishaji wa wageni, hasa mateka waliochukuliwa katika mashambulio, katika nchi za jirani kulirahisisha kuleta badiliko la kuwa na ulimaji mkubwa kati ya Waovambo. Mazao makuu yalikuwa mtama na ulezi. Mimea ya Kimarekani kama karanga, maharagwe na mahindi pia yalilimwa lakini kwa kiwango kidogo. Uzalishaji ulidhibitiwa na mfalme ambaye aligawa ardhi na kupanga kazi za umwagiliaji.

Hivyo, ongezeko katika uzalishaji ulioletwa na ushindi dhidi ya udongo hafifu ulizidisha tofauti zilizokuwepo katika mgawanyo wa idadi ya watu. Kulikuwa na ongezeko la haraka katika idadi ya watu katika maeneo ambayo yalikuwa na ziada kutokana na ongezeko katika uzalishaji wa kilimo. Ovambo, Ovimbundu na Luba ni mifano ya sehemu hizo. Hii ina maana kuwa watu kutoka sehemu nyingine walivutwa kwenye kanda hizi za kilimo, hivyo kuyaacha maskani yao ya asili bila watu. Kupungua huku kwa watu kulichangiwa pia na sababu za kiuchumi. Kwa mfano tabia ya ukusanyaji chakula ilikuza kutawanyika kwa watu kwenye msitu kwa kwenda kukusanya pembe, nta na vitu vingine. Aidha, uanzishaji wa vituo vya biashara katika mabonde ya mito ulileta watu mbalimbali pamoja na hivyo kusababisha wingi wa idadi ya watu.

## *Afrika ya Kati katika Uchumi wa Dunia Unaobadilikabadilika*

Uchumi wa Afrika ya Kati haukujihusisha na kazi za uzalishaji pekee kama ukulima, uzalishaji wanyama, uvuvi na ukusanyaji; bali pia ilikuwepo biashara, na umuhimu wake ulitegemea hali ya kihistoria. Kwa ujumla, matatizo ya uchukuzi yalipunguza vitu vya biashara vilivyohitajika sana kama chumvi, chuma na bidhaa za anasa kuwa vichache. Kwa upande mwingine, mazao ya kilimo hayakusafirishwa kwa masafa marefu.

Kukua kwa uchumi wa biashara ya kimataifa ambako kulianza katika karne ya kumi na sita polepole kuliathiri uchumi wa baadhi ya sehemu za Afrika ya Kati. Ilipofika karne ya kumi na tisa, kulikuwa na upanuzi wa biashara na Afrika ya Kati



**12.3** *Ngoma za kifalme za karne ya kumi na tisa kutoka kwenye falme ya Wakuba*

ikajihusisha zaidi katika biashara duniani kote. Bidhaa muhimu iliyosafirishwa kote duniani ilikuwa watumwa. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1850 bidhaa nyingine kama vile pembe, nta, sandarusi, mafuta na kahawa zikaanza pia kusafirishwa. Katika kipindi cha karne ya kumi na tisa kulikuwa na ukuaji mkubwa wa soko la biashara la Afrika ya Kati.

Namna mitandao ya biashara na mawasiliano ilivyofanya kazi ndani ya bara la Afrika iliamua wingi wa bidhaa za Kiafrika zilizofika kwenye masoko ya dunia. Mitandao hii ilionyesha kanda kuu za kiuchumi zilizokuweko Afrika ya Kati katika karne ya kumi na tisa licha ya mipango ya kisiasa na kiuchumi iliyokuwepo kwenye ukanda huu.

Kila moja ya kanda hizi mpya za uchumi ilikuwa na historia yake na vilevile hali ya kisiasa na kijamii iliyokuwa pekee. Matakwa ya biashara ya nje yalitawala katika kanda hizi. Hali ya kawaida miongoni mwa kanda hizi tofauti ni kuwa kila moja ilifanikiwa kubadilisha vipengele muhimu vya mfumo wa zamani wa uchumi wa Kiafrika, ukiunganika kidogo tu na uchumi wa dunia.

## *Kanda za kiuchumi na mitandao ya kibiashara*

Katika kipindi cha 1800-80 kulikuwa na kanda kuu za uchumi nne katika Afrika ya Kati. Mbili kati ya hizi zilitawaliwa zaidi na wafanyabiashara wa Kiislamu, na kanda nyingine mbili zilijihusisha na vituo vya wafanyabiashara wa Kizungu katika pwani ya Atlantiki.

Mtandao wa biashara wa kwanza ulikuwa na Waarabu/Wasudani uliokuwa kaskazini-mashariki ya Afrika ya Kati ambao ulijumuisha vituo vya wafanyabiashara kutoka Kairo, Bahari ya Shamu na Khartoum. Mtandao huu ni matokeo ya kibiashara na kijeshi ya Wamisri katika Sudan na Darfur. Wafanyabiashara wa Kimisri, Kikoptiki na Kizungu waliohusika na mtandao huu walijenga ngome ambazo walizitumia kama vituo wakati wa kubadilishana bidhaa. Mtandao huu wa Kisudani ulikuwa na sifa muhimu. Mojawapo ilikuwa tofauti kati ya biashara ya taifa na ile ya binafsi. Nyingine ilikuwa utumiaji wa nguvu kukamata watumwa na kuvamia pembe, na sera ya kuendeleza mashamba makubwa, hasa yale ya pamba, ili kufanikisha mahitaji ya kibiashara.

Kanda ya kibiashara ya pili ilikuwa mtandao wa Waswahili ukiwa na vituo kwenye bandari katika pwani ya Waswahili na katika sehemu nyingine za Bahari ya Hindi kama vile Zanzibar na Bagamoyo. Njia za Waswahili zilikuwa katika vikundi vikubwa viwili. Kimoja kilipitia Unyanyembe katikati ya Tanzania ya leo, kikivuka Ziwa Tanganyika. Kingine kiliunganisha kanda ya Luapula-Moero kwa kupitia aidha Ziwa Malawi au kusini-magharibi ya Tanzania. Mtandao huu wa biashara uliendeshwa na misafara midogo ambayo iliishia katika makao ya watemi maarufu. Pia ilikuwa chanzo cha makazi ya jumuia ya wafanyabiashara kuanzia miaka ya 1870, kwa mfano yale ya Tippu Tip ambayo yalianzishwa huko Kasongo mwaka 1875. Muhimu zaidi, ilikuwa ni kwa kupitia mtandao huu ambapo nchi ya Waswahili ilikuwa kituo kilichotumiwa na wakoloni kuingia katika upande wa mashariki wa Afrika ya Mashariki.

Kanda ya tatu ilikuwa kanda ya biashara ya mto Zaire iliyokuwa inakumbatia vituo




**12.4** *Magharibi ya Afrika ya Kati: Zoni za biashara 1880 (Baada ya J.L. Vellut)*

vya biashara vya Kidachi, Kifaransa na Kiingereza katika mto wa Zaire wa chini na pembezoni mwa pwani ya kaskazini ya Angola. Kanda hii ilipata vitu kutoka kwenye biashara ya Kongo na pia biashara ya mtoni. Biashara ya mtoni ilianza katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa na punde ikawa bora kuliko njia za zamani za nchi. Vikundi vilivyokuwa vikiishi kandokando ya mto viliitawala biashara hii ya mtoni. Vilikusanya pembe na watumwa kutoka bara na kuwachukua kupitia mtoni hadi katika masoko ya Tio huko Pool. Vilianzisha vituo vya biashara na kuanzisha bidhaa mpya kama bunduki, pete za shada na aina mbalimbali za mazao katika mikoa ya misitu ya mvua. Vituo vya biashara vilikuwa na wafungwa, wakimbizi na makundi mengine ambayo yalifanya idadi ya watu ifurike. Vituo vilivyokuwa na watu wachache kwa namna nyingine pia viliweza kukua kupitia watu binafsi ambao walitajirika kutokana na biashara.

Mtandao wa mwisho kabisa ulikuwa wa Kireno/Kiafrika ambao ulikuwa wa zamani na mkubwa kushinda yote katika Afrika ya Kati. Katika karne yote ya kumi na tisa njia hii ilipitia mabadiliko mengi. Katika nusu ya kwanza ya karne, njia kuu zilielekea Luanda na Benguela. Njia nyingine iliunganisha miinuko ya Ovimbundu hadi pwani. Katika 1840 falme za Lozi na Luanda ziliingizwa kwenye mtandao huu. Hata hivyo katika nusu ya pili ya karne hii mtandao huu ulikua sana. Njia mpya iliunganisha Malanje na mji mkuu wa Muant Yav. Jozi nyingine za njia ziliwachukua wafanyabiashara wa Kiafrika wa Ambaka hadi bonde la Lulua katika mkoa wa Luba na pia kwenye masoko ya Kuba. Huko Kuba, walipata ushindani kidogo kutoka kwa wafanyabiashara wa Ovimbundu.

Vituo hivi vya biashara kwenye njia tofauti vilitimiza mambo muhimu. Kazi hizo zilihusu pia kuwapa wafanyabiashara mkopo, kutoa maeneo ya kuhifadhi mali, kutoa na kuwapatia nyenzo misafara ya biashara. Vituo muhimu katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa vilikuwa Luanda na Benguela hali Mocamedes ilipata umaarufu katika nusu ya pili ya karne hii. Utamaduni wa Kikrioli na wa Kiafrika ulishamiri sana katika sehemu ya Wareno katika Luanda. Kulikuwa pia na nafasi ya kujiendeleza kijamii na nafasi nyingi za kujilimbikizia mali. Ilipofika 1850 kusema kweli Luanda, ilikuwa kubwa kuliko vituo vyote vya Angola vilivyokuwepo bara. Vituo vingine kama Dondo, Pungo, Andongo, Caconda na hata Bie vilikuwa vituo muhimu katika mtandao. Miji mikuu ya temi ndogo ndogo au masoko ya jumuia ambayo hayakuwa na mfumo wa kitovu yalikuwa ndiyo moyo wa mtandao ambamo mabadilishano yalifanyika.

Chini ya mfumo huu wa mtandao, kulikuwa na tofauti zilizokuwa zikiongezeka kati ya vituo vikubwa ambavyo vilihusika na mapato mengi yaliyosababishwa na shughuli za sokoni na vile ambavyo vilikuwa na nafasi chache za kupata mali. Katika sehemu zilizokuwa na bahati zaidi vitu kama silaha, nguo na watumwa wa nyumbani vilikuwa vingi, lakini vichache katika sehemu nyingine. Katika nyakati za kukua kwa uchumi sehemu kubwa ya biashara ya bara ilifanywa na Waafrika, lakini katika wakati wa hali mbaya ya uchumi Wareno walijitahidi kuhodhi faida yote kwa kuwatoa wafanyabiashara wa kati wa Kiafrika kwenye biashara.

Mtandao huu wa Kireno/Kiafrika ilibidi pia uende sawa na mizunguko mikuu



**12.5** *Mfalme Munza wa Mangbetu 1870*



**12.6** *Kazembe 1831*

**12.7** *Mwanamke wa Kimbundu wa tabaka la Kiteni na mjakazi wake, katika miaka ya 1850*

**12.8** *Kimbundu na mwanake wa tabaka la Kiteni katika miaka ya 1880*







**12.9** *Pembe iliyochongwa ya katikati ya karne ya kumi na tisa kutoka pwani ya Loango ya Congo/Angola, ikionyesha matukio ya biashara na ya Wazungu*

kadhaa ya biashara katika karne ya kumi na tisa. Ilipofika mwaka wa 1840 kazi muhimu zaidi ilikuwa biashara ya watumwa. Brazil ndio iliyokuwa inaingiza watumwa kwa wingi, ambao walitumiwa kwa kupanua uchumi wa uzalishaji kahawa. Ilipofika mwisho wa mwaka 1860 usafirishaji wa watumwa ulikuwa umekwisha kabisa na kwa sehemu ya karne iliyobaki, kahawa, sukari, nta, pembe, ambari, mawese na mpira asilia vilisafirishwa badala yake.

Mwisho, kukua kwa kanda kuu za uchumi za Afrika ya Kati kulizidisha uonevu katika jamii. Kanda zote za biashara zilipendelea ukuaji wa aina fulani ya uzalishaji uliotegemea nguvu kazi ya watumwa. Sio kwamba kabla ya karne ya kumi na tisa watumwa hawakutumika kwa uzalishaji, isipokuwa katika karne hiyo nguvu kazi ya watumwa ilikuwa katika kiwango kikubwa kwani bidhaa zilizotengenezwa nao zilikuwa na soko kubwa. Hata hivyo, utumiaji wa watumwa wa nyumbani ulileta upanuzi wa kilimo ambao nao ulisababisha kukua kwa idadi ya watu katika baadhi ya jumuia za kanda hii. kama vile Wakongo, Waovimbundu na Waovambo. Utumiaji wa nguvu kazi ya watumwa uliendelea hata katika jamii ya kikoloni ya Angola. Ingawa utumwa ulisimamishwa rasmi Angola mwaka 1878, nguvu kazi ya watumwa iliendelea kukuza uchumi wa mashamba. Kwa kweli, ilipofikia mwaka 1880, pombe iliyotengenezwa Angola kwa kutumia miwa ilikuwa bidhaa muhimu ya Wareno. Jinsi watu weupe walivyoanza kukaa katika eneo hili ndivyo utumwa ulivyozidi kuhitajika.

## *Ubepari wa Wareno Angola*

Baada ya kuangalia kanda kuu za biashara katika Afrika ya Kati, pamoja na uhusiano wao na uchumi wa dunia, tupo katika nafasi nzuri ya kufahamu historia ya maslahi ya nchi za nje na matukio katika ukanda huu kwenye karne ya kumi na tisa. Hakika inawezekana kutambua hatua kadhaa katika upanuzi na kunywea kwa himaya za Wareno katika Angola kwenye kipindi cha karne hii. Kunywea na kupanuka huku kulionyesha kubabaika kwa magavana wa Kireno kwenye koloni hili kuhusu sera ya kufuata ili kuhodhi uchumi wa biashara ya Kiafrika. Kwa upande mmoja kulikuwa na wazo la kuhodhi biashara kukiwa na lengo la kukuza biashara huru na Waafrika, na kwa upande mwingine kulikuwa na sera ya kuunganisha makoloni ya Afrika katika mfumo wa kiuchumi wa Wareno, ambapo makoloni yatatawaliwa kama majimbo ya Ureno yakiwa na jumuia ya masetla weupe. Njia hii ya pili pia ilihusisha kuwajenga wafanyabiashara wa kikoloni dhidi ya wafanyabiashara wa kati wa Kiafrika. Kutokana na ukweli kuwa Wareno walishindwa kuamua kati ya haya mawili wachukue lipi ili kuhodhi biashara ya Kiafrika katika Angola kwenye karne ya kumi na tisa, kulikuwa na mabadiliko kidogo kwa sera zote mbili. Mambo mengine kama vile hali ya uchumi ya Ureno, upinzani wa kijeshi wa Waafrika, tabia za magavana wa Kireno, na hali ya uchumi wa dunia pia yalichangia kuporomoka kwa sera ya ubepari wa Kireno katika Angola.

Ubepari wa Kireno katika Angola ulianza na sera ya kuyashirikisha kabisa makoloni ya Kiafrika. Hii iliendelea hadi 1860 wakati Wareno walipoanza kujitoa baada ya kushindwa kijeshi na Waafrika. Ilipofika mwanzoni mwa miaka ya 1870

kujitoa huku kukakamilika. Nguvu za kikoloni zilikuwa pwani tu na wafanyabiashara wa Kiafrika kwa haraka walikuwa wakidhibiti biashara. Kati ya 1867 na 1873 Angola ilishuhudia kukua kwa haraka kwenye biashara.

Mara baada ya hili, Wareno wakaanza kufufua sera yao ya upanuzi wa nchi pale dola za kigeni zilipoanza kuonyesha kuvutiwa na Angola. Wareno walianza kujenga reli kutoka Luanda kwenda bara; walifanya makubaliano kadhaa ya kidiplomasia na pia wakaanza kuingia bara kwenye jitihada yao ya kuondoa tishio lililoletwa na wageni Afrika ya Kati.

## *Jamii na Mamlaka Katika Afrika ya Kati (1800-80)*

Kulikuwa na aina mbili za mfumo wa siasa katika Afrika ya Kati katika muda unaozungumziwa. Mmoja ulikuwa utawala msonge, mfumo ambao ulipangwa vizuri chini ya misingi wa upokeaji wa ushuru, mwingine ulikuwa aina ya serikali isiyokuwa rasmi iliyoundwa na baraza la wazee na watu mashuhuri. Kwa vitendo, katika vipimo tofauti, vipengele vya mifumo hii miwili viliweza kuonekana pamoja katika jumuia nyingi. Kipengee kipi kati ya hivi kilishamiri zaidi katika jamii moja moja ni hali iliyotegemea mambo kama vile hali ya mazingira, idadi ya watu, aina ya kazi za uchumi, hali ya kihistoria na upendeleo binafsi wa viongozi.

Kulikuwa na mifano kadhaa ya jamii zenye mfumo wa utawala msonge wa kudumu na miji yao mikuu ikiwa na idadi kubwa ya watu. Lakini jamii hizi zilikuwa chache kwa sababu mambo fulani hasa ya kiuchumi yalikuwa lazima yawepo kabla ya hali hiyo kutokea. Miongoni mwa mambo hayo ilikuwa sekta imara ya kilimo, kuchukua kodi katika uzalishaji wa vifaa muhimu kama chumvi, shaba na chuma, ukusanyaji wa ushuru kutoka kwenye nchi zilizoshindwa kwenye vita na kutoka kwenye biashara. Nguvu za watemi zilitegemea sekta za uchumi katika jamii, kukua au kudidimia kwa sekta yoyote kati ya hizi kungeathiri uwezo wa nchi. Tukio muhimu katika jumuia hizi katika karne ya kumi na tisa lilikuwa kuongezeka kwa nafasi za jamii kujiendeleza ambapo watu hodari waliweza kukwea na kufikia nafasi ambazo kabla ya hapo zilishikwa na watemi pekee. Nguvu za watemi ziliongezeka, lakini upanuzi wa biashara ulikuwa mara nyingi chini ya uwezo wa mali waliyokuwanayo watawala.

Kulikuwepo pia na aina ya nguvu za kimila kama inavyoonekana katika mambo ya ofisi na hirizi zilizotengenezwa dhidi ya maadui waliotarajiwa kutoka ndani na nje ya jumuia hizi. Hata hivyo, uhusiano kati ya kiwango cha nguvu za kimila na kudidimia kwa hali nzuri ya uchumi na kijeshi katika jamii ni jambo linalohitaji uchunguzi zaidi.

## *Jamii zilizoongozwa Kidola*

Moja ya dola za zamani ambazo zimeendelea hadi karne ya kumi na tisa ilikuwa nchi ya Kilunda ya Kalagne na itakuwa kama mfano wa nchi yenye mfumo wa mamlaka katika sehemu moja. Ilifikia kikomo cha ufanisi hata katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa na kuanza kudidimia katika miaka ya 1870. Cheo kikubwa kabisa cha kisiasa



**12.10** *Kinyago cha Chibinda Ilunga mwanzilishi mkumbukwa wa ufalme wa Lunda. Kinyago hiki kinadhaniwa kuwa ni cha karne ya kumi na tisa*

miongoni mwa Walunda kilikuwa Mwant Yav. Mmojawapo wa watawala wakuu wa Kalagne katika karne hii alikuwa Mwant Yav Nawey (1820-52). Alikuwa mwenye tamaa ya makuu, akiogopwa na watu, na aliongeza mamlaka ya ofisi yake kwa kiasi kikubwa. Ilikuwa ni wakati wa enzi yake ambapo bunduki ziliingia Lunda. Alijaribu kuweka uhusiano mzuri na Wachokwe ambao aliwaruhusu kuingia mji wake mkuu. Jambo lingine muhimu la utawala wa Nawey lilikuwa kuongezeka kwa haraka kwa biashara ya masafa marefu na Waimbangala, Waovimbundu na Wamanbari.

Licha ya kuwa biashara ya masafa marefu ilisitawi chini ya utawala wake, Nawey alikuwa na sifa mbaya kwa wafanyabiashara. Baada ya kifo chake katika mwaka 1852, alirithiwa na kaka yake Mulaj kama Mwant Yav mpya, lakini utawala wake uliharibiwa na migogoro ya ndani. Mambo yalirudia hali ya utulivu katika utawala mrefu wa Muteba (1857-73). Hali ya amani katika utawala huu iliendeleza sana biashara. Wakati biashara ikisitawi katika utawala wa Mwant Yav Muteba, makundi ya wasafiri wa Kimbudu yaliruhusiwa kukaa kwenye mji wake mkuu. Moja ya makundi hayo liliongozwa na Lourenco Bezzerra aliyejulikana na Walunda kwa jina lake la utani, Lufuma, ambaye baadaye alikuja kuwa mtu mwenye mvuto katika kitala cha Walunda. Kundi likaanzisha ukulima wa Kimbundu na uzalishaji wa wanyama katika ukanda, na mimea iliyotoka nje kama vile mpunga, mahindi na tumbaku ikaanza kulimwa mashambani. Wambundu pia walitumika katika nchin ya Lunda kama mafundi stadi katika nafasi mbalimbali . Hivyo, katika kipindi cha 1800-80 shughuli za biashara katika eneo hili zilimilikiwa na watawala wa Kilunda na wafanyabiashara wa Angola ambao waliingia na kukaa katika eneo hili kutokana na ndoa na mahusiano mengine ya kiuchumi. Lufuma na kundi lake waliondoka nchi ya Walunda na kwenda nchi ya Maiange na hawakurudi tena.

Wakati huohuo, kutawanyika kwa Wachokwe kutoka kwenye vijiji vyao na kuja kwenye nchi hii iliyo kati ya mto Tshikapa na Kasai kuliendelea katika miaka ya 1870 na hatimaye wakawa na nguvu ya kutosha kuwazidi watemi wa Kilunda. Kuanguka huku kwa mamlaka ya Walunda kulizidishwa zaidi na migogoro ya ndani. Wachokwe walimsaidia mtemi mmoja kushika madaraka kama Mwant Yav Mbumba. Naye aliendelea kuwategemea Wachokwe kuzuia Walunda wengine wasishike madaraka. Alifariki 1883 baada ya utawala wa nguvu , na Wachokwe walichukua utawala na kumtawaza mmoja wa watoto wa Mbumba ambaye alichukuliwa na kulelewa na familia moja ya Kichokwe.

## *Tawala za watemi na kusambaratika kwa madaraka*

Ukiacha nchi zenye nguvu kama vile nchi ya Kilunda ya Kalagne kulikuwepo na sehemu nyingine ndogondogo katika eneo tunalolizungumzia. Jumuia hizo ndogondogo zilikuwa, kwa hali fulani, ni matokeo ya nchi zilizovunjika na hazikuwa chini ya mamlaka moja licha ya kuwa na utamaduni mmoja. Katika hali nyingine, ambapo nchi hazikuvunjika kabisa, kulikuwepo na mwelekeo wa kugatua madaraka na kuvunjika ambako kulisababisha watemi kupoteza mamlaka yao.

Mfano mmojawapo wa njia hii ya mvunjiko kwa mamlaka unaonekana katika nchi



**12.11** *Mwant Yav Mbumba*

iliyopo kusini mwa miinuko ya Ovimbundu katika Angola ambako hapo awali kulikuwa na falme maarufu ambapo baadaye zikavunjika na kuwa tawala kubwa kubwa zilizotawaliwa na watemi. Mojawapo ilikuwa falme ya Wanyaneka ya Mwila ambayo ilitawala kanda hii kwenye karne ya kumi na nane lakini ikavunjika katikati ya karne ya kumi na tisa. Temi zilizoirithi zikaja kuwa vituo vya kibiashara kwa ajili ya mishumaa, pembe na mifugo, ikihudumia kusini ya Angola yote katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa. Kuanguka kisiasa kwa kanda hii kulisababishwa na vikosi vya ushambulizi na utekaji nyara vya majasiri.

Mfano mwingine wa mvunyiko huu ulikuwa wa ufalme wa Luba ambao ulikuwa na eneo kubwa sana. Katika kilele cha umaarufu wake kwenye nusu ya karne ya kumi na tisa nchi zenye nguvu za Waluba zilitawala temi ndogondogo. Kuingiwa kwa eneo hili na misafara ya kibiashara kutoka kwenye eneo la Waswahili na Angola kulizidisha migogoro ya ndani kwa ndani nchini humo. Ilipofika 1880 nchi za Waluba na temi zote zilikuwa tayari huru na mamlaka yakawa yametawanywa.

## *Majasiri, wafanyabiashara: mabwana wapya*

Jambo muhimu la historia ya karne ya kumi na tisa ya ukanda unaozungumziwa lilikuwa kutokea kwa aina mpya za mamlaka. Katika sehemu nyingine, nafasi ya watemi haikuwa muhimu na katika nyingine, upanuzi wa biashara uliwafanya baadhi ya watu binafsi jasiri au vikundi kuwa kileleni kama watemi. Mifano ya aina hii inaonekana kote Afrika ya Kati. Kwa mfano, katika msitu wa mvua wa bonde la kati linalotokana na mto wafanyabiashara kadhaa wa mitumbwi katika kingo za mto Zaire walitajirika kutokana na biashara ya watumwa, wakalimbikiza silaha na kujenga kituo cha biashara. Mfano unaojulikana zaidi wa jambo hili ulikuwa, kwa hakika, kukua kwa falme ya Msiri. Mfuatano wa matukio ulianza kwa safari za biashara kutoka Tanzania hadi bonde la Luapula na nchi jirani. Wafanyabiashara hawa walivutiwa zaidi na pembe na shaba ambazo zilipatikana kwa wingi katika eneo hili. Mwaka 1855, mtoto mmoja wa wafanyabiashara hao, Ngelengwa Mwenda, alikaa katika nchi ya mtemi Katanga, ambayo ilikuwa kituo kikubwa cha uzalishaji wa shaba.

Mwenda aliweza kuwa na jeshi kubwa lenye silaha za kutosha ambalo lilifanikisha kukaa kwake kwenye eneo teule. Alivutia watu wengi kwenye makazi yake na akaingilia migogoro ya kisiasa ya watemi wengine kandani; akigonganisha kundi moja dhidi ya lingine. Ilipofika 1880, akawa ameanzisha nchi yake mwenyewe na Buukenya ukiwa mji wake mkuu. Pia alichukua jina la `Msiri' akimaanisha anayemiliki ardhi.

Ufalme wake ulijihusisha sana na mitandao ya kibiashara ukandani. Ulisafirisha bidhaa kutoka Zanzibar hadi Benguela na kutoka nchi ya Waluba hadi kwenye vituo vya Kireno katika Msumbiji au Waarabu waliokuweko Ziwa Nyasa . Ilikuwa kama vile bohari ya kusafirishia. Kama mtawala, Msiri hakuwa tu mkarimu, bali hakuwa na huruma - kizazi halisi cha wakati wake.

## *Hitimisho*

Kutokana na melezo yaliyopita ni wazi kuwa taratibu za kulimbikiza mali zilibadilishwa katika karne ya kumi na tisa kutokana na kukua kwa sehemu zenye idadi ya watu wengi, maendeleo katika uzalishaji unaotokana na kilimo na katika kazi za mikono kadhaa na upanuzi wa haraka wa baadhi ya sekta za uchumi. Biashara ilikua kutokana na hali halisi iliyokuwepo na ilichangia katika mwanzo wa matabaka katika jamii nyingi.

Pia katika karne husika ofisi ya siasa za asilia ilizidi kushikwa na majasiri ambao ama wameiteka biashara na msingi wa uchumi wa nchi au walianzisha msingi mpya wa mamlaka ili kuondoa ule wa zamani. Nafasi ya mtemi ilikuwa isiyotabirika katika karne hii. Aidha kulikuwepo na baadhi ya temi zilizokua bila uunganishaji wa mamlaka kutoka sehemu moja. Hata hivyo, kusambaratika sio wazo kuu lililotawala historia ya Afrika ya Kati miaka ya 1800 - 1880. Mipaka haikuwa ikitambulika kutokana na nguvu za kisiasa, au kikabila kama hapo zamani, bali kwa nguvu za kiuchumi kama tulivyoona katika kanda kadhaa za kiuchumi kwenye eneo hili.

# 13 Kipindi cha mvuvumko wa Misri, 1805-81

## *Mjongeo wa taifa la Misri*

Kinyume na maoni yaliyoenezwa na historiografia ya kikoloni, kuibuka kwa utaifa wa Misri hakukutokana na Msafara wa Wafaransa ulioongozwa na Napoleon, au jitihada za Waingereza za kuwang'oa Wafaransa. Msafara huu ulilengwa dhidi ya maslahi ya Waingereza, lakini Wamisri waliuchukulia kuwa ni uvamizi. Itikadi ya kimapinduzi ya Ufaransa na sifa za kitaaluma za utafiti wa Wafaransa uliochapishwa baadaye kwenye chapisho mashuhuri *Description of Egypt* (Maelezo ya Misri), havikuwa na ushawishi kwa Wamisri wa zama hizo. Wakati ambapo watu wa matabaka ya chini - wachuuzi, wachukuzi wa mitaani, mafundistadi, waongoza punda, watunza farasi, makuwadi na malaya walijihisi kuwa wamekombolewa, watu mashuhuri na wa matabaka ya kati walipambana na vikwazo vingi vya kiuchumi kutokana na kuzuiliwa kwa maduhuli na mahuruji (bidhaa zinazoingia na zinazotoka).

Mizizi ya utaifa wa Misri inarudi nyuma zaidi, na karne ya kumi na nane yapaswa kuonwa kama maabara ambamo Misri mpya ilitungwa. Maelemeo matatu katika karne ya kumi na nane yaliashiria mwelekeo huu. Kwanza, ni mageuzi ya watu kama vile Ali Bey al-Kabir yaliyojaribu kupunguza idadi ya miundo ya kikabaila iliyodhibitiwa na Mamluki katika delta ya Misri ya Chini. Kisha kulikuwepo na vuguvugu la uhuishaji katika Uislamu lililoongozwa na Sheikh Hassan al-Attar; na tatu, kuibuka katika majiji ya Kairo, Aleksandria na mengineyo, kwa kikundi cha watu mashuhuri, wasomi na wafanyabiashara, waliotajirika hasa kutokana na ardhi, na waliokuwa tayari kutoa rasilimali zao kuendeleza kile kichokuja kujulikana kama "juhudi ya kitaifa."

Yote haya yaliungana na mambo mengine na kuzaa vuguvugu la kitaifa la Misri lililokuwa na athari kubwa iliyoenea kote. Vuguvugu hilo lilipelekea kwenye maasi mawili ya Kairo ya 1798 na 1800 yaliyoongozwa na watu mashuhuri wa Misri. Uhamishwaji wa jeshi la wavamizi wa Kifaransa mwaka 1801 ulitoa nafasi kwa vuguvugu la kitaifa la Misri kujiimarisha na kutaka kujitawala ndani ya himaya ya Kituruki. Kwa maneno mengine, maasi ya Kairo, ambayo yalidhoofisha uwezo wa Wafaransa, yaliimarisha uongozi wa wenyeji. Hata hivyo, hadhi ya Misri kunako 1805 bado ilikuwa ile ya jimbo la himaya ya Kituruki. Sifa muhimu za uanzishwaji wa dola lenye nguvu hata hivyo zilikuwepo, yaani mamlaka kuu yenye jeshi imara na madaraka




**13.1** *Himaya ya Misri ya Muhammad Ali )1804-49) (Baada ya A. Abdel-Malele)*

halisi yenye kuwakilisha matabaka yote ya kijamii katika jamii ya Misri. Kilichokosekana ni uongozi imara na wenye kuelewa haraka ambao ungetumia kwa werevu hali ya mambo iliyokuwepo kwa faida ya Misri. Hivyo mambo yote yalikuwa tayari kwa ajili ya mzinduko mpya nchini Misri endapo ungeibuka uongozi uaofaa.

Muhammad Ali na Ismail

Wazo la Misri huru vilevile halikutoka kwa Muhammad Ali. Kabla hajajitokeza, "Jeshi la Makhufu" *(Coptic Legion)* la jumuiya ya "Ndugu Huru" ya Jenerali Yakub lilikuwa tayari limekwisha kulitangaza, lakini vuguvugu lao lilivunjika kufuatia kumalizika kwa Msafara wa Wafaransa na kuondolewa kwa kiongozi wao. Bila shaka Wafaransa walihimiza wazo la Misri huru kupinga utamalaki wa Waingereza. Hata hivyo, mawazo ya Muhammad Ali ya uhuru wa Misri yalitofautiana na yale ya Wamisri au Wafaransa. Lengo lake lilikuwa kuijenga Misri kijeshi, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni, na kuitumia kuchukua nafasi ya Uturuki iliyokuwa inafifia kama himaya mpya ya Kiislamu. Hivyo kampeni za Ali na mwanaye Ibrahim zililenga kuichomoza Misri sio tu kama nchi ya Kiafrika bali pia kama taifa la Kiislam na Kiarabu.

Baada ya kushika madaraka huko Misri, Ali alijizatiti kuimarisha nafasi yake na kulijenga taifa lake. Katika harakati hizo, kunako 1807 aliwashinda Waingereza ambao walikuwa wakifanya hujuma dhidi ya mamlaka yake. Kisha alikomesha athari za Mamluki katika Misri ya Juu, hasa kwa vile walikuwa wakishirikiana na Waingereza. Kunako 1811, aliwafutilia mbali viongozi wa upinzani wa Mamluki ambao walikuwa wakikwamisha juhudi zake za kupata mamlaka ya kisiasa katika Misri ya Chini. Baada ya kuwaondoa Mamluki, Ali alishughulikia ujenzi wa himaya na jukumu la ufufuaji wa taifa.

Itakuwa vema zaidi sasa kuchunguza dhana ya kujitawala kwa Misri ya Muhammad Ali na jinsi ilivyoendana na nafasi yake katika himaya ya Kituruki. Alitaka Misri kuwa taifa huru huku likiendelea kuwa sehemu ya himaya ya Kituruki. Kunako 1810, aliomba kwa siri msaada wa Ufaransa kwenye kitala cha Sultani imuunge mkono katika madai yake ya kutaka Misri ijitawale, na baada ya hapo alimwomba Sultan kuipatia Misri hadhi ya uhuru ndani ya himaya. Uvamizi wake wa kijeshi huko Arabia (1813-19) na Sudan (1820-23) hata hivyo ulimfanya akwaruzane na Waingereza ambao walihisi kutishwa kwa sababu alikuwa akijipenyeza kwenye maeneo ya mamlaka yao. Kwa hakika, kuongezeka kwa nguvu za Misri kuliwakera kabisa Waingereza. Misri yenye nguvu mpya ndani ya himaya ya Kituruki ingeibuka punde na kuimarisha himaya ya Waturuki, jambo ambalo Waingereza hawakutaka kabisa litokee.

Hali hii hatimaye ilipelekea kwenye vita mwaka 1827 kati ya Uingereza na himaya ya Kituruki ikisaidiwa na Misri. Jeshi la majini la Misri liliangamizwa katika mapambano hayo. Wakati huohuo, Ufaransa ilikuwa haiungi mkono tena Misri na Muhammad Ali alilazimika kutafuta urafiki wa Sultani wa Uturuki kwa ajili ya mpango wake wa kufufua himaya. Mpango wake ulikataliwa na Ikulu ya Sultani, na matokeo yake kukawa na mlolongo wa matukio ambayo hatimaye yalipelekea kwenye vita kati ya Uturuki na Misri. Ushindi wa awali wa jeshi la Misri lililoongozwa na Ibrahim, mwana



**13.2** *Muhammad Ali (mchoro wa Sir David Wilkie)*



13.3 *Ibrahim, mtoto wa Muhammad Ali na jenerali mkuu*

wa Muhammad, uliyashitua mataifa ya Ulaya ambayo yaliamua kumuokoa Sultani wa Uturuki. Hii ni kwa sababu walijua kwamba kama Muhammad Ali angeachiwa kuiangamiza himaya ya Kituruki na kuanzisha mamlaka yake, upanuzi wa ukoloni wao ungepingwa, na majimbo mengine ya himaya ya Kituruki yangehuishwa na kuimarishwa chini ya uongozi wake.

Zaidi ya hayo, Ibrahim alikuwa na mtazamo tofauti wa uhuru wa Misri ukilinganishwa na ule wa baba yake. Wakati ambapo Muhammad Ali mwanzoni alitaka uhuru wa Misri ndani ya himaya ya Uturuki, Ibrahim aliamini kwamba uhuru wa Misri ungekuwa na maana tu kama Misri ingechukua nafasi ya Uturuki na kuwa kitovu na kiongozi wa himaya ya Waarabu. Kusema kweli, Ibrahim alisisitiza umuhimu wa ufungamano wa Waarabu katika ujenzi wa taifa la Misri, yaani, kwamba Misri ilitakiwa kuwa kitovu cha ufufuo wa Waarabu. Mtazamo huu, hata hivyo, ulitoweka pamoja na Ibrahim baada ya 1840.

Ismail (1863-79), aliyerithi baada ya tawala fupi za al-Abbas na Said, aliona kuwa tatizo la kitaifa lilihusu uhuru na kujitawala kitaifa. Alibuni mkakati wa kupunguza utegemezi wa Misri kwa Uturuki kwa njia ya mazungumzo, ambapo baadaye angeifanya Misri iwe nchi huru na kisha angeanzisha asasi za serikali ya ndani. Kwa maneno mengine, Ismail alidhani kwamba njia za taratibu za kulishughulikia suala la uhuru wa Misri zingekuwa bora zaidi kuliko papara za kutumia nguvu. Ili kuimarisha nafasi yake, alianzisha mfumo wa kurithishana ufalme wa Misri, na pia akajipatia cheo cha *Khedive*. Zaidi ya hayo, alijitwalia haki ya kutangaza sheria za kiutawala na ya kujadiliana juu ya mipango ya kiuchumi na nchi za kigeni bila kulazimika kuidhinishwa kwanza na Sultani. Na mnano 1873 aliifasili Misri kama "taifa/dola."

Katika sera zake za kiserikali, Ismail alionyesha kuwa alitambua umuhimu wa kujenga taifa huru lenye nguvu kutokana na Misri, na kadhalika umuhimu wa kutafuta kutambuliwa kimataifa kwa taifa lake kwa kujipanua ndani ya Afrika mithili ya mojawapo ya mataifa ya Ulaya yenye makoloni yaliyokuwa yakiinukia. Kusema kweli upanuzi wa namna hiyo ndani ya Afrika mwanzoni haukupingwa na Uturuki wala Uingereza. Vyombo vya habari vya kiliberali (vinavyopendelea mabadiliko ya wastani) vya Ulaya vilisifu sana mafanikio ya kimiundombinu ya Misri, yaani, kundi la manowari lenye nguvu za wastani, ngome 18, huduma nzuri za simu na telegrafu na mwanzo wa ujenzi wa reli iliyopangwa kufika hadi Khartoum na Suakin.

Zaidi ya hayo, uingizwaji wa mtaji wa kigeni katika uchumi wa Misri baada ya 1840 ulizuia jitihada za Misri za kuwa na uchumi huru. Kwa kweli, ujenzi wa mfereji wa Suez ulikamilisha ujumuishwaji wa uchumi wa Misri katika mfumo wa dunia na ulipelekea moja kwa moja kwenye kumilikiwa kijeshi mnamo 1882. Hivyo Misri ililazimika kujihusisha na misukosuko ya uchumi wa kimataifa ambayo hapo awali ilijitenga nayo.

Utengukaji mwingine katika uchumi wa Misri ulisababishwa na maendeleo yasiyo na urari. Misri ya Chini (yaani, eneo la kaskazini) ilikuwa na maendeleo makubwa zaidi kuliko Misri ya Juu (ya kusini). Hii ilisababishwa na ukweli kwamba sehemu kubwa zaidi ya ardhi ya kilimo ilipatikana huko kwa sababu ya Delta ya Nile na hivyo kupelekea kwenye ukuaji wa miji mikubwa. Hivyo Aleksandria na Kairo vilikuwa vituo muhimu vya kibiashara vikiwa na tabaka la watawala wenyeji likijumuisha makabaila mashuhuri, wakati Misri ya Juu ilibakia kuwa bara ya pembezoni.

## *Kilimo na Matumizi ya Ardhi*

Kwa vile kilimo kinafungamana na matumizi ya ardhi, usimamizi wa ardhi lilikuwa suala muhimu. Kabla ya karne ya kumi na tisa, ardhi ilisimamiwa na *wamultazim* ambao jukumu lao kuu lilikuwa kukusanya mapato yaliyohitajika toka kwenye vijiji vyao na kuyapeleka hazina kuu. Hata hivyo, madaraka waliyokuwa nayo *wamultazim* juu ya ardhi yalionekana kwamba yangekwamisha maendeleo ya Misri kama taifa unganifu la kisasa. Ili kutatua tatizo hili, Muhammad Ali alibuni sera ya mgawanyo wa ardhi ambapo ardhi yote inayofaa kwa kilimo nchini Misri iligawanywa katika baadhi (kategoria) sita ambazo ziligawiwa kwa matabaka ya watu yafutayo: familia ya

Muhammad Ali na maofisa wa kijeshi; Mamluki; *Maulama;* wataalam wa kigeni nchini Misri; *Mafallahin* (wakulima wadogo wadogo); na Mabedui.

Sera hii ya mgawanyo wa ardhi haikupokewa vizuri na watu, hususani wale waliopokonywa ardhi yao na dola. Hata hivyo, sera ya ardhi ya Muhammad Ali yapaswa kuchukuliwa kama hatua ya mpito kati ya ukabaila na ubepari. Kwa maneno mengine, ilikuwa ni hatua ya lazima endapo Misri ilitaka kujitoa kutoka taifa lenye utegemezi mkubwa kwa ardhi na kuwa taifa linalotegemea nguvu za mitaji na masoko. Ilikuwa pia wakati wa utawala wa Muhammad Ali ambapo uendelezaji wa mashamba makubwa ya watu binafsi ulianzishwa. Haya yalianzishwa ili kurahisisha usimamizi na ukusanyaji wa kodi.

Muhammad Ali pia aliugeuza uchumi wa kilimo wa Misri kutoka ngazi ya kijungujiko na kuwa uchumi wa mazao ya biashara kwa kuhimiza ulimaji wa pamba sambamba na kilimo cha nafaka. Zaidi ya mifereji thelathini ilichimbwa kwa ajili ya kumwagilia mashamba ya taifa. Hata hivyo, umuhimu halisi wa mafanikio ya Ali katika kilimo cha umwagiliaji haukuwa kwamba alikuwa na mfumo mzuri zaidi wa umwagiliaji katika historia ya Misri, bali ni kwamba alianza kuigeuza Misri iwe nchi ya kisasa kwa lengo la kuihakikishia uhuru wake dhidi ya nchi nyingine.

Kipindi cha 1840-79 ndicho kilichokuwa cha mpito kwa Misri kutoka ukabaila kwenda kwenye hatua za mwanzo za uchumi wa kibepari ambao kwa kiwango kikubwa ulikuwa wa kilimo. Kwa kweli, sera ya serikali kumiliki ardhi ilikuwa ni matayarisho ya umilikaji ardhi wa binafsi. Mwaka 1858, sheria ilipitishwa ambayo iliauzisha haki ya umilikaji binafsi wa ardhi na ilipofika 1880 watu kadhaa walikuwa wameshajitwalia maeneo makubwa ya ardhi.

Sera ya kutumia mikopo kutoka nchi za nje kwa mitaji ya majenzi yanayosimamiwa na serikali ilianza wakati wa Abbas ambaye kunako 1851 alipata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kwanza katika Misri, ambayo ingeunganisha Aleksandria na Kairo. Chini ya Ismail, miradi mingi ya majenzi ya serikali kama vile ujenzi wa mifereji, madaraja, reli, minara ya taa ya kuongozea meli pwani, viwanda vya kusafisha sukari, nyaya za simu na majenzi mengine ya manispaa huko Kairo na Aleksandria ilifanyika.

Makabaila wakubwa walikuwa ndio kikundi cha kwanza cha kijamii kuibuka kama tabaka katika maeneo ya vijijini. Hawa ndio watu waliopatiwa maeneo makubwa ya ardhi na Muhammad Ali na baadaye Ismail. Walijumuisha viongozi wa ngazi za juu wa serikali, maofisa wa kijeshi, baadhi ya watu mashuhuri wa vijijini, baadhi ya machifu wa Kibedui, Maulama na *Makhufu*. Kikundi hiki kilimiliki 14.5% ya ardhi iliyolimwa kunako 1863, ambayo iliongezeka hadi 28.8% ilipofika 1891. Ardhi iliyobaki nje ya utaratibu wa mashamba makubwa ilikuwa 85.5% mwaka 1863 na 71.2% mwaka 1891.

Maulama na Masheikh pia walikuwa na umaarufu fulani chini ya utawala wa Ismail. Ingawa kuanzishwa kwa umilikaji binafsi wa ardhi chini ya Said kuliwapunguzia nguvu yao, Ismail aliimarisha mamlaka yao. Kusema kweli, wakati ambapo Abbas na Said walitaka kupunguza madaraka ya viongozi hawa wa vijiji, Ismail aliwategemea sana wamuunge mkono kisiasa na akawapatia nafasi ya kuzengea madaraka katika medani ya siasa za kitaifa. Kikundi hiki baadaye kilimsaidia sana wakati wa mapinduzi ya Urabi



13.4 *Shehe Rifa'a al-Tahtaun*

mwaka 1882. Lakini wakati huohuo baadhi ya *mafallahin* walizidi kuwa masikini ilhali watu wengine katika jamii wakizidi kutajirika.

## *Maendeleo ya kitamaduni*

Katika kutafuta mvuvumko wa kitaifa, suala la maendeleo ya kitamaduni linahitaji kutiliwa maanani. Baadhi ya watu walifikiri kwamba usasishaji wa uchumi, viwanda na siasa lazima uambatane na uigaji wa maadili ya nchi za Magharibi, ilhali wengine waliamini katika uanzishwaji wa falsafa halisi ya utamaduni wa kitaifa. Yapaswa kuzingatia hapa kwamba wakati ambapo serikali ilitoa msukumo katika maendeleo haya ya kitamaduni, maandishi na mawazo ya Sheikh Rifaa al-Tahtawi (1801-73) yalikuwa muhimu katika mchakato huu. Yeye alipigania urejeshwaji wa utambulisho wa Misri ambao alidhani ulikuwa ni muhimu kwa awamu ya utaifa ya maendeleo. Hili lingewezekana tu kama lingefuatiliwa kitaifa. Kwa mtazamo wake, mawazo ya siasa kali na mkabala wa kihakiki kwa mawazo ya kigeni na urithi wa taifa vingeigeuza nchi na kuleta usitawi wa wananchi kupitia uhuru, kazi na mawazo chanya.

Uwili wa mapokeo na usasa ulijitokeza wazi zaidi kwenye medani ya elimu, kwa vile kulikuwepo na mifumo miwili tofauti ya elimu nchini Misri. Wa kwanza ulikuwa wa

kimapokeo na kijadi uliokitwa katika urithi wa Misri. Wa pili ulikuwa wa kisasa na ulipangwa kwa namna iliyokidhi mahitaji ya serikali ya kijeshi na ya uhuishaji wa utamaduni uliokuwa ukiendelea. Asasi za elimu zilizoendelea za wakati wa Muhammad Ali zilipanuliwa na kupatiwa nguvu za kisheria na sera ya elimu ya taifa ya Ismail. Hivyo mfumo wa elimu wa Misri ulichanganya sifa za kimapokeo na za kisasa; ulikuwa na chuo kikuu cha kimapokeo chenye kiwango cha juu kabisa cha taaluma, na asasi nyingi za kisayansi zenye mtaala uliokitwa katika mawazo ya kisasa ya kisayansi na kielimu-jamii.

Kwa hiyo, palitokea jumuiya ya wasomi nchini Misri ambayo, kwa upande wake, iliwezesha usitawi wa vyombo vya habari na vuguvugu la uchapishaji. Zaidi ya hayo, Misri ilikuwa kimbilio la wasomi na waandishi kutoka sehemu mbalimbali za himaya ya Kituruki waliokimbia mateso kutoka kwa utawala wa kifalme. Hii ilitoa chachu kwa utamaduni wa kisomi nchini Misri na ikafanya pawepo na mawazo mengi na matapo ya kijamii na kitamaduni yenye nguvu. Kwa hiyo Misri ilitoa mchango mkubwa kwa elimu na taaluma kwa ujumla katika ulimwengu mzima wa Kiarabu na Kiislamu. Hata hivyo, ili kutilia nguvu uhai wa kisiasa, hatimaye Misri ilibuni dhana ya "nchi ya uzawa" mahala pa "jumuiya ya waumini," na hivyo kuwakilisha ipasavyo juhudi zake za kisiasa za kujipatia uhuru kutoka kwa Uturuki.

Ukiiweka katika muktadha mpana wa harakati za mataifa ya Ulaya za kupata makoloni, Misri sasa ilitaka kuhalalisha matakwa yake ya kuwa huru na pia kuwa taifa la kibeberu. Ufumbuzi haungeweza kupatikana kwa kuigiza mno nchi za Magharibi kwa kisingizio cha kufanya "mageuzi." Mbinu hii kwa hakika lilikataliwa na watu ambao walihitaji ufumbuzi wa kufaa zaidi.

## *Siasa za kijiografia na vibaraka*

Kujipenyeza Misri kwa wafanya biashara wakubwa wa Ulaya wakisaidiwa na vibaraka wa wakati huo, ambako kulipingwa sana na Abbas, kulishamiri wakati wa utawala wa warithi wake. Said (1854-63) alitoa ruhusa ya ujenzi wa Mfereji wa Suez kwa Ferdinand de Lesseps, mgeni, kunako 1854; na huu ndio ulikuwa mwanzo wa kujipenyeza nchini Misri kwa mitaji mikubwa ya kibiashara toka Ulaya. De Lesseps alifanya mikataba mingi ya mikopo toka nje ili kutekeleza mradi huo, na hivyo kuzidi kuiingiza Misri katika mfumo mkuu wa uchumi wa ulimwengu wa kibepari. Hali ilikuwa mbaya mno kiasi kwamba Said alilazimika kuuza baadhi ya mali zake kwa bei ndogo (ya hasara) ili kupunguza madeni yake.

Ismail, aliyemrithi Said, alijitahidi kupunguza deni lililoikabili Misri kutokana na ujenzi wa Mfereji wa Suez. Lakini majukumu mengine ya kitaifa kama vile juhudi kubwa za kuendeleza uchumi wa taifa, ofisi za balozi na shughuli za majeshi nje ya Misri ziliongeza kwa kiwango kikubwa deni la Misri. Kadiri deni la Misri lilivyozidi kuongezeka, ndivyo masharti ya mikopo yalivyofanywa kuwa magumu zaidi. Zaidi ya hayo, punguzo la kodi ya ardhi kwa 50% la 1871 halikusaidia chochote. Hatimaye, kunako 1875, ili kuikwamwua Misri kutokana na hali mbaya ya kiuchumi, Islamil aliuza

kwa Uingereza hisa zote za Misri katika mradi wa Mfereji wa Suez kwa bei ya chini kabisa.

Wakazi wa kigeni nchini Misri walikuwa wengi na mchanganyiko, na idadi yao ilizidi kuongezeka katika kipindi chote cha karne ya kumi na tisa. Ilipofikia 1897, idadi yao ilikuwa 112,568. Walijumusha Wamediterania, Walevanti na Wazungu wa Ulaya. Baadhi walikuwa na ajira muhimu (kwa taifa la Misri) ambapo wengine ajira zao hazikuwa muhimu. Hawa walikuwa na dhima kubwa wakati wa kuitwaa Misri mwaka 1882.

Kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, udhibiti wa uchumi wa Misri polepole uliponyoka toka mikononi mwa wananchi. Biashara ya jumla, maduhuli na mahuruji, ukopeshaji wa fedha na mabenki nchini Misri, na hali kadhalika biashara ya rejareja, vyote vilikuwa mikononi mwa wageni. Mafundistadi na mafundi mchundo pia walikuwa wageni - Wamediterani na Walevanti. Hivyo ilipofikia 1897, ni 17% tu ya Wamisri ikilinganishwa na 50% ya wafanyakazi wa kigeni ndio waliojishughulisha na viwanda na biashara, ilhali idadi kubwa zaidi ya wafanyakazi wazawa (asilimia 64) walijishughulisha na sekta ya kilimo, ambako walikuwepo wageni 0.7% tu.

Ardhi vilevile ilipokonywa toka mikononi mwa wananchi. Ilipofikia 1918, kila mmiliki ardhi wa kigeni alikuwa na *feddan* 400 za ardhi, ambapo Wamisri waliohodhi ardhi kubwa walikuwa sana sana na wastani wa *feddan* 150 kila mmoja. Kwa upande wa mapato wageni pia walikuwa na mapato makubwa zaidi kupita Wamisri.

## *Mapinduzi ya Misri: 1881-82*

Wakati ambapo mabwanyenye wa Misri walipata umashuhuri baada ya 1840 na watu kama vile Tahtawi na A. Mubarak wakaanzisha utamaduni halisi wa kitaifa, jeshi la Misri lilikuwa ndilo lenye nguvu zaidi katika Afrika. Jeshi hili lilikuwa na dhima kubwa katika jitihada za kuleta mapinduzi nchini Misri. Kuibuka kwa kikundi chenye nguvu kiitwacho "Kikundi hiki cha Hilwan" kikiongozwa na Urabi ulikuwa ndiyo mwanzo wa mapinduzi. Kikundi kilishinikiza matakwa yake kwa taifa na kikafanikiwa wakati mwingine. Hatimaye kilibadilika kabisa na kuwa chama cha kitaifa mwaka 1879, ambacho kilishirikiana kwa karibu na vikundi vyenye wafuasi wengi nchini, na kufungamana mno na jeshi.

Kufuatia kung'atuliwa kwa nguvu kwa Ismail kunako 1879, chama kilipinga ongezeko la athari za mataifa ya Ulaya nchini Misri. Chama cha kitaifa, kikiungwa mkono na jeshi, kilimdhibiti kwa werevu mtawala mpya, Khedive Tawfik, na kumfanya kibaraka. Kutokana na hali hii, mataifa ya Ulaya yaliamua kulishughukia suala la Misri kwa uvamizi wa kijeshi. Hivyo kunako 1882 kikosi cha manowari cha Waingereza kiliishambulia kwa mabomu Aleksandria. Uvamizi huu uliliangamiza jeshi la Misri. Baada ya kuona jinsi baadhi ya viongozi wa mapinduzi ambao walikuwa maofisa wa ngazi za juu kabisa walivyouawa au kupelekwa uhamishoni, idadi kubwa ya viongozi wenyeji walijiunga na majeshi ya uvamizi, huku wakisaliti mapinduzi.

Ingawa mapinduzi ya Misri hayakutekeleza malengo yake ya muda mfupi,

yalikuwepo mafanikio kadha yaliyotokana na kipindi hicho. La kwanza ni uhuishaji wa fikra za Kiislamu. Hili lilitumiwa kuhamasisha uungaji mkono wa mapinduzi. Chimbuko la uoza wa kitaifa uliochochea ari ya mapinduzi lilionekana kuwa ni upotoshaji wa Uislamu. Hivyo mageuzi yoyote ya maana nchini ilibidi yafungamane na misingi ya dini. Uislamu huu wa siasa kali kwa hiyo ulikuwa na nafasi muhimu sio tu katika uhuishaji wa kisiasa uliopelekea kwenye mapinduzi yaliyoshindwa, bali pia katika masuala ya kijamii ya ufufuaji wa taifa.

Tokeo jingine muhimu la kipindi hiki cha historia ya Misri ni kuibuka kwa Abdallah al-Nadim (1843-96), aliyeufundisha umma mingi na mawazo ya utaifa. Aliweza kuamsha maoni ya umma kupitia magazeti yake. Kupitia maandishi yake alichochea itikadi ya kitaifa ambayo wakati huo ilizidi kuwa kali na kuwa chachu muhimu kwa ufufuaji wa taifa. Hivyo alikuwa msemaji mkuu wa umma wa *wafallahin* ambao baadaye aliwatangaza kuwa wadhibiti wa mapinduzi.

## *Taathira ya Misri*

Katika kuhitimisha, lazima tujaribu kueleze sababu za mvuvumko wa Misri na kufifia kwake.

Jambo la kwanza la kuangalia tunapozingatia mfululizo wa matukio nchini Misri kwenye karne ya kumi na tisa ni nafasi ya Misri na athari za nafasi hiyo katika siasa za nchi hiyo. Kusema kweli, idadi kubwa ya mambo yaliyoathiri hali nchini Misri yalikuwa na mizizi nje ya nchi ambayo ilichochea mvuvumko. Hata hivyo, msukumo wa mwamko na sababu za kuporomoka kwa muda kwa mvuvumko zina chimbuko lake ndani ya Misri. Misri haikuwa na mfumo uliooshikamana wa mawazo ya kijamii ambao ungeongoza siasa zake. Kulikuwepo na upinzani kati ya wale waliosaka mabadiliko ya wastani ya kuleta usasa na Waislamu wa siasa kali ambao haukutafutiwa suluhu hadi katikati ya karne ya ishirini. Mvurugano huu wa kiitikadi haukuweza kudumisha mvuvumko wa Misri.

Licha ya hivyo, ufufuaji wa Misri ulikuwa na athari iliyofika mbali. Baadhi ya maeneo barani Afrika kama vile Sudan, Ethiopia, Pembe ya Afrika (eneo la Kaskazini Mashariki mwa Afrika) na eneo la Maziwa Makuu katika Afrika ya Kati yalipambana kwa mara ya kwanza na ubeberu wa Misri uliobuniwa wakati wa kipindi cha mvuvumko. Mzinduko wa Misri pia ulitishia "mpango wa dunia" kama ulivyokuwa wakati huo, na mataifa yenye makoloni yaliona suluhisho la tishio hili ni upunguzaji wa silaha kwa Afrika. Uzoefu wa Misri pia ulitoa funzisho kwa Japan mwaka 1868 wakati wa kujifufua kwake huko Mashariki ya Mbali kwamba sharti la awali kwa maendeleo ni kuhifadhi uhuru wa kitaifa. Huko Uturuki msingi wa marekebisho ya kikatiba yaliyofanywa na *Watanzimat* ulitokana moja kwa moja na mageuzi ya awali yaliyotokea nchini Misri. Hivyo mvuvumko wa kitaifa wa Misri ulioleta matatizo makubwa nyumbani ulichangia katika ufufuo wa Afrika, Asia na Mashariki ya Kati kwenye karne za kumi na tisa na ishirini.

# 14

# Sudani katika karne ya kumi na tisa

## Utangulizi

Athari ya Waarabu miongoni mwa watu wa Sudani Mashariki imeanza karne ya tisa. Hadi mwanzoni mwa karne ya kumi na sita eneo hilo lilikuwa linatawala na himaya mbili za Usultani wa Kiislamu: Funj na Für. Masultani wa Für walitawala Darfur upande wa Magharibi hadi mwaka 1874. Usultani wa Funj, uliokuwa na makao yake makuu mjini Sennar, ulitekwa kati ya mwaka 1820-21 na Muhammad Ali, aliyekuwa Pasha wa Misri. Kwa hakika, kabla Muhammad Ali hajaushambulia usultani huo mwaka 1820-21, himaya ya Funj ilikwisha sambaratishwa na ushindani wa kinasaba na kugawanywa katika tawala dhaifu na zenye chokochoko za kishehe. Hali hii ya vurugu na kukosa utulivu ndiyo iliyoifanya himaya ya Funj kupigwa kirahisi na Muhammad Ali na kuendelea kuwa koloni kwa miaka sitini iliyofuata.

Wakati Muhammad Ali alipoipiga sehemu hii ya Sudani, Misri ilikuwa bado ni jimbo la Ufalme wa Ottoman na sio taifa linalojitawala. Kwa hiyo, ushindi dhidi ya Sudani unapaswa kuonekana kama ushindi wa Uturuki na wala sio wa Misri. Hali hii inathibitishwa zaidi na ukweli kwamba baadhi ya maafisa wa ngazi za juu wa kisiasa na kijeshi hawakuwa Wamisri halisi, bali wazungumzaji wa Kituruki. Muhammad Ali mwenyewe alikuwa afisa wa Kialbania wa jeshi la Kituruki, ijapokuwa alijinasibisha na matamanio ya Wamisri. Watu wenye asili ya Misri waliongezeka polepole katika jeshi lake, lakini watu wa mataifa mengi, wakiwemo Wazungu, walitumika pia katika utawala wa Sudani. Kwa hiyo, Sudani ilikuwa ni koloni la Kituruki; haikuwa koloni la Kimisri au hata la Kituruki-Kimisri.

Yapo mambo matatu ambayo yanatakiwa kuzingatiwa. Kwanza, mkakati wa ushindi na jinsi ulivyopokewa na watu wa Sudani ya Kaskazini. Pili, upinzani dhidi ya ubeberu ulioelekezwa sehemu za Kusini, kati ya mwaka 1840-80. Tatu, dhima ya utawala mpya katika kuleta maendeleo nchini Sudani.

## Ushindi na jinsi ulivyopokewa Sudani Kaskazini

Tunahitaji kuwa waangalifu tunapoelezea mkakati wa uvamizi wa Kituruki nchini




14.1 *Sudan chini ya utawala wa waturuki*

Sudani. Madhumuni makuu ya Muhammad Ali ya kuanzisha utawala Sudani yalikuwa sio kwa maslahi ya nchi hiyo na watu wake. Vilevile hatua hiyo haikutokana na haja ya kulinda mshikamano wa Bonde la Nili kwa kuziweka Misri na Sudani chini ya utawala mmoja kama ilivyodaiwa na baadhi ya waandishi. Nia yake kuu ilikuwa ni kuwatumia watu wa Sudani na raslimali zao za kiuchumi ili kufanikisha haja zake nchini Misri na ng'ambo. Hata hivyo, Misri haikuweza kuweka utawala kamili nchini Sudani kwa kutumia haki za ushindi kwa vile uvamizi ulifanyika chini ya Sultani wa Ottoman ambaye alibaki kuwa mtawala wa Misri hadi karne ya ishirini. Zaidi ya hayo, ni himaya ya Funj pekee na wala sio Sudani nzima iliyotekwa mwaka 1820-21.

Kabla tu ya ushindi dhidi ya Sudani, Muhammad Ali alianza kazi ya kuunda jeshi imara la kisasa. Baada ya ushindi, alianza kutekeleza azma ya kuwaingiza Waafrika wa Wasudani sio tu kwenye jeshi bali pia katika miradi yake ya uchumi ya kilimo na viwanda nchini Misri. Ili kufanikisha azma hii, aliamrisha makamanda wake waliokuweko nchini Sudani kuanzisha uvamizi wa kutumia silaha ili kukamata watumwa. Mahitaji ya watumwa yalizidi upatikanaji wake hasa pale Wasudani weusi walipoanza kupambana na uvamizi kwa njia mbalimbali. Hali hii ilimfanya Muhammad Ali kuajiri wakulima wa Kimisri *(fallahin)* kwa wingi katika jeshi lake.

Wakati huo huo, baadhi ya Wasudani weusi walioandikishwa katika jeshi la serikali nchini Sudani walionyesha kutopendezewa kwao na mpango huu kwa kupanga maasi ya kijeshi dhidi ya serikali. Kati ya maasi hayo yaliyokuwa muhimu sana ni yale ya Medani ya mwaka 1844 ambamo baadhi ya maafisa wa kijeshi wa Kituruki waliuawa. Serikali iliweza kuzima maasi hayo kwa taabu sana.

Siasa za Muhammad Ali nchini Sudani hazikuwa za kijeshi tu. Aliendesha pia mpango wa kuchimba madini ya Sudani hasa dhahabu. Mradi huu baadaye haukuleta natija yoyote, kwani ulikuwa ghali sana kuuendesha na dhahabu haikupatikana Sudani. Wazo kwamba Sudani ina dhahabu nyingi likaja kudhihirika kuwa ilikuwa ni njozi tu.

14.2 Huenda sera ya utawala wa Kituruki nchini Sudani iliyokuwa na makuruhu zaidi ni ile ya mfumo wao wa utozaji kodi. Kuanzishwa kwa utozaji kodi wa kikandamizaji kulivuruga maisha ya kiuchumi ya watu na kuzua kelele nyingi. Njia za kikatili za kukusanya kodi, msisitizo wa serikali wa kulipa kwa fedha taslimu na utendaji mbovu wa maafisa wa Kituruki, yalifanya hali kuwa mbaya zaidi. Ukandamizaji huu wa kiuchumi ulizusha upinzani wa kivita kutoka kwa Wasudani, japo baadhi yao walihama makwao na kukimbilia mpakani na Ethiopia au Darfur. Kulikuwa na maasi mengi ya kupinga kodi kote Sudani; labda maasi yaliyokuwa mabaya zaidi ni yale ya mwaka 1822 yaliyopoteza maisha na mali kwa wingi. Wakati huohuo kule Darfur ambako masultani wa himaya ya Fur waliondolewa mwaka 1874, utozaji kodi wa ukandamizaji na utawala mbovu ulichochea upinzani mkubwa dhidi ya utawala wa Kituruki uliodumu kwa kipindi kifupi katika eneo hilo. Matokeo yake ni kwamba Waturuki walishindwa kuimarisha utawala wao na mwishowe walipinduliwa na wananchi kwa kushirikiana na himaya ya Mahdi mwaka 1884 maasi makali zaidi ya kijeshi yalitokea Kassala mwaka 1865. Maasi haya yalisababishwa na kusimamishwa kwa malipo ya kikosi (rejimenti) kilichokuwa Kassala. Maasi haya hayakutoa changamoto kali kwa utawala wa Kituruki wa jimbo la Kassala tu, bali pia kwa mfumo mzima wa kibeberu nchini Sudani.



**14.2** *Sennar mwaka 1821: Mji mkjuu wa Usultani wa Fundjya Kale wakati wa mavamizi ya Turuki-Misri*

**14.3** *Msafara wa wachukua watumwa huko Kordofan*



Mafanikio pekee ya ubeberu wa Kituruki yalikuwa ni upanuzi wa kilimo nchini Sudani. Waliboresha mfumo wa umwagiliaji maji, waliendeleza mazao yaliyokuwepo na kuanzisha mazao mapya, na walipambana na maradhi ya tauni, na wadudu na wanyama waharibifu. Pia walitunza vizuri mifugo na kuwafundisha Wasudani jinsi ya kuhifadhi ngozi. Lakini utajiri uliopatikana kutokana na upanuzi wa kilimo haukukusudiwa kuhudumia ustawi wa watu wa Sudani. Kinyume chake, ulisafirishwa hadi Misri, maana Muhammad Ali aliweka ukiritimba wa serikali katika ununuzi na uuzaji nje wa bidhaa zote za Sudani.

## *Upinzani Sudani ya Kusini, 1821-80*

Karne ya kumi na tisa, hususani nusu ya pili ya kipindi hicho, ilikuwa ni kipindi cha ghasia na upotevu mkubwa wa mali miongoni mwa watu wa Sudani Kusini. Walipata mateso mengi kutokana na ubeberu wa Kituruki nchini Sudani, na waliathirika sana na vita vingi, utumwa na utiishwaji. Vita vya kutamalaki na uvamizi wa kutumia silaha wa kukamata watumwa ulifanywa dhidi ya wananchi na maafisa wa kikoloni wa Kituruki na Kimisri nchini Sudani. Kama ilivyotajwa awali, madhumuni makubwa yalikuwa ni kukusanya kodi na watumwa ili kujaza jeshi la Kimisri. Uvamizi huu wa kukamata watumwa haukuwa kaskazini tu bali ulienea hadi kusini. Hali hii ilisababisha kukua kwa biashara ya watumwa hadi kuwa biashara kubwa baada ya mwaka 1840.

Wafanyabiashara wa Ulaya walishiriki pia katika biashara hii. Mwanzoni walishiriki katika biashara ya pembe za ndovu, lakini faidi iliposhuka waliamua kuwalipa wasaidizi na waongozaji wao wa Kiarabu kwa kuwapa watumwa badala ya fedha taslimu. Hali hii iliimarisha biashara ya watumwa. Katikati ya karne ya kumi na tisa, mji wa Kaka ulioko kaskazini mwa nchi ya Shilluk ulistawi na kugeuka kuwa soko kuu la watumwa na kupokea watumwa wengi kutoka Kusini.

Hata hivyo, watu wa kusini walikataa kushirikiana na wafanya biashara ya watumwa na kukataa kata kata kuwepo kwao nchini. Kulikuwa na mapambano mengi ya kijeshi kati ya pande hizo mbili. Wabari walikuwa watu wa kwanza kushambulia wavamizi. Mnamo mwaka 1854, walishambulia vikundi viwili vya kibiashara kutoka Ulaya na kuua watu wengi. Wabari walimshambulia pia chifu yeyote aliyeonyesha dalili za kushirikiana na wafanya biashara ya watumwa. Kwa mfano Chifu Nyagilo aliwindwa hadi kuuawa na kikosi cha vijana wa Kibari waliokuwa na silaha mwaka 1859 kwa sababu ya kushirikiana na wafanyabiashara hao. Kadhalika Walokoya, kabila jingine la kusini, waliwaua baadhi ya wafanya biashara ya watumwa mwaka 1860.

Labda tukio dhahiri zaidi la upinzani dhidi ya uchuuzaji wa watu lilikuwa lile la Washilluk ambao mara kwa mara waliwashambulia wafanyabiashara hao katika mto wa Nili nyeupe (*White Nile*). Mwanzoni, uhusiano kati ya Washilluk na wahamiaji walioingia Kaka kutokea eneo la kskazini lililotawaliwa na Waturuki ulikua mzuri. Lakini jinsi biashara nchini Kaka ilivyokuwa inaendelea kutawaliwa na wageni hawa, Mfalme wa Kaka alighadhabika na kuwafukuza nchini mwake wafanyabiashara wengi mwaka 1860. Baadhi ya wafanyabiashara walijibu mapigo na kuharibu Fashoda, mji mkuu wa kifalme wa himaya ya Shilluk. Washilluk nao waliitikia pigo hili kwa

mashambulizi mengine ya kikatili na kiharibifu, na ambayo yaliendeleza uhasama kati yao na serikali ya Kituruki.

Serikali ya Kituruki baadaye iliamua kuishikisha adabu Shilluk, hasa baada ya kushindwa kwake kuwapiga katika mapigano ya kijeshi ya mwaka 1868. Utawala huo uliwatoza kodi na ushuru wa kikandamizaji watu wa Shilluk na kuwaandikisha kwa nguvu kwenye kilimo cha pamba katika eneo la Fashoda. Majibu ya Wa-Shilluk kwa suala hili yalikuwa ni maasi.

Mnamo mwaka 1874-75 walichukua silaha na kupigana na majeshi ya serikali katika nchi yao na kuwaua wengi wao. Serikali ya Kituruki ikalipiza kisasi mwaka 1876 kwa kuwashambulia Washilluk na kuwaua wengi wao. Wengi kati ya waliobaki waliandikishwa kwa nguvu kwenye jeshi na kupelekwa Kairo. Fashoda ikawa soko la watumwa ambapo majeshi ya serikali yaliwauza mateka wa Kishilluk kwa kundi moja lilitoka kaskazini liitwalo Jallaba. Kwa hiyo, idadi ya Washilluk ikapungua na nchi ikawa ni kivuli tu cha Shilluk ya zamani.

Lakini sio makundi yote ya kusini yalipata mateso kama yale ya Washilluk. Wajieng na Wanaath, kwa mfano, walimudu kujilinda dhidi ya uvamizi wa wateka watumwa kwa kukimbilia kwenye vinamasi visivyopitika ambako waliweza kuwapiga vibaya wavamizi. Mfumo imara wa kisiasa wa Wazande pia uliwasaidia kuhimili mashambulio hayo ya wateka watumwa. Hata hivyo palikuwepo na makundi dhaifu ambayo hayakuweza kufanya mashambulizi makali dhidi ya wavamizi. Watu katika makundi hayo ama waliuawa au kukamatwa utumwa katika mapambano. Hali hii ilisababisha watu wengi kuangamia katika jamii nyingi za Kusini.

Wakati huohuo, kutawazwa kwa Ismail kuwa kiongozi wa Misri kuliimarisha uvamizi wa Kituruki kwenye maeneo makubwa ya bara katika Sudani ya kusini. Nia ya Ismail ilikuwa ni kujipanua kufuata Mto Nili na kujijengea himaya ya Kiafrika. Alitegemea kuwa utawala wake ungeweka uongozi bora na kukomesha mashambulizi ya wateka watumwa. Jitihada hii ya kuunganisha Equatoria ilikuwa chini ya amri ya maafisa wawili wa Kiingereza: Samwel Baker, 1869-73 na Charles George Gordon, 1874-76, kama Magavana wa Equatoria. Gordon alikuwa pia Gavana Mkuu wa Sudani miaka ya 1877-79.

Shughuli zao zilizaa matokeo madogo kwa sababu ya ukaidi wa wananchi. Kwa mfano, Baker hakuweza kupata ushirikiano wa Waafrika huko Sudani ya Kusini. Alipambana na uadui wa watu wa Bari na Lokoya. Baadaye alihamia eneo la Acholi la Uganda Kaskazini ambako alianzisha vituo vya serikali na kuandikisha mamluki ndani ya majeshi ya serikali. Upande wa magharibi, alikumbana pia na upinzani wa Kabarega, Mtawala la Bunyoro, na ikambidi kurudi nyuma mwaka 1872.

Uzoefu wa Gordon haukuwa bora zaidi ya ule wa Baker. Yeye pia alikumbana na upinzani mkali wa wenyeji. Gordon alikumbana na ukatili wa Moogie Bari ambao waliwaua askari zake wengi. Kusonga kwake mbele kuelekea Uganda kulizuiliwa pia, kwani Kabaka Mutesa alimzunguuka na kuvuruga mipango yake yote. Yote haya yalifanya kuingia kwa Waturuki katika Equatoria kuwe na mwisho mbaya.

Katika kipindi hicho hicho, uvamizi wa Waturuki eneo la kusini ulitishiwa na Milki



14.4 *Manju wa Kizande*

kubwa ya kibiashara ya al-Zubayr Rahama Mansur huko Bahr al Ghazal. Umaarufu na nguvu zake zilimfanya Ismail kumtambua kama Gavana wa Bahr al-Ghazal, na alikuwa mstari wa mbele katika kuiunganisha Darfur kwenye utawala wa Kituruki mwaka 1874. Lakini, Waturuki hawakuweza kuanzisha utawala madhubutu huko Bahr al-Ghazal baada ya kuanguka kwa Zubayr. Mwishowe, mnamo mwaka 1883, wananchi walishirikiana na majeshi ya Mahdi kuangusha utawala wa Kituruki.

Ingawa kuja kwa utawala wa Kituruki sehemu za kusini kulisitisha uvamizi wa wateka watumwa, lakini pia kulisababisha kuvurugika kwa jamii za Sudani ya kusini. Waturuki walitumia nguvu kukomesha maasi mengi dhidi ya utawala wao kwa sababu watu walikataa kuupokea utawala wao. Hali hii mwishowe ilisababisha kuuimarika kwa vuguvugu la upinzani ambalo hatimaye lilifanikiwa kukomesha utawala wa Kituruki katika ukanda huo.

## *Usasa na upinzani*

Licha ya ukweli kwamba jusura za Kituruki nchini Sudani zilishindwa kwa kiasi kikubwa, bado wengi wanakubaliana kwamba historia ya kisasa ya Sudani ilianza kwa ushindi wa Kituruki dhidi ya nchi hiyo mwaka 1820-21. Kwa maneno mengine, utawala wa Kituruki ulitoa mchango muhimu katika kuleta hali ya usasa katika Sudani.

Kwanza, utawala wa Kituruki uliiunganisha Sudani katika mipaka yake ya sasa. Kwa hiyo, hadi miaka ya 1880, Sudani ilikuwa eneo kubwa lililoanzia kwenye maporomoko ya pili ya maji hadi kwenye maziwa sehemu za ikweta, na kuanzia Bahari ya Shamu hadi Darfur. Utawala wa Kituruki ulianzisha kazi ya kuleta usasa katika Sudani kwa kuingiza taratibu za Ulaya za kisiasa na kiuchumi, na mbinu (za Ulaya) za uzalishaji, mawasiliano na usafirishaji. Yote haya yalileta mambo mapya na mageuzi katika jamii ya Sudani.

Mambo mapya matatu ya kiufundi yaliyokuwa muhimu zaidi ambayo yaliletwa na utawala wa Kituruki ni: silaha za moto, meli na simu za telegrafu zenye kutumia umeme. Bunduki ziliingizwa nchini Sudani katika nusu ya pili ya karne ya kumi na saba, lakini zilianza kutumika kwa wingi zaidi katika kipindi cha utawala wa Kituruki. Kufikia miaka ya 1860 na 1870 meli za kutumia mvuke zilikuwa zimekwisha letwa Sudani, na tayari idadi kubwa ya meli za aina hiyo ilikuwemo nchini humo. Telegrafu za umeme ziliingia Sudani wakati wa utawala wa Khedive Ismail.

Hata hivyo, upanuzi wa himaya ya Kituruki sehemu za kusini ulisaidiwa sana na bunduki na meli za mvuke. Teknolojia hizi mbili mpya ziliwawezesha wakoloni na vibaraka wao wa Kisudani kushinda vizuizi vikuu viwili katika kusonga mbele kuelekea juu ya mto Nili Nyeupe. Vizuizi hivyo vilikuwa: upinzani mkali wa Wasudani na kipingamizi kikubwa cha vinamasi vya Sudd, ambavyo vilizuia vyombo vya majini kutokea Nili kuingia Nili ya Ikweta na Bahr-al-Ghazal.

Upanuzi wa himaya katika eneo la kusini ulisababisha kuzuka kwa kundi lililojulikana kama al-Jallaba. Hawa walikuwa watu wa kaskazini waliokwenda kusini baada ya majeshi ya himaya kuvamia eneo hilo ili kupata mafao ya kiuchumi. Awali ya yote watu hawa walikwenda kusini kama watumishi na walinzi wa wafanyabiashara wa kigeni. Baadaye, wakawa wafanyabiashara na kujikusanyia majukumu na nguvu.



14.5 *Ujenzi wa utawala wa Kiturku-Kimisri: Kasri ya Hukunda huko Khartoum na mashua mtoni*

Shughuli zao huko kusini zilikuwa na faida kuu mbili: Kwa upande mmoja ziliongeza kasi ya kuingiza Uarabu na Uislamu huko kusini. Kwa upande mwingine zilichochea uhasama kutoka kwa watu wa kusini kutokana na tabia yao ya kupenda vita, udhalimu, na mabavu. Hali hii ya pili ilifanikiwa kujenga kutoaminiana na hofu ambayo mpaka sasa inatawala mahusiano kati ya watu wa sehemu za kaskazini na wale wa kusini mwa Sudani.

Utawala wa Kituruki ulifanikiwa pia kuanzisha utawala unganifu nchini Sudani. Hapana shaka, chombo cha uongozi kilikuwa cha ukandamizaji, kilichojaa rushwa, na kisichokuwa na ufanisi, hasa kwa vile maafisa wa Kituruki walikuwa ni wa kiwango cha chini. Lakini utawala huu ulikuwa unganifu hasa, ukilinganisha na aina nyingine za serikali zilizokuwepo. Utawala uliongozwa na Gavana-Jenerali aliyeitwa *Hukumdar*. Baadhi ya Wasudani walioshirikiana na utawala wa himaya walipewa majukumu katika serikali kuu. Katika vipindi vifupi ambapo nafasi ya Gavana-Jenerali ilifutwa, hasa mwaka 1843 na 1882, mikoa ya Sudani iliwekwa chini ya idara moja ya serikali huko Kairo ili kuendeleza sera ya uunganifu wa utawala. Aidha, uboreshaji wa mawasiliano, kama vile mtandao wa meli na simu, ulitoa mchango mkubwa katika uunganifishaji wa utawala. Jeshi pia lilikuwa la msaada mkubwa kwa serikali katika kuidhibiti Sudani. Kwa maneno mengine, watawala wa Kituruki walilitumia jeshi na mawasiliano mazuri katika kudumisha usalama wa jamii, kuzima maasi ya Wasudani, na kulazimisha ulipaji wa kodi.

Mageuzi yaliyoletwa na utawala wa kifalme yaliathiri pia maisha ya kidini ya Wasudani wa kaskazini. Ijapokuwa Wasudani na Waturuki walikuwa wote Waislamu, palikuwepo na tofauti ya kimadhehebu kati yao. Wakati Wasuni wa utawala wa Kituruki waliegemea sana kwenye imani halisi za kale, Wasufi wa Sudani walikuwa zaidi wanapendelea imani za vikundi. Utawala wa Kituruki ulidhoofisha hadhi ya uongozi wa Wasufi wenyeji kwa kueneza Uislamu asilia na kwa kuanzisha kundi pinzani la viongozi wa kidini ambalo lilipendelea zaidi uasilia, lenye mtazamo wa kigeni na lenye kutegemea sana serikali. Udhoofishaji huu wa hadhi ya viongozi wa kidini wenyeji uliwafanya baadaye kupinga serikali ya himaya na kuunga mkono jitihada za Mahdi za kuiangusha serikali hiyo.

Jambo jingine lililofanywa na utawala wa kihimaya wa Kituruki ambalo lilisababisha upinzani mkali kutoka kwa wananchi lilikuwa ni kupenyezwa kwa wageni nchini Sudani. Kuajiriwa kwa Wazungu katika huduma za serikali na jeshi na hivyo kuzuia kupandishwa vyeo kwa Wasudani na hata Wamisri wa ngazi za juu kuliwaudhi wengi. Walikuwepo pia Wazungu na Wamarekani wengine waliokuja Sudani kama wasafiri, wamisionari, wataalamu na washauri. Kwa sababu ya kuwa na lugha, tabia na dini ngeni, kuwepo kwao kuliibua wasiwasi miongoni mwa Wasudani kiasi kwamba hawakuwaamini na waliwaogopa. Katika mkesha wa vuguvugu la Mahdiyya, palikuwepo na fikra za ujumla za kutawaliwa na makafiri na kwamba Misri imekoma kuwa nchi ya Kiislamu. Kwa hiyo, tangazo la Mahdi la kuikomboa nchi kutoka katika utawala wa kigeni na wa Kikristo liliungwa mkono sana na watu.

## *Hitimisho*

Ari ya Waturuki ya kuvuna raslimali za Sudani pamoja na mbinu mpya za kiuchumi na kiteknolojia walizozileta, zilizua upinzani miongoni mwa watu wengi. Hata hivyo, maasi yaliyochochewa na hali hii, hayakuwa na nguvu kubwa kiasi cha kuiangusha serikali kwa sababu yalikosa itikadi ya kimapinduzi. Ilikuwa hadi mwaka 1885 ndipo Mahdi walipoleta itikadi hiyo na kuwaunganisha watu na hatimaye kuangusha utawala wa Kituruki na Sudani kupata Uhuru. Huko kaskazini, kipindi hiki kilitawaliwa pia na mapambano dhidi ya utawala wa kibeberu wa Kiingereza uliokuwa ukisonga mbele.

Hata hivyo, katika eneo la kusini, uvamizi wa kuteka watumwa, uporaji na utekaji nyara uliendelea bila kizuizi. Uporaji ulihimizwa pia na serikali ya Mahdi ambayo iliivamia kusini na kukamata watu wa kuingiza jeshini kwa nguvu. Vitendo vyote hivi vilionyesha sura mbaya ya Waarabu na Uislamu kwa watu wa kusini. Kilichotokea baadaye ilikuwa ni kuunda utamaduni wa upinzani miongoni mwa watu wa Sudani ya kusini.

# 15 *Ethiopia na Somalia*

## *Ethiopia katika muongo wa kwanza wa karne ya 19*

Miongo michache ya awali ya karne ya kumi na tisa ilitawaliwa na kuvurugika kwa maisha ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika Ethiopia. Madaraka ya kifalme yalipungua na mamaliki walikuwa na mamlaka madogo tu ya utawala. Walizidiwa nguvu na makabaila ambao hawakuwa chini yao. Zaidi ya hayo, uhusiano baina ya makabaila ulikuwa wa wasiwasi kiasi cha kuwepo mapigano ya mara kwa mara kati yao. Uharibifu uliosababishwa na mapigano hayo ulileta umaskini katika majimbo kadha. Hata jimbo la Bagemder, ambapo mji mkuu ulikuwepo, halikunusurika: kilimo kilitelekezwa kwa vile wakulima wengi waliacha mashamba yao kutokana na kutokuwepo kwa usalama na wakatafuta maslahi kwingineko. Gonda, mji mkuu na wenye sifa, ulitelekezwa na kukawa na upungufu mkubwa wa udhamini wa kazi za sanaa.

Kwa jumla, kulikuwa na mkengeuko mkubwa wa madaraka katika dola. Kulikuwa na maasi ya viongozi wa vita kwenye majimbo waliojichukua mamlaka ya kifalme. Hali hii iliibua makudi yenye kuzozana na kusababisha mvurugiko mwingine katika muundo wa kiuchumi na wa kijamii wa jamii hiyo. Kipindi hiki kimeelezwa katika historia ya Ethiopia kuwa ni kipindi cha *Masafent*, neno lenye maana ya "Mahakimu," dhana ya kidini inayorejelea katika maandiko matakatifu katika kitabu cha *Waamuzi* ambapo "hakukuwa na mfalme Israeli: kila mtu alifanya vile alivyoona kuwa ni sawa." Kutokana na mchanguko huu wa kisiasa, nyanda za juu zilizokaliwa na Wakristo, ambazo ndizo zilizokuwa kitovu cha himaya, ziligawanywa katika dola tatu huru, ambazo ni Tigre, Amhara na Shoa, pamoja na tawala nyingine ndogo za kisiasa. Tigre ilikuwa kaskazini zaidi na ilikuwa ndiyo yenye nguvu zaidi kati ya madola hayo matatu. Watu wake wengi walikuwa Wakristo, na ilikuwa na Waislamu wachache mashariki na kusini. Kwa sababu ya kuwepo kwake pwani, ilikuwa rahisi kwa watawala wake kutajirika kutokana na biashara na kupata silaha nyingi zaidi kuliko majirani zake.

Mnamo nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, Tigre ilitawaliwa na machifu wenye nguvu ambao enzi zao zilitawaliwa na vita vingi dhidi ya majirani zao. Labda ambaye alikuwa maarufu zaidi ni Ras Walda Sellasé (1797-1816) ambaye alijulikana kutokana na nguvu zake za kijeshi. Zaidi ya kuonyesha uwezo wake mkubwa wa




**15.1** *Ethiopia mapema karne ya kumi na tisa*

kiutawala, Walda Sellasé alikuwa ni mhalisia aliyetafuta jinsi ya kuifikia bahari ili aweze kuwasiliana na nchi za Ulaya ambazo zilikuwa zimeendelea kiufundi.

Warithi wake, Dajazma Sabagadis (1822-31) na Ras Webé (1839-55), walithamini mawasiliano na nchi za nje ambayo waliyatumia kwa faida yao. Waliweza kupata silaha nyingi kutoka Uingereza na Ufaransa. Lakini hali hiyo ilikuwa na matokeo mabaya yaliyoletwa na kuongezeka kwa mashambulizi, na hivyo kuchangia katika vurugu za kijamii na kisiasa katika eneo hili.

Amhara ilikuwa kaskazini magharibi. Watu wake wengi walikuwa Wakristo, ingawa kulikuwapo na idadi ya kutosha ya Waislamu. Amhara ilipata umaarufu wake kutokana na kuidhibiti Bagemder na Gondar. Hata hivyo, watawala wake hawakuweza kuhodhi silaha nyingi kama wenzao wa Tigre, kwani walikuwa mbali na bahari na walitegemea kuzipata kutoka Bahari ya Shamu kwa kupitia Sudani au Tigre. Watawala wa Amhara wa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa walikuwa Aligaz Gwangui (1788-1803), na Ras Yeman (1825-8). Gugsa Mersa alianzisha sera ya kujitanua na pia alijaribu kuvunja nguvu za makabaila kwa kutaifisha ardhi zao. Sifa kubwa ya historia ya Amhara ya wakati huu ni jinsi kila mtawala alivyoitumia dini (iwe ya Kikristo au Kiislamu) kwa ajili ya kufikia malengo yake ya kisiasa.

Kusini mwa Amhara kulikuwa na jimbo ambao takriban lilikuwa huru lililoitwa Gojam. Lilikuwa likikaliwa hasa na Wakristo walioongea Kiamhari. Ingawa eneo hilo liliunganishwa mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mtu mmoja aliyeitwa Ras Haylu, ushindani wa kisiasa ulilifanya eneo hilo liweze kuingiliwa kwa urahisi na ufalme wa Yajju wa Amhara. Ingawa Wayajju walikuwa na nguvu ya kuitawala Gojam, hawakuweza kuwatetetresha Wagojam au kuwaletea mtawala kutoka sehemu nyingine.

Shoa ilikuwa kusini mashariki. Ilikuwa na watu wenye mchanganyiko wa dini: Wakristo, Waislamu na Wanaasilia. Kutengwa kwa jimbo la Oromo kuliwapa fursa watawala wake kujipatia uhuru na kuendelea kwa wakati wao. Shoa ilianzisha uhusiano na vituo vikuu vya kiuchumi ambako walipata silaha nyingi. Iliweza kupanua mipaka yake na kuendelea kudhibiti biashara kwa kutumia silaha hizo. Wafalme wa Shoa walipigana vita vingi kupanua eneo lao na kupata uhuru wao kutoka Gondar. Maarufu zaidi kuliko wote labda ni Sahla Sellasé (1813-47), ambaye aliwastahamilia majirani zake. Pia alianzisha uhusiano na Uingereza na Ufaransa ambako alipata silaha. Ingawa utawala wake ulikuwa wa amani, kifo chake kiliibua matatizo mengi na mapambano ya kisiasa ambayo yalileta vurugu nyingi.

Massawa ilikuwa ni kisiwa mbali kidogo na ufuko wa Bahari ya Shamu. Kisiwa hicho pamoja na bandari ya karibu ya bara ya Arkiko, kwa pamoja zilipokea karibu biashara yote ya Ethiopia kaskazini. Wenyeji walikuwa ni Waislamu waliozungumza Kitigre lakini lugha nyingine zilizungumzwa pia kutokana na kuwepo kwa wafanyabiashara wa mataifa na lugha mbalimbali. Kulikuwa na mgogoro wa muda mrefu katika eneo hili baina ya makundi manne makubwa: Himaya ya Ottoman, Misri, ukoo wa kimwinyi wa eneo hilo ulioongozwa na *naibu*, na magavana wa Tigre. Kila kimoja cha vikundi hivi kilikuwa na madai juu ya bandari hiyo, na historia ya bandari hii ilijaa magomvi na mivutano baina ya makundi hayo manne yaliyopigana. Ijapokuwa



**15.2** *Dajazma Webe wa Tigre*

mamlaka ya manaibu yalihatarishwa na watawala wa Misri na Tigre, Tigre ilikwenda hatua mbele kwa kuomba msaada wa nje ili iweze kulipata eneo hilo kutoka kwa manaibu wa Wamisri, kwani ilifikiria kuwa bandari hiyo ilikuwa muhimu katika kuifikia bahari. Wamisri walitwaa madaraka ya Massawa mnamo 1846 baada ya mtawala wa Tigre kufanya majaribio kadha ya kuiteka na kushindwa. Hata hivyo, bandari ya bara ya Arkiko iliharibiwa sana kutokana na mapigano ya mara kwa mara baina ya Misri na Tigre.

Mabonde ya Afa yalikuwa kusini masharíki mwa Massawa na yalikuwa na wahamiaji waliozungumza Kikushi. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa watu hao walitawaliwa na sultani wa Ausa. Kifo cha sultani mnamo mwaka 1810 kilileta vurugu nyingi katika eneo hilo kwani watu wa Adoimara, ambao walikuwa maadui wa usultani huo, waliiteka Ausa na kumshurutisha mrithi wa sultani kugawana nao madaraka. Zaidi ya hayo, nguvu zao ziliongezwa na kuibuka kwa bandari ya Tajura na ongezeko la biashara na Shoa. Kutokana na kutekwa kwa Aden na Uingereza mnamo 1839, pwani ya Danakil ilianza kutambuliwa kimataifa. Maafisa wa Uingereza na Ufaransa walianza kufanya biashara na machifu mbalimbali wa eneo hili.

## *Somalia na Pembe ya Afrika*

Mashariki walikuwepo Wasomali, ambao ni Waislamu walioishi kwenye mabonde ya jangwa ya ghuba ya Aden. Walizungumza lugha ya Kikushi na walikuwa wameathiriwa na Waarabu kwa muda mrefu. Zeila ilidhibitiwa na Waarabu wakati sehemu zilizobakia za ukanda wa pwani, pamoja na Berbera, zilikuwa chini ya Wanomadi wa Kisomali. Mnamo nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, Wamisri walianza kuivamia Berbera. Kuondoka kwao kwenye eneo hilo mwaka 1841 kulisababisha kutokea kwa mfanyabiashara wa Kisomali mwenye tamaa, Al-Haj Ali Shermerki, kuwa na umaarufu wa kisiasa. Alinunua ugavana wa Zeila na pia aliiteka Berbera lakini baadaye aligongana na mtawala wa Harar na kusababisha kuanguka kwake.

Pwani ya kuanzia Bender Ziada ufukoni mwa ghuba ya Aden hadi Ilig ufukoni mwa bahari ya Hindi ilidhibitiwa na Usultani wa Majertein. Wakazi wa Usultani huu walikuwa nusu-Wanomadi waliopata mapato yao kwa kuuza nje ubani na magome yanukiayo, na pia kutokana na ubaharia. Hadi kufikia karne ya kumi na tisa, Sultani alikuwa na mamlaka kiasi juu ya watu wa bara. Alisaini mkataba mnamo mwaka 1839 na Waingereza huko Aden ambapo alipata malipo fulani kila mwaka kutoka kwao ili alinde maisha na mali za mabaharia wa Kiingereza wanapoharibikiwa na meli katika upwa wake.

Mamlaka ya Benadir yaligawanywa baina ya Sultani wa Geledi aliyedhibiti sehemu kubwa ya bara, na watawala wa Zanzibar. Vita vya jihadi vilianzishwa mnamo miaka ya 1830 na wanamageuzi huko Bardera dhidi ya watu wa Somalia ya kusini. Sultani wa Geledi alijibu kwa kupeleka jeshi kubwa dhidi ya wanamageuzi ambalo liliiteka Bardera. Ushindi huu ulimfanya Sultani wa Geledi awe kiongozi mwenye nguvu zaidi katika Somalia ya kusini. Wakati huohuo, wimbi la mwisho la wahamiaji wa Kisomali

lililoanza mwanzoni mwa karne liliwaleta Wanomadi kuelekea mto Juba na mbele zaidi, ambako walipambana na Waoromo ambao mwishowe waliwasukuma kuelekea Mto Tana.

Harari ulikuwa mji wa Waislamu uliokuwa bara ya pwani ya Somalia. Wakazi wake waliongea Kiadare, lugha ya Kisemiti ambayo haikujulikana kwingineko. Kwa karne kadha, mji huo ulikuwa ni dola huru lililotawaliwa na amiri. Lilitengeneza fedha zake na lilifanya biashara nzuri ya kahawa, zafarani, ngozi, pembe za ndovu na watumwa, tambuu, nguo na bidhaa nyingine kutoka nje. Mji huu ulikuwa ni kituo cha biashara kwa makundi ya jirani kama vile Washoa, Waarusi, Wagurage, na Waogaden. Harar ulikuwa pia kituo cha uwanazuoni wa Kiislamu, ukiwa na misikiti mingi na madhabahu ya Kiislamu na ulieneza athari yake ya kidini na kitamaduni kwa majirani zake.

Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, mji huo ulivurugwa na migongano ya ndani lakini amiri wake shupavu, Ahmad bin Muhamad (1794-1821), aliweza kuuunganisha na kuwazuia maadui zake, hasa Waoromo, wasiuingilie. Hata hivyo, mambo yaliharibika baada ya kifo chake, na Waoromo walitumia fursa iliyotokana na migongano ya ndani kuiteka nchi ya Harari na maeneo yake. Mji wenyewe ungeweza kutekwa kama si uimara wa kuta zake, mizinga michache na jeshi dogo la watu wenye bunduki lililoutetea.

Eneo la Gurage vilevile lilikuwa bara. Watu wake walizungumza lugha ya Kisemiti na waligawanyika kati ya Waislamu na Wakristo. Ilipofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa eneo hili halikuwa tena chini ya wafalme wenyeji, bali chini ya kaya huru saba ambazo, kutokana na kutengana kwao, ilikuwa rahisi kwa watafuta watumwa kuzishambulia, na hatimaye kutekwa na mtawala wa Shoa.

Ufalme wa Kaffa ulikuwa kusini magharibi mwa eneo la Ethiopia. Watu wake walizungumza lugha yao wenyewe ya Katicho. Eneo hili lilikuwa ni chanzo cha bidhaa za thamani zilizouzwa nje ambazo zilikuwa ni pamoja na ngano, pembe za ndovu, watumwa na kahawa. Mnamo karne ya kumi na nane ufalme wa Kaffa ulinyemelea maeneo ya majirani zake, kiasi kwamba ilipofika 1820 mfalme wake, Hoti Gaotscho, alitawala kuelekea kaskazini na mashariki hadi kufikia mito ya Gibbe na Omo.

Waoromo walipatikana katika eneo la kusini mwa Nili ya Bluu. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa kulikuwa na mabadiliko ya kisiasa. Mfumo wa zamani wa serikali wa zama za utawala wa marika ulipingwa na viongozi matajiri na wenye nguvu za kijeshi waliodai haki ya kuasisi nasaba tawala, na hata kufanikiwa kufanya hivyo. Hivyo falme tatu za Kioromo ziliibuka kunako miongo ya awali ya karne: Enarya, Goma na Guma. Enarya, ambao ndio uliokuwa ufalme wenye nguvu zaidi, ulitawaliwa na Bofu, ambaye alisilimu ili kuimarisha mamlaka yake. Mrithi wake, Aba Bagibo (1825-61) alijijengea madaraka kwa kuwa na mahusiano ya kiutawala na majirani zake waliotoka kwenye kaya tawala na kwa kujipatia bunduki kutoka Gojani. Biashara ilishamiri wakati huo na ufalme ukawa tajiri na wenye nguvu. Hata hivyo, kifo chake kilifuatiwa na kuanguka kwa haraka kwa ufalme huo.

Miaka michache baada ya kuibuka kwa Enarya, falme nyingine ziliibuka kusini. Dola lililodumu zaidi ni lile la Jima Kaka ambalo lilianzishwa na Aba Magal.



**15.3** *Mfalme Sahk Sellase wa Shoa*

**15.4** *Amiri Ahmad bin Muhammad wa Harar, 1794-1884*



Kupendelea kwake nguvu za kijeshi kuliendelezwa na wanawe, ambao pia walifanya mageuzi ya kisiasa na kiutawala na pia kueneza Uislamu katika majimbo.

Hadi sasa, tumeangalia madola kadhaa na vikundi vya kisiasa, kila kimoja kikiwa na uhuru wake chenyewe. Hata hivyo, kulikuwa na mahusiano baina yao, hasa ya kibiashara. Ingawa tofauti za kikabila na lugha ziliendelezwa, kulikuwa na mahusiano ya kiutamaduni ambayo yalichochea matumizi ya lugha mbili katika baadhi ya jamii za kibiashara.

## *Jitihada za Mfalme Téwodros II za kuiunganisha Ethiopia*

Nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa ilishuhudia majaribio mawili ya kuiunganisha Ethiopia. La kwanza lilifanywa na Dajazmek Kasa Heyku ambaye baadaye akawa Mfalme Tewodros II, au Theodori wa Ethiopia.

Kassa alizaliwa mnamo 1820 na Chifu wa Kwara, jamii iliyoishi mpakani na Sudani. Alilelewa kwenye nyumba ya watawa na baadaye akawa askari huria. Alijifanya kuwa bwana wa Kwara na akijipachika cheo cha Dajazmak. Madaraka yake yalivyozidi, alimwasi Yaju, mtawala wa Bagemdar mara kadha kabla hajamshinda mnamo 1853 katika mapambano ya kijeshi ambayo mtawala wa Tigré alijiingiza kumsaidia Yajju. Ushindi huo uliashiria mwisho wa ufalme wa Yajju na ulikuwa mwisho wa kipindi cha *Masafent*. Kassa aliwashinda pia watawala wa Gojam na Tigré, na hivyo kuwaondosha maadui zake wakuu wa Ethiopia ya kaskazini. Hapo ndipo alipojitawalisha kuwa Maliki (Mfalme Mkuu) na akachagua *Tewodros* kuwa jina lake la kutawazwa.

Mfalme Tewodros alijipa kazi ya kuunganisha majimbo mbalimbali ya Ethiopia. Baada ya kutawazwa kwake aliingia Wallo na kuteka ngome asilia ya milimani ya Magdala ambayo baadaye aliifanya kuwa makao yake makuu. Aliiteka pia Shoa na kumchukua mateka Menelik, mtoto wa mfalme.

Aliamua kulipangilia upya jeshi lake kama sehemu ya mabadiliko, kwani hiyo ndiyo ilikuwa njia pekee ya ufanisi ya kuidhibiti nchi. Kwa hiyo, alianza kujenga jeshi lenye vifaa vya kutosha la askari wataalamu. Aliwatumia Waturuki na jasusi wa Kiingereza, John Bell, kulipa nidhamu jeshi lake. Alianzisha dhana ya kuwalipa ujira wanajeshi wake. Aliwapanga askari wake katika rejimenti zilizochanganya watu kutoka katika majimbo mbalimbali na hivyo kuzima mfumo wa ukabaila ambapo watu waliungana chini ya chifu wa wilaya yao. Alianzisha maghala kwa ajili ya jeshi, na aliwaamuru askari wake wanunue chakula badala ya kuwavamia wakulima. Aliongeza silaha zake kwa kuwalazimisha wamishionari na mafundi stadi wa kigeni kutengeneza bunduki, mizinga, makombora na mabomu ili vitumiwe na jeshi lake. Alianzisha miradi ya ujenzi wa barabara ili kuwezesha jeshi lake lisafiri haraka. Barabara hizo zilikuwa ziiunganishe Dabra Tabor na Gondar, Gojam na Magdala.

Téwodros alijaribu pia kufanya mageuzi ya kiuchumi. Alifuta kodi za kibiashara zilizokuwa za kikandamizaji na aliamuru kuwa ushuru wote ukusanywe mahali patatu tu katika dola lake. Alirudisha amani na usalama katika njia za biashara.

Katika uwanja wa siasa, alipunguza nguvu za machifu wa kikabaila. Aliliweka jeshi la makabaila wa majimbo chini ya amri ya wafuasi wake badala ya machifu wa



**15.5** *Mfalme Tewedros akikagua ujenzi wa barabara*



15.6 *Mzinga mkubwa wa Mfalme Tewedros uitwao 'Sebastopol'*

majimbo. Ili kuleta amani katika nchi iliyotawaliwa na vita, aliwaamuru watu warudi katika stadi zao. Mageuzi yake ya kijamii yalikuwa pamoja na kupiga marufuku biashara ya watumwa, kuondoa ujambazi na rushwa. Alijaribu kumaliza tofauti za kidini kwa kuwaamuru Waislamu waliokuwa kwenye dola yake kuwa Wakristo na kwa kuwafukuza Wakatoliki. Matatizo makubwa katika mageuzi yake yalikuwa ni mageuzi yake ya kanisa. Alijaribu kupunguza idadi ya makasisi, kupunguza ardhi iliyomilikiwa na kanisa, na kuwafanya mapadri wategemee mishahara kutoka kwenye dola. Hayo yote yalisababisha upinzani mkubwa kutoka kwa makasisi, na upinzani huo ulipoungana na uadui wa mamwinyi wa majimbo, idadi kubwa ya watu ilimpinga maliki, na hilo lilichangia katika kuanguka kwake.

Téwedros alikuwa na wakati mgumu kupambana na upinzani wa majimbo. Upinzani wa kwanza ulitokea Tigré. Agaw Negusé aliongoza uasi huo. Negusé aliachia bandari ya Zulla kwa Wafaransa na aliahidi kukubali askofu wa Wakatoliki kuwa mkuu wa kanisa la Ethiopia. Lakini kutokana na upinzani wa Waingereza, Negusé hakuungwa mkono na Wafaransa kama ilivyotegemewa na aling'olewa mnamo 1860. Baada ya hapo kulitokea mfululizo wa maasi katika miaka ya mwisho ya utawala wake kutoka kwa malodi wa Walo, Shoa, Gojam na Gondar. Mnamo mwaka 1865 Menelik, mrithi wa kiti

cha ufalme cha Shoa, alitoroka kutoka Magdala na akajitangaza kuwa mfalme huru. Akikabiliwa na matatizo hayo, Téwodros alizidi kuwa mkali na mwenye hasira, akaziteka Gondar na Dambeya na kuwanyonga watu kadhaa.

## *Mgongano na Waingereza*

Utawala wa Téwodros kama maliki wa Ethiopia uliishia kwenye mzozo na Uingereza. Mahitaji yake ya msaada wa kiufundi yalimfanya amwandikie Malkia Viktoria wa Uingereza mnamo mwaka 1862, akipendekeza ampelekee mabalozi. Serikali ya Uingereza ilipuuza barua hiyo, kwani kwa wakati huo haikutaka kushiriki kwenye masuala ya Ethiopia. Téwodros hakuweza kustahimili muda ulivyozidi kwenda bila kupata majibu ya barua yake. Ilimuudhi kwamba Uingereza haikuonyesha kuvutiwa na masuala ya Ethiopia. Matukio mengine yalimfanya ahakikishe hofu yake kuwa Waingereza hawakuwa tayari kumsaidia. Taarifa ya mkuu wa nyumba ya watawa wa Kiethiopia ya Yerusalemu kwamba Waingereza hawakusaidia wakati makasisi wa Kikhufu wa Misri walipojaribu kuiteka nyumba hiyo ilifanya mambo yawe mabaya zaidi. Téwodros aliona kuwa amedharauliwa na Waingereza, na kwa hasira, alimfunga balozi mdogo Cameron, mwakilishi wa Uingereza, pamoja na washirika wake.

Habari za kufungwa kwa Cameron ziliistusha serikali ya Uingereza, na barua ya Téwodros iliyosahauliwa kwa muda mrefu ilijibiwa. Hii ilimfanya amwachie Cameron, lakini mara aliwafunga Wazungu wengine waliokuwa Ethiopia. Madai yake aliyoyashikilia ya kutaka msaada wa kiufundi kutoka Uingereza; ukosefu wa busara wa baadhi ya Wazungu waliokuwa Ethiopia; na matukio madogo madogo, kama vile taarifa iliyomfikia mfalme kwamba kampuni ya Kiingereza ilikuwa ikijenga reli Sudani kuwasaidia katika uvamizi wa Ethiopia – yote haya yalikuza mgogoro katika uhusiano baina ya Téwodros na serikali ya Uingereza.

Wakati huohuo, mambo yalikuwa hayamwendei vizuri Téwodros nyumbani. Madaraka yake yaliporomoka sana na ufalme wake ulikuwa unaelekea kuanguka. Waingereza walijua hivyo na waliamua kupambana naye kijeshi mwaka 1867 ili kuwafungulia watu aliowafunga. Jeshi la Uingereza, likiongozwa na Sir Robert Napier, liliwaua askari wengi wa Téwodros ambao hawakutumia vyema mizinga yao. Alipoona hali hiyo ya kutoweza kujiokoa, Téwodros alijiua na hivyo kuepuka kudhalilishwa kwa njia yoyote ile na Waingereza.

Ingawa wafungwa wote walitolewa na malengo ya mapambano kufikiwa, Waingereza bado waliharibu ngome ya Magdala na mengi ya makombora yake, na walimchukua mtoto wa Téwodros na baadhi ya nyaraka. Walimtunza mtawala wa Tigré kwa zawadi ya silaha kwa kushirikiana nao.

Wakati huohuo, nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa ilishuhudia ongezeko la raghba ya Wafaransa katika kuidhibiti bandari ya Oboke. Mnamo 1856 balozi mdogo wa Wafaransa alinunua bandari hiyo, lakini hapakuwa na athari yoyote ya maana. Makubaliano mapya yalitiwa sahihi mnamo mwaka 1862, ambapo machifu wanne wa Afar waliachia nchi yao kwa Wafaransa kwa kiasi kikubwa cha fedha. Mnamo mwaka



15.7 Mfalme Tewodros akijiua mbele ya Sir Robert Napier (tafsiri ya kisasa)

1869, Wamisionari wa Kiitaliano nao walinunua bandari ya Asab kwa niaba ya Wizara ya Bahari ya Italia kutoka kwa machifu wa Afar.

## *Maliki Yohana na ujenzi wa umoja wa Ethiopia*

Ethiopia iligawanywa tena baada ya kifo cha Téwodros. Kati ya watu watatu waliokuwa na madaraka katika kipindi hiki, Kassa wa Tigré ndiye aliyekuwa na nguvu zaidi. Hivyo baada ya kumshinda mtawala wa Amhara, alitawazwa kama Maliki Yohana IV huko Aksum mnamo Januari, 1872.



**15.8** *Mfalme Yohannes IV*

Ili kufanikiwa katika kuunganisha taifa, Yohana aliweka sera ya upatanishwaji na mamwinyi. Kama sehemu ya mageuzi yake ya kidini, alifanya urafiki na makasisi na alichukua mkuu wa kanisa kutoka Misri. Pia, alipeleka fedha kwa jumuiya ya Waethiopia waliokuwa Yerusalemu. Alijenga makanisa mengi mapya, mathalan yale ya Adwa na Magdala. Aliyapatia makanisa ardhi kubwa huko Aksum na alitoa msaada mpya wa fedha kwa ajili ya nyumba ya watawa wa Dabra Bizau. Zaidi ya hayo, alijaribu kuwabatiza Waislamu kwa wingi na alisakama wamisionari wa Kikatoliki. Alijaribu kuongoza maadili ya kidini kwa kupiga marufuku uchawi, uvutaji sigara na ugoro.

Mapambano makubwa ya kivita ya Yohana yalikuwa dhidi ya Misri pale Wamisri, walipojaribu kuingia kwenye dola yake. Baada ya kuwaomba msaada Waingereza dhidi ya Wamisri na kutopata jibu, aliyakusanya majeshi yake mnamo mwaka 1875. Katika pambano lililofuata, karibu wavamizi wote wa Kimisri waliangamizwa. Wamisri walipojaribu kujibu mapigo mnamo 1876, walishindwa vibaya. Ushindi wa Ethiopia haukuzima tu ndoto za Wamisri za kujenga himaya, lakini ulimwaibisha Khedive Ismail kule kwao. Matatizo hayo yalisababisha kuondolewa kwake madarakani mnamo Juni 1879.

Ingawa Ethiopia ilikuwa mshindi lakini nayo pia iliathirika kutokana na mapigano hayo. Sehemu kubwa ilikimbiwa na maeneo mengi yaliharibiwa vibaya. Hata hivyo, ushindi dhidi ya Misri uliongezea hadhi Ethiopia, na Yohana akawa mtawala wa kwanza aliyekuwa na silaha nzuri katika nchi yake, kwani alipata silaha nyingi kutokana na mapigano yake dhidi ya Misri. Kama sehemu ya azma yake ya kuunganisha taifa lake, Yohana alifanya mkataba wa amani na Menelik wa Shoa. Walijadili matatizo ya kidini ya nchi yao na wakakubaliana kushirikiana kuifanya Ethiopia kuwa nchi kamili ya Kikristo. Wakati huohuo, mazungumzo ya amani yaliyoanzishwa na Misri hayakufanikiwa, kwani Yohana alikataa kufikia suluhu na Misri, dola la Kiislamu ambalo lilikataa kuiachilia Massawa, mlango pekee wa Ethiopia wa kuifikia bahari.

Yakijumuishwa, mafanikio ya Yohana kama maliki wa Ethiopia yalikuwa mengi na makubwa. Alileta amani Ethiopia kwa kushughulikia vitisho vya Misri na kuleta umoja nyumbani. Lakini amani hiyo ilivurugwa na matukio ya baadaye kama vile maasi ya Mahdi ya 1881, kutekwa kwa Massawa na Italia mwaka 1885, na kuibuka kwa magonjwa ya kuambukiza na njaa mwishoni mwa karne ya kumi na tisa.

## *Hitimisho*

Utawala wa Yohana, ingawa ndio uliokuwa na nguvu zaidi katika eneo hili na ndio pekee uliojishughulisha sana na mahusiano na nchi za nje, ulihusisha sehemu tu ya nchi iliyozungumziwa katika sura hii. Himaya hiyo iliyokuwa na makao yake makuu Tigré ilienea katika uwanda wote wa juu uliokaliwa na Wakristo. Madola ya Gojam, Shao na Walo yalikiri mamlaka ya himaya hiyo. Usultani wa Ausa uliokuwa mashariki, ulikuwa huru, ambapo mabonde yaliyokuwa kaskazini mashariki na kaskazini magharibi mwa Tigré yalikuwa chini ya Wamisri. Maeneo ya magharibi, kusini na mashariki kama vile majimbo ya Guragé, madola ya Oromo na mengineyo pia yalikuwa na uhuru wao wa kisiasa.

Harar, ambayo ilikuwa kusini mashariki ilikuwa chini ya utawala wa Misri, ingawa Menelik baadaye aliutwaa mji huo. Pwani ya Somalia iliyokuwa kwenye ghuba ya Aden na ambayo ilikuwa chini ya utawala wa Misri, baadaye iliwekwa chini ya Waingereza, Wafaransa na Waitaliano. Bandari nyingine za Somalia zilizokuwa chini ya Oman baadaye ziliwekwa chini ya Waitaliano. Hata hivyo, utawala wa kigeni katika eneo la Somalia uliishia pwani tu.

# 16

# *Bukini (Madagascar) 1800-1880*

## *Utangulizi*

Bukini ya karne ya kumi na tisa ilikuwa na jumla ya makabila 18. Kabila la Wamerina ndilo lililokuwa kubwa na muhimu zaidi kuliko yote. Kabila hili lilikuwa na makazi yake katika uwanda wa juu wa kati. Idadi ya watu katika kundi hili ilikuwa ni moja ya sita tu ya watu wote wa Bukini, lakini ndilo lililotawala kisiwa cha Bukini kabla ya kuchukuliwa na kutawaliwa na Wafaransa. Makabila yote ya Kimalagasi (wenyeji wa Bukini) yalizungumza lugha moja na yalikuwa na mila na desturi zinazofanana, hivyo yaliweza kujenga umoja wa kitamaduni na kikabila uliowafanya wawe jamii moja kimsingi.

Wamerina waliweka makao makuu ya utawala wao mijini Antananarivo; kutoka hapo waliweza kueneza mamlaka yao katika sehemu nyingine za kisiwa hicho. Hivyo mjadala wa historia ya kiuchumi-jamii ya Bukini katika karne ya 19 umejikita hasa katika historia ya Wamerina walioishi kwenye uwanda wa juu wa kati, maana hadi kufikia 1880 walikuwa wanamiliki zaidi ya theluthi mbili ya kisiwa chote.

Katika muktadha huu, tutachunguza matukio makuu mawili yaliyoijenga historia ya Bukini kati ya 1800 na 1880. Tukio mojawapo ni mabadiliko ya kisiasa ya nchi hiyo na uhusiano wa kidiplomasia baina ya dola hiyo iliyokuwa ikibadilika na nchi za kigeni, hasa Ufaransa na Uingereza. Mabadiliko haya ya kisiasa kwa kiasi kikubwa yalihusu uimarishaji wa utawala wa Kimerina na upanuzi wake katika sehemu nyingine kisiwani humo, ilhali uhusiano wake wa kidiplomasia na mataifa mengine makubwa ulikuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi hiyo. Tukio jingine lililohusiana na mabadiliko makubwa ya muundo wa kiutawala na kijamii katika nchi ambayo yalisuhulisha maendeleo ya kiuchumi. Mchakato wa urekebishaji wa mpangilio wa kijamii ulihusu pia usasishaji (kuingia katika usasa), kipengele muhimu katika usasishaji huo kikiwa ni ukumbatiaji wa dini ya kigeni.

## *Kipindi cha Andrianampoinimerina 1792-1810*

Uchunguzi wa namna Andrianampoinimerina, muasisi wa ufalme wa Merina, alivyopata madaraka na kuimarisha nafasi yake katika uwanda wa juu wa kati ni muhimu sana katika kuifahamu historia ya Bukini katika karne ya kumi na tisa.

Mwaka 1875, Andrianampoinimerina alijipa madaraka ya kuwa mfalme wa mojawapo ya falme zilizokuwa zikipigana vita katika Imerina ya kati baada ya kumpindua mtawala aliyepita. Kwa kutumia mbinu za kidiplomasia na za kijeshi aliendelea kuzichukua na kuziingiza tawala za jirani katika himaya yake.

Mnamo mwaka 1792 aliuhamishia mji mkuu wake huko Antananarivo, ambapo alianza kujenga mifumo ya kisiasa na kijamii ya ufalme mpya. Baada ya 1800 alianzisha sera ya kuyapiga vita majimbo mengine visiwani humo kwa nia ya kuyaunganisha makabila yote 18. Katika kutimiza jukumu hili, alikabiliana na upinzani wa hali ya juu kutoka katika makabila mengine kisiwani humo kama vile Wasakalava, Wabezanozano na Waambongo. Hata hivyo, wakati wa kifo chake hapo 1810, Andrianampoinimerina alikuwa tayari ameifanya Imerina kuwa pengine ni ufalme wenye nguvu zaidi kuliko falme zote katika kisiwa cha Bukini.

## *Mwanausasa mkubwa: Mfalme Radama I (1810-28)*

Mfalme Radama alirithi kiti cha ufalme mwaka 1810 akiwa na umri wa miaka 18. Jukumu lake la kwanza kabisa baada ya kushika ufalme lilikuwa ni kuyapiga makundi ya ndani ya ufalme huo yaliyoasi. Kwa kufanya hivyo, alifanikiwa kuiimarisha nafasi yake katika Imerina. Hata hivyo, mafanikio yake makubwa zaidi yalihusiana na upanuaji wa mipaka. Alitafuta njia moja kwa moja hadi baharini ili kufanikisha biashara baina yake na Wazungu na kuupanua utawala wa Merina.

Shauku ya Radama kuifikia bandari ya Tamatave ambayo ilikuwa ikidhibitiwa na utawala wa kichifu ilimlazimisha afanye mawasiliano ya kidiplomasia na Gavana wa Mauritius, Bwana R.T. Farquhar. Kwa bahati, Farquhar pia alikuwa na shauku ya kuendeleza utawala wa Waingereza hapo Bukini au angalau kuathiri hali ya mambo nchini humo. Hali hii ilisababisha kuzuka kwa mikataba mingi baina ya Radama na watawala wa Uingereza waliowakilishwa na Gavana wa Mauritius. Matokeo ya mikataba hii ni kuanzishwa kwa makazi ya Waingereza huko Bukini mwaka 1820 kwa kuteuliwa Bwana James Hastie kuwa balozi mkazi wa Kiingereza kisiwani humo.

Mikataba ya kidiplomasia kati ya Radama na Waingereza ilitoa msukumo wa kuendeshwa kwa shughuli za kimisionari kisiwani humo. Chama cha Wamisionari cha London (*London Missionary Society*) kiliingia mjini Antananarivo mwaka 1820 na kilitoa mchango mkubwa Bukini katika uwanja wa elimu na msaada wa kiufundi. Walifungua shule ya kwanza mnamo mwaka 1820 ikiwa na wanafunzi 3 na kwa kuungwa mkono na Radama, hadi 1829 kulikuwa na shule 23 zenye wanafunzi 2,300. Wamisionari waliifasiri Biblia katika lugha ya Kimalagasi ambayo tayari waliweza kuiandika. Hivyo, ukuaji wa elimu si tu kwamba ulisaidia ueneaji wa dini ya Kikristo na kisomo, bali pia ulisuhulisha kukua kwa lugha na fasihi ya Kimalagasi kama chombo cha umoja wa kitaifa kisiwani Bukini.

Zaidi ya hayo, wamisionari waliwapeleka vijana wa Bukini Uingereza au Mauritius ili kupata elimu ya ufundi. Aidha walianzisha stadi mbalimbali kama useremala, ujenzi, utengenezaji ngozi, utengenezaji vitu mbalimbali kwa kutumia bati na ufumaji kisiwani Bukini. Mmojawapo wa wamisionari hao, Bw. James Cameroun, aliwasaidia sana




**16.1** *Upanukaji wa ufalme wa Merine (1810-40)*

Wamalagasi katika kutoa elimu ya ufundi. Wake wa wamisionari hawakubaki nyuma katika kusaidia jambo hili. Walitoa maelekezo yenye maana kwa kaya za wenyeji kuhusu utunzaji wa nyumba, na pia walikuwa wabunifu na watengenezaji wa nguo zilizovaliwa na wanawake wa tabaka tawala.

Msaada muhimu sana wa kiufundi kuliko yote ambayo Radama aliupata ulikuwa katika jukumu la kujenga jeshi. Waingereza walimsaidia kulifundisha jeshi lake kwa kufuata mfumo wa jeshi lao. Aidha walimsaidia kununua bunduki kwa ajili ya matumizi ya jeshi hilo. Matokeo ya msaada huo ni kuwa Jeshi la Radama lilikuwa ndilo zuri kuliko yote kisiwani humo kwa nidhamu na vifaa vya kijeshi, hali iliyopelekea kufanikisha mipango yake ya upanuzi wa himaya.

Jeshi lake si tu kuwa lilitumika kuyapiga majimbo mengine bali pia kudumisha sheria na utulivu katika maeneo yaliyotekwa. Hadi 1825, Radama alikwisha kuliteka eneo lote la pwani ya mashariki ya Bukini kuanzia Vohema hadi Ngome ya Dauphin. Aidha aliishinda sehemu kubwa ya magharibi, ila ilikuwa vigumu kuiteka Sakalava. Lakini pamoja na hayo yote, hadi 1823 Radama aliweza kuupanua utawala wa Merina katika sehemu kubwa sana ya kisiwa hicho. Ingawa utawala wake katika kisiwa hicho chote haukukamilika, hakukuwa na kipingamizi chochote kikubwa dhidi ya kujitangaza kwake kuwa mfalme wa Bukini. Alifariki 1828 akiwa na umri wa miaka 36.

## *Ranavalona I (1828-1861): Upingaji wa mabadiliko au uimarishaji wa utawala?*

Malkia Ranavalona I alikuwa ni binamu na mke wa kwanza wa Radama I. Kwa kuwa alisaidiwa kupata umalkia na makabaila na wakuu wa majeshi ambao Radama aliwaondoa madarakani katika harakati zake za kukijenga kisiwa hicho upya, washauri wake walikuwa ni watu waliozipinga sera muhimu za mfalme aliyefariki. Mkazo wa sera za Ranavalona ulikuwa ni kuulinda uhuru wa Bukini dhidi ya taathira za kigeni, hasa zile zilizoathiri asasi za kitaifa, mila na desturi. Kuhusu sera ya mambo ya nje, aliegemea zaidi katika kuitoa nchi yake kutoka kwenye taathira ya Waingereza, hasa katika nyanja za siasa na dini.

Katika uwanja wa dini, viongozi wa Bukini walijaribu kuipiga marufuku dini ya Kikristo iliyokuwa inaenea tangu enzi za Radama. Waligundua kuwa dini ya Kikristo ilikuwa inazihujumu asasi zao za kijadi, hasa utawala wa kifalme. Ukristo uliitikisa misingi ya madaraka ya kifalme kwa kukataza kuabudu Mungu-mtu aliyesaidikiwa kuwa ndiye aliyehusika na ustawi wa nchi. Kanuni zake za usawa pia zilipingana na mgawanyiko wa kiasili wa makundi ya jamii. Mambo haya yote yalimfanya malkia achukue hatua kali dhidi ya ueneaji wa dini ya Kikristo na hadi kufikia 1835 dini hiyo ilipigwa marufuku rasmi. Wakristo wengi waliteswa, na baadhi yao walikufa kama mashahidi; lakini pamoja na hayo, dini hiyo haikutoweka kabisa bali ilikuwa ikiendeshwa kichinichini. Hakika hiki kilikuwa ni kipindi kigumu sana kwa dini ya Kikristo kisiwani Bukini.

Kufuatana na sera hizi, Ranavalona alimuomba Balozi Mkazi wa Kiingereza



**16.2** *Andrianampoinimerina, d. 1810*



**16.3** *Mfalme Radama I, 1810–28*



**16.4** *Malkia Ranavalona I, 1828–61*



**16.5** *Mfalme Radama II, 1861–3*



**16.6** *Malkia Rasoherina, 1863–8*



**16.7** *Malkia Ranavalona II, 1868–83*

kuondoka Bukini mwaka 1828. Aidha aliwanyang'anya vyeo vyao raia wa Uingereza wenye nyadhifa muhimu walioishi kisiwani. Zaidi ya hayo alibatilisha mikataba yote iliyowekwa baina ya nchi yake na Uingereza. Lakini baada ya viongozi wa Bukini kugundua baadaye kuwa nchi yao ilihitaji mawasiliano na sehemu nyingine za dunia ili kuweza kupata bidhaa za viwandani kama vile bunduki, zana za vita na bidhaa nyinginezo za anasa, mwaka 1836 walituma ujumbe kuweka mikataba ya kirafiki na Uingereza na Ufaransa. Kutofanikiwa kwa ujumbe huu, kukifuatiwa na shambulio lililofanywa na Waingereza na Wafaransa kwa pamoja huko Tamatave mwaka 1845, ndiko kulikomfanya Ranavalona kuwafukuza wafanyabiashara wageni wote na kusimamisha biashara na nchi za nje, hasa uuzaji wa bidhaa za nyama ya ng'ombe na mchele huko Mauritius na Réunion.

Kukoma kwa biashara na nchi za nje isipokuwa Marekani kulizaa utamaduni wa kujitegemea miongoni kwa Wamalagasi. Waliendelea kuikuza elimu ya Wazungu na kuwatumia raia wa nje kama vile William Marks kutoka Marekani na de Lastelle na Jean Laborde, hasa Laborde, kutoka Ufaransa, kuanzisha viwanda kwa ajili ya kutengeneza bidhaa muhimu ambazo hawakuweza kuziagiza tena kutoka nje ya nchi. Kutokana na hali hiyo, miradi mingi ilianzishwa kama vile mashamba ya miwa na kiwanda, na mkusanyiko wa viwanda vilivyotengeneza bidhaa mbalimbali kuanzia bunduki, mizinga, vioo, mvinyo uliotengenezwa kutokana na miwa; na sabuni.

Malkia Ranavalona aliendelea na upanuzi ambao Radama I aliuanzisha na kuimarisha utawala wake katika majimbo aliyoyateka. Kabila la Wasakalava liliendelea kuupinga utawala wake. Hatimaye majeshi ya serikali yalipowashinda machifu wa Sakalava, walikimbia na watu wao na kwenda kwenye visiwa vya jirani ambapo walijiweka kwenye hifadhi ya Wafaransa. Hali hii baadaye ilikuwa ndiyo msingi wa madai ya Wafaransa kwa majimbo yaliyoko magharibi mwa Bukini.

Muongo wa mwisho wa utawala wa Malkia Ranavalona ulishuhudia mabadiliko makubwa ya sera za Bukini. Hali hii ilisababishwa na kifo cha Rainiharo, ambaye alikuwa mkuu wa serikali tangu 1830, mwaka 1852; na kuzuka kwa vijana katika siasa za Bukini ambao hawakukubaliana na mawazo ya washauri waliopita wa Malkia ya kutotaka mabadiliko. Vijana mashuhuri kati ya hawa walikuwa ni watoto wa kiume wa Rainiharo. Mtoto mkubwa, Rainilahiarivony, baadaye alikuwa mtawala kivuli kuanzia 1864-1896, wakati mdogo wake alipokuwa mkuu wa jeshi. Aidha alikuwemo Rakoto Radama, mwanamfalme mtarajiwa. Mtazamo wao ulikuwa ni wa Kizungu na walihakikisha kuwa wanabadilisha sera za Ranavalona. Kupigwa marufuku kwa biashara kati ya Bukini na visiwa vya Réunion na Mauritius kuliondolewa mnamo 1853. Wamisionari waliruhusiwa kuingia tena nchini mnamo 1856. Mwaka 1857 kulikuwa na jaribio la kumpindua Malkia ambapo mwana wa mfalme alikuwa mshiriki lakini jaribio hilo halikufanikiwa. Ranavalona alifariki 1861 baada ya kumtangaza Rakoto Radama kuwa ndiye atakayetawala baada yake.

Utawala wake unaweza kuelezwa katika namna mbili. Kwa upande mmoja, ulikuwa ni utawala wenye vitisho kwa wamisionari na watu wengine waliotekwa na kuwa chini ya utawala wa Kimerina. Kwa upande mwingine, kilikuwa ni kipindi cha maendeleo

makubwa ya viwanda, na ambacho kiliimarisha elimu ya Kizungu na kuiweka nchi katika mwelekeo wa usasa. Kwa jumla, kwa raia zake wengi, Ranavalona alikuwa ni ishara ya utaifa wa Kimalagasi.

## *Sera ya Uwazi: Mfalme Radama II 1861-1863*

Shughuli za mfalme Radama II zilielekezwa katika kuzibadilisha sera zote zilizokuwa zinapinga mambo yaliyoletwa na Wazungu ambazo mfalme aliyetangulia alikuwa akizitumia. Mwelekeo huu ulisababisha upinzani mkubwa dhidi ya utawala wake kutoka kwa watu mashuhuri nchini humo, hali iliyosababisha kuanguka kwake.

Radama alikuwa na shauku ya kuiendeleza nchi yake kwa kuvutia wafanya biashara wa nje, wawekezaji na wamisionari. Katika hali hii aliwaita nyumbani Wamalagasi Wakristo wote waliokuwa wamefukuzwa Bukini. Hii ilipelekea hata Wazungu wamisionari wengine kuanza kurudi polepole nchini Bukini. Wamisionari wa makanisa yote mawili, la Waroma (RC) na Chama cha Wamisionari wa London (LMS) walifika katika mji mkuu na kuanza shughuli zao. Kadhalika, mfalme alianzisha tena uhusiano wa kidiplomasia na nchi za Uingereza na Ufaransa ambazo ziliwateua mabalozi na kuweleta Bukini.

Hata hivyo, matatizo yalianza wakati Radama alipofanya mikataba mingi ya kirafiki na kibiashara na mataifa makubwa ya Ulaya na kuyapa tahafifu na upendeleo mkubwa kiasi cha kuwafadhaisha na kuwatisha maofisa wa Kimalagasi. Sera ya mfalme ya kusaini mikataba ya siri bila ya maofisa wake kufahamu iliongeza mashaka zaidi kwa viongozi hao. Zaidi ya hayo, kuongezeka kwa athari za wamisionari na Wazungu wengine kitalani kwa mfalme hakukusaidia kitu. Mfalme aliwategemea sana watu hao kutoka nje ya nchi katika uendeshaji wa serikali kama ilivyoonyesha katika uteuzi wake wa Mmarekani na Mfaransa kuwa makatibu wa nchi katika masuala ya mambo ya nje mnamo 1862.

Jambo lililommaliza kabisa ni jaribio lake la kuwaondoa baadhi ya maafisa waandamizi wa nchi ambao ndio walikuwa uti wa mgongo wa serikali yake na badala yao kuwaweka marafiki zake wa ujanani. Hili lilifufua mlolongo mrefu wa malalamiko dhidi ya mfalme, na tarehe Mei 12, 1863 akauawa.

## *Sera za Bukini zafanyiwa marekebisho 1863-1868*

Baada ya kifo cha Radama II, madaraka halisi ya serikali ya Bukini yaliingia mikononi mwa maafisa wakuu wa utawala, ambao walimtawaza Malkia Rasoherina kama mtawala kibaraka. Watu hawa hawakupinga uendelezaji wa nchi na wala hawakuwachukia Wazungu. Lakini sera yao ya mambo ya nje ililenga katika kuakisi uhuru wa nchi yao kwa imani kwamba uendelezaji wa nchi kulingana na wakati usifanywe kwa namna itakayoua mila za Kimalagasi. Hivyo, serikali mpya iliazimia kufanya marekebisho muhimu katika sera za Radama.

Walibatilisha tahafifu zote za kibiashara zilizotolewa na Radama kwa Wazungu. Aidha waliichunguza upya mikataba iliyowekwa baina ya nchi hiyo na Ufaransa na Uingereza ili kuuondoa upendeleo mkubwa uliokuwa ukitolewa katika kumiliki ardhi na



*16.8 Jumba la Malkia huko Antananarivo lilianzwa mwaka 1839 na Jean Labonde kwa kuombwa na Malkia Ranavalona I*

misamaha ya ushuru iliyokuwa ikitolewa kwa wafanya biashara Wazungu kisiwani Bukini. Maamuzi haya hayakuwazuia raia wa kigeni waliohitaji kuja kutoa msaada katika miradi ya maendeleo nchini humo na wala hayakuwafukuza wamisionari, ingawa shughuli zao ziliruhusiwa kufanyika katika baadhi ya miji tu. Hata hivyo, katika utekelezaji wa sera hizi, utawala wa Bukini ulikumbana na vikwazo vikubwa, hasa kutoka nchi za nje.

Uingereza na Ufaransa zilipokea taarifa za kupinduliwa kwa Radama na mapendekezo ya mabadiliko ya sera ya mambo ya nje ya Bukini kwa hisia tofauti. Wakati ambapo Uingereza ilikataa kuhusishwa katika ugomvi na Bukini kwa sababu ya mapendekezo ya marekebisho ya mikataba baina ya nchi mbili hizo, Ufaransa iliumizwa na kuchukizwa sana na hatua hizo za Bukini. Ufaransa ilifahamu kwa uhakika kabisa kuwa ingepoteza mambo mengi zaidi iwapo mikataba iliyokuwepo ingefanyiwa marekebisho, hivyo ilisisitiza kulipwa fidia na Bukini kabla haijayakubali marekebisho yoyote yale. Mkataba mpya baina ya Uingereza na Bukini ulitiwa saini mnamo 1865, na ule wa Bukini na Ufaransa ulisainiwa 1868. Katika Mikataba yote miwili, Wamalagasi walifanikiwa kupata madai yao yote, na hasa lile la kubatilishwa upendeleo wa kumiliki ardhi uliotolewa kwa Wazungu. Hata hivyo, mwenendo wa Uingereza wa kukubali mara moja mapendekezo ya Bukini wakati wa mgogoro huo uliifanya Uingereza

ipendwe zaidi na Wamalagasi, ilhali uhasama wa Ufaransa na madai yake ya gharama kubwa vilichochea upinzani dhidi yake. Hali hii iliathiri uhusiano wa baadaye baina ya Wafaransa na Wamalagasi.

## *Maendeleo ya ndani ya nchi 1861-1880*

Sasa tuangalie maendeleo ya kiuchumi-jamii na ya kiutawala kisiwani Bukini kati ya 1861-1880. Mojawapo ya matukio muhimu yaliyoathiri maendeleo ya baadaye nchini humo ni ya kugeuzwa kwa viongozi wake kuwa Wakristo. Ueneaji wa haraka wa shughuli za Wamisionari kisiwani humo baada ya 1861 na kuonekana kwa mafanikio mazuri kutokana na hali hiyo, kuliliwezesha kundi la Wakristo kuwa lenye nguvu na kubwa nchini humo.

Lilikuwa ni kundi ambalo lisingeweza kudharauliwa na kutotiliwa maanani hasa kwa kuwa wengi wa wananchi maarufu walikuwa katika kundi hilo. Matokeo ya hali hiyo ni kwamba ili kuziimarisha nafasi zao na kuungwa mkono na Wakristo, viongozi muhimu wa Bukini, Malkia Ranavalona II na Waziri Mkuu Rainilahiarivony, ambaye pia alikuwa mumewe, kama alivyokuwa kwa malkia aliyepita, Rasoherina, waliukubali Ukristo mwaka 1869.

Ni jambo muhimu kuwa Ukristo wa aina ya Uprotestanti ndio walioupokea viongozi wa Bukini, maana ulikuja mara tu baada ya kukamilisha mkataba baina ya Ufaransa na Bukini mnamo 1868, mkataba ambao ulitanguliwa na uadui mkubwa ulioonyeshwa na Wafaransa. Viongozi wa Kimalagasi waliuona Uprotestanti kuwa dini ya Waingereza na Ukatoliki kuwa dini ya Wafaransa. Hivyo kuukubali Uprotestanti kulikuwa ni kuimarisha urafiki wao na Waingereza na kuukataa utamaduni na athari ya Wafaransa kisiwani humo.

Kipindi hiki pia kilishuhudia wimbi la mzinduko wa kidini kisiwani humo. Wakatoliki walizidisha juhudi zao za kuwafikia wananchi wa kawaida vijijini na walifanikiwa sana katika jambo hilo katika jimbo la Betsileo.

Zaidi ya hayo, kulikuwepo pia na mzinduko wa dini za kiasili na uenezaji wa dini hizo uliofanywa na makuhani wake katika kupambana na ueneaji haraka wa dini ya Kikristo. Kwa mchanganyiko huu wa imani za kidini, Bukini katika nusu ya pili ya karne ya 17 ilikumbwa na homa ya kidini.

Vyama vya kimisionari, hasa vya Waingereza, kwa kushirikiana na serikali, vilipata mafanikio makubwa katika jamii ya Wamalagasi. Mafanikio yao makubwa sana yalikuwa katika nyanja za elimu, usanifu majengo na huduma za matibabu. Katika uwanja wa elimu, shule nyingi zilifunguliwa na uamuzi wa kwamba kila mtoto wa umri wa miaka saba ni lazima aende shule ulitolewa mnamo mwaka 1881. Inasemekana kuwa uwiano wa watoto wa Kimalagasi waliokwenda shule katika miaka ya 1880 ulikuwa karibu sawa na ule wa nchi nyingi za Ulaya. Idadi kadhaa ya wanafunzi pia walipelekwa nje ya nchi kwa ajili ya masomo zaidi. Maendeleo haya ya elimu yalisuhulishwa pia na idadi (kubwa) ya mashine za uchapaji zilizowekwa na mashirika ya kidini ambayo yalichapisha vitabu, magazini na magazeti.

Badiliko jingine muhimu la kijamii ambalo lilitokea wakati huu lilikwa ni uanzishaji

wa kalenda ya Gregori, uliofanywa na Wamisionari Waingereza mnamo mwaka 1864. Kalenda hiyo ilichukua nafasi ya kalenda ya kiasili iliyofuata majira ya mwezi.

Kulikuwepo pia na uigaji wa usanifu majengo kutoka kwa wamisionari, hasa uliotokana na kujengwa kwa makanisa mengi na minara ya kumbukumbu kwa mashahidi wa dini. Hayo yalifanywa ili kuuwezesha mji mkuu, Antananarivo, kuwa mji mtakatifu. Huduma za matibabu zilianza kutolewa Bukini na Chama cha Kimisionari cha London (*London Missionary Society*) kwa kufunguliwa kwa zahanati mnamo mwaka 1862, na hospitali mwaka 1865, katika mji mkuu. Mwaka 1875 serikali ya Bukini ilianzisha utoaji huduma za matibabu zilizotolewa na wafanyakazi waliokuwa wanalipwa mishahara. Hadi kufikia 1880 Bukini ilikuwa tayari imeanza kuwapata madaktari bingwa wa kwanza nchini humo. Mbali na kuenea kwa dini ya Kikristo na shughuli nyingine za misioni za Kikristo, kipindi hicho pia kilishuhudia maendeleo muhimu katika nyanja za kikatiba na kiutawala kisiwani Bukini. Kulikuwa na mabadiliko kutoka kwenye utawala wa binafsi wa kifalme hadi kwenye utawala wa kikatiba. Hali hii ilitokea kwa sababu ya madaraka kuponyoka kutoka mikononi mwa ufalme wa Kimerina na kuingia mikononi mwa kikundi cha watawala wa Kihova. Wafalme wa Kimerina waliendelea kutawala katika kipindi hiki, lakini utawalaji wenyewe na utamalaki wa mamlaka na madaraka ya kiserikali ulikuwa mikononi mwa kikundi cha watawala wa Kihova ambao walihodhi nafasi za juu za utawala nchini humo. Kwa kadiri muda ulivyopita, malkia hakuweza tena kutawala kufuatana na hiari yake. Mwaka 1864 Waziri Mkuu alikuwa na nguvu ya utawala na hivyo kumpita Malkia kimadaraka na kuwa mtu maarufu zaidi nchini humo, hasa aliposhika uongozi wa jeshi na kumwoa Malkia.

Kuhusu maendeleo ya kiutawala, orodha ya sheria zenye jumla ya ibara 101 ilikuwa imekwisha kutangazwa hadi 1868 na kufikia 1881 ibara ziliongezeka na kufikia 305. Azma ya jambo hili ilikuwa ni kuhifadhi amani na utawala wa sheria, na kuboresha utendaji kazi wa vyombo vya utawala vya nchi hiyo. Kulikuwepo pia na marekebisho katika uendeshaji wa utoaji haki. Katika mji mkuu kulianzishwa mahakama kuu tatu, kila moja ikiwa na majaji 13. Mahakimu na wakuu wa vijiji walisimamia utoaji haki katika majimbo yao. Hata hivyo, uamuzi wa mwisho katika kesi zote ulikuwa mikononi mwa Waziri Mkuu. Ingawa utaratibu huu ulimlimbikizia majukumu mengi mtu mmoja, lakini pia uliiwezesha serikali kuu kufahamu kinachotokea katika majimbo. Aidha, mpangilio wa mfumo wa kiserikali ulibadilishwa kwa kuunda baraza la mawaziri lililokuwa na mawaziri wanane.

Kulikuwepo pia mabadiliko katika jeshi. Mnamo 1872, Waziri Mkuu alizifufua sera zilizokuwepo zamani za kulibadilisha jeshi kuwa la kisasa. Huku ikisaidiwa na Mkufunzi wa Jeshi la Waingereza, serikali iliwaajiri askari, iliwapa mafunzo ya kijeshi na iliweza kujenga jeshi la kitaalamu. Silaha nyingi ziliagizwa kutoka Uingereza na Marekani kwa ajili ya kutumiwa na jeshi hilo, na silaha ndogondogo zilitengenezwa nyumbani ili kuhifadhi fedha za kigeni. Mabadiliko ya kijeshi yaliyoletwa 1876 yalijumuisha ukomeshaji wa utumiaji mbaya wa mfumo wa wapambe. Mwaka 1876 kulianzishwa mtindo wa kulitumikia jeshi kwa mujibu wa sheria kwa kipindi cha miaka mitano. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa jeshi imara sana ambalo lilikuwa ni chombo



*16.9 Kitanda chenye paa (aina ya machela yenye paa) cha Malkia Rasoherina. Nyuma ni kanisa la Kiprotestranti lililojengwa wakati wa Rasoherina na Ranalona II*



**16.10** *Makao ya Ranavalona aliporudi kutoka Fianarantsoa, 1873*

muhimu cha kuwapiga waasi waliogoma katika majimbo.

Mambo mengine yaliyofanywa ili kuijenga kisasa Bukini ni: Upigaji marufuku wa biashara ya pombe; utekelezaji wa amri ya kupiga marufuku biashara ya watumwa na utumwa wenyewe, na kuondolewa kwa sheria za ukandamizaji. Hata hivyo, baadhi ya Waingereza na Wafaransa waliiasi serikali ya Bukini na kuendelea na biashara ya watumwa. Mnamo 1877, serikali ya Bukini iliwaachia huru watumwa wote 150,000 kisiwani humo.

## *Maendeleo ya Kiuchumi*

Kabla ya Bukini kuanza kushiriki kwenye biashara ya kimataifa, na hasa kabla ya kuwasili kwa Wazungu wengi kisiwani humo mwaka 1860, Bukini ilikuwa na uchumi wa kujitegemea. Walizalisha karibu kila kitu walichokihitaji. Idadi kubwa ya watu kisiwani humo ilijihusisha na kilimo. Mchele ndicho kilikuwa chakula kikuu kisiwani humo na mpunga ulilimwa kwa kiwango kikubwa kiasi cha kuwafanya Wamalagasi wawe wataalamu katika ulimaji wake. Aidha walifuga mifugo kama vile kondoo na nguruwe, na samaki walikuweko kwa wingi; lakini katika mifugo yote ng'ombe ndio waliokuwa muhimu zaidi. Mchele na nyama ya ng'ombe ndizo zilizokuwa bidhaa muhimu zilizosafirishwa nje ya nchi. Wamalagasi pia walianzisha viwanda vya

usokotaji nyuzi na ufumaji, uchimbaji madini na uhunzi. Kama ilivyoonyeshwa hapo awali, katika miaka ya 1830 eneo kubwa la viwanda lilijengwa huko Mantasoa ambapo aina mbalimbali za bidhaa zilitengenezwa chini ya usimamizi wa Jean Laborde.

Kutawazwa kwa Mfalme Radama I kulikuwa ndiyo chanzo cha Bukini kujihusisha kikamilifu katika biashara ya kimataifa. Vitu muhimu vilivyoingizwa kisiwani humo ni watumwa kutoka bara la Afrika. Usafirishaji huu wa binadamu kutoka bara ulikomeshwa rasmi mwaka 1847, lakini uliendelea kwa miaka kadhaa baada ya hapo kabla ya kutokomea kabisa. Bidhaa nyingine ziliizoingizwa kisiwani Bukini ziliijumuisha nguo, bunduki, pombe ya miwa na mashine, na bidhaa zake kuu zilizosafirishwa nje ya nchi zilikuwa mchele na nyama ya ng'ombe. Katika karne ya kumi na tisa Bukini ilifanya biashara na Uingereza, Ufaransa, Réunion, Mauritius, Zanzibar, Ushelisheli na Marekani.

Biashara hii ya kimataifa ilijikita katika mikataba ya urafiki na biashara. Mwaka 1862 mikataba hiyo ilifanywa na Uingereza na Ufaransa, na baadaye ilidurusiwa katika mwaka 1865 na 1868. Mnamo mwaka 1867 mkataba mwingine uliwekwa baina ya nchi hiyo na Marekani.

Bukini pia ilianzisha ofisi ya ubalozi katika nchi za Mauritius, Uingereza na Ufaransa ili kufanikisha shughuli za biashara. Kisiwa hicho pia kilihimiza ushiriki wa watu binafsi katika biashara ya kimataifa, ingawa dola ndiyo iliyokuwa mstari wa mbele katika suala hilo. Wafanyabiashara kutoka nje ya nchi walipewa tahafifu katika kuwavutia ili wawekeze mali zao nchini humo, lakini hawakuruhusiwa kabisa kumiliki ardhi.

## *Hitimisho*

Katika sura hii tumechunguza namna Bukini ilivyobadilishwa na kuwa nchi ya kisasa - mabadiliko yaliyoanzishwa na Mfalme Radama I mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Mchakato huu wa usasishaji ulihusisha pia hatua za kuhimiza biashara na athari za nje, kukubali Ukristo, na kutekeleza mabadiliko fulani yaliyolenga katika kuzitumia rasilimali na nguvukazi za nchi kwa ajili ya kupata maendeleo zaidi katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Umuhimu wa suala hili ni kuwa kabla mataifa makubwa hayajaigombania Bukini, kisiwa hicho hakikuwa masikini na kisichokuwa na maendeleo, na kiliweza kujitawala.

Hivyo, haja ya kuwa na utawala kutoka nje ya nchi haikuwepo. Lakini pamoja na yote hayo, kisiwa hicho hatimaye kiligeuzwa kuwa koloni. Hii ni kwa kuwa, ingawa sera ya kuisasisha Bukini kwa namna fulani iliimarisha uwezo wa nchi hiyo wa kutetea uhuru wake, lakini kwa jumla sera hiyo ilidhoofisha ufalme huo kwa kuongeza utegemezi wake kwa mataifa ya kigeni.

# 17

## *Sura mpya ya maendeleo ya maghrib: Algeria, Tunisia na Libya*

### *Utangulizi*

Maghrib ilikumbana na misukosuko mikubwa katika karne ya 19. Mojawapo ya matukio hayo muhimu ni kupokonywa kwa uhuru wa nchi hizo na mataifa ya Ulaya. Algeria ilishindwa na Wafaransa mnamo 1830. Libya iliangukia tena katika utawala wa Ottoman mwaka 1835, na baadaye kuvamiwa na Waitaliano mwaka 1911. Tunisia iliwekwa chini ya himaya ya Wahispania mnamo mwaka 1881, na Moroko ilivamiwa na Wafaransa pamoja na Wahispania mnamo mwaka 1912. Matukio haya yaliwasilisha, ama upeo, ama, kwa baadhi yake, kitangulizi cha mikondo mipya ya mabadiliko ambayo iliathiri hali ya jamii kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Hivyo, sababu za kutokuendelea kwa Afrika ya Kaskazini katika kipindi hiki zisitafutwe tu katika mazingira ya nchi hizo, bali pia katika hali ya ujumla ya ulimwengu wa nje, hususani Ulaya, kwani hali ya "kutokuendelea kwa Afrika" inahusiana sana na "kuendelea" kwa Ulaya.

Katika sura hii, tutachunguza misingi ya jamii katika Maghrib na pia kutathmini uimara na udhaifu wake mwanzoni mwa Karne ya 19. Zaidi ya hayo tutatazama pia hulka na matokeo ya athari za Wazungu katika Maghrib kufuatana na hali mbalimbali za nchi hizo.

Maghrib katika kipindi hiki ilijumuisha Moroko na tawala tatu za ufalme wa Ottoman ambazo ni Algeria, Tunisia na Libya. Msisitizo utawekwa katika sifa za jumla za tawala hizi tatu na katika hulka ya jamii katika nchi mbalimbali.

### *Dola la Makhzen mwanzoni mwa karne ya 19*

Sifa kuu ya dola la Makhzen kwenye miji ya Algiers, Tunis na Tripoli ni kuwa halikuchanganyika na watu lililowatawala. Watu walioshika madaraka na mamlaka walijiona kuwa wako tofauti kabisa na wale waliowatawala. Watu hawa walikuwa Waturuki na Mamluki waliokuwa wamesimilishwa kwa viwango tofauti tofauti katika jamii walizozitawala. Mamluki walikuwa watumwa wa Kikristo ambao walisilimishwa na kupewa mafunzo maalumu ili kuweza kufanya kazi katika kitala au jeshi. Zana kuu za serikali kama vile fedha, silaha za kisasa, karatasi za kuandikia na mbinu za utunzaji vitabu viliigwa na kuchukuliwa kutoka nje ya jamii hiyo. Hivyo Makhzen iliwakilisha



**17.1** *Eneo la ndani ya Msikiti wa Ketchwawa jijini Algiers mwaka 1833 (Msikiti ulijengwa 1794)*

hatua ya kati baina ya "usasa" wa Waturuki au Wazungu na "ujadi" wa jamii za wenyeji katika jimbo hilo.

Dola hilo liliweza kuzinyonya jamii zilizoishi vijijini kwa kushirikiana na watu mashuhuri katika miji, hali ambayo, kwa kiasi kikubwa ilizifanya jamii za vijijini kuwa na hali duni na hata kudidimia zaidi kiuchumi.

Kabla ya kuingia kwa wakoloni, dola la Makhzen liliungwa mkono kwa kiasi kikubwa na makundi ya wapiganaji, watu mashuhuri walioishi mijini, familia maarufu za vijijini na viongozi wa kidini kama vile maulama (wanazuoni), wacha Mungu na wakuu wa jumuiya mbalimbali mijini na vijijini. Zaidi ya hayo, kiwango cha uungwaji mkono ambacho utawala huo uliweza kukipata kiliukilia si tu hulka ya utawala huo bali pia uwezekano wake wa kuendelea kutawala. Hivyo, huko Algiers, kuzuka kwa vikosi maalumu vya askari wa Kituruki, na magavana wa Kilevanti, kulizihujumu juhudi zote za kuiunganisha serikali katika jamii (ya wenyeji), ilhali huko Tunis na Tripoli kwenye miongo ya kwanza ya karne ya 18, watawala tayari walikuwa wamesimilishwa zaidi katika (jamii za) nchi walizozitawala.

## *Jamii ya mijini*

Licha ya kuwepo kwa mfumo wa kiukoo na utamaduni wa Kiislamu unaofanana katika Maghrib, hadi kufikia karne ya 18 tayari jamii hiyo ilikuwa ya mchanganyiko ambapo mtu angeweza kutofautisha kati ya watu wa mijini, watu wa makabila mbalimbali walioishi vijijini, na wakazi wa nyanda za juu, hasa Waberiberi walioishi milimani. Kulikuwepo na miji mikubwa mingi, kwa sababu wakati mji ulikuwa ni kielezo muhimu cha utamaduni wa Kiislamu. Hata hivyo, katika majimbo yote ya Maghrib, ni Tunisia pekee ambapo maisha ya mjini yalikuwa yamejengeka vizuri. Baadhi ya miji mikubwa nchini humo wakati huo ilikuwa ni Rabat, Fez, Tripoli, Tilimsan, Algiers, Konstantini, Tunis, Susa na Kayrawan. Miji hii ndiyo iliyokuwa vituo vikuu vya shughuli muhimu na zenye faida kubwa kama vile biashara, sanaa za ufundi, mafunzo ya dini, utamaduni na elimu ya jumla; kadhalika uendeshaji wa shughuli za siasa, utawala na jeshi, maana mamlaka ya dola yalijikita zaidi mijini. Hivyo, maisha ya mjini yalihusisha pia uchumi wa kifedha, utamaduni wa usomaji wa fasihi, na ubinafsi katika mahusiano ya binadamu, tofauti na maisha ya jamii za vijijini zilizoishi kwa mshikamano na kutegemeana.

Hata hivyo, jamii hii iliyoishi mijini haikuweza kuibadilisha nchi nzima. Hii ni kwa kuwa tabaka la kati la Maghrib ambalo lilikuwa na jukumu hilo lilikuwa na udhaifu mwingi. Maendeleo yake yalikwamishwa na ukinzani wa jamii zilizoishi vijijini ambazo hazikutaka kushirikiana na tabaka hilo; ushindani mkubwa kutoka kwa mabepari wa Kizungu; na sera za ukiritimba za dola ambazo zililidhoofisha tabaka la kati kwa kuziwekea vikwazo shughuli zake za biashara. Hivyo watu wa tabaka hili walioshughulika na biashara na sanaa za ufundi walipata matatizo kuendesha shughuli zao katika misingi ya uhuru. Zaidi ya matatizo haya, tabaka hili la kati vilevile halikuwa na teknolojia ya kuliwezesha kuongoza nchi nzima katika kufanya mabadiliko makubwa kama yaliyokuwa yakitokea Ulaya wakati huo.



**17.2** *Shule ya Madrasa jijini Algiers mwaka 1830*

## *Jamii ya vijijini*

Mara nyingi upambanuzi wa wazi umefanywa baina ya wakazi wa mijini na wale wa shamba katika jimbo la Maghrib. Upambanuzi huu ulijikita katika masuala kadhaa. Kwanza mijini kulikuwa na utamaduni changamano uliojikita katika jadi ya fasihi ya maandishi, ilhali vijijini kulikuwa na utamaduni wa masimulizi.

Katika masuala ya dini, mafunzo ya kisharia yaliyotolewa na wanazuoni mijini yalikuwa tofauti na mafunzo ya wacha Mungu yaliyotolewa vijijini. Katika uwanja wa uchumi, mfumo wa fedha ulizuka mijini ilhali shamba kulikuwa na uchumi wa kujikimu tu na teknolojia duni. Katika masuala ya kijamii, wakazi wa mijini walionekana kujali sana hadhi na ubinafsi, huku wale wa vijijini wakizidi kutegemeana na kudumisha uhusiano madhubuti wa kiukoo.

Hata hivyo, tofauti hii isitiwe sana chumvi. Hii ni kwa sababu si jumuia zote za vijijini zilikuwa na sifa zote zilizoelezwa hapo juu. Baadhi ya vijiji vilivyokuwa karibu na miji au karibu na masoko pia vilikuwa na utamaduni unaofanana na ule wa mijini. Ijapokuwa suala la ukoo lilikuwa muhimu kabisa katika maeneo haya, jamii hizi pia zilikuwa na sifa nyingine ambazo hazikufahamika katika vijiji vya ndani zaidi.

Udhaifu wa jumuiya za Kiafrika Kaskazini kwa jumla, na wa Wamakhzen ambao waliwatawala, ulikuwa ni wingi wa makabila yao, kujitenga kwao na teknolojia duni waliyoitumia. Lakini, kwa ujumla, Wamakhzen walifanikiwa kudumisha uwiano mzuri katika jamii ambao ulivurugwa tu na maingilio ya Wazungu katika eneo hilo baada ya mwaka 1815.

## *Uvamizi wa wazungu*

Mashambulizi ya Wazungu huko Maghrib katika karne ya 19 yalichukua sura mbili muhimu ambazo zilipelekea Wazungu kulitawala eneo hilo. Sura ya kwanza ilihusika na uhusiano wa kibiashara baina ya Wazungu na dola katika nchi mbalimbali za Maghrib, uhusiano uliowapendelea zaidi Wazungu. Wafanya biashara wa Kifaransa walinufaika zaidi na unyonyaji huu wa kibiashara.

Kwa kiasi fulani uvamizi wa Wazungu huko Maghrib ulifanywa ili kuonyesha ufahari wa kitaifa wa nchi za Ulaya, na vilevile kulinda maslahi ya kidhalimu yaliyopatikana kutokana na mikataba ya kibiashara.

Uvamizi huu pia ulichukua sura ya kiuchumi kwa kuijaza Maghrib na mitaji ya Wazungu. Jambo hili lilieneza biashara ya ukopeshaji kwa riba. Wakati wa matatizo, watawala wa Maghrib waliwafuata wafanya biashara Wazungu kuomba mikopo. Wazungu nao walitumia fursa hiyo kwa manufaa yao binafsi kwa kuwafanya watawala wa Maghrib wawategemee zaidi kwa kuwapa mikopo zaidi na kuwalazimisha kutoa tahafifu zilizovuka mpaka. Mchakato huu wa ukopeshaji fedha ulikua polepole katika karne hii na uliongezeka kasi yake baada ya 1860 kwa kuwa nchi huru za Maghrib zilitafuta mikopo zaidi ili kufanya "mageuzi" yaliyolenga katika kuziendeleza nchi zao.

Muelekeo huu ulionekana zaidi nchini Tunisia ambapo kwanza raslimali ya fedha ya nchi hiyo ilinyonywa na kisha kuwekwa chini ya udhibiti wa Wazungu kabla ya kupita

miaka 10 kati ya 1859 hadi 1869. Mikopo yote iliyopatikana katika kipindi hiki, kwa bahati mbaya, ilipotezwa katika kugharamia miradi isiyo na maana. Ubadhirifu wa maafisa wa serikali haukusaidia chochote na mwaka 1869 nchi hiyo ililazimika kuikubali Tume ya Kimataifa ya Fedha ili kudhibiti mapato yote na kuhakikisha kuwa madeni yote yanalipwa. Licha ya unafuu ambao nchi hiyo iliupata kati ya 1870 na 1881, ubepari uliendelea kushamiri na kuenea kupitia shughuli za mabenki. Hivyo, si jambo la kushangaza kwamba wasemeaji wa ubepari walihimiza Tunisia ifanywe koloni moja kwa moja ili kulinda maslahi yao. Hili lilipelekea kuanzishwa kwa koloni la Kifaransa la Tunisia mnamo Mei, 1881.

Kujipenyeza kwa Wazungu nchini Algeria kulichukua sura tofauti kwa sababu ya nchi hiyo kutawaliwa mapema mnamo 1830. Si tu kwamba ubepari wa kibiashara na kibenki uliingizwa nchini humo, bali pia masetla wa kikoloni polepole waliwapokonya wananchi ardhi yao. Hadi kufikia 1890, watu wengi walikuwa hawana ardhi tena.

## *Mambo yaliyochochea mabadiliko*

Urari uliokuwepo katika jamii ya Maghrib ambao umeelezwa hapo awali uliharibiwa kwa njia mbalimbali kutokana na kuingia kwa Wazungu katika jamii hiyo. Athari ya hali hii ilionekana katika nyanja za biashara na fedha ama moja kwa moja au kwa namna nyingine. Sasa tujaribu kuchunguza mambo makuu yaliyochochea mabadiliko hayo, hulka ya mabadiliko hayo, na athari za shinikizo la Wazungu kwa makundi mbalimbali ya wakazi wa jimbo hilo.

Kichocheo cha kwanza cha mabadiliko ni kile cha biashara ya baharini iliyofanywa na wafanya biashara Wazungu. Biashara hiyo ilidhoofisha na mwishowe kuipiku biashara ya jadi ya misafara mirefu, na biashara ya bahari kati ya Maghrib na nchi za mashariki mwa Mediterania (Levanti).

Uanzishwaji wa mfumo wa fedha katika uchumi na ile hali ya umaskini wa watu kwa jumla vilisababisha kuongezeka kwa ukopaji wa fedha na riba. Wakopeshaji fedha, wengi wao wakiwa Wayahudi, walineemeshwa na hali hii, lakini wenyeji waliingia katika madeni makubwa. Hali hii haikuishia mijini tu, bali pia ilienea hadi kwenye jamii za vijijini.

Kodi za kidhalimu pia zilichangia katika kukuza mgogoro wa jamii huko Maghrib. Nchini Algeria, ongezeko la kodi lililoletwa na utawala wa kikoloni lilisababisha migomo mingi. Maasi makubwa yaliyotokea Tunisia mnamo 1864 yalisababishwa na uamuzi wa kuongeza kiwango cha kodi mara mbili. Hali kama hiyo pia ilikuweko Moroko. Kama vile matatizo yote hayo hayakutosha, kulikuwepo pia na matatizo ya hali ya hewa katika karne hiyo - matatizo ambayo yalisababisha maafa makubwa kwa wananchi. Maafa yaliyotokea 1866-1889 nchini Algeria na Tunisia na yale ya 1878-1881 nchini Moroko yalipunguza kiasi kikubwa cha watu na hivyo kusababisha kudhoofika kwa uchumi na utaratibu wa jadi wa maisha.

## *Walionufaika na zahama hizo*

Baadhi ya makundi ya watu yalinufaika kutokana na zahama zilizotokea Maghrib katika

karne ya 19. Kundi la kwanza ni lile la masetla wa Kizungu, ambao wengi wao waliishi Algeria na Tunisia kuliko Libya. Ingawa wengi wao walitoka katika familia duni, lakini walipata hadhi ya upendeleo kwa kulingamishwa na wenyeji walio wengi. Kulikuwepo pia kundi la Wayahudi, ambao walitekeleza dhima muhimu sana ya kuwa watu wa kati baina ya mabepari wa Ulaya na wenyeji. Baadhi ya Waislamu pia walishirikiana na Wazungu na kuwa watu wa kati baina yao na wenyeji wazawa. Waislamu hao walijumuisha pia maafisa wenye vyeo vya juu serikalini ambao walizitumia vibaya nafasi zao na kujinufaisha wenyewe kwa kuifisidi dola.

Wanufaikaji wengine walikuwa ni baadhi ya watu mashuhuri waliokuwa na mamlaka katika jamii zilizokuwa chini ya utawala wao na ambao dola za Tunisia na Algeria ziliwategemea. Idadi kadhaa ya familia za kidini pia zilijitokeza na kuhodhi nafasi muhimu ama katika jamii za wasomi za jumuia za Waislamu, ambamo walikuwa na hadhi iliyokaribia kuwa rasmi, au miongoni mwa jumuiya mbalimbali za Waislamu kama ilivyokuwa katika Algeria na Moroko.

## *Wahasirika wa zahama hizo*

Watu wengi sana waliathiriwa na hali iliyobadilika ya Maghrib ya karne ya 19. Matokeo yaliyoonekana mara moja ni ufukara mkubwa uliowakumba watu na kuvurugwa kwa mifumo ya kijamii iliyokuwepo. Kwa sababu hii, maafa ya kiuchumi na kibinadamu wakati wa zahama za 1866-69 hayangeepukika.

Wahasirika waliyapokea maafa haya kwa namna mbalimbali. Kwanza walijisalimisha kwa majaaliwa yao na kuzikumbatia jumuiya za Kiislamu kuliko ilivyokuwa kwanza. Hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa huko Algeria, Tunisia na Moroko.

Mwelekeo huu ulidhihirika zaidi huko Moroko. Lakini ilikuwa nchini Libya ambapo Sanusiyya, jumuiya (ya kidini) iliyoanzishwa mwaka 1843 huko Sirenaika, ilikuja kuwa maarufu sana kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Aina nyingine ya matokeo ya hali hiyo ni matukio mengi ya maasi huko Maghrib katika karne ya 19. Maasi ya wenyeji yalienea, siyo tu katika Algeria, ambako tayari kulikuwa na utawala wa kikoloni, bali pia Tunisia na Moroko, ambako yalitokea mara kwa mara. Aidha Libya haikuiepuka misukosuko hii. Hata hivyo, maasi hayo hayakufanikiwa kwa kuwa watawala waliokuwa wakishambuliwa walikuwa na silaha bora zaidi na hakukuwa na mshikamano miongoni mwa waasi wenyewe.

Ni muhimu kuzingatia kuwa majaribio yote ya kufanya marekebisho katika nyanja mbalimbali ili kurejesha uwiano wa kijamii uliovurugwa hayakufanikiwa. Hebu sasa tutazame majaribio hayo katika kila nchi ya Maghrib.

## *Algeria*

Mwanzoni mwa karne ya 19 utawala wa Algiers, kati ya serikali zote za Maghrib, ulifanikiwa kuhifadhi sifa yake ya ugeni. Serikali ilibaki mikononi mwa Waturuki ambao walijitenga kabisa na makabila mengine katika jamii hiyo. Hali hii ilitokea kwa sababu

Algeria ilikuwa ni nchi yenye mfumo wa maisha ya vijijini ambao haukuchipuza tabaka. la kati ambalo lingeweza kuwasimilisha watawala hawa.

Hii haina maana kuwa serikali ya Algeria haikutaka kabisa mabadiliko. Kuanzia karne ya 18, mabadiliko mengi yalitokea, mabadiliko ambayo yaliwafanya watawala hao warekebishe sera zao kuhusu kuwa na ushirikiano na viongozi wa huko vijijini. Lakini pamoja na mabadiliko haya, uongozi wa Algeria uliendelea kuidumisha sifa yake ya ugeni, hali iliyoleta migongano mingi katika jamii.

Hivyo, hisia za "utaifa" dhidi ya hali hiyo zilikuwa tayari zimekwisha anza kujitokeza kabla ya uvamizi wa Wafaransa.

Miaka iliyofuata baada ya uvamizi wa Wafaransa nchini Algeria ilishuhudia mikinzano kadhaa na mashaka katika sera ya Wafaransa, hasa katika suala la kumiliki ardhi. Maeneo ya pwani yalikaliwa na Wafaransa, na mipango ilifanywa kutawala sehemu za bara kwa kuwatumia watawala wenyeji. Ahmad, Gavana Mturuki wa Wilaya ya Konstatini, na Amir Abd al-Kadir, walikuwa watu wawili mashuhuri katika masuala yote yaliyohusu sehemu ya bara. Wakati Ahmad aliendeleza mfumo wa utawala wa Waturuki, Amir Abd al-Kadir aliwahamasisha watu kwa kutumia dini, akachochea hisia zao za uzalendo na kuongoza vuguvugu la upinzani dhidi ya utawala wa Wafaransa kati ya 1832 na 1847. Ingawa aliweza kuwahamasisha karibu theluthi mbili ya watu wa Algeria, mwishowe Abd al-Kadir alishindwa na Wafaransa.

Baada ya hapo Wafaransa walianzisha ukoloni pamoja na asasi zake zote nchini Algeria. Nchi iliwekwa chini ya utawala wa Gavana Mkuu na kugawanywa katika eneo la kiraia ambamo Wazungu waliishi na kuanzishwa utamaduni wa Kifaransa na asasi zake, na eneo la kijeshi ambamo jamii za wenyeji ziliishi chini ya utawala wa jeshi. Kushindwa kwa Wafaransa katika vita vyao na Wadachi mwaka 1870, na tishio la upanuzi wa eneo lililokuwa chini ya utawala wa Wazungu, ambamo Wazungu walimiliki ardhi yote, kulipelekea kwenye maasi mkubwa zaidi kuliko yote huko Kabylia na majimbo yaliyo karibu na sehemu hiyo mnamo 1871. Maasi hayo yalizimwa kwa ukatili na Wafaransa, na watu wakawekwa chini ya utawala wa mabavu zaidi wa Wafaransa. Matokeo ni watu hao kuwa maskini kwa sababu ya kunyang'anywa ardhi yao. Zaidi ya hayo, wenyeji walinyimwa fursa ya kuendeleza mila na desturi za jamii zao. Hivyo, walipoteza haki zao na walinyonywa waziwazi kwa manufaa ya Wazungu wachache walioishi miongoni mwao.

## *Tunisia*

Tunisia ilikuwa nchi ya kwanza katika Maghrib kufanya mageuzi kwa kuiga mtindo wa kimagharibi. Hii ilitokana na kuwepo kwa mahusiano makubwa baina yake na nchi za nje. Matokeo ya uigaji huo yalikuwa mabaya sana.

Uhusiano wa Tunisia na nchi za nje uliotokana na mahusiano ya kibiashara, na kuongezeka kwa uwezo wa wenyeji mashuhuri, kulianza kuathiri mfumo wa kisiasa. Matokeo ya hali hiyo ni kuwa uongozi ulijaribu kujinasibisha na watu na hivyo kuzua utawala wa kifalme ulioelekea kwenye utaifa. Na wakati huo huo utawala uliendelea kuwategemea askari wa Kituruki na Mamluki. Wananchi vilevile waliunga mkono



17.3 Wanawake wa tabaka la kati nchini Algeria wakiwa na mtumishi wa kike mweusi ambaye pia ni mtumwa.

17.4 Wanajeshi waliovaa sare zilizofanana na zile za Askari wa Mataifa ya Magharibi



utawala huo. Serikali ya nchi hiyo ilifikia kilele cha uwezo wake chini ya utawala wa Hammuda Pasha kuanzia 1782 hadi 1814; baada ya hapo matatizo yalianza kutokea.

Ahmad, Gavana wa Kituruki mjini Tunis (1837-55), aliamua kukopa fedha kutoka Ulaya haada ya kukabiliana na matatizo yaliyotokana na kujipenyeza kwa biashara ya Wazungu nchini Tunisia, pamoja na tishio la majeshi kutoka kwa majirani zake, Ufaransa na himaya ya Waturuki. Aidha alianzisha mabadiliko yasiyo na faida bila kutilia maanani rasilimali za nguvukazi fedha. Mabadiliko hayo yalijumuisha uundaji wa jeshi jipya lililofanana na lile la Wazungu. Ili kukidhi mahitaji ya jeshi hili jipya, alijenga kiwanda ili kutengeneza bunduki, baruti, nguo na viatu. Aidha alikomesha utumwa katika mwaka 1846. Kutokana na hisia ya utaifa, alipunguza upendeleo waliopewa Waturuki na hivyo kuwaweka katika hali ya usawa na wenyeji. Mengi ya mageuzi hayo hata hivyo hayakutoa matunda yaliyotarajiwa na, mbaya zaidi, yalitumia gharama kubwa kutoka kwenye mapato ya serikali. Suluhisho lilitafutwa kwa kuongeza kodi, lakini hatua hiyo, badala ya kutatua tatizo, ilisabisha kutokea kwa upinzani na uadui mkubwa dhidi ya serikali hiyo.

Kutofanikiwa kwa mageuzi haya kulichangiwa na ukweli kwamba hayakuweza kukifu mazingira ya kibinadamu ambamo yalikuwa yakifanywa. Zaidi ya hayo, nchi za Ulaya ziliyachukulia mageuzi hayo kama fursa ya kujipatia mikataba yenye faida kubwa. Hadi 1885, ambapo Gavana Ahmad alifariki, mabadiliko hayo yalikuwa yamekwisha sababisha kuzuka kwa kundi lililopendelea zaidi ujenzi wa usasa, na yalikuwa tayari yamepanda mbegu ya kuundwa kwa dola la kitaifa. Wakati huo huo, mageuzi yaliongeza hatari ya kuingiliwa na mataifa ya kigeni, na yalizidisha udhaifu wa ndani. Wazungu na wenyeji waliowaunga mkono walitumia hali hii kujinufaisha.

Hadi kufikia 1856-7, mataifa ya Ulaya yalitoa shinikizo kubwa la kutaka mabadiliko ambayo yangeendeleza shughuli za kibepari kwa kuwaruhusu wageni kumiliki mali, na kufanya kazi yoyote waliyoitaka katika misingi ya biashara huria. Hali hii ilisababisha kutungwa kwa katiba ya Tunisia mwaka 1861 ambayo ilitenganisha matawi matatu ya serikali: makahama, baraza la kutunga sheria na mamlaka ya utawala. Aidha, baraza la manispaa lilianzishwa jijini Tunis. Zaidi ya hayo, wizara na huduma za utawala zilifanyiwa marekebisho, na kiwanda cha uchapaji kilijengwa huko Tunis.

Licha ya kutofanikiwa kwa mabadiliko haya, shughuli za makampuni ya Wazungu zilizidi kupanuka, hasa kuhusu biashara ya nje. Kiwango cha matumizi ya Serikali ya Tunisia kiliongezeka bila kulingana na ongezeko la mapato yake. Matokeo ya hali hii ni kwamba nchi hiyo iliingia katika madeni makubwa. Ili kulitatua tatizo hili, Gavana Muhammad al-Sadik aliamua kuongeza kodi mara mbili ya kiwango cha kawaida mwishoni mwa 1863. Jambo hili lilisabisha maasi makubwa mwaka 1864 ambayo serikali iliyazima kwa taabu sana. Pamoja na hali hiyo, mavuno hafifu yaliyopatikana 1866-1870, baa kubwa la njaa na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu mwaka 1870 uliyakuza matatizo yaliyokuwepo na kusababisha nchi ifilisike. Mnamo Julai 1869, Tume ya Kimataifa ya Fedha ilianzishwa mjini Tunis ili kudhibiti mapato yote ya nchi na kuhakikisha kuwa inalipa madeni yake.

Uwezo wa kiutendaji wa mawaziri ambao Gavana aliwaunga mkono pia uliukilia

jinsi ambavyo Tunisia iliendesha shughuli zake wakati ule wa kipindi kigumu. Kwa mfano serikali potovu ya Mustafa Khaznadar (1837-1873) ilileta maangamizi nchini humo, lakini kipindi cha Khayr al-Din (1873-77) kilishuhudia uboreshaji wa hali ya jumla za nchi kutokana na uadilifu, uzalendo, busara na utambuzi wake wa kisiasa. Hata hivyo, njaa ya 1876-77 na kukua kwa ufahari wa Ufaransa kulihakikisha kwamba hata Khayr al-din asingaliweza kudumu madarakani. Nafasi yake ilichukuliwa na Mustafa ibn Ismail, waziri aliyemtumikia Gavana hapo awali. Wakati wa utawala wake Tunisia iliwekwa chini ya "ulinzi" wa Wafaransa mnamo 1881.

## *Libya*

Kutokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya nchi ya Libya imechukuliwa na jangwa la Sahara kuliko nchi nyingine yoyote ya Maghrib, nchi hiyo haikutamaniwa sana na Wazungu. Misafara ya zamani ya biashara iliweza kuendelea nchini humo hadi katika karne ya ishirini.

Kutoka muongo wa mwisho wa karne ya 18 hadi 1835, Libya ilikumbwa katika mgogoro wa harakati za kuwania madaraka baina ya serikali kuu iliyowakilishwa na nasaba ya Karamanli na makundi ya Wanomadi. Tabaka la kati lililoishi pwani mijini ndilo lililokuwa mhimili mkubwa wa nasaba-tawala ya Karamanli. Tabaka hili la kati lilikuwa na familia kubwa kubwa zilizokuwa maarufu katika masuala ya kijeshi, kiuchumi na kidini.

Vyanzo vyao mapato ya serikali vilijumuisha biashara ya masafa marefu, biashara ya kikanda, sanaa za ufundi, na hadi 1815, uharamia wa baharini. Hatimaye mgogoro wa kuwania madaraka ulipatiwa ufumbuzi ufalme wa Uturuku ulipoamua kuitawala Libya moja kwa moja. Waturuki walitumia jeshi na diplomasia kudhoofisha upinzani wa wanomadi, na baada ya 1858 walipanua utawala wao katika Tripolitania na baadhi ya maeneo ya Fezzan.

Sehemu ndogo ya watu walilima sehemu ya ardhi iliyofaa kwa kilimo katika jangwa, lakini sehemu kubwa ya watu walikuwa ni Wanomadi waliofuga kondoo na ngamia. Jamii zenye nguvu zaidi ni zile zilizoishi ndani kabisa jangwani. Ni katika jamii hizo ndimo mlimostawi jumuiya ya Sanusiyya katika *zawiya* zake kuzunguka maeneo ya Oasisi kubwa. Walitilia mkazo sana katika kukuza kiwango cha maisha ya kidini kati ya makundi ya Wanomadi. Walikuza biashara kwa kuongoza misafara kutoka Barka huko Sirenaika hadi Wadai na kutoa nafasi ya malazi na huduma nyingine kwa misafara hiyo. Aidha walitumia umaarufu wao kusuluhisha migogoro iliyotokea katika jamii mbalimbali za Wanomadi jangwani. Ili kuhakikisha kuwa kabila hili la wahamaji jangwani haliwi tishio katika utawala wao, Waturuki waliwatumia Sanusiyya katika Barka kama watu wa kati baina yao na Wanomadi hao.

Ili kuimarisha mamlaka yao, Waturuki walianza kufanya mageuzi kadha nchini Libya. Mabadiliko yalifanywa katika mahakama, utawala serikalini, serikali ya manispaa, shule, hospitali na soko kuu kati ya 1865 na 1880. Kulianzishwa pia vituo vya kuwagawia watu chakula wakati wa baa la njaa. Wakati mabadiliko yaliyofanywa zamani yaliwanufaisha watu wa tabaka la kati tu, mabadiliko haya yaliwanufaisha sana



**17.5** *Kaburi la Marehemu Muhammad ben Ali al Sanusi, Muasisi wa Sanusiyya.*

watu wa kawaida. Zaidi ya hayo, uchumi ulikua zaidi licha ya ongezeko la bidhaa zilizoagizwa kutoka Ulaya baada ya 1850.

Matatizo yalijitokeza wakati wa kipindi kirefu cha upungufu wa chakula (1881-89). Hali hii iliathiri sana kiwango cha bidhaa zilizouzwa nje ya nchi, na kiasi cha vyakula vilivyoagizwa kutoka nje pia kiliongezeka. Mapato kutokana na biashara ya Sahara pia yalipungua. Hali hii ilitokea wakati Sanusiyya ilipokuwa inakabiliana na shinikizo kutoka nje pamoja na matatizo ya ndani. Baada ya kupunguka kwa mapato yake kutokana na biashara, Sanusiyya iligeuka na kuanza kuhodhi ardhi na kilimo kwa kuwadhulumu baadhi ya wafuasi wake. Hali hii ilihimiza kujitokeza kwa jumuiya kinzani na vyama vingine vya kidini. Hadi mwaka 1910, umaarufu wa Sanusiyya katika jimbo hilo ulikuwa umepungua kwa kiasi kikubwa.

Picha inayoonekana katika maelezo haya ni ya jamii iliyokuwa ikibadilika sana na ambamo mambo ya zamani yalikuwa yakitoweka kwa haraka. Wazungu hawakuzubaa katika kuhakikisha kuwa wananufaika na hali hii kwa kujihusisha kikamilifu katika uchumi wa jamii hiyo. Kuanzia 1911 kulikuwa na jaribio la uvamizi lililofanywa na Italia, harakati za upinzani na vita hadi 1932.

*Hitimisho*

Nchi za Maghrib zimekuwa chini ya utawala wa kikoloni katika nyakati tofauti. Sababu ya kupoteza uhuru isiangaliwe katika matukio yaliyotokea katika jamii hizo, bali katika hali ya kuenea kwa ubepari wa Ulaya.

Hali hii haikuwepo Maghrib tu, ilitokea pia katika sehemu nyingine za dunia (nje ya Ulaya) ambazo ziliwaniwa na ubeberu wa Ulaya.

Pamoja na hayo, hali fulani ya ndani ya nchi hizo huweza kueleza sababu ya kutofautiana kwa kasi ya kutekwa kwa nchi mbalimbali za Maghrib, njia zilizotumiwa katika kuziteka nchi hizo, na jinsi wenyeji walivyoikabili hali hiyo. Algeria ilitwaliwa kwa nguvu kabla ya 1850, na huko "pigo" la Wazungu lilihusisha kuingia kwa walowezi, na kuporwa kwa ardhi kubwa, jambo lililokuwa la kikatili na la kufadhaisha kwa jamii ya asili na utamaduni wake. Tunisia iliingiliwa polepole kwa njia ya mitaji, lakini Libya kwa muda fulani iliepuka kukumbwa na uchu wa Wazungu kwa kuurudisha tena utawala wa Waturuki mwaka 1835, na pia kutokana na ufukara wake na umbali wake (kutoka kwenye vituo vya biashara na utawala wa Wazungu). Tajiriba zote hizi zilikuwa na athari ya kudumu katika jamii ya Maghrib.

# 18 Moroko kutoka mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa hadi 1880

Misingi ya Moroko mpya iliwekwa katika karne ya kumi na nane wakati wa utawala wa Sultani Muhammad III (1757-1790) ambao ulikuja baada ya kipindi cha utawala huria katika historia ya nchi hiyo. Dola hii mpya iliimarishwa na Sulayman (1792-1822) aliyeitawala nchi hiyo kufuatana na Sharia (sheria ya Kiislam) na kuipa serikali msingi wa mtazamo wa kimji zaidi. Alizitawala jamii za wakulima wa Hauz, Dir na Gharb moja kwa moja, na aliyatawala majimbo ya milimani na jangwani kwa kuwatumia machifu - Ma-*kaid* na viongozi wa vikundi mbalimbali vya kidini. Hali hii ilileteleza kuwepo kwa sura mbili katika maeneo yaliyotawaliwa: eneo la *bilad-al-makhzen* lililotawaliwa moja kwa moja na Sultan na maeneo yaliyokuwa chini ya machifu, *bilad-al-siba*, ambayo aliyatawala kwa kuwatumia machifu, japo tofauti hiyo haikujitokeza sana.

Watawala wa Moroko waliofuata walikabiliwa na jukumu la kuipangilia upya nchi hiyo. Makundi ya watu waliokuwa wanafaidika sana kwa kupata upendeleo fulani kutoka katika serikali yaling'olewa katika madaraka. Ilikuwa ni katika kipindi hiki ambapo Wazungu walianza kuingia kwa nguvu Moroko, hasa baada ya Wafaransa kuutwaa mji wa Algiers mwaka 1830. Hivyo serikali ya Moroko ilishughulika kujijenga kisiasa, kujipanua kijiografia na kujiimarisha ili kuweza kukabiliana na hatari ya kuvamiwa na wageni. Licha ya ubora wa kipekee wa watawala wa Moroko katika karne ya kumi na tisa, walikabiliwa na upinzani kutoka ndani ya nchi na shinikizo kutoka kwa Wazungu kiasi kwamba nchi hiyo haikuweza kuepuka utawala wa kigeni. Lakini mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki ni kukua kwa utambulisho wa kiasili wa Moroko ambao uliipa Moroko nafasi maalum huko Maghrib.

## *Muundo wa kisiasa-jamii*

Katika kipindi hiki, asasi muhimu ya kisiasa nchini Moroko ilikuwa ni *bay'a* (mkataba wa kukabidhi madaraka) ambayo iliwaunganisha pamoja sultani na makundi mbalimbali ya watu. Ulikuwa ni mkataba wa maandishi uliohalalisha mamlaka ya kisiasa. Kufuatana na mkataba huo, mfalme alitarajiwa kulinda nchi dhidi ya maadui wa kigeni na kuimarisha amani nyumbani. Watu nao walimpa heshima kubwa na kumsikiliza ili mradi tu havunji sharia na desturi za Kiislamu. Pamoja na mambo mengine, raia

walitarajiwa kutii amri za serikali, kulipa kodi halali, kushiriki katika jeshi wakati wa amani iwapo hapana budi, na kuiunga mkono serikali wakati wa vita.

Ili kufanikisha shughuli hizi, mfalme alikuwa na serikali iliyoundwa na jeshi na utawalamsonge. Jeshi lilijumuisha makundi makubwa matatu: Kundi la *bwakher* lililoundwa na mamia kadha ya watumwa; kundi la *gish* lililoundwa na vikosi kutoka katika baadhi ya jumuia; na kundi la *nuaib* ambalo liliundwa na vikosi vya muda vilivyotolewa na baadhi ya jamii baada ya kuombwa na sultani kufanya hivyo. Jeshi hili lilikuwa na jukumu kubwa la kudhibiti nchi nzima na kuchunga utulivu nchini. Utawalamsonge uliundwa na mawaziri na makatibu wakuu wa wizara ambazo ziligawanywa katika idara mbalimbali. Asili ya wengi wa maafisa hao ilikuwa ni Andalusia, na utawala huo uliendeleza jadi ya Andalusia kwa kutoa mafunzo katika chuo kikuu cha Karawiyyin kilichokuwa Fez. Hata hivyo, kulizuka aina mpya ya maafisa wa serikali katika nusu ya pili ya karne ya 19 ili kukidhi mahitaji yaliyotokana na uhusiano na bara la Ulaya ambao ulizidi kupanuka. Maafisa hawa hawakuwa wanafahamu vizuri historia au ulumbi, lakini walifahamu vizuri sana lugha za Ulaya na matatizo ya kifedha.

Kwa kuwa dola ya Moroko ilijengwa kwenye misingi ya dini ya Kiislam na maelekezo yake, vyanzo vyake vya fedha vilikuwa ni vile vilivyothibitishwa na dini hiyo na hivyo njia nyingine zote zilikuwa si halali. Vyanzo halali vya mapato vilikuwa ni mapato kutokana na ardhi, kodi kutokana na mtaji wa biashara na mazao ya kilimo, na kodi kutokana na biashara ya nje. Kwa sababu ya kuwa na mapato kidogo, Sultani alilazimika kupunguza kiasi kikubwa cha matumizi.

Majaribio mbalimbali yaliyofanywa na Masultani Muhammad III, Sulayman Abd-al-Rahman na Muhammad IV (1822-59) ili kuongeza kodi au kuanzisha kodi mpya hayakufanikiwa. Hivyo katika kipindi chote cha karne ya 19, tatizo la kodi katika historia ya Moroko lilibaki kuwa kubwa, na halikuweza kupatiwa ufumbuzi wa kuridhisha. Pamoja na *Makhzen* (serikali) kutafuta suluhisho la tatizo hilo kwa kupunguza mapato yake, bado kulikuwepo na haja ya kufanya mabadiliko ya jumla, hasa baaada ya kuongezeka kwa shinikizo kutoka kwa Wazungu.

Licha ya jeshi na utawalamsonge, kulikuwepo na makundi mengine ya kati katika jamii hiyo. Makundi haya yalisimama kati ya serikali kwa upande mmoja na watu wa mijini na vijijini kwa upande mwingine. Kwa kweli, watu hawa wa kati walikuwa ni sehemu ya *Makhzen*. Walilinda haki za kiasili za watu wao dhidi ya Sultani na pia kutekeleza amri za serikali kwa kuwa walikuwa wanawajibika kwa Sultani. Makundi ya watu hawa yaliundwa na tabaka la makarani, pamoja na masharifu, *wazawiya* na machifu wa makabila. Tabaka la makarani liliundwa na maulama (walimu), makadhi na watawala wengine wa wakfu za kidini, na maofisa waliosimamia masoko. Kundi hili lilitumia amri za sharia, na ingawa walikuwa chini ya usimamizi wa Sultani, waliweza kufanya jambo lolote bila kuulizwa. Hata sharia za dini ya Kiislam zilizotumika katika maisha ya jamii, zilikuwa chini ya mamlaka ya maulama, na mfalme asingeweza kujaribu kuzibadilisha.

Masharifu walikuwa ni watu wa nasaba moja na Mtume Muhammad na waliunda tabaka la makabaila wa kidini lililoenea sehemu zote za Moroko. Walikuwa wengi na



**18.1** *Mfalme Abd al - Rahman (1822 - 59) kwenye mwaka 1832*

walipata upendeleo na kuheshimiwa na jamii. Walisamehewa kulipa kodi nyingi na walipatiwa zawadi nyingi za lazima kutoka kwa mfalme. Uhusiano wao na Mtume Muhammad si tu kuwa uliwawezesha kuwa katika hadhi ya juu katika jamii, bali pia uliwatunuku vipaji vya kutenda "miujiza" waliovyovitumia ili kujipatia kipato kikubwa. Hata Sultani alikuwa katika orodha ya wateja wao.

*Wazawiya* walikuwa ni makundi ya kijamii yenye misingi ya kidini na yaligawanyika katika makundi makubwa mawili katika Moroko ya karne ya 19. Kundi la kwanza lilikuwa la udugu wa *zawiya* ambao kila mtu aliruhusiwa kujiunga nao bila ubaguzi wa tabaka la kijamii, utajiri, kazi au kabila. Mifano ya jumuiya za aina hiyo ni makundi ya Tijaiyya na Darkawiyya. Kundi la pili lilikuwa ni la *zawiya* iliyokuwa na utawala wa kifalme ambapo mkuu wa wakfu wa dini alitawala sehemu maalum ambayo alikuwa na mamlaka nayo kama vile Wazzaniyya na Nasiriyya. Makundi haya mawili ya *zawiya* hayakutengana moja kwa moja. Baadhi yalijumuisha sifa za makundi yote mawili. Lakini jukumu lao kubwa lilikuwa ni kufanya kazi kama mabaraza ya nidhamu katika jamii, na yalikuwa ni chombo cha mamlaka ya *Makhzen* licha ya kuonekana kuwa "huru."

Machifu wa makabila waliyatawala majimbo maalum (*makabila*), yaliyokuwa ama wilaya za milimani, ama muungano wa Wanomadi, ama jumuiya za maaskari wafugaji. Kwa kila jimbo mamlaka yalikabidhiwa kwa *kaid* aliyeteuliwa kwa amri ya mfalme baada ya kupata idhini ya watu wa wilaya hiyo. *Kaid* alitekeleza dhima mbili kwa wakati mmoja. Alikuwa mwakilishi wa Sultani na pia msemeaji mkuu wa watu. Wakati mwingine alifanya kazi za gavana kwa kukusanya kodi na ushuru wa kugharimia vikosi vya jeshi. Kwa kila jimbo kulikuweko na familia mbili za ki-*kaidiya* (ambamo ma-*kaid* wangeweza kuchaguliwa) ambazo zilikuwa ni sehemu ya tabaka la watawala la nchi hiyo.

Baada ya yote, vyombo hivi vya kati, iwe mijini au vijijini, vilikuwa ni kama meno ya gurudumu tu la serikali ya Sultani. Mfumo wa siasa-jamii wa Moroko kama ulivyofanyiwa marekebisho na Muhammad IV ulionyesha kurudi katika Uislamu asilia. Mfumo huo si tu kwamba uliutambua uhuru wa kujitawala wenyewe wa vyombo hivyo vya kati, bali pia ulizima tamaa ya kutawala ya serikali kuu. Kwa kuyaruhusu makundi kutoa malalamiko yao ndani ya muundo wa serikali, mfumo huo uliimarisha dhana ya nchi ya Moroko. Si sahihi moja kwa moja kuueleza mfumo huo kuwa ulikuwa ni wa serikali inayoongozwa na sharia, wala kusema kuwa ni mfumo ambamo mfalme alikuwa ni ishara na kiungo tu cha taifa bila mamlaka - ulijumuisha yote mawili. Lakini kabla mfumo huo haujaimarika ilibidi ukabiliane na shinikizo kubwa kutoka kwa Wazungu.

## *Mageuzi machache ya Makhzen*

Kipindi cha kati ya 1800-1880 kilikuwa ni cha amani nchini Moroko, kutokana na kutoingiliwa na Wazungu, tofauti kabisa na hali ilivyokuwa katika nchi nyingine za Maghrib. Si Ufaransa wala Hispania ilipanua mipaka yake kiasi cha kutishia uhuru wa Moroko, na bidhaa kutoka Uingereza hazikupewa upendeleo maalum wa kibiashara nchini humo. Hapakuwa na mwafaka wowote kati ya madai ya nchi za Ulaya na




18.2 Manco ya kihistoria ya Moroko karne ya kumi na tisa

mamlaka ya Sultani. Hali hii ilitokea kwa sababu mikono ya mfalme ilifungwa na maulama, ambao hawakutaka mabadiliko, na waling'ang'ania sana sharia ambayo haikukubaliana kabisa na matakwa ya Wazungu. Hivyo kwa Wazungu, Sultani alikuwa ni mtu asiyeelimika na asiye na maendeleo ilhali maulama walimuona kama mtu mbunifu aliyetaka kuleta mabadiliko nchini Moroko kwa kushinikizwa na Wazungu.

Katika karne ya 19, mfalme na wawakilishi wa serikali za Wazungu nchini Moroko waliona umuhimu wa kufanya mabadiliko katika jeshi na serikali. Lakini tatizo lilikuwa ni kwa namna gani mabadiliko hayo yalipaswa kufanywa. Wazungu walipendelea mabadiliko hayo yafuate misingi na dhana za Magharibi, lakini *Makhzen* ilitaka mabadiliko hayo yafanywe katika misingi ya sharia. Hivyo mabadiliko yaliyofanywa katika misingi hiyo mara nyingi yalionekana kuwa na mikinzano na utata.

Muhammad IV akiwa mwanafalme na mrithi wa ufalme mtarajiwa, alikuwa amiri jeshi mkuu wa jeshi lililopigwa na majeshi ya Wazungu na hivyo kushindwa vita mnamo 1844. Alikuwa Sultani (1859-73) wakati Moroko iliposhindwa tena vita mwaka 1860-61, na hivyo kulipishwa fidia kubwa kwa madhara yaliyotokana na vita hivyo. Hivyo, alidhamiria kubadilisha na kuboresha ufanisi wa jeshi. Aliwatumia baadhi ya Watunisia kulifundisha jeshi lake ili lilingane na lile la Ulaya. Aidha alianzisha shule ya uhandisi huko Fez ili kuwafundisha wapimaji ardhi, wanatopografia, wanakatografia na wapiga mizinga. Pamoja na kuwa na matatizo ya fedha, hasa yaliyomkabili baada ya 1860, aliwapeleka baadhi ya vijana wake huko Misri kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi. Mwanawe ambaye pia alirithi utawala, Hassan I (1873-94), aliendeleza sera hii ya kulijenga upya jeshi kwa kuanzisha mfumo wa uandikishaji wa kila mara wa wanajeshi. Vijana waliochaguliwa kujiunga na jeshi walipelekwa Ulaya kwa mafunzo na waliporudi nyumbani waliunda rejimenti iliyoongozwa na kamanda Mwingereza, Meja Maclean. Kwa kutumia jeshi hili lililosukwa upya, Hassan aliyatawala tena majimbo ya mbali ya ufalme wake ambayo yalitamaniwa sana na nchi za Ulaya.

Mwaka 1856 Sultani Abd al-Rahman alitia saini mkataba wa urafiki na wa biashara kati yake na Uingereza. Mkataba huo ulilifungua soko la Moroko kwa wafanya biashara wa nchi za Ulaya kwa kuridhia kanuni ya uhuru wa kibiashara na hivyo kuwapa upendeleo fulani wafanya biashara wa kigeni. Hata hivyo, jambo hili lilileta madhara katika uchumi wa Moroko. Tatizo la kwanza ni kuwa lilileta mgogoro wa kifedha. Thamani ya fedha ya Moroko ilishushwa, na hivyo kusababisha mfumuko wa bei na matatizo yanayoambatana nao, kama vile, kupanda kwa bei za bidhaa, kufukarishwa kwa wananchi, matatizo ya fedha kwa serikali, na wananchi wachache kuhodhi mali nyingi. Juhudi zote za kulitatua tatizo hili la kiuchumi zilizofanywa na *Makhzen* zilishindikana kwa sababu Sultani alitakiwa ayalipe madeni yake ya nje kwa fedha za kigeni ambazo zilipatikana katika viwango vikubwa vya ubadilishaji wa fedha. Isitoshe, wafanya biashara wa kigeni walifanya hali iwe mbaya zaidi kwa kulipa ushuru katika fedha ya nchi hiyo iliyoshushwa thamani, na hivyo kupunguza mapato ya serikali.

Gharama za mageuzi haya zilipounganishwa na ulipaji wa madeni na fidia kwa nchi za Ulaya, na kwa wafanya biashara wa fedha, matumizi ya *Makhzen* yaliongezeka kwa kiasi kikubwa bila kuwiana na mapato ya nchi. Ilibidi hatua za kuongeza mapato ya dola

18.3 Sultani Hassan I (1873 - 94)






1 8.4 Reale ya fedha iliyotengenezwa
Paris (Ufaransa) mwaka 1881 kwa ajili ya Hassan I

zichukuliwe. Lakini Sultani hangeweza kufanya mabadiliko yoyote kuhusu masuala ya fedha bila idhini ya maulama ambao hawakuwa tayari kuridhia kuwatoza watu kodi ya ziada na ya kudumu kwa madhumuni hayo. Jambo hili lilileta matatizo makubwa sana kwa Muhammad IV, lakini Sultani alikataa pingamizi zao, akaendelea na azima yake ya kuwatoza watu kodi ya kificho, kodi ambayo ilipingwa sana hasa na wakazi wa mijini. Hassan I pia alipambana na matatizo kama hayo na alipingwa vikali na wananchi na viongozi wa jeshi ambao walimzuia kuendelea kufanya marekebisho ya kifedha.

Katika miaka ya 1860 *Makhzen* ilianzisha mpango wa kurekebisha serikali kwa kuitikia malalamiko ya jumuia ya Wazungu nchini Moroko ambayo idadi yao iliongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi hicho. Kikosi cha wakaguzi wa ushuru walioitwa *umana* kilianzishwa 1861 kusimamia ukusanyaji wa ushuru wa forodha katika bandari nane zilizokuwa zinashughulikia biashara ya nje nchini humo. Asilimia 60 ya ushuru huu ilipelekwa kulipia fidia ya vita. Umana na kundi jingine la maofisa lililoitwa *tulba* walipata upendeleo katika utawalamsonge. *Tulba* walipelekwa Ulaya kwa mafunzo ya kazi hiyo na pia kujifunza lugha, na baada ya kurudi walifanya kazi katika wizara ya mambo ya nje na katika kitengo cha ukusanyaji kodi kilichokuwa chini ya idara ya usarifu, ambayo ilikuwa chini ya kiwanda cha zana za vita kilichoendeshwa na Waitaliano huko Fez.

Wazungu wafanyabiashara pia walitafuta namna ya kuuwekea mipaka utawala wa wenyeji kwa kubuni mbinu za kujiondoa katika mamlaka ya watawala hao. Wazungu walipendelea zaidi kuhukumiwa na gavana au baraza la hukumu lililoundwa na gavana na Wazungu wawakilishi. Mwaka 1863 Muhammad IV alitia saini mkataba na Ufaransa ambao ulitoa upendeleo katika masuala ya kisheria kwa wafanya biashara kutoka nje na washirika wao kutoka Moroko. Hivyo, kesi zao ilibidi zihukumiwe na gavana akiwepo balozi anayehusika. Lakini mara kwa mara upendeleo huohuo kwa washirika wao wa Kimoroko ulitumika vibaya hadi 1880 ulipofanyiwa marekebisho.

Kwa jumla shinikizo la Wazungu lilileta mabadiliko katika jeshi la Moroko, serikali na mifumo ya fedha na kodi. Mawanda ya mabadiliko hayo yalifinywa na vikwazo vya nje ya nchi na matatizo ya ndani. Ingawa Wazungu waliikubali hatua yoyote iliyowahakikishia usalama wao na kuweka mazingira mazuri ya biashara zao, hawakutaka serikali ya Moroko iwe na nguvu kiasi cha kuingilia kupendelewa kwao na faida yao (ya kibiashara). Kwa upande mwingine, Sultani hakupewa uhuru katika utendaji kazi wake nchini mwake: Maeneo mengine, kama vile elimu, mahakama na siasa za dini, hayakufanyiwa mabadiliko kutokana na mwelekeo wa maulama wa kutopenda ushirikiano. Sultani pia alikwazwa na upungufu wa fedha. Matokeo yake ni kuwa kila badiliko lilimsogeza Sultani karibu zaidi na Ulaya kwa sababu, kadiri wafanya biashara wa kigeni walivyoongezeka Moroko, kulikuwa na matukio mengi yaliyoisababisha Moroko ilipe faini kubwa au iachie sehemu ya ardhi yake au ipoteze ardhi yake.

Msululu huu wa matukio ulisababisha kuwepo kwa upinzani mwingi kutoka kwa watu wa Moroko, kwani watu walianza kuhusisha ufukara wao wa kitaifa na kuingia kwa wageni kutoka nje ya nchi. Hivyo, wananchi waliwachukia wageni, na kuwalaumu kwa maafa yote yaliyoikumba Moroko.

## Majibizo ya Umma

Karne ya 19 ilishuhudia kuongozeka zaidi kwa shinikizo la Wazungu huko Moroko, na pia matatizo ya kijamii-uchumi, ambayo yaliwachukiza wananchi, na yalihusishwa na kuwepo kwa Wazungu. Kutokana na kuongezeka kwa shinikizo kubwa katika ardhi kulikosababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya wafanya biashara Wazungu waliopeleka bidhaa nje ya nchi, pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, kulikuwa na matukio kadhaa ya mabaa ya njaa yaliyowaathiri sana watu wa mijini na vijijini katika nusu ya pili ya karne hiyo. Watu wa vijijini wakawa masikini. Wakulima na wafugaji wengi walihama vijijini na kuingia mijini. Uhamaji huu kutoka vijijini kuingia mijini uliiathiri karibu theluthi moja ya ardhi ya kilimo huko Moroko.

Jamii ya mijini pia ilikuwa katika hali mbaya sana. Hadi 1881, ilikisiwa kuwa karibu asilimia 15 ya wakazi wa mijini waliishi kutokana na uhisani (ufadhili), na karibu Wamoroko 64,000 walilazimika kuihama nchi yao. Zaidi ya hayo, makazi ya watu maskini yalianza kujitokeza nje ya ukuta wa miji. Kulikuwa na ongezeko kubwa la bei za bidhaa muhimu kama vile nafaka, sufu na ngozi. Bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi zilikuwa rahisi lakini zilikuwa katika ushindani mkubwa na zile za viwanda vya nchi hiyo ambazo ndizo zilizokuwa nguvu ya uchumi wa mjini. Aidha wafanyakazi wa serikali waliathirika sana kutokana na kushtuka kwa thamani ya fedha ya nchi hiyo kwani uwezo wao wa kununua bidhaa ulipungua kwa kiasi kikubwa.

*Makhzen* pia ilipata mgawo wake wa dhiki kutokana na matatizo haya. Mapato ya kodi kutokana na mtaji wa biashara na mazao kutoka shambani yalipungua kwa sababu ya matatizo yaliyowaathiri watu wa mijini na vijijini. Serikali pia iliombwa na Wazungu kulipa madeni ya watu binafsi kama vile magavana. Kana kwamba hiyo haikutosha, baadhi ya wafanya biashara wa Kizungu na washirika wao wenyeji walianzisha vitendo vya kuhujumu uchumi ambavyo ilikuwa vigumu kwa Sultani kuvidhibiti. Hawa walikuwa ndio watu pekee walioepuka ufukara ulioikumba nchi nzima. Kundi hilo lilijinufaisha kwa gharama ya serikali kwa kulipa bei ndogo kupindukia kwa bidhaa walizonunua nchini humo, na kukopesha fedha kwa viwango vikubwa sana vya riba.

Licha ya shida hizi za kiuchumi, kulikuwa pia na matatizo ya kijamii. Mamlaka ya viongozi wa kidini, Sultani na Uislamu kwa jumla yalishuka kwa kiasi kikubwa. Huu ulikuwa ni wakati ambapo Wazungu walikuwa wakisisitiza kupewa heshima yao ya kitaifa na haki zao za kibinadamu. Hili liliwaweka maafisa wa serikali katika hali ngumu zaidi; kuwaridhisha Wazungu kungekuwa ni kudharau mila za nchi, na kuwakatalia kungesababisha matatizo kwa Sultani katika uhusiano wake na nchi za nje. Kulihali, maafisa hawa waliathirika sana na matokeo ya vitendo vyao wenyewe.

Hivyo, viongozi wa dini nchini Moroko walipinga vikali jaribio lolote la Sultani kulinda au kuruhusu vitegauchumi vya kigeni. Walijenga pia uadui kwa Wamoroko wengine walioshirikiana na Wazungu, na kuwashawishi wananchi kuwapinga, hasa pale Sultani aliposhindwa kuwaunga mkono maulama kwa kuchelea kuzua matatizo na mataifa ya Ulaya. Matokeo ya hali hii ni kuwepo kwa chuki ya jumla dhidi ya wageni nchini Moroko. Hali hiyo ilikuzwa na imani ya watu kuwa ufukara wao ulitokana na kuwepo kwa Wazungu nchini mwao.

Kila mtu alijitahidi kuwa mbali na wageni au kupunguza kabisa mawasiliano nao. Jamii ilikataa kupokea athari za kigeni na badala yake ilianza kujali zaidi mambo yake ya ndani. Mtazamo huu wa kugeukia ndani ulichukua sura ya kutukuza enzi za kale wakati hali ya mambo ilikuwa nzuri na maisha yalikuwa ya furaha. Viongozi wa dini walitaka sharia itumike katika nyanja zote za maisha ya jamii, na watu wajitakase kibinafsi, kimaadili na kidini.

Mabadiliko hayakutazamwa tena kwa jicho la kimagharibi, bali yalichukuliwa kumaanisha kuyarejelea maisha ya zamani wakati Uislamu na jamii vilikuwa havijachafuliwa na athari za kimagharibi. Vuguvugu hili lilijulikana kwa jina la *usalafi* (Uislamu wenye msimamo mkali). Ili kupunguza uga wa shughuli za Wazungu, Sultani aliyarefusha makusudi mazungumzo kuhusu mikataba, na kila ilipowezekana alichelewesha na kukwamisha utekelezaji wake.

Hivyo mbegu ya chuki dhidi ya wageni ilipandwa katika jamii hiyo kutokana na uzoefu wa pamoja wa umma. Madhila yote yaliyoonekana katika jamii hiyo yalisababishwa na kuingia kwa mtaji wa wazungu nchini humo na viongozi wa Moroko walitaka kuyaondoa maradhi haya. Lakini walikuwa wakiililia kale ambayo tayari ilikwisha kutoweka. Waliutukuza sana ukale, wakashindwa kuyaona matazamio mapya ya siku za baadaye.

## *Hitimisho*

Wakati Moroko ikikabiliwa na matatizo ya ndani ya nchi kama ilivyokwisha kuelezwa, haikufanya vibaya katika masuala ya kimataifa. Hadi kufikia 1880, ilikuwa inakaribia kuyatatua mengi ya matatizo yake ya kiuchumi, hii ikiwa na maana kuwa hata madeni yake ya nje yalikuwa takribani yamelipwa. Mkataba wa kimataifa uliotiwa saini hapo Julai, 1880 uliihakikishia uhuru wa Moroko. Nchi hiyo ililindwa na Ufaransa ikishirikiana na Uingereza na Hispania. Hivyo, utawala wa Hassan I ulikuwa ni kipindi cha fanaka nchini Moroko ambacho kilimfanya aonekane kiongozi shupavu nyumbani na nje ya nchi.

Aidha, wakati huo matatizo ya ndani ya nchi yalionekana kuwa yangeweza kudhibitiwa. Mageuzi yaliyofanywa wakati wa utawala wa Hassan I yalifikiriwa kuwa yangetosha kuvyaza Moroko mpya ya kisasa, huru, na yenye nguvu, kama isingalivamiwa na Ufaransa na Hispania. Hata hivyo, mwelekeo wa kimageuzi wa *Makhzen*, Uislamu wenye msimamo mkali wa maulama, na chuki ya watu wa vijijini kwa wageni - vyote kwa pamoja vilichangia katika kuchipuza uzalendo mkali wa Wamoroko katika karne ya ishirini.

Katika kutathmini matokeo ya sera hii ya mageuzi, ni lazima kutambua ukweli kuwa yalitokea katika kiunzi kilichoachwa na Muhammad III, ambaye alilazimika kusimamia mabadiliko katika uhusiano wa kimadaraka kati ya Moroko na Ulaya. Hivyo, unahitajika welewa wa kutosha wa mazingira ambamo Muhammad III alifanyia kazi yake kabla ya kufanya tathmini sahihi ya akuo wa jamii ya Moroko katika karne ya kumi na tisa.

# 19 Ruwaza Mpya za maingilioya Ulaya katika Maghrib

## *Utangulizi*

Ukoloni wa Wazungu katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa ulijitokeza zaidi katika upanuzi wa biashara na harakati za kutawala njia za biashara. Harakati hizi zilichukua umbo la vita vya majini kati ya madola ya Kizungu na watu wa Maghrib. Hadi ilipofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, maharamia wa Afrika ya Kaskazini walikuwa tishio kubwa kwa wafanya biashara wa Kizungu. Pia uhusiano kati ya Ulaya na Maghrib ulipooza kutokana na ugomvi huu kuhusu kodi za biashara na ushuru uliokuwa unalipwa na Wazungu kwa tawala hizi za Maghrib.

Hali ilizidi kuwa mbaya wakati maharamia kutoka Naples na Malta walipoanza kupora meli za kibiashara za Waislam kutoka Maghrib. Kana kwamba hilo halikutosha, baada ya vita vya Napoleon, Wazungu waliamiri safari nyingi za manowari dhidi ya Maghrib kwa kisingizio cha kupambana na uharamia. Nchi za Maghrib zilipigwa mabomu kwa mfuatano, na hadi ilipofikia mwishoni mwa muongo wa tatu wa karne ya kumi na tisa, mfumo wa meli wa Maghrib pamoja na jadi yao ya vita vya majini ilikwisha kuangamizwa. Hili lilifuatiwa na upanuzi mkubwa wa biashara ya Wazungu ndani ya Maghrib.

Jitihada zilizofanywa na Moroko na Algeria kulinda nafasi zao zilififiza uhusiano uliokuwepo kati yao na mataifa ya Ulaya. Sio tu kwamba serikali ya Algeria ilikataa kutoa haki maalum na upendeleo kwa Wafaransa, bali pia ilikataa kuwapa tahafifu maalum katika shughuli za kibiashara zilizozihusisha nchi hizo mbili. Jibu la Wafaransa kwa hatua hii lilikuwa ni kuizingira Algiers kwa manowari mnamo mwaka 1827. Moroko kwa upande wake iliamua kuwasusia wageni na kufuatilia kwa karibu mahusiano yake nao.

## *Shinikizo la Wazungu kwa jamii ya kijadi*

Miji ya Tunis na Tripoli ilikumbana na matatizo mengi ya kifedha kutokana na ukuaji wa biashara ya Wazungu na matatizo yaliyoambatana na hali hiyo. Wakati serikali za Tunisia na Tripolitania (Libya) zinatia sahihi hati za madai, mawaziri wake nao

walikuwa wanadidimia kwenye madeni. Hali hii iliwalazimisha kukubali kwa urahisi shinikizo la Wazungu na kuachana kabisa na upinzani wa kisiasa. Mikataba kati ya Tunis na Tripoli, na kati ya Tunis na madola ya Ulaya, ilipogoka. Nchi za Ulaya, hasa Ufaransa, zilipewa upendeleo mkubwa huko Tunis na Tripoli: Wazungu hawakutakiwa kulipa ushuru wa kibiashara, kanuni za biashara huria ziliimarishwa, na Ufaransa ilitangazwa kuwa taifa lililopendelewa zaidi. Kutokana na hali hiyo nafasi ya Ufaransa katika Afrika ya Kaskazini iliimarishwa, na wakati huo Tunisia ilikaribia sana kugeuzwa kuwa kibaraka wa Wafaransa. Kuongezeka kwa athari za Wafaransa katika Afrika Kaskazini kuliistua sana Uingereza, mshindani wake mkuu, na ili kudhibiti nguvu za Wafaransa katika eneo hilo, Uingereza ilifanya kila liwezekanalo kuhakikisha ushindi wa kikosi cha Uturuki kilichopelekwa Tripolitania mnamo mwaka 1835.

Waturuki, hata hivyo, walikutana na upinzani mwingi kutoka kwa wenyeji wa eneo lile baada ya kuanzisha upya utawala wao huko Tripoli, na walilazimika kuzima maasi mengi. Waturuki walipokuwa wanaituliza nchi, walianzisha mageuzi yaliyofuata mwelekeo wa Kizungu. Waliupangilia upya mfumo wa utawala, kodi, sheria na utaratibu wa kisheria. Mnamo 1851, mahakama ya mchanganyiko iliundwa huko Tripoli ambayo iliimarisha nafasi ya wageni. Mageuzi haya yote hata hivyo yalidhoofisha misingi ya jamii za jadi na kusababisha malalamiko kutoka kwa wenyeji.

Huko Tunisia, mageuzi yalianzishwa mwaka 1830 na kuendelezwa na Ahmad (1837-55) ambaye aliunda upya jeshi na kuanzisha kiwanda cha silaha. Pia alitaifisha uchumi kwa kuanzisha ukiritimba wa kiserikali. Benki ya taifa ilianzishwa mwaka 1847, na sarafu mpya ilianza kutumika. Zaidi ya hayo, alikomesha utumwa na kupiga marufuku uuzaji wa watumwa mnamo mwaka 1841. Kulikuwepo pia mageuzi katika elimu. Mwaka 1838 chuo cha kijeshi na cha ufundi vilianzishwa, na Watunisia walianza kusafiri nje ya nchi kutafuta elimu ya kigeni.

Serikali za Tunis na Tripoli pile ziliruhusu shughuli za wamisionari wa Kikristo. Wakatoliki walianzisha shule huko Tripoli, wakianzia na shule ya wavulana mwaka 1816 na kufuatiwa na shule ya wasichana mnamo 1846. Huko Tunisia walianzisha Chuo cha Mtakatifu Louis na shule chache za msingi. Kuanzishwa kwa matbaa ya Kiarabu pia kunaweza kuhusishwa na kipindi hiki. Gazeti la kwanza la Tunisia likiwa limechapishwa kwa Kitaliano lilitoka mwaka 1838.

Kufuatia maendeleo yote haya ya kisasa, hofu dhidi ya Wazungu huko Tripoli na Tunisia ilififia taratibu na kutoweka. Kuongezeka kwa mahusiano kati yao na Wazungu kulichangia katika mwamko wa kisomi wa nchi hizi na kuwafanya watawala wao kuwa na mwelekeo wa Kimagharibi. Hata hivyo, umma mzima, ambao mzigo wa mageuzi hayo yote uliwakabili, hawakuridhika na kuongezeka kwa athari za wageni, wala kugeuzwa kwa nchi yao kuelekea Magharibi. Waliwaona watawala wao kama wasaliti na hivyo waliendelea na maisha yao ya jadi. Wakati huohuo watawala wa Moroko na Algeria waliendelea kutilia shaka athari za Magharibi, na hawakuathiriwa nazo.

## *Ushinde wa Algeria*

Ushinde wa Algeria ulisuhulishwa na kutokujishughulisha kwa serikali yake. Baada ya

kuichokoza Ufaransa, Husayn Dey, mtawala wa Algeria, hakufanya lolote kujenga ngome, wala kuwapa watu wake silaha za kujihami na mashambulizi ya Wafaransa. Hivyo wakati wa mashambulizi ya Wafaransa Algeria haikuwa imejitayarisha kwa hali yoyote kuingia katika vita. Ijapokuwa ilikuwa na idadi kubwa ya askari - 40,0000 dhidi ya askari 37,000 wa Wafaransa - Algeria ilishindwa kabisa. Hii pia ilitokana na kutojitosheleza kwa jeshi lake katika mbinu za kijeshi na katika teknolojia pia. Kutokana na ushinde huu, Algeria ilikaliwa na Ufaransa mwaka 1830.

Julai 1830, Husayn Dey aliisalimisha Algeria kwa Wafaransa. Hapo ndipo aliporuhusiwa kuihama nchi yeye pamoja na familia yake, wajumbe wa baraza (madiwani) na familia zao, pamoja na askari wa Kituruki. Utawala wa Algeria kuanzia hapo uliachwa mikononi mwa jeshi la kivamizi, ambalo halikuwa na mpango wa kiutawala. Nchi iligawanywa sehemu mbili: Jili la Algiers na baadhi ya miji ya pwani ilikabidhiwa kwa Wafaransa, wakati wilaya za Oran na Konstantini sehemu za bara ziliwekwa chini ya utawala wa Tunis. Mgawanyo huu, hata hivyo, uliingiliwa mara kwa mara na Wafaransa ambao waliendelea kupanua himaya yao kuingia sehemu za bara kwa kadiri walivyotaka.

Mwaka 1834 Gavana Mkuu wa maeneo ya Wafaransa huko Afrika Kaskazini aliteuliwa. Wazo la kuikalia Algeria bila kuifanya koloni kamili, ambapo Wafaransa wasingaliitawala moja kwa moja, lilikubaliwa rasmi hadi mwaka 1840. Mara nyingi hii ilichukuliwa kumaanisha mfumo wa serikali usio dhahiri, ambapo watemi wa jadi walitumika kuwatawala watu. "Ofisi za Kiarabu" zilianzishwa kama kiungo kati ya makamanda wa Kifaransa na wenyeji. Wakati huo huo utawala wa kiraia ulioiga muundo wa utawala wa Ufaransa ulianza kujitokeza katika miji mikuu na miji ya pwani. Mwaka 1845, Algeria yote ilikuwa imegawanyika katika maeneo mawili: "eneo la Waarabu" ambamo sharia ilifuatwa, na "eneo la raia" ambamo mfumo wa kijamii wa Kifaransa uliendelezwa.

## *Upinzani wa Algeria*

Ushindi wa Wafaransa na kukaliwa kwa Algeria, vitu ambavyo vilileteleza kusalimu amri kwa mtawala Husayn Dey, vilisababisha ombwe la kisiasa nchini. Vituo kadhaa vya jadi havikutambua tena mamlaka yoyote, na idadi kubwa ya watu walikuwa na chuki kali dhidi ya kukaliwa kwao na Wafaransa. Watu walikuwa wamepania kulinda utamaduni na uhuru wao. Hata hivyo, upinzani huu ulijikita katika kiwango cha janibu tu kutokana na kukosekana kwa mamlaka unganishi ambayo ingeweza kuhamasisha umma wote. Upinzani huo haukuratibiwa vizuri na ulikuwa wa namna nyingi, kuanzia kukataa kutambua kukaliwa na wageni hadi kuuliwa kwa Wazungu kadhaa pamoja na wenyeji washirika wao.

Jinsi upinzani ulivyoongeza kasi, vituo viwili vikuu vilianzishwa: kimoja kilikuwa mashariki na kingine magharibi. Kituo cha upinzani cha mashariki kilichoongozwa na Ahmad Dey, gavana wa zamani wa Konstantini, kilikuwa ndicho tishio kuu kwa Wafaransa katika siku za mwanzoni za harakati. Ahmad alijaribu kurejesha mfumo wa

utawala wa *dey* na kujiimarisha kwa kutumia mabaki ya askari wa Kituruki. Alisitisha uoza wa utawala, na kuimarisha vyombo vya dola na kuliongezea jeshi nguvu.

Maasi huko magharibi mwa nchi yaliongozwa na Ábd al Kadir, ambaye alitegemea msaada wa kisiasa kutoka Moroko. Madhumuni yake yalikuwa: Kukomesha machafuko katika nchi; kutetea sharia, na kuongoza vita vitakatifu dhidi ya Wafaransa. Alikuwa gavana wa magharibi ya Algeria mwaka 1832 na alitambulika hivyo na Wafaransa. Aliweza kuimarisha mamlaka yake kwa kutumia nguvu zake, ari, na ushujaa, pamoja na ushindi wake dhidi ya Wafaransa mwaka 1835. Katika jitihada zake za kuleta mageuzi Algeria, ilimbidi kupambana na upinzani kutoka vikundi kadhaa na watu binafsi kama vile ma-*bey* wa Oran na Titeri. Mwishowe, alifanikiwa kuunda taifa unganifu la Kiarabu lililoungana na ambalo lilijumuisha theluthi mbili ya nchi ya Algeria ya sasa. Baada ya kukomesha machafuko na vurugu zilizokuwepo nchini, alianzisha mfumo wa kisheria na utawala ulioratibiwa. Pia alianzisha jeshi la kudumu, na uchumi uliodhibitiwa na dola kupitia mfumo wa uchumi wa kuhodhi. Kadhalika, alijenga viwanda vya silaha na ngome za kulinda nchi.

Katika hatua za mwanzo, upinzani wa Waalgeria dhidi ya Wafaransa ulikuwa na mafanikio makubwa kutokana na sera dhaifu za Wafaransa na pia kutokana na uwezo wao mdogo wa kupigana vita vya kuvizia (vya jangwani). Hadi 1837 Waalgeria waliweza kuwadhibiti Wafaransa vilivyo. Lakini mwaka 1837 Wafaransa walivamia Konstantini, makao makuu ya wapinzani wa Mashariki, na kuikalia. Ahmed Dey alikimbilia milimani ambako aliendelea kuwabughudhi Wafaransa pamoja na serikali yao waliyoianzisha huko mashariki hadi 1848.

Kuanguka kwa Konstantini kuliacha upinzani wa magharibi kama tishio kuu katika mapambano. Àbd al-K_dir alingolewa na Wafaransa 1843 na kutoka hapo alikimbilia Moroko akiwa na wafuasi wake kadhaa. Mfumo wa jeshi na utawala aliouanzisha nao pia ukaporomoka. Kushindwa kwake katika kipindi hiki kulitokana na vita vya jumla ambavyo Wafaransa waliviamiri dhidi yake. Kutoka hapo alijaribu kufufua mapambano kutoka kituo cha Moroko huku akisaidiwa na Sultani wa Moroko. Jambo hili lilisababisha vita baina ya Wafaransa na Moroko mnamo mwaka 1844. Matokeo ya vita hivyo yalikuwa ya maafa makubwa kwa Moroko kiasi kwamba Sultani alimkana Àbd al-K_dir kama kafiri na kuondoa msaada aliokuwa anampatia. Hili halikumzuia Àbd al-K_dir kuendelea kupigana na Wafaransa hata bila msaada wa Moroko. Jitihada zake zilipewa msukumo na udugu wa Taibiyya, ambao nao walitangaza jihadi dhidi ya Wafaransa. Mwishowe upinzani wake ulizimwa na Wafaransa mnamo mwaka 1847 na alilazimika kusalimu amri.

Baada ya tukio hili, vikundi vingine vidogovidogo viliendeleza upinzani huko Algeria lakini vyote viliishia kuzidiwa nguvu na Wafaransa. Ni baada ya mwaka 1857 ndipo nchi nzima iliwekwa chini ya utawala wa kijeshi wa Wafaransa.

## *Ukoloni na utumwa wa kifedha*

Wafaransa hawakueneza ukoloni wao katika mikoa ya bara ya Algeria kwa sababu ya kuchelea maasi ya umma katika maeneo hayo. Katika kuongoza maeneo yaliyofanywa



19.1 'Abd al-Ḳādir



**19.2** *Kikosi cha miguu cha Àbd al-K_dir*



**19.3** *Kikosi cha Farasi*

**19.4** *Kusalimu amri kwa Àbd al-K_dir*



makoloni sehemu za pwani kuzunguka Algeria na miji mingineyo, kwanza Wafaransa walichukua hatua ya usimilishaji ambayo iliifanya Algeria sehemu muhimu ya Ufaransa. Lakini hatua hii ilikomeshwa na (utawala wa) Himaya ya Pili Napoleon III hakuilaani tu sera hii, bali pia alitangua uwakilishaji wa Wafaransa walioishi Algeria katika bunge la Ufaransa. Kisha aliitangaza Algeria kuwa "Ufalme wa Kiarabu," hatua iliyowapendelea watemi wa jadi na kuwasononesha wakoloni. Eneo la makazi ya wakoloni wa Kifaransa (eneo la kiraia) vilevile liliwekewa mipaka maalum. Katika sehemu nyingine za Algeria, jeshi la Wafaransa lilishirikiana kutawala na uongozi wa jadi wa Kiislamu chini ya usimamizi wa "ofisi za mambo ya Waarabu."

Napoleon III pia aliweka taratibu nyingine za kiutawala nchini Algeria. Walowezi wa Kizungu walitakiwa kuishi mijini tu na kujihusisha na biashara na mambo ya kiufundi bila kujiingiza katika masuala ya bara. Baada ya 1863, ardhi ilitakiwa kuhifadhiwa kwa ajili ya jumuiya za Algeria na kumilikiwa kufuatana na kanuni za jadi za Kiislamu za umilikaji wa ardhi. Ardhi "ya ziada" ndiyo iliyochukuliwa kwa ajili ya serikali ya kikoloni na kukabidhiwa kwa makampuni na watu binafsi wa kigeni. Ujasirimali binafsi katika viwanda na biashara hazikuwekewa mipaka yoyote, na ukiritimba wa aina yoyote ulioanzishwa na watawala wa Algeria waliotangulia ulipigwa marufuku. Zaidi ya hayo, mfumo wa kisharia wa Kiislamu uliundwa upya mnamo 1854: Mahakama za mchanganyiko za kifaransa-Kiislamu na baraza kuu la sharia la Waislamu liliundwa. Desturi za kidini za Waislamu kama vile ujenzi wa misikiti na safari za kwenda kuhiji Makka zilihimizwa. Waalgeria walipewa fursa ya kujiunga na jeshi la Wafaransa pamoja na utawala. Mwishowe, mwaka 1869, rasimu ya katiba ilitayarishwa kwa ajili ya Algeria, ikitoa nafasi ya nchi kuwa na utawala wake wa ndani, na kuwa na wawakilishi wa Kiislamu katika mabaraza yote yaliyochaguliwa.

Ilipofikia katikati ya karne ya 19, Tunisia tayari ilikuwa ni nchi iliyojitawala yenyewe, ikiwa na ma-*bey*, ilhali Tripolitania ilikuwa chini ya utawala wa moja kwa moja wa Kituruki tangu 1835. Hata hivyo, kwa sababu ya kukua kwa athari na mitaji ya Wazungu katika Maghrib yote, mageuzi ya aina hiyo hiyo yalifanyika huko Tunisia na Tripolitania. Huko Tunisia kikundi kilichopendelea mabadiliko ya wastani (ya kiliberali), kikiwa kinaungwa mkono na mataifa ya Ulaya, kilitoa programu yake ya mageuzi mwaka 1857 na matokeo yake yakawa kupigwa marufuku ukiritimba wa dola na badala yake kuanzishwa kwa biashara za kibinafsi. Manispaa iliundwa upya, na katiba iliyowafanya mawaziri kuwajibika kwa baraza la wawakilishi lililoitwa Baraza Kuu ilitangazwa rasmi mwaka 1856. Huko Tripolitania utawala ulisukwa upya, na mahakama za kushughulikia biashara, uraia, na mambo ya jinai zilianzishwa mwaka 1865.

Mageuzi haya yalileteleza kuanzishwa kwa biashara za binafsi na kuingia kwa mtaji wa kigeni huko Maghrib. Kukomeshwa kwa vipingamizi vya ushuru kati ya Algeria na Ufaransa, kwa mfano, kulifungua milango ya masoko ya nchi hizi kwa bidhaa za kigeni. Makampuni kadhaa yenye mitaji mikubwa hatimaye yalianzishwa huko Maghrib. Benki a kwanza ya kigeni huko Algeria ilifunguliwa mwaka 1851, na huko Tunisia mwaka 1873. Huko Tripolitania, benki za kwanza kabisa zilijitokeza mwaka 1880. Mabenki, wafanya biashara waliopewa tahafifu na makampuni, walikuwa na uhusiano wa karibu karibu sana, na walinufaika na upendeleo wa kipekee huko Algeria na Tunisia. Huko

Tunisia, makampuni hayo yalichimba risasi, yalisafirisha nje majani ya esparto, na yalifanya majaribio ya kilimo cha pamba, viazi na tumbaku. Ujenzi wa (njia za) reli ulianzishwa huko Algeria mwaka 1857 na huko Tunisia 1859. Makampuni hayo ya kigeni pia yaligeuza bandari kuwa za kisasa, yalijenga njia za mawasiliano kwa telegrafu, yalijenga barabara, na yalianzisha mipango miji katika ukanda wa pwani.

"Maendeleo" ya Afrika ya Kaskazini kwa kutumia mtaji wa kigeni yaliimarishwa na mafunzo ya watendaji waliosharabu uzungu. Huko Algeria, shule ya kwanza ya sekondari ya mchanganyiko wa Wafaransa -Waarabu, ilianzishwa mnamo mwaka 1875, ikifuatiwa na chuo cha kufundisha ualimu. Pia huko Tunisia na Tripoli kulikuweko na shule ambazo zilifundisha lugha za kigeni. Matbaa ya Kiarabu pia yalianzishwa kwa mfululizo huko Algeria, Tunisia na Tripoli, na yalichapisha magazeti ya kijanibu.

Kuingia kwa mtaji wa kigeni katika nchi za Maghrib kulitokea katika vipindi tofauti. Huko Algeria, mtaji ulifika baada ya nchi kukaliwa na wakoloni na mtaji wa Wafaransa ndio uliochukua nafasi ya juu zaidi. Lakini huko Tunisia na Tripolitania, mtaji ulitangulia kutakiwa kwa nchi hizo na ulikuwa wa mataifa mengi. Mageuzi katika hizi nchi nyingine yaligharimiwa kwa mikopo ya kigeni chini ya masharti magumu sana. Jambo hili lilizidisha madeni yao ya kigeni. Hali ya Tunisia ilikuwa mbaya kiasi kwamba ilipofikia 1869 deni lake la kigeni lilikuwa limeongezeka kufikia mara kumi na mbili ya pato lake la taifa. Hali hii ilifanya serikali kujitangaza mufilisi na kukubali Tume ya Fedha ya Kimataifa (TFK) ambayo ilichukua udhibiti wa mambo ya kifedha, na kuigeuza Tunisia kuwa nusu koloni la utawala wa kizungu.

Maslahi ya Waingereza na Waitaliano katika Tume hii (TFK) yalikuwa makubwa. Lakini wakati Waingereza walijishughulisha zaidi na masuala ya Misri, Serikali ya Italia haikuweza kusukuma madai yake hadi miaka ya 1880. Ufaransa nayo kwa upande mwingine, baada ya kuzinduka kutoka katika ushinde wake wa 1870, ilianza kuitawala TFK. Waitaliano walielekeza matamanio yao huko Tripolitania. Lakini utawala wa Kituruki pamoja na umaskini wa kiasi fulani wa Tripolitania, uliihakikishia uhuru wake hadi baada ya 1911.

Moroko nayo ilishuhudia shinikizo la aina hiyo kutoka kwenye mitaji ya Kizungu, ijapokuwa iliweza kuizuia kwa muda mrefu zaidi kuliko nchi nyingine yoyote ya Afrika ya Kaskazini. Ingawa mkataba wa 1856 kati ya Moroko na Uingereza ulifungua milango ya Moroko kwa mitaji ya kigeni, ule wa 1860 kati yake na Hispania uliiwekea Moroko masharti magumu sana ya kifedha. Mikataba ya aina hiyo hiyo na Ufaransa *na* nchi nyingine za Ulaya ulifungua milango kwa nchi hiyo kutawaliwa na wakoloni.

Kushindwa kwa Algeria na kupenyezwa kibiashara kwa Tunisia, Moroko na Tripolitania kulifuatiwa na kukaliwa kwa nchi hizo na idadi kubwa ya wageni. Wageni hao walikuwa mawakala wa kibiashara ambao waliwakilisha viwanda vya kigeni na kufanya biashara kwa mapana, na hivyo kujikusanyia utajiri mkubwa. Walinufaika pia na upendeleo wa aina kwa aina ambao haukutolewa kwa wenyeji wa nchi hiyo. Kati ya walowezi wa kigeni, wale waliokuwa Algeria ndio waliopendelewa zaidi kuliko wengine. Hawa hawakuvutiwa tu na biashara, bali pia walitamani kumiliki ardhi ya

binafsi na kuendeleza kilimo. Walikuwa na mfumo wa kipekee wa sheria na utawala, na waliunda jamii iliyoshikamana na iliyojenga chuki kubwa kwa wenyeji wao. Kwa vile idadi yao iliongezeka upesi zaidi kuliko katika nchi nyingine, walibuni mbinu za kueneza athari yao katika utawala wa nchi na kuteka ardhi zaidi kutoka kwa wenyeji kuliko ile waliyokuwa wamepewa na manispaa.

## *Jibu la jamii za jadi*

Wenyeji walikasirishwa zaidi na zaidi na wageni hawa ambao, licha ya kutawala uchumi wao, walikuwa wanajipenyeza katika nyanja zote za maisha ya taifa lao. Ingawa baadhi ya maliberali wa Afrika Kaskazini walitambua matatizo ya nchi zao na kuelewa umuhimu wa mageuzi hayo, idadi kubwa ya wananchi waliwachukia wageni hao pamoja na programu za mageuzi za dola. Mageuzi hayo yalichochea chuki ya wacha Mungu wa *Kiislamu (murabiti)* na wenyeji wa vijijini ambao waliyaona kama hatua nyingine ya kutawaliwa na wakoloni. Zaidi ya hayo, Waislamu waliosharabu Uzungu walionekana na wenyeji wakulima na Wanomadi kama wasaliti na washirika wa wakoloni na walikataa kabisa kuwa na imani nao.

Hivyo mapambano dhidi ya wageni yaliungwa mkono na watu wengi karibu katika nchi zote za Kiislamu mwanzoni mwa miaka ya 1860. Wakati watu walipojiingiza katika propaganda kali ya jihadi ya Waislamu wote, maasi ya kijanibu dhidi ya serikali yalizuka karibu kila mahali. Katika kipindi hiki Udugu wa Sanusiyya uliouchunga Uislamu kwa ukali usichafuliwe na Uzungu, ulionyesha uwezo wake. Kwa vile maasi haya hayakuwa yamepangiliwa, yalichukua sura mbalimbali, kama vile uporaji wa vitu, uuaji wa watu, na kuharibu majengo ya Kizungu. Baadaye yalifuatiwa na maasi makubwa ya kitaifa.

Maasi ya kwanza ya kitaifa yalifumuka huko Tunisia mwaka 1864 na yaliongozwa na Udugu wa Tijaniyya. Hata hivyo serikali ya *bey* ilifanikiwa kuuokoa mji mkuu na kuangamiza maasi hayo kutokana na kutengwa kwa waasi hao na kukosa msimamo. Maasi mengine ya aina hiyo yaliyoongozwa na Udugu wa Dergawa yalizuka huko magharibi mwa Algeria mwaka 1864, na Wafaransa walifanikiwa kuyazima kwa taabu kubwa. Mwaka 1871, maasi ya kitaifa yaliyofikiriwa kuwa ni jihadi yalizuka mashariki mwa Algeria na kuenea sana, na Wafaransa hawakuweza kuyadhibiti kabla ya 1872.

Kuzimwa kwa maasi haya kulifuatana na uonevu wa jumla jumla, faini, utekaji wa ardhi pamoja na kuwanyanganya wenyeji silaha. Hata hivyo, wakati mambo haya yote yalipokuwa yanaendelea, walowezi wa Kizungu hawakujiunga na Waislamu; badala yake waliunga mkono mapambano ya silaha dhidi yao. Hata huko Algeria ambako walowezi weupe walikuwa pia wakipigania kanuni za kidemokrasia na kijamaa, hawakujitambulisha na matamanio ya Waislamu wa Afrika Kaskazini.

## *Kuelekea katika sera ya kibeberu*

Baada ya kuzimwa kwa maasi yaliyoelezwa hapo juu, njia iliandaliwa ya kuiingiza Afrika kaskazini katika ukoloni. Hali hii ilijitokeza wakati maendeleo ya huko Ulaya na kuenea kwa ubepari kulihitaji upanuzi wa kikoloni. Upanuzi huu hatimaye ulichukua muundo wa mapambano miongoni mwa tawala za Kizungu ili kuugawanya ulimwengu na kuhodhi vyanzo vya mali ghafi.

Ukoloni ulipata ushindi wake mkubwa mmojawapo huko Algeria. Nchi hiyo ilitawaliwa moja kwa moja na wakoloni waliojiita "wananchi" ambao walijiunda katika tabaka lenye kupendelewa lililofaidika na haki zote za kiraia na za kisiasa. Wenyeji walinyimwa haki yoyote ile na waliitwa kwa dharau kama "raia." Masetla weupe pia walijipatia ardhi kubwa kwa kuwanyang'anya wenyeji. Kwa kuongezea, uwekezaji wa mitaji ya Wafaransa uliongezeka sana, na uhusiano wa kiuchumi na Ufaransa ulikuzwa.

Tunisia nayo ilishuhudia hali ya namna hii kuelekea mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Mwaka 1881, vikosi vya Ufaransa viliingia nchini, na kiongozi wa wenyeji alitakiwa atie sahihi mikataba kadhaa ambayo iliwapatia Wafaransa haki ya kuiweka nchi hiyo chini ya ulinzi wake. Moroko na Tripolitania zilifanikiwa kuahirisha kukaliwa na Wazungu, ijapokuwa Moroko haikufanikiwa kukatiza upendeleo na kiburi cha wageni walioishi nchini humo.

Kwa Waislamu wa Afrika ya Kaskazini, kukaliwa kwa nchi hizi na Wazungu kulionekana kama mashambulizi dhidi ya Uislamu. Hivyo mapambano ya Waislamu yaliungwa mkono na nchi za Kiislamu za Mashariki. Huku wakitegemea sana kuungwa mkono, Waislamu wa Algeria na Tunisia walijaribu kwa mara nyingine kupinga ukoloni kwa nguvu. Lakini licha ya ujasiri na ukali wa vuguvugu hizo, maasi hayo yalishindwa kufikia malengo yake. Hatua hizi hata hivyo zingeweza kuchukuliwa kama hatua za wananchi zilizochelewa za kulinda jadi, utamaduni na utambulisho wao; vitu ambavyo tayari vilikuwa vimekwisha kudhoofishwa na ushindi wa wageni na kumomonyolewa na ubepari wa kikoloni ulioanzishwa katika ardhi yao.

# 20 *Sahara katika karne ya kumi na tisa*

Sura hii inaiangalia historia ya Sahara katika karne ya kumi na tisa katika viwango viwili. Kiwango cha kwanza kinaangalia historia ya ndani ya Sahara, ambayo hasa inahusu mageuzi na mabadiliko-badiliko katika maisha ya Wanomadi na wakazi wa oasisi. Kiwango cha pili kinachunguza mahusiano kati ya watu wa Sahara na dunia ya nje, kwa kutilia mkazo kwenye athari za kujipenyeza kwa uchumi wa Ulaya katika maisha yao. Kutokana na uhaba wa maandishi juu ya historia ya jamii kadhaa za Sahara, tutajaribu tu kukagua maendeleo yaliyokuwepo jangwani kwa kuzingatia zaidi Wanomadi waliotumia ngamia. Kikundi hiki kilikuwa mashuhuri sana huko jangwani kwa sababu utajiri wao uliotokana na kumiliki ngamia uliwapa uwezo mkubwa wa kijeshi ambao waliutumia katika kupora na kunyang'anya mali za wakazi wa oasisi na jumuiya nyingine za wakulima. Hata hivyo, ni lazima ieleweke kwamba ijapokuwa Wanomadi hawa waliwavamia wakulima ili wapate watumwa na hata kuwadai ushuru ili wawalinde dhidi ya maadui, lengo lao kuu halikuwa kuwaangamiza bali kujaribu kudhibiti uzalishaji wao. Kutokana na hilo, wakiwa ni watendaji wakuu wa mabadiliko ya kisiasa, kijeshi na kidini huko Sahara katika karne ya kumi na tisa, Wanomadi hawa waliotumia ngamia wanastahili kuzungumziwa kwa mkazo maalumu.

## *Jamii na mazingira*

Kutokana na mazingira ya ukame jangwani, watu walijiunda kama Wanomadi (wahamahamaji) huku wakifuga wanyama wa aina mbalimbali. Lakini hii siyo kusema kuwa eneo lote la Sahara lilikuwa kame, au kwamba watu wote walioishi humo walikuwa Wanomadi. Kulikuwepo na tofauti, siyo tu katika hali ya hewa bali pia katika mandhari ya jangwa, mambo ambayo yaliathiri wakazi na miundo ya jamii zao.

Huko jangwani kiasi cha mvua kilitofautiana kutoka upande mmoja hadi mwingine. Kipande cha kati mashariki ndicho kikame kuliko zote; kipande hicho kiko eneo la sasa la Misri na mashariki ya Libya. Sehemu nyingine zinanufaika na mvua za zaidi ya wastani, ambazo hukatisha jangwa kutoka kaskazini hadi kusini, na kuvuka sehemu kame za katikati. Idadi ya watu katika maeneo yenye maji mengi ni kubwa, na wasafiri walikuwa wakikwepa mikoa yenye ukame mkali zaidi. Kilimo kinawezekana katika maeneo yenye unyevuunyevu na baadhi ya sehemu zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Tofauti hizi katika mazingira ya jangwani zimewaathiri watu wanaoishi humo. Wafugaji imewalazimu kuhama kutoka eneo moja hadi jingine pamoja na mifugo yao ili kutafuta malisho. Watu wanaoishi ukingoni mwa jangwa wametumia vizuri fursa ya mazingira yao na kujirekebisha kulingana na hali hiyo. Katika eneo la pwani ya kusini ya jangwa hili, lililoitwa Sahel, Wanomadi wenye kufuga ng'ombe na jumuiya za wakulima walifanya makazi na kuishi katika hali ya uhusiano wa kutegemeana na wa amani. Kutokana na mahitaji ya mazingira yale, baadhi ya Wanomadi walilazimika kuwafanya baadhi ya ndugu zao kuwa wakulima huku wengine wakihudumia mifugo. Wengine walipanda mazao, wakaondoka pamoja na mifugo yao kwenda kutafuta malisho, na kisha kurejea kuvuna mavuno yao machache kutoka mashamba yao yasiyotunzwa. Katika sehemu za katikati, yaani sehemu kame kuliko zote za jangwa, Wanomadi walitunza wanyama wa aina mbalimbali lakini waliwategemea sana ngamia ambao waliweza kuzoea vizuri kabisa mazingira ya ukame. Aidha, walilazimika kuhama kwa masafa mafupi au marefu kila baada ya muda fulani, kutegemeana na upatikanaji wa malisho yaliyohitajika.

Mazingira ya ukame pia yaliathiri miundo ya kisiasa ya Wanomadi hao. Walijenga mifumo ya kisiasa inayofanana, isiyo unganifu, na ambayo imeelezewa kama "mifumo ya kinasaba iliyogawanyika." Muundo huu uliwawezesha watu kutawanyika ili kutafuta malisho, na pia kuunganika wakati ilipolazimu kukabili uvamizi kutoka nje. Jamii za aina hiyo zilipangiliwa kwa mujibu wa uhusiano wa kinasaba, yaani kutoka babu mmoja. Mamlaka ya kinasaba yalikuwa makamilifu, migogoro ya ndani iliweza kusuluhishwa bila kuhusisha mamlaka kuu ya nje. Kadhalika, koo hizi tofauti ziliweza kuungana ili kupambana na tishio kutoka nje, na kiini cha muungano huo kiliwakilisha mamlaka kuu (unganifu). Hata hivyo, watu wasiohamahama na wale wenye kuhamahama baadhi ya nyakati tu waliweza pia kusimilishwa na vikundi vya Wanomadi na hivyo kuonyesha kwamba udugu (wa damu) haukuwa kanuni pekee ya ushirikiano kati ya wakazi wa jangwani.

Kitu kingine kilichowafanya watu wa jangwani wafanane ni muundo wa kitawalamsonge wa jamii zao. Kwenye kilele cha ngazi ya jamii zilikuwepo nasaba za maaskari wa tabaka la waungwana. Chini yao vilikuwepo vikundi vya watu huru lakini waliotawaliwa kisiasa. Hawa walikuwa ni vizalia vya Wanomadi waliotiishwa. Watu wa chini kabisa walikuwa ni watumwa au dhuria wa watumwa waliofanya kazi kama watumishi, wachungaji, mafundi mchundo, wataalamu wa biashara na wakulima.

## *Kubadilisha mahusiano na dunia ya nje*

Maisha ya jangwani hayakuwa ya kutengwa moja kwa moja. Ijapokuwa wanomadi, kwa mfano, waliishi katika dunia yao wenyewe, walilazimika kutegemea jumuiya za wakulima wakazi kuwapatia r..faka pamoja na vifaa vingine muhimu walivyohitaji kwa vile hawakuweza kuishi kwa kutegemea mifugo yao tu. Ili kupata vifaa hivi vingine hawakutegemea kupora na kutoza ushuru tu, bali pia walitegemea biashara ya amani kati yao na wale wenye makazi ya kudumu. Mahusiano makunjufu kati ya Wanomadi na

vikundi visivyohamahama yalihimizwa kwa vile Wanomadi hao wachokozi hawakuwa tishio kubwa la kijeshi kwa watu walioishi mahali pamoja katika kundi kubwa, na walioweza kuutumia vizuri wingi wao kujihami.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, ruwaza ya maingiliano kati ya Wanomadi na dola za wakazi wa kudumu katika ukingo wa kaskazini wa jangwa, zilitofautiana sana na zile za ukingo wa kusini. Katika kingo za kusini mwa jangwa, wakazi wa kudumu walijaribu kupunguza usumbufu wa Wanomadi kwa kuwahusisha katika uchumi wa maeneo yenye rutuba. Jambo hili lilifanyika kwa kuwashirikisha katika biashara ya ukingo wa jangwa, kilimo na ukuaji wa miji. Walijaribu pia kuvigombanisha vikundi vya Wanomadi. Ijapokuwa vizuizi vya kijiografia vya Afrika ya Kaskazini kama vile milima ya Atlasi na safu nyingine za milima viliwaweka Wanomadi katika umbali wa kutosha, wakazi wa ukingo wa kaskazini wa jangwa bado walihitaji kupambana nao. Zaidi ya njia zilizotumiwa na wakazi wa ukingo wa kusini kupambana na Wanomadi hawa, nchi za Maghrib zilizokuwa kaskazini mwa jangwa zilionyesha ustadi mkubwa na hila katika kuwatawala Wanomadi na kugonganisha kundi moja dhidi ya jingine, na hivyo kuondokana na mgogoro wa moja kwa moja kati yao na Wanomadi hao. Pia utajiri wa nchi hizi za Maghrib uliziwezesha kuwa na vikosi vya jeshi vyenye silaha nzuri vilivyoingilia mara kwa mara kukomesha kiburi cha Wanomadi. Lakini badala ya kutegemea nguvu za kijeshi pekee, watawala wa Afrika Kaskazini pia walitumia nafasi zao kama watawala wa nchi za Kiislamu kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na Wanomadi hao ambao wengi wao walikuwa wamekwisha kusilimu.

Wafaransa walipoanza kuingia ndani ya Algeria, na Waturuki kujipenyeza nchini Libya, kulitokea mabadiliko katika mahusiano kati ya jamii za Sahara na dunia ya nje. Msukumo wa kuelekea kusini wa Waturuki na Wafaransa huko jangwani ulikuwa na lengo lililofanana, yaani kudhibiti na kutoza ushuru biashara iliyovuka Sahara, na kuzuia mataifa mengine yasipate mahali pa usalama katika bara iliyo nyuma ya Mediterania. Lakini pamoja na kuyafanya haya wakati uleule na kwa kasi ileile, mitindo ya mataifa haya mawili ilitofautiana sana.

Waturuki walikuwa na hadhari kubwa katika kushughulika na Wanomadi waliokuwa ndani ya himaya zao huko Libya. Walitumia vizuri mgawanyiko na urafiki uliokuwepo kati ya vikundi vya Wanomadi kwa manufaa yao wenyewe. Ufahamu wao wa siasa ya wenyeji na uzoefu wao wa kutawala jamii za watu walioishi katika vikundi vidogo vidogo uliwasaidia katika mahusiano yao na Wanomadi wa jangwani. Walianzisha muungano wa kidiplomasia na vikundi vile ambavyo walishindwa kuvitawala, na kuwa na athari kubwa kutokana na hadhi yao kama viongozi wa kitovu cha kisiasa cha dunia ya Uislamu. Walichukua udhibiti wa moja kwa moja wa Libya mnamo mwaka 1835 kutoka nasaba ya utawala ya Karamanli ili kuzuia kuenea kwa athari ya Wafaransa kutoka Algeria nchini Libya. Maofisa wa Kituruki waliwekwa jangwani kusimamia jitihada za kukusanya kodi zilizotozwa kwenye mitende ya Jalo na Awjila na kulinda usalama katika maeneo ya jangwa yaliyowazunguka.

Baada ya muda Waturuki walianza kujihusisha katika migogoro ya Wanomadi katika juhudi ya kuwalinda wakazi wa oasisi wa Awjila dhidi ya mashambulizi ya Wanomadi

hao. Maofisa wa Kituruki pia walijaribu kutawala kwa kupitia viongozi wa jadi, lakini athari ya jumla ya Waturuki huko jangwani haikuwa kubwa. Na ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, maeneo ya ndani ya jangwa yalikuwa tayari yanatawaliwa na Sanusiyya, udugu wa kidini ulioanzishwa miaka ya 1840.

Ni vizuri kutilia maanani kwamba kujiingiza kwa Waturuki huko Sahara, ijapokuwa hakukuwa kwa mapana, kulikumbana na upinzani mkali kutoka kwa Wanomadi. Lakini licha ya rasilmali zao ndogo za kijeshi, Waturuki waliweza kuingilia siasa za Wanomadi na kusababisha vurugu za kutosha miongoni mwao. Mfano mmojawapo ni kuvurugwa kwa kikundi cha Awlad Sulayman na washirika wake mwaka 1840-41 kulikosababishwa na Ali Askar, aliyekuwa Pasha (gavana) wa Kituruki wa Tripoli.

Wafaransa, kwa upande wao, walikosa ustadi wa kuingilia siasa za wenyeji na badala yake walitegemea sana matumizi ya nguvu za silaha. Walianza kwa kumshinda Abd al-Kadir ambaye walimwona kama kipingamizi cha kwanza kwa upanuzi wa himaya yao huko Algeria mnamo 1847. Ili kutoa ulinzi kwa biashara iliyovuka Sahara kati ya Algeria na Sudan ya Magharibi ambayo walitaka kuiendeleza, Wafaransa walianzisha vituo vingi vya ulinzi wa kijeshi huko jangwani. Hata hivyo, shughuli zao huko jangwani zilivurugwa na maasi kutoka kwa vikundi vya Wanomadi kama vile vya Awlad Sidi Shaykh na Ahaggar Tuareg. Ni mpaka Wafaransa walipoanza kuwaandikisha Wanomadi katika jeshi lao la uvamizi ndipo walipoweza kuangamiza karibuni upinzani wote mkali uliokuwepo dhidi ya upanuzi wao. Hii ni kwa sababu waliweza kuunganisha ubora wa silaha zao na wepesi wa kusafiri jangwani na ufahamu wa janibu hizo wa Wanomadi waliongizwa katika jeshi.

Serikali ya Moroko nayo pia ilikuwa na maslahi yake huko jangwani, nayo ni kupanua nchi yake kuvuka milima ya Atlas hadi jangwani. Lakini tofauti na Wafaransa, serikali hiyo haikuwa na uwezo wowote wa kuajiri jeshi la kufanya shughuli hiyo. Walichokifanya masultani wa Moroko ni kuingiza mizengwe katika uhusiano wa kijeshi na wa kidiplomasia uliokuwepo baina yao na jamii za jangwani. Walijiingiza katika siasa za wenyeji kwa kuunga mkono kikundi kimoja cha Wanomadi dhidi ya kingine, kwa kusuluhisha migogoro, na kwa kutumia hadhi yao kama viongozi wa kidini kama walivyofanya Waturuki. Njia hii ya mwisho ya kueneza athari yao ilikuwa na nguvu sana kwa vile athari za kidini za Sultani wa Moroko katika karne ya kumi na tisa zilikuwa zimeenea mbali sana hadi Sudan ya Magharibi.

Kati ya nguvu zote za nje zilizokuwa zinajaribu kujipenyeza jangwani katika karne ya kumi na tisa, Wafaransa ndio waliokuwa muhimu zaidi. Hii ilitokana na sababu kwamba kukaliwa kwa jangwa la Algeria na Wafaransa ndiko kulikoanzisha kipindi maalumu cha mahusiano kati ya jamii za jangwani na dunia ya nje. Kukaa kwa Wafaransa (katika jangwa hilo) kulidumu zaidi kuliko safari za nadra za kuingia jangwani zilizofanywa na Sultani wa Moroko au ziara zisizopangiliwa zilizofanywa na maofiza wa Kituruki katika oasisi za Sirenaika. Wanomadi, kwa mara ya kwanza, walijikuta wakipambana na jeshi lililokuwa na silaha za kisasa, viongozi wa njia na wapiganaji wenye kulifahamu jangwa vizuri sana. Si hivyo tu, Wafaransa waliwatawala Wanomadi kupitia Ofisi za Kiarabu, zilizoendeshwa na maofisa wasomi waliosomea mitalaa ya Waislamu ili kuwa na uwezo

mkubwa zaidi wa kuwasimamia, na waliowatawala wenyeji kupitia kwa machifu walioteuliwa. Kwa jumla, kukaliwa kwa Sahara na Wafaransa kulikamilika zaidi kuliko kule kulikofanywa na jumuiya nyingine zilizoshi katika kingo za jangwa. Aidha, kulisababisha kunyonywa kwa rasilmali chache za kilimo zilizopatikana jangwani.

Kama jibu la kukaliwa na Wafaransa, Wanomadi walianza kushirikiana zaidi ili kulinda maslahi yao na kuepuka kujisalimisha bila masharti kwa mvamizi kutoka nje. Dini ilitumika kama kipengele cha kuunganisha watu katika vyama vikubwa vya upinzani vilivyovuka mahusiano ya kiukoo. Mashirika ya kidini na viongozi wao walioheshimika, ambao walikuwa wakitoa huduma muhimu za kisiasa na za kidini, walitokea kuwa mabingwa wa kisiasa na kijeshi wakati wa migogoro hiyo. Hivyo upinzani dhidi ya Wafaransa ulijidhihirisha kupitia kwa viongozi na jumuiya za kidini.

Zaidi ya kuchochea upinzani, kujiingiza kwa nguvu kwa Wafaransa katika jangwa pia kulizusha hali ya uchumi isiyokuwa ya kawaida. Kwa mfano, Waahaggar Tuareg, baada ya kutenganishwa na masoko yao ya kaskazini, walibadilisha msingi wa uchumi wao. Marekebisho haya ya kiuchumi yalichukua sura ya kuingiza bidhaa mpya za biashara na kuanzisha njia mpya ya biashara katika miaka ya 1880. Hili liliwezekana kutokana na umoja wa Waahaggar ambao, nao ulitokana na migongano baina yao na majirani zao katika miaka ya 1870.

Jambo jingine katika upinzani dhidi ya Wafaransa lilikuwa ni ongezeko la kuhamahama kwa Wanomadi waliotumia ngamia pamoja na mifugo yao. Mfano halisi wa tukio hili ulikuwa ni tukio la Wajeramna ambao waligongana na Wafaransa mwaka 1881 karibu na Géryville. Kutoka hapo walianza kuvinjari jangwa kutoka pembe moja hadi nyingine, kwa karibuni miaka hamsini, kabla ya kurejea maskani yao ya awali huko Géryville mnamo mwaka 1925.

## *Biashara ya jangwani na Wanomadi*

Mabadiliko ya kiteknolojia huko Ulaya katika karne ya kumi na tisa hayakurahisisha tu kutekwa kwa Sahara, bali pia yalibadilisha maisha ya kiuchumi ya jangwani. Hii ni kwa kuwa uzalishaji wa bidhaa rahisi ulikuza awamu mpya ya kujipenyeza kwa Wazungu. Biashara na Ulaya iliongezeka sana katika karne ya kumi na tisa ikiwa na athari tofauti kwenye uchumi wa ukanda wa Sahara. Vikundi kadhaa katika ukingo wa Sahara vilijihusisha katika kusafirisha nje bidhaa kama vile sandarusi, manyoya ya mbuni na ngozi za mbuzi zilizotiwa rangi. Kupenya kwa uchumi wa Wazungu pia kuliathiri vionjo vya walaji; kwa mfano desturi ya kunywa chai yenye sukari nyingi ilienea katika karne hiyo.

Biashara ya kuvuka Sahara ilisababisha pia kuanzishwa kwa mahusiano ya karibu zaidi na uchumi wa dunia. Waliohusika katika biashara hiyo walikuwa wafanyabiashara, viongozi wa misafara, wasafirishaji, na wahariji (wauzaji wa bidhaa nje ya nchi). Wakazi wa oasisi za kaskazini kama vile Tafilalet na Fezzan walikuwa na dhima muhimu sana katika kupanga na kugharamia biashara hiyo. Ijapokuwa vikundi vya Wanomadi kama vile Waaggar Tuareg na Watubu walifanya biashara ya watumwa na bidhaa nyingine kwa kiwango kidogo, kazi yao kubwa ilikuwa ni kutoa wanyama wa



**20.1** *Biashara ya kwenye ukingo wa jangwa: Wafanya biashara kutoka Afrika Kaskazini wakinunua sandarusi katika kituo cha Bakel kwenye mto Senegal.*

kusafirisha mizigo, viongozi wa misafara, na jeshi la kusindikiza misafara hii. Hivyo karibuni Wanomadi wote wa Sahara walishiriki kikamilifu katika biashara iliyopitia maeneo walimoishi.

Hata hivyo, biashara katika njia mbalimbali za Sahara haikuwa imara. Biashara ilipanda na kushuka kwa kadiri ilivyofifia au kukua, na hali hii iliathiri maendeleo ya jamii za jangwani. Udhibiti wa njia za biashara hiyo ulitafutwa kwa nguvu kiasi hicho kwa sababu ya pato kubwa lililotokana nayo. Hata hivyo, ulimbikizaji wa utajiri mkubwa mikononi mwa vikundi maalumu mara nyingi ulitibua uwiano wa kisiasa-jamii, na kufifia kwa njia hai ya biashara hiyo kulisababisha kujirekebisha kwa makundi yaliyoathiriwa. Kujirekebisha huko kuliweza kuwa ni kujiingiza zaidi katika biashara ya kikanda ya ukingoni mwa jangwa, au kuwavamia majirani matajiri, au kujishughulisha na ufugaji.

Jinsi eneo na ukubwa wa biashara ya kuvuka Sahara vilivyozidi kubadilika, biashara hiyo ilihama kutoka kwa Wafaransa wa Algeria na kuwatia uchungu sana mabeberu wa Kifaransa. Wafaransa walijaribu kurekebisha hali hiyo lakini mwenendo wa biashara haukuwakubalia. Hali ilikuwa ni ya kubahatisha: njia nyingine za biashara zilikuwa zinastawi wakati nyingine zinadidimia. Kwa mfano, njia ya Tripoli-Kano ilipata umaarufu hasa baada ya katikati ya karne ya kumi na tisa kutokana na ongezeko la biashara katika njia hiyo. Biashara katika njia hii ambayo iliendeshwa na Watuareg ilianza kudidimia kutokana na sababu kadhaa, muhimu zaidi ikiwa ni ile ya kuanzishwa kwa reli huko Kano katika mwaka 1911. Njia ya Benghazi-Wadai ilirithi umaarufu wa njia ya Tripoli-Kano na kudumu hadi kuingia karne mpya kwa sababu ya Sanusiyya, na pia kwa kuwa maeneo yaliyohudumiwa na njia hiyo yalikuwa makubwa sana.

Sanusiyya kilikuwa ni kikundi cha udugu wa Kiislamu kilichoenea miongoni mwa



20.2 *Mnara wa Msikiti wa Agades*

Mabedui wa Sirenaika baada ya 1843 na baadaye kusambaa kuelekea kusini kwa kufuata njia ya Banghazi-Wadai. Udugu huu uliovuka eneo zima la njia hiyo, uliwapatia wafanyabiashara mfumo wa pamoja wa kisheria, kijamii na kibiashara, pamoja na mfumo wa posta. Viongozi wa udugu huo walijitahidi kuendeleza biashara katika njia hii kwa kudumisha amani. Hata hivyo walinufaika na biashara hiyo kutokana na makusanyo ya ushuru, malipo ya sehemu za kuhifadhi bidhaa, na zawadi kutoka kwa wafanyabiashara.

Biashara ya kuvuka Sahara iliathiri maisha ya Wanomadi kwa njia mbalimbali. Wanomadi wengine karibu na Sahel ya Afrika ya Magharibi waliwavamia Wasudan kwa ajili ya kupata watumwa ambao waliwachuuza kama bidhaa yao wenyewe, ijapokuwa wao zaidi walikuwa ni wasafirishaji na sio wafanyabiashara. Athari kubwa zaidi ya biashara ya watumwa kwa jamii ya Sahara labda ilikuwa ni upatikanaji kwa urahisi wa nguvukazi ya watumwa ambayo ilitumika kupanua jamii, hasa zile zilizoishi ukingoni mwa jangwa, ambako nguvukazi ilihitajiwa kwa ajili ya kuchunga mifugo, kilimo na shughui za ufundi. Hali hii ilikuwa hasa hivyo kwa umma wa Tuareg. Idadi ya watumwa waliovushwa jangwani iliongezeka kadiri karne ilivyozidi kusonga mbele, Afrika ya Kaskazini na ya Mashariki ya Kati zikiwa zinapokea watumwa wengi zaidi ya idadi ziliyoipokea katika karne za nyuma.

Biashara ya silaha ya kuvuka jangwa pia iliendelea pamoja na kwamba zilikuwepo jitihada za Wazungu kuizuia. Silaha za Kizungu zilikuja kupendwa sana huko Sahara kiasi kwamba bunduki za Kizungu zilikuwa jambo la kawaida katika miaka ya 1890. Kuenea huku kwa silaha miongoni mwa waporaji bila shaka ndiko kulikosababisha ongezeko la wasiwasi katika njia ya Tripoli-Kano baada ya 1898. Athari nyingine ya biashara iliyovuka Sahara ilikuwa ni uimarishaji wa Watuareg ambao nguvu zao za kiuchumi huko jangwani zilitegemea sio tu uwezo wao wa kusafiri haraka na umiliki wa ngamia, bali pia umilikaji wa silaha zilizopatikana kutokana na biashara ya kuvuka Sahara. Jambo hili liliwafanya wawe na nguvu nyingi, na wenye kuogofya: walikuwa ni marafiki wenye nguvu kwa sababu ya uwezo wao wa kiuchumi, na maadui wa kutisha kutokana na nguvu zao za kijeshi.

Watu wa jangwani pia waliathiri watu wa Sudan kiuchumi, kisiasa na kidini. Kisiasa, jihadi ya karne ya kumi na tisa ilipelekea katika kuundwa kwa Ukhalifa wa Sokoto, nchi kubwa ambayo ilikuza uchumi katika eneo lake la kati karibu na Kano, Katsina na Zaria. Mazao ya ziada ya maeneo haya, hasa nguo, yalisafirishwa nje kuuzwa huko Sudan ya kati na nchi ya Tuareg huko kaskazini. Hivyo, ukuaji wa uchumi wa jangwani ulichangia katika matukio ya eneo la savana.

Sahara ya Kusini pia ilitumika kama hazina ya taaluma ya Kiislamu ambayo katika karne ya kumi na tisa watu wa savana waliendelea kunufaika nayo. Jambo muhimu katika jamii za Sahara lilikuwa ni mgawanyiko kati ya nasaba shujaa na nasaba takatifu. Wakati nasaba za mashujaa zilitamani vita na siasa, zile za watakatifu zilikuwa na itikadi ya ukadiri na amani, uzoefu katika biashara na ushiriki katika jadi ya usomi. Nasaba za watumishi wa dini zilibobea katika sayansi mbili muhimu kisiasa, yaani falsafa ya sharia na imani ya Mungu. Kwa hali hiyo walijikuta wakitenda kazi za upatanishi na shughuli

zao zilichanganya mambo ya uchumi, siasa na uanazuoni. Walidumisha na kuendeleza uanazuoni wa Kiislamu, na athari yao ilienea hata kusini mwa jangwa.

## *Hitimisho*

Karne ya kumi na tisa ilikuwa ni kipindi chenye mabadiliko ya kusisimua huko jangwani. Umoja wa uchumi wa Afrika Kaskazini ulibomolewa na Wafaransa walipoikalia Algeria na kukengeua njia za biashara ziliyovuka Sahara mashariki na magharibi ya Algeria. Hadi ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, biashara ya kuvuka Sahara ilikuwa karibu imedidimia kabisa. Hata hivyo, utafiti zaidi unatakiwa ufanyike kuhusu athari za biashara hii katika maisha ya Wanomadi. Mazingira ya jangwa yaliamua namna Wanomadi walivyokabiliana na uvamizi wa kigeni, kama ule wa Wafaransa. Lakini utafiti zaidi pia unahitajika juu ya athari za kupenya kwa Wazungu katika uchumi wa ukanda uliokuwa ukingoni mwa jangwa. Hata hivyo, wazo kuu linalojitokeza katika historia ya Sahara ni athari kubwa ya hali ya hewa juu ya watu pamoja na maendeleo yao ya kihistoria, ijapokuwa kwa wakati huu upo upungufu mkubwa wa data zenye kina za kuthibitisha jambo hili.

# 21 Mapinduzi ya Kiislamu katika karne ya kumi na tisa huko Afrika Magharibi

Eneo tunalotaka kulichunguza katika sura hii lilijulikana kwa wasafiri wa Kiarabu na wanahistoria kama *Bilad el-Sudan* (nchi ya watu weusi). Ukanda huu ulikuwa na nduni za kipekee zilizoathiri umuhimu wake katika historia. Moja ilikuwa ni urari wa kuvutia uliodumishwa kati ya mazingira, mwanadamu na wanyama. Ulinganifu huu pia uliweza kupatikana kati ya wakulima waliotulia kwenye maeneo yao na Wanomadi wachungaji; kati ya watu huru na watumwa; na kati ya Waislamu na wafuasi wa dini za jadi. Mkoa huu pia ulikuwa ni kituo muhimu cha biashara ambapo bidhaa kutoka nje na bidhaa asili ziliweza kubadilishwa. Zaidi ya hayo, eneo hilo liliruhusu kusafirisafiri sana na kuchanganyika kwa wakazi wake, kama inavyodhihirishwa na kuenea kwa Wafulbe, kutoka maskani yao ya asili huko Futa-Toro, katika eneo pana la Bilad el-Sudan lililotanda kutoka Bahari ya Atlantiki hadi Ziwa Chad na hata Kameruni. Tena, ukanda huu ulishuhudia kuanza kwa *dar al-Islam* huko Afrika Magharibi, na baada ya kipindi kirefu cha kuenea kwa Uislamu kupitia mafundisho na mahubiri, ukanda huu ulishuhudia vuguvugu lililozaa miliki kuu tatu za ukhalifa katika karne ya kumi na tisa: ukhalifa ya Sokoto huko Nigeria ya Kaskazini, ukhalifa wa Hamdallahi huko Massina, na ukhalifa wa Tijaniyya huko Senegambia na Massina.

## *Usuli wa kidini*

Lengo kuu la vuguvugu la jihadi huko Afrika Magharibi katika karne ya kumi na tisa lilikuwa ni dini, yaani kuurejesha Uislamu katika usafi wake wa asili. Lakini kwa vile Uislamu ni dini pana inayojumuisha mambo yote yanayohusu maisha ya binadamu, jihadi nayo ilihusisha masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyotokana na hali halisi iliyokuwepo huko Sudan ya Magharibi wakati huo.

Vuguvugu za jihadi ziliongozwa na masahilina na wacha-Mungu kama vile Shehe Uthman dan Fodio, Shehe Ahmad Lobbo (Seku Ahmadu) na al-Haji Umar. Watu hawa hawakuwa wanazuoni tu bali pia waumini wakuu wa Uislamu walioitii sharia kikamilifu. Walijiona kama watu waliokwisha kupewa madaraka ya uongozi wa dini na Allah, na waliiona jihadi kama njia mojawapo ya kutimiza utabiri wa Mtume Muhammad. Kwa mtazamo wao, walikuwa wanatimiza amri ya Mungu.

Ili kuunga mkono matendo yao, viongozi wa jihadi walitegemea sana aya kadhaa za Kurani, hadithi (jadi za unabii) na maandiko mengine ya Kiislamu. Wakati huu wazo la

jihadi lilichukua sura ya imani, na iliwalazimu viongozi kufuata kanuni ngumu za nidhamu ya uadilifu na kujihini. Watetezi wa jihadi kwa hali hiyo walitakiwa kuishi kwa kufuata mfano wa maisha ya usafi na kutekeleza kwa vitendo yale waliyohubiri. Ili kuthibitisha usahihi wa jihadi, viongozi wake pia waligeukia utabiri wa Muhammad kwamba Allah atamtuma mwanamageuzi kwa Waislamu wote wa kweli kila baada ya miaka mia moja ili kuitakasa na kuihuisha dini. Ilisemekana kwamba miongoni mwa wanamageuzi hao, kumi na wawili walikuwa wametajwa na Mtume: kumi wa mwanzo waliaminika kutokea huko Mashariki na wa kumi na moja alikuwa ni Askia al-Muhammad, mfalme wa Songhai katika *Bilad al-Sudan*. Wa kumi na mbili alitarajiwa katika karne ya kumi na tisa. Viongozi wa jihadi walikuwa wepesi sana katika kuitumia imani hii: kwa pamoja Shehe Uthman dan Fodio na Seku Ahmadu kila mmoja wao alidai kuwa yeye ndiye mwanamageuzi wa mwisho aliyeahidiwa na Allah, wakati al-Haji Umar alijiona kama mtu aliyekuwa anatimiza wito wa kiungu ulioamriwa kabla.

Ili kudhibitisha zaidi uhalali wao, wanamageuzi wote watatu walidai kwamba kazi hiyo ya kiungu ya kufanya jihadi walikabidhiwa rasmi na Mtume pamoja na viongozi wa vikundi vya udugu mbalimbali ambavyo walikuwa wamejiunga navyo. Uthman da Fodio alidai kuwa yeye aliamuriwa na Mtume Muhammad pamoja na Abd al-Kadir al-Jilani, mkuu wa udugu wa Kadiriyya, katika ndoto kuendesha jihadi. Kwa msimamo huohuo al-Haji Umar pia alidai kupewa masharti katika ndoto ya kuendesha jihadi na Mtume pamoja na Shehe al-Tijani, mnasihi wa udugu wa Tijaniyya.

## *Urithi wa Torodbe*

Licba ya hali za kiimani za jihadi za Afrika Magharibi katika karne ya kumi na tisa, bado jihadi hizo hazikuwa matukio yaliyojitenga; matukio haya yaliwakilisha mawimbi mapya katika jadi ndefu ya mabadiliko ya kidini yaliyokuwepo tayari huko Sudan ya Magharibi yakiwa yamelengwa katika uanzishaji wa utawala wa haki na usawa, vitu ambavyo vilikuwa vimepuuzwa na watawala wa jadi. Viongozi wa jihadi hizi walipata kariha (msukumo wa moyoni) kutoka vyanzo vya wakati wao vilivyokuwa karibu zaidi na makao yao: kama vile mafanikio ya jumuiya ya Torodbe katika Bundu, Futa Jallon na Futa Toro; majaribio ya Shehe al-Kunti na Muhammad ibn Abd al-Karim al-Maghili ya kuleta mabadiliko ya amani; mkabala wa jumuiya mbalimbali (za kidini) dhidi ya mlipuko wa ujahidina wa Wahhabi huko Arabia; na mlipuko wa jihadi ya Uthman da Fodio huko Sokoto ambayo ilitumiwa kama kigezo na Seku Ahmadu na al-Haji Umar.

Jamii ya Torodbe iliwajumuisha wasomi wa Kiislamu waliotoka kwenye vikundi tofauti vya jadi kote Sudan ya Magharibi na ya Kati, kama vile Wafulbe, Wawolof, Wamande, Wahausa, na Waberiberi wenye asili ya watu huru, au wenye asili ya watumwa au waliotokana na matabaka ya kiamali (*castes*). Utamaduni wa Wafulbe ndio uliokuwa muhimu zaidi kwa vile Watorodbe walitokana na makabila tofauti, walizungumza lugha ya Kifulfude na kukumbatia desturi na imani zao. Pia walioana na Wafulbe na kuandamana nao kwenye uhamahamaji wao usiokwisha. Matokeo yake ni kwamba Watorodbe walijitambulisha na Wafulbe, na kusema kweli hao ndio waliokuwa tawi la wasomi la Wafulbe. Watorodbe walifuata mageuzi ya Kiislamu kwa moyo kwa

vile walitamani kuanzisha jamii ambayo watu wake hawatahusiana kwa damu, bali kwa kuikiri imani moja, yaani Uislamu, na kushiriki katika utamaduni mmoja wa Wafulbe.

Watorodbe walikuwa na mafanikio kadhaa ambayo yaliwatia kariha wanamageuzi wa karne ya kumi na tisa. Kulikuwa na jihadi za Kitorodbe katika jihadi za karne ya kumi na saba na kumi na nane ambazo zilifanikiwa na kuunda tawala za kiimamu za Bundu, Futa Toro na Futa Jallon. Watorodbe pia walikuwa na familia za wasomi kama vile Watoronkawa wa Uthman dan Fodio, Wabari wa Seku Ahmadu, na familia ya al-Haji Umar. Wanamageuzi wa karne ya kumi na tisa walitiwa moyo sana na urithi wa Watorodbe ambao waliutumia kuhamasisha kuungwa mkono kwa jihadi zao.

## *Wanamageuzi wa Afrika Magharibi*

Mbali na urithi wa Torodbe, chanzo kingine cha kariha ya wanamageuzi ni mfano wa mageuzi yasiyotumia nguvu ya Shehe al-Mukhtar al-Kunti (1729-1811). Al-Kunti alikuwa kiongozi wa udugu wa Kadiriyya huko *bilad al-Sudan* kuanzia 1750 hadi 1811. Aliitumia nafasi yake hiyo kuandika sana mambo yaliyohusu dini na kueneza athari zake huko Sudan ya Magharibi. Uthman dan Fodio na Seku Ahmadu walimwona kama kiongozi wao wa kiroho katika njia ya Kadiriyya. Hata al-Haji Umar ambaye alikuwa katika udugu wa Tijaniyya pia alimwenzi sana al-Kunti. Wanamageuzi hawa watatu wa karne ya kumi na tisa walitumia mawazo ya kidini ya al-Kunti kuunga mkono na kuhalalisha vitendo vya kuleta mapinduzi.

Mawazo ya Muhammad ibn Abd al-Karim al-Maghili, msomi mtembezi wa Maghrib wa karne ya kumi na sita, pia yaliwaathiri wanamageuzi wa Afrika Magharibi. Al-Maghili alitofautisha kati ya makao ya Uislamu na yale ya vita, akafafanua hali ya kutoamini, na kubainisha watawala wenye msimamo hafifu (wa kiimani), na maulama (wanazuoni) "ambao wameufunika ukweli kwa uongo kiasi cha kufanya idadi fulani ya Waislamu wajinga kupotoka.". Aliamuru kwamba jihadi dhidi ya maulama na watawala kama hao wenye kuchanganya imani mbalimbali ilikuwa ni kitu cha lazima.

Licha ya kuathiriwa na matukio ya ndani ya Afrika Magharibi, wanamageuzi waliathiriwa pia na athari kutoka nje. Hii ni kwa sababu maendeleo ya kisiasa na kidini huko Mashariki ya Kati, chimbuko la Uislamu, yalikuwa yanaathiri dunia yote ya Uislamu. Moja ya matukio hayo ni kutekwa kwa Makka na Medina mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa na Wahhabi waliokuwa na msimamo mkali, na jibu la jumuiya za udugu za Mashariki kufuatia kutekwa huko. Sio tu kwamba mapinduzi ya Wahhabi yalichochea matendo ya kijeshi katika dunia ya Uislamu, bali pia yalichochea uhuishaji mkubwa wa jumuiya za kidugu za kidini. Sehemu moja ya uhuishaji huo ilikuwa ni kuzaliwa kwa jumuiya ya Tijaniyya iliyoongozwa huko Sudan Magharibi na al-Haji Umar. Jihadi ya Uthman dan Fodio pia inasemekana kuwa ilipata msukumo fulani kutoka kwa mfumuko wa jumuiya kama hizo za Kimashariki.

Mwisho, jihadi ya Uthman dan Fodio ilikuwa ni mfano wa kuigwa kwa wanamageuzi wale wengine wawili wa karne ya kumi na tisa. Kwanza kabisa jihadi ya dan Fodio ilizindua ari ya mapinduzi ambayo ilikuwa imejilimbikiza huko Sudani ya Magharibi. Fasihi iliyohusu jihadi ya Sokoto pia ilihimiza mageuzi makali na kuwatia

moyo viongozi wengine wa jihadi. Al-Haji Umar na Seku Ahmadu wenyewe binafsi walifahamu kilichokuwa kikitokea katika Ukhalifa wa Sokoto, na huko ndiko walikopata msukumo wa kufanya mageuzi yao wenyewe.

## *Uchangamani*

Vuguvugu za mageuzi ziliendeshwa na nguvu kadhaa ambazo zilijiunga pamoja chini ya bendera ya Uislamu ili kuwaondoa madarakani watawala fulani wenyeji wa Sudan Magharibi. Lakini kabla hatujachanganua muundo wa "nguvu" hizo, kwanza tuone walikuwa wakipigana dhidi ya kitu gani.

Uislamu, kama ulivyofuatwa huko Sudan Magharibi katika karne ya kumi na tisa haukukidhi matakwa ya wanamageuzi. Waumini wa Sudan Magharibi hawakufutilia mbali matendo ya dini zao za jadi. Walichanganya Uislamu na imani zao za jadi za Kiafrika. Uislamu huu changamani ulifuatwa na watawala wa Sudan Magharibi na wafuasi wao wa Kiislamu. Maulama wa ukanda huu walivumilia uchangamani huu kwa vile walipenda waendelee kunufaika na ulezi na ulinzi wa nasaba tawala. Pia walitumika kama maofisa wa kisiasa na kiutawala katika vitala vya kifalme. Wafanyabiashara wa Kiislamu, kutokana na mahusiano yao ya kimataifa, walivutia utajiri mwingi katika nchi za Sudan Magharibi. Kwa hali hiyo kulikuwepo na uhusiano wa kirafiki baina ya watawala wa Afrika ya Magharibi na jumuiya za wafanyabiashara na wasomi wa Kiislamu. Uhusiano huu uliwafanya wasomi wa Kiislamu washindwe kukemea matendo ya watawala yaliyokiuka Uislamu.

Hata hivyo, wanamageuzi walichukia sana mwafaka huu na walijaribu kwa nguvu zote kufutilia mbali matendo yote ya dini za jadi yaliyokuwa yameingizwa katika Uislamu. Walianza kwa kutoa hotuba za kukemea matendo hayo na kuwasihi Waislamu warejee kwenye Uislamu safi unaotakiwa na sharia (sheria ya Kiislamu). Walihubiri pia dhidi ya vitendo vya ukandamizaji na ulaji rushwa uliofanywa na watawala, matumizi mabaya ya madaraka yao, mwelekeo wao wa kidunia na utozaji wa kiwango kikubwa cha kodi kwa wale waliowatawala.

Jibu la watawala hawa kwa jaribio hili la kutaka kuwapunguzia mamlaka yao lilikuwa ni kujaribu kuyazima mapinduzi haya katika hatua zake za mwanzo. Lakini wanamageuzi waliona jitihada hizi kama vitendo vya utovu wa imani na kuzitangaza nchi za watawala waliochukua msimamo huo kuwa "makazi ya vita" ambayo yalitakiwa yapigwe vita na baada ya kuyashinda yajumuishwe katika jumuiya ya Waislamu. Matokeo ya jambo hili yalikuwa ni kufagiliwa mbali kwa mamlaka ya watawala. Badala yake miliki tatu za ukhalifa zilizuka kuchukua nafasi ya mamlaka ya kienyeji yaliyoondolewa: moja huko Sokoto, moja huko Massina na ya tatu huko Senegambia.

## *Kuungwa mkono kulikoenea*

Nguvu za jihadi zilizoangusha watawala wenyeji wa Sudan Magharibi zilitokana na usuli tofauti wa kikabila na kijamii. Watu hawa waliongozwa na mashehe ambao kutokana na mahubiri yao na mafundisho yao waliwakusanya Waislamu wengine, wakati huohuo

wakieneza athari za udugu uliowahusu. Kiini cha vuguvugu hili kilikuwa ni *jamaa* (jumuiya ya Waumini) ambayo iliundwa na wanachama na wafuasi wa jumuiya mbalimbali za udugu, wanafunzi wa mashehe hao na wasomi huru wengine. Lakini wajamaa hawa hawakuwa na nguvu za kutosha kushinda majeshi ya watawala wa Afrika Magharibi. Kwa hiyo waliwaandikisha watu wengine katika majeshi yao. Makuruta hawa walioandikishwa ndio waliofanya idadi kubwa ya vikosi vya wapiganaji. Hawa walikuwa ni Waislamu waliovutiwa na haiba kubwa ya viongozi wa mageuzi haya. Walikuwa ni Waislamu ambao wangeweza kushutumiwa kwa kuchanganya Uislamu na matendo ya jadi, lakini kushiriki kwao kwenye jihadi kuliwafutia chochote kile ambacho kingeweza kuwatupa nje ya jamaa kama wachangamani.

Kipengele kimoja muhimu katika jihadi kilihusu suala la Wafulbe. Idadi kubwa ya wajamaa walikuwa ni Wafulbe kwa asili, na uongozi wa ukhalifa kwa sehemu kubwa ulichukuliwa pia na Wafulbe. Athari hizi za Wafulbe zimewafanya wengi kuhitimisha kwamba jihadi hizi ziliwakilisha maasi ya Wafulbe dhidi ya nchi wenyeji wao. Hata hivyo mawazo haya hayana mashiko kwa sababu wakati Wafulbe wengine walijiunga na jihadi kwa ajili ya mshikamano wa asili moja, wengine walipigana upande wa majeshi ya wapinga jihadi. Pia, jihadi za Seku Ahmadu na al-Haji Umar kwa kiasi fulani zilielekezwa kwa uongozi wa kisiasa wa Wafulbe (Torodbe) huko Senegambia na Massina.

Hata hivyo, Wafulbe wa Massina walikuwa na sababu za kutosha kuunga mkono wanamageuzi. Kulikuwepo na milolongo ya mapambano kati ya wafugaji wa Kifulbe na jumuiya za wakulima huko kusini, na kati ya Wafulbe na Watuareg huko kaskazini. Wakati matatizo kati yao na jumuiya za wakulima mara zote yalijikita katika ulipaji wa kodi na faini za uharibifu uliosababishwa na mifugo ya Wafulbe kwenye mazao yao, tatizo lao na Watuareg lilitokana na Watuareg kuvamia mifugo ya Wafulbe. Kwa hali hiyo jihadi iliwaondolea Wafulbe adha ya kodi na faini, na kuwapatia ulinzi dhidi ya uvamizi wa Watuareg.

Aidha, Wafulbe wa Massina na wale wa Senegambia walikuwa na sababu nyinginezo za kuunga mkono jihadi. Wafulbe wa Massina walikuwa wakiteseka kutokana na utawala wa ukandamizaji wa Wabambara wa Segu tangu katikati ya karne ya kumi na nane. Wabambara waliwavamia mara kwa mara, waliwatoza ushuru mkubwa na kuwafanya watumwa. Kwa hivyo Wafulbe wa Massina hawakusita kutoa kura yao kwa Seku Ahmadu na jihadi yake dhidi ya mabwana wao wa Kibambara huko Massina. Wafulbe wa Senegambia nao pia walikumbwa na jaala kama iliyowapata wenzao kutoka kwa watawala wa Torodbe. Pamoja na tatizo hilo kulikuwepo na urafiki kati ya watawala wa Torodbe huko Senegambia na Wafaransa waliokataa kulipa ushuru kwa Wafulbe. Wafulbe wa Futa Toro, kwa hiyo, walikuwa na ari kubwa ya kuunga mkono jihadi ya al-Haji Umar dhidi ya watawala wenyeji wapotofu na Wafaransa "makafiri."

Mwisho, wanamageuzi waliungwa sana mkono na idadi kubwa ya watumwa na vikundi vya matabaka ya kiamali vya Sudan Magharibi. Ongezeko la uvamizi wa kuteka watumwa liliwafanya waathiriwa watarajiwa kujiunga na viongozi wa jihadi, ilhali watumwa waliahidiwa uhuru wao endapo wangejiunga na kupigana upande wa

wanamageuzi. Kwa hivyo Waislamu na watu wasiokuwa Waislamu walijiunga na jihadi kwa ajili ya kutafuta ukombozi na usalama. Watumwa ndio waliounda idadi kubwa ya vikosi vya wapiganaji wa jihadi na walituzwa vizuri baada ya vita.

Ni wazi, basi, kuwa jeshi la wapigania mageuzi lilitokana na asili tofauti. Wapiganaji walitokana na Wafulbe, Wamande, Wawolof, na Watuareg; walitokana na wafugaji wa Kinomadi, jumuiya za wakulima wenye makazi ya kudumu, safu za maulama wasomi na wafuasi wao, na watu wasiojua kusoma wala kuandika. Walitoka pia miongoni mwa vikundi vya matabaka ya kiamali na watumwa. Kila kundi lilikuwa na manung'uniko yake maalumu, na wote walikuwa na ndoto ya kunufaika endapo hali (mbaya) iliyokuwepo ingebadilishwa.

## *Waumini katika dar al-Hijira*

Tukio muhimu katika vuguvugu la mageuzi lilikuwa ni hijira (uhamaji) ya wanamageuzi na wafuasi wao kutoka kwenye nchi za watawala wenyeji ambao walikuwa wametishwa na mwenendo wao. Uthman da Fodio na wafuasi wake walikimbia kutoka Degel na kufanya makazi huko Guru mwaka 1804; Seku Ahmadu aliondoka Kuby huko Massina na kuelekea Nukuma mwaka 1816-17, na al-Haji Umar aliondoka Jugunku huko Futa Jallon na kuhamia Dinguiraye mwaka 1849. Kuhama huku hakukuwa kwa hiari bali walilazimishwa na watawala wenyeji ambao waliwafukuza wanamapinduzi kwa sababu walikuwa wakijilimbikizia silaha, wakiandikisha wafuasi, na wakizidisha uchochezi wao wa kudai mageuzi.

Kutoka kwenye vituo vyao vipya, wanamageuzi sasa walijitayarisha kwa mapambano yasiyokwepeka tena kati yao na watawala wenyeji. Silaha nyingi sana zilikusanywa, ngome zilijengwa, na Uthman dan Fodio na Seku Ahmadu walijichukulia cheo cha *amir al-mu minin* (amiri [kamanda] wa waumini). Wakimbizi wengi waliokuwa wanakimbia ama kutokana na kuteswa au kuitika mwito wa mashehe waliingia kwa wingi katika makazi haya mapya. Kulikuwepo na ari kubwa ya dini katika vituo hivyo. Wanafunzi wengi waliingizwa katika vikundi vya udugu wa kidini. Kulikuwepo na majadiliano yasiyokuwa na mwisho kuhusu matukio yaliyosababisha hijira pamoja na matayarisho ya vita. Kwa hivyo, sio tu kwamba hijira iliwaondolea wajamaa hatari iliyokuwa ikiwakabili, bali pia iliwapa fursa ya kujiandaa kwa jihadi.

Hata hivyo wanamageuzi walikuwa na nafasi nzuri kuliko adui zao kwa kuwa waliungwa mkono na idadi kubwa ya watu. Kwa vile waliiona kazi yao kama amri ya Mungu, walijitolea kwa moyo wote na pia kutetea matakwa ya umma wote uliokuwa umekatishwa tamaa. Walipata utiifu wote wa wajamaa. Wanamageuzi pia walionekana kama watu waliokuwa na uwezo wa kiungu, na kushindwa mara kadhaa kwa jitihada za kuwaua kulizidi kuthibitisha kutokuonekana kwao pamoja na ulinzi wa kiungu waliokuwa nao. Yote haya pamoja na usomi wao bora na maisha yao ya kinidhamu vilikuza taswira zao mbele ya umma na kuwavutia wafuasi wengi.

Ni vizuri pia kutia maanani njia zilizotumiwa na wanamageuzi kushambulia watawala wenyeji. Ushindi wao juu ya maeneo makubwa kiasi hicho, licha ya nguvu nyingi za wapinzani wao, ulikuwa ni ushahidi tosha wa uangalifu wao katika kupanga mambo yao.

Jambo hili pia liliukilia kadiri ya ushindi wao. Wakati Uthman da Fodio na Seku Ahmadu walipigana jihadi zao katika maeneo ya nyumbani kwao tu katika nchi za Hausa (dan Fodio) na Massina (Ahmadu), al-Haji Umar alilenga katika kushinda eneo lote la Sudan Magharibi. Aliweza kujiingiza katika mpango huu wa kifahari kwa sababu majeshi yake yalikuwa yametawanywa mbali zaidi kuliko yale ya Uthman da Fodio na Seku Ahmadu, na walikuwa na silaha bora na mafunzo mazuri. Ndoto zake zilihitimishwa na kifo chake katika mwaka 1864.

## *Matokeo kadhaa ya jihadi hizo*

Matokeo ya mara moja ya jihadi hizo yalikuwa ni kuanzishwa kwa tawala za kidini zilizoitwa khalifa. Himaya hizi za kisiasa zilikuwa kubwa sana, ila viwango vya uunganifu wake vilitofautiana. Labda kiwango cha juu cha uunganifu kilifikiwa huko Hamdollahi (1818-1862) kutokana na uchache wa wakazi wake wenye asili moja na mawasiliano mazuri yaliyokuwepo. Hivyo Seku Ahmadu na warithi wake waliweza kutumia sharia kwa kiwango kikubwa katika ukhalifa wao.

Pili, vyeo vya kisiasa vilitolewa kwa wanamageuzi. Cheo cha juu zaidi cha *amir al-mu'minin* kilishikiliwa na madhuria wa wanamageuzi walioishi katika miji mikuu. Mikoa iliyogawanywa katika miliki ya khalifa ilitawaliwa na maofisa wa ngazi za juu, wengi wao wakiwa ni wanazuoni. Watumwa kadhaa waliokuwa waaminifu katika jihadi pia nao walizawadiwa vyeo vya juu. Kwa vile Wafulbe ndio waliounda idadi kubwa ya vikosi vya wapiganaji wakati wa jihadi, walikuja kuwa watawala wa Sudan Magharibi kwa vile nguvu za jadi pamoja na hadhi ya kijamii vilihawilishwa kwao. Walijaza karibuni nafasi zote za uendeshaji na kuunda tabaka la wasomi. Watumwa walioshiriki katika jihadi waliachiliwa huru; wale ambao hawakushiriki walitiwa tena utumwani, ilhali watumwa wapya waliendelea kukamatwa wakati wa uvamizi uliokuwa unafanyika nje ya mipaka, na pia wakati wa kuzima maasi.

Watu wote binafsi na vikundi vilivyokuwa katika ukhalifa vilihakikishiwa ulinzi na usalama. Mahakama za sharia ziliundwa na shughuli nyingi zisizokuwa za Kiislamu zilipigwa marufuku. Hata hivyo nyingi ya shughuli hizo zilibadilishwa kwa matendo mengine yenye dosari kama hayo ya mwanzo. Zaidi ya hayo, kutokana na ukubwa wa miliki hizi za ukhalifa, desturi kadhaa za kale zilifanikiwa kuzuka tena, na maafikiano mengi yalifikiwa baada ya jaziba za mwanzo za dini kufifia. Labda mafanikio makubwa zaidi ya mapinduzi hayo yalikuwa katika uwanja wa elimu na usilimishaji. Shule nyingi zilianzishwa katika khalifa zote, na jihadi hizo ziliimarisha Uislamu na vikundi viwili vya udugu vya Kadiriyya na Tijaniyya huko Afrika Magharibi.

# 22 *Ukhalifa wa Sokoto na Borno*

## *Utangulizi*

Katika sura hii, tutadokezea kuhusu miundo ya kisiasa na maendeleo ya jumla katika ukhalifa wa Sokoto na Borno. Maendeleo haya hayakuhusu tu miundo ya ndani ya madola hayo mawili, bali pia muelekeo wa jumla wa historia ya Sudan ya Kati. Hapa haiwezekani kujaribu kuchunguza kwa ukamilifu mada zote zinazotarajiwa, bali madhumuni ni kuweka kiunzi kwa ajili ya kuielewa historia ya ukanda huo kati ya 1820 na 1880. Kwa kuanzia, hatuna budi kuyapitia matukio makuu ya kipindi cha miaka arobaini na tano iliyotangulia.

Wanamageuzi wa Kiislamu walipata mafanikio makubwa sana katika kampeni zao katika majimbo ya Hausa na Nupe. Nia yao mwanzoni, katika mahubiri yao, ilikuwa ni kuwashawishi watawala kuleta mabadiliko; na idadi kadhaa ya watawala wa eneo hilo, katika Kano, Zaria, Gobir, Katsina na Zamfara, walionekana kuwa tayari kushirikiana kwa kuanzisha mageuzi ya kidini. Hata hivyo, baada ya 1788, vuguvugu la mageuzi lilichukua hatua nyingine - ile ya kuanzisha jumuia za Kiislamu zilizokuwa zikijitawala zenyewe ndani au nje ya majimbo ya Hausa ambamo Waislamu wanakuwa na haki kama kundi huru. Hali hii ilitokea kwa sababu wanamageuzi walitambua kwamba mabadiliko yaliyoletwa na viongozi wa nchi hiyo hayangedumu, hasa kwa sababu ya mgawanyiko wa kisiasa katika ukanda huo. Mkakati huu mpya wa *dar al-hijra*, uliotokana na uzoefu wa Mtume mwenyewe, ulikuwa ni mwanzo usioepukika kabla ya kukabiliana kivita.

Hadhi ya upendeleo iliyodaiwa na jumuia ya Waislamu ilisababisha mivutano katika majimbo ya Hausa. Kukataa kwao kuwa chini ya udhibiti wa dola, na tabia yao ya kuwatia moyo watumwa waliokimbia kutoka kwa mabwana wao, ilisababisha zahama. Ili kuyarudisha tena madaraka yao katika jumuia ya Waislamu, watawala hao walitumia nguvu. Walianzisha mashambulizi dhidi ya wafugaji wa kabila la Wafulbe kama njia ya kuwashinikiza wanamageuzi; lakini njia hiyo haikufanikiwa kwa sababu iliwasukumizia Wafulbe kwa maelfu ndani ya kambi ya wanamageuzi. Hali hiyo ililipa kundi la wafugaji-wanajeshi umaarufu ambao haukukusudiwa katika ukhalifa wa Sokoto.

Baada ya Sheikh Uthman na jumuia yake kufanya hijira kutoka Degel hadi Gudu, kulitangazwa vita rasmi mnamo mwaka 1804. Hatua hiyo ilifuatiwa na ugawaji wa




22.1 *Ukhalifa wa Sokoto, Borno na jirani zao*

bendera na uteuzi wa makamanda kutoka katika kila jimbo mwaka 1806, na hivyo kuyapa majimbo madaraka ya kuendesha mapambano katika maeneo yao. Ingawa wanamageuzi walikuwa wachache na hawakuwa na vifaa vya kutosha wakilinganishwa na vikosi vya serikali, lakini mwishoni waliweza kushinda vita kwa sababu ya kuwa na morali mkubwa na mipango mizuri. Kufikia mwaka 1809, majimbo makuu ya Hausa yalikuwa yamechukuliwa na vikosi vya jihadi na watawala wake kuondoka nchini mwao kama wakimbizi. Ni katika Borno tu ambako mamlaka ya *mai* (mfalme) yalikuwa imara kiasi cha kuweza kuhimili kutekwa kwa mji wake mkuu, Birni Ngazargamu.

## *Athari zilizojitokeza baada ya vita*

Suala kubwa baada ya jihadi lilikuwa ni la ujenzi mpya na hii ilikuwa na maana tofauti kwa kila upande uliohusika katika vita. Kwa watawala wa majimbo ya Hausa waliong'olewa madarakani, kazi kubwa iliyowakabili ilikuwa ni kuhamasisha watu ili kuungwa mkono na hivyo kuyarudisha tena maeneo yao yaliyochukuliwa na wanamageuzi. Kwa wanamageuzi Waislamu walioshinda, ujenzi mpya ulikuwa mgumu kwa vile walilazimika kufuata sharia za Kiislamu, ilhali hawakuwa na wataalamu wa kutosha wa kuongoza ngazi mbalimbali za utawala katika ukhalifa, maana wanazuoni na wanafunzi wengi ambao wangeweza kuifanya kazi hiyo walikufa wakati wa vita.

Hatua kadhaa zilichukuliwa ili kutatua tatizo la upungufu wa wafanyakazi. Ndugu wa Shehe (mtawala) waliteuliwa kufanya kazi katika ofisi ya utawala na kusimamiwa na makao makuu. Maafisa wa utawala uliopita pia waliajiriwa lakini hawakuaminiwa sana na ukhalifa. Kutoaminiwa huko kulikochanganyika na kutokuwa na uzoefu wa kuongoza kuliifanya kazi ya kuongoza ukhalifa kuwa ngumu zaidi. Malalamiko na mizozo mingi kutoka katika ukhalifa wote ilifikishwa kwa Shehe kwa usuluhishi. Mwaka 1812 jukumu la kusuluhisha migogoro lilikabidhiwa kwa Abdullah dan Fodio na mtoto wa kiume wa Shehe, Muhammad Bello. Hivyo, Shehe alipofariki dunia mwaka 1817, hakukuwa na mabadiliko makubwa katika sera za ukhalifa. Mbali na ukweli kwamba nchi zilizokuwa chini ya utawala kamili wa wanamageuzi zilikuwa chache, hakukuwa na serikali nyingine ya umma ambayo ingeweza kushindana na utawala mpya. Hivyo, jukumu lilikuwa ni kuupanua utawala hadi vijijini na kuyajumuisha maeneo hayo katika ukhalifa. Lakini huko Borno, ma-*mai* walikuwa wakijitahidi kutumia udhibiti wao wa maeneo ya vijijini kulijenga upya dola lao na kuhifadhi uhuru wake dhidi ya milki mpya ya ukhalifa.

Uanzishaji na uendeshaji wa ukhalifa wa Sokoto na majimbo yaliyounda ulileta mabadiliko makubwa katika mfumo wa siasa wa zamani. Badala ya mfalme wa jadi (kabla ya jihadi) mwenye nafsi tukufu, sasa kulikuwa na amiri ambaye hakuwa "mtukufu." Mungu, na siyo dola lililowakilishwa na mfalme, alikuwa ndiye chanzo cha mamlaka. Tofauti na mfalme aliyepita ambaye kwa namna fulani alikuwa juu ya siasa, amiri alikuwa ni kiongozi wa kwanza tu miongoni mwa watu wenye hadhi sawa; wafuasi wake kwa pamoja walishirikiana kutawala chini ya uongozi wake. Matokeo yake ni kwamba dhima ya zamani ya maofisa-watumwa wa kitala ilibadilika: badala ya kuwa watumishi wa utawala sasa wakawa watumishi wa watu binafsi. Aidha, wadhifa rasmi wa mama malkia au dada wa mfalme uliondolewa. Na ingawa wadhifa wa wafalme

waliopita ulikuwa ni wa kurithi, ule wa amiri kinadharia ulikuwa wazi kwa mcha Mungu yeyote aliyefaa. Utawalamsonge ulirahisishwa, na sharia kama ilivyofafanuliwa na tapo la Wamaliki, ndiyo iliyoongoza mahusiano katika dola hilo jipya.

Madhumuni ya mabadiliko haya yalikuwa ni: kurasimisha na kuuwekea mipaka utekelezaji wa shughuli za nchi; kuzuia utumiwaji vibaya wa sheria ambazo hazikuwa zimeandikwa; kuondoa makao makuu ya serikali kutoka kwenye jumba la mfalme; na kuanzisha uongozi ambao mamlaka yake yangetoka kwa Allah pekee na kuwajibika kwa jumuia ya Waislamu. Kwa jumla, majaribio haya ya kisiasa yalifanywa ili kutekeleza mawazo ya wanamageuzi kuhusu ujenzi wa dola la Kiislamu. Hata hivyo, ingawa walijaribu kuongoza kulingana na mipango hiyo iliyoelezwa, na kwa kuzingatia sharia, walitambua umuhimu wa kulegeza msimamo kulingana na mazingira mahususi, na pia kwa kuzingatia mahitajio maalumu. Katika kiwango cha uchumi, jaribio hilo liliuunganisha uchumi wa vijijini wa ukanda huo, na kisha kuuhusisha kwa karibu zaidi na uchumi wa Mediteranea na baadaye wa Atlantiki.

## *Utawala wa khalifa*

Makao makuu ya khalifa yalikuwa Sokoto na mamlaka ya kutawala majimbo mbalimbali yalianzia kwake. Ukhalifa haukufungamana na utambulishi wa janibu au kabila lolote kwa sababu ulijikita katika maongozi ya katiba ya Kiislamu. Utawala wa khalifa vilevile haukufungamana na sherehe na miviga ya kimila, au ufahari wa kuonyesha utajiri.

Alipofariki Shehe Uthman mwaka 1817 mgawanyiko wa himaya ya Khalifa katika sehemu kuu mbili uliendelezwa: Tawala za mashariki zilikuwa chini ya utawala wa Muhammad Belo ambaye alichukua nafasi ya ukhalifa, na makao makuu yake yalikuwa Sokoto; na tawala za magharibi zilizokuwa chini ya Abdulla ambazo makao yake makuu yalikuwa Gwandu. Kama hapo awali, Bello alimkabidhi madaraka kamili ya utawala wa magharibi mjomba wake, Abdulla, lakini alijihusisha kikamilifu na utawala wa mashariki, na kumwachia shughuli za utendaji waziri wake aliyeitwa Gidado. Tawala za mashariki zilikuwa na utajiri mkubwa na mapato yake yalisaidia kugharimia hatua za mwanzo za maendeleo ya ukhalifa.

Uhusiano baina ya Sokoto na Gwandu ulikuwa mgumu na kwa kiasi fulani ulitegemea viongozi waliokuwa wanatawala maeneo hayo. Lakini ni wazi kuwa Gwandu iliwakilisha uongozi wa kidini kwa sababu viongozi wa Gwandu walijulikana sana kwa uchaji Mungu wao, wakati khalifa wa Sokoto alikuwa mkuu na mwenye mamlaka ya mwisho kuhusu masuala ya kisiasa. Uhusiano baina ya maamiri na khalifa katika kipindi cha 1820-45 uliambatana na usawa kwani hapo awali walisoma pamoja. Aidha kulikuwepo na kiwango kikubwa cha uhuru wa kujiamulia mambo kwani kila amiri aliimarisha nafasi yake katika jimbo.

Jukumu kubwa la utawala wa khalifa lilikuwa ni usimamizi wa tawala za mashariki na udumishaji wa njia za mapato ambayo ukhalifa uliyategemea. Ili kufanikisha kazi hizi khalifa aliyategemea makundi matano: Wafanyakazi wake wa ndani; wapiganaji wenzake ambao sasa walikuwa washauri wake na matarishi maalum, wanafamilia na ndugu wa karibu wa marehemu Shehe Uthman ambao walishika majukumu makubwa

katika milki ya Sokoto; viongozi wa koo za wenyeji za Kifulbe ambao pia walishikilia vyeo muhimu katika milki hiyo, na mwishoni, familia zilizounda jumuiya ya baba yake ambazo zilijenga tabaka la wasomi mjini humo. Kundi hili la mwisho lilipewa majukumu ya kisharia na kidini katika utawala mpya, au nafasi ndogo za kiutawala katika majimbo.

Washauri wa khalifa, muhimu zaidi akiwa ni waziri, walikuwa ndio kiungo baina ya tawala za majimbo na khalifa. Kusema kweli, tawala nyingi za maamiri zilikuwa chini ya ofisi ya waziri. Kupitia kwa washauri hawa, khalifa aliteua au kuidhinisha uteuzi wa maamiri na kusuluhisha mzozo wowote uliohusu urithi wa madaraka. Mbali na kazi hizi, khalifa na wajumbe wake ndio walioundа mahakama ya juu kabisa ya rufaa. Aidha utawala wa khalifa ulikusanya kodi iliyokusudiwa kwenda kwenye hazina ya Sokoto. Mapato hayo yalitolewa kama zawadi, kodi, na ushuru kutoka katika majimbo. Hata hivyo, umaskini wa ndani ya bara la Sokoto, na ukweli wa kwamba watu wake wengi walikuwa ni wanazuoni na wafugaji, na wakulima walikuwa wachache sana, na wote hao hawakulipa kodi, ulisababisha khalifa ategemee mapato kutoka majimboni. Baadhi ya matatizo mengine ya utawala yalijkuwa ni ukubwa wa eneo la ukhalifa uliosababisha matatizo ya mawasiliano, na kutotumika sana kwa nguvu za kijeshi.

## *Shughuli za kijeshi na kidiplomasia*

Shughuli za kijeshi za ukhalifa wa Sokoto hazikuwa nyingi kwa sababu milki hiyo haikuwa na jeshi la kudumu. Upanuzi wa milki hiyo ulikuwa mikononi mwa maamiri na haukuwa unaratibiwa kutoka mahali pamoja. Jeshi lake halikuwa la kitaalamu na wanajeshi wake walichaguliwa hobelahobela (bila kufuata kanuni maalum). Likiwa na mikuki, pinde na majambia, na baadhi yao wakiwa wamepanda farasi na ngamia, jeshi hilo lilivamia Wahausa na makabila mengine katika majimbo mengine. Kwa sehemu kubwa ya karne hiyo, ukhalifa huo ulikumbwa na vita vya msituni kutokana na kutenguliwa kwa watu makazini kwao kwa sababu ya jihadi, upungufu wa chakula uliosababishwa na kuvurugwa kwa kilimo, au tamaa tu ya kupata faida kwa kuuza mateka wa vita. Hali hii ilipunguza usalama wa maisha, lakini biashara haikuathirika kwa sababu misafara ya biashara wakati wote ilikuwa na walinzi wenye silaha.

Kutokana na mapungufu ya kijeshi ya ukhalifa, diplomasia ilikuwa ni kipengele muhimu katika sera yake. Mawasiliano ya kidiplomasia yalishughulikiwa na makhalifa wenyewe. Hata hivyo, hakuna safari za nje zilizofanywa na khalifa, wala hakuwapeleka wafanyakazi kufungua ofisi za ubalozi nje ya nchi. Ila wanazuoni, mahujaji na wafanyabiashara waliopitia nchini humo ndio waliopeleka ujumbe na kuleta habari za maendeleo ya nchi za nje. Aidha yalifanyika mawasiliano na Moroko, Tripoli na Uingereza. Hamu ya Muhammad Bello juu ya mahusiano na nchi za nje haikuwa ni udadisi wa kisomi tu, bali pia ilizingatia masuala mazito ya kisiasa na kiuchumi. Hivyo, masuala hayo ndiyo yaliyoukilia uhusiano wake na nchi za Kiislamu na makundi mengine kama vile Watuareg, Watimbuktu, Wamassina na Waborno. Uhusiano baina ya Sokoto na Massina na Borno haukuwa mzuri; lakini uhusiano wake na Timbuktu ulikuwa mzuri, na uhusiano na Tuareg ulikuwa na utata na usiotabirika. Wakati

mwingine ukhalifa ulichanganya diplomasia na vita ili kuzishughulikia jumuiya ndogo ndogo za jirani. Lakini licha ya diplomasia na vita, zana ya kawaida katika mahusiano na nchi nyingine ilikuwa ni sera za uchumi, kama vile vikwazo au vipingamizi vya biashara, na hivi vilionyesha kufanikiwa zaidi kuliko vita.

## *Muundo wa kisiasa wa majimbo yaliyoongozwa na maamiri*

Kulikuwepo na tofauti za msingi katika muundo wa kisiasa katika majimbo, ingawa uteuzi wa maamiri kwa kawaida ulizingatia kanuni za urithi na uandamizi. Huko Zaria, uamiri ulikuwa ukipokezanwa miongoni mwa koo tatu mahsusi, ilhali katika majimbo mengine uamiri ulirithishwa ndani ya ukoo mmoja tu, ingawa wakati mwingine ukoo huo ulitambua matawi mawili au zaidi. Dhima na uteuzi wa uongozi chini ya amiri havikufuata ruwaza moja tu. Katika majimbo yaliyokuwa na jamii moja ya watu kama vile Zaria, Kano, Sokoto na Katagum, baadhi ya nyadhifa na wilaya ziligawanywa kwa wanajamii zilizohusika, na zilirithiwa na dhuria wa viongozi wa kwanza. Lakini katika majimbo yenye watu mchanganyiko, nasaba za watawala hazikujitokeza, wala nyadhifa na mali za kiofisi havikuwa vitu vya kudumu. Katika maeneo hayo, ama madaraka yalihodhiwa na amiri katika makao makuu, huku kukiwa na watumwa wengi katika utawala, kwa mfano katika jimbo la Hadejia, au madaraka yalikuwa katika baadhi mbili kama ilivyokuwa huko Borno, Nupe na Ilorin, ambako mtawala wa jadi alisimamia uongozi akishirikiana na wanamageuzi Waislamu. Mishowe watawala wa jadi katika tawala hizo za mamlaka-pacha waling'olewa, na hivyo uongozi wote kushikwa na amiri.

Katika majimbo yenye nasaba maalumu za watawala, kuishi kwa viongozi hao katika mji mkuu kulikuwa ni muhimu, na kabla ya karne hiyo kupita, uongozi katika mji mkuu ulikuwa na nguvu zaidi kuliko uongozi wa mikoani. Viongozi wenye nguvu katika mikoa walionekana kuwa ni watu hatari kwani wangeweza kudai uhuru kamili wa kuendesha mambo yao na kuiomba Sokoto iwatambue kama maamiri huru. Matukio kama hayo kila mara yalisababisha vita.

Zaidi ya hayo, uwezo wa kiuchumi wa majimbo tajiri kama Kano na Zaria uliulazimisha ukhalifa kuyategemea kifedha. Aidha kulikuwa na uwezekano kuwa iwapo amiri wa majimbo kama hayo angepata madaraka kamili angeshawishika kushindana na khalifa. Hivyo utawala wa khalifa, ukishirikiana na vikundi ambavyo havikupewa madaraka ya uamiri, ulijipa lengo la kuwazuia maamiri hao kujilimbikizia madaraka makubwa.

Utawala katika ngazi za chini zaidi (kwenye mashina) ulikuwa ni wa aina moja katika majimbo yote kuliko utawala wa ngazi za juu kama ilivyokwisha kuelezwa. Wafugaji walijiongoza wenyewe kupitia viongozi wao, na walikuwa na uhusiano mkubwa wa kiukoo ambao uliwawezesha kuwa na umoja wa hali ya juu.

Jumuia za wakulima pia zilitawaliwa na viongozi wake wenyewe. Kiungo baina ya wawakilishi wenyeji na utawala wa amiri kilikuwa ni watumishi au mawakala wa mtawala ambao walipewa wajibu wa kuwaangalia watu hao. Kazi ya msingi kabisa ya utawala huu wa kijanibu ilikuwa ni ukusanyaji kodi; utawala ulijihusisha na masuala mengine ya kijamii kwa kadiri tu yalivyohusiana na jukumu hili la kukusanya kodi.

## *Muundo wa kijamii*

Kulikuwa na makundi makuu mawili ya kijamii katika ukhalifa. Kundi la kwanza lilikuwa ni lile lenye kushika madaraka ambalo liliundwa na watu maarufu, ndugu zao, watu waliowaunga mkono na watumwa wao wa ndani. Kundi la pili ni lile la watu wasiokuwa na madaraka ambao walijishughulisha na kilimo, biashara na sanaa za ufundi wakiwa pamoja na watumwa wao. Mgawanyiko huu haukuwa umejifunga, kwani kulikuwa na maingiliano katika makundi yote hayo. Kwa mfano, wanazuoni na watumwa waliweza kuhusishwa na makundi yote mawili.

Kundi la wenye madaraka lilikuwa na sifa nyingine pambanuzi. Licha ya kuziongoza ofisi za serikali, moja ya sifa hizo ni kutokuhamahama. Tofauti na watu wa kawaida, hawakuweza kuhama kwa urahisi kutoka jimbo moja hadi jingine, kwani kama wangehama kutoka katika majimbo ambako walishikilia madaraka, ni wazi kuwa wangepoteza madaraka yao, maana haikuwezekana kuhama na vyeo vyao. Zaidi ya hayo, walijali sana nasabu zao na mahusiano yaliyofungamana na ndoa za kinasaba, na walizingatia kwa dhati kanuni za urithi wa upande wa kuumeni. Ama kwa upande wa watu wa kawaida, wao hawakutilia maanani sana mambo ya ukoo na waliendelea kushikilia utambulisho wao wa ujumla wa eneo au kabila kwa chale za usoni na mila mahsusi zilizowawatofautisha na watu wengine. Pia wake wa wenye madaraka walitawishwa wakati wake wa wengine hawakuwekewa vizuizi na hivyo kuwawezesha kushiriki katika biashara, sanaa za kiufundi na kilimo.

Nafasi ya watumwa katika ukhalifa pia yafaa kuchunguzwa. Kulikuwa na watumwa wengi sana katika ukhalifa. Waliruhusiwa kuwa na mali, walikuwa na muda wa kufanya kazi zao wenyewe, na walitarajia kupata fursa ya kujikomboa. Wanawake watumwa waliweza kuolewa na watumwa wengine na watoto wao kuwa sehemu ya jamaa ya wenye watumwa hao, ingawaje hadhi yao ilibakia kuwa ya utumwa. Lakini watumwa wanawake waliweza pia kuzaa na wanaume huru, na hivyo kuzaa watoto huru, na wao wenyewe kuwa huru pia baada ya bwana wao (aliyewamiliki) kufariki. Watumwa wa Kiislamu walichukuliwa kama wanajamii ya Kiislamu na hivyo hawakupaswa kuuzwa nje ya nchi hiyo, hasa kwenye nchi zilizofuata dini ya Kikristo. Watumwa hawakulipa kodi bali waliwafanyia kazi mabwana zao.

Kiasi cha kodi kilicholipwa na watu huru katika hali yoyote ile kilikuwa ni cha chini. Wenye madaraka walilipa kodi zao nyingi katika umbo la kodi ya urithi, kodi ya kushika madaraka, na zawadi maridhawa walizompelekea amiri au khalifa wakati wa kutawazwa kwake. Vigezo vya utajiri kwa jamii ya viongozi vilikuwa ni pamoja na farasi, nguo na kundi kubwa la wafuasi. Miongoni mwa watu wa kawaida, kuwa na idadi kubwa ya watumwa ndiko kulikoashiria utajiri. Hata hivyo, mawazo ya kidini yaliyouongoza ukhalifa yalionyesha shaka kuhusu thamani ya utajiri mkubwa na matumizi yake.

Katika nusu ya pili ya karne hiyo, ukhalifa ulishuhudia upanukaji wa shughuli za kilimo kwa sababu ya kuwepo kwa nguvukazi kubwa ya watumwa, uhimizaji wa ukulima wa binafsi, uanzishaji wa umwagiliaji maji mashamba na kupatikana kwa chuma kwa ajili ya kutengeneza zana za matumizi mahsusi. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa mazao ya kilimo na kupanua shughuli za uchumi katika ukhalifa.

## *Mabadiliko katika ukhalifa wa Sokoto 1820-80*

Tunaweza kutoka muhtasari kuhusu mabadiliko yaliyotokea katika ukhalifa wa Sokoto kati ya 1820 na 1880 katika awamu tatu: Awamu ya kwanza 1820-45 ilikuwa ni awamu ya kujijenga; ya pili 1845-55 ulikuwa ni muongo wa kipindi cha mpito na wasiwasi, wakati ambapo awamu ya tatu 1855-80 ilikuwa ni ya upanuzi wa uchumi.

*1820-45*

Kipindi hiki, si tu kuwa kilishuhudia haja ya kuwepo kwa ulinzi wa kijeshi dhidi ya mashambulizi ya watu walioshindwa au kuachwa bila makazi wakati wa jihadi, bali pia kiliona haja ya kujenga upya jamii ya wakulima. Majukumu haya yalihitaji viongozi wenye haiba, na maafisa walichaguliwa kwa kuzingatia sifa za Ufulbe na Uislamu. Ingawa kipindi hiki kilikuwa na vita dhidi ya maadui wa nje ya nchi na kampeni za kupanua mipaka ya ukhalifa, kilikuwa pia ni kipindi cha utulivu wa kisiasa ndani ya nchi kikiwa na miundo mipya ya kiutawala na nafasi za kazi kupewa watu wapya. Hata hivyo Kano, Katsina na Zaria zilikuwa ni tofauti kwa sababu waliendeleza miundo ya kiutawala ya madola ya zamani ya Hausa.

Hadi mwisho wa kipindi hiki (1845), majimbo mengi yalikuwa tayari yamekwisha anzishwa isipokuwa Nupe. Miji mikuu ilikuwa imekwisha kujengwa kila mahali isipokuwa katika Hadejia, na biashara ilikuwa tayari imeshamiri. Kielimu, ukhalifa ulistawi sana katika kipindi hiki, kama inavyodhihirishwa na idadi ya vitabu, mashairi na barua zilizoandikwa na Khalifa Muhammad Bello na wanazuoni wengine. Kulikuwa pia na upanuzi wa elimu mijini na vijijini katika ukhalifa uliosuhulishwa na upatikanaji wa vitabu vya kiada na mchango wa walimu wanawake katika kaya kubwa kubwa na pia katika hatua za awali za madrasa ya Kurani.

*1845-55*

Muongo huu ulishuhudia mabadiliko makubwa ambayo yaliwakilisha usaili wa kanuni za Uislamu ambazo zilikuwa msingi wa ukhalifa huo. Maelezo muhimu yaliyotolewa kwa ajili ya mabadiliko haya ni umri mkubwa (uzee) wa wanamageuzi, yaani viongozi wa majimbo, hadi kufikia 1840. Hali hii iliwafanya wawe dhaifu na hivyo kutofanya kazi ipasavyo. Aidha hali hiyo ilisababisha matatizo katika urithi wa uongozi. Suala jingine katika muongo huo lilihusu ulinzi. Kulikuwa na maasi makubwa na machafuko, hasa huko Katsina 1843/44; Zaberna, Kabbi na Gobir 1849/54; na Hadejia 1848. Maasi hayo yote yalitishia usalama wa Sokoto na Gwandu ambazo zilikuwa kitovu cha ukhalifa.

Mwishowe muongo huo ulishuhudia vuguvugu la kisomi na kidini lililosababisha uhamaji kutoka katika ukhalifa. Ubishani wa Tijaniyya ulioongozwa na al-Haji Umar ulisababisha mgawanyiko wa kiitikadi miongoni mwa wanazuoni katika ukhalifa, na hivyo kuleteleza baadhi yao kuanza kuhama kama ishara ya kupinga jambo hilo.

Hata hivyo, licha ya mageuzi ya kijeshi, kielimu na kidini, ukhalifa ulifanikiwa kudumisha utulivu wa ndani kwa kiwango kikubwa. Katika kipindi hicho chote, khalifa na amiri wa Gwandu walibakia katika madaraka yao. Ingawa mabadiliko mengine

yangeweza kusemwa kuwa yalitokana na utawala mbovu wa Sheikh Umar, lakini sababu ya msingi zaidi huenda ni uhusiano wa Borno na uchumi wa ukhalifa uliokuwa unapanuka, ambao uliiweka Borno pembezoni.

Upanukaji wa ukhalifa kuelekea mashariki, na ule wa Baghirmi na Wadai mashariki mwa Borno, pia ulipunguza nafasi ya kupanuka kwa Borno. Mwishoni mwa kipindi hiki, utulivu uliokuwepo chini ya Sheikh Umar ulizidi kupungua na vurugu na chuki kuchukua mahali pake.

## *Hitimisho*

Kulikuwa na tofauti kadhaa katika historia za ukhalifa wa Sokoto na Borno. Wakati ambapo al-Kanemi alishirikiana madaraka na kiongozi muhimu wa kijadi, *mai*, hakukuwa na mtawala wa kijadi wa aina hiyo katika Sokoto ya Muhammad Bello. Pili, al-Kanemi hakuwa na mahusiano mapana ya kifamilia na kiukoo ambyo yangemuimarisha madarakani kama yale aliyokuwa nayo Muhammad Bello. Al-Kanemi aliwategemea sana watumwa na marafiki, na hivyo kuweka madaraka yote mikononi mwake. Aidha, Muhammad Bello aliwapa madaraka wana-jihadi wenzake, ambao waliunda makundi ya kinasaba au ya kutetea maslahi ya kijamibu. Zaidi ya hayo, mpango wa al-Kanemi wa kuiunganisha Borno baada ya kuishinda ulitegemea sana utii wa kijadi wa watu kwa *mai*, haiba yake mwenyewe, maslahi ya binafsi na upinzani wa pamoja kwa Wafulbe, ilhali Bello alitumia itikadi ya Kiislamu kuwaunganisha maamiri waliokuwa wametapakaa sehemu mbalimbali. Kiuchumi, Borno iliuza watumwa nje ya nchi wakati Sokoto iliwanunua na kuwaleta nchini na hivyo kuwatumia katika kuendeleza uchumi wake. Matokeo yake ni kuwa, hadi mwishoni mwa kipindi hicho (1880), utajiri mkubwa wa kiasili wa ukhalifa ulikuwa unaunyonya uchumi wa Borno.

yanaweza kuelezwa kuwa yaliwakilisha makabidhiano madaraka kutoka kizazi kimoja hadi kingine, siyo tu katika ukhalifa, bali pia katika madola yaliyopingana nao, lazima ieleweke kuwa tukio hilo halikuwa maalumu lililouhusu ukhalifa wa Sokoto na maeneo yanayouzunguka tu. Madola mengine ambayo yalifanya mageuzi makubwa mwishoni mwa karne iliyotangulia kama vile Ufaransa, Misri, Austria na Ujerumani, yalikuwa pia katika kipindi cha zahama. Zaidi ya yote hayo, kipengele muhimu zaidi katika msukosuko huo ulioukabili ukhalifa kilikuwa ni ubishani wa kitaaluma ambao ulielekea kusaili msingi wa kuwepo kwa dola hilo, yaani itikadi ya Kadiriyya.

*1855-80*

Sifa kuu mbili za kipindi hiki zinazojitokeza katika historia ya majimbo hayo ni amani na kutoyumba kwa eneo hilo, na upanukaji wa kiuchumi wa ukhalifa huo, ambao kwa namna fulani ulisuhulishwa na hali ya utulivu iliyokuwepo. Bado kulikuwa na uvamizi na mashambulio mengi katika sehemu mbalimbali za ukhalifa, lakini huu haukuwa uvamizi ambao ungeweza kuihatarisha himaya. Biashara na uzalishaji mali ulipanuliwa katika ukhalifa wa Sokoto, huku ardhi yake iliyokuwa tupu ikianza kukaliwa na watu na kuendelezwa, na wafanya biashara wa himaya hiyo wakifanya shughuli zao katika maeneo ya mbali. Upanukaji huu wa kiuchumi ulienda sambamba na mfumuko wa bei ambao si tu kuwa uliathiri kiwango cha maisha ya watu, bali pia ulichochea ushindani wa kuwania madaraka, na matarajio ya maisha bora ya baadaye. Katika taaluma, kipindi hicho kilishuhudia pia kuongezeka kwa matumizi ya Kihausa kuliko Kiarabu au Kifulani katika vitabu na ushairi. Katika serikali, amali za utawala za Wahausa na mkabala wao kuhusu mamlaka vilijumuishwa polepole katika mfumo wa siasa.

## *Borno 1820-45: Mamlaka-Pacha*

Historia ya Borno katika kipindi kilichotajwa inaonyesha kutegemeana baina ya Borno na ukhalifa. Matukio katika himaya moja yalikuwa na umuhimu mkubwa katika himaya nyingine. Borno haikuunga mkono jihadi ya Uthman dan Fodio, na ili kuyarudisha nyuma mashambulio hayo, *mai* (mtawala wa jadi) aliomba msaada kutoka kwa Sheikh Muhammad al-Amin al Kanemi, mwanazuoni aliyekuwa na uhusiano wa kimataifa na wa ndani na Waarabu wa Shuwa na Wakanembu.

Kufuatia ushindi wake dhidi ya majeshi ya jihadi, al-Kanemi aliteuliwa na *mai* kuwa chifu mwenye uhuru fulani wa kujiamulia mambo ya jimbo lake. Hakuwa na wadhifa maalum katika muundo wa kisiasa wa Borno. Badala yake alitumia muda wake kutawala sehemu aliyopewa. Alilipanua eneo lake kwa kuzimeza sehemu nyingine za jirani za machifu waliokuwa na uhuru fulani wa kujitawala. Alikuwa na jeshi la kudumu la askari wa mikuki wa Kikanembu na nguvu yake ya uchumi ilitegemea zaidi biashara na uuzaji wa mateka nje. Halmashauri yake ya utawala iliundwa na marafiki zake sita. Hakuwa na baraza kubwa, lakini aliwatumia sana watumwa kama maafisa. Wakati huohuo, madaraka ya *mai* yalikuwa yanazidi kupungua. Hakuwa na jeshi imara tena, ingawa bado alikuwa anayo mamlaka ya kiasili yaliyoendeleza (utaratibu wa jadi) na hivyo kudumisha utulivu wa dola.



22.3 *Sheikh Muhammad al-Amin al-Kanemi*

Hivyo hadi 1820, Borno ilikuwa imekwisha gawanyika katika kanda mbili za kisiasa: Eneo moja lilitawaliwa na *mai*, makao makuu yake yakiwa Birni Kafela, na eneo jingine lilikuwa chini ya Sheikh al-Kanemi, makao makuu yake yakiwa Kukawa. Kwa hakika, nafasi ya al-Kanemi iliimarishwa kwa kiasi kikubwa hapo 1820 kutokana na kifo cha Mai Dunama na kutawazwa kwa mwanawe wa kiume, Ibrahim. Polepole al-Kanemi aliimarisha madaraka yake, lakini si kwa kutaka kugombana waziwazi na *mai*. Hii ni kwa kuwa wengi wa makabaila wa ukoo wa Kanuri walimuunga mkono na kumhudumia *mai*. Aidha, wakati al-Kanemi alipokuwa anapanua mipaka yake kuelekea kusini na magharibi mwa Borno, sehemu kubwa ya Borno halisi, mashariki mwa Ziwa Chad, bado iliendelea kuuenzi utawala wa *mai* na kufuata uongozi wa kijadi wa Kanuri. Hivyo, *mai* alitawala sehemu kubwa ya Kanuri Borno na kupata mapato yake humo, ambapo al-Kanemi alitawala maeneo ya mipakani magharibi na kusini, akiwatumia askari wapanda farasi wa Borno na kupeleka sehemu ya mapato yake kwa *mai*. Mpangilio huu baina ya mai na Al-Kanemi uliweza kufanya kazi kwa kuwa tu al-Kanemi hakuwa na tamaa ya ukubwa, na hakuwa na imani kali. Al Kanemi hakujiona kuwa na jukumu muhimu na la haraka kama viongozi wa Sokoto wala hakuwakaribisha watu waliokuwa na matarajio hayo. Hivyo hakufanya jaribio lolote la kutaka umaarufu kuzidi baraza la *mai*. Wakati al-Kanemi aliweza kuyatumia mamlaka ya *mai* yaliyokuwa makubwa kuliko maslahi finyu ya vikundi vidogovidogo, na yaliyokuwa halisi kama asasi ambayo ingeweza kuiunganisha Borno, *mai* pia angeweza kumtumia al-Kanemi kwa manufaa yake kwa sababu hakuwa na ari ya kufanya mageuzi ambayo yangetishia kuiharibu Borno ya asili.

Hata hivyo, kutegemeana huku baina ya Mai Ibrahim na al-Kanemi hakukudumu baada ya kifo cha al-Kanemi. Mtoto wa al-Kanemi na mrithi wa utawala, Umar, alijaribu kuuhujumu utawala wa mai. Hali hii ilileta migongano baina ya pande hizo mbili na kuwa mwisho wa miaka ishirini ya ushirikiano uliokuwepo baina ya *mai* na marehemu Shehe al-Kanemi.

## *Borno 1845-80: Kutoka mamlaka-pacha hadi utawala wa mashehe*

Muongo wa 1845-55 ulikuwa mgumu kwa Borno kuliko ulivyokuwa kwa ukhalifa wa Sokoto. Borno ilipitia katika mabadiliko ya msingi katika mfumo wa kisiasa, mbali na matatizo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na migogoro ya hapa na pale. Madaraka ya *mai* yalikomeshwa na baraza lake lilivunjwa na Sheikh Umar kuwa mtawala mkuu wa nchi hiyo. Kilichotokea ni kwamba, katika kujaribu kuokoa utawala wake uliokuwa unadidimia, mnamo 1846 Mai Ibrahim alimwalika sultani wa Baghirmi kumwangamiza Sheikh Umar, lakini badala yake alikufa mwenyewe mikononi mwa Sheikh.

Sheikh pia alimshinda na kumuua Ali, mrithi wa Mai Ibrahim. Baada ya hapo, Umar alipata matatizo na kaka yake mwenyewe, Abd al-Rahman, ambaye alimwondoa madarakani. Baadaye Umar alirejea tena katika madaraka, akaamuru Abd al-Rahman auawe, na akaendelea kutawala hadi 1881.

Ushindani huu katika Borno uliwezekana tu kwa sababu ya kutokuwepo kwa tishio lolote kutoka nje, hali iliyoruhusu kuwepo kwa ushindani ndani ya nchi. Wakati Borno



22.4 *Blauzi ya mwanamke wa Borno iliyotarizwa ambayo imetengenezwa katika miaka ya 1870*

ilipokuwa katika msukosuko, Sokoto ilikuwa pia imekumbwa na matatizo ya maasi na machafuko. Kipengele muhimu katika matukio hayo ni kushindwa kwa kila dola kuyatumia matatizo ya mwenzake kujinufaisha. Katika nchi zote mbili, hali ilirudia kuwa ya kawaida kwa haraka baada ya 1855.

Baada ya hapo, Borno iliunganishwa chini ya Sheikh Umar kama mkuu wa nchi. Alihodhi madaraka yote na kumpatia yeyote aliyemchagua. Hali hii lilijenga mazingira ambamo kumtii Sheikh kulikuwa ndio sifa ya msingi ya kuweza kupanda ngazi katika muundo wa kisiasa.

Ushindani kwa ajili ya madaraka ulikuwa wazi kwa kila mtu, bila kujali haki ya kuzaliwa wala daraja. Hivyo baraza la kifalme halikuhusisha tu ndugu wa mfalme, bali pia watu huru mashuhuri, na watumwa waliokuwa maofisa. Muundo huu wa kisiasa ulikuwa ni tofauti na ule ulioendeshwa na al-Kanemi ambamo maofisa muhimu wa dola hawakuwa waajiriwa wake hasa, bali washirika wake.

Kulikuwepo pia na mabadiliko katika uchumi. Polepole Borno iliingizwa katika mzunguko wa uchumi wa ukhalifa kama mtoaji wa mali ghafi kama vile bidhaa za ngozi, pembe za ndovu, manyoya ya mbuni, watumwa na magadi, na kama mlaji wa bidhaa za anasa ambazo zilikuwa na faida ndogo kwa watawala kuliko hapo awali. Msingi wa uzalishaji wa Borno haukukua haraka kama ule wa ukhalifa wa Sokoto. Matokeo yake ni kuwa madeni ya biashara ya Borno yaliongezeka. Ingawa matatizo haya ya kiuchumi




**22.2** *Bidhaa za kazi za mikono za Wahausa zilizokusanywa na Gustav Nachtigal mnamo 1870*

# 23 Messina na himaya ya Kitorodbe (Kitukuloor) ¹adi mwaka 1878

## *Utangulizi*

Historia ya Afrika Magharibi mwishoni mwa karne ya kumi na nane na kumi na tisa ilidhihirisha kukua kwa athari ya Wanomadi wa Kifulbe. Siyo tu kuwa idadi yao iliongezeka katika kipindi hiki, lakini umuhimu wao wa kiuchumi pia uliongezeka sana. Huko Futa Jallon na Futa Toro, kidogo kidogo waliutupilia mbali utawala wa jamii za wakulima wastakimu. Harakati hizi zilisambaa mpaka nchi ya Wahausa na kutoka hapo zikafika Liptako na Massina mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Lakini huko Massina walipambana na upinzani mkali kutoka kwa Wabambara wa Segu walioendelea kuwatawala.

Katika karne ya kumi nane, madaraka ya Wasegu yalipanuka haraka katika nchi zote jirani, na waliwatoza raia zao, hasa wafugaji wa Kifulbe, kodi kubwa. Wakati huo huo, kwa sababu ya kuendelezwa kwa vitendo vyenye kupingana na Uislamu, vituo vya Kiislamu kama kile cha Jenne vilipoteza hamasa yake. Kufaulu kwa mapinduzi ya Kiislamu huko Futa Toro na Futa Jallon katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane, na huko Sokoto mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, kulisaidia kueneza fikra za kimapinduzi huko Massina na kuchoehea hamu ya kutaka kubadilisha hali ya mambo.

Warabiti kadha walijaribu kuitumia hali ya kimapinduzi iliyokuwepo katika eneo la delta ili kujipapatua kutoka katika utawala wa Kibambara. Wote hawa walidai kuwa ni watiifu kwa Uthman dan Fodio, na kiongozi wa upinzani mkubwa zaidi huko Massina alikuwa ni Ahmadu Hamadi Buba Sangara. Ingawaje, Seku Ahmadu ndiye aliyefaulu kutayarisha harakati zilizoweza kuuangamiza utawala wa Wabambara na kuifanya Massina iwe dola la Kiislamu lenye nguvu, na pahala pa kuanzia katika kupenyeza himaya yake katika maeneo mengine.

## *Seku Ahmadu (Sheikh Ahmad Lobbo)*

Seku Ahmadu, aliyezaliwa Massina mwaka 1773, alipata umaarufu kutokana na uchamungu, uaminifu na unyenyekevu wake. Alijipatia mafunzo huko Jenne chini ya sufii mashuhuri na alihubiri wazo la kurejea kwenye Uislamu safi. Seku Ahmadu alivutia wafuasi wengi na aliendeleza uhusiano na Uthman dan Fodio wa Sokoto ambaye alimpa




**23.1** *Massina katika kilele chake mwaka 1830 (Kutoka kwa M Ly-Tall)*

cheo cha *Shaykh* (Shehe) na kumpelekea bendera. Harakati zake zilichukua sura ya uasi dhidi ya watawala wa kienyeji na washirika wao wa Kisegu. Segu ilishindwa katika mapambano yaliyotokea na jambo hilo liliwavutia Wafulbe wengi ambao walijiunga naye.

Jenne ilitekwa na wapiganaji hawa mwaka 1819, na baada ya hapo Messina ilifanywa kuwa dola la Kiislamu lenye nguvu.

Lakini kabla Messina haijaweza kujiimarisha katika eneo hili, ilibidi ipambane na maadui wachache. Wa kwanza alikuwa Segu. Wabambara wa Segu walikataa kuitambua Massina kama ni dola huru ya Kiislamu. Jambo hili lilisababisha vita vya muda mrefu ambavyo vilimalizika pale tu Wabambara walipokuwa tayari kukubali kuwepo kwa dola ya Kiislamu mipakani mwao. Upinzani mwingine dhidi ya Massina ulitokana na Wafulbe wa Fittuga ambao walitaka kuanzisha jihadi yao wenyewe katika eneo la ndani ya delta ya Niger pasi na kumhusisha Seku Ahmadu. Waliungwa mkono na Wakunta, watawala wa Timbuktu, na Muhammad Bello kutoka ukhalifa wa Sokoto. Utawala wa Sokoto uliiunga mkono Fittuga kwa sababu Seku Ahmadu alitumia fursa ya kifo cha Uthman dan Fodio kuiasi Sokoto. Juu ya kuungwa mkono kote huku, Wafulbe wa Fittuga mwishowe walishindwa na Seku Ahmadu katika mwaka 1823.

Baada ya hapo, Seku Ahmadu alijishughulisha na Timbuktu ambayo wakati huu ilikuwa ikitawaliwa na Wakunta, kikundi cha machotara wa Kiberiberi ambao walianzisha mamlaka yao huko katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane. Timbuktuu pia ilitekwa na Seku Ahmadu. Kwa hivyo ilipofika mwaka 1845 madaraka ya kisiasa ya Massina yalienea kutoka Jenne hadi Timbuktu na kutoka eneo la Napala hadi nchi ya Dogon.

## *Asasi za dola ya Dina*

Seku Ahmadu (1818-45) aliweza kuanzisha vyombo imara vya kidini na vya kiutawala katika dola mpya yenye msingi wa kidini iliyoitwa *dina*. Kama ilivyokuwa katika madola mengine ya Kiislamu, sharia ilitumika katika nyanja zote za maisha nchini. Kulikuwa na baraza kuu lililokuwa na wajumbe arobaini walioteuliwa na Seku Ahmadu mwenyewe ambalo lilimsaidia katika masuala yote ya utumiaji wa mamlaka, ingawa mara nyingine aliyapinga maamuzi ya baraza hilo. Mbali ya baraza kuu, kulikuwa na baraza la ushauri ambalo wajumbe wake walikuwa ni Seku Ahmadu mwenyewe na wajumbe wawili kutoka baraza kuu. Baraza la ushauri lilizizingatia shughuli zote za dola kabla hazijawasilishwa katika baraza kuu.

Hukumu kortini kwanza zilitolewa na makadhi. Kwa kawaida adhabu zilikuwa kali, na muendesha mashtaka vilevile alikuwa mkali sana. Kodi na ushuru, zikiwemo ada za kawaida zilizoruhusiwa na sharia ya Kiislamu na michango ya vita iliyoanzishwa na baraza kuu, ilikusanywa na maafisa wa dola. Mateka wa vita walifanyishwa kazi za kilimo katika mashamba makubwa kwa ajili ya dola. Hivyo majimbo ya Massina yaliweza kutoa kwa wingi mchele, mahindi na aina mbalimbali za mboga. Hata hivyo, wakati huu biashara iliathirika kwa sababu ya vita vya muda mrefu dhidi ya Wabambara.

Ili kuleta utawala wenye ufanisi, nchi iligawiwa katika majimbo matano ya kijeshi,



23.2 *Magofu ya mnara wa kujahami wa tata (ngome) huko Hamdalla*

kila jimbo likiongozwa na jamaa au mfuasi mtiifu wa Seku Ahmadu. Majimbo yenyewe yalikuwa ni: (a) Niger na eneo la mpakani baina ya mto Niger na mto Bani, (b) mpaka ya magharibi, (c) eneo la kulia kando kando mwa mto Bani, (d) mpaka wa mashariki na (e) eneo la ziwa. Mji mkuu, Hamdallahi, ulianzishwa mwaka 1820. Majengo yake yaliyovutia zaidi ni msikiti na kasri. Mji mkuu ulilindwa imara na askari wa polisi na ulikuwa nadhifu mno. Maisha katika mji mkuu huu yalikuwa na nidhamu ya hali ya juu. Mathalan kulikuwa na taratibu kali zilizoelekeza jinsi matabaka mbalimbali katika jamii yalivyotakiwa kutumia wakati wao.

* Fanikio muhimu kabisa la Seku Ahmadu ni juhudi yake ya kuwageuza Wanomadi wa Kifulbe waunde jamii zenye maskani ya kudumu. Ili kufanikisha azma hii, alianzisha vijiji vingi vya shughuli za kilimo na ufugaji. Juhudi hizi zilizaa matunda wakati wa utawala wa mwanawe, Ahmadu Seku.

## *Ahmadu Seku (1845-53) na kipindi kilichofuatia*

Kipindi cha utawala wa Ahamdu Seku kinachukuliwa kuwa ndicho kilichopindukia kwa amani na neema huko Massina katika karne hiyo. Jambo hili halimaanishi kwamba hakukuwa na matatizo ya awali nchini na nje ya nchi. Matatizo ya ndani yalitokana na mizozo iliyofuatia kifo cha Seku Ahmadu. Matatizo ya nje yalisababishwa na Wabambara wa Saro na Watuareg wa eneo la Timbuktu ambao walitumia fursa ya kifo cha Seku Ahmadu kufanya uasi dhidi ya mamlaka ya Massina. makundi yote mawili yaliweza kudhibitiwa, ingawa Watuareg walishughulikiwa kwa ukatili zaidi. Baada ya vita hivi Wabambara wa Monimpe vilevile walidhibitiwa.

Licha ya matatizo haya ya awali, miaka ya mwisho ya utawala wa Ahmadu Seku

ilikuwa ya amani. Aliweza kuilinda mipaka ya utawala wake kutokana na hujuma kwa kutumia mbinu za zilizochanganya diplomasia na mabavu. Pia alifaulu kudumisha amani ndani ya nchi. Lakini baada ya kifo chake mwaka 1853 matatizo ya ndani na nje yalifumka kwa kasi kubwa. Mgogoro wa urithi uliwahusisha watu mbalimbali katika familia ya Seku Ahamdu, na uliigawa Massina katika kambi zilizohasimiana. Ahmadu mo Ahmadu ambaye hatimaye alirithi ufalme hakuwa na ustadi wa kisiasa na sifa za uongozi ambazo zingeweza kuiondoa mifarakano hii. Kinyume chake, utawala wake ulizidisha sakata. Alifanya mabadiliko makubwa katika vyombo vya dola kwa kuwaondoa viongozi wa dini na warabiti wakongwe walioheshimiwa na badala yao kuwaweka vijana wa rika yake wenye mtazamo wa kiliberali zaidi. Dola lake lilitawaliwa na majungu, uhasama na migongano. Massina ilikuwa katika hali hii wakati al-Haji Umar alipoishambulia.

## *Kuzuka kwa himaya ya Kitorodbe (Kitakuloor)*

Mwanzoni mwa karne hii dola nyingi zilichipuka huko Sudan ya Magharibi na Kati ambazo uhai wake wa kisiasa na kiuchumi ulitegemea kudumu kwa biashara ya watumwa. Wafulbe ambao walikuwa miongoni mwa wale waliokutishwa madhila makubwa sana wakati huu waliathirika sana na hali hii. Na inaweza kusemwa kwamba jibu lao kwa hali hii lilichukua sura ya vuguvugu la kitaifa lililoambatana na mageuzi ya Kiislamu yaliyoanzisha dola za kimapinduzi huko Futa Toro, Futa Jallon na Sokoto, ambako tayari kulikuwa na jamii kubwa za Kiislamu. Ingawaje, utumwa haukuondolewa bali uliendeshwa kwa mujibu wa sharia za Kurani. Baadhi ya tawala ndogo ndogo zilizokuwepo baina ya Massina, Futa Jallon na Futa Toro ambazo zilikuwa bado kukumbwa na sharia ya Kiislamu baadaye ziliingia mikononi mwa Tijaniyya.

Jihadi ya Al-Haji Umar ilikuwa matokeo ya hali iliyokuwako Futa Toro katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Huko Futa Toro, kama ilivyokuwa katika madola mengine ya Kiislamu katika Sudan wakati huu, Uislamu ulitishiwa na mizozo ya urithi wa ufalme kutoka ndani na upanuzi wa himaya ya Wafaransa kutoka nje.

## *Jihad ya Al-Haji Umar*

Umar Saidu (Al-Haji Umar) alizaliwa mwaka 1796 katika ukoo wa Waislamu wachamungu ambao walishiriki kikamilifu kwenye mapinduzi ya Kiislamu mwishoni mwa karne ya kumi nane. Aliyakana madhehebu ya Kadriyya ambayo yalikuwa miongoni mwa tarika za kale kabisa katika Afrika ya watu weusi, na akajiunga na tarika ya Tijaniyya; kisha alisafiri mpaka Afrika kaskazini na Mashariki ya Kati ili kujielimisha zaidi kuhusu misingi ya tarika mpya. Baada ya kusafiri kwa muda ya miaka ishirini (1826-47), na kujipatia katika kipindi hiki maarifa na tajiriba kubwa, alirudi nyumbani akiwa na cheo cha Khalifa Mkuu wa Tijaniyya aliyepewa jukumu la kukamilisha shughuli ya kuisilimisha Afrika ya watu weusi.

Alikaa Sokoto kwa muda fulani (1830-38) ambapo alijifunza kwa Muhammd Bello namna ya kutayarisha vita vya jihadi kabla ya kuelekea nyumbani. Mwishowe alifanya




**23.3** *Himaya ya Kitorodbe wakati ilipofikia kilele chake (kutoka M.Ly-Tall)*

maskani yake Futa Jallon, badala ya Futa Toro, na kuifanya Jugunku kuwa ndiyo makao makuu ya shughuli zake. Huko alikusanya wafuasi, akanunua silaha nyingi na kufanya kampeni kubwa kwa ajili ya vita vya jihadi. Mwaka 1847 aliyahamishia makao makuu yake Dinguiraye, ambako alipigana na mtawala wa huko aliyeitwa Gimba Sacko mwaka 1852.

Wabambara wa Segu na utawala jirani wa Kaarta, kama tulivyokwisha eleza, waliupinga sana Uislamu. Walizionea fahari dola zao ambazo zilipata nguvu sana na kustawi kuanzia Mande mpaka Timbuktu. Nguvu zao zilitegemea jeshi hodari la askari wa farasi na pia jeshi lililopata mafunzo kamili la watumwa wa kifalme wenye utiifu mkubwa kwa bwana zao na ambao kiongozi wao alipata fursa maalum katika dola, hasa nyakati za urithi wa utawala. Pia waliunda wenyewe baadhi ya silaha na pia risasi zao. Kwa njia hii, Wambambara waliweza kuupanua utawala wao hadi katika nchi nyingi za jirani, na pia kufanya biashara kubwa ya watumwa wa kusafirishwa nchi za ng'ambo, na wa kulima mashamba ya kifalme.

Hata hivyo, Wabambara walishindwa kuungana ili kukabiliana na tishio la Watijaniyya. Segu ilivutia upande mmoja na Kaarta upande wa pili. Hata Kaarta alijitumbukiza kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya watawala wa Kimassassi na Wajawara waliowanyang'anya madaraka. Umar aliamua kuhujumu dola moja moja. Alianza kwa mashambulizi dhidi ya Koniakary, halafu Nyoro, mji mkuu wa Kaarta. Kutoka hapo, mnamo mwaka 1857, aliwageukia Wafaransa katika mji wa ngome wa Medina mpakani na Futa Toro. Juu ya ushujaa na ujasiri uliooneshwa na Waislamu, Jenerali Faidherbe alifaulu kuwaauni Wafaransa waliokuwa wameelemewa. Wafaransa sasa wakawa ndio maadui wasiosuluhika wa Umar wakati Watijaniyya walipoelekeza harakati zao upande wa mashariki.

Al-Haji Umar alirejea kutoka Futa mwaka 1859 na kuamua kwamba wakati wa kuishambulia Segu, mji mkuu wa Wabambara, ulikuwa umefika. Wakati huu Segu tayari ilikuwa imeanza kudidimia. Al-Haji Umar aliliingilia eneo la Segu kwa nyuma na kuyakamata baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakidhibitiwa na kuilipa kodi Segu. Majeshi ya jihadi yalipokuwa yanasonga mbele, mtawala wa Segu alijaribu kujiunga na Massina ambayo viongozi wake pia waliyaogopoa majeshi ya Watijaniyya. Lakini kutokana na matatizo makubwa ya ndani, si Segu wala Massina iliyoweza kulizuia jeshi la Umar. Jeshi la Watijaniyya liliingia Segu mwaka 1862 na mtawala wake akakimbilia Massina.

## *Vita na Wamassina*

Kabla ya jihadi ya Al-Haji Umar, Massina, kama dola nyingine za Kiislam katika eneo hili, ilikuwa tayari inakabiliwa na matatizo kutoka kwa majirani zake waliokataa kudhibitiwa. Wakati vita vya jihadi vya Al-Haji Umar vilipoanza kusonga mbele, Massina ilihisi imekabiliwa kweli na tishio la dola nyingine kutaka kuunyakua uongozi wake wa kisiasa na kidini katika eneo lile. Wakati Umar alipomnyoshea Ahmadu mo Ahmadu mkono wa urafiki ili waungane kumpiga vita kafiri, Ahmadu mo Ahmadu alikataa akidai kwamba eneo lote tangu Segu mpaka Kaarta lilikuwa katika himaya yake. Hii inashangaza, maana licha ya Massina kushindwa kuisilimisha Segu na maeneo

mengine yaliyokuwemo kwenye sehemu iliyodai kuwa katika himaya yake, vilevile haikuwa na mamlaka ya kisiasa juu yao.

Mwaka 1860, kufuatia ushirikiano kati ya Massina na Segu ulioundwa ili kumzuwia Al-Haji Umar asisonge mbele, majeshi ya muungano ya dola mbili hizi yaliweka kambi dhidi ya Sansanding, ambayo ilikwisha tekwa na Umar. Mwanzoni Umar alisita kupigana na Massina, dola ya Kiislamu kama yake, lakini mwishoni aliutumia ushirikiano kati ya Massina na Segu, dola isiyokuwa ya Kiislamu, kuwa ndio sababu ya kuhalalisha vita dhidi ya Ahamadu mo Ahmadu. Umar aliishambulia Massina mwaka 1862 na kuiteka Hamdallahi, mji mkuu wake. Aliweka mji huo chini ya utawala wa mwanawe Ahmadu na akawatia adabu kali wale machifu wasaliti wa Massina. Hapo tena alikabiliwa na muungano wa Timbuktu na Massina.

Chifu wa Kikunta wa Timbuktu, al-Bekkai, aliendeleza sera ya kuwaunga mkono maadui wa Umar ili amvunje moyo. Kwanza, mwaka 1860, el-Bekkai alifanya mawasiliano na Wabambara na kuwaunga mkono kihali. Baadaye, mwaka 1862, baada ya kutekwa kwa Massina, aliuunga mkono uasi uliokuwa ukitokota huko Hamdallahi dhidi ya majeshi ya Umar. Uasi huu ulilizuilia pale, na kulishinda vibaya, jeshi kubwa la Umar. Hatimaye uasi huu ulipelekea kwenye kifo cha Al-Haji Umar mwaka 1864. Lakini juu ya ushindi wao wa awali, waasi hawakuweza kuyashinda kabisa majeshi ya jihadi. Msaada wa kijeshi, ukiongozwa na Tijani Alfa, mtoto wa mjomba wa Umar, ulifika kutoa auni kwa majeshi ya Kiislamu na hivyo yakaweza kuwashinda waasi wote pamoja na washirika wao.

## *Mpangilio wa himaya ya Watorodbe (Watukuloor)*

Himaya ya Watukuloor iliyoasisiwa na Al-Haji Umar ilikuwa kubwa sana ikikusanya maeneo kuanzia Gidimaka mpaka Timbuktu, na kuanzia Dinguiraye mpaka Sahara. Serikali yake, ingawaje, haikuwa unganifu. Mamlaka yalihamishiwa kwenye vituo mbalimbali vya utawala vilivyohusika na shughuli za kisiasa na kidini na kuongozwa na wafuasi waliojulikana kwa jina la ma*talib*. Al-Haji Umar hakujishughulisha sana na mambo ya utawala bali aliwakabidhi wafuasi wake shughuli hizo. Alijiona yeye mwenyewe kuwa ni sufii ambaye dhamana yake ya mwanzo kabisa ilikuwa kuwasilimisha watu weusi.

Wasaidizi wake wa karibu walikuwa Alfa Umar Thierno Bayle Wan na Abdulaye Hausa; wote wawili walifanya kazi kubwa katika vita vya jihadi. Aliwapa ma*talib* fursa kubwa ya kutoa uamuzi katika mambo yote makubwa kwa kuwasilisha mipango yake mwenyewe kwenye baraza la ma*talib* ili kupata kibali chao. Na kwa sababu ya ukarimu wake aliwavutia wafuasi wengi.

Majeshi ya jihadi yalikuwa na mchanyiko wa makabila mbalimbali, yakiwa na vikosi kutoka Futa Toro, nchi ya Wahausa, Futa Jallon, Khasso, Kaart na Segu. Vikosi kutoka Futa Toro ndivyo vilivyokuwa na askari wengi kabisa. Jeshi hili, ambalo lilikuwa na batalioni nne, kila moja ikiongozwa na kikosi kutoka Futa Toro, lilikuwa na bunduki za biashara, panga na bunduki chache za mitutu pacha. Wahunzi wa kienyeji walitengeneza matufe ya chuma yaliyotumika kwenye mizinga. Pia kulikuwa na mizinga miwili




23.4 *Kutoka Dingiraye mpaka Hamdallahi (Kutoka kwa M. Ly-Tall)*

iliyotekwa kutoka kwa Wafaransa. Uwezo mkubwa wa majeshi ya jihadi haukutokana na nguvu za silaha zao, bali ulitokana na imani yao pamoja na mikakati madhubuti. Umar aliyashajiisha majeshi yake kwa kuwahubiria habari za pepo na tunza zinazowasubiri huko ahera. Hii iliwapa moyo zaidi askari na walichukulia vita kuwa ni wajibu wao wa kidini.

Mambo mengine pia yalisaidia kufanikisha jihadi. Mojawapo ni kwamba mara nyingi jeshi la jihadi lilipigana na jeshi lililogawanyika. Pia waliwazidi maadui zao katika kupanga mikakati ya kijeshi. Aidha walitumia vitisho kama silaha ya kuogopesha watu. Ingawaje, kabla ya kupigana na kikundi chochote, kwanza walikipa kikundi hicho hiari ya kusilimu kwa amani na kunusurika na vita. Kukataa shauri hilo moja kwa moja kulisababisha mapigano. Baadhi ya vikundi hivi vilikubali ushauri wa kujipatia amani na kuepukana na janga la vita. Lakini pia mara nyingi watu walikataa kusilimu na hivyo vita kutangazwa dhidi yao.

Uchumi wa jeshi kwa kiasi kikubwa ulitegemea ngawira zilizopatikana vitani. Ingawa Al-Haji Umar alijaribu kugawa ngawira kihalali na mara kwa mara, na hivyo kuweza kudumisha umoja na mshikamano wa jeshi hadi alipofariki, matatizo yalizuka wakati wa mrithi wake, Ahmadu. Juu ya hivyo jeshi lilichangia sana katika kudumisha utiifu wa majimbo mbalimbali ya himaya hii.

## *Utawala wa majimbo*

Hapa na pale katika majimbo kulikuwa na vituo vyenye ngome; kuanzia vituo hivyo Uislamu ulitarajiwa kuenea sehemu nyingine. Baadhi ya vituo muhimu kabisa vilikuwa ni Dinguiraye, Nyoro na Segu. Dinguiraye kilikuwa ndicho kituo cha kwanza cha kihistoria cha himaya hii. Hapo ndiko familia nzima ya Al-Haji Umar ilipoishi. Ngome madhubuti ilijengwa hapo ambayo ilihakikisha usalama wa sehemu hii ya himaya. Jimbo hili liliendeshwa na mtoto wa mjomba wa Al-Haji Umar. Baada ya Ndinguiraye ilifuatia Nyoro, jimbo kubwa kabisa katika himaya hii. Nyoro iikuwa na ngome nyingi na watu kadha waliokimbia madhila ya Wafaransa ambao waliongeza idadi ya wakaazi wa jimbo hili. Nyoro kwanza ilitawaliwa na Alfa Umar Thierno kabla Mustafa hajamrithi. Kabla ya mwaka 1864, Segu ulikuwa mji mkuu wa jimbo ulioendeshwa na mtoto mkubwa wa Umar. Lakini baadaye ulikuwa mji mkuu wa himaya ya Torodbe chini ya Ahmadu.

Katika ngome zote hizi za Kiislamu kwenye maeneo yaliyosilimishwa karibuni, utawala ulikuwa na sehemu mbili. Kulikuwa na mkuu wa dini ambaye kazi yake ilikuwa kuendeleza usilimishaji wa watu, na mtawala wa kijeshi aliyekuwa akimlinda. Al-Haji Umar pia alikuwa na nyumba katika kila jimbo ambamo aliweka sehemu ya familia yake. Hakujifikiria mwenyewe kuwa ni mtu mwenye makazi pahala pamoja kama walivyokuwa watawala kidunia. Kila moja kati ya majimbo haya lilikuwa na utawala wake huru. Umar alikuwa mkuu wa kidini tu wa himaya hii. Ingawa kulikuwa na sehemu ndogo ndogo zenye chokochoko, utulivu na usalama ulitawala katika jimbo zima. Katika majimbo yote hukumu zilitolewa na kadhi kufuatana na sharia za Kurani

katika kesi za daawa; na kesi za kisiasa na za jinai zililetwa mbele ya mkuu wa dini wa jimbo.

Mtazamo wa Al-Haji Umar kuhusu utawala wa himaya yake, kama ulivyokwisha elezewa hapo juu, haukutoa nafasi kwa maendeleo ya kiuchumi katika maeneo yaliyotekwa. Majimbo yaliathirika vibaya kiuchumi kutokana na vita vya mara kwa mara, na hali hii iliendelea mpaka wakati wa kifo chake. Ingawa matokeo ya kiuchumi yalikuwa mabaya sana kwa maeneo yote yaliyotekwa, lakini maeneo haya hayakuathirika kwa kiwango kile kile. Pia kilimo, ambacho kiliathirika zaidi kutokana na vita vya jihadi, kilifufuliwa mwaka 1863-4. Kwa mfano, Wamandika walikuwa na utajiri wa zao la pamba, Wakita utajiri wa zao la tumbaku, mboga mboga, matikiti na mishea (miti yenye kutoa mafuta). Maeneo mengine kama vile Kaarta, Dyangunka na Segu pia yalistawi kwa upande wa kilimo.

Biashara pia iliendelea katika baadhi ya maeneo ya Sudan ya Kati licha ya kuweko kwa vita. Njia kuu zilizoiunganisha Sudan na sehemu za kusini na kaskazini zilibaki ziliendelea kutumika sana. Mbali ya shughuli za biashara na kilimo, ngawira kutoka vitani pia zilisaidia katika kulitajirisha dola. Kutokana na utajiri uliopatikana kwenye vyanzo hivi, Al-Haji Umar mara moja moja alisambaza utajiri mwingi kwa ma*talib* wake. Mapato ya dola yalipatikana pia kutokana na malipo mbalimbali kama vile zaka, ambayo walitozwa Waislamu, *mudu*, ambayo ni sadaka ya kila mwaka iliyotolewa na Waislamu wakati wa karamu ya Ramadhani, na ushuru uliolipwa na misafara na wafanya biashara. Wakati wa utawala wa Ahmadu, mrithi wa Al-Haji Umar, kiwango cha malipo kiliongezwa sana na hivyo kusababisha uasi wa mara kwa mara. Ma*talib* pia walimshutumu kwa kutokuwa na nkarimu kama ule wa baba yake.

Jamii katika himaya ya Watukuloor ilitawaliwa na ma*talib*. Hawa walikuwa watu kutoka kabila na nchi mbalimbali na kutoka katika hali mbalimbali kwenye jamii ambao walitukuzwa na Umar katika juhudi zake za kupinga utawala wa kijadi. Ma*talib* waliajiriwa kutokana na ujuzi wao na uzingativu wao wa maadili ya Kiislamu. Ma*talib* walikuwepo katika miji mikuu yote ya majimbo na pia katika vijiji vikubwa ili kuwasaidia wakazi waliosilimu karibuni kuyaelewa maadili ya Kiislamu. Walihodhi nyadhifa zote za juu katika himaya, na kuunda kikundi kipya cha waali wa kisiasa-kidini.

Ahmadu, ambaye hakuwa na sifa za kidini na kiaskari alizokuwa nazo baba yake, Al-Haji Umar, alishindwa kuwadhibiti ma*talib*. Kwa hivyo aliwategemea ma*sofa*, ambao walikuwa ni tabaka la kijeshi lenye maarifa haba ya Uislamu. katika juhudi zake za kuvunja nguvu za ma*talib*. Hii ilisababisha ushindani kati ya ma*talib* na ma*sofa*, ushindani ambao uliubainisha utawala wa Ahmadu.

## *Urithi mgumu: Ahmadu (1862-78)*

Tatizo la kwanza liliomkabili Ahmadu alipotawala ni zile njama dhidi yake huko Segu na Hamdullahi. Katika kupambana na hali hii alifanya kosa lililomfanya aipoteze Sansanding, kituo muhimu cha biashara. Kulikuwa na tatizo la msingi zaidi la mgawanyiko miongoni mwa ma*talib*. Ahmadu alijikuta akiongoza kambi mbili za



**23.5** *Lango la kuingilia Kasr, huko Segu-Sikoro*

**23.6** *Ahmadu akipokea wageni kwenye uga wa Kasr*



*matalib*. Badala ya kutafuta njia ya kuzipatanisha, aliunda kikundi cha tatu, kile cha *masofa*, ambacho kilikuwa kikundi cha mateka waliojiunga na jeshi la jihadi. Kwa hivyo juu ya uhodari na uchamungu wake mkubwa, Ahmadu hakufaulu kabisa kutumia mamlaka yake kwa ufanisi kama alivyoweza kufanya baba yake.

Pia alikabiliwa na uasi katika jimbo zima, uasi mkubwa kabisa ukitokea Beledugu. Kilimo na biashara viliathirika vibaya kutokana na uasi huu. Uasi huu pia ulimfanya ashindwe kushughulikia sawa sawa sehemu nyingine za himaya yake. Hii iliwapa watawala wa majimbo uhuru wa kujitendea watakalo na kuwafanya wakatae kuwajibika kwake au kumpelekea rasilimali za kumsaidia. Ingawa Mustafa, ambaye aliitawala Nyoro, aliwajibika kikawaida kwa Ahmadu kuhusiana na shughuli zake za uongozi, Tijani Alfa alilitawala jimbo la Massina kwa uhuru kamili na kuifanya Bandiagara ndio mji wake mkuu. Kana kwamba haya hayakutosha, Ahmadu alikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa ndugu yake, Muhammadu Habibu, ambaye alikasirishwa kwa sababu hakupewa mamlaka yenye maana katika himaya hii. Habibu na ndugu mwingine Mukhtar aliwashawishi *matalib* kadha kumpinga Ahmadu na hivyo kudhoofisha mamlaka yake.

Mwaka 1869 Ahmadu alianza mchakato wa kuyaimarisha mamlaka yake dhidi ya matishio kutoka kwa ndugu zake. Kwa kipindi cha miaka minne aliendesha mapambano makali dhidi yao na wote wale waliounga mkono madai yao ya kutaka sehemu ya urithi wa baba yao. Wakati huo huo alividhibiti baadhi ya vituo vya uasi vya Bambara na Soninke. Aliibuka mshindi katika vita hivi na ndugu zake. Ilipofika mwaka 1874, Ahmadu alikuwa katika kilele cha madaraka yake. Kufuatia mapendekezo ya *matalib*, aliwaachia ndugu zake baadhi ya maeneo ya utawala wake, japo alihakikisha kuwa wanaendelea kuwa chini ya mamlaka yake. Pia aliuimarisha utawala wake katika mji wake mkuu huko Segu.

Biashara na vituo vya biashara vya Kifaransa vilivyokuwepo Senegal ya Juu na vya Kiingereza vya Sierra Leone vilianzishwa tena. Kwa hivyo uchumi wa himaya hii uliingizwa katika mikondo mingi. Biashara ya huko Hausa na biashara ya kola pia zilipanuka, na hali ya uchumi huko Sudan ilitulia kwa kipindi fulani.

## *Hitimisho*

Ilipofika mwaka 1878, Ahmadu alikwisha kiuka vizingiti vyote vilivyomkabili baada ya kifo cha baba yake. Wabambara bado walikuwa shida kuwadhibiti lakini hawakuhatarisha sana himaya yake. Uenezaji wa Uislamu, na ile sera ya kushirikiana na jamia zote na vikundi vyote vya kijamii iliyoanzishwa na Al-Haji Umar iliendelezwa na mrithi wake na kuleta muungano wa hali ya juu wa tamaduni tofauti katika ukanda huo. Uhakika wa mshikamano huu unathibitishwa na ukweli kwamba wakati wa ukoloni katika karne ya ishirini, Sudan, ambayo ndilo eneo la himaya ya Torodbe ya kale, ilikuwa na matatizo machache tu ya kikabila. Vilevile ule urithi wa kidini ambao Al-Haji Umar aliwaachia warithi wake ulichangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mshikamano wa kitamaduni katika eneo hili.

# 24 Nchi na Watu wa Senegambia na Upper Guinea

Sura hii inachunguza historia ya watu wa pwani ya Magharibi ya Afrika kuanzia Senegambia hadi Bandama katika karne ya kumi na tisa. Kuna ufanano katika historia ya eneo hili katika karne ya kumi na tisa ijapokuwa hatuwezi kusema hivyo kuhusu karne za nyuma zaidi. Ufanano huu ulíletwa na kuwepo kwa Wazungu na kuanzishwa kwa himaya zao katika pwani yote. Lakini badala ya kuikabili historia ya ukanda huu kwa mwelekeo wa kuwepo kwa Wazungu, tutaingalia kwa mwelekeo wa Waafrika. Kwa vile ukanda huu una maeneo ya tamaduni mbalimbali, tutaziangalia tamaduni hizi kila moja peke yake, kwa kuzitaja kwa majina, yaani: Senegambia, Upper Guinea na Futa Jallon, nchi ya Kru, na Mande kusini.

## *Senegambia*

Ukanda wa Seneganıbia umeunganishwa na pwani ya Atlantiki upande wa Magharibi ambako uliingiliwa na athari ya Wazungu kutokana na biashara ya watumwa. Jamii ya Senegambia ilikuwa na hulka ya Wasudani na Waislamu na hili liliwafanya watu hao kuwa imara zaidi kuliko wale wa Ghuba ya Guinea. Hata hivyo, pamoja na uimara huu, ukanda huu uliathiriwa sana na mabadiliko ya kiuchumi. Moja kati ya athari hizo ilitokana na mabadiliko ya soko la nje kwa bidhaa zake pamoja na watumwa. Ijapokuwa biashara ya watumwa ya nchi hiyo ilipungua kutokana na jitihada za kukomesha biashara hiyo, haikufifia hadi ilipofikia katikati ya karne ya 19. Badiliko muhimu zaidi katika ukanda huu lilikuwa ni kuongezeka sana kwa bei za bidhaa za Senegambia kama vile sandarusi, dhahabu, ngozi, vipusa, nta na njugu.

Mabadiliko haya ya biashara ya kigeni yaliathiri uchumi wa wenyeji. Pato lilihama kutoka mikononi mwa wafanya biashara ya watumwa kwenda kwa vikundi vya watu waliokuwa wanasimamia uzalishaji huu mpya. Uislamu mpya wa kiuchokozi vilevile ulipata nguvu zaidi katika jamii ya Senegambia ilipofikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Uchokozi huo ulikuwa ni njia ya malalamiko ya watu wa kawaida, ambao walianza kusilimishwa kwa wingi, dhidi ya tabaka tawala ambalo ilitaka kunufaika na uzalishaji mpya kwa kuwavamia wanyonge badala ya kuwalinda. Jambo hili lilisababisha machafuko na vurugu ambazo zilikuwa kubwa, zaidi katika falme za kaskazini za Wolof na Sereer – falme tutakazozijadili hivi punde. Hali hii iliendelea katika karne ya kumi na tisa hadi ushindi wa Wazungu ulipoleta utaratibu mpya.




**24.1** *Nchi na watu wa Senegambia na Upper Guinea (mfano wa Y. Person)*

Huko Waalo, wakati watawala wakizidi kushikilia ukale katika matendo ya jadi ya kidini, watu wa kawaida waliingia Uislamu kwa makundi. Katika uwanja wa uchumi, uhusiano mpya wa kibiashara na Ulaya ulianza kujengeka, na bidhaa za kilimo kama vile sandarusi, ngozi na nta zilibadilishwa na wafanyabiashara wa Kizungu. Matarajio mazuri ya biashara hii yaliwahimiza Wafaransa kujaribu kuanzisha mashamba yaliyoendeshwa na Wazungu katika mto Senegal, lakini jaribio hili lilishindikana kutokana na mchanganyiko wa sababu, miongoni mwao zikiwemo: Makosa ya kiufundi, upungufu wa nguvukazi, upinzani kutoka kwa wafanyabiashara, na chuki kutoka kwa majirani zao wa Kiafrika. Wakati huo huo, wasiwasi ulianza kukua kati ya jamii ya kifalme ya Wolof huko Waalo na umma wa Kiislamu. Hili lilitokea wakati jamii yenyewe ya kifalme ikikabiliwa na mgogoro wa urithi. Jambo hili, miongoni mwa mambo mengine, liliwapatia wapinzani wa Kiislamu fursa ya kuishinda nchi na kuangamiza mfumo wa jadi. Hata hivyo, Wafaransa waliingilia kati katika siasa ya ndani ya Waalo na kumshinda kiongozi wa upinzani wa Waislamu. Baada ya kushindwa kwa jitihada nyingi za wenyeji za kurudisha amani nchini, Ufaransa hatimaye iliitwaa Waalo mwaka 1855. Waliigawanya nchi katika majimbo matano na, licha ya kupata upinzani mkali kutoka kwa wenyeji, waliweza kuweka utawala thabiti kuanzia 1855 hadi 1880.

Huko Kayor, mfumuko wa Uislamu katika karne ya kumi na tisa ulitishia mamlaka ya jadi. Ili kuleta umoja wa kitaifa katikati ya vurugu hii, mtawala, Laat Joor, alisilimu. Hii ilileteleza kuenea kwa kikundi cha Tijaniyya nchini, ambapo awali nchi hiyo ilikuwa na kikundi cha Kadiriyya pekee. Mfarakano wa vikundi hivi vya Kiislamu ulisababisha kuenea kwa murabati kama viongozi wa jumuiya hizi, hali ambayo iliubainisha wazi ukanda huu wakati wa ukoloni, na baadaye kuwa kielezo cha upinzani wa Waafrika dhidi ya utawala wa Wazungu. Ili kuleta umoja miongoni mwa watawala na watawaliwa, Laat Joor alianza jitihada za kusilimisha nchi yote. Pia alipaswa kupambana na kuenea kwa ubeberu wa Kifaransa. Kifo chake mnamo mwaka 1886, baada ya vita virefu vya msituni, kilihitimisha ufalme huo na kushuhudia kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni huko Kayor.

Historia ya Jolof iliunganishwa na ile ya Kayor. Jolof haikukabili shinikizo la Wazungu moja kwa moja kwa vile ilikuwa maskini na ilikuwa imetengwa huko bara lakini ilikabiliana na mfumko wa Uislamu. Mtawala wa Jolof, Albrury Njay, hatimaye alilazimika kupambana na ubeberu wa Wazungu. Akiwa pamoja na Ahmadu wa Segu, mtoto wa al-Haji Umar, alipinga shinikizo la ukoloni hadi alipofariki huko Sokoto mwaka 1900.

Nchi ya Siin ilikuwa imara zaidi kwa vile haikuguswa na Uislamu hadi wakati wa utawala wa Wafaransa. Hali hii pia iliifanya kuwa ya watu wa aina moja. Watu walioishi humo, Wasereer, walikuwa na uchumi uliochanganya kilimo na ufugaji, katika mfumo wa kijamii uliofanana sana na ule wa Wawolof.

Nchi ya Salum ilikuwa na nguvu zaidi kuliko Siin lakini ilikosa umoja. Ilijipanua kijeshi hadi kufikia Gambia katika karne ya kumi na nane. Waislamu walikuwa wachache zaidi na wamisionari Wakatoliki walijitokeza mapema mnamo mwaka 1849.

Ingawa Waislamu walikuwa wachache huko Salum, lakini walikuwa wachokozi sana. Utawala wa jadi ulijikuta katika hali ngumu, ukiwa umebanwa kati ya matakwa ya Wazungu na waasi wa Kiislamu ambao waliwaongoza wakulima na watu wa makabila madogo kupinga utawala huo. Nguvu za Tijaniyya pia ziliongeza wasiwasi uliokuwepo. Hatimaye, Salum ilishambuliwa na murabiti wa Tukuloor, Maba (mfuasi wa al-Haji Umar wa Tijaniyya), ambaye aliupindua utaratibu wa zamani na kuanzisha utawala wake. Hata hivyo aliuawa mwaka 1871 wakati wa harakati za kupambana na Waareer wa Siin. Kufuatia kifo chake; himaya yake ilidhoofika kutokana na mgogoro wa kugombea urithi. Hivyo ilikuwa rahisi kwa Wafaransa kuukalia ukanda huo mwaka 1887.

## *Upper Guinea na Futa Jallon*

Upper Guinea, ambayo pia inajumuisha Guinea Bissau, Sierra-Leone na Liberia, ilikuwa moja ya vituo vya mwanzoni kabisa vya athari za Wazungu katika ukanda huo. Hii ilitokana na umuhimu wa biashara ya watumwa katika karne ya kumi na sita, ijapokuwa biashara hiyo ilipungua katika karne ya kumi na nane. Isipokuwa kwa eneo la pwani lililokaliwa na Wajuula, vikundi muhimu zaidi katika eneo la Upper Volta vilikuwa ni Waalinke na Wafulbe.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, wakati athari za Wareno zilikuwa zinadidimia katika eneo hilo, biashara ya watumwa ambayo wakati huo ilikuwa imeshapigwa marufuku, iliendelea kwa muda zaidi. Katika kipindi hiki, himaya ya Wamalinke wa Kaabu ilikuwa na matatizo ya kuwadhibiti vibaraka wake wachache kama vile Wabainuk. Wakati huo huo, Wafulbe wa huko Kaabu, ambao walikuwa wachache, walikuwa wanazidi kukosa subira kutokana na hali yao ya kutawaliwa katika jamii. Huko Mashariki, Wafulbe wa Futa Jallon waliwatawala Wamandinka hadi kufikia mto Gambia huko Kantora. Pia wakati huu, Wafaransa walikuwa wanaanzisha vituo vya biashara katika eneo hilo na matokeo yake ni kwamba biashara ya njugu ilikua haraka sana.

Utaratibu wa utawala ulioelezewa hapo juu ulipinduliwa katika mfululizo wa matukio ambayo yanaweza kukadiriwa kuwepo tangu 1859 wakati Wafulbe wa Futa Jallon walipoanza pambano la makataa dhidi ya Kaabu. Matokeo ya pambano hili yalikuwa kifo cha mfalme wa Kaabu na kuporomoka kwa himaya yake. Kuporomoka kwa himaya ya Kaabu kulikuwa na matokeo makubwa: Idadi ndogo ya Wafulbe katika himaya hiyo waliasi dhidi ya watawala wa Mandinka na maasi haya yalisambaa hadi kufikia ukingo wa mto Gambia; aidha waliuandaa ufalme wa Fuladugu ambao uliendelea kuwa tishio kwa Mandinka. Miaka michache iliyofuata ilishuhudia Wamandinka wakijaribu kujijenga upya chini ya viongozi wapya.

Kwanza walijaribu kufidia hasara zao huku wakiongozwa na mtu mmoja aliyejulikana kama Sunkari Kamara. Upinzani wake dhidi ya biashara ulilazimisha Wafaransa kupingana naye, na baada ya harakati zisizokuwa na mafanikio yoyote, amali yake ilifika ukingoni mnamo 1882. Kiongozi mwingine, Fode Kaba Dumbuya, alijaribu

kuiunda upya jamii ya Wamandinka kandokando ya mto Gambia mwaka 1875, lakini alirudishwa nyuma na kufukuzwa kutoka eneo hilo na Wafulbe. Hata hivyo, chini ya viongozi hawa wawili, Sunkari na Dumbaya, Wamandinka waliweza sio tu kupinga Wafaransa na Wafulbe katika Kasamansi, lakini pia kuhifadhi utambulisho wa asili wa kabila lao kwa kuingia Uislamu kwa idadi kubwa.

Historia ya eneo lililotanda kati ya Gambia na Sierra-Leone kuanzia karne ya kumi na nane ilitawaliwa na maendeleo ya dola lenye nguvu la Kifulbe huko Futa Jallon. Kukua kwa taifa hili kulikuwa ni kichocheo kikuu kwa biashara ya masafa marefu kutoka bara la Sudan hadi pwani ambako iliunganishwa na ile ya Wazungu. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, biashara ya watumwa iliendelezwa kwa siri katika vituo vya biashara vya Wazungu hadi katikati ya karne. Kung'ang'aniwa kwa biashara ya watumwa katika eneo hili kulisadiwa na kuwapo kwa maezi na vighuba vingi vyenye kina, na ujirani wa Futa Jallon, ambayo ilivamia sehemu nyingi kutafuta watumwa, na kisha kuwaleta hapa kwa ajili ya kusafirishwa nje kibiashara.

Huko Futa Jallon, jamii ilionekana tulivu kwa kiasi fulani mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Baada ya vita vitakatifu vya karne iliyotangulia, washindi walishaanzisha uongozi wa kikabaila katika jamii iliyokuwa haipendi mabadiliko na iliyokuwa na matabaka mengi. Majimbo yaliyokuwa huru na parishi ambazo ziliunda nchi hiyo zilitawaliwa kutoka makao makuu huko Timbo na tabaka la makabaila ambalo lilikalia daraja la juu la muundo wa jamii. Chini yao kulikuwepo raia wao, Wajallonke, ambao walikandamizwa sana kiasi cha kupoteza lugha yao. Watu hawa, ambao waliunda robo tatu ya umma wote, walinyonywa vikali na shughuli zao zilisimamiwa kwa karibu sana.

Kati ya tabaka la juu na la chini kulikuwepo na kundi jingine la watu. Hawa walikuwa ni wa koo za kimaskini za Wafulbe ambao hawakuweza kuteka ardhi yoyote wala nyara za kutosha kwenye vita vile. Hata hivyo, licha ya kutokubadilika, na ukandamizaji ambao uliiainisha jamii ya Kifuta, kulikuwepo na utamaduni wa Kiislamu wa hali ya juu katika Futa Jallon. Utamaduni huo ulifuatana na matumizi ya mara kwa mara ya lugha ya Kifulani katika maandishi. Kwa upande wa dini, Wafulbe na Wafuta Jallon hawakuhodhi mamlaka yote. Walikabidhi dhima ya heshima kuu kwa watu wa nje kama vile Wajaksaanke ambao waliwapendelea kutokana na kutofungamana kisiasa. Kwanza kabisa Wajaksaanke walikuwa ni watu wa dini, lakini pia walikuwa wafanyabiashara wa masafa ya mbali.

Nguvu za Wafulbe na Wafuta Jallon zilikuwa katika jeshi ambalo nguvu zake zilitegemea umoja wa dola ambalo lilidhoofishwa na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Ijapokuwa hali hii ilikuwepo, umoja wa ufalme ulidumishwa na seti ya kanuni ambazo zilidhibiti kiwango cha machafuko ya kisiasa nchini. Kanuni hizi ziliruhusu mzunguko wa uongozi wa dola kati ya familia/vyama viwili vilivyopingana - Alfaya na Soriya, katika mji mkuu wa Timbo. Kutokana na mgawanyiko huu wa ndani, Wafulbe na Wafuta Jallon hawakuweza kufuata sera zozote za uchokozi za upanuzi. Matokeo yake ni kwamba majirani zao kama vile Wajallonke waliweza kuanzisha madola yenye nguvu ya kutosha kama vile Tamba na Solimana ambayo yaliziba baadhi ya njia za biashara zilizokuwa zinatumiwa na Wafulbe.

Ni huko Labe pekee, jimbo mojawapo Futa Jallon, ambako kulikuwa na kiwango fulani cha upanuzi kuelekea kaskazini katika himaya Kimandinka ya Kaabu.

Lakini wakati Labe ilipokuwa inaendelea huko kaskazini, vita vikali vya wenyewe kwa wenyewe vilikuwa vinaendelea huko Futa Jallon. Hivi vilipamba moto mwaka 1844, wakati al-Haji Umar alipoanza kuishi Jugunku katika mipaka ya Futa Jallon baada ya kurejea kutoka hija. Hatimaye amani ilirejeshwa wakati viongozi wa Futa walipokabiliwa na maasi ya Wahubbu na kuamua kusawazisha tofauti zao na kushirikiana kumkabili adui yao wa pamoja.

Wahubbu walikuwa ni kundi la watu wachache wa Kadiriyya wenye siasa kali ambao walipinga vikali Watijaniyya na ukoo wa kikabaila wa Kifulbe. Walijumuisha wakulima wa Kifulbe, watwana wenye asili ya Jallonke, na watumwa wapya walioingizwa nchini. Mwanzoni harakati zao zilizimwa wakati zilipolipuka kila mahali huko Futa mwaka 1849. Lakini waasi walikimbilia katika maeneo ya pembezoni na kujichimbia huko Fitaba chini ya uongozi wa mtu aliyejulikana kama Jue na mtoto wake Abal, na kutoka huko wakawa tishio kubwa kwa watawala wa Futa. Wahubbu walikuwa wapiganaji wa hali ya juu, na Bokatto, ngome yao, haikuweza kupenywa na watawala wa Futa. Mara mbili Wahubbu waliuchoma moto Timbo, mji mkuu wa Wafuta. Hatimaye Wafulbe walilazimika kuomba msaada dhidi yao kutoka kwa Samori. Urafiki wao na Samori, mbali na kupunguza tishio la Wahubbu, pia ulionyesha kuwa na manufaa kwa Wafulbe wa Futa Jallon ambao walimwuzia mifugo kwa kubadilishana na watumwa. Wakati huohuo, Futa Jallon ilibakia imegawanyika kutokana na migogoro ya ndani.

Kama ilivyoelezwa mwanzoni, kukua kwa Futa Jallon kuliifungulia biashara ya Sudani njia pana ya kufika pwani ya bahari. Kwa maneno mengine, athari za Wasudani zilipenya hadi pwani na kimsingi zilibadilisha utamaduni wa wakazi wa pwani, hasa kwa vile wengi wao walilazimika kukubali mamlaka ya kisiasa ya Futa Jallon. Eneo ambalo leo linajulikana kama Guinea Bisau lilikuwa chini ya Wafulbe wa Futa Jallon; vivyo hivyo ilikuwa kwa Wasusu na Walanduman wa Boke ambao walipinga mamlaka ya Wafulbe bila mafanikio. Uislamu uliingia Kwa Wasusu pamoja na utawala wa kisiasa wa Futa Jallon, na utamaduni wao uligeuzwa kuwa wa Kisudani kwa kiasi kikubwa hadi kipindi cha ukoloni. Hata hivyo, Wabeafade wa Guinea Bisau na Wanalu wa Rio Nunez walikwepa athari za Wafulbe kutokana na mazingira ya kinamasi, na kutopendelea kwao kushiriki katika biashara ya masafa ya mbali.

Hivyo, japo mamlaka ya siasa ya Futa hayakuenea hadi baharini, lakini athari za Sudani zilishamiri sana katika eneo hilo kutokana na mahusiano ya kibiashara.

Kuwasili kwa wafanyabiashara wa Kisudani katika pwani kimsingi kulibadilisha tamaduni za wakazi wa pwani kusini mwa nchi ya Wasusu na katika maeneo ya Walimba, Waloko na Watemne. Vikundi vya koo za Kimandinka na Kifulbe vililowea sehemu nyingi huko pwani, vikalitawala kisiasa na kuingiza mawazo mapya ya kisiasa katika eneo hilo. Matokeo yalikuwa kwamba jamii zilizopenda usawa na ambazo hazikuwa na matabaka sasa ziligeuzwa kuwa tawala za kivita na dola zilizokuwa nusu unganifu. Hata hivyo, watu hawa wa pwani walibakisha utambulisho wao na utamaduni kwa kuwasimilisha wageni wachache waliofika kwao katika lugha yao. Moja ya athari za

kijamii za kuwepo kwa Wasudani huko pwani ni kuanzishwa kwa miundo ya kisiasa-jamii ambayo ilivuka mipaka ya mifumo ya kisiasa iliyokuwepo na kupanuka hadi nchi za msituni za huko kusini, kupita mipaka ya biashara za Wasudani katika maeneo yaliyotajwa hapo mwanzoni. Kwa mfano, vyama vya siri kama vile Poro, vilienea kwa wingi miongoni mwa watu wa pwani kuanzia Watemne hadi Wakpelle wa Liberia.

Historia ya nchi za msituni za kusini katika karne ya kumi na tisa inaainishwa na kusambaa kwa watu kuelekea pande mbalimbali na kukua kwa biashara. Katika nusu ya kwanza ya karne, Watemne walikuwa wanapambana kulinda eneo lao dhidi ya uvamizi wa ghafla wa Wasusu na Wakpa-Mende, waliokuwa wanasambaa kuelekea upande wao. Katikati ya karne, mtandao wa biashara uioendeshwa na Wakrioli wa Sierra Leone ulipenya ndani na hivyo kuingiza ukanda huo katika soko la dunia. Wakati huo huo Wamende waliokuwa wanaishi kusini mwa Watemne walikuwa nao wanasambaa. Waliunda falme kuu za kivita ambamo wanawake walipewa nyadhifa muhimu za uongozi. Kupanuka kwao kulitenganisha jamii mbili za Wamande wa kusini zilizaohusiana sana, yaani Wakono na Wavai.

Wavai walidumisha tawala kubwa za wastani, na walikuwa na dhima muhimu katika ukuaji wa biashara ya watumwa ambayo ililiainisha eneo hilo katika karne za kumi na nane na kumi na tisa. Mahusiano haya ya nje yalisababisha utamaduni wa Wavai ubadilike sana na kuibua ari yao ya ubunifu. Katika mwaka 1818, Wavai walibuni maandishi yao wenyewe. Wagola walikuwa kundi jingine kutoka bara ambalo lilianzisha mpango wa nguvu wa kupanuka katika karne ya kumi na nane. Walijipenyeza dhidi ya makundi mengine kama vile Wavai, Wade, na Wakpelle walipokuwa wakielekea baharini. Kusini zaidi kulikuwepo na mto Saint Paul ambao unaunga pwani ya Monrovia na mpaka wa falme za Konyan, na kubainisha mpaka wa dunia ya Wasudani wa Mandinka. Katika kingo za mto huu kulikuwepo na njia pekee kati ya savana na bahari ambayo ilibainisha eneo la Wavai na eneo la baadaye la Monrovia.

## *Jumuiya za Wakru*

Wakru walikalia ukanda wa pwani uliotandaa kuanzia Monrovia hadi Bandama. Walikuwa wakulima wa msituni na wawindaji, lakini muhimu zaidi walijulikana zaidi kama mabaharia. Katika karne ya kumi na tisa, hakukuwepo na kiungo kati ya bahari na savana iliyo magharibi ya Bandama. Hii ni kwa sababu bonde lililokuwepo kati ya bahari na savana lilikuwa limefungwa na Wabaule kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, na pia kwa kuwa mito ya eneo hilo haikufaa kuabiria. Kwa hali hiyo, hakukuwepo na dola unganifu wala biashara ya masafa ya mbali katika eneo hilo. Hata hivyo kulikuwepo na biashara ya kupokezana ambayo ilipitisha bidhaa kutoka kundi moja hadi jingine. Kwa hivyo historia ya eneo hilo ni ya vikundi vidogovidogo vilivyoathiriana, na mahusiano yao na dunia ya nje. Ijapokuwa Wakru walikuwa na lugha moja bado waliweza kugawanywa katika jumuiya zenye kukaribiana, ambazo nazo ziliweza kuwekwa katika makundi mawili makubwa: Wabete-Dida waliokuwa mashariki ya Mto Sassandra, na Wabakwe waliokuwa magharibi, ambamo walifahamika zaidi.

Mabadiliko kadhaa muhimu yalitokea kwenye eneo hilo katika karne ya kumi na tisa.



24.2 *Wapga makasia wa kru*



24.3 *nyumba za wakru*

Mguro wa baadi ya koo za Wakru kutoka mashariki kwenda magharibi, ambao ulikuwa ukiendelea kwa karne nyingi huko bara, ulisitishwa katikati ya karne wakati walipokutana na vikundi vingine vyenye nguvu zaidi. Maendeleo mengine muhimu yalikuwa ni kujumuishwa kwa wakulima wadogo na mabaharia katika baadhi ya jumuiya za Wakru. Kabla ya karne ya kumi na tisa, kulikuwa na tofauti ya muda mrefu kati ya wakulima na mabaharia. Lakini jinsi wakulima walivyozidi kushiriki katika biashara ya watumwa ndivyo walivyozidi kujiweka karibu na mabaharia, na kwa njia hiyo kusababisha kuchanganyika kwa vikundi hivyo viwili.

Uhusiano maalumu pia uliundwakati ya vikundi kadhaa vya Wakru na Sierra Leone. Hii ni kwa kuwa wafanyabiashara wa Kizungu ambao waliitumia Ghuba ya Guinea katika biashara ya siri ya watumwa na katika biashara halali, waliwatumia mabaharia wa Ki-kru kama wakalimani wao. Matokeo yake ni kwamba Wakru walijijenga kwa idadi kubwa huko Freetown na baadaye huko Monrovia kama vibarua na watema kuni. Waliendelea na mshikamano wao, lakini pia walichukua nduni kadha za utamaduni wa Wakrioli. Athari za Uprotestanti kwa Wakru, kutoka Sierra Leone na Liberia, kwa hakika zilichangia katika kuzuka kwa Ufalme wa Grebo ulioiga muundo wa shirikisho la Wafante la 1871 huko Gold Coast, na katika kuleta mwamko wa kitaifa na lugha ya maandishi. Utaifa huu wa Grebo ulitoa usuli kwa amali ya baadaye ya Nabii Harris huko Cote d'Ivoire.

Jinsi wakati ulivyopita, jumuiya ya zamani ya wavuvi wa pwani ilizidi kuwekwa chini ya athari ya shughuli za Wazungu. Baada ya 1821, ukanda wa pwani uliingia kwa kiasi fulani chini ya mamlaka ya serikali ya Liberia. Mpaka wa Sassandra ulibakia imara katika nchi ya Wakru, lakini mbele zaidi, mikusanyiko ya watu wengine ilipatikana katika nchi ya Wakru miongoni mwa Wabete wa Gagnoa na baadhi ya Wadida. Biashara

ya Wazungu ilikuwa inaenea na iliathiri utamaduni wa baadhi ya vikundi kwenye mdomo wa mto Sassandra. Hata hivyo, katika kipindi chote hiki, mikoa ya pwani iliishi kwa wasiwasi na ilikuwa na milipuko mingi ya mapambano.

## *Dunia ya Mande ya kusini*

Wamande wa kusini waliishi katika nchi iliyokuwa kati ya savana za Guinea na watu wa pwani. Vikundi muhimu vya Wamande wa kusini vilikuwa ni Wamande, Watoma, Wakpelle, Wadan na Wakwenu. Walikuwa na tabia nyingi zilizofanana na zile za watu wa pwani kwenye mito. Kwa mfano, hawakuwa na miundo ya dola unganifu bali walikuwa na vyama vingi vya kumbi za siri. Hivyo, ingawa historia ya Wamande wa kusini haiwezi ikatenganishwa na ile ya watu wa pwani waliochanganyika nao mara kwa mara, ilikuwa pia imeingiliana na ile ya Wamandika wa kusini, watu wa Kisudani ambao athari yao katika eneo hilo ilianza tokea kuporomoka kwa himaya ya zamani ya Mali.

Wamandinka wa kusini walikalia eneo la Niger ya Juu kutoka mpaka wa Futa Jallon hadi mto Bandama.

Hadi ilipofikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, tayari walikuwa wameshaanzisha mtandao wa biashara ya masafa ya mbali ambao ulisafirisha kola za msitu wa kusini kuelekea Niger. Wamandinka wa kusini walikuwa ni jumuiya ya jadi iliyotawaliwa na makabaila wa kivita. Uislamu ulifuatwa na watu wachache waliohusiana na mtandao huo wa biashara. Hata hivyo, mtandao huo wa biashara haukuungana na bahari. Nchi ya Wamandinka wa kusini kwa hiyo ilikuwa ni kama mwisho wa njia kwa vile kijadi walijihusishsa zaidi na Niger na Sudan ambako mababu zao walitokea.

Magharibi ya mbali zaidi ya ukanda huu, kulikuwa na kijiji cha Kankan ambacho kilikuwa tayari ni kituo muhimu cha kibiashara katika karne ya kumi na nane, kikijinufaisha kwa kutumia upenyo wa Futa Jallon kuelekea baharini. Hiki kilikuwa ni kituo cha Wamandinka, ambao utamaduni wao ulienea katika dunia ya Wajuula, ambao walikuwa wafanyabiashara wa masafa ya mbali. Kankan ilitawaliwa na Wakaba ambao walikuwa familia ya wanasiasa, wanadini na wafanyabiashara. Baada ya Wakaba kusilimishwa na al-Haji Umar kati ya 1845 na 1850, walianzisha kampeni zisizofanikiwa za kueneza mamlaka yao juu ya majirani zao waliokuwa wanajadi. Hali hii ilisababisha mlolongo wa matukio ambayo hatimaye yalivuruga utaratibu wa zamani uliokuweko miongoni mwa Wamandinka wa kusini.

Vurugu hii inaweza kuelezwa kwa kuangalia kuongezeka kwa umuhimu wa wafanyabiashara wa Kiislamu kutokana na kufunguliwa kwa njia nyingi kuanzia karne ya kumi na saba. Zaidi ya hayo, kikundi hiki cha Waislamu wachache, kilizidi kupata taarifa nyingi kuhusu vita vitakatifu na tawala za Kiislamu za Kaskazini. Kwa hali hiyo ilifikia wakati ambapo Wajuula na vikundi hivi vya Kiislamu hawakuweza tena kuendelea kukubaliana na nafasi duni walizopewa na watawala ambao waling'ang'ania ujadi na kukataa mageuzi. Jambo hili lilisababisha mfululizo wa migogoro ya kijanibu katika ukanda huo, ikianzia kwenye maasi ya Moriule Sise mwaka 1835. Migogoro hii ilihusiana kwa namna fulani na Uislamu na dunia ya biashara, lakini haikuleta matokeo

yaliyotarajiwa ya kuwakomboa Waislamu wa Juula. Hata hivyo, ilidhihirisha kuwa Wajuula hawakukubali tena nafasi duni waliyopewa kijadi na kwamba walikuwa na uwezo wa kuvuruga jamii yote (katika kudai haki yao).

Hii ndiyo hali iliyokuwepo wakati Samori Ture alipojitokeza katikati ya karne ya kumi na tisa. Akiwa amezaliwa 1830 miongoni mwa watu waliofuata jadi, Samori alijiingiza mapema katika biashara ili kuepuka mamlaka ya baba yake. Mwaka 1848 aliingia uaskari ili kusaidia kumwokoa mama yake aliyekuwa ametekwa vitani. Uwezo wa pekee aliouonyesha ulimpatia marafiki na maadui hadi alipoamua mnamo 1861 kuunda jeshi na kuanza amali yake mwenyewe ya kijeshi. Kwanza aliungwa mkono na wanajadi wa Toron ya chini, watu wa upande wa mama yake, kabla hajaendelea kushinda maeneo mengine. Kati ya 1871 na 1881 aliliingiza eneo kubwa lililokuwa limekaliwa na Wamandinka chini ya utawala wake. Mtindo wake wa uongozi na mabadiliko aliyoiletea jamii ya Wamandinka kwa kumaliza migogoro ya ndani, kufungua njia za biashara ambazo zilikuwa zimezuiwa wakati wa maasi yaliyotangulia na kuwakomboa Waislamu wa jamii ya Wajuula bila ya kuwatia utumwani wanajadi, ulimletea wafuasi wengi kutoka pande zote.

Himaya ya kwanza ya Samori ilikuwa ni utawala wa kijeshi ulioingilia nchi nyingine na kubadilisha jamii ya Wamandinka bila kuiangamiza. Wafanyabiashara wa Kiislamu walipewa nafasi muhimu zaidi, na wanajadi walibakia na uhuru wao. Pamoja na hali hiyo, himaya ya Samori haiwezi ikaitwaa nchi ya Kiislamu ijapokuwa ilitawaliwa na tabaka la wanajeshi waliosilimishwa. Hii ni kwa sababu Samori hakuwa Shehe aliyeelimika katika Kiarabu au kubobea katika utamaduni wa Kiislamu. Mara nyingi alikopa mifano ya Wafulbe na Watukuloor, lakini hakuipa dini nafasi ya kwanza katika uongozi wake wa nchi. Alizingatia hali halisi katika kulikabili tatizo la Mandinka. Katika miaka ishirini, alifanikiwa kuipa jamii yake uwiano mpya ambao uliwapendelea Wajuula na hivyo kusuluhisha migogoro iliyoikumba jamii yake kwa nusu karne. Hivi ndivyo ilivyokuwa hali ya Wamande wa kusini wakati Wafaransa walipoishambulia miaka ya 1880.

## *Hitimisho*

Kuingia kwa athari ya Wazungu ndio kipengee pekee kilichouhusisha ukanda mzima unaojadiliwa. Athari ya Wazungu ilikuwa madhubuti sana huko pwani ambako biashara ya watumwa iliendelea kiharamu hadi katikati ya karne ya kumi na tisa. Kubadilishwa kwa bidhaa mpya za Kiafrika kama vile mawese na njugu bidhaa za kizungu kuliliingiza zaidi eneo la pwani katika soko la dunia. Ijapokuwa athari hizi zilikuwa dhaifu zaidi huko bara ambako mila za Wasudani na za Kiislamu zilishamiri zaidi, maasi ya Juula yanaweza kuelezwa kama tokeo la kukua kwa biashara hii na ulimwengu wa nje. Himaya ya Samori, kwa hiyo, inaweza ikaitwa, kwa kiasi fulani, jibu la athari za ulimwengu wa nje kwa jamii yake. Wakati huo huo, alikuwa pia ameathiriwa waziwazi na mifano ya wanamapinduzi wa Kiislamu wa Sudani.

# 25

# Nchi na watu wa mzingo wa Niger na Volta

## *Utangulizi*

Nchi za bonde la Volta na mzingo wa Niger zilikuwa kitovu cha mfumo wa siasa ulioenea hadi nje ya ukanda huo katika karne ya kumi na nane, kwa kujaza ombwe lililosababishwa na kuanguka kwa Gao katika karne ya kumi na sita, na kujinufaisha kutokana na hali mpya za kiuchumi na kisiasa zilizojitokeza huko Gold Coast kutokana na biashara ya watumwa na kuzuka kwa miliki ya Asante. Hata hivyo, katika karne ya kumi na tisa, nguvu mpya zilileteleza kuanguka kwa falme kuu na kusababisha vikundi vidogovidogo visivyokuwa na tawala unganifu kuhama. Hivyo karne ya kumi na tisa katika ukanda huo kilikuwa ni kipindi cha mabadiliko makubwa.

Kwanza kabisa, kulikuwepo na misukosuko mikubwa ya kisiasa na ya kiasasi. Himaya kubwa kama vile Asante na Kong, na Mossi na Bambara, zilianguka kutokana na mchanganyiko wa mivutano ya ndani na shinikizo kutoka nje. Mambo haya yalichochea miguro ya watu, hasa kutoka vikundi visivyokuwa na tawala unganifu; baadhi ya watu hao walisambaa kwenye maeneo mapana sana. Kulikuwepo pia na mabadiliko dhahiri katika mwenendo, bidhaa na masharti ya biashara ambayo mara nyingi yalikuwa ni matokeo au sababu za mabadiliko ya kisiasa. Mabadiliko haya yaliashiria mwisho wa enzi moja na mwanzo wa enzi nyingine, yaani mwisho wa kipindi cha biashara ya watumwa na mwanzo wa kipindi cha ukoloni. Ukristo na Uislamu navyo vilienea sana. Kuenea kwa Ukristo kulisuhulishwa na kukua kwa athari za Kizungu, ilhali Uislamu uliendelezwa na utawala wa Kiislamu ulioenea katika Sahel. Maendeleo yote haya yaliudhoofisha ukanda huu na kuwawezesha Wazungu kushinda na hivyo kuanzisha utawala wa kikoloni.

## *Mfumo wa Asante: Kukua na kuanguka kwake*

Himaya ya Asante iliyoanzishwa katika karne ya kumi na nane, na ambayo kitovu chake kilikuwa Kumasi, ilichipuza mfumo unganifu sana wa kisiasa, ambao umoja wake wa kisiasa na kiroho uliwakilishwa na asasi ya Kigoda cha Dhahabu. Himaya hii ilikuwa na nguvu nyingi za kiuchumi na kisiasa, sio tu katika falme tegemezi za kaskazini, bali pia katika tawala za kichifu za Fante zilizojitegemea, na katika madola mengine ya pwani.




**25.1** *Afrika Magharibi: Madola na makabila ya mzingo wa Mto Niger na Mto Volta imetayarishwa na K. Arhin)*



**25.2** *Kigoda cha Dhahabu cha Asante*

Kwenye kitovu cha himaya hiyo kulikuweko makundi yaliyohusiana na ukoo wa Oyoko wa Kumasi uliochipuza mfumo ungamfu wa kifalme. Falme za jirani za Akan, kama vile Mampong, Nsuta, Dwaben, Bekwai n.k. pamoja na falme za kaskazini za Gyaman, Gonja, Dagomba na Mamprusi ziliunganishwa katika himaya hiyo. Mfalme wa Kumasi alikuwa ndiye Asantehene (maliki mkuu) na aliitawala himaya nzima kutokea hapo.

Chini ya Asantehene Osei Bonsu (1801-24), Asante ilijipanua kwa nguvu kuelekea pwani katika jitihada kubwa za kuimarisha udhibiti wa uchumi dhidi ya upinzani wa watu walioishi katika ukanda wa pwani. Hata hivyo, mwaka 1826 Waasante walishindwa na muungano wa madola ya Fante yaliyoundwa kwa udhamini na msaada wa Waingereza. Hii iliashiria mwanzo wa kudidimia kwa himaya ya Asante.

Katika kilele cha nguvu zake mwanzoni mwa karne ya tisa, himaya ya Asante ilijumuisha aina tatu tofauti za nchi. Aina ya kwanza ilikuwa ni kundi la kati la tawala za kichifu za Asante. Kundi hili lililokuwa chini ya mamlaka ya Asantehene, liliunganishwa na lugha na utamaduni unaofanana, mtandao wa mahusiano ya kiukoo, karne nzima ya shughuli za pamoja za kijeshi, na fahari juu ya mafanikio yao ya pekee. Kigoda cha Dhahabu kilikuwa ni kielelezo cha umoja wa taifa. Aina ya pili ilikuwa ni kundi la nchi jirani za Akan. Nchi hizi ziliukubali ukuu wa Kigoda cha Dhahabu pamoja na asasi nyingine za Asante, na watu wake waliishi kama Waasante chini ya utawala wa Asantehene. Aina ya tatu ni kundi la madola yaliyokuwa mbali kijiografia na kiutamaduni, kama vile Dagomba, Mamprusi na Gonja. Mchango wao mkubwa katika himaya hiyo ulikuwa katika maendeleo ya uchumi wa Kumasi, hasa kwa kulipa ushuru kwa njia ya fedha taslimu au mali.

Hata hivyo ni bora kutilia maanani kwamba mwainisho huu haukuwa dhahiri kama unavyoonyeshwa hapa. Athari za Asante katika mikoa hii hazikuwa imara sana na mara nyingi zilitegemea hali halisi iliyokuwepo ndani ya maeneo hayo kwa kipindi kinachohusika. Kwa mfano, kujishughulisha kwa Asante na madola ya kati ya Akan hakukuwa kwa sababu za kisiasa tu, bali pia za kiuchumi. Halikadhalika, nchi za kaskazini zisizokuwa za Akan zilikaliwa kijeshi na kisiasa kwa lengo la kutaka kunyonya rasilimali zao za kiuchumi.

Kuanzia mwaka 1826 hadi 1874 mielekeo mitatu muhimu ilijitokeza katika ukanda wa Gold Coast. Kwanza kabisa ni jitihada za Waingereza kuanzisha utawala usio rasmi juu ya wakazi wa pwani. Pili ni jitihada za watu wa pwani kujipangilia upya ili kulinda uhuru wao dhidi ya matishio mawili: la Waingereza na la Waasante. Tatu ni jitihada za Waasante zilizokuwa zinaendelea, japo bila mafanikio, za kudumisha utawala wao kama ulivyokuwa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa.

Jitihada za Waingereza kuanzisha uongozi usio rasmi huko Gold Coast zilipata ushindi mkubwa chini ya Gavana George Maclean (1830-43). Madhumuni yake yalikuwa ni kuzuia upanuzi wa Waasante na kutumia tishio la Waasante kuwalazimisha wakazi wa pwani kukubali kwa hiari udhibiti wa Waingereza. Akiwa na malengo haya, alianzisha mkataba wa makundi matatu ya Wafante, Waasante na Waingereza, ambao wote kwa pamoja walitambua kujitawala wenyewe kwa jumuiya za pwani kusini mwa mto Pra, walikubali kuweka wazi njia za biashara, na pia kuahidi kupeleka mizozo yote

kwa Waingereza ili kupatiwa ulumbuzi. Mfumo huu wa mkataba uliwekwa katika muundo wa kiasasi mwaka 1843 wakati serikali ya Uingereza ilipochukua uongozi wa moja kwa moja wa ngome za pwani kutoka mikononi mwa makampuni ya biashara, na kumweka Gavana kuendesha ngome hizo akiwa na mamlaka ya kuanzisha baraza la kutawala na la kutunga sheria kwa jamii za jirani.

Wafante na watu wengine wa pwani walifanya bidii nyingi kudumisha uhuru wao kutokana na uvamizi wa Wazungu pamoja na tishio la kutawaliwa na Waasante. Waliwalalamikia Waingereza dhidi ya kuingiliwa kwa utawala wao, na kuanza majaribio kadhaa ya kuanzisha asasi unganifu zaidi za kisiasa ambazo zingewahakikisha uhuru wao vizuri zaidi. Hususani, machifu wa Fante, na wajumbe kutoka maeneo ya Denkyira, Wassa, Twifu na Assin yaliyoko upande wa magharibi wa pwani, waliunda Shirikisho la Wafante mwaka 1868 huku wakiungwa mkono na kikundi cha wasomi kilichokuwa kinaibuka. Shirikisho hilo lilipewa katiba ya maandishi yenye kuainisha asasi za utawala, mahakama na ofisi za fedha. Waga na jamii nyingine za mashariki vilevile walijaribu kuunda shirikisho, ijapokuwa shirikisho lao halikuwa rasmi sana. Hata hivyo, ilipofikia mwaka 1872, hata Shirikisho la Wafante lilikuwa linafifia hasa kutokana na chuki za Waingereza ambao walijitahidi sana kuwagawa machifu, na kuwanyamazisha na kuwakatisha tamaa wasomi Waafrika waliochochea uundaji wa Shirikisho, na ambao walitegemea biashara kati yao na Wazungu ili kuendesha maisha yao.

Hata hivyo, Shirikisho la Wafante lilikuwa na umuhimu mkubwa japo lilidumu kwa kipindi kifupi. Liliwakilisha jitihada za mwisho za watu wa pwani kupinga uvamizi wa wakoloni. Lilijaribu kufufua umoja wa Wafante ambao ulikuwa umeangamizwa na kuwepo kwa Wazungu katika eneo hilo. Pia lilitangulia kufanya yale ambayo yangefanywa na tabaka la wasomi katika historia ya baadaye ya Gold Coast, yaani kuwaongoza machifu wa jadi katika vuguvugu la utaifa. Hivyo Shirikisho hilo lilionyesha jinsi ambavyo shughuli za kikoloni zilikuwa zinajichimbia kaburi kwa kuwapatia wenyeji elimu ya magharibi, silaha muhimu ya Waafrika katika mapambano dhidi ya ukoloni.

Wakati huohuo, Asante ilikuwa inajaribu kutetea mamlaka yake huko pwani. Shambulio lake kwa Elmina mwaka 1872 liliwachokoza Waingereza na kuwafanya wapeleke msafara wa kijeshi kuishambulia Kumasi mwaka 1874. Kumasi ilitekwa na kuchomwa moto, na Asante ilitakiwa kukana haki zake zote juu ya Gold Coast, ambayo sasa iliwekwa rasmi chini ya utawala wa Waingereza. Jambo hili liliharakisha kuchanguka kwa ufalme wa Asante. Maasi ya Dwaben, mji shupavu miongoni mwa miji ya kati ya Asante, katika mwaka 1875, yalisababisha vurugu huko Kumasi na katika madola vibaraka ya upande wa kaskazini. Waingereza walitumia fursa ya mfarakano huo kuivamia Kumasi mwaka 1896, wakamkamata Asantehene na kumshawishi akimbilie uhamishoni.

## *Nchi za Mossi*

Falme za Mossi ambazo zilikua polepole na kupata umaarufu katika karne ya kumi na



**25.3** *Kitala cha Hazina, Kumasi 1817*



**25.4** *Wamossi waliovaa majuso; huenda ni "makuhani wa ardhi" waliowakilisha mamlaka za asili; picha ya Y, mwanzoni mwa karne ya ishirini.*

sita, na ambazo zilifikia kilele cha kukua kwake katika karne ya kumi na nane, ziliingia katika kipindi cha kuoza katika karne ya kumi na tisa. Kuoza huko kulikuwa ni matokeo ya matatizo ya ndani na ya nje katika nchi hiyo. Falme za Wagadugu na Yatenga ndizo ziliathirika zaidi na matatizo haya, ilhali ufalme wa Busama ulisitawi kwa kuwatumia majirani zake.

Ufalme wenye nguvu wa Wagadugu uliangamizwa katika vita ulivyopigana na Busuma na Lallè. Vita vya Busuma ambavyo vilichukua miaka kadhaa viliidhoofisha sana Wagadugu, wakati Busuma ilitumia fursa hiyo kupanuka kwa kuidhulumu Wagadugu na madola mengine madogo madogo katika ukanda huo. Vita vya Lallè vilianzishwa kwa tukio dogo la kipuuzi na hili linaonyesha kiwango cha kuoza cha mfumo wa Mossi wakati huo. Vita hivyo vilijikokota kwa zaidi ya miaka hamsini, na viliendelea kuvutia idadi kubwa ya washiriki hadi Wafaransa walipoichukua nchi hiyo.

Ijapokuwa Yatenga haikuwa na nguvu kama Wagadugu, ufalme huo pia ulikumbwa na uoza katika karne ya kumi na tisa. Tatizo la kwanza lilitokana na mpango wa Yatenga kutaka kupanua mipaka yake na kujumuisha vikundi vingine kama vile falme za Yako na Riziam. Vita vilivyopiganwa na Yatenga katika maeneo haya vilikuwa ghali sana kwa kuangalia idadi ya watu waliopoteza maisha yao na raslimali zilizotumika. Pili, tishio kutoka nje kwa Wajelgoji lilichokoza mfululizo wa mashambulizi kutoka kwa Yatenga ambayo pia yalikuwa aghali. Vita vya wenyewe kwa wenyewe visivyokwisha katika ufalme wa Yatenga vilifanya mambo kuzidi kuwa mabaya. Washindani walipokezana mara kwa mara kutawala, kila mmoja kwa wakati wake au hata kwa pamoja wakati mwingine. Kwa kweli, vita vya wanandugu baina ya vikundi vikuu viwili katika ufalme huo vilitoa fursa kwa Wafaransa kuwaingilia mwishoni mwa karne hiyo.

## *Nyanda za juu za magharibi na kusini za Volta*

Katika eneo hili, jumuiya zisizo unganifu za kimbari na kiukoo zilijaribu kukabiliana na misukosuko ya wakati huo. Watu hawa wasiokuwa na mifumo ya kisiasa ya kitawala msonge waliweza kukwepa machafuko ya karne ya kumi na tisa vizuri zaidi kuliko nchi zilizokuwa na serikali kuu. Kukosa kwao serikali kuu kulifidiwa na asasi zisizokuwa za kisiasa kama vile chama cha *Poro* cha Senufo. Kwa hivyo uzoefu wa vikundi vya Volta katika karne hiyo ulikuwa ni wa uvamizi, mashambulizi ya kujikinga, upinzani kwa wavamizi, kujitohoa kufuatana na mazingira, na kuoana kimseto. Wakati wakipinga majaribio ya vikundi vya Mande, Mossi, Zerma, Marka, na Fulbe kuwatawala, walizoea upesi kuwapo kwa watu hao na fursa za kiuchumi zilizoletwa nao. Hivyo jumuiya hizi zilihama tu wakati ziliposhindwa kuvumilia shinikizo la watawala hao.

Katika karne ya kumi na tisa, Wagwiriko, Wakenedugu na watu wengine wa kusini-magharibi mwa eneo ambalo sasa ni Burkina-Fasso walikumbwa pia na hali kama ya wenzao hapo juu iliyosheheni shinikizo, kuyumbayumba, na migogoro. Jibu lao kuu lilikuwa ni kuhama. Vikundi tofauti kama vile Wapwa, Wasissala, Wagan na Wadyan vilipigana miongoni mwao, vilioana na kuhama kuelekea pande tofauti, hasa katika miongo ya mwanzo ya karne. Wakati vikundi hivi vya Volta vilipokuwa vinahama, bado viliendelea kudumisha utambulisho wao pekee wa utamaduni, japo kulikuwepo na

ufanano mkubwa katika utamaduni wao kwa jumla. Walilazimika kutumia muda wao mwingi kujijenga na kujilinda wenyewe, sio dhidi ya majirani zao wa karibu, bali hasa dhidi ya vikundi vya Wajuula ambavyo viliendelea kuwaghasi bila kufanikiwa kuwatawala.

Watu wengine wa Volta wasiokuwa na tawala unganifu, kama vile Wagurunsi, Wabisa na Wasamo, pia walishuhudia hali ya wasiwasi wa kisiasa katika karne ya kumi na tisa. Wakati Wagurunsi wakiporwa na vikundi vya jirani, kinyume chake kilitokea kwa Wabisa ambao walipanua maeneo yao kwa kuwadhulumu majirani zao. Nchi ya Wasamo haikushindwa na kikundi chochote, bali ilitumiwa mara kwa mara kama mahali pa kufikia na vikundi vya kijeshi vilivyokuwa vinarudi nyuma. Kwa jumla, mafanikio ya watu hawa wasiokuwa na tawala unganifu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa yalikuwa makubwa. Vikiwa vimetunukiwa nguvu na ustahimilivu mkubwa, vikundi hivi ambavyo pia viliendelea kujihusisha na dini za asili, vilionyesha akili pevu kwa namna ambavyo vilizipinga nguvu za kikoloni mwishoni mwa karne.

## *Maeneo ya mashariki ya nyanda za juu za Volta*

Katika maeneo haya, kulikuwa na nchi za Jelgoji na Liptako ambazo zilipakana na Messina na Sokoto upande mmoja, na Yatenga upande wa pili. Sehemu hii ya kijiografia ilisababisha mwingiliano mkubwa katika historia ya karne ya kumi na tisa ya watu hawa. Mwanzoni mwa karne, makundi tofauti ya Wafulbe, pamoja na makambi yao, yalipatikana katika eneo hili. Huko Jelgoji walikuwepo Wafulbe wa Jelgobe ambao walikuwa raia wa Jallube waliowatumikia kama wachungaji wa mifugo yao. Jinsi karne ilivyosonga mbele, Wafulbe waliasi dhidi ya mabwana zao, wakapata uhuru wao na kuanzisha tawala mbili mpya za machifu, Jiibo na Barbulle. Waferrobe walikuwa ni kikundi kingine cha Wafulbe walioishi katika eneo hili. Walikuwa chini ya Wagulmanseba huko Liptako. Wakiwa wamehamasishwa na jihadi ya Sokoto, kikundi hiki cha Wafulbe kilianzisha maasi dhidi ya mabwana zao wa jadi chini ya uongozi wa Brahima Saidu ambaye baadaye alikuja kuwa amiri wa jimbo jipya la Liptako.

Mpangilio wa kisiasa wa Liptako chini ya Wafulbe ulifanana sana na ule wa Jelgoji na ulilengwa katika kudumisha uwiano kati ya vikundi tofauti katika nchi. Madaraka ya utawala miongoni mwa jamii ya watawala ya Waforroba yalirithishwa kupitia kuumeni kuanzia kwa Saidu, baba yake Brahima ambaye aliongoza jihadi. Watorodbe, ambao walikuwa kikundi kingine cha Wafulbe nchini humo, waliunda jopo la uchaguzi ambalo lilichuja na kuteua maamiri wapya. Mfumo huu ulisaidia kuwashirikisha Watorodbe katika jamii, licha ya kunyimwa fursa ya kujihusisha moja kwa moja na uongozi. Sherehe ya kumsimika amiri ilikuwa pia ni fursa iliyokutanisha Uislamu na dini za asili kwa lengo la kuleta uwiano mzuri wa kijamii na kuhakikisha ukwasi kwa utawala mpya. Koo kongwe za Wafulbe ambazo hazikuweza kugombea cheo cha amiri zilifidiwa kwa kupatiwa vyeo vingine vya chini zaidi.

Kitu kingine cha kipekee katika historia ya ukanda huo upande wa mashariki wa nyanda za juu za Volta katika karne ya kumi na tisa kilikuwa ni mabadiliko ya ruwaza za ushirikiano miongoni mwa jumuiya mbalimbali. Wakiwa wametishwa na Massina



25.5 Mogho Naaba Sanem akiwa anasalimiwa na raia wake, 1888.

25.6 Aina za nyumba za Bambara, 1887



mwaka 1858, Wafulbe wa Jiibo na Barbulle waliomba msaada wa Wayatenga na Wadatenga kutoka nchi ya Mossi ili kuwaangamiza maadui zao. Baada ya Massina kushindwa, Wafulbe waliwageukia marafiki zao waliotoka Mossi, wakawaua na kurejesha tena maelewano mazuri na Massina. Wakati huohuo, vikundi vyenye kushindana huko Jiibo na Barbulle vilitafuta kuungwa mkono ama na Massina au na Yatenga katika mapambano yao ya kutafuta utawala wa ndani. Hata hivyo, hadi ilipofikia mwisho wa karne, Wakurumba, ambao walikuwa wakazi wa asili wa Jelgoji kabla ya kuhamia kwa Wafulbe, tayari walishakuwa tishio la kutosha kusababisha muungano kati ya Jilgoji na Liptako. Watuareg nao walikuwa na dhima muhimu katika siasa za ukanda huo.

## *Falme za Bambara za Segu na Kaarta*

Historia ya Segu na Kaarta katika karne ya kumi na tisa ilikuwa na vitendo vya uchokozi ambavyo vilionekana kama vitendo vya ushujaa, uvamizi uliofanywa bila mpangilio mzuri, na vita vikali baina ya falme mbalimbali, na ndani ya ufalme mmoja mmoja, yote hayo yakiashiria mambo yaliyokuwa hasi kabisa katika mfumo wa kisiasa uliokuwa unaporomoka. Uhusiano kati ya Segu na Kaarta haukuwa mzuri, hasa kwa kuwa watawala wa Kaarta waliwadharau wafalme wa Segu. Hali hii ndiyo ilikuwa sababu ya mashambulio ya mara kwa mara yaliyofanywa na Segu dhidi ya Kaarta. Segu, ambayo ilikuwa na watu wengi na nguvu zaidi, aghalabu iliishinda Kaarta japo haikufanikiwa kuitwaa. Kipindi hiki kilibainishwa pia na ongezeko la umaarufu wa *watonjon*, mashujaa mashuhuri na wafanya biashara waliotumia vyema umaarufu wao wa kijeshi kujiongezea mamlaka. Hii ndiyo hali iliyokuweko katika falme za Bambara kabla jihadi ya Al-Haji Umar haijazifagilia mbali.

Hivyo, katika karne ya kumi na tisa, miundo ya kisiasa iliyokuwepo katikati na kaskazini mwa eneo linaloshughulikiwa katika sura hii ilididimia kwa kasi kubwa na baadhi yake kutawaliwa na nguvu mpya zilizochochewa na jihadi ya Sokoto. Nguvu hizi mpya zilitumia vizuri matatizo ya ndani yaliyosababishwa na kuporomoka kwa tawala zilizokuwepo, na hivyo kuongeza kasi ya kudhoofika kwake, na kuhakikisha kwamba hata zenyewe hatimaye zingefutiliwa mbali na mataifa ya kigeni.

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, kuna maelezo kadhaa kuhusu kudhoofika huku. Ingawa kulikuwa na athari kutoka nje kama vile shinikizo la kibiashara kutoka pwani na msukumo wa Wazungu, lakini yalikuwepo pia matatizo ya ndani kama vile misukosuko ya kisiasa na miguro ya watu. Katika hali hii, mgawanyiko wa kijamii uliongezeka na kuibadilisha miundo ya kiusawa ya kijamii iliyozibainisha jamii za Sahel wakati zilipokuwa zikiinukia. Tukio jingine muhimu kwa wakati huu lilikuwa ni kuzuka kwa vuguvugu la kidini ambalo liliingiza siasa kali na kushindwa kustahimili imani za jadi. Hata hivyo, pamoja na vurugu zote hizi na kutibuliwa huku katika karne ya kumi na tisa, bado watu wengi waliendelea kufanya kazi ili kuhakikisha kwamba jumuiya zao zinadumu. Watu wa kawaida hawakujipweteka tu kusubiri majaaliwa yao, bali, licha ya misukosuko iliyokuwepo, walionyesha uwezo mkubwa wa kujirekebisha ili kukabiliana na changamoto kuu za wakati huo kama vile uvamizi wa ukoloni.

## *Misukosuko ya kiuchumi-jamii*

Kilimo ndicho kilichokuwa msingi wa maisha ya uchumi ya watu wa mzingo wa Niger na Volta. Wakati idadi kubwa ya watu ilijiingiza katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, wengine walijihusisha na biashara, hasa katika bidhaa za kilimo. Vikundi vingine kama vile Wajuula vililazimika kuchanganya shughuli zote mbili. Mikoa ya pwani ilinunua dhahabu na watumwa na kuuza bidhaa za Kizungu kwa majirani zake walioishi bara, wakati watu wa Sahel waliagiza kola kutoka bara na silaha kutoka pwani kwa kubadilishana na chumvi, mifugo na watumwa. Kati ya Saheli na pwani kulikuwa na maeneo ya savana ambayo yalitoa watumwa, mifugo, nafaka na dhahabu.

Hali hii iliathirika kidogo tu kutokana na kukomeshwa kwa biashara ya watumwa na Waingereza mwaka 1807. Sehemu za pwani, amri ya kuzuia biashara ya watumwa ilitekelezwa, ila utumwa wa nyumbani ulivumiliwa. Hata hivyo, utumwa ulipanuka huko bara katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa. Hii ilisababishwa na kuongezeka sana kwa bei ya silaha, jambo ambalo lilimaanisha kwamba idadi kubwa zaidi ya watumwa ilitakiwa ili kubadilishwa kwa kiasi kilekile cha risasi na baruti. Kufuatia hali hiyo, vikundi kadhaa, kama vile Wazamberma, vilibobea kama wauza watumwa. Chanzo chao kikuu cha kupatia watumwa kilikuwa ni jihadi zilizoendeshwa na viongozi wa Kiislamu wa kaskazini, migogoro katika nchi ya Mossi, uvamizi kwa Watuareg na maeneo yaliyopakana na vituo vya biashara huko pwani, na vita vingine viliyotokea katika ukanda huo. Mateka walitoka zaidi kwenye jamii za wakulima ambazo hazikufanikiwa kujilinda nyakati zote.

Katika Gold Coast yenyewe, ambamo watumwa walitimiza asilimia 90 ya biashara ya nje mwanzoni mwa karne, ukomeshaji wa biashara ya watumwa ulibadilisha hali ya uchumi kwa kiasi kikubwa. Mafuta ya mawese na mpira vilichukua nafasi ya biashara ya watumwa kama mahuruji (bidhaa za kuuza nje) ya kwanza huko pwani. Dhahabu ilichimbwa huko bara na kupelekwa kusini, wakati kola, bidhaa nyingine ya bara, ilipelekwa kaskazini. Kadhalika, bidhaa za anasa kutoka Ulaya zilipelekwa kusini kupitia Afrika ya Kaskazini, Fezzan na nchi ya Hausa hadi mzingo wa Niger. Hariri na mazulia kutoka Uturuki na Tripoli, natroni (magadi) kutoka Borno, na nguo za Hausa zilibadilishwa kwa kola, dhahabu, na vitambaa vya pamba kutoka Dagomba, Mossi na Mande, pamoja na siagi ya mshea (aina ya mti ambao mbegu zake hutoa mafuta), na mifugo kutoka Saheli ya Sudan.

Biashara hii ya kubadilishana ilileteleza kukua kwa Salaga, mji uliokuwa katika nchi ya Gonja, kama kituo muhimu cha kuhifadhi na kusambazia bidhaa. Mji huu ulikua sana na kugeuka mji mkubwa sana na ustawi wake uliendelea hadi dola ya Asante ilipoanguka na kusababisha njia za biashara zichepukie sehemu nyingine. Mapatano ya kibiashara huko Salaga yaliendeshwa hasa kwa mpango wa kubadilishana bidhaa, ijapokuwa vumbi la dhahabu pamoja na simbi mara nyingine vilitumika kama fedha.

Mbali na Asante na Lobi, dhahabu pia ilipatikana katika ukingo wa kushoto wa Black Volta ya juu. Dhahabu hii ilichimbwa na wanaume wenye asili mbalimbali na wanawake pia walihusishwa katika uzalishaji wake. Nguvukazi ya watumwa ilitumika kwa kiwango kikubwa. Ni muhimu hata hivyo kutilia maanani hapa kwamba, uzalishaji wa dhahabu



25.7 *Mfanyabiashara wa Mossi, 1888*




25.8 *Kintampo: Mji wa biashara katika bara ya Gold Coast (imetayarishwa na L.G. Binger, 1892).*

katika eneo hili haukusimamiwa na serikali kuu yoyote, bali wazalishaji walikuwa wajasirimali binafsi. Wachimbaji kadhaa wa dhahabu walijihusisha katika kusaka watumwa kwa vile watumwa walikuwa na faida zaidi na kwa vile pia watumwa hao waliweza kutumika katika kusafisha dhahabu.

Wakati dhahabu kutoka Lobi ilipelekwa Gold Coast na Liberia, ile ya ukingo wa kushoto wa Black Volta ya juu ilikwenda Sahara na Moroko. Ilisafirishwa kupitia njia za biashara za wenyeji au za ukanda, baadhi kati ya hizo zikipitia Salaga. Katika biashara ya wenyeji dhahabu ilitumika kununulia chumvi, kola, watumwa, nafaka na mabubu (makanzu marefu hadi chini kwenye unyayo). Chumvi ilikuwa kifaa kingine muhimu cha biashara na ilipatikana katika hali mbalimbali. Kati ya bidhaa zote zilizelezewa hapo juu biashara ya watumwa pekee ndiyo iliyopanda sana kwa thamani katika nusu ya pili ya karne.

Mtandao wa njia za biashara ulichomoza kutoka Dori, na hili linaonyesha kwamba Saheli ilikuwa wazi kwa biashara kutoka pande zote. Biashara hii iliendeshwa na Wajuula, Wahaussa, Wamossi, machotara wa Kiberiberi, na Watuareg. Bidhaa zilizoingizwa Dori kutoka nje zilijumuisha tumbaku, mikeka, mifugo, na chumvi kutoka kaskazini, vitu ambavyo vilibadilishwa kwa vitambaa vya pamba, vilemba vya Kihausa na bidhaa zilizotengenezwa Ulaya. Bidhaa nyingine zilizobadilishwa ni watumwa, shaba iliyofuliwa, nguo za Guinea, vifaa vya ujenzi na kola. Kwa jumla, ingawa shughuli za wafanyabiashara zilikuwa ni sehemu ndogo sana ya uchumi wa ukanda huu, zilikuwa na athari kubwa katika maisha ya watu wote. Jumuiya za mpakani ambazo zilikusanya watu na mawazo mbalimbali zilianzishwa, na hivyo kuunda jamii za mchanganyiko wa watu. Umuhimu wa jamii kama hizo ulikuwa katika mgawanyo dhahiri wa kazi na shughuli maalumu ambazo ziliendeshwa humo: kulikuwepo na wamiliki wa ardhi, wapangaji, madalali na utitiri wa mafundi wa fani mbalimbali.

## *Mabadiliko ya kijamii*

Si jambo la kushangaza kuwa, katika karne ya kumi na tisa, kulikuwa na mabadiliko makubwa ya kijamii katika nchi zilizoko katika mzingo wa Niger na katika bonde la Volta, ikizingatiwa mistikostiko iliyokuwepo wakati huo. Mabadiliko haya yalijidhihirisha zaidi katika madola unganifu kuliko katika madola yasiyokuwa na mfumo huo. Pia yalijidhihirisha zaidi katika ukanda wa pwani kuliko ilivyokuwa huko bara, na zaidi pia katika maeneo ya Waislamu kuliko maeneo mengine.

Katika madola unganifu, hali za watumwa na wana-matabaka ya kiamali zilikuwa mbaya zaidi: walibaguliwa, kukandamizwa na kunyonywa na mabwana zao Wafulbe. Jambo hili, kwa mfano, lilisababisha maasi ya watumwa huko Liptako mwaka 1861. Wenyeji wa Gulmanceba waligeuzwa watumishi. Hata mafundi mchundo walinyimwa haki walizokuwa nazo watu huru na malodi; lakini bado wengine kati yao, kama vile wahunzi, waliogopwa kwa sababu ya ubunifu na ujusi (uganga wa kimiujiza) uliohusishwa na kazi yao. Katika himaya ya Mossi ya Wagadugu, idadi kubwa ya

watumwa walifanywa matowashi. Wakati huohuo watu binafsi katika uongozi wa mambo ya kijamii sio tu kwamba waliishi katika ukwasi, bali walitegemewa na idadi kubwa ya wafuasi. Zaidi ya zawadi, ushuru wa mavuno, na kodi zilizotozwa kwa wafanyabiashara. Machifu hawa pia walipokea asilimia fulani ya mali iliyoporwa wakati wa uvamizi.

Hata hivyo katika jamii zisizokuwa unganifu, uhusiano kati ya watumwa na waliowamiliki ulikuwa wa kirafiki zaidi. Huko Pura na Lobi, kwa mfano, watumwa walitendewa vyema, na asasi ya utumwa kwa kweli ilitumika kama njia ya kuimarisha ukoo na vikundi vya kijanibu. Hii ni kwa kuwa watumwa waliunganishwa barabara katika jamii na kupewa kiasi fulani cha haki za binafsi.

Katika madola unganifu, chanzo kingine cha mvutano kilikuwa ni ushindani kati ya watawala na malodi. Katika nchi kama vile Asante, falme za Bambara, Yatenga, ufalme wa Wagadugu na Gwiriko, kulikuwepo na mapambano makali kati ya malodi na watawala.

Katika maeneo ya pwani, biashara na elimu pia vilileta mabadiliko dhahiri katika jamii. Mageuzi kutoka biashara ya watumwa na kuingia katika biashara ya mafuta ya mawese, mpira, pembe za ndovu na dhahabu yalisababisha kuzuka kwa tabaka jipya la wafanyabiashara ambao pia walifanya kazi kama mawakala wa makampuni ya Wazungu. Wafanyabiashara hawa wakubwa walisaidia idadi kubwa ya wafanyabiashara wengine wa Kiafrika na kudhibiti upatikanaji wa bidhaa kutoka bara.

Kuenea kwa elimu ya kimagharibi katika pwani pia kulisababisha kuzuka kwa matabaka mapya ya jamii. Haya yalijumuisha dhuria wa familia za wafanyabiashara wakuu ambao walikuwa wameelimishwa Ulaya tangu mwanzoni mwa karne au katika Chuo cha Fourah Bay huko Sierra Leone. Watu hawa walipata nafasi zenye wajibu mkubwa katika jamii zao. Walikuwepo pia wale waliokuwa na elimu ndogo tu ambao walifanya kazi za ukarani kwa wafanyabiashara wa Kiingereza na wa Kiafrika na kuishi kama vimelea wa machifu wasiokuwa na kisomo pamoja na watu wao. Baina ya makundi haya mawili ya wasomi, kulikuwepo na watu waliokuwa na elimu ya kutosha kuwawezesha kuwa wafanyabiashara waliojitegemea na mameneja katika miji ya pwani. Licha ya tofauti zao, vikundi hivi tofauti viliingiliana mara nyingi na kushirikiana, kama ilivyodhihirishwa na tendo lao la pamoja kuhusiana na Shirikisho la Fante lililojadiliwa hapo awali.

## *Mabadiliko ya kidini*

Karne ya kumi na tisa katika ukanda huu ilikuwa ni kipindi cha maendeleo ya haraka ya Uislamu huko kaskazini na kati, na kuhuishwa kwa Ukristo huko Kusini. Dini zote mbili zilisisitiza hadhi ya elimu na pia ziliwapa watu upeo mpana zaidi. Katika sehemu ya kaskazini ya ukanda huo, kariha (msukumo wa kutenda jambo) iliyotokana na jihadi zilizopita za Uthman da Fodio wa Sokoto, Seku Ahmadu wa Massina na Al-Haji Umar, ilisababisha jihadi ya wenyeji iliyoleteleza kuundwa kwa utawala wa kiamiri huko Liptako. Na, licha ya upinzani uliosifika sana wa Wamossi na Wabambara dhidi ya Uislamu, bado waliingiliwa na athari za Uislamu katika karne ya kumi na tisa. Watawala



**25.9** *Salaga katika mwaka 1888.*

**25.10** *Karakana ya seremala ya misioni ya Basel huko Christiansborg (Akkra). Mchoro kutoka picha ya fotografia, labda ya 1870.*



wa Bambara huko Segu sio tu kwamba waliomba ushauri wa warabiti, bali pia waliwakaribisha katika vitala vyao. Idadi kubwa ya falme za Mossi pia ziliukumbatia Uislamu jinsi karne ilivyosonga mbele kwa kuwa ziliathiriwa na Uislamu kupitia shughuli zao za kibiashara. Uislamu pia ulikuwa dini iliyoongoza huko Dagomba, Mamprusi na Sansanne Mango, na katika maeneo hayo maimamu walikuwa ni watu mashuhuri katika siasa. Watawala wa Asañte nao walionyesha upendeleo kwa Uislamu. Wafanyabiashara Waislamu kutoka ulimwengu wa kiarabi walimiminika kwenye mji mkuu wa Asante, na vifaa vya kidini vilivyotengezwa na warabiti viliuzwa kwa bei kubwa. Ingawa Uislamu ulishindwa kuzing'oa dini za asili ambazo zligeuka kuwa msingi wa miundo ya kisiasa katika ufalme wa Asante, bado uliweza kuwazuia wanamfalme wa Asante wasiingie katika Ukristo.

Wakati Uislamu ulikuwa unaosonga mbele huko kaskazini, Ukristo nao ulikuwa unaingizwa upya huko kusini mwa ukanda unaojadiliwa. Ilipofikia mwaka 1828, Misioni ya Kiinjili ya Basel na Misioni ya Bremen tayari zilikwisha anzishwa kusini-mashariki mwa Gold Coast. Misioni hizi zilianzisha mashamba ya maonyesho na shule za ufundi. Wamisionari wa Kimetodi nao walikuwa wakijishughulisha katika pwani ya magharibi, Cape Coast ikiwa ndiyo kituo chao kikuu. Nao pia walianzisha mashamba ya maonyesho katika wilaya ya Gold Coast, walifungua shule nyingi, na kufasiri kazi za msingi za Ukristo kwa lugha ya Kiga. Mchungaji J.G. Christeller aliandika kitabu cha sarufi ya Kitwi mwaka 1874, na kamusi ya Kiakan mwaka 1881. Hata hivyo, licha ya jitihada hizi za Ukristo na Uislamu, dini ya asili iliweza kudumu katika ukanda huo.

## *Hitimisho*

Jamii za nchi ya mzingo wa Niger na bonde la Volta zilialika uchokozi kutoka nje katika karne ya kumi na tisa kutokana na migogoro yao ya ndani. Lakini mizizi ya migogoro hii inaweza kutafutwa katika karne za nyuma wakati biashara ya watumwa ilipozusha migongano kadha ya kiuchumi katika ukanda huo. Hivyo kuhama kwa watu, kulowea kwa vikundi vipya vya watu, mivutano ya kijamii na hata upanuzi wa kisiasa na kidini katika karne ya kumi na tisa - yote haya ni matokeo ya tukio hili kuu lililotawala karne zilizotangulia. Kwa hiyo, kwa namna fulani, karne ya kumi na tisa iliashiria mwisho wa kipindi kirefu sana, sio tu katika historia ya ukanda huu, bali pia katika Afrika kwa ujumla.

# 26 Dahomey, nchi ya Yoruba, Borgu na Benin katika karne ya kumi na tisa

*Utangulizi*

Eneo linaloelezewa katika sura hii limepakana na mto Mono kwa upande wa magharibi, Niger kwa upande wa kaskazini na mashariki, na bahari ya Atlantiki upande wa kusini. Karibu eneo lote ni uwanda wa mabonde na miinuko, yakipanda na kushuka huku vilele vyake vikiwa katika vilima vya Atakora na Kukuru. Uoto haukushikamana, ijapokuwa ipo misitu minene ya mvua upande wa kusini-mashariki, eneo ambalo lilikuwa ufalme wa kale wa Benin.

Yapo maeneo manne ya tamaduni tofauti lakini zinazohusiana katika ukanda huo, yaani: Waaja kwa upande wa magharibi, Wayoruba katika eneo la katikati, Waborgu upande wa kaskazini, na Waedo upande wa mashariki. Kila moja ya maeneo haya ya utamaduni linaweza kugawanywa kufuatana na lahaja za lugha zake kuu, ekolojia, na shughuli maalumu za wakazi wake. Watu wanaozungumza lugha ya Kiaja wako katika makundi madogo matatu, yaani Wafon ambao walitawala ufalme wa kale wa Dahomey; Wagun wa bonde la mto Weme na mkoa wa Porto Novo-Badagry; na Waewe ambao sasa wanapatikana katika sehemu za kusini-magharibi mwa Jamhuri ya Benin, kusini mwa Togo, na kusini-mashariki mwa Ghana.

Eneo la utamaduni wa Wayoruba ndilo pana kuliko yote katika ukanda wa Mono-Niger. Linakumbatia sehemu kubwa ya kusini-magharibi mwa Nigeria. Vipo vikundi kadhaa vidogovidogo vya Wayoruba kama vile Waoyo, Waibarapa, Waife, Waijabu, Waijesa, Waegba, Waegbado, Waondo, Waikale, Waekiti, Waowo, Waakoko na Waawori. Pia katika mpaka wa Niger-Benin kutoka kaskazini hadi kusini vipo vikundi vidogovidogo vya Wayoruba kama vile Waketu, Waohori, Waifonyin na Waanago.

Eneo la utamaduni wa Borgu limeundwa na vituo muhimu vitatu vya tawala za jadi, yaani Busa, Illo na Nikki. Busa na Illo vilikuwa katika eneo la serikali ya kijanibu ya Borgu ya dola la zamani la Kwara pamoja na sehemu zinazopakana na dola la Sokoto la Nigeria. Nikki, dola kubwa zaidi la jadi katika eneo hili, iligawanywa na mpaka wa sasa wa Nigeria-Benin, matokeo yake yakawa kwamba baadhi ya sehemu zake zilikuwa upande wa mpaka wa Nigeria na nyingine upande wa Benin. Lugha mbili kuu zilizungumzwa huko Borgu: Kibatonu (au Kibariba) na Kiboko, kila moja ya lugha hizo ikiwa imegawanyika tena katika lahaja tofauti kadhaa.



**26.1** *Sanamu ya askari akiwa juu ya mabega ya babalawo (mganga wa kienyeji) kutoka kaskazini-mashariki wa nchi ya Yoruba; (labda) ilichongwa kati ya 1850 na 1875.*

Eneo kubwa la nne la kitamaduni katika ukanda huu ni lile la watu wa ufalme wa kale wa Benin waliozungumza lugha ya Edo. Hawa walijumuisha sio tu Waedo wa mji wa Benin, bali pia vikundi vilivyohusiana kiisimu na kihistoria kama vile Waesan, Waivbiosakon, Waakoko, Waitsekiri, Waurhobo na Waisoko.

Maeneo haya makuu manne ya kitamaduni hayakuwa kanda zilizojitenga kwani yalikuwa yakiingiliana kwa kiwango kikubwa. Hili linaonyeshwa katika masimulizi yaliyohifadhiwa na watu, ambayo yanadai asili moja kwa jamii hizi, yanasisitiza dhana ya umoja wao, na kujaribu kuwanasibisha watawala wote wa meneo haya manne ya kitamaduni. Licha ya jambo hili, vipengele vya kiisimu, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa navyo vinaashiria uhusiano wa vikundi hivi katika ukanda huo. Mahusiano haya yanaelekeza katika mfululizo wa uhamaji, na miguro ya watu wanaoondoka na wanaorejea, miguro ambayo iliendelea katika karne ya kumi na tisa hadi ilipowekewa vigingi na kuanzishwa kwa mipaka ya kikoloni mwishoni mwa karne hiyo.

Hivyo historia ya eneo la Mono-Niger ni ile inayoelezea maingiliano ya Waaja, Wayoruba, Waedo na Wabariba, na ambayo pia inaakisi kuingiliana baina ya maeneo ya kitamaduni ya ukanda huu na majirani zao wengine.

## *Kuporomoka kwa Oyo Kongwe*

Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, himaya ya Oyo Kongwe ilikuwa ni nchi pekee yenye nguvu nyingi katika ukanda wa Mono-Niger kwa sababu ilitamalaki juu ya eneo kubwa la ardhi pamoja na watu wa ukanda huo. Ingawa kitovu cha himaya hiyo hakikuenea hadi kwenye mabonde ya mito ya Ogun na Osun, nchi zilizoilipa kodi zilijumuisha takriban nusu ya eneo la magharibi la Mono-Niger. Ndani ya himaya ya Oyo Kongwe ilikuwemo Dahomey, ambayo kuanzia 1748 ilikuwa katika nafasi ya utwana na ilibakia hivyo hadi katika miaka ya 1820. Porto Novo pia ilichukuliwa na kuwa bandari kuu ya Oyo kwa ajili ya kusafirisha watumwa nje. Nchi za Egba na Egbado zilitwaliwa kwa sababu njia za biashara zilizounganisha Porto Novo na Oyo zilipitia katika maeneo yao. Sio tu kwamba athari za kisiasa za Oyo zilikuwa na nguvu sana miongoni mwa Waegba na Waegbado kama ilivyoonyeshwa na kuwepo kwa *ajele* (maafisa wakazi) wake miongoni mwao, athari zake za kiuchumi na kiutamaduni nazo pia zilidhihirishwa kwa kuwepo kwa makoloni ya walowezi wa Oyo. Ijapokuwa Ketu na Sabe zilidai kujitawala zenyewe, lakini zilidumisha mahusiano ya kirafiki na Oyo. Borgu ya mashariki na sehemu ya kusini-magharibi ya Nupe pia zilikiri mamlaka ya *Alafin* (mfalme) wa Oyo. Kuenea kwa athari ya Oyo katika eneo lililotajwa hapo juu kuliwezekana kutokana na mandhari yake ya wazi, ambayo yalirahisisha mawasiliano na kuwezesha kufanikiwa kwa matumizi ya jeshi la farasi la Oyo.

Nusu ya mashariki ya ukanda wa Mono-Niger ambayo ilijumuisha sehemu iliyobakia ya eneo la utamaduni wa Yoruba, yaani Ife, Ijese, Ekiti, Ondo, Ijebu, Akoko, Owo, Ikale, Okiti-pupa, Awori, na ufalme wa Benin, haikuwa moja kwa moja chini ya athari ya Oyo. Hata hivyo, Oyo ilijihusisha nyakati zote katika historia ya falme kadhaa za Yoruba. Yalikuwepo pia mahusiano makubwa baina ya Oyo na Benin. Kwa kweli, nasaba tawala za pande zote mbili zilidai kuwa na asili moja kutoka kwa Ife na kutoka




**26.2** *Nchi ya Yoruba-Aja ikionyesha himaya ya Oyo Kongwe (mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa)*

Chanzo: Ade Ajayi na M. Crowder (Wah) *History of West Africa* (Historia ya Afrika Magharibi), Longman, 1974, uk.131

kwa mwanzilishi yuleyule, Oranyan. Hisia hizi za kidugu huenda zilishikiliwa kwa sababu hakukuwepo na fursa kubwa ya misuguano kati ya madola hayo mawili kwa vile kila moja liliendesha shughuli zake katika eneo tofauti, kila eneo likiwa na matarajio tofauti ya kibiashara - Oyo ilikuwa ndani ya eneo la savana, na Benin ilikuwa katika msitu mnene wa mvua.

Kwa kuangalia yaliyopo hapo juu, inaweza kuonekana kwamba Oyo ilikuwa katika kiini cha historia ya ukanda mzima, kutoka Mono hadi Niger, kiasi kwamba kuporomoka kwake katika muongo wa tatu wa karne ya kumi na tisa kulisababisha mabadiliko makubwa ya kijamii-kisiasa ambayo yalihisiwa sio tu katika nchi ya Yoruba pekee, bali pia huko Dahomey, Borgu na Benin. Kuanguka kwa himaya ya Oyo Kongwe kulisababishwa na mambo ambayo yalikuwa na mizizi yake katika karne ya kumi na nane, lakini ambayo yalipata uzito zaidi katika miongo miwili ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa. Haya yalijumuisha mambo ya ndani ambayo yalijitokeza katika migogoro ya kugombea madaraka kati ya ma-*alafin* mbalimbali na machifu wa kinasaba katika nusu ya pili ya karne ya kumi na nane. Matatizo haya nayo yalizidishiwa ukali na nguvu za nje, kama vile kupanuka kuelekea kusini kwa jihadi ya Uthman dan Fodio, na kushuka kwa biashara ya ng'ambo ya watumwa. Pamoja na matatizo haya kulikuwepo na suala la kudidimia kwa muundo wa himaya na kudhoofika kwake kijeshi. Jambo hili linaelezea kushindwa kwa Oyo na Egba mwaka 1774, Borgu mwaka 1783, na Nupe mwaka 1791. Kufikia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, hali ya kisiasa ya ndani ilikuwa imekwisha kusambaratika kabisa, kama inavyoonyeshwa na ma-*alafin* waliotawala bila mafanikio na kwa kipindi kifupi, kama vile Aole na Maku; na kipindi kirefu kisichokuwa na mtawala kilichodumu kwa takriban miongo miwili. Katika hali hii ya wasiwasi, maasi ya Afonja, aliyekuwa kiongozi wa kitaalamu wa jeshi la Oyo, yalianzisha mfululizo wa matukio ambayo hatimaye yalipelekea kwenye kifo cha himaya hiyo.

Kuporomoka kwa Oyo kuliuathiri zaidi upande wa magharibi wa ukanda huo ambako athari za himaya hiyo zilikuwa kubwa na za moja kwa moja zaidi. Athari kubwa ya kuanguka kwa himaya ilikuwa ni kuibuka kwa hali ya jumla ya kivita na ukosefu wa usalama. Hali hii ilivuruga kilimo na biashara ya wenyeji, ilivuruga biashara ya pwani, na kuhimiza kuingilia kwa Wazungu katika siasa za ndani ya bara. Vita vilivyosababishwa na kuanguka kwa Oyo vilikuwa vya aina mbili. Kulikuwepo na vita vya jihadi na vita miongoni mwa nchi za Wayoruba. Matukio mengi yanaweza kujumuishwa katika vita vya jihadi: kudhulumiwa kwa mashabiki wa Wafulbe katika nchi ya Egbado; vita vya Eleduwe vya 1836 kati ya Wafulbe kwa upande mmoja, na Borgu na Oyo kwa upande wa pili; na vita vya 1840 ambavyo Wafulbe walishindwa huko Osogbo. Vita baina ya dola za Wayoruba vilikuwa vya maangamizi zaidi na vinaweza kugawanywa katika awamu tatu zinazobainishwa na vita vya Owu 1820-5, vita vya Ijaye 1860-5, na vita vya Ekitiparapo au Kiriji 1877-93.

Vita vya Owu vilikuwa kati ya Waife na marafiki zao Waijebu, wakisaidiwa na wapiganaji wa Oyo, na Waowu, ambao waliungwa mkono na Waegba. Matokeo ya vita hivyo yalikuwa ni kuanzishwa kwa makazi mapya kama vile Ibadan, Abeokuta, na Ijaye.



**26.3** *Lango la mji wa Wayoruba wa Ijebu uitwao Ipara, k. 1855. 55. (Misioni ya kanisa ya Gleaver 1855)*

Kulikuwepo pia na kuundwa upya kwa mji mkuu wa Oyo huko Ago-Oja katika miaka ya 1830. Makazi haya yalikuja kuwa vituo vipya vya madaraka katika nchi ya Yoruba, kila kimoja kikigombania kutambuliwa na kurithi ukuu katika ombwe la kisiasa lililosababishwa na kuanguka kwa Oyo.

Vita vya Ijaye vilikuwa ni mashindano kati ya Ijaye na Ibadan, huku Egba na Abeokuta zikiwa zinaisaidia Ijaye bila mafanikio yoyote. Kwa kweli hizi zilikuwa ni harakati za kugombania uongozi. Harakati hizi zilifikia kilele chake kwa maangamizi ya Ijaye mnamo mwaka 1862, japo vita viliendelea taratibu kwa awamu mbalimbali hadi pambano lililopiganwa nje ya Ikorodu mwaka 1865. Waikitiparapo walikuwa ni muungano mkubwa wa Waekiti, Waijesa, na Waigbomina, wakiungwa mkono na Waife na wengineo, wakipigana ili kupinga kutawaliwa na Ibadan. Vita hivi vilijikokota hadi Waingereza walipoingilia kuleta amani mwaka 1886, na hata hivyo havikuisha kabisa hadi 1893.

Athari nyingine muhimu ya kuanguka kwa Oyo Kongwe ilikuwa ni kuibuka kwa Dahomey kama ufalme unaojitawala wenyewe mwaka 1820, na uvamizi wake wa mara kwa mara kwa nchi za Yoruba hadi ilipotekwa na Wafaransa mwaka 1892. Uimara wa kisiasa wa Dahomey katika karne ya kumi na tisa ulikuwa ni matokeo ya utawala mrefu wa wafalme wake, kuanzishwa kwa mfumo unganifu wa utawala uliokuwa na ufanisi

mkubwa, na nguvu zake za kiuchumi. Ni mchanganyiko wa mambo haya yote uliomfanya Gezo, mfalme wa Dahomey, kutumia fursa ya kuanguka kwa uongozi wa ndani wa Oyo kutangaza uhuru wa Dahomey mwanzoni mwa miaka ya 1820. Hili lilifuatiwa na mfululizo wa uvamizi wa Dahomey kwenye ardhi ya Yoruba, hasa katika nchi za Waegbado, Waketu, Wasabe, Waoke-Odan na Waegba wa Abeokuta. Hata hivyo Dahomey ilishindwa mara mbili na Waegba mwaka 1851 na 1864. Licha ya matukio haya, mashambulizi ya Dahomey katika eneo la juu la Ogun yaliendelea hadi ilipotwaliwa na Wafaransa mwaka 1892.

Vita hivi vya Dahomey-Yoruba vya karne ya kumi na tisa, havitakiwi hata hivyo kutazamwa kwa upekee na kutafsiriwa kama vita baina ya makabila. Vinapaswa vichukuliwe sambamba na vita kadhaa vya ndani ya Yoruba vilivyotajwa juu, na vita vya ndani vya Ija vya wakati huohuo: kwa mfano vita vya Dahomey katika bonde la mto Weme na Porto Novo katika miaka ya mwisho ya 1880 na ile ya mwanzoni mwa 1890. Angalau ruwaza ya urafiki na ufafanuzi wa maslahi na aula katika vita hivi vinapaswa vituelekeze katika kuona uhusiano wa kitamaduni kati ya makabila ya ukanda mzima, na kuhoji dhana ya ukabila na umbari (*ethnicity*) kama ilivyoendelezwa katika kipindi cha ukoloni.

Vita vilivyopiganwa baada ya kuanguka kwa Oyo Kongwe vilikuwa na athari muhimu sana hasa kwenye eneo la nusu ya magharibi ya ukanda wa Mono-Niger. Kwanza kabisa, kulikuwepo na mabadiliko makubwa sana ya kidemografia na miguro ya watu katika ukanda huo, na kama ilivyotajwa hapo juu, vitu hivi havikuheshimu mstari wa "umbari" ambao baadaye ulikuja kuchorwa katika kipindi cha ukoloni. Uharibifu mkubwa wa miji mikuu iliyokuwepo kabla ya karne ya kumi na tisa kama vile Oyo Kongwe yenyewe, Igboho, Ikoyi, Igbon, Iresa, Oje, Ketu na Sabe ulianzisha miguro mikubwa ya watu kuelekea kwenye maeneo mapya. Miji mingine mipya ilianzishwa katika maeneo mapya kama vile Ibadan, Abeokuta, Sagamu na Aiyede, ikiwakaribisha wakimbizi kutoka mbali. Wakimbizi nao waliongeza kwa wingi idadi ya watu katika miji ya zamani kama vile Ogbomoso, Oshogbo, na Offa. Kulikuwepo na kukamatwa utumwa kwa idadi kubwa ya watu, pamoja na ongezeko kubwa katika matumizi ya watumwa wa nyumbani. Matokeo yake ni mwingiliano wa hali ya juu wa watu wenye asili tofauti kwani watumwa wa Yoruba walijikuta katika nchi ya Aja, na wakimbizi wa Aja walimgia katika jumuiya za Wayoruba zilizohusiana.

Athari za kijamii za miguro hii ya watu zilikuwa nyingi na zilizotofautiana. Kulikuwepo na ongezeko kubwa la kiwango cha ukuaji wa miji, kwani miji yenye ngome na walinzi wenye silaha ilionekana kuwahakikishia wahamiaji usalama wa kutosha. Miji mipya ilifanya majaribio na mifumo mipya ya serikali kama vile udikteta wa kijeshi huko Ijaye chini ya uongozi wa Kurumi, shirikisho huko Abeokuta chini ya Sodeke, na ufalme wa kikatiba huko Epe chini ya Kosoko. Hasa, maaskari walijitokeza kama tabaka tawala jipya kisiasa karibu katika kila mji mpya, na punde waliweza kuwa na nguvu kuliko matabaka ya kifalme yaliyokuwepo kabla yao. Mchakato huu wa kujizoeza mambo mapya ulionekana pia miongoni mwa jumuiya za Waaja zilizokuwa zinaishi katika maeneo ya Yoruba; jumuiya hizo baadaye zilipokea asasi za ki-*oba* za mtindo wa

Kiyoruba katika mchakato wa taratibu ambao uliendelea hadi karne ya ishirini.

## *Kufifia kwa Ufalme wa Benin*

Ufalme wa Benin, kama himaya ya Oyo Kongwe, haukuweza kuepuka athari za maangamizi ya karne ya kumi na tisa. Lakini tofauti na Oyo, uliepuka kuyaonja maangamizi kamili kabla ya kipindi cha utawala wa Wazungu kwa sababu ya uimara wa asasi zake za kisiasa. Hadi ilipofikia 1800, ufalme mzima ulikuwa umejumuisha takriban nusu yote ya mashariki ya ukanda wa Mono-Niger. Ufalme huo ulijumuisha dola za mashariki mwa Yoruba za Ekiti, Ondo, Owo; jumuiya za magharibi za Igbo; pamoja na Urhobo, Itsekiri na Ijo huko kusini. Ingawa Bini Edo, iliyoingia na kuzunguka mji wa Benin, iliunda eneo la mji mkuu, ufalme ulikumbatia pia maeneo yaliyokaliwa na watu waliozungumza lugha ya Edo kama vile Waesan, Waedo wa kaskazini, Waurhobo na Waisoko. Zaidi ya nchi hizi, mamlaka ya Benin ilitambulika kote katika pwani ya Atlantiki hadi Lagos huko magharibi. Benin pia ilidumisha mahusiano ya kinasaba-tawala kati yake na Itsekiri, Awori-Yoruba na falme nyingine zilizohusiana za Kianago.

Mambo mengi yalichangia katika kuanguka kwa ufalme wa Benin. Kuanzia karne ya kumi na nane hadi karne ya kumi na tisa, ufalme huo ulishuhudia mporomoko wa taratibu uliokuwa unakatishwakatishwa na vipindi vya ustawi na upanuzi wa nchi. Katika miongo mitatu au minne kabla ya kutwaliwa na Wazungu katika karne ya kumi na tisa, ufalme ulianza kusinyaa kwa sababu ya mashambulizi ya kutokea pande tatu dhidi yake. Shambulio La kwanza lilitoka kwa watawala wa Wafulbe wa Nupe ambao walizipenyeza athari za jihadi sehemu za kaskazini na kaskazini mashariki ya ufalme wa Benin. Pili, upanuzi wa Ibadan uliathiri maeneo yaliyotawaliwa na Benin katika nchi za mashariki mwa Yoruba, na Benin ilikuwa dhaifu sana katika kipindi hiki kiasi cha kutoweza kupeleka msaada wowote kwa vibaraka wake hao waliokuwa wanatishiwa. Msukumo wa mwisho ulitoka kwa Wazungu waliokuwa wanajipenyeza katika ufalme wa Benin kutokea Lagos na delta ya Niger huko kusini-mashariki. Matokeo yake ni kwamba maslahi ya Benin katika biashara ya pwani yalitishiwa na wafanyabiashara wa Kiingereza na walanguzi wa Kiafrika kama vile Waitsekiri na Waijo. Matokeo ya haya yote ni kwamba bandari ya Benin ya Ughoton ilidhoofika na ukiritimba wa Benin katika biashara ya pwani ulikatishwa ghafla na kufikia mwisho wake.

Wakati huohuo usitawi na nguvu zilizotokana na biashara ya pwani zilizifanya baadhi ya nchi zilizokuwa tegemezi kama vile Waitsekiri na Waagbor kupinga mamlaka ya Benin na kuanza kushindana nayo. Ingawa utajiri huu mpya ulisababisha mvutano mwingi na migogoro ya kisiasa katika ufalme wa Kiitsekiri wa Warri kwa kipindi cha karne kilichobakia, Benin wakati huo ilikuwa dhaifu mno na haikuweza kutumia fursa ya hali iliyojitokeza kurejesha mamlaka yake kama ilivyokuwa ikifanya kabla.

Wakati Benin ikipambana na uvamizi huo kutoka nje, ilikuwa pia inapambana na matatizo makubwa ya ndani. Haya yalikuwa zaidi katika umbo la migogoro ya urithi wa ufalme ambayo ilianza takriban katikati ya karne ya kumi na tisa na kuendelea hadi kuporomoka kwa ufalme. Ni katika muktadha wa mivutano na migawanyiko hii ya ndani

ambapo hali ya kupinga Uzungu ilijitokeza huko Benin katika miaka ya 1890.

## *Kukua kwa shauku ya Wazungu*

Kulikuwa na awamu mbili za kukua kwa shauku ya Wazungu kuhusu ukanda huo katika karne ya kumi na tisa. Katika awamu ya kwanza iliyohitimishwa mwaka 1861 wakati Waingereza walipoiteka Lagos, kulikuwepo na kiasi fulani cha uhuru wa kusafiri na ushirikiano miongoni mwa Wazungu (wa mataifa) mbalimbali. Awamu ya pili ilikuwa ni kipindi cha ongezeko la ushindani wa kimataifa, hasa kati ya Uingereza na Ufaransa, Wajerumani wakiingia katika mashindano haya katika miaka ya 1880. Awamu hii ya mwisho ilihitimishwa kwa kuligawa eneo hilo kati ya Uingereza na Ufaransa mwaka 1889. Hata hivyo haina budi kutiliwa maanani kwamba ruwaza ya shughuli za Wazungu katika awamu zote mbili iliukiliwa kwa kiwango kikubwa sio tu na matakwa ya serikali za Kizungu pekee, bali pia na hali ya mabadiliko ya ndani ya janibu zenyewe.

Hivyo, katika awamu ya kwanza ya kukua kwa shauku ya Wazungu kwa ukanda wa Mono-Nger, kulikuwepo na aina fulani ya mnyumbuko katika muundo na shughuli za jamii mbalimbali za Wazungu kama vile wafanya biashara, wapelelezi, wasafiri na wamisionari waliojishughulisha na Afrika. Walifanya shughuli zao bila kujali sana mataifa yao binafsi. Kama ilivyogusiwa hapo juu, kulikuwepo pia na kutojali sana uasili wa kijamii katika ruwaza ya urafiki wa mataifa ya Waafrika. Lakini wakati shughuli za Wazungu ziliamuriwa zaidi na dhati yao ya kukubali au kukataa ukomeshaji wa biashara ya watumwa, watawala wa Kiafrika na jumuiya zao hawakujishughulisha kabisa na suala hilo.

Bila shaka Wazungu walipaswa kukabiliana na hali halisi ya Afrika ambamo waliendesha shughuli zao. Wapelelezi, wamisionari na wafanyabiashara walilazimika kutumia mifumo ya mawasiliano na usafirishaji iliyokuwepo, na kuzingatia ruwaza ya mahusiano ya kijiografia na ya vikundi mbalimbali vya wenyeji. Kwa kweli haikuwachukua Wazungu muda mrefu kutambua kwamba kila mara maendeleo katika eneo moja la ukanda yaliathiri maeneo mengine kwa sababu ya mahusiano yaliyokuwepo kati ya watu na tamaduni mbalimbali, pamoja na mifumo ya dini na uchumi. Kwa mfano, Wazungu waliokuwa wanakomesha biashara ya watumwa waligundua kwamba vita vilivyoendelea huko bara vilikuwa na athari kubwa katika ukanda wa pwani na kwamba haikutosha kutia sahihi mikataba na watawala wa pwani peke yao. Ili kukomesha biashara ya watumwa, wakomeshaji walitakiwa kujihusisha na watu wa bara pia, na kutafuta njia za kuzuia vita miongoni mwao. Mtazamo wa Wazungu katika hali hii ulikuwa ni wa hatua kwa hatua, na wa kuleta mgawanyiko. Kwa mfano, kwa kutilia mkazo juu ya Lagos na delta ya mashariki ya Niger, Wazungu waliharibu biashara na athari ya Benin huko pwani. Hili halikutarajiwa, na lilikuwa na maana kubwa kuhusiana na mgawanyo wa madaraka katika ukanda huo.

Kutekwa kwa Lagos na kushambuliwa kwa Porto Novo na meli za Waingereza mwaka 1861 kuliashiria mwanzo wa hatua mpya na kuingiza awamu ya pili ya kukua kwa shughuli za Wazungu katika ukanda huo. Vitendo vya Waingereza huko Porto Novo viliwashtua Wafaransa waliokuwa na maslahi makubwa ya kibiashara katika eneo hilo pia. Jambo hili lilisababisha ushindani mkali kati ya mataifa hayo mawili huko bara ya Yoruba



**26.4** *Altare ya madhabahu katika ua wa mfalme, Benin.*

**26.5** *Sura ya mji wa Benin wakati wa kuvamiwa na Waingereza, 1897.*



na Aja. Hata hivyo, medani kubwa zaidi ilikuwa huko Yoruba ya magharibi ambako wenyeji walijaribu kutumia kwa faida yao ushindani wa Waingereza na Wafaransa kama ufumbuzi wa tatizo la kudumu la uvamizi wa mara kwa mara wa nchi yao uliofanywa na majirani waliokuwa na nguvu zaidi yao. Ushindani huu hatimaye ulifikia kilele chake katika kutekwa kwa Dahomey na Ufaransa mwaka 1892, kugawanywa kwa Borgu kati ya Waingereza na Wafaransa mwaka 1895, upanuzi wa utawala wa Waingereza kwenye eneo zima lililobaki la nchi ya Yoruba, na kutekwa kwa Benin na Waingereza mwaka 1897.

## *Mabadiliko ya kijamii-kiuchumi*

Vita vya karne ya kumi na tisa vilipokuwa vikiendelea na Wazungu kutumia fursa hiyo kuingilia katika mambo ya ukanda wa Mono-Niger, mabadiliko mengi makubwa nayo yalikuwa yakitokea miongoni mwa jamii zenyewe za wenyeji. Kwa kuanzia, miguro mikubwa ya watu ndani na nje ya ukanda huo ilisababisha matokeo makubwa. Uhamaji ndani ya eneo hilo uliwezesha kuwepo na maingiliano na kuchanganyika kwa watu wenye asili tofauti. Pia ulisababisha kukua kwa makazi mapya na ongezeko la mtiririko wa watumwa kutoka eneo hilo kwenda Dunia Mpya (Amerika). Kiwango (kikubwa) cha ukamataji watumwa katika karne ya kumi na tisa kilikuwa ni sababu muhimu iliyodumisha utamaduni wa Kiyoruba na Kiaja katika Dunia Mpya. Uhamiaji wa watumwa waliopatiwa uhuru wao kutoka Cuba, Brazil na maeneo mengine waliorudi katika maeneo yao ya asili katika pwani ya ukanda wa Mono-Niger ulikuwa pia kipengele muhimu katika uenezaji wa Ukristo, elimu na ufundi wa Magharibi, na katika kuleta mabadiliko ya kisasa kwa jumla.

Miguro ya wenyeji nayo pia ilikuwa na matokeo muhimu. Uhamaji wa watu wa Dahomey waliozungumza lugha ya Aja kutoka magharibi kwenda mashariki ulileteleza ongezeko la ukubwa wa makazi ya watu wa Aja yaliyokuweko huko mashariki kama vile Badagry, Ajido na Koga, na pia kuanzishwa kwa idadi kubwa ya makazi mapya katika maeneo ya jirani. Waoyo nao walihama kuelekea kusini. Hadi ilipofikia 1830, vituo muhimu ambavyo vilikaliwa na Waoyo vilikuwa Ibadan, Ijaye na mji mpya wa Oyo. Waoyo wachache pia walihamia Igbomina, Ijesa, Ekiti, Akoko, Ondo, Ikale, na Ilaje. Wakati huohuo, idadi kubwa ya watu kutoka katika vikundi vingine vya Wayoruba wa mashariki kama vile Waekiti na Waijesa waliingia Ibadan na katika makazi mengine ya Osun, Ijebu na Egba katika nchi ya Yoruba kama mateka au watu huru. Huko Borgu, jihadi ya Wafulbe ilisababisha mwondoko mkubwa wa watu kuelekea kusini, na mwondoko huo ulikuwa na athari kubwa magharibi mwa nchi ya Yoruba.

Kuchanganyikana kwa makundi ya kikabila na kimbari kulipelekea kwenye mabadilishano makubwa ya mawazo na vitu vya kitamaduni, au kuliimarisha mabadilishano ya aina hiyo pale ambapo tayari yalikuwepo. Waaja wa Badagry waliiga asasi ya u-*Oba* ya Wayoruba.

Athari za kitamaduni za Oyo, kama vile ibada za Muungu aitwaye Sango, viunzi vya kufumia vya wanaume, na ngoma za kuning'iza begani, zilienea mashariki mwa nchi ya Yoruba. Halikadhalika, athari ya Benin yaweza kuonekana katika sherehe na nembo za kifalme, na vyeo vya kichifu huko Owo, Ekiti, Akoko, Ondo, Ijesa na miongoni mwa Waawori. Athari za kisiasa na kitamaduni za Benin zilienea pia hadi kwa Waitsekiri, Waurhobo, Waisoko, na wazungumzaji wengine wa Kiedo.



26.6 Sanamu ya mwanaume akimwakilisha Mfalme Gezo 1818-58.



26.7 Mfalme Glélé aliyesimama, labda (1858-89) akionyeshwa kiishara kama simba.

Badiliko jingine muhimu katika karne ya kumi na tisa lilikuwa ni kusambaa kwa makazi katika maeneo ya pwani yaliyokuwa yamekaliwa na watu wachache. Hili lilisababishwa na mambo mengi. Kwanza kabisa, vita vya karne ya kumi na tisa vilisababisha maeneo ya pwani ya kinamasi kuwa kimbilio la kuvutia kwa wahamaji waliokuwa wanayakimbia maeneo ya vita huko bara ambayo yalikuwa wazi zaidi.

Pili, biashara ya Wazungu ya kuvuka bahari polepole ilikuwa inachukua umaarufu kuliko biashara ya nchi kavu kwa sababu ya mabadiliko kutoka biashara ya watumwa kwenda kwenye biashara "halali", na hivyo kuyapatia maeneo ya pwani faida ya kiuchumi ya uhakika. Mwisho, kulikuwepo na kukua kwa uhakika kwa shauku ya Wazungu huko pwani, na jambo hili lilipanua dhima ya kijadi ya miji kadhaa ya pwani kama vile Lagos, Porto Novo na Kotonu, ambayo ilichukua wajibu mpya wa ziada, sio tu kama bandari, lakini pia kama vituo muhimu vya shughuli za Wazungu, na miji mikuu ya baadaye ya nchi za kikoloni zilizokuwa zinaanzishwa, na nchi huru za Kiafrika zilizozirithi.

Hata hivyo, sababu za kiuchumi zilichukua nafasi kubwa sana katika mabadiliko yote haya, hasa kwa kuzingatia kuwepo kwa Wazungu. Wakati biashara iliwaingiza Wazungu katika ukanda huo, ilihalalisha pia kuendelea kuwepo kwao mahali pale. Kwa hivyo

mabadiliko ya biashara ya watumwa hadi kupata biashara "halali" yalihitaji marekebisho makubwa ya kimuundo kutoka kwa wafanyabiashara wa Kizungu. Hata hivyo, kwa upande wa Waafrika, licha ya msisitizo uliowekwa katika kusitasita kwa madola ya Kiafrika kuachana na biashara ya watumwa, na mapambano yao dhidi ya wakomeshaji wa biashara hiyo, mabadiliko haya kwa kweli yalifanywa kwa utulivu mkubwa. Mfano wa Dahomey unathibitisha jambo hili vizuri sana. Dahomey ilikuwa msafirishaji mashuhuri wa watumwa kutoka pwani ya Afrika ya Magharibi na iliendelea katika nafasi hiyo hadi mwaka 1888 wakati utumwa ulipokomeshwa huko Brazil. Lakini wakati ilipokuwa ikisafirisha watumwa, ilianza pia kuongeza biashara yake ya mafuta ya mawese kuanzia katikati ya karne ya kumi na tisa, kwanza kama nyongeza ya biashara ya watumwa, na hatimaye kuwa bidhaa muhimu katika uchumi wa taifa. Mbadiliko haya kutoka biashara ya watumwa kuingia biashara "halali" yalimaanisha kwamba watumwa wengi zaidi walihitajika kwa uzalishaji wa mafuta ya mawese. Hivyo, kama ilivyokuwa katika maeneo mengine ya ukanda wa Mono-Niger, mateka wa kivita ambao vinginevyo wangeuzwa nje kama watumwa walitumika sana katika sekta ya kilimo.

Matokeo muhimu sana katika shughuli hizi za ukomeshaji wa biashara ya watumwa ni yale yaliyohusishwa na mchakato wa kuleta mabadiliko ya kisasa, na katika jambo hili, kurudi kwa watumwa waliochiwa huru kutoka Sierra Leone, Kuba na Brazil kulikuwa na maana kubwa zaidi. Ilikuwa ni hawa "Wasaro" na Wabrazili ambao mwanzoni waliwavutia wamisionari wa Kikristo na kuchukua dhima muhimu kama kizazi za kwanza cha tabaka la kati katika kipindi hicho. Miongoni mwao walikuwemo watu kama Askofu Samwel Ajayi Crowther, Mchungaji James Johnson, na mamia ya watu wengine wasiokuwa mashuhuri ambao waliingia katika amali mbalimbali kama vile useremala, usanii na ujenzi wa majengo, ushonaji na uchapaji.

Kwanza kabisa walilowea pwani kwenye maeneo kama vile Whydah, Agwe, Porto Novo, Badagry na Lagos, na kutoka huko athari zao zilienea ndani katika bara la Aja na Yoruba. Wakati athari za Wasaro zilionekana zaidi sehemu zilizokuwa zimeathiriwa na ukoloni wa Waingereza, Wabrazili walijizatiti zaidi katika maeneo ambayo hapo baadaye yalikuja kuwa chini ya utawala wa Wafaransa. Hata hivyo, pamoja na tofauti hizi, wote kwa pamoja, Wasaro na Wabrazili, walitoa mchango mkubwa sana kwenye maendeleo ya ukanda wa Mono-Niger kwa ujumla.

Zaidi ya hayo, Wabrazili, ama katika Lagos au Porto Novo, walikuwa na uhusiano wa kifamilia, sio tu miongoni mwao wenyewe, bali pia na kule walikotoka katika Dunia Mpya. Jambo hili lilifanya kiungo cha Brazil kuwa mfano, sio tu wa umoja wa historia ya Afrika, bali pia wa uhusiano uliopo kati ya kontinenti la Afrika na diaspora (sehemu walikotawanyikia) ya watu weusi kote duniani.

# 27

# Delta ya Mto Niger na eneo la Kameruni

## *Utangulizi*

Eneo linalozungumziwa katika sura hii ni ukanda wa pwani wa Bahari ya Atlantiki unaoanzia kwenye mlango wa Mto Benin upande wa magharibi na kuishia kwenye mlango wa bonde la Ogowe upande wa mashariki. Ukanda huu unaweza kugawanywa katika maeneo matano. Eneo la kwanza linajumuisha sehemu yenye vijito na vinamasi katika delta ya Mto Niger inayokaliwa na Waijo na Waitsekiri kwenye ukingo wake wa magharibi. Katika bara ya magharibi ya eneo hili kulikuwa na ufalme wa Benin. Eneo la pili ni lile la bara ya Igbo ambayo iko kaskazini mwa delta ya Niger na imeenea zaidi mashariki mwa Niger. Bonde la Mto Cross ambalo liko mashariki mwa delta ya Niger ndilo eneo la tatu. Eneo hili lina Waefiki, Waibibio na jamii nyingine zenye kuhusiana na Wabantu. Eneo la nne ni lile la pwani ya Kameruni na bara yake mashariki mwa bonde la Mto Cross, na la mwisho ni bonde la Ogowe na maeneo yanayolizunguka ya Guinea ya Ikweta na Gabon.

Wakazi wote wa maeneo haya wanatokana na kundi la lugha la Niger-Kongo. Mahusiano ya awali baina yao yalitiwa nguvu na mahusiano ya biashara katika karne ya kumi na tisa. Njia za biashara zilitoka magharibi hadi mashariki mwa eneo hili, na nyingine zilitoka pwani hadi bara, zikiunganisha watu wa makundi mbalimbali. Mito ilikuwa muhimu kwani ilikuwa ndio njia kuu za biashara zilizokutanisha watu tofauti tofauti pamoja.

Jambo jingine la pamoja katika historia ya eneo hili lilikuwa kuweko kwa Wazungu pwani na hivyo kuwafanya watu wawe na mtazamo unaofanana (kuhusiana na Wazungu hao). Watu wa pwani walipitia mabadiliko katika asasi zao za kisiasa kutokana na chachu hiyo kutoka nje. Chachu hiyo ilikuja kwa njia ya biashara ya watumwa na athari ya kupigwa kwake marufuku mnamo karne ya kumi na tisa; badiliko la kuuza bidhaa nyingine za maeneo hayo badala ya watumwa ("biashara halali"); kuingia kwa wamisionari wa Kikristo kwenye eneo hili, na kuanza kwa ubeberu wa Ulaya na ukoloni. Tutayachambua maendeleo hayo tutakapolijadili kila eneo ili kupata picha halisi ya historia ya karne ya kumi na tisa ya delta ya Niger na eneo la Kameruni.




27.1 *Delta ya Niger na Kameruni mnamo karne ya kumi na tisa (kulingana na E.J. Alagoa).*

## Delta ya Niger

### Delta ya magharibi

Ufalme wa Itsekiri ndio uliokuwa kituo muhimu zaidi cha siasa na biashara katika delta ya Magharibi kuanzia karne ya kumi na tano hadi mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Makundi mengine katika eneo hili kama yale ya Waijo, Waurhobo na Waisoko hayakuwa na tawala unganifu. Katika biashara Waitsekiri walikuwa ndio walanguzi baina ya jamii hizi nyingine na Wazungu waliofika pwani. Juu ya kuwa Waitsekiri walikuwa walanguzi, hadi kufikia karne ya kumi na tisa, Wazungu wengi waliofanya biashara walisafiri kupitia Mto Benin hadi bandari ya Ughoton kufanya biashara moja kwa moja na mawakala wa *Oba* wa Benin ambaye alitambulika kuwa ndiye mwenye nguvu zaidi katika eneo hili.

Katika karne ya kumi na tisa, madaraka ya Benin yalianza kufifia katika delta ya Magharibi. Bandari ya Benin ya Ughoton iliacha kuwa kituo cha biashara na nchi za nje. Hivyo wafanyabiashara wa Kiitsekiri wakawa wadhibiti hasa wa biashara ya eneo hili, na ilibidi Benin ipate bidhaa za Kizungu kupitia kwao.

Ili kudhibiti biashara ya mto Benin, Olu Akengbuwa, mtawala wa ufalme wa Itsekiri mnamo nusu ya kwanza ya karne (ya kumi na tisa), alitumia mawakala aliowaita "Magavana wa Mito". Gavana alikusanya ushuru kutoka kwa wafanyabiashara wa Kizungu na alipanga bei ya bidhaa za wenyeji. Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa utaratibu ulioeleweka wa kuteua magavana, na kwa sababu ya manufaa yaliyotokana na ugavana, kuingia katika cheo hicho kukawa ni suala gumu baada ya kifo cha Akengbuwa mwaka 1848. Migongano iliyotokana na ugomvi wa kupata cheo hiki iliwafanya Wazungu waingilie kati masuala ya Waitsekiri. Waingereza, kwa mfano, hawakusita kuchukua fursa hiyo kuwaweka na kuwatoa magavana wengi kwa utashi wao. Kwa kweli, Nana Olomu (1884-94), gavana wa mwisho na aliyekuwa maarufu zaidi wa mto Benin, ilibidi apigane vikali na Waingereza katika harakati zake dhidi ya kuingia kwa utawala wa kikoloni, ingawa mwishowe alikamatwa na kuhamishiwa Kalabar.

Waijo wa delta ya magharibi walidhibiti njia nyingi za majini za eneo hili. Kwa vile hawakuweza kuwafikia moja kwa moja wafanyabiashara wa Kizungu, waliishia katika uharamia na kushambulia vyombo vya Waitsekiri na Wazungu. Lakini hawakuishia hapo tu. Baadhi yao walifanya biashara ya ndani na Waitsekiri na makundi mengine yaliyoishi kandokando ya delta ya Niger na Mto Niger kwa kuelekea baharini.

Katika kipindi chote cha karne ya kumi na tisa, delta ya magharibi haikuwa kituo muhimu cha biashara ya nje ya watumwa na mazao ya michikichi kama ilivyokuwa delta ya mashariki. Hali hii ilithibitishwa na ukweli kwamba hadi kufikia miaka ya 1840 kulikuwa na kampuni mbili tu za Kiingereza, na athari ya ukoloni wa Kiingereza ambayo ingewakilishwa na ofisi ya kibalozi katika eneo hili, haikujitokeza hadi makamu balozi mdogo alipopelekwa Sapele mwaka 1891. Hadi kufikia wakati huu, kinyang'anyiro cha nchi za Afrika kilikwishaanza, na Nana Olomu tayari alikwishaanza kupigana na utawala wa kikoloni ambao uliwaingiza wamisionari wa Kikristo katika delta ya magharibi.



27.2 Nana Olomu wa Itsekiri

## Delta ya mashariki

Delta ya mashariki inajumuisha madola kadhaa ya miji kama vile Boni, Nembe, Okrika na Elem-Kalabari ya karne ya kumi na tisa. Mambo makuu matatu yalisababisha kukua kwa madola haya. Mambo hayo ni: hali tofauti ya ekolojia ya mabwawa ya mikoko ya delta ya mashariki; biashara ya masafa marefu iliyofanywa na bara ya Igbo, na biashara na delta ya magharibi. Katika madola haya, biashara ilikuwa chini ya watawala: Wafalme walioitwa *amanyanabo* na wakuu wa koo walioitwa wakuu wa kaya.

Kukomeshwa kwa biashara ya watumwa na Waingereza mnamo 1807 kulileta mabadiliko mengi katika delta ya mashariki. Kwanza, juhudi za kukomesha biashara ya watumwa zilileta uhusiano mpya baina ya maafisa wa Kiingereza na madola ya delta. Ikawa mwanzo wa diplomasia ya kutumia mizinga ambapo mabalozi wa Kiingereza walitumia majeshi ya wanamaji kufikia maafikiano yaliyowanufaisha wafanyabiashara wao, wamisionari na wapelelezi. Mikataba mingi ilitiwa saini baina yao na machifu wenyeji; mikataba hiyo ilizuia biashara ya watumwa iliyofanywa na machifu na kuwataka kufanya biashara ya bidhaa nyingine. Mikataba hiyo iliweka pia kanuni za

kuendesha biashara halali, liliweka bayana kiasi cha ushuru cha kulipwa nawafanyabiashara, na ruzuku ambazo serikali ya Uingereza ingewalipa machifu kwa kukubali kuacha biashara ya watumwa.

Zaidi ya hayo, baadhi ya shughuli za Waingereza pwani zilipunguza nguvu za watawala wenyeji polepole. Mfano dhahiri ulikuwa ni uanzishwaji wa mfumo huria wa sheria uliojulikana kama Mahakama za Haki uliofanywa na wafanyabiashara wa Kiingereza kwa kushirikiana na wakuu wachache wa kaya au machifu lakini chini ya udhibiti wa Waingereza. Wakati huohuo, wamisionari na wafanyabiashara wa Kiingereza walijaribu kuingia bara, kwa mfano, kwa kudhamini safari za upelelezi. Kuvumbuliwa kwa mlango wa Mto Niger kulitokana na safari kama hizo na kuliongeza shauku ya wafanyabiashara na wamisionari wa Kiingereza juu ya bara ya Nigeria.

Wamisionari wa Kikristo, hasa wa CMS walianza kuwa na mashiko katika delta ya mashariki. Chini ya uongozi wa Askofu Samuel Ajayi Crowther, CMS ilianzisha misheni Boni mwaka 1864, Nembe mwaka 1868, Elem Kalabari mwaka 1874 na Okrika mwaka 1880. Watawala wa Boni na Nembe waliwakaribisha wamisionari kwa sababu kadha: kuanzisha shule ambamo watoto wao wangejifunza kusoma, kuandika na kusema Kiingereza ili waweze kuwa na mahusiano ya kibiashara na makampuni ya Kiingereza. Hali hiyo ingefanya uhusiano wao na Serikali ya Uingereza iliyowakilishwa na mabalozi na maafisa wa wanamaji uwe mzuri na kuwawezesha kuwa na nguvu kuwazidi maadui zao wa jirani ambao walikuwa wakipambana nao katika kuwania madaraka. Hata hivyo, wamisionari hawakupendwa kwenye maeneo yote. Watu wengine waliokuwa na mamlaka kwenye madola ya delta walipinga kuanzishwa kwa misheni za Kikristo katika maeneo yao na Ukristo ukawa sababu mojawapo ya kutokuwepo kwa utulivu wa kijamii katika karne ya kumi na tisa.

Madola ya delta yalipitia vurugu za kijamii na kisiasa karne ya kumi na tisa ambazo zilitokana na matatizo yaliyoletwa na mabadiliko ya kiuchumi kutoka katika uchumi uliotegemea biashara ya watumwa hadi katika uchumi uliotegemea mazao ya michikichi. Jambo hili halikuleta tu mabadiliko katika tabia na njia za zamani za biashara, bali yaliibua pia viongozi wapya wajasirimali badala ya wale wa zamani. Maendeleo makuu matatu makubwa yaliletwa na mabadiliko haya; kwanza biashara mpya iliongeza biashara ya ndani ya watumwa ili kukidhi haja ya nguvukazi kwenye madola ya delta; pili, ukuaji wa kaya mpya na wakuu wake ulisababisha vurugu katika siasa za ndani; na, tatu, ushindani wa kupata masoko ya bara ulisababisha vita kadha kwenye madola ya delta.

Watumwa walikuwa ni sehemu ya maisha ya madola ya delta kwa muda mrefu kabla ya karne ya kumi na tisa, na kila jamii ilikuwa na njia zake za kuwasimilisha. Hata hivyo, idadi ya watumwa waliotakiwa kushirikishwa katika jamii iliongezeka sana katika karne ya kumi na tisa, hivyo kila dola lilibidi litafute njia mpya za kuwaingiza kwenye utamaduni wa jamii zao kulingana na hali hiyo. Watumwa walipata haki kamili za wanandugu wa koo za mabwana zao na waliweza kupewa vyeo kulingana na uwezo wao, hata kuwa wakuu wa kaya. Vyama vya siri kama vile vya *Ekine* au *Sekiapu* vilitumiwa pia kuwatamadunisha watumwa kama hao; na huko Elem Kalabari, watumwa



27.3 *Mfalme Jaja wa Opobo*

27.4 *Nyumba ya Mfalme Bell mnamo miaka ya 1840*



ambao hawakujifunza haraka mila waliadhibiwa na chama kingine kilichoitwa *Koronogbo*.

Hata hivyo, jinsi idadi ya watumwa walioingizwa kwenye jamii ilivyozidi ili kukidhi haja ya biashara ya mafuta ya mawese, kaya nyingi za machifu wadogo zikawa kubwa mno hata kusababisha zigawanyike kutoka kwenye kaya kuu na kuunda kaya zao. Hali hii ilipunguza fahari na mali ya kaya za zamani kwa vile wanakaya walihamia kwenye kaya tajiri zaidi kutokana na madeni au sababu nyinginezo. Ushindani huu wa kuwania biashara na watumwa ulileta mabadiliko katika uongozi wa siasa wa madola. Huko Boni, kwa mfano, mapambano ya madaraka kati ya makundi mawili ya kifalme mnamo miaka ya 1860 yalisababisha kujitenga kwa kundi moja lililoongozwa na Jaja wa Opobo, na kuanzisha dola lake lenyewe la Opobo mwaka 1869. Mapambano ya namna hiyohiyo yalitokea Elem Kalabari kati ya 1882-84, na matokeo yake yalikuwa ni kuvunjika kwa dola hilo na kuanzishwa madola mapya ya Bakama, Buguma na Abonema. Huko Nembe na Okrika hakukutokea vurugu kubwa katika mfumo wa kisiasa. Hii labda ni kwa kuwa walipata machafuko ya kisiasa mwanzoni mwa karne ya kumi na nane na hawakushiriki katika biashara na nchi za Ulaya katika kiwango kikubwa kama Boni na Elem Kalabari.

Zaidi ya vurugu za ndani katika madola ya delta, kulikuwa na vita baina ya makundi yaliyoshindania masoko ya bara katika karne ya kumi na tisa. Elem Kalabari ndio ilikuwa kiini cha vita hivyo vyote. Ilipigana na Nembe iliyokuwa magharibi kwake, Boni iliyokuwa kusini mashariki na Okrika iliyokuwa mashariki. Madola haya mengine yalishirikiana katika vipindi mbalimbali. Dola jipya la Opobo ndilo lilikuwa rafiki pekee wa Elem Kalabari kwenye robo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa.

Wakati huohuo, mabalozi wa Kiingereza waliokuwa pwani walijaribu kutumia fursa hiyo ya vurugu zilizotokana na vita baina ya madola kufungua njia kwa ajili ya wafanyabiashara wao na wamisionari kuingia bara. Ili kufanikisha azima hiyo, mabalozi hao walijifanya wasuluhishi kati ya madola ya delta. Hata hivyo, vita hivyo havikudhoofisha nia ya kila dola ya kuwazuia wafanyabiashara wa Kizungu kuingia katika ardhi yake. Hali hii ilisababisha migongano mingi baina ya Waingereza na madola ya delta ambayo mwishowe ilisababisha kuingizwa kwa utawala wa kikoloni katika eneo hili mwishoni mwa karne hiyo.

### Bara ya Igbo

Uigbo ilikuwa na idadi kubwa ya watu na madola madogomadogo. Hali hii iliwafanya waathiriwe na watafuta watumwa kwani hakukuwa na dola kubwa lililoweza kuwalinda watu wake. Vikundi mbalimbali vya Waigbo vilipigana vita ili kukamata watumwa ambao waliwauza kwa madola ya delta na kwa Waefiki ambao ndio walikuwa walanguzi wa watumwa. Kwa vile Uigbo ilikuwa bara, haikuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Wazungu kabla ya karne ya kumi na tisa, ingawa ndiyo iliyotoa watumwa wengi waliouzwa pwani. Hata sehemu za nchi ya Igbo zilizojulikana kwa wageni wa Kizungu hadi mwishoni mwa karne hiyo ni zile zilizokuwa kwenye njia za mito kama Niger, Imo na Cross. Jumuiya za maeneo hayo ni pamoja na Waakwette, Waohombele wa mto Imo, Waaboh, Waosomari, Waoguta, Waasaba na Waonitsha wa mto Niger.

Waaro, ambao walidhibiti njia za biashara ya ndani na baadhi ya masoko, walijulikana kama wafanyabiashara na wasimamizi wa mzimu maarufu.

Ingawa biashara ya watumwa ilipigwa marufuku na Waingereza mwaka 1807, na iliendelea huko pwani hadi karibu na 1850, lakini huko Uigbo iliendelea kwa karne nzima na kuwa sababu muhimu ya mabadiliko ya kijamii. Biashara ya watumwa ilileta vurugu Uigbo. Kwanza, njia ya kuwapata watumwa ilikuwa ni kwa kuwateka nyara, uvamizi na vita ambavyo viliharibu miundo ya kijamii na kisiasa. Pili ilivuruga shughuli za kawaida za kilimo. Zaidi ya hayo, walichokipata Waigbo kutokana na watumwa hakikulingana na hasara iliyotokana na biashara hiyo. Mifano ya vitu vilivyobadilishwa na watumwa ni vileo, bunduki, kofia, shanga, nguo, chuma, shaba na mikuo, vingi vya hivyo vikichukua nafasi ya bidhaa zilizozalishwa na wenyeji na kuzuia ukuzi wa viwanda vya wenyeji.

Wapelelezi ndio waliokuwa Wazungu wa kwanza kuingia katika bara ya Igbo; baadaye wafanyabiashara na wamisionari walifuata. Kituo cha kwanza cha biashara kilianzishwa na Macgregor Laird huko Onitsha mnamo 1856. Mnamo 1886, kampuni ya Royal Niger ilianzisha ghala lake kuu katika Uigbo huko Asaba. Shughuli za wamisionari, zikiongozwa na CMS, zilianzishwa pia miongoni mwa Waigbo wa Niger.

Hata hivyo, Waigbo walipinga sana kuingiliwa katika nchi yao. Vyama vya siri vya magharibi mwa Uigbo vilivyoitwa *ekumeku* vilianzisha mapigano makali kati ya 1898-1911. Lakini Waingereza waliuzima upinzani huo kikatili. Msafara wa Aro wa 1900 uliofanywa na Waingereza kuwatiisha Waigbo ndio ulioashiria kushindwa rasmi kwa watu wa Uigbo. Hata hivyo inafaa ieleweke kwamba wakati wa msafara huo hakuna jeshi lililojitokeza kuwapinga Waingereza, kwani upinzani wa Waaro kwa mamlaka ya Waingereza haukuwa wa kijeshi, bali ulikuwa wa kibiashara na wa kichinichini. Baada ya Waingereza kuishinda Uigbo, jamii iliweza kuathirika kwa urahisi na watu kutoka nje. Baadhi ya watu waliupokea Ukristo, lakini wengi waliendelea kushikilia utamaduni na dini zao za asili.

## *Bonde la Mto Cross*

Dola la Efiki la Kalabar lilitawala biashara ya bonde la Mto Cross. Cha kushangaza, Waibibio, ambao ndio waliokuwa wengi kwenye eneo hili, ndio walikuwa watumwa wengi waliouzwa nje kutoka eneo hilo. Bidhaa nyingine zilizouzwa nje na Waefiki zilitoka bara ya Igbo na bonde la juu la Mto Cross kupitia kwa wafanyabiashara wa Kiaro. Ingawa baadhi ya makundi ya wakazi wa bonde la Mto Cross, kama vile Waitu, Waumon na Waakunakuna, walijaribu kupata manufaa yabiashara baina yao na Waefiki kwa kudai ushuru na kwa njia nyingine, wengine walifanya biashara moja kwa moja na watu wa eneo la Kameruni kaskazini.

Muundo wa kijamii na historia ya Kalabar ilikuwa tofauti na ile ya madola ya delta. Kwa mfano, watumwa waliokuwa kwenye jumuiya mbili kubwa za Duke Town na Creek Town ambazo ziliunda dola la Efiki hawakushirikishwa kikamilifu kwenye jamii hiyo. Tofauti na jamii ya siri ya *Ekine* na *Seakipu* ya madola ya delta, madhehebu ya siri ya *Ekpe* ya Kalabar hayakuwaruhusu watumwa kupata mamlaka ya kisiasa.

Hata hivyo, wafanyabiashara, mabalozi na wamisionari wa Kizungu walikuwa na athari kubwa Kalabar. Ingawa mwanzoni wafanyabiashara hawakuruhusiwa kuanzisha vituo nchi kavu, walikuwa na athari kubwa ya kiuchumi kutoka kwenye meli zao zilizokuwa mtoni, wakitoa mikopo kwa wafanyabiashara wa Kiefiki na kuweka vikwazo vya kiuchumi kwa yeyote ambaye hakutimiza masharti yao. Baadaye walitumia fursa iliyojitokeza kutokana na mizozo miongoni mwa Waefiki kuwaingilia katika mambo yao.

Wamisionari wa CMS waliingia Kalabar mwaka 1846. Japo kituo cha misheni kilikuwa wazi kwa walioingia Ukristo na wakimbizi kutoka kwenye jumuiya, kilitumika pia kwa kazi za upelelezi. Wamisionari walichunguza mambo ya wenyeji na kutoa taarifa ya matukio kwa balozi wa Kiingereza. Aidha, waliingilia kati mambo ya wenyeji kwa njia nyingine.

Mwaka 1842, mkataba wa kuzuia biashara ya watumwa ulitiwa saini na watawala wa Kalabar ili kukomesha biashara hiyo, na ilikuwa walipwe fidia kila mwaka. Kuanzia wakati huo, mamlaka ya Waingereza kwa Kalabar yalizidi kuongezeka polepole hadi kufikia 1891, utawala wa Ulinzi ulipoanzishwa.

## *Obong wa Kalabari*

Asasi ya kifalme ya Kalabari ilikuwa na matatizo mengi mnamo karne ya kumi na tisa. La kwanza likiwa udhaifu wa *obong*, mfalme wa Kalabari. Tatizo hilo lilitokana na upya wa ufalme. Cheo cha mfalme au *obong* kilianzishwa karne ya kumi na tisa. Kabla ya hapo, huenda Kalabar ilitawaliwa na wakuu wa koo au watu walioshika cheo cha *Ekpe*. Pili, kuwepo kwa wafalme wawili walioshindana kulileta matatizo Kalabari: kulikuwa na mfalme mmoja Duke Town na mwingine Creek Town. Wote wawili waliweza kuwatawala wenzao waliokuwa na mahusiano ya kiukoo kama yao kwa sababu ya utajiri mkubwa walioupata kutokana na biashara ya watumwa. Tatu, kulikuwa na ushindani mkubwa wa vyeo baina ya viongozi kadhaa wa kisiasa na wanajumuiya wa chama cha *Ekpe*. Mara nyingine ushindani huo uliingiliwa kati na Waingereza. Tatizo la mwisho na labda kubwa zaidi la kisiasa la Kalabari lilitokea karne ya kumi na tisa pale cheo cha *obong* kilipoambatanishwa na biashara ya nje kikiwa na shughuli kidogo za mila au mamlaka. Mamlaka ya kutunga sheria na utendaji yalikuwa mikononi mwa viongozi wa chama cha *Ekpe*. Kazi kubwa ya *obong* ilikuwa ni kuwa mtu wa kati baina ya jumuiya za wenyeji na Wazungu.

Mamlaka ya wafalme wa Duke Town na Creek Town hayakuwa yaleyale kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Duke Ephraim wa Duke Town alikuwa ndiye chifu tajiri zaidi katika eneo la mto baina ya 1800-34, ambapo Eyo Honesty II wa Creek Town alikuwa mfanyabiashara mwenye mamlaka zaidi baina ya 1836-48. Zaidi ya hayo, mfalme wa Duke Town alihodhi cheo kikuu zaidi kilichotolewa na chama cha Ekpe, cheo cha *Eyamba*, ilhali kiongozi wa Creek Town alishika cheo cha pili cha *Obunko*.

Katika kipindi chote cha karne hiyo, ugomvi wa urithi wa ufalme wa Duke Town na Creek Town ulichukua nafasi kubwa ya shughuli za kisiasa kwenye Mto Cross, na hivyo kutoa fursa kwa Waingereza kuingilia mambo ya ndani ya watu wa eneo hili.

## Chama cha Ekpe na "Wadamu"

Chama cha *Ekpe* cha Kalabar kilikuwa ni jumuiya ya siri iliyojadili mambo ya jamii. Ndicho kilichotunga sheria na kushika mamlaka Kalabar katika karne ya kumi na tisa. Kilikuwa ni chama kilichopangwa kitabaka; kilikuwa na madaraja kumi na moja mwaka 1858. Watumwa waliingizwa kwenye madaraja ya chini na madaraja ya juu yalihodhiwa na maadinasi matajiri, ila madaraja mawili ya juu kabisa yalikuwa ni kwa ajili ya viongozi wa kisiasa wa Duke Town na Creek Town tu. Hivyo, Chama cha *Ekpe* kiliwabagua watumwa na maskini kwa sababu kupanda cheo kwenye chama hicho kuliwezekana tu kwa kulipa ushuru mkubwa, na jambo hili, pamoja na aina nyingine za ubaguzi, lilisababisha vurugu za kijamii za katikati ya karne ya kumi na tisa. Kwa upande mwingine, *Ekpe* inaweza kuonekana kuwa ni nguvu chanya katika mfumo wa siasa wa Kalabari kwani kuliwaunganisha waungwana matajiri na wenye mamlaka wote katika asasi moja.

"Wadamu" kilikuwa ni chama cha watumwa wa viungani ambacho kilianzishwa kupingana na utoaji wa kafara ya watumwa wakati wa vifo vya wafalme au wakuu wa koo. Chama hicho hakikugombania kuachiwa huru kwa watumwa wala hakikutaka kutwaa madaraka ya kisiasa kutoka kwa *Ekpe*. Walichofanya tu Wadamu ni kuja Kalabari kutoka kwenye viunga katika makundi makubwa kila kulipokuwepo na hatari ya watumwa kutolewa kafara kutokana na kifo cha mtu mkubwa, au kulazimishwa kula sumu. Chokochoko zao ziliilazimisha *Ekpe* itunge sheria mwaka 1850-51 kuzuia utolewaji wa binadamu kama kafara.

Kutokana na maelezo yaliyotangulia, ni wazi kwamba historia ya siasa na jamii ya Kalabari ilifanana na ile ya madola ya delta kuhusiana na athari kutoka nje zilizowakumba. Tofauti iko katika namna walivyoyakabili matatizo hayo yaliyotoka nje.

## *Pwani ya Kameruni na bara yake*

Pwani ya Kameruni ilikaliwa na jumuiya za Wabantu wa kaskazini magharibi ambao walikuwa wakulima, wawindaji na wavuvi. Pwani hii ilikuwa na mabwawa ya mikoko, vijito na milango ya mito, na nyuma yake ilipakanwa na misitu minene ya kitropiki. Wakazi wa pwani hii walijiweka chini ya vijiji huru, lakini mara nyingine baadhi ya vijiji vilikuwa na machifu wakuu. Miongoni mwa watu wa pwani kama vile Waduala, Waisuwu na wengineo, chama muhimu cha siri kilikuwa ni kile cha *Jengu* ambacho kilihusu ibada ya pepo wa maji. Kama ilivyokuwa kwa wakazi wa delta ya Niger, wakazi wa pwani ya Kameruni walikabiliwa na shinikizo kutoka nje, hasa za wamisionari, wafanyabiashara na mabeberu wa Ulaya. Shinikizo kubwa, kusema kweli, lilitoka kwa wapinzani wa biashara ya watumwa, kwani utumwa ulikuwa muhimu katika jumuiya za eneo hili.

Waduala walikuwa ni kikundi kimojawapo cha watu wa pwani ya Kameruni waliojiunga katika dola unganifu mnamo karne ya kumi na nane wakiwa na chifu mkuu. Hata hivyo, kutokana na ugomvi wa urithi, wafanyabiashara wa Kiingereza waliingilia kati mambo yao mnamo karne ya kumi na tisa, na hali hiyo ilisababisha mgawanyiko

katika siasa za Waduala. Lakini, ili kuhifadhi umoja wa kabila lao, Waduala waliunda baraza la watu mashuhuri lililoitwa *Ngondo* ambalo lilikuwa na wawakilishi kutoka vijiji mbalimbali vya Waduala.

Waisuwu walikuwa ni kikundi kingine cha watu wa pwani. Walianzisha makazi ya biashara yaliyoitwa Bimbia ambayo yaliundwa na vijiji vitatu vilivyotawaliwa na wakuu wa koo. Mamlaka ya watu hao yalitokana na nafasi yao ya ulanguzi katika biashara na nchi za nje. Mfanyabiashara-mtawala wa Bimbia aliyekuwa tajiri na maarufu zaidi ni Bile, ambaye katika enzi zake kulianzishwa mahusiano thabiti na Waduala. Kitamaduni, uanachama wao wa pamoja katika chama cha *Jengu* uliwaunganisha, na kibiashara, wafanyabiashara wa Bimbia na wa Duala walishirikiana katika kuendeleza biashara ya eneo hili pamoja na kuanzisha mahusiano ya pamoja na wakazi wa nyika za Bamenda zilizokuwa bara. Watumwa wengi waliofika pwani baina ya miaka ya 1820 na 1840 walitoka bara ya Bamenda na walipitia mikononi mwa wafanyabiashara wa Duala na Bimbia.

Kama ilivyoelezwa awali, kuzuiwa kwa biashara ya watumwa kulileta matatizo kwa wakazi wa pwani ya Kameruni. Hata hivyo, watumwa walikuwa bado sehemu muhimu katika kipindi cha mpito kutoka biashara ya watumwa hadi kufikia biashara halali. Hii ilitokana na ukweli kwamba nguvukazi ya watumwa ilitumiwa katika uzalishaji wa mafuta ya mawese, mise (kokwa za mawese) na bidhaa nyingine za kilimo. Kwa kweli, wafalme wa mto Kameruni waliwakodisha baadhi ya watumwa wao kwa Wazungu huko Fernando Poo na hii ilikuwa njia mojawapo ya kujipatia mali zaidi. Ili kuzuia biashara ya watumwa na kuanzisha biashara halali, mikataba kadhaa ilitiwa saini baina ya Waingereza na watawala wenyeji, na hii, pamoja na mambo mengine, iliwapa fursa Waingereza kuingilia siasa za wenyeji na polepole mamlaka ya watawala wenyeji yalipotea. Waingereza pia walitumia vijisababu vya ugomvi baina ya Wazungu na wafanyabiashara wenyeji katika ulipaji wa madeni ya kibiashara ili kuingilia kati mambo ya wenyeji.

Wamisionari walikuwa njia nyingine muhimu ya kuingia kwa Waingereza katika pwani ya Kameruni. Wamisionari wa Chama cha Wamisionari wa Kibaptisti wa Uingereza ndio waliokuwa wa kwanza kuingia katika eneo hili. Walianzisha makanisa, shule, karakana na viwanda vya uchapaji. Hata hivyo, upinzani wa wenyeji dhidi yao uliongezeka walipoanza kubatiza watu kwa wingi.

Biashara ya pwani ya Kameruni ilididimia kwenye miongo ya 1860 na 1870 na kuleta hisia ya ukosefu wa usalama miongoni mwa watawala wa eneo hili. Ni katika mazingira haya Wadachi (Wajerumani) walipoitwaa Kameruni Julai 1884. Upinzani dhidi ya utawala wa Wadachi ulitokea mara moja na uliendelea mpaka mwanzoni mwa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Lakini upinzani huo haukuwazuia Wadachi kuingia katika bara ya Bamenda na kudhibiti biashara ya bara.

## *Bonde la Ogowe na maeneo yanayolizunguka*

Bonde la Ogowe na maeneo yanayolizunguka yako kusini mwa Kameruni na analingana na nchi za sasa za Guinea ya Ikweta na Gabon. Eneo hili lilikaliwa na watu



27.5 *Mfanyabiashara wa Mto Ogowe, Wassengo, akiwa na pembe za ndovu na wanakaya wake wa kike.*

27.6 *Antchuwe Kowe Rapontchombo ("Mfalme Denis"), mtawala mmojawapo wa mto Ogowe, akiwa na mkewe mkubwa.*



wazungumzao Kibantu ambao walishiriki katika kilimo cha kuhamahama, uwindaji, uvuvi na sanaa. Watu hao waliunda makundi mengi ya kisiasa yenye ukubwa mbalimbali mnamo karne ya kumi na tisa, kuanzia madola ya vijiji hadi falme. Mazao ya shughuli zao za kiuchumi yalisababisha kuwepo kwa shughuli nyingi za kibiashara miongoni mwa jumuiya mbalimbali. Zaidi ya hayo, kufika kwa Wareno pwani mnamo karne ya kumi na tano kuliikuza sana biashara ya pwani.

Maendeleo haya ya shughuli za kibiashara pwani yalileta athari kubwa. Kwanza, yalisababisha jamii kadha kuhama, kama vile Wafang na Wakele ambao waliyaacha makazi yao ya asili na kutafuta maisha bora zaidi pwani. Pili, yalisababisha mabadiliko katika miundo ya kijamii ya wenyeji. Zaidi ya matabaka ya zamani katika jamii ambayo yaligawika katika matabaka matatu, yaani, wazawa menyu, machotara na watumwa, kuliibuka tabaka jipya la wafanyabiashara lililotokana na utajiri na ambalo lilihodhi biashara kubwa.

Kulikuwa pia na athari kubwa ya wazungu katika eneo hili. Mikataba ilitiwa saini kuanzia 1839 ambayo ilianzisha kituo cha biashara cha Wafaransa huko Gabon. Safari nyingi za upelelezi zilianzia kwenye kituo hiki na kupanua maeneo yaliyodaiwa na Wafaransa hadi bara. Wakati huohuo, wafanyabiashara wa Kizungu na wamisionari walitamakani katika eneo hili. Kwa mfano, kulikuwa na makampuni tisini ya biashara ya Wazungu katika bonde la Ogowe na maeneo yanayolizunguka ilipofika mwaka 1882. Aidha kulikuwa na vituo vingi vya wamisionari na shule.

Ingawa kulikuwa na athari hizi za kimagharibi, jumuiya za wenyeji ziliweza kudumisha utambulishi wao wa kitamaduni. Walipambana vikali na mawazo ya Kizungu ili kuhifadhi urithi wao wa kitamaduni.

## *Hitimisho*

Ingawa karne ya kumi na tisa ilishuhudia kuenea taratibu kwa athari za Wazungu katika eneo kubwa lililozungumziwa, sehemu za bara za eneo hili hazikuwa chini ya athari ya moja kwa moja ya Ulaya. Hata kwenye maeneo ya pwani, historia yao ya ndani ilitegemea sana mambo yaliyotokea kwenye eneo lenyewe kuliko yale yaliyotoka nje. Ndio maana jumuiya mbalimbali za pwani zilikabili changamoto zilizotokana na biashara ya watumwa na nchi za nje kwa njia tofauti kutegemeana na historia na mila zao maalumu. Hivyo vyama vya *Ekine* au *Sekiapu* vya dola la delta vilikuwa tofauti na chama cha *Ekpe* cha *Waefiki* au cha *Jengu* cha makundi ya pwani ya Kameruni.

Ingawa biashara na nchi za nje ilikuwa muhimu kwa jumuiya hizi, mikondo ya biashara ya ndani na mabadilishano ya bidhaa za wenyeji yaliendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa watu wengi katika karne yote ya kumi na tisa. Kwa maneno mengine, haifai kupuuza matukio ya ndani katika historia ya watu wa delta ya Niger na eneo la Kameruni katika karne ya kumi na tisa. Hii haina maana ya kukanusha kuwepo kwa athari kutoka nje, bali kuonyesha kuwa vipengele vya utamaduni na asasi za wenyeji viliendelea kuwepo licha ya athari ya Magharibi katika eneo hili.

# 28 Kutawanyika kwa waafrika duniani

## Utangulizi

Moja ya matukio makuu katika historia ya Afrika na ya Ulimwengu ni kuhama kwa Waafrika kwenda sehemu nyingine duniani chini ya biashara ya watumwa waliovushwa Bahari ya Atlantiki ama kwa njia nyingine. Kuhama huku kuliendelea kwa karne nyingi na kulisababisha kuwepo kwa jumuiya za Kiafrika zenye ukubwa mbalimbali si Ulaya tu lakini pia Mashariki ya Kati na Amerika.

Uhamiaji wa awali kabisa wa Waafrika huko Asia Ndogo na Mediteranea ulianza karne chache kabla ya enzi ya Kristo na kufikia kilele chake mnamo karne ya saba. Waafrika wengi walifika Mediteranea kupitia njia za biashara zilizovuka Sahara ambapo wengine walihamia kama watu huru, kama vile wanazuoni, mahujaji na wafanyabiashara kwenda Maka na Madina. Wengi wao pia walipatikana katika madola mengine ya Kiislamu kama vile ufalme wa Ottoman ambako walipata hadhi muhimu katika jamii.

Kuenea kwa Uislamu India na Mashariki ya Mbali pia kuliwaleta Waafrika wengi kama askari na warasimu waliotoa huduma katika sultani za Kiislamu kwenye eneo hilo. Pia, shughuli za kibiashara za Mediteranea ziliwaingiza Waafrika Ulaya kiasi kwamba mnamo karne ya kumi na tano kulikuwa na idadi kubwa ya Waafrika waliopatikana Sisilia, Kuprosi, Krete na pwani ya kusini ya Iberia. Watu Weusi huko Uingereza na Ufaransa waliongezeka haraka mwishoni mwa karne ya kumi na nane kutokana na mahusiano ya moja kwa moja ya ubaharia baina ya Ulaya na Afrika.

Mtawanyiko wa Waafrika ulikuwa dhahiri zaidi Amerika ambako walishiriki vilivyo katika maendeleo ya jamii za Dunia Mpya. Walisaidia katika kupoza maisha magumu ya maporini yaliyoenea katika Dunia Mpya na walishiriki kikamilifu katika kuunda jumuiya mpya. Baina ya karne ya kumi na sita na kumi na tisa Waafrika hawa walifanya shughuli zote za kijamii isipokuwa zile zilizopata hadhi za juu za kijamii. Hivyo, kabla ya kufutwa kabisa kwa biashara ya watumwa huko Amerika, Waafrika wengi walikuwa watumwa ambao walifanya kazi nyingi za mtulinga katika jamii hizo. Hali hiyo iliwawezesha wawe na athari kubwa katika lugha, utamaduni, uchumi na muundo wa kitaifa wa jumuiya nyingi za Dunia Mpya.

## Mashariki ya Kati na Asia ya Kusini Mashariki

Kulikuwa na sababu kadhaa zilizofanya Waafrika wahamie Mashariki ya Kati na Asia ya



28.1 *Kinyago cha mtu mweusi chenye kijambia cha Kiindonesia kwenye mshipi mgongoni; inawezekana kinatoa Vietnam ya sasa na inawezekana kimechongwa karne ya kumi na saba.*

Kusini Mashariki mnamo karne ya kumi na tisa. Sababu kubwa ilikuwa ni biashara ya watumwa. Chanzo kikubwa cha watumwa waliokwenda Asia kilikuwa Afrika ya Mashariki. Biashara ya watumwa iliyofanywa Zanzibar ilipeleka watumwa Ghuba ya Uajemi ambako waliuzwa tena kwenda kwenye masoko muhimu ya Asia ya Kusini Mashariki. Idadi kubwa ya watumwa ilitoka pia Ethiopia. Watumwa hawa kutoka Ethiopia walishikwa kutokana na vita mbalimbali vya eneo hilo na wakasafirishwa hadi pwani ambako walisafirishwa kwa meli na wafanyabiashara wa Kiarabu hadi kwenye masoko ya Arabuni na India. Watumwa wa Kihabeshi walikuwa wakipendwa sana katika maeneo haya kwa sababu ya akili na maumbile yao. Kisiwa cha Bukini kilikuwa chanzo kingine cha watumwa waliopelekwa India. Biashara hiyo iliendeshwa na wafanyabiashara wa watumwa kutoka Uingereza na Uholanzi, na wengi kati ya watumwa walionunuliwa walipelekwa kwenye makoloni ya Waingereza yaliyokuwepo India. Hata hivyo, Waafrika hawakuwa taifa pekee lililovimjari kwenye Bahari ya Hindi mnamo karne ya kumi na tisa. Wengine, kama vile Wamalaya, Wahindi na Wachina walihama kama watumwa au manamba.

Kuhiji Maka kulikuwa sababu nyingine ya kuhama kwa Waafrika ingawa lililkuwa ni tukio la kila mwaka. Mahujaji wengi kutoka Afrika Magharibi walifika Maka kupitia msafara wa Kairo au kwa kupitia bandari za bahari ya Shamu. Mahujaji wa Kiafrika waliokuwa matajiri walisafiri na watumwa wengi ambao waliwatumia kulipia gharama njiani. Hii inamaanisha kuwa watumwa walitumika kama njia ya kubadilishana bidhaa. Matokeo yake yakawa kuwepo Maka kwa watumwa wengi wa Kiafrika pamoja na waliotoka Asia, na hao walitawanywa na wanunuzi binafsi katika ulimwengu wote wa Kiislamu. Hata hivyo, watumwa hawakuwa Waafrika pekee waliokuwa Uarabuni. Baadhi ya waungwana wa Kiafrika walibaki baada ya hija na kuendelea na masomo ya juu ya dini kwenye miji mitakatifu ya Uarabuni Magharibi.

Hebu tuangalie kazi walizofanya Waafrika hawa katika baadhi ya jamii za watu wa Mashariki ya Kati na Asia. Huko India, watumwa wa Kiafrika walifanya kazi nyingi za nyumbani. Walitumiwa kama vibarua viungani, lakini hasa walitumika kama wafanyakazi wa ndani kama vile vijakazi, matowashi, wateka maji, vinyozi, walinzi na watunza farasi katika madola yenye wafalme. Katika makazi ya Waingereza yaliyokuwa India, watumwa wa Kiafrika walifanya kazi mbalimbali kama askari, mabaharia na makuli na wengine walijenga ngome. Pia, kwenye Funguvisiwa la Malaya watumwa wa Kiafrika walifanya kazi kama vibarua wa viungani, mafundi stadi, askari na wachimbaji. Huko Mashariki ya Kati, watumwa wa Kiafrika walishughulikia kazi za nyumbani wakiwa watumishi wa ndani, na pia kama mabaharia, askari, waendeshaji wa utawala na wasaidizi madukani mijini, ambapo huko mashambani walifanya kazi kama wateka maji, vibarua wa shamba, waendesha ngamia na wachungaji. Mahujaji maskini au wale waliokwama walifanya kazi pia kama wapagazi, wafagizi wa barabara, watema kuni, wapikaji pombe, makuli na wafinyanzi.

Watumwa wa Kiafrika, waliokuwa Mashariki ya Kati au Asia, walikuwa ni watu wa hadhi ya chini kabisa katika jamii. Walikuwa katika tabaka la watwana. Kwa mfano, hawakujumuishwa kwenye jamii za wenyeji wa Asia bali walitengwa na kubaguliwa.

Kwa hiyo waliunda kundi tofauti katika jamii. Huko Kusini Magharibi mwa Uarabuni, waliishi katika makazi tofauti kwa sababu walichukuliwa kama ni watu waliotengwa na jamii na hakuna Mwarabu menyu aliyeweza kumwoa mtumwa wa kike aliyeachiwa huru. Hata hivyo, jambo moja muhimu kuhusu jumuiya hizi zilizosambaa za Waafrika ni kwamba walikuwa na utaratibu mzuri wa maisha na waliendeleza mila za mataifa yao.

## *Mtawanyiko wa Waafrika Ulaya*

Waafrika walikuwepo Ulaya ya Magharibi tangu zamani sana lakini hawakuwa wengi. Idadi yao iliongezeka tu kuanzia karne ya kumi na tano ambapo Waafrika weusi, kwanza wakiwa watumwa na baadaye wakiwa huru walianza kuonekana Hispania ya Kusini na Ureno. Huko, hata waungwana wa Kiafrika walikuwa kwenye ngazi za chini za kijamii. Hadhi yao ya kisheria pia ilikuwa ya mashaka. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba ingawa utumwa haukukubalika katika sheria za Kifaransa na Kiingereza kuanzia karne ya kumi na saba na kumi na nane, uliendelea kuwepo kwenye makoloni yao ya ng'ambo mpaka karne ya kumi na tisa, na Waafrika huru waliokuwa Ulaya walifanywa kama Waafrika wenzao waliokuwa watumwa kwenye makoloni yaliyokuwa nchi za tropiki.

Hata hivyo, Waafrika huru walikuwepo Ulaya ya Magharibi kwa idadi ya kutosha kuanzia kati ya karne ya kumi na nane na kuendelea. Ingawa idadi yao ilikuwa ndogo ikilinganishwa na jumla ya watu katika nchi yoyote ya Ulaya, kuwepo kwao kulionekana wazi kuliko idadi yao halisi kwa sababu walijazana kwenye miji mikubwa. Kwa kweli kabla ya miaka ya 1840 kulikuwa na Waafrika wengi kutoka nchi za tropiki kuliko walivyokuwa Wazungu katika nchi za tropiki za Afrika.

Makundi haya ya Waafrika ya Ulaya yalijazana katika kazi maalumu. Mojawapo ilikuwa huduma za majumbani ambapo wengi walifanya kazi kama watumishi. Walijishughulisha pia na huduma za uchuuzi ambapo walifanya kazi kama mabaharia hasa Ureno. Kundi jingine dogo liliundwa na wanafunzi ambao walianza kuwasili Ulaya kati ya karne ya kumi na nane. Wengi wao walikuwa walinzi wa machifu tajiri wa Kiafrika ambao walikuja Ulaya kwa hisani ya wafanyabiashara ya watumwa wa Kizungu waliokuwa Afrika na walisoma Ulaya chini ya ulinzi wao. Sifa kubwa ya jumuiya za Waafrika zilizokuwa Ulaya ni kwamba zilikuwa na wanaume wengi zaidi. Ili kuendeleza jumuiya, Waafrika wapya waliletwa kila mara kutoka ng'ambo.

Waafrika walikuwepo pia Ulaya ya Mashariki. Walifika huko kupitia biashara ya watumwa ya Waturuki ambayo ilipata watumwa kutoka Afrika ya Kusini mwa Sahara na Afrika ya Kaskazini. Katika sehemu chache, makundi madogo ya Waafrika kwenye sehemu maalumu za ufalme wa Uturuki yalibaki na utamaduni wao hadi kufikia karne ya ishirini. Mfano ni jumuiya ndogo za wazungumzaji wa Kihausa katika eneo la sasa la Yugoslavia.

## *Mtawanyo wa magharibi wa Waafrika: Usuli wa karne ya kumi na tisa*

Mtawanyiko wa Waafrika ulikuwa mkubwa zaidi huko Amerika kuliko hata Asia na Ulaya. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, idadi ya Waamerika wenye asili ya



**28.2** *Mtumishi wa Kiafrika na towashi na mtoto wa bwana wao huko India Mashariki mnamo karne ya kumi na tisa.*

Kiafrika ilikuwa milioni 8.5 ukijumuisha waungwana na waliotiwa utumwani katika Dunia Mpya. Uzoefu wa watu hao weusi ulitofautiana kulingana na sababu kadhaa kama vile mlingano wa Wazungu na wasio Wazungu katika jamii; uwiano wa watumwa waliokuwa waachiwe huru; ukubwa wa biashara ya watumwa; jinsi kila koloni lilivyoendelea na mabadiliko ya kiuchumijamii katika eneo. Kwa mfano, katika mabara ya Amerika, watumwa na waungwana wa Kiafrika walioishi kwenye miji mikubwa walikuwa na fursa zaidi ya kupata hadhi ya juu na uhuru kuliko wenzao waliokuwa viungani. Hata hivyo, kwa jumla kiwango cha vifo kilikuwa cha juu kwa Waafrika wote walioishi katika Dunia Mpya. Wengi wao walikufa wakiwa watumwa na ilikuwa dhahiri kwamba jumla ya watu milioni 8.5 ya Waafrika na Waamerika wenye asili ya Kiafrika waliokuwepo katika mabara ya Amerika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa iliwakilisha watu wachache zaidi ya Waafrika walioingizwa kwenye bara hilo baada ya 1600.

Zaidi ya hayo, hakukuwa na tofauti kubwa juu ya uendeshaji wa utumwa katika maeneo mbalimbali ya Amerika. Ingawa ni kweli kwamba Amerika ya Kusini, kwa mfano, ilikuwa na uzoefu wa muda mrefu zaidi kuhusu utumwa kuliko makoloni mengine ya Waingereza na Wafaransa huko Amerika, hakukuwa na tofauti za kimsingi katika mfumo wa utumwa wa Amerika yote. Tofauti ilikuwa tu kwenye kiwango cha kushiriki katika biashara ya watumwa ya maeneo mbalimbali.

Uingizaji mkubwa wa watumwa wa Kiafrika katika Amerika ulikuwa huko Brazil. Katika kipindi cha biashara ya watumwa Brazil ilipokea kiasi cha 38% ya Waafrika walioingizwa Dunia Mpya. Hata hivyo, ili kuelewa tajiriba ya Waafrika kwenye Dunia Mpya inabidi tuangalie uwiano wa ushiriki wa maeneo mbalimbali katika biashara ya watumwa karne hadi karne. Utaratibu huo ni muhimu kwani tofauti za tarehe za kuingia katika biashara ya kuvuka Atlantiki na mabadiliko ya wingi wa watumwa walioingizwa kutoka kila eneo haukuathiri tu ueneaji wa watu bali pia misimamo ya jamii zilizoibuka huko Amerika ilipofikia mwisho wa karne ya kumi na tisa.

Kabla ya 1600, wakoloni wa Kihispania na Kireno waliokuwa kwenye Dunia Mpya walipokea watumwa wote wa Kiafrika waliofika kwenye bara hilo wakati huo. Waafrika hao hawakutumiwa tu kama wafanyakazi wenye gharama nafuu bali pia waliendeleza jamii kwani wenyeji wa Kihindi waliuawa na magonjwa mapya yaliyoletwa Amerika na Wazungu na Waafrika. Ilipofikia mwisho wa karne ya kumi na sita, Waafrika wa Dunia Mpya walijiona bora kuliko wenyeji wa Kihindi.

Karne ya kumi na saba ndio ilikuwa mwanzo wa biashara rasmi ya watumwa ya kuvuka Bahari ya Atlantiki. Katika karne hii idadi ya watumwa walioingizwa kila mwaka iliongezeka sana. Katika kipindi hiki tunashuhudia pia kushuka kwa ushiriki wa wakoloni wa Kihispania katika biashara ya watumwa. Brazil, hata hivyo, ilikuwa ndio mpokeaji mkubwa wa watumwa katika Dunia Mpya kwa ajili ya viunga vyake vya miwa.

Kilele cha mtawanyo wa Waafrika katika Dunia Mpya kilifikiwa katika karne ya kumi na nane. Jamii za viungani na biashara ya watumwa ya Amerika vilifikia upeo wake kamili. Ukuaji huu mkubwa wa biashara ya watumwa unaweza kudhihirishwa na

ukweli kwamba zaidi ya nusu ya Waafrika wote walioingizwa Dunia Mpya walifika wakati wa karne ya kumi na nane. Zaidi ya hayo, karne hii ndiyo ilikuwa wakati ambapo mahusiano ya biashara baina ya Afrika na sehemu nyingine za dunia yalishamiri. Brazil pia ilipokea watumwa wengi kuliko eneo jingine lolote la Amerika katika karne hii. Hivyo, kukua kwa jamii ya watumwa wa viungani wa Dunia Mpya kulikuwa dhahiri katika karne ya kumi na nane. Jinsi viunga vilivyoshamiri ndivyo uchumi wa biashara ya nje ulivyoongezeka na kuimarika. Mwisho, karne hii ndio kipindi ambacho unyonyaji na ugandamizaji mkubwa na wa kikatili wa Waafrika ulitokea katika Dunia Mpya. Wakati Wazungu wa makoloni ya Amerika walikuwa wakigombea uhuru wao, walijishughulisha sana kupunguza uhuru na haki za kisheria za watu wasiokuwa Wazungu.

## *Kipindi cha kuzuia biashara ya watumwa*

Karne ya kumi na tisa ilishuhudia uzuiaji wa biashara ya watumwa. Mfumo wa utumwa wa Kiamerika ulivurugika kutokana na mashambulizi ya ndani na nje. Uzuiaji wa biashara ya watumwa ya Kiingereza uliotokea 1808 uliathiri sana utumwa na Waafrika. Kampeni dhidi ya utumwa iliyofanywa na Waingereza ilipunguza idadi ya Waafrika waliopelekwa Amerika katika karne hii ingawa jumla yao ilibakia kuwa kubwa. Ilipofika 1870, ruwaza ya biashara ya watumwa ilirudia kuwa ile ya kabla ya 1600 ambapo makoloni ya Wahispania na Wareno yalikuwa ndio waingizaji wakuu wa watumwa. Watumwa waliobakia walikwenda kwenye makoloni ya Wafaransa kukiwa na idadi ndogo sana iliyoingia Marekani.

Waafrika wengi waliokuwa Amerika walifanya kazi kwenye mfumo wa viunga vya kilimo. Lakini kwa kuwa mfumo wa viunga ulitofautiana kote Amerika, Waafrika walikabiliwa na kani tofauti zilizounda utamaduni wao wenyewe wa Kiamerika hata kama idadi yao ilikuwa kubwa kiasi gani. Kwa mfano, kulikuwa na mabadiliko mengi yaliyohusu ibada ya Shango, Mungu wa Kiyoruba, na hata maumbo ya Shango yalitofautiana sana kuanzia Cuba, Trinidad, Haiti hata Brazil. Hali ilivyokuwa kwa ibada ya Shango ndivyo ilivyokuwa kwa vipengele vingine vya maisha ya watu. Hali hiyo ilitokana na ukweli kwamba ilibidi wajirekebishe kulingana na hali mpya waliyoikuta kwenye Dunia Mpya.

Zaidi ya hayo, hali ya Waafrika ilitofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine ya bara la Amerika. Huko Karibia ni Waafrika ndio waliokuwa wengi. Kwa upande mwingine, huko Marekani watu weusi walikuwa wachache ikilinganishwa na mataifa mengine. Katika baadhi ya sehemu za Amerika ya Kusini kama vile Ekwado, Chile na Argentina, kumekuwa na mchanganyiko mkubwa baina ya Waafrika, Wahindi wa Amerika na makundi ya Wazungu kiasi kwamba hakukuwa na wanu waliochanganya damu tu bali watu weusi "wamepotea" kabisa.

Pia, maendeleo ya watu katika maeneo mbalimbali ya Dunia Mpya hayakulingana na ushiriki wao katika biashara ya watumwa ya kuvuka Bahari ya Atlantiki. Kwa maneno mengine, maeneo ambayo yaliingiza watumwa wengi wakati wa biashara ya watumwa hayakuwa na watu wengi weusi ilipofika mwisho wa utumwa. Isipokuwa kwa Marekani, idadi ya watumwa ilipungua sana katika bara la Amerika kuelekea mwishoni mwa karne

ya kumi na tisa. Hii inaonyesha kwamba mfumo wa utumwa wa Kiamerika ulishindwa kuunda jamii inayojiongeza au ambayo inajizalisha kwa kiwango cha kutosha na kuongeza wafanyakazi. Mbaya zaidi, ni mabaki ya athari ya utumwa yaliyorudisha nyuma kwa kudumu uwezo wa watu weusi wa Amerika kushindana kwa ufanisi katika jamii ambamo walikuwa wachache.

## *Athari za Afrika*

Wakati ambapo mfumo wa utumwa wa Kiamerika ulikuwa ukivunjika mnamo karne ya kumi na tisa, jamii za Kiamerika zilikuwa zikichukia Waafrika na utamaduni wao kwa jumla. Hata hivyo, Waafrika wameathiri vipengele vingi vya jamii za Kiamerika, kama vile katika lugha, muziki, dini, vyakula, sanaa, kilimo na usanifu majengo. Katika baadhi ya sehemu, athari ya Waafrika imekuwa kubwa kiasi cha kuunda utamaduni tofauti wa Kiamerika wenye mwelekeo wa Kiafrika ambao ulishindana na mara nyingine ulishamirisha utamaduni uliotokana na Wazungu.

Nafasi ya Waafrika katika muundo wa siasa ilitofautiana sana Amerika. Huko Marekani, kulikuwa na mgawanyiko dhahiri baina ya weusi na weupe. Kusema kweli, mtu yeyote mwenye kiasi chochote cha Uafrika kwenye asili yake aliteremshwa kweye daraja la weusi. Hivyo Waamerika wenye asili ya Kiafrika wa Marekani waliunda idadi ndogo ya watu ambao hawakuwa na nguvu za kisiasa. Kinyume chake, katika sehemu nyingine zote zilizobakia za Amerika, jamii iligawanywa katika makundi matatu ya watu weusi, mchanganyiko na weupe. Hii ilikuwa na maana kwamba watu weusi waliunda kundi la jamii lililotambulika lenye haki zake za kisheria na upendeleo wa kijamii. Fursa za kuendelea kwa ajili ya watu weusi zilitofautiana kutoka mahali pamoja hadi pengine.

Wakati wa enzi ya utumwa, Waafrika wengi na Waamerika wenye asili ya Kiafrika walifanya kazi kama vibarua wa mashambani, au kwenye huduma za majumbani. Walijishughulisha pia na kazi nyingine tangu uuzaji duka hadi uchimbaji migodi. Ilipofikia mwisho wa karne ya kumi na nane, mifumo ya usafiri ya bara na pwani ya Jamaika ilihodhiwa na Waafrika. Hali hii haikubadilika sana baada ya utumwa kufutwa. Hata hivyo, fursa ya kujiendeleza na ubora wa maisha ya jumla ya weusi ulitegemea hali zilizowakabili moja kwa moja katika kila jumuiya. Katika jamii ambazo hazikuwa na utulivu, Waafrika na Waamerika wenye asili ya Kiafrika waliiathiri miundo ya jamii kwa faida yao.

Zaidi ya hayo, Waafrika walichangia sana kwenye jamii kama jinsi walivyofaidika nazo. Ubunifu wa Waafrika ulijidhihirisha zaidi kwenye makoloni ambayo idadi yao ilikuwa kubwa na ilibidi wajenge jamii yenye mshikamano kutokana na makundi tofauti ya watu ambao ingawa walikuwa weusi lakini walikuwa na asili tofauti. Hii inaonyesha kuwa hawakukaa tu bila kushika hatamu.

Wakati utumwa wa Waafrika ulipofutwa Amerika, nafasi ya Waafrika ilikuwa imeshuka sana ikilinganishwa na ilivyokuwa karne moja iliyotangulia. Kwa mfano Marekani kulikuwa na ubaguzi wa kisheria na kuwanyima haki za kijamii na uchumi watu wasiokuwa weupe. Sehemu nyingine, kama vile Cuba, Jamaika, Barbados na



28.3 *Toussaint L'Ouverture, kiongozi wa mapinduzi ya Saint-Domingue na Baba wa uhuruwa Haiti.*
*and fathe*

Brazil, Waamerika wachache wenye asili ya Kiafrika wachache walipata vyeo vyenye hadhi kijamii na nguvu za kisiasa. Huko Haiti, waliongoza nchi baada ya mapinduzi ya 1789.

Katika karne ya kumi na tisa, mafanikio ya Waamerika wenye asili ya Kiafrika yalikuwa makubwa. Juu ya vipingamizi vya Waamerika weupe na vikwazo vya kijamii na kiuchumi, Waafrika waliweza kuunda jumuiya zilizofanikiwa Amerika nzima. Walianzisha asasi za elimu kama vile vyuo vya Codrington huko Barbados na vyuo kadhaa Marekani. Waamerika wenye asili ya Kiafrika walikuwa na nafasi muhimu katika maendeleo ya teknolojia ya Amerika kwa kugundua mashine nyingi muhimu.

Juu ya kuwa maeneo waliyotawanyikia yalikuwa ya shida na magumu kwa watumwa wa Kiafrika, walikuwa wavumilivu na walitumia vyema fursa walizozipata. Miaka mingi ya taabu, kuvuja jasho na mapambano ilitokea kuwa sehemu muhimu ya maisha ya jamii nyingi za Kiamerika.

## *Afrika na maeneo ya mtawanyiko wa Waafrika*

Suala la mtawanyiko wa Waafrika huko Amerika limekuwa likiangaliwa kila mara kwa viwango tofauti vya uzingatiaji na Waamerika weusi na weupe. Huko Marekani, wazo la kuwarudisha Waafrika lilianzishwa. Urudishaji huo ulianza kwa uthabiti baada ya 1815 na ilipofika 1830 Liberia ikawa koloni la Waafrika waliorudishwa. Watumwa wa zamani, waliopata uhisani wa jamii za wakoloni na msaada wa fedha wa Serikali ya shirikisho na majimbo mengi, ndio waliunda kundi kubwa la Waafrika waliorudi. Baadhi walikuwa ni Waafrika waliotoka kwenye meli zilizokamatwa mnamo karne ya kumi na tisa na kurudishwa Afrika na Waingereza. Wengine walikuwa ni wamisionari walioajiriwa kusini ya Marekani kusaidia kueneza Injili ya Kikristo Afrika Magharibi.

Hata hivyo, ni maelfu machache tu ya Waafrika walirudi nyumbani ikilinganishwa na mamilioni waliokwenda Dunia Mpya. Hii ilitokana na sababu nyingi. Kwanza, hakukuwa na msaada wa kuanzisha mfumo wa usafiri uliolingana na ule uliowapeleka watumwa Amerika kwa ajili ya kuwarudisha Afrika. Pili, kurudi Afrika wakati wa karne ya kumi na tisa hakukuwa na marupurupu ya kutosha kwa Wazungu au wasio Wazungu.

Kwa hiyo, ilipofika mwishoni mwa karne ya kumi na tisa wazo la kurudi Afrika lilikufa polepole. Waamerika wenye asili ya Kiafrika walijishughulisha na maendeleo yao kwenye mazingira waliyokuwemo. Walijizatiti katika kujijengea maisha mazuri na kutumia vizuri fursa zozote zilizojitokeza mbele yao.

Hivyo, mpango wa kurudi Afrika ulififia polepole lakini haukufa kabisa. Wahamasishaji kama vile Henry Sylvester Williams na baadaye Marcus Garvey waliibuka mwaka 1897 na katika miaka ya 1920, na walitoa uhai mpya kwa mpango huo wa kurudi. Hivyo hadi Chama cha Maendeleo ya Jumla ya Wanegro cha Marcus harvey kilipokufa mwaka 1927, Afrika ilikuwa imeanza kuingia kwenye mwanga wa habari za dunia.

# 29

## *Hitimisho: Afrika kwenye mkesha wa ushindi wa Wazungu*

### *Utangulizi*

Sura hii ya kuhitimisha itaangalia maendeleo makuu ya historia ya Afrika mwishoni mwa robo ya tatu ya karne ya kumi na tisa. Msisitizo maalumu utakuwa kwenye muongo wa 1875-85 ambao ulishuhudia ongezeko kubwa la maslahi ya Ulaya katika Afrika, na kupelekea kwenye kinyanga'nyiro cha Wazungu kugombana nchi za Afrika, na hatimaye kutekwa kwa Afrika. Kulikuwa na mielekeo mingine iliyofanana katika maendeleo ya Afrika ilipokaribia kutekwa na Wazungu, mmojawapo ukiwa ni juhudi za viongozi mbalimbali wa Afrika za kujizatiti wao na madola yao. Majaribio hayo, hata hivyo, yalikwamishwa na kuwepo kwa Wazungu.

Sura za juzuu hili zimeonyesha kuwa karne ya kumi na tisa ilikuwa ni kipindi cha mabadiliko makubwa katika Afrika. Tumeona pia kwamba mabadiliko yaliyokuwa na athari kubwa na ambayo yalienea sana yalitokana na sababu za ndani. Mabadiliko mengine yalitokana na athari za, na hata kuanzishwa na, shughuli za Wazungu waliokuwa pwani na walioanza kuingia bara baada ya 1850. Mabadiliko hayo yalileta matokeo na mielekeo iliyotofautiana na mara nyingine hata kupingana. Kwa mfano, ambapo mwelekeo wa jumla ulikuwa ni kujizatiti kwa mifumo ya dola, taathira ya awali ya uundwaji wa madola mara nyingi iliyatingisha maeneo makubwa na kusababisha baadhi ya madola kuibuka ama kuanguka ghafla. Juhudi za baadhi ya viongozi za kuiunganisha Ethiopia na kurekebisha asasi zake zinaweza kuchukuliwa kama mfano wa matukio yaliyokuwa na athari kwenye eneo lake tu. Juhudi nyingine za mageuzi, kama zile za watawala wa Misri, ziliathiri eneo lote. Kadhalika, mabadiliko mengine kama yale ya Mfekane na jihadi za Sudani ya Magharibi na Kati, yalikuwa na athari zilizodumu kwa muda mrefu kwenye eneo kubwa.

Mahitaji ya Wazungu ya mazao ya kilimo, na shughuli zao za biashara kwa jumla, zilikuwa sababu kubwa za mabadiliko katika jumuiya nyingi za Afrika. Hii ni kwa kuwa biashara iliathiri upatikanaji wa silaha na utajiri, na vyote viwili vilikuwa muhimu katika kuibuka na kuanguka kwa madola katika sehemu nyingi za Afrika. Mawazo ya kimagharibi kuhusu miundo ya kisiasa jamii yaliyoletwa na wamisionari na wafanyabiashara wageni vilevile yalileta mabadiliko muhimu kwenye maeneo ya pwani kuanzia Siera Leone hadi Kusini mwa Afrika na Bukini.

Mabadiliko haya mbalimbali ni lazima yaangaliwe kwa kuzingatia muktadha wa juhudi za makusudi za viongozi wa Kiafrika za kubadili jamii zao. Baadhi yao

walihamasishwa na mabadiliko yaliyotokana na mawazo ya Waislamu, wengine kutokana na mawazo ya Wamisionari na wafanyabiashara wa Kizungu, na wengine waliendelea na mambo yao ya kabla ya karne ya 19, wakitumia asasi na maadili ya jadi katika kuunda madola mapya. Bila kujali walivyohamasishwa, viongozi mbalimbali walijaribu kunufaika na kuwepo kwa Wazungu kibiashara kwa kujipatia teknolojia mpya ya kuwasaidia katika miradi yao, lakini wakagundua kuwa maliasili zao zilikuwa zikichukuliwa kwa ajili ya kuimarisha teknolojia za Wazungu bila kuwanufaisha wao. Hivyo, kuwepo kwa Wazungu kulikwamisha juhudi za Waafrika za kujiletea maendeleo.

## *Miundo ya kisiasa*

Juhudi hizi za kujiletea maendeleo labda zilikuwa wazi zaidi kwenye uwanja wa siasa. Hali hii ilitokana na maeneo mbalimbali yaliyoshiriki katika biashara ya watumwa kutambua kuwa njia bora ya kuhimili na hata kufaidika na biashara hiyo ni kuyazatiti madola yao na misingi ya kijeshi ya mamlaka yao Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, miundo ya kiuchumi na kisiasa katika sehemu nyingi za Afrika ilikuwa inalegalega. Madola mengine yaliibuka, mengine yalianguka. Baadhi ya miundo ya zamani ya dola ilikuwa dhaifu, na haikuwa na mashiko kwa watu. Ni huko Maghrib na Misri tu ndiko kulikokuwa na madola imara yenye miundo ya kisiasa ya kudumu,ambayo ilitokana na majaribio ya muda mrefu ya utekelezaji wa sharia ya Kiislamu. Katika maeneo mengine ya Afrika, juhudi za kuunda madola yenye nguvu mnamo karne ya kumi na tisa zilisababisha ushindani mkali wa kisiasa ambao uliharibu mifumo ya kisiasa iliyokuwepo kama ilivyokuwa kwa eneo la Volta. Mifano mingine ya kuanguka kisiasa ni ile ya athari za awali za Mfekane, kuenea kwa biashara ya Wazungu na kupanuka kwa Chokwe na Ovimbundu katika mifumo ya madola ya Luba na Lunda. Madola kadhaa yalitoweka kutokana na maendeleo haya. Wakati huohuo, kuliibuka madola imara yenye miundo fanifu zaidi ya kiutawala.

Madola mengi yaliyodumu tangu karne ya kumi na nane yaliweza kufanya hivyo kutokana na mageuzi makubwa ya ndani. Hii ni kwa kuwa karne ya kumi na tisa ileleta changamoto mpya zilizolazimisha kila dola kuchagua ama kubadilika na kupanuka na kuwabana majirani zake, au kukubali kuathiriwa na upanuzi wa wengine. Ingawa madola machache kama Benin yalinywea kidogo na kuendelea kuwepo, mengine yalipitia mateso makubwa lakini yaliyoyanufaisha. Madola kama hayo ni Asante, Dahomey na Buganda, ambayo yalipangua kabisa, japo kijanja, miundo yao ya kisiasa na kufanya mabadiliko makubwa ya kuzizatiti asasi zao za serikali. Mengine kama Borno, yalifanya mabadiliko ya nasaba za watawala bila kuonekena kuwa yamebadili sana mifumo yao ya jadi ya kisiasa.

Mfekane, zaidi ya uharibifu wa awali iliyousababisha, ilifaulu kuunda madola kadhaa makubwa, yenye nguvu zaidi, yaliyokuwa na miundo ya kudumu kuliko madola yaliyokuwepo kabla. Ilieneza mtindo mpya wa dola la kimapinduzi la Wanguni wa kaskazini lililounda jeshi la kudumu la marika, kuingiza mateka katika utamaduni unaotawala, na kuleta dhana mpya kabisa ya uhusiano wa mtawala na mtawaliwa. Mtawala akiwa zaidi mkuu wa usimamizi na utendaji wa dola, aliweza pia kutumia ukuu

wake wa madhehebu mbalimbali ya kidini kuwaunganisha watu na kuhalalisha mamlaka yake.

Madhumuni ya mabadiliko ya Ethiopia yalikuwa kufufua upya dola la zamani la Kikhufu ambalo lilikuwa limegawanyika katika tawala kadhaa zenye kuzozana zilizotawaliwa na machifu sugu na wakaidi. Ingawa maliki wawili, Tewodros II na Yohane IV, walifaulu kwa kiasi fulani kufufua moyo wa utaifa, hawakuwa na uwezo wa kutosha wa kukabiliana na tamaa ya ukubwa ya machifu wa chini yao kwa ufanisi na kwa namna ya kudumu.

Watawala wa Misri walitaka kurudisha utukufu wa kale wa mafirauni. Ili kufikia nia hiyo, Muhammad Ali alinuia kuwadhoofisha Mamluki, kuanzisha utawalamsonge mpya, kuimarisha udhibiti wake wa ardhi na kilimo, kujenga uchumi unaotegemea zaidi viwanda, kusaidia jeshi lililorekebishika, na kuwa huru kutokana na utawala wa Waturuki. Khedive Ismail aliendelea na ari hiyo ya mageuzi kwa kuwaajiri Wazungu kusimamia shughuli za biashara na za uzuiaji wa biashara ya watumwa huko Sudani, na kwa kujenga mfereji wa Suez, mifereji mingine na mifumo ya umwagiliaji maji na mawasiliano. Nia yake ilikuwa ni kununua teknolojia ya Wazungu na kuitumia kuweka miundo na asasi za kisasa nchini Misri.

Katika ukanda wa Sudani, vuguvugu za jihadi zilinuia kuunda jamii za Kiislamu kwa kuweka viongozi wacha Mungu ambao wangetawala kufuatana na Kurani. Huko Sokoto, nia hii ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa. Himaya ya Kiislamu ya Masina pia iliwaunganisha watu wa jamii kadhaa chini ya mfumo wa dola unganifu yenye miundo ya utawala na kanuni za sharia za kudumu, licha ya ushindani wa ndani wa koo za kifalme na uhasama wa Wafaransa. Zaidi ya hayo, chini ya Al-Haji Umar, tarika ya Tijaniya ilitoa watu aina aina walioenea katika eneo kubwa wakiungaishwa na utiifu wao kwa mtawala huyo. Kwa njia hiyo, Uislamu ulisaidia kuenea kwa madola ya Kiislamu katika maeneo yasiyokuwa ya Kiislamu kama ilivyokuwa kwa Ilorin na Nupe huko Nigeria. Samori Ture pia alijaribu kutumia Uislamu kuwaunganisha watu wake bila kujali kama walikuwa Waislamu au Wanajadi kabla ya hapo.

Ukristo nao ulifanya kazi kama hiyo. Ulizipa kiunzi cha wa utamaduni jamii za Krioli zilizoundwa Freetown, Libreville, Freretown na katika makazi mengine ya watumwa walioachiwa huru. Waafrika wengi waliwakaribisha wamisionari, sio kwa ajili ya neno la Mungu pekee, bali kwa ajili ya elimu ya Kizungu waliyokuwa wakiitoa. Watawala wa Bukini, kwa mfano, walijaribu kutumia mawazo ya Kimagharibi waliyoyapata kutokana na Wamisionari wa Kikristo katika kupanga upya mifumo yao ya kisiasa. Walijaribu kuweka urari baina ya athari za Wakatoliki wa Kifaransa na za Waprotestanti wa Kiingereza. Walipoona usalama wao unatishiwa, walijaribu kuyafukuza makundi yote mawili, lakini walifanikiwa tu kuwafanya washughulike chinichini. Waliishia kuwa na Uprotestanti madhubuti kwenye kitala, Ukatoliki katika maeneo ya shamba, na Wafaransa wachokozi waliodhamiria kuanzisha utawala wa kikoloni. Kwa mwelekeo huohuo, baadhi ya madola mapya ya kusini mwa Afrika yaliwakubali wamisionari kama washauri au watetezi wao wa nje, lakini aghalabu waligundua kwamba utiifu wa wamisioni hao uligawanyika. Katika madola mengine,

viongozi wachache wenye elimu ya Kimagharibi walitumia stadi zao za kusoma na mawazo ya Kizungu ya uundaji wa serikali kurekebisha mifumo yao ya serikali za jadi.

## *Mifumo ya kijeshi*

Kudumu kwa miundo ya kisiasa kulitegemea jeshi, na kauli hii ilithibitishwa zaidi katika karne ya kumi na tisa. Kabla ya hapo, nguvu za mfumo wa kisiasa zilitegemea mitandao ya kimadhehebu na uhusiano wa kindugu. Wakati jeshi lilipokuwa la mg'ambo na lililotokana na umma wa wakulima, ambao walikuja na silaha zao wenyewe na vyakula vyao, lilikuwa muhimu zaidi katika uhusiano na jamii za jirani kuliko katika kulinda miundo ya mamlaka ya ndani ya dola. Kuibuka kwa majeshi ya askari wa farasi hakukuanzisha tu kundi la waali katika jeshi bali pia tabaka lenye nguvu ambalo watu wake ilibidi wagawane na mtawala raslimali zilizopatikana ili waweze kupata farasi na kuajiri wapanda farasi.

Mpaka katikati ya karne ya kumi na tisa, silaha za moto (bunduki) zilizoingizwa kutoka nje au zile zilizotengenezwa na wenyeji hazikuleta tofauti katika muundo wa dola katika Afrika. Ingawa silaha za aina hiyo katika mikono ya majeshi yenye nidhamu, zingeweza kuleta mafanikio kwa muda, zisingeweza kufua dafu mbele ya jeshi lenye nidhamu la wapanda farasi lenye mikuki na mishale ya sumu. Kwa mfano Waegba wa Abeokuta walitumia bunduki kupinga uvamizi wa Wadahome, lakini hawakuweza kufua dafu kwa askari wenye nidhamu zaidi wa Ibadan mnamo miaka ya 1860 ambao zaidi walipigana kwa kutumia silaha walizozitengeneza wenyewe. Vilevile, mafanikio ya Tewodoros huko Ethiopia yalitegemea mkakati wake wa mashambulizi ya kushtukizia na misafara ya lazima ya majeshi yaliyokuwa na mizigo michache kuliko matumizi ya bunduki.

Hata hivyo, karne ya kumi na tisa ilishuhudia kuibuka kwa askari wataalamu, na jambo hili hatimaye liliongeza umuhimu wa jeshi katika muundo wa madaraka katika dola. Hawa ni watu ambao walikuwa na silaha takribani muda wote kutokana na vita vya mara kwa mara na ushindani wa kisiasa. Baadhi ya watu walichukulia vita kama aina ya kitegauchumi ambacho mwishowe kilileta madaraka ya kisiasa na udhibiti wa raslimali za kiuchumi. Hivyo, askari aliyefanikiwa angeweza kupata cheo ambacho angekitumia kujiingiza katika nafasi nzuri katika mfumo wa kisiasa. Katika mifano michache, mtawala alikuwa ndiye kiongozi wa vita. Shaka aligeuza marika kuwa askari wataalamu kwa kuwapa mafunzo na vifaa, na kuwafundisha nidhamu. Jeshi lake likawa kiini cha dola. Hata majemadari walionwasi walitumia majeshi yao kulazimisha utawala wao juu ya watu wa makundi tofauti na kuunda falme mpya kadhaa. Nidhamu yao, mafunzo na matunzo yao yaliwafanya wawe watiifu kwa makamanda wao hata kwenye hali ngumu. Majeshi yaliyokuwa na mafanikio zaidi mnamo karne ya kumi na tisa ni yale yaliyotegemea raslimali za ndani kwa ajili ya silaha na kujikimu.

Uingizaji wa bunduki kutoka Ulaya uliofanywa na watawala wa Kiafrika ulienea sana mnamo karne ya kumi na tisa. Hii haina maana kuwa bunduki za Ulaya hazikuingizwa kabla ya karne ya kumi na tisa, bali ilikuwa katika robo ya tatu ya karne hiyo ndipo bunduki zinazofaa zaidi zilianza kuingia, na silaha za Wazungu kuanza kuonekana kuwa

zimeleta athari kubwa katika vita na mifumo ya siasa ya Afrika. Jinsi uingizaji wa bunduki hizo ulivyozidi kuwa muhimu katika vita, ndivyo zilivyokuwa sehemu muhimu ya biashara, diplomasia na uendeshaji dola.

Kuongezeka huko kwa umuhimu wa silaha za Kizungu kulisababisha kushuka kwa hadhi ya askari wa farasi katika maeneo ambamo walikuwa muhimu. Badala yake askari wa miguu wa mtindo wa kizungu ndio waliokuwa tabaka aali la jeshi. Hivyo askari wa farasi wakachukua nafasi ya pili kama walinzi na askari wa akiba. Hali hii ilikuwa na athari muhimu za kijamii na kiuchumi ambazo mwishowe zilimuimarisha mtawala na kumsaidia kuibuka kama mtendaji mwenye mamlaka ya juu kabisa katika dola.

## *Mabadiliko ya kijamii na kiuchumi*

Karne ya kumi na tisa ilishuhudia mabadiliko makubwa ya kijamii katika Afrika. Tumekwishaona kuibuka kwa tabaka la wapiganaji. Tunahitaji pia kujadili kwa ufupi mabadiliko katika utumwa na kuibuka kwa tabaka muhimu kisiasa la wafanyabiashara.

Kulikuwa na mahitaji makubwa ya nguvukazi katika karne ya kumi na tisa ambayo yalisababisha kupanuka kwa viwango vya nguvukazi ya watumwa, kuongezeka kwa maeneo yaliyotumia mtindo wa kazi za kulazimishwa na matumizi makubwa ya wafanyakazi wahamiaji. Katika robo ya tatu ya karne, mwelekeo wa kawaida ulikuwa ni kuongeza wingi wa watumwa katika kaya kwa ajili ya uzalishaji. Kuongezeka kwa ushindani wa kisiasa katika karne ya kumi na tisa, kama tulivyoona, kulisababisha ongezeko kubwa la vita na mashambulizi ya mara kwa mara. Mashambulizi hayo yalitokana na sababu nyingi, lakini matokeo yalikuwa ni kuongezeka kwa idadi ya mateka wa vita. Mateka hao walitumika kutosheleza mahitaji ya nguvukazi katika kilimo, sanaa za ufundi, machimbo, na kama wapiganaji katika majeshi ya kulipwa yaliyokuwa yakiibuka. Kwa hiyo kundi aali la watawala katika jamii mbalimbali lilianza kutegemea kaya kubwa za wafuasi na watumwa waliofanya kazi kwenye mashamba makubwa, badala ya wanandugu wengi katika kuendeleza kaya zao na kuwakimu wapiganaji waliokuwa vitani. Ziada ilibadilishwa na bidhaa nyingine katika masoko ya kijamibu na kuingizwa katika biashara ya masafa marefu. Mazao ya shughuli hizo za kibiashara yalitumika kununulia silaha kutoka nje na kuvutia wafuasi zaidi.

Kufuatia kuisha kwa biashara ya watumwa ya Atlantiki, kulikuwa na ongezeko la mahitaji ya watumwa wa kuzalisha na kusafirisha mazao kama mafuta na kokwa za mawese, dhahabu, karanga, miwa, pembe za ndovu, na karafuu kwa vichwa au kwa mitumbwi kwenda pwani. Hali hii ilisababisha, kati ya mambo mengine, kuongezeka kwa utumwa wa viungani. Pia, kukawa na ongezeko kubwa la watumwa kwenye jumuiya nyingi. Ingawa kulikuwa na matukio ya maasi ya watumwa, kwa kawaida watumwa hawakuunda tabaka maalumu. Hii ni kwa sababu ya tofauti kubwa katika mapato na hali ya maisha ambayo ilifanya iwe vigumu kuwaweka pamoja kama tabaka. Zaidi ya hayo, kwa jumla waliingizwa kwenye utamaduni na kushirikishwa, hata kwa kiwango kidogo, katika jamii kwa kupitia kaya binafsi, isipokuwa katika maeneo machache kama huko Kalabri Kongwe, ambako takriban walitengwa daima

Kupanuka kwa shughuli za kibiashara kulisababisha ongezeko la idadi na umuhimu

wa wafanyabiashara. Biashara ya masafa marefu, vituo vya misafara na suhula nyingine saidizi ziliundwa Afrika Kaskazini, Magharibi, Mashariki na Kati ilipofika katikati ya karne ya kumi na tisa. Kulikuwa na aina nyingine za kazi za kulazimishwa zaidi ya utumwa, kama vile "mateka wa madeni" ambao nguvukazi yao ilitumika kama riba ya deni lililokopwa kabla, na kwa sehemu kama dhamana kuwa mwishowe deni litalipwa. Ilipofikia miaka ya 1870, mfumo huu ulienea sana Ghana (Gold Coast), ambako ulianza kushindana na utumwa kwa umuhimu. Ilielezwa kuwa utumwa ulikuwa ni njia ya kupata wafanyakazi wa kulazimishwa kutoka nje, na "mateka wa madeni" walikuwa ni vibarua wa kulazimishwa waliopatikana kutoka ndani ya jamii yenyewe. Wakati huohuo, tabaka maalumu la wafanyabiashara lilianza kuibuka Afrika ya Kaskazini, lakini halikuibuka haraka katika maeneo mengine ya bara hili. Hata kwenye maeneo ambayo yaliathiriwa na Ukristo na mawazo ya Kizungu, wafanyabiashara hawakufanya kazi kama tabaka maalumu la kibepari. Badala yake, waliishia kupata vyeo vya uchifu katika madola yao katika kusaka umashuhuri wa kisiasa.

Katika sehemu kadha za Sudani Magharibi na Senegambia, wafanyabiashara mashuhuri aghalabu walikuwa viongozi wa dini. Kwenye maeneo mengine, wafanyabiashara walikuwa pia askari, na hivyo kuwafanya wawe sehemu ya tabaka la watawala.

Hali ya Kusini mwa Afrika mnamo karne ya kumi na tisa ilikuwa ni ya kipekee. Ilipofikia miaka ya 1870, Makaburu na Waingereza walihitaji wafanyakazi zaidi, hasa kwenye migodi ya almasi ya Grikwa Magharibi. Suluhisho la tatizo hilo halikupatikana tu kutokana na wakimbizi wa Mfekane, lakini zaidi kwa kuwafanya Waafrika wapoteze ardhi yao, na kuwapa uchaguzi wa pekee wa kufanya kazi kwa wakulima na wajasirimali wa Kizungu chini ya masharti magumu sana. Wakoloni wa Kizungu wa Kusini mwa Afrika walijipachika haki ya kukamua, takriban kwa mabavu, nguvukazi ya Waafrika.

## *Mabadiliko ya urari wa madaraka*

Kwa hiyo, kwa njia kadhaa, mageuzi muhimu ya miaka ya 1870 katika Afrika yalikuwa ni mabadiliko makubwa katika majukumu na uwezo wa Wazungu katika Afrika. Mabadiliko hayo yaliakisi mabadiliko yaliyotokea Ulaya wakati huo. Mapinduzi ya viwanda yaliathiri madola ya Ulaya kwa njia mbalimbali na kusababisha mabadiliko katika urari wa madaraka. Kwa hiyo, ushinde wa Ufaransa kwa Ujerumani, kwa mfano, ulisababisha sera mpya ya upanuzi wa himaya ya Ufaransa huko Algeria na Senegambia kama njia ya kufidia ushinde wake. Hali hii iliongeza ushindani wa kikoloni baina ya mataifa makubwa ya Ulaya.

Wapelelezi, Wamisionari na Wafanyabiashara wote walikuwa waandaa njia kwa ajili ya ubeberu wa Kizungu Afrika. Wakati huohuo, jitihada za watawala wa Kiafrika kutumia mawazo na teknolojia ya Kizungu kurekebisha na kusasisha jamii zao zilikatishwa tamaa. Hivyo basi, watawala wa Kiafrika ambao, kwa jumla, walishirikiana na wafanyabiashara wa Kizungu na wamisionari katika kubadilisha biashara ya watumwa ya Atlantiki na biashara "halali", waliona dhahiri mabadiliko ya msimamo wa Wazungu mnamo miaka ya 1870. Wazungu walichushwa na kufungiwa katika biashara ya pwani

tu. Walitaka sana kuingia bara na kuingilia msingi wa uchumi wa pwani kwa kuwaachia huru watumwa wa majumbani na kuwaandikisha katika majeshi tangulizi ya kikoloni ambayo yangeongoza kujiingiza kwao kwa nguvu barani.

Wamisionari pia walikuwa na dhima muhimu katika kudhoofisha madola ya Kiafrika kwenye mkesha wa kutekwa kwa Afrika. Wamisionari waliweza kujipenyeza kwenye jumuiya kadha za Kiafrika kama sehemu ya mkakati wa mageuzi wa watawala wengi. Waliendeleza kisomo na kuwaingiza waumini wao katika matumizi ya bidhaa za Kizungu. Lakini hawakuweza kuwalinda watu dhidi ya uvamizi mpya wa kibeberu. Badala yake, baadhi yao walianza kupendekeza kuwa uanzishwaji wa utawala wa Wazungu ni muhimu kwa ajili ya mafanikio ya uenezaji wa neno la Mungu na maendeleo. Taarifa walizozikusanya juu ya jumuiya za Waafrika zilikuwa chanzo muhimu cha upelelezi wa kijeshi wakati wa vita vya Wazungu vya kuiteka Afrika. Shughuli za wamisionari pia zilileta migawanyiko kwa kushawishi ushindani ambapo baadhi ya madola ya Kiafrika yaliungana na Wazungu wa taifa fulani ili kujinufaisha kuwakandamiza majirani zao.

Hata hivyo, kati ya shughuli zote za Wazungu katika Afrika, ni biashara ndiyo iliyoleta matatizo makubwa zaidi kwa Waafrika. Wakati Waafrika walijitahidi kudhibiti biashara hiyo na kunufaika nayo kwa kiwango cha juu, Wazungu nao walitaka kunufaika kwa kiasi walichoweza kutokana nayo. Hata hivyo, Wazungu waliwashinda Waafrika katika hili. Huko Afrika ya Kaskazini, walipata upendeleo wa hali ya juu kutokana na mikataba na watawala wa Kituruki, na hivyo kudhoofisha uwezo wa watawala wenyeji kudhibiti biashara katika nchi yao wenyewe. Isitoshe kwa kisingizio cha kuanzisha biashara huria, Wazungu waliwashawishi watawala wa Kiafrika kukopa kutoka kwenye mabenki ya Ulaya kwa riba kubwa kupita kiasi. Hivyo walidhoofisha uchumi wa madola ya Kiafrika na udhibiti wa watawala juu ya uchumi huo. Kwa jumla, vitendo hivi vya kuiangamiza Afrika vilidhoofisha uwezo wa kujitawala wa watawala na kasababisha kupoteza uhuru wao.

Makubaliano yalipovunjika, Wazungu walilazimisha matakwa yao kwa hali mpya ya kujiamini na jeuri ambayo ilionekana kuanzia miaka ya 1870 na kuendelea. Hali hii ilitokana na kutambua kuwa walikuwa na uwezo mkubwa zaidi kutokana na ubora na wingi wa silaha na risasi zao. Bunduki mpya zilizoanza kuingizwa mnamo miaka ya 1870 ziligeuza urari wa madaraka kwa kunufaisha majeshi yaliyoongozwa na Wazungu. Hali hii pamoja na uzoefu wa nchi walioupata kutokana na kuwatumia Waafrika, ambao walikuwa marafiki zao, washiriki au watumwa walioachiwa huru, katika majeshi yao, uliwafanya wajiamini sana. Lakini hii haikuwa na maana kuwa ushindi ulikuwa rahisi: makamanda wa Kizungu mara chache waliwadharau wapinzani wao wa Kiafrika, nasi hatupaswi kufanya hivyo.

## *Mirathi ya vita*

Ilipofika 1870, jitihada za kurekebisha jamii za Kiafrika zilileta mabadiliko ambayo kwa

jumla yaliongeza uwezo wa Waafrika kujilinda. Wakati huohuo, kuwepo kwa Wazungu kulitishia usalama wa Waafrika, hasa kwa kuwa mafanikio ya viongozi wa Kiafrika yalifikiwa kutokana na vita vikali, na kwa kupuuza mshikamano wa jadi baina ya majirani, msimamo ulioanza wakati wa enzi ya biashara ya watumwa. Madola makubwa na yenye nguvu zaidi yaliyoibuka yakiwa na nguvu kubwa za utendaji yalifanya hivyo kwa kuyaonea madola dhaifu. Vitendo hivyo, kama tulivyoona, vilileta vita vingi ambavyo vilizidi kuwa vya kikatili na vya maangamizi zaidi kuliko hapo awali. Jumuiya kadha zilipoteza utambulisho wao wa pamoja. Madola yaliyoibuka katika kipindi hiki yalikuwa na asasi za kisiasa za kudumu na mipaka iliyokuwa dhahiri zaidi. Kwa hiyo, ingawa vita vya karne ya kumi na tisa viliongeza nguvu za madola, vinaweza kusemwa pia kuwa vilipuuza mshikamano wa jadi kwa jumla na hasa ule wa kabila. Kuna mifano mingi ya hali hiyo katika karne ya kumi na tisa, kama vile vita vya Yoruba, Maasai na Mfekane.

Wazungu waliweza kutumia matokeo hayo ya vita vya karne ya kumi na tisa katika azma yao ya kuzuia ongezeko la nguvu za madola ya Kiafrika. Mbinu yao ya kwanza ilikuwa kusisitiza maslahi ya kitaifa, hivyo kurudisha nyuma mwelekeo wa awali wa ushirikiano wa kimataifa. Wafanyabiashara, wapelelezi na wamisionari wa Kizungu waliokuwa Afrika walianza kujitambulisha kama Waingereza, Wafaransa au Wajerumani. Hali hii haikufaa sana, kwani watawala wa Kiafrika waligundua mara moja kwamba Wazungu wote walikuwa mawakala wa ubeberu, na walijifunza haraka jinsi ya kugonganisha taifa moja la Kizungu na jingine.

Hali hii iliwafanya Wazungu wabuni mbinu mpya; iliyofaa zaidi ni ile ya makubaliano ya kimataifa ya kuratibu "kinyanganyiro" cha makoloni, na kupunguza uingizaji wa silaha na risasi Afrika, na hasa kuzizuia zisiwafikie maadui zao wa Kiafrika. Huku Afrika, Wazungu walijihusisha na watawala na dola mojamoja, na walifikia makubaliano nao, lakini huko Ulaya waliamua kutotambua madola ya Kiafrika katika sheria za kimataifa. Kwa hiyo, walichukua hatua ya kuigawa Afrika bila kuwashirikisha watawala wa Kiafrika kana kwambwa Afrika haikuwa na wenyewe. Waafrika, kwa upande wao, hawakuweza kujenga mshikamano wa Afrika nzima kama ule wa Wazungu. Kila dola la Kiafrika lilijishughulisha kwa ajili ya maslahi yake. Maelezo kadha yanaweza kutolewa kuhusiana na hali hiyo, lakini sababu muhimu inayoonekana ni mirathi ya vita, ushindani na uadui ambao ulikuwa kama ufa uliotokea ukutani wakati uleule mjusi dukizi alipotaka kujipenyeza.

# *BIBLIOGRAFIA*


**Abdel-Malek, A.** (1969) *Idéologie et renaissance nationale: l'Egypte moderne* (Paris: Anthropos)

**Abir, M.** (1977) 'Modernisation, reaction and Muhammad Ali's 'Empire', *Middle Eastern Studies*, 13, 3, kur. 295-313

**Abitbol, M.** (1979) *Tombouctou e les Arma de las conquête marocaine du Soudan nigérien en 1591 à l'hégemonie de l'Empire du Macina en 1833 (Paris: Maisonneuve a Larose)*

**Abubakar, S.** (1970) *The Lamibe of Fombina: A Political History of Adamawa* 1809-1901 (Zaria; Ahmadu Bello University Press)

**Abun-Nasr, J. M.** (1962) Some aspects of the Umari branch of the Tijanniyya', *JAH*, 3, 2, kur. 329-31

**Abun-Nasr, J. M.** (1975) *A History of the Magrib* (2nd edn. Cambridge: CUP)

**Adamu, M.** (1978) *The Hausa Factor in West African History* (Zaria: Ahmadu Bello University Press)

**Ageron, C. R.** (1968) *Les Algériens musulmans et la France*, 1871-1919, ) Juz. 1, Paris: Faculté des Lettres et Sciences Humaines, Sorbonne)

**Ageron, C. R.** (1972) *Politiques coloniales au Maghreb* (Paris: PUF)

**Ageron, C. R.** (1973) *De l'insurrection de 1871 au declenchement de la guerre de libérations (1954), Histoire de l'Algérie contemporarine,* 2 (Paris: PUP

**Ahmed, J. M.** (1966) *The Intellectural Origins of Egyptian Nationalism* (London: OUP

**Ajayi, J.F.A** (1969) *Christian Missions in Nigeria, 1841-1891: The Making of a New Elite* (Evanston: NUP)

**Ajayi, J. F. A.** na **Crowder, M.** (wah.) History of West Africa Juz. 2 (2nd edn. London: Longman)

**Ajayi, J. F.A.** na **Crowder, M.** (wah.) (1985) *Historical Atlas of Africa*, (London: Longman)

**Ajay, J.F.A.** na **Peel, J.D.Y** (wah.) (1992) *People and Empires in African History" Essays in Memory of Michael Crowder* (London: Longman)

**Ajayi, J.F.A.** na **Smith, R.S.** (1964) *Yoruba Warfare in the Nineteenth Century* (Cambridge: CUP)

**Akinjogbin, I.A.** (1965) 'The prelude to the Yoruba civil wars of the nineteenth century', *Odu*, 2, 2, kur. 81-6

**Akinjogbin, I.A.** (1967) *Dahomey and Its Neighbours, 1708-1818* (Cambridge:CUP)

**Akinjogbin, I.A.** na **Ekemode, G.O.** (wah.) (1976) *Proceedings of the Conference on Yoruba*

*Civilization held at the University of Ife, Nigeria, 26-31 July 1976*

**Akintoye, S. A.** (1969) 'The north-eastern districts of the Yoruba country and the Benin kingdom', *JHSN*, 4, 4, kur. 539-53

**Akintoye, S. A.** 1971) *Revolution and Power Politics in Yorubaland, 1840-1893* (London: Longman)

**Alagoa, E. J.** (1964) *The Small Brave City Starte: A History of Nembe-Brass in the Niger Delta* (Madison" University of Wisconsin Press)

**Alagoa, E. J.** (1970) 'Long-distance trade and states in the Niger Delta', *JAH*, 11, 3, kur. 319-29

**Alagoa, E. J.** (1971a) 'The development of institutions in the states of the Eastern Nigeria Delta', *JAH*, 12, 2, kur. 269-78

**Alagoa, E. J.** (1971b) 'Nineteenth-century revolutions in the states of the eastern Niger Delta and Calabar', *JHSN* , 5, kur. 565-73

**Alagoa, E. J.** na **Fombo, A.** (1972) *A Chronicle of Grand Bonny* (Ibadan: IUP)

**Ali, A. I. M.** (1972) *The British, the Stave Trade and Stavery in the Sudan, 1820-1881* (Khartoum: KUP

**Allen, J. de. Vere** (mh.) (1977) *Al-Inkishafi. Catechism of a Soul* (Nairobi, Kampala and Dar es Salaam. EALB)

**Alpers, E.A.** (1969) 'Trade, state and society among the Yao in the nineteenth century', JAH, 10, 3, kur. 405-20

**Alpers, E. A.** (1975) *Ivory and Slaves in East Central Africa* (London" Heinemann)

**Alpers, E. A.** (1976) 'Gujarat and the trade of East Africa, c. 1500-1800', *IJAHS*, 9, kur. 22-44

**Andrews, G.R.** (1980) *The Afro-Argentines of Buenos Aires 1800-1900* (Madison: UWP

**Anstey, R.** (1975) *The Atlantic Slave Trade and British Abolition, 1760-1810* (London: Macmillan)

**Ardener, E.** (1956) *Coastal Bantu of the Cameroons* (London, IAI)

**Arhin, K.** (1970) 'Aspects of the Ashanti northern trade in the nineteenth century', *Africa*, 40, 4, kur. 363-73

**Arhin, K.** (1979) *West African Traders in Ghana in the Nineteenth and Twentieth Centuries* (London: Longman)

**Asad, T.** (1966) 'A note on the history of the Kababish tribe', *SNR*, 47, kur. 79-87

**Asiegbu, J.U.J.** (1969 *(Slavery and the Politics of Liberation, 1787-1861: A Study of Liberated African Emigration and British Anti-Slavery Policy* (London: Longmans Green)

**Asiwaju, A. I.** (1973) "A note on the history of Sabe: an ancient Yoruba Kingdom', Lagos Notes and Record, 4, kur. 17-29

**Asiwaju, A. I.** (1976) *Western Yorubaland Under European Rule, 1889-1945: A Comparative Analysis of French and British Colonialism* (London: Longman)

**Asiwaju, A. I.** (1979), The Aja-Speaking people of Nigeria: a note on their origins, settlements and cultural adaptation up to 1945' *Africa*, 49. 1 kur. 15-39

**Atmore, A.** na **Marks, S.** (1974) 'The imperial factor in South Africa in the nineteenth century: towards a reassessment', JICH, 3, 1, kur. 105-39

